

الامطهء من سيرة المهطهئ - سواحيلئ

KUCHAGUA KUTOKA KATIKA HISTORIA YA MTUME MTEULE

Prof. Dr. Awwad Abdullah Al-Mu'taq



Islamhouse.com



المحتوى الإسلامي

KCHAGUA KUTOKA KATIKA HISTORIA YA MTUME MTEULE

Amekifanyia ufupisho toka katika kitabu chake kiitwacho -
Rasulullahi Wakhaataman Nabiyiin Diini wa Daula.

USTADH. DOCTOR. ABDUL AZIZI BIN IBRAHIIM AL-UMARIY

Mkufunzi mstaafu wa Historia ya Mtume, katika Chuo kikuu cha
kiislamu cha Imamu Muhammad Bin saud kilichopo Riyaadh.

شركاء التنفيذ:



المحتوى الإسلامي



رواد الترجمة



جمعية الربوة



دار الإسلام

يتاح طباعة هذا الإصدار ونشره بأي وسيلة مع
الالتزام بالإشارة إلى المصدر وعدم التغيير في النص.

☎ Telephone: +966114454900

@ ceo@rabwah.sa

✉ P.O.BOX: 29465

☎ RIYADH: 11557

🌐 www.islamhouse.com

Utangulizi:

Shukurani zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote na rehema na amani ziwe juu ya aliyebora katika mitume na manabii Bwana wetu Mtume Muhammad na watu wake na maswahaba zake wote na wenye kumfuata, na baada ya hayo;

Kwa hakika vitabu vilivyotungwa katika Historia ya Bwana Mtume ni vingi, na ni juhudi kubwa sana zimetolewa, na vitabu vilivyotungwa kwa nyakati tofauti tofauti ni vingi na wala havihesabiki, na ubora wake ni mkubwa, na kwa hakika Historia kwa ujumla imegubikwa na mafunzo na Adabu na Elimu, ameshiriki katika hilo kila aliyeandika au kutunga kitabu cha historia, kiasi kwamba imezoeleka kuwavutia watu na kuvifikisha kwa namna tofauti na kwa kila aina ya Lugha na kwa ngazi tofauti.

Na pamoja na kukubali kwangu na kushukuru kwangu na Kuelekeza dua zangu kwa wote hawa walionitangulia katika medani za Historia, kwa hakika nimekusudia kujiunga katika Safu yao, huenda nikapata nafasi ya kuweka mguu, kama mwenye kusimama nyuma ya imamu wake katika swala (Imamu wa Mitume Rehema na amani ziwe juu yake).

Na nimeona kuwa kuandika kuhusu Historia ya Mtume Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kunanipa furaha natarajia kwa kuandika historia hiyo nikawa mimi ni miongoni mwa watakaokuwa kwenye safu ndefu nyuma Mtume Rehema na Amani ya Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, huenda nikapata uombezi wake na nikapata nafasi ya kukutana naye, na hakika mimi natarajia hilo toka kwa Mwenyezi Mungu.

Na wakati wa kupitia Historia ya Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Amani*-au kuandika kuhusu historia hiyo, kunapelekea kumpenda Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Amani*- katika kila hali zake na matendo yake, hivyo utahisi kuwa mapenzi yanazidi katika moyo wako, na roho ya imani, kwa hivyo huzidi nguvu na yakini, na Historia yake ipo karibu sana na mwanadamu, kuipata na kuifanyia kazi ni jambo jepesi wanaweza watu wote kifanyia kazi, hasa kwa kikundi fulani au wakafanyia kazi baadhi ya watu na wengine wasiifanyie kazi au tabaka fulani.

Na huenda jambo muhimu lililonisukuma kuandika Historia ni mapenzi ya kumpenda Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Amani*- na kujikurubisha kwake kwa hilo, na huu ni utukufu ambao najifaharisha nao na ninautaja na ninaukusudia na kuurudiarudia, na ninatamani kwa kufanya hivyo kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu na mapenzi toka kwa Mtume wake -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Amani*- itakapoletwa chemchem yake kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na kwa Rehema zake.

Na huenda mimi nikamfaidisha mwenye kuisoma Historia, na kwa hakika nimefanya jitihada ya kufuata njia maalumu katika hili kwa kutilia umuhimu wa kumuhudumia msomaji wa Historia ya Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Amani*-kwa waislamu wote kwa kuwawekea yaliyo yakweli pasi na kuzidisha.

Na kwa hakika kimetoka kitabu hiki katika chapa yake ya Asili kwa jina la (Rasulullahi wa Khaataman Nabiiyiina) kikiwa kwenye juzuu tano zenye kukusanya Historia pamoja nakuwa kila juzuu moja ilikuwa ina maudhui yake.

Na kwa hakika walinitaka mimi vipenzi vyangu wengi nifanye kazi ya kukifupisha ili iwe ni wepesi kukisoma, na ili iwe ni wepesi kukifanyia tarjama ambayo imefuata mkondo wake kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu katika lugha nyingi, hivyo nikaandaa

huu ufupisho ambao upo mikononi mwenu, baada ya kujitahidi na kuangalia lenye kuwezekana kukiwacha au kukipunguza kutoka katika kitabu changu cha asili, ikiwa ni pamoja na kufanya baadhi ya mabadiliko mengine.

Na kwa hakika nimechagua njia ya uandishi wa hiki kitabu kilichofupishwa njia ambayo nilikuwa nimeifanyia kazi katika kitabu changu cha asili chenye kutoa faida itokanayo na chimbuko la sunnah katika riwaya zilizo sahihi zenye mafungamano na Historia na kuzipa kipaumbele kuliko riwaya zingine, na hasa riwaya ambazo zinamafungamano na hukumu za sheria, na nimeziashiria kwa uwazi katika sehemu zilipo pembeni mwa kitabu (Haamishi).

Na nimejaribu kuhusisha kati ya kutaja tukio na ufahamu wake, na kupata faida kutokana na mafunzo yake katika maisha ya watu wote na watu maalumu, na nikajaribu kuibua upande wa maendeleo ya kibinadamu na mipangilio na uongozi kutoka katika Historia ya bwana Mtume.

Na nikagusia nidhamu za uislamu katika nyakati za Mtume - **Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**-, na kuanzisha kwake dola ya kiislamu, na nikagusia nidhamu za ukuwaji kimaendeleo na kimiji, nidhamu ambazo alizieneza katika jamii ya wanadamu, na akaisambaza kwa mafanikio na kuwa ya kipekee, na ikawa ni taa kwa wanadamu na uongozaji mzima wa kibinadamu.

Na hata kama sijaandikiwa kupata nafasi ya kumuona - **Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- basi natarajia kutokuiokosa nafasi ya kuwa pamoja na Historia yake na maisha yake, kupitia vitabu vikubwa na muandiko wa kalamu, na mapenzi mengi na hisia, na kuwanukulia Historia na maisha yake kwa vipenzi vyake waliomwamini na wenye kupenda kumjua -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani.

Pamoja na kuwa umepita muda mrefu lakini nilikuwa nahisi kuwa karibu naye Mtume -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- na mafungamano yangu na wakati ambao ulikombolewa uwanadamu kutoka katika pingu za kuabudu masanamu na kuingia watu katika kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumyenyekea na pia kumuabudu yeye, na nikapenda msomaji mtukufu ashirikiane nami katika hisia hiyo.

Na ninakuta hapa kuwa ni wajibu juu yangu kutanguliza shukrani njema na kutambua mchango wa muheshimiwa Doctor Ally Bin Ibrahim Bin Hamdi An-namlat, ambaye alinihamasisha kufanyia kazi kitabu hiki kama alivyonihamasisha kukifupisha kitabu hiki ambacho kipo mikononi mwenu kutoka kwenye kitabu cha asili kiitwacho (Rasuulullah wakhaatama Nabiyyiina) Maana yake Mtume wa Mwenyezi Mungu na Nabii wa mwisho kitabu ambacho kimetoka katika juzuu tano, na nimepata faida kutokana na Angalizo lake, Allah amlipe malipo mema, vilevile ninamuomba kila aliyenisaidia kufanikisha kitabu hicho na kukisambaza.

Na inakuja chapa hii ya pili ya huu ufupisho baada ya kutoa chapa ya kwanza, na kwa hakika nimekifanyia baadhi ya masahihisho na mapitio na nikakifupisha kidogo, kwa vile ambavyo wamenifahamisha hilo baadhi ya waliokisoma kitabu, wapewe shukurani na malipo. Ninamuomba Mwenyezi Mungu na kuwaomba wote kupata elimu yenye manufaa na matendo mema hakika yeye ndiye mmiliki na muweza wa hilo.

Mjini Riyaadh

Mwezi wa Ramadhan 1438 H

Malengo ya kuisoma Historia ya Mtume na faida zake.

Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- ni kiumbe apendazea zaidi kwa Mwenyezi Mungu na amemchagua kutoka kwa viumbe hao, na akambebesha ujumbe wake, hivyo mapenzi ya Mwenyezi Mungu na sisi kumpenda Mtume kunapelekea kumjua yeye na kusoma Historia yake.

Na hii ni sehemu ya haki yake kwetu sisi -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani na ni alama ya hakika ya kumpenda kwake na kumpenda Mwenyezi Mungu mtukufu: Sema, ewe Mtume,

﴿قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ نُؤْتِبْكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾

[آل عمران: 31]

«Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani mimi Atawapenda Mwenyezi Mungu na Atawasamehe madhambi yenu na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwenye huruma". [Al-Imran: 31].

Kama ambavyo kuisoma Historia ya Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- kuna kujifunza ndani yake alivyokuwa akiujenga uhai wa uislamu, pale alipoishi -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- hali yakuwa ni Mja wa Mwenyezi Mungu aliyekusanya Mambo ya Dunia na Akhera, na namna hii inatoa mfano wa tabia zake-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-katika utekelezaji wa uislamu kivitendo na sheria zake na hukumu zake, na kujitolea Nafsi na mali katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Kama vile ilivyo kuwa historia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- ndani yake kuna kujifunza Historia Mwanadamu mtukufu na mbora kwa wote, na watu wameumbwa kupenda kusoma Historia za watu watukufu kwa ujumla, na kujua historia na maisha yao na visa vyao, kila umma

miongoni mwa Umma unajaribu kuwaibuwa watukufu wao, na wanajifaharisha nao na historia zao ulimwenguni, na sivyo hivyo tu bali wanawapamba na kuwatengenezea visa vya uongo wakati mwingine, ili wawaonyeshe watu kuwa wanao watu wakujifaharisha nao.

Ama sisi waislamu kipenzi chetu jemedari wetu na kiongozi wetu -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani ndiye mzuri zaidi na ni mbora wa viumbe Bwana wa watoto wa Adamu. kwa hivyo basi sisi kwa kusoma Historia ya Bwana Mtume -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- twaitikia hitajio hili la kimaumbile liliyopo kwa watu, kwa kukidhi haja ya hitajio hilo kwa kutoa elimu sahihi ya ukweli, ambayo kwa kawaida watu ni wenye kuipupia kwakuisoma na tunakidhi haja kwa yule ambaye ni wajibu juu yetu kuyasoma Maisha yake na Historia yake ili tufungamane naye, na hapa lazima tukubali kuwa wasiokuwa waislamu wamemfanya Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na aman-ni mtu mashuhuri, basi vipi kwetu sisi wafuasi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ambao hatupaswi kumpa kipaumbele yeyote kabla yake na wala hatupaswi kuisoma Historia ya mwanadamu yoyote kabla yake,siyo Historia ya mfalme wala waziri wala mkubwa yeyote wala wala kiumbe kilichokuwepo kabla ya Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani.

Na huyu hapa Michael Hart, Mwana Historia wa Amerika, alidai kutunga Historia ya Mwanadamu katika kitabu chake kiitwacho (Watu Mia Mashuhuri katika Historia ya Wanadamu) amemuweka Mtume kuwa ndiye mwanadamu wa kwanza katika Historia ya Wanadamu, pale aliposema maneno yake haya: (Kwa hakika nimemchagua Muhammad ili awe wa kwanza katika Orodha, na ni lazima wengi watapigwa na butwaa kwa kuchagua huko na ni haki yao kupigwa butwaa, lakini Muhammad ni mwanadamu wa kipekee katika Historia iliyofanikiwa kwa kiwango cha juu katika dini na

dunia, naye ni kiongozi aliyelingania katika uislamu na akaueneza kama moja ya dini tukufu kuliko dini zingine, na akawa ni kiongozi wa kisiasa na kijeshi na kidini, na baada ya kupita karne kumi na tatu 13 tokea kufa kwake kwa hakika athari ya Muhammad -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na aman-bado inaendelea kuwa na nguvu yenye kuendelea)¹Na jambo hili linatukumbusha maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ﴾ [الشرح: 4]

"Na tukauwinua utajo wako". [Ufafanuzi: 4]

Na alisema (Gustave Le Bon) kuhusu Mtume -**rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- katika kitabu chake kiitwacho " Hadhwaaratul Arab" maendeleo ya waarabu. ((Ikiwa utapima thamani ya watu kutokana na matendo yao matukufu anakuwa Muhammad ni katika watu watukufu zaidi kuliko yeyote aliyetambulika kihistoria))²

Na alisema (Wiliam Muer) kuhusu Mtume: Kila tunavyosoma maisha yake tunayakuta yana ubora wa hali ya juu na historia iliyotakata, na tabia njema, na ubora huo utabakia milele katika zama zote.(3)

¹ Michael Hart, (Watu Mia Mashuhuri katika Historia Wanadamu) amekifanyia Tarjama Anis Mansour, chapa ya Maktaba ya Misri Cairo ukurasa wa 14.

² Ni maneno ya Gustave Le Bon katika kitabu chake kiitwacho Maendeleo ya waarabu, kimetafsiriwa na Adil Zuaitar, chapa ya Daaru ih-yaa Turaathil Arabiy, nchini Beirut mwaka 1399 H uk 14.

Hakika Mwenyezi Mungu - kutakasika na machafu ni kwake na mtukufu- ameutaka umma wa kiislamu kufanya ibada kwa kusoma Historia ya manabii waliopita na kusoma mwenendo wa Mwenyezi Mungu kwa umma uliotangulia kwa mujibu wa hali zao zitokanazo na mitume wao na ulinganiaji wao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa hakika Mwenyezi Mungu amewafanya kuwa ni Taa ifuatwayo na ukumbusho wenye kusomwa na ni kiigizo na uthibitisho wa Mtume-**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**-na hivyo basi visa vya Mtume-**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- na Historia yake ni uthibitisho tosha kwa waislamu wenye kujifunza na hasa ukizingatia kuwa visa hivyo vina mafungamano na kitabu cha Mwenyezi Mungu -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**-na mwenendo wa mtume wake ambaye ni miongoni mwa waliofanywa kuwa ni taa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿تَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ أَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ هَذَا الْقُرْآنَ وَإِنْ كُنْتَ مِنْ قَبْلِهِ لَمِنَ الْغَافِلِينَ﴾ [يوسف: 3]

"Sisi tunakusimulia wewe, ewe Mtume, visa vizuri zaidi kwa wahyi tuliyokuletea wa hii Qur'ani, na ingawa, kabla ya kukuteremshia, ulikuwa ni miongoni mwa walioghafilika navyo, hujui chochote kuhusu habari hizi". [Surat Yusuf: 3].

Amesema mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَقَدْ كَانَ فِي قَصصِهِمْ عِبْرَةً لِأُولِي الْأَلْبَابِ مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَى وَلَكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ كُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ﴾ [يوسف: 111]

"Kwa hakika katika habari za Mitume tulizokuelezea na mambo yaliyowakumba wenye kukanusha kuna mawaidha kwa wenye akili timamu. Hii Qur'ani haikuwa ni habari ya uongo iliyoziuliwa, lakini tumeiteremsha ikiwa ni yenye kutolea ushahidi ukweli wa vitabu vilivyoteremshwa vilivyotangulia na kwamba vinatoka kwa Mwenyezi Mungu, na ikiwa ni ufafanuzi wa kila ambalo waja wanalihitaji la kuhalalishiwa na kuharamishiwa, linalopendeza na linalochukiza na mengineyo, na ikiwa ni muelekezo kutoka kwenye upotevu na ni rehema, kwa wenye Imani, ya kuzifanya nyoyo zao ziongoke, wapate kuyafuata kivitendo maamrishi na makatazo yaliyomo". [Surat Yusuf: 111]

Na amesema Allah Mtukufu:

﴿ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْفَرَى نَقْصُهُ وَعَلَيْكَ مِنْهَا قَائِمٌ وَحَصِيدٌ﴾ [هود: 100]

"Haya tuliyokutajia wewe, ewe Mtume, ni miongoni mwa habari za watu wa miji ambayo tuliwaangamiza watu wake, twakupasha habari zake. Na miongoni mwa miji hiyo kuna iliyo na athari zilizosalia; na miongoni mwazo kuna ambazo athari zake zimefutika, hakuna chochote katika hizo kilichosalia". [Hud: 100].

Na amesema Allah Mtukufu:

﴿تِلْكَ الْفَرَى نَقْصٌ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِهَا وَلَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِنْهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا مِنْ قَبْلُ كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِ الْكَافِرِينَ﴾ [الأعراف: 101]

"Miji hiyo iliyotangulia kutajwa, nayo ni miji ya watu wa Nūḥ,, Hūd, Šāleḥ, Lūṭ, na Shuaibu, tunakupatia, ewe Mtume, habari zake na zile zinazohusu mambo ya Mitume wa Mwenyezi

Mungu waliotumwa kwa watu wa miji hiyo, zinazofanya mazingatio yapatikane kwa wenye kuzingatia na pia makemeo kwa madhalimu. Hakika watu wa miji hiyo walijiwa na Mitume wetu na hoja zilizo wazi juu ya ukweli wao, lakini hawakuwa ni wenye kuyaamini yale waliyokuja nayo hao Mitume kwao kwa sababu ya kupita mipaka kwao na kuikanusha haki. Na mfano Alivyopiga chapa Mwenyezi Mungu kwenye nyoyo za makafiri hawa waliotajwa, Atapiga mhuri kwenye nyoyo za wenye kumkanusha Muhammad Rehema na Amani ziwe juu yake". [Surat Al-a'raf 101].

Na amesema Allah Mtukufu:

﴿كَذَلِكَ نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِ مَا قَدْ سَبَقَ وَقَدْ آتَيْنَاكَ مِنْ لَدُنَّا ذِكْرًا﴾ [طه: 99]

"Na kama tulivyokusimulia, ewe Mtume, habari za Mūsā na Fir'awn na watu wao, tunakupa habari za waliokutangulia wewe. Na tumekuletea Qur'ani hii kutoka kwetu iwe ni ukumbusho kwa mwenye kujikumbusha". [Surat Twaha 99].

Na Aya zote hizi na zinginezo zinatilia nguvu kuwa kusoma yaliyopita kwa manabii waliotangulia ni sehemu ya Qur'ani na ni sehemu katika dini na elimu ya kisheria, Elimu ambayo inatoa muelekeo wa maisha ya Mtume- **Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- na maisha ya umma wake pamoja nae, na kinachofuata ni kuwa kuyasoma maisha yake ni malezi ya Umma na ni elimu tusiyoweza kuiepuka mpaka siku ya kiyama.

Kama vile ambavyo kuisoma Historia yake ni kutekeleza Amri ya Mwenyezi Mungu -kutakasika na machafu ni kwake na mtukufu- na ni ishara ya utumwa wake, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu-:

﴿لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا﴾
[الأحزاب: 21]

(Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na kumtaja Mwenyezi Mungu sana). [Surat Ahzaab 21],

Mwalimu wetu wa kwanza -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- kutufundisha Amri za Mwenyezi Mungu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِنْكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ﴾ [البقرة: 151]

"Kama Tulivyowaletea mjumbe anayetokana nanyi, anawasomea Aya zetu, na kuwasafisha na uchafu wa ushirikina na tabia mbaya, kuwafundisha Kitabu, Sunna na hukumu za Sheria na kuwafundisha habari za Mitume na visa vya umma zilizopita, mambo ambayo mlikuwa hamyajui". [Suratil Baqara: 151]

Na kiuhalisia kwa hakika kumfuata hakuwezi kuwa isipokuwa kwa elimu na kufuata mwenendo wake, na vitendo vyake ni sehemu ya sunna zake ndani yake kuna kiigizo kwa waumini na hali zao zote, hivyo basi yeye ni kiigizo kwa walinganiaji kwenye kubeba matatizo na kazi nzito na kuwa na malengo ya hali ya juu na kupendelea watu yaliyo ya kheri na kuwaonea huruma.

Pia ni kiigizo kwa wana Ndoa kwenye kufanyiana miamala na kuoneana huruma na upole na kupendana kikweli.

Na kwa wenye vyeo na uongozi ni kiigizo katika uongozi, na kuyapa kipaumbele maslahi ya umma, na kuwaonea huruma watu, na kujiepusha na umimi, na kuchunga amana na kufanya mambo kwa moyo safi, na kuongoza kwa namna ambayo inamridhisha Allah, na kufanya mambo yenye maslahi zaidi kwa watu katika kazi zao.

Na kwa upande wa majirani yeye ni kiigizo chema katika kujua haki zao, na kuamiliana vizuri na majirani, na kuwaonea huruma na kuwaongoza na kuzihifadhi haki zao na kuungana nao kwa wema.

Na kwa wenye kusuluhisha yeye ni kiigizo chema, na kuwa na malengo ya hali ya juu na kuyapangilia mambo kwa mujibu wa vipaumbele, na mabadiliko ya kijamii kwenye mambo yenye maslahi zaidi kiutaratibu na kiutendaji, na kuwa na pupa ya maendeleo ya mwanadamu, na kuzihifadhi haki zake.

Na yeye kwa wazazi ni kiigizo chema kwa upole, na malezi na huruma, na mapenzi ya ukweli na mafunzo, na ni kiigizo kwa mafukara kwenye kusubiri njaa na kuwa msafi na muaminifu, na

kwa Matajiri ni kiigizo chema kwenye Sadaka na unyenyekevu, na kujitolea na kuchunga amana na kutekeleza ahadi, na kutofanya ubadhirifu, na kwa mgonjwa ni kiigizo kwa upande wa kutaka thawabu, na kutafuta ujira na kuzisaka dawa katika vile alivyo vihalalisha Mwenyezi Mungu na kutowatia uzito watu wengine.

Na kwa ujumla Mtume ni kiigizo chema kwa mwenye kutarajia kukutana na Mola wake na siku ya mwisho, ni kiigizo kwa umma wote, na tunakumbusha kuwa bila kuwa na elimu haiwezekani kumuiga.

Katika kuisoma Historia yake -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- ni kuthibitisha kumpenda kwake.

Hivyo kumpenda kunatangulizwa kuliko kuipenda nafsi na kumpenda yeye ni kuzipenda tabia zake na mema yake, upendo wa mwenye kufanyiwa wema kwa mwenye kufanya wema kwa kumsifu na kumtukua na kumuheshimu, kwanini isiwe hivyo na hali ya kuwa wema wake upo kwa ajili ya waislamu na wanadamu wote mpaka siku ya kiyama, kutokana na kuwabebea muongozo wa Mwenyezi Mungu, hivyo mapenzi yake ni makubwa na yapo katika ngazi ya juu zaidi, naye ni katika watu wenye athari kubwa zaidi katika maisha yetu, ili tutekeleze baadhi ya haki zake zilizopo kwetu na kumtanguliza kuliko nafsi zetu, na kuliko kitu kingine chochote, ili tuchukue toka kwake na kutanguliza maamrishi yake kabla ya mtu mwingine, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ ﴾ [الحشر: 7]

(Na yale yote aliyokuleteeni Mtume basi yachukueni) [Al-Hashr 7]. Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: ((Na ninamuapia yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake hawezi kuwa na imani mmoja wenu mpaka mimi niwe ni mwenye kupendeka kwake zaidi kuliko mtoto mzazi na wake zake, na katika mapokezi mengine: na kuliko watu wote)) (4)

Na vilevile tunabaini Fadhila za Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- na fadhila zake Mwenyezi Mungu kwetu sisi.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدَىٰ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿52﴾ صِرَاطَ اللَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ أَلَا إِلَى اللَّهِ تَصِيرُ الْأُمُورُ ﴿53﴾﴾ [الشورى: 52-53]

"Na kama vile tulivyowapelekea wahyi Manabii kabla yako wewe, ewe Nabii, tulikuletea wewe wahyi wa Qur'ani itokayo kwetu, hukuwa unajua kabla yake ni vitabu vipi vilivyotangulia wala nini Imani wala zipi Sheria zinazotokana na Mwenyezi Mungu, Lakini tumeifanya Qur'ani ni mwangaza kwa watu ambao kwao tunawaongoza waja wetu tunaowataka kwenye njia iliyolingana sawa. Na hakika wewe, ewe Mtume, unaelekeza na kuongoza kwa amri ya Mwenyezi Mungu kwenye njia iliyolingana sawa, nayo ni Uislamu, njia ya Mwenyezi Mungu Aliye na mamlaka ya vyote vilivyoko mbinguni na vilivyoko ardhini, hana mshirika katika hayo. Jua utanabahi kwamba kwa Mwenyezi Mungu , enyi watu, yatarudi mambo yenu yote ya kheri na ya shari, na huko Amlipe kila mtu kwa matendo yake, yakiwa mema alipwe wema na yakiwa mabaya alipwe ubaya". [Surat Shuura: 52-53]

Na ni mashuhuri kwa waislamu wote, Umuhimu wa kuisoma Historia ya manabii bali kwa waliowatangulia katika umati pia wanajua umuhimu wake.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَقَدْ كَانَ فِي قَصصِهِمْ عِبْرَةٌ لِأُولِي الْأَلْبَابِ مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَىٰ وَلَٰكِن تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ كُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿111﴾﴾ [يوسف: 111]

"Kwa hakika kwenye habari za Mitume tulizokuelezea na mambo yaliyowakumba wenye kukanusha kuna mawaidha kwa wenye akili timamu. Hii Qur'ani haikuwa ni habari ya uongo iliyozuliwa,

lakini tumeiteremsha ikiwa ni yenye kutolea ushahidi ukweli wa vitabu vilivyoteremshwa vilivyotangulia na kwamba vinatoka kwa Mwenyezi Mungu, na ikiwa ni ufafanuzi wa kila ambalo waja wanalihitaji la kuhalalishiwa na kuharamishiwa, linalopendeza na linalochukiza na mengineyo, na ikiwa ni muelekezo kutoka kwenye upotevu na ni rehema, kwa wenye Imani, ya kuzifanya nyoyo zao ziongoke, wapate kuyafuata kivitendo maamrisha na makatazo yaliyomo". [Surat Yusuf: 111]. Na kwa kujua kwetu Historia ya Bwana Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-*tunazijua umati mbalimbali ambazo zilihukumu ulimwengu na zikapata hadhi, kisiasa au kifikra na kidini na kitabia, na tunazijua neema ambazo uislamu umezileta kwa watu, kama alivyosema Omar -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. (Hawezi kuujua uislamu asiye jua enzi za ujinga).

Hakika ukweli katika Historia ya Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-* haiwezi kufananishwa na toleo lolote la kihistoria linalozungumzia utu vyovyote utakavyokuwa utu huo hauwezi ukafananishwa na utu wake Mtume.

Hivyo sisi kwa kujifunza Historia, tunajifunza ukweli na siyo uongo kama inavyotokea kwa baadhi ya watu, kama ambavyo sisi tunafikia uwazi na uhakika ambao haupatikani kwa yeyote asiyekuwa Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-*

Na ni lazima tujuwe yakuwa utajo wake -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-* ulikwisha tangulia zamani, pale ambapo ilikuwa kutajwa kwake Mtume kulikuwa ni katika zama zilizotangulia, na katika wakati wa Nabii Issa -Amani iwe juu yake- anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ بِنَتِيِّ إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ
التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ
مُبِينٌ ﴿٦﴾ [الصف: 6]

"Wakumbushe ewe Mtume, watu wako pindi Iṣṣā, mwana wa Maryam, alipowaambia watu wake, «Mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenu, ni mwenye kusadikisha Taurati iliyokuja kabla yangu na ni mwenye kushuhudia ukweli wa Mtume atakayekuja baada yangu, jina lake ni Ahmad, naye ni Muhammad, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na ni mwenye kulingania watu wamuamini, basi alipowajia Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kwa Aya zilizo wazi walisema, «Huu ni uchawi wazi wazi.» [Surat swaffi: 6]

Kama alivyosema Mussa -Amani iwe juu yake- katika zama zake-anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُمْ
بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبَائِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ
إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۗ فَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَاتَّبَعُوا النُّورَ الَّذِي أُنزِلَ
مَعَهُ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾ [الأعراف: 157]

"Rehema hii nitawaandikia wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu na kujiepusha na mambo ya kumuasi, na wanaomfuata Mtume aliye Nabii, ambaye hasomi wala haandiki, naye ni Muhammad, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani imshukie, ambaye wanazipata sifa zake na mambo yake yameandikwa huko kwao katika Taurati na Injili; anawaamrisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtii na kila lijulikanalo kuwa ni jema, na anawakataza ushirikina na maasia na kila lijulikanalo kuwa ni baya, na anawahalalishia vyakula na vinywaji vizuri na kuoana, na

anawaharamishia vichafu vya hivyo kama nyama ya nguruwe na vile ambavyo walikuwa wakijihalalishia miongoni mwa vyakula na vinywaji ambavyo aliviharamisha Mwenyezi Mungu, na anawaondolea wao mambo magumu waliokalifishwa nayo kama kukata mahali pa najisi nguoni, kuzichoma moto ngawira, ulazimu wa kisasi juu ya aliyeya kwa kukusudia au kwa kukosea. Basi wale ambao walimuamini Nabii asiyejua kuandika wala kusoma kilichoandikwa, Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani imshukie, na wakaukubali unabii wake, wakamheshimu, wakamtukuza na wakamuhami na wakaifuata Qur'ani aliyoteremshiwa, wakaufuata mwendo wake kivitendo, hao ni wenye kufaulu kwa kupata yale ambayo Mwenyezi Mungu Aliwaahidi waja wake Waumini". [Al A'raf: 157]. Kwa hakika habari za Muhammad -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani*- na sifa zake zilijulikana kabla ya kuzaliwa kwake kwa karne nyingi, pale ambapo maulamaa wa kiyahudi na kinaswara walipokuwa wanasubiri kutumwa kwake, na wala hakujaacha kuwa na ishara zenye nguvu na zilizo wazi za Mtume wa Mwenyezi Mungu katika vitabu vya manaswara kuwa Mtume ni Nabii wa zama za mwisho³

Kwa kuisoma Historia tunapata kukijua kitabu cha Mwenyezi Mungu kilichojaa matukio ambayo Qur'ani iliteremka kwa ajili yake kutoka katika kitabu cha Mwenyezi Mungu -kutakasika na machafu ni kwake na mtukufu- katika matukio mbali mbali.

Kama vile ambavyo baadhi ya majina ya sura katika Qur'ani tukufu yamefungamana na matukio ya kihistoria, kama ilivyo katika

³ Angalia: Maudhui yenye kuhusiana na (Ulimwengu na kumsubiri Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani), katika kitabu hiki.

Surat Anfaal, Tauba, Israa, Twaha, Ah'zaab, Ash-sharhu, Al'alaq', Al-humaza, Quraish, Al-kauthar, Al-kaafiruun, An-nasru, na Al-falaq.

Pamoja nakuwa sura zilizobakia hazikosi Aya zenye mafungamano na matukio ya kihistoria.

Na pamoja na hivyo, basi kusoma Historia yake kunampa mwanadamu twaswira sahihi ya kilichokuja katika kitabu cha Mwenyezi Mungu kutokana na sababu ya kuteremka Aya, na humpa mtu hisia fulani kama vile anaishi zama za kuteremka Qur'ani, na changamoto ambazo zilimpata Mtume wa Mwenyezi Mungu - Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani), na zilizoupata umma na jamii ya kiislamu, na historia humpa mwanadamu Taswira ya namna gani ambavyo Mwenyezi Mungu alizifanya imani zao kuwa thabiti kwa kile walichokishuhudia katika matukio waliyoyajua kwenye Qur'ani waliyoteremshiwa katika kipindi kile.

Hakika katika kuisoma Historia kuna kujua kizazi cha maswahaba -Radhi za Allah ziwe juu yao- nakujua ubora wao na hukuza mapenzi ya kuwapenda, na kujua vyeo vyao ambavyo Mwenyezi Mungu ameviaشيرia katika maneno yake:

﴿وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلِلَّهِ مِيرَاتُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا يَسْتَوِي مِنْكُمْ مَنْ أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَتْلَ أَوْلِيَاءِ اللَّهِ أَعْظَمَ دَرَجَةً مِنَ الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدِ وَقَتْلُوا وَكَلَّا وَعَدَّ اللَّهُ الْحَسَنَىٰ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ﴾ [الحديد: 10]

{Na mna nini hamtoi katika njia ya Mwenyezi Mungu na urithi wa mbingu na Ardhi ni wa Mwenyezi Mungu, hawawi sawa miongoni mwenu wale waliotoa kabla ya kushinda na wakaendelea kupigana, hao wanadaraja kubwa zaidi kuliko wale waliotoa baadae na wakapigana, na Mwenyezi Mungu amewaahidi wema wote hao ahadi nzuri, na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda} [Surat Al- hadiid: 10]

Na ameweka wazi Imamu Bukhari na wengineo katika kitabu chake sahihi Fadhila za hawa maswahaba.{6}

Haya maneno yametoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Mussa akawapa habari wana wa israil kabla ya miaka alfu moja iliyopita tangu kutumwa kwake Mtume - Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani), Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ الَّذِي الْأُمِّيَّ﴾ [الأعراف: 157]

{Wale ambao wanamfuata Mjumbe ambaye ni Nabii asiyejua kusoma wala kuandika} [Al A'raf: 157].

Hao ndio wanafunzi wa Muhammad -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani, ambao miongoni mwao walikuwa ni makhalifa waongofu na viongozi wenye uzoefu na wanasiasa na mashujaa wenye kukomboa miji, na ni wasomi waliouongoza ulimwengu na wakaleta uadilifu na Tauhidi na huruma.

Na kwa kuisoma historia tunatambua mambo maalumu kwa Mtume (7) ambayo Mwenyezi Mungu amemneemesha Mtume wake.

Mambo maalumu kwa ajili yake tu ni mengi, jambo la kwanza ni kuwa na huruma kwa viumbe vyote, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾ [الأنبياء: 107]

"Na hatukukutuma, isipokuwa uwe ni Rehema kwa watu wote" [Al Anbiyaa: 107]. Na

amesema Allah Mtukufu:

﴿وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّىٰ نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلَ اللَّهِ ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ ﴿١٢٤﴾﴾

[الأنعام: 124]

"Na pindi inapowajia washirikina hawa, miongoni mwa watu wa Maka, hoja iliyo waziwazi juu ya unabii wa Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, wanasema baadhi ya wakubwa wao, «Kamwe hatutaukubali unabii wake mpaka Mwenyezi Mungu atupe unabii na miujiza mfano wa Aliyowapa wajumbe wake waliotangulia» Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Aliwajibu kwa neno lake.: "Mwenyezi Mungu Anajua zaidi wapi auweke ujumbe Wake.» Kwa maana kuwa anawajua wale wanaofaa kubeba ujumbe Wake na kuufikisha kwa watu. Utawapata unyonge wakiukaji mipaka hawa, na watakuwa na adhabu iumizayo ndani ya Moto wa Jahannamu kwa sababu ya vitimbi vyao kwa Uislamu na watu wake". [An-aam: 124] Hivyo yeye ni mwanadamu mtukufu, Amemuelimisha na kumfundisha adabu Mola wa walimwengu wote kama alivyosema Mtume - Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani) ((Alinifunza adabu Mola wangu na akaifanya adabu yangu kuwa nzuri zaidi))⁴.

Alimchagua Mwenyezi Mungu na kumteua, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

⁴ Hadithi hii wameifanya kuwa ni Hasan idadi kubwa ya maulamaa, na inaushahidi mwingi, angalia matokeo yake kwa: Imam Ahmad Al-Haddad katika kitabu kiitwacho, Akhlaaq Nabiy fil qur'an wa Sunnah juzuu ya 2/ik 1033

﴿هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا مِن قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ﴾ [الجمعة: 2]

"Mwenyezi Mungu, kutakasika na kila upungufu ni Kwake, Ndiye Aliyetuma kwa Waarabu, wasiojua kusoma wala kuandika Mtume anayetokana na wao aliyetumwa kwa watu wote, ili awesomee Qur'ani na awatakase wao na itikadi mbovu na tabia mbaya, na awafundishe wao Qur'ani na Sunnah. Na wao, kwa kweli, tangu alipokuwa hajatumilizwa, walikuwa kwenye ukengeukaji ulio waziwazi kwa kuwa kando na haki. Na Mwenyezi Mungu, kutakasika na kila upungufu ni Kwake", [Suratil Jum'aa: 2]

Ni wa mwisho katika manabii, na ni mtu mwenye huruma zaidi kuliko wote, na ni mkarimu kuliko wote, na ni mkweli zaidi, na msafi zaidi, na ni mtakasifu kuliko watu wote.

Alitiwa nguvu kwa miujiza na ufafanuzi na dalili na karama nyingi, walishuhudia hayo walioishi naye zama hizo na wakaikuta miujiza hiyo maulamaa na vipenzi vyake, utajo wake umekuwa wa kiwango cha juu kuliko viumbe wote kwa haki alizokuwa nazo, na kwa kile alichomuahidi mkweli aliyetakasika na kutukuka.

Mwenyezi Mungu anamrehemu na malaika humuombea rehema, na amewaamrisha waja kufanya jambo hilo, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾ [الأحزاب: 56]

"Hakika Mwenyezi Mungu Anamsifu Nabii, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, mbele ya Malaika waliokurubishwa. Na Malaika Wake wanamsifu Nabii na wanamuomba kwa Mwenyezi Mungu, basi enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkazifuata sheria Zake

kivitendo, mswalieni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mtakieni amani, kwa kumwamkia na kumtukuza. Na namna ya kumswalia Nabii, rehema na amani zimshukie, imethibiti kwenye Sunnah kwa aina mbalimbali, miongoni mwazo ni: «Ewe Mola! Mrehemu Muhammad na watu wa Muhammad, kama ulivyowarehemu watu wa Ibrāhīm, hakika wewe ni Mwingi wa kushukuriwa ni Mwingi wa kutukuzwa. Ewe Mola! Mbariki Muhammad na watu wa Muhammad kama ulivyowabariki watu wa Ibrāhīm, hakika wewe ni Mwingi wa kushukuriwa, ni Mwingi wa kutukuzwa.» [Ah zaab: 56].

Mwenyezi Mungu amemfungulia na amemnusuru na kumsamehe madhambi yake, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾ لِيُغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٢﴾﴾ [الفتح: 1-2]

"Sisi tumekufungulia wewe, ewe Mtume, ufunguzi ulio waziwazi, ambao ndani yake Mwenyezi Mungu Ataipa nguvu Dini Yako na Atakupa ushindi juu ya maadui wako" [1]
 "Tumekufungulia ufunguzi huo na tukakufanyia sahali, ili Mwenyezi Mungu akusamehe dhambi zako zilizotangulia na zitakazofanyika baadaye, kwa sababu ya utiifu mwingi ulioufanya unaotokana na ufunguzi huu na kwa usumbufu ulioubeba, na ili Akutimizie neema zake kwako kwa kuipa ushindi dini yako" [2]
 [Suratul Fat'hi: 1-2].

Hakika kusoma Historia ya Mtume kunaipa nguvu azma ya muumini na huwafunza Subira na huwafungulia matarajio ya haki kuishinda batili, na dini ya Mwenyezi Mungu kuzishinda dini zingine zisizokuwa uislamu, na huwapa matarajio ya kuwa na nguvu na kuondoka na udhaifu, na kuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye kuinusuru dini yake na mtume wake na umma wake mpaka siku ya kiamaa.

Hakika Historia ya Mtume ni elimu yenye kujitegemea, na ni ufunguzi wa elimu mbalimbali, na ndani ya historia hiyo ya mtume muislamu hujifunza tabia na namna ya kuitekeleza tabia hiyo na hujifunza itikadi na misingi yake, na pia hujifunza hukumu za kisheria na kuchunga adabu, na hujifunza uadilifu na nidhamu za uislamu na siasa zake za kisheria na kuwavuta watu kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu.

Kama ambavyo wanajifunza wenye kusoma Historia ya Mtume mambo mengi ya uhakika ambayo yanafungamana na matukio ya kihistoria.

Na hupata kujua mwanadamu mapito mbalimbali ya maisha ya Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- na kuyaingiza mapito hayo katika kulingania kwake.

Namna ya kuisoma Historia ya Mtume.

Hakika kila mfanya uchunguzi au msomaji wa Historia ya Mtume anapaswa kuwa na hisia ya utu wa Bwana Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- na haki alizonazo, na mambo maalumu ambayo Mwenyezi Mungu amempa, amemchagua kati ya viumbe vyake kwa ajili ya wahyi wake na ujumbe wake, na amempa hifadhi madhubuti isiyokuwa na shaka katika dini na tabia katika utakasifu wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu -kutakasika na machafu ni kwake- na kumuhifadhi na kufanya ushirikina, na kusema uongo kabla ya kupewa utume na baada yake, katika uadilifu na usawa na kutekeleza kwake amana na kuwaonea watu huruma kabla ya utume na baada yake, katika kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu na kumuhifadhi na kuwa na heshima nae kabla ya kupewa utume na baada yake tangu kuzaliwa kwake -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- na haipaswi kwa yeyote kumkosoa Mtume -Rehema za Mwenyezi

Mungu ziwe juu yake na amani- isipokuwa kwa yale makosa aliyoyataja Mola wake Mtukufu katika sehemu ya kumfunza Heshima, kama ilivyotokea kwenye kisa cha kipofu kilichopo katika surat Abasa, au mateka wa Badri, au katika yale aliyoyataja yeye Mtume, na wala haikubaliki kwa yeyote katika wanadamu kumkosoa kwa mambo ambayo hayakutajwa.

Na kinachofuata, kwa hakika kwa mwenye Historia anapaswa kulazimiana na kumuheshimu Mtume wakati anapo mzungumzia, na kuwa na heshima na Historia yake na haki zake na kumpenda yeye - *Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-* na kuheshimu haki alizonazo kwenye nafsi zetu na nyoyo zet, na ni lazima kufungamana na dalili za kisheria, na kukumbuka yaliyokuja katika kitabu cha Mwenyezi Mungu- kutakasika na machafu ni kwake- na kuheshimu yale aliyotufahamisha Mtume wa Mwenyezi Mungu - *Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-* kuwa yeye ni mja wa Mwenyezi Mungu, lakini yeye ni bora zaidi ya wanadamu wote kama alivyosema -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani:* ((Mimi nitakuwa Bwana wa watoto wa Adam siku ya kياما na wala sijifaharishi, na mkononi mwangu kutakuwa na bendera ya shukurani na wala sijifaharishi, na hatokuwa Nabii yeyote siku hiyo kuanzia Adam na asiyekuwa yeye isipokuwa atakuwa chini ya bendera yangu, na mimi nitakuwa wa mwanzo atakaye pasukiwa na Ardhi))⁵

⁵ Ameipokea Tirmidhiy katika sahihi yake. mlango unaozungumzia Ubora wa Mtume -*Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-* Hadithi namba (3615) na akapokea Bukhariy sehemu kutoka katika hadithi hiyo katika sahihi yake, kitabu cha tafsiri ya surat Israa. na Muslimu katika kitabu cha Imani. Ibnu Kathiir, Tafsiri ya surat Israa, juzuu2/1085.

Na katika chujio la watukufu yeye ndiye wa mwanzo hakuna yeyote wa kumshinda, lakini yeye Mtume Rehema za Mola wangu na amani zake ziwe juu yake, ametilia mkazo kuwa yeye ni mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama ilivyopokelewa katika Aya nyingi zitokazo kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu kama katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنَ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾ [الإسراء: 1]

"Mwenyezi Mungu Anajisifu na kujitukuza kwa uweza Wake juu ya yasiyowezekana na yeyote isipokuwa yeye, hapana Mola isipokuwa yeye, hapana Mlezi isipokuwa yeye. Yeye ndiye ambaye Aliyempeleka mja Wake Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kipindi cha usiku, kwa mwili wake na roho yake, akiwa macho hajalala, kutoka msikiti Mtukufu Uliyoko Makka, kwenda msikiti wa Aqṣā uliyoko Bayt al- Maqdis, ambao Mwenyezi Mungu Amezibariki sehemu zinazouzunguka kwa matunda, nafaka na vinginevyo, na Akaufanya ni mahali pa Manabii wengi, ili ajionee maajabu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu na dalili za upweke wake. Hakika Mwenyezi Mungu, Aliyetakata na kutukuka, Ndiye Mwenye kuzisikia sauti zote, Ndiye Mwenye kukiona kila cha kuonekana, na Atampa kila mmoja anachofaa kupata duniani na Akhera". [Surat Israa: 1] Na unakuja utiliaji mkazo kuhusu kuwa ni mja katika sehemu ya hadithi inayohusu kuinuliwa kwake na kwenda kwake safari ya usiku, ili asijitokeze mtu mwenye kwenda katika njia ya imani ya manaswara akamtoa kwenye uanadamu wake, wakituka mipaka kama walivyopituka mipaka kwa Issa -Amni iwe juu yake- kwa kutaja karama hizi za kipekee za Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- ndio unakuja utiliaji mkazo wa kuwa kwake ni mja wa Mwenyezi Mungu:

﴿سُبْحٰنَ الَّذِيْٓ اَسْرٰى بِعَبْدِهٖٓ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اِلَى الْمَسْجِدِ الْاَقْصَا الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهٗ لِنُرِيَهُٓ مِنْ ءَايٰتِنَاۤ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيْرُ﴾ [الإسراء: 1]

"Mwenyezi Mungu anajisifu na kujitukuza kwa uweza wake juu ya yasiyowezekana na yeyote isipokuwa yeye, hapana Mola isipokuwa yeye, hapana Mlezi isipokuwa yeye. Yeye ndiye ambaye aliyempeleka mja wake Muhammad, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kipindi cha usiku, kwa mwili wake na roho yake, katika hali ya kuangaza na siyo ya kulala, kutoka msikiti wa Ḥarām Uliyoko Makkah, kwenda msikiti wa Aqṣā uliyoko Bayt al- Maqdis, ambao Mwenyezi Mungu Amezibariki sehemu zinazo uzunguka kwa matunda, nafaka na vinginevyo, na Akaufanya ni mahali pa Manabii wengi, ili ajionee maajabu ya uweza wa Mwenyezi Mungu na dalili za upweke wake. Hakika Mwenyezi Mungu, Aliyetakata na kutukuka, Ndiye Mwenye kuzisikia sauti zote, Ndiye Mwenye kukiona kila cha kuonekana, na Atampa kila mmoja anachofaa kupata duniani na Akhera". [Surat Israa 1] Pamoja nakuwa lau ingetajwa Aya kupelekwa kwa Mtume ingelikuwa ni kweli, lakini Aya inatilia mkazo nafasi ya kuwa mja ambaye kwake yeye ni takirima na kwa wanadamu wote, kama ilivyokuja katika kauli yake -kutakasika na machafu ni kwake: Sema, ewe Mtume, kuwaambia hawa washirikina,

﴿قُلْ اِنَّمَا اَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحٰى اِلَيَّْ اِنَّمَا اِلٰهُكُمْ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهٖ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صٰلِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهٖۤ اَحَدًا﴾ [الكهف: 110]

«Kwa kweli, mimi ni binadamu kama nyinyi, ninaletewa wahyi kutoka kwa Mola wangu kwamba mola wenu ni Mola Mmoja. Basi yeyote anayekuwa ni mwenye kuiogopa adhabu ya Mola wake na ana matumaini ya kupata malipo yake mazuri siku ya Kiyama, basi na atende matendo mema na asimshirikishe yeyote pamojanaye katika ibada.» [Suratul Kahaf: 110]. Hali ya kukumbusha Uja wake

kwa Mwenyezi Mungu na pamoja na hivyo hakika nafasi yake hakuna yeyote awezaye kuifikia, Hivyo muislamu asimtangulize yeyote katika wanadamu, si mke wala watoto wala wasiokuwa hao katika kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu alimkirimu kwa kumfanya kuwa mja pamoja na kumchagua kwa kumpa wahyi na ujumbe, na katika hili hakuna udhaifu wala kumdhaliisha Mtume wa Mwenyezi Mungu, bali huo ni ukamilifu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani kuwa kwake ni mja, lakini si kama waja wote kwakuwa Mtume alikuwa ni mja mwenye kushukuru kama alivyosema Rehema za Mola wangu na amani zake ziwe juu yake -kumuambia Aisha - Radhi za Allah ziwe juu yake- pindi alipomuona akisimama usiku anaswali mpaka miguu yake inachanikachanika, kana kwamba Aisha alikuwa akimuashiria Mtume kuwa yatosha, akasema Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- ((Hivi kwanini nisiwe ni mja mwenye kushukuru)),⁶Hakusema Nabii mwenye shukurani wala Mtume mwenye shukurani, kwa sababu yeye anaona kuwa miongoni mwa ukamilifu wa unabii wake ni yeye kuwa mja wa Mwenyezi Mungu, na hilo ni kwa kusadikisha kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿بَلَىٰ لِلَّهِ فَأَعْبُدْ وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِينَ﴾ [الزمر: 66]

"Bali Mwenyezi Mungu muabudu, ewe Mtume, kwa kumtakasia ibada Peke yake asiye na mshirika, na uwe ni miongoni

⁶ Kutoka katika hadithi ya Bukhariy, katika Dibaji, mlango wa kisimamo cha usiku, na Muslimu katika sifa za kisimamo" mlango wa kukithirisha matendo na kujitahidi kufanya ibada" namba: (2820)

mwa wenye kuzishukuru neema za Mwenyezi Mungu". [Surat Zumar: 66]

Lakini yeye Mtume ni bwana wa wanadamu, na yeye ni kiigizo chema, alikuja ili awaongoze kuwa waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu -Mtukufu- peke yake, na akawa Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- mbele yao katika amri za Mwenyezi Mungu.

Alikuwa akiishi maisha ya mwanadamu, na analala na anaoa na ananunua na kuuza na kufanya urafiki na uadui yote hayo ni yenye kuingia katika kuwa kwake mja wa Mwenyezi Mungu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾ [الأنعام: 162]

Sema, «Hakika Swala yangu na kuchinja kwangu wanyama, na uzima wangu na kufa kwangu yote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu muumba wa walimwengu wote". [Al-an-aam 162].

Hakika yeyote mwenye kuisoma Historia ya Bwana Mtume na matukio yake anapaswa kuishi zama alizoishi Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- na uwezo wake na hali yake ili afahamu mazito yaliyokuwa yakimpata yeye na maswahaba zake, na ajue hali ya hewa na nyuzi joto ya wakati ule, na ajue kiasi cha uzalishaji wa mimea na mifugo na ajue uchumi wa mkoa wake na ukomo wa uwezo wake wa hali na mali, na uchumi wa asili katika mazingira yake kisha alinganishe na sehemu nyingine.

Kama ambavyo yampasa kujua hali ya kijografia pamoja na Ada na tamaduni na hali za waarabu kabla ya uislamu, ni katika mambo ambayo yatamfanya awe na taswira sahihi ya hali ambayo alikuwa akiishi nayo bwana Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani, ili ampe haki yake ya kumuheshimu yeye na maswahaba zake -Radhi za Allah ziwe juu yao wote-.

Na ni wajibu juu yake kufahamu mapito mbalimbali ya Historia ya Bwana Mtume na ulinganiaji wake.

Kama ilivyowajibu kwa mwenye kuisoma Historia kufungamanisha matuko ya Historia na yaliyopokelewa kutoka katika kitabu cha Mwenyezi Mungu -Kutakasika na machafu ni kwake- na arejee kwenye vitabu vya Tafsiri na sababu za kuteremka Aya ikiwa jambo lithitajia kufanya hivyo.

Kama vile ambavyo inapaswa kufungamanisha Historia na matukio ya kisasa katika jamii ya kiislamu na jamii ya watu wote⁷ na zama za Mtume na kuathiri zama zetu, na kujua mwenendo wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake.

Kama ambavyo inampasa kujua kuwa yeye yupo mbele ya mtu ambaye Allah amemchagua -kutakasika na machafu ni kwake na mtukufu- na ni haramu kumsingizia uongo, na akumbuke kauli ya Bwana Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: ((Yeyote atakayeningizia Uongo kwa makusudi basi ajiandalie makazi yake kuwa ni motoni))⁸

⁷ Angalia: Kitabu kiitwacho Sirrul khatmi Othman Ally,ufundishaji wa Historia ya Bwana Mtume katika silabasi za Historia za Madrasa, kimetolewa na Daarul uluum, Riyadh,1402 Ukurasa 35.

⁸ Wamewafikiana Bukhari na Muslim, kutoka katika riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, Kitabu cha Elimu, Mlango unaozungumzia madhambi ya mwenye kumsingizia Mtume uongo - *Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani*: Juzuu ya 1/ukurasa 36.

Na kifuatacho nikuwa Bwana Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani hana haja ya kusingiziwa uongo au kusemewa uongo.

Na mchunguzi wa elimu katika historia ya Bwana Mtume - Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani Anakuta kuwa historia imefunikwa na matukio yaliyochambuliwa kwa uyakinifu.

Na kwa hakika wengi katika Wajuzi wa elimu ya historia wanaichukulia historia ni elimu yenye kujitegemea yenyewe na walikuwa wanaiona ni sehemu katika sunna za Bwana Mtume.

Mambo maalumu yaliyoko kwenye Historia ya Bwana Mtume.

Hapana shaka kuwa Historia ya Bwana Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani ni Elimu tukufu itokanayo na utu wa aliyechaguliwa kutoka kwa Mola Mtukufu, na matukio yaliyoshuhudiwa na Qur'ani kwa kuteremka Aya nyingi zikisomwa mpaka siku ya mwisho, na kifuatacho ni kuwa Historia imetofautishwa kwa mambo maalumu miongoni mwake ni:

*Na kuwa mwenye Historia ni katika watu watukufu, Mwenyezi Mungu ameuinua utajo wake, na akamfunza adabu mpaka akawa ni Bwana katika watoto wa Adamu kwa ujumla, tangu kupatikana mwanadamu mpaka atakapo irithi Ardhi ya Mwenyezi Mungu na vilivyomo.

*Chimbuko la hali ya juu katika Historia hii ya Bwana Mtume yenye kutiliwa nguvu na Qur'ani tukufu katika mengi ya matukio yake, na vita vya Bwana Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani na tabia zake na sifa zake.

*Hakika Historia ya Bwana Mtume ndiyo bora zaidi katika Historia za manabii na wema kwa upande wa upambanuzi na ubora kwa vile walivyofuatilia maswahaba upande wa maisha yake yote ya

kibinafsi na kiujumla na wakayahamisha kwetu kwa njia iliyo bora zaidi isiyo na ukomo, kama vile ambavyo haikuwahi kunukuliwa Historia ya mwanadamu yeyote kabla yake Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani.

*Kwa hakika Historia ya Bwana Mtume ni Historia sahihi wanadamu walimfahamu mwenye Historia kuwa ni mkweli muaminifu -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: Waliinukuu wakweli kati ya maswahaba zake, walitambulika walioinukuu na zikawa sahihi cheni zao za upokeaji.

*Kwa hakika Historia ya Bwana Mtume imekusanya pembezoni mwake matendo ya Bwana Mtume ya kiibada na kidunia, na siasa ya kisheria na jihadi zake na vita vyake, na wote walioishi naye katika maswahaba mataifa na watu mbalimbali.

*Mafungamano ya Historia na matukio yake na tabia ya kijografia ni maalumu na ni zenye kujulikana, huchangia na kuupa nguvu ukweli wake na hutuwezesha kufuatilia matukio yake.

*Kwa hakika Historia ya Bwana Mtume imejaa mafunzo na mazingatio ambayo haswa kwa muislamu na kwa watu wote wanaweza kupata faida kwa hali yoyote ile aliyokuwanayo na cheo chake na wadhifa wake, ili aweze kufikia sababu za kufaulu, na kupata raha Duniani na Akhera.

*Hakika katika maisha ya Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na kulelewa na Mwenyezi Mungu wakati alipokuwa yatima na kuhifadhiwa na Mwenyezi Mungu na kuepushwa kwake na watu ni muujiza wenye kushuhudiwa, huleta hisia kupitia Historia ya Bwana Mtume na kupitia nusura ya Allah na uhifadhi wa dini yake na kuenea kwake na mapito ya maisha yake na da'awa zake, amesadikisha Mwenyezi Mungu katika maisha yake yale aliyomuahidi Mtume wake na waja wake wema katika zama zake.

Kwa hakika Historia ilitiliwa umuhimu mkubwa kutoka katika umma kuanzia wasomi na maulamaa wake na wataalamu wa maswala ya hadithi.

*Hakika ndani ya Historia kuna utekelezaji uliohai wa kujua mienendo ya Mwenyezi Mungu katika ulimwengu na maisha na nusura ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ﴾ [غافر: 51]

"Sisi tutawapa ushindi mitume wetu na wale waliowafuata, na tutawapa nguvu juu ya wale waliowaudhi katika uhai wa kiulimwengu na siku ya Kiyama, Siku ambayo watatoa ushahidi Malaika, Manabii na Waumini juu ya watu waliopita waliowakanusha Mitume wao; watatoa ushahidi kwamba Mitume walifikisha jumbe za Mola wao na kwamba watu hao waliwakanusha". [Suratul ghaafir :51].

*Hakika Historia ya Bwana Mtume ni Tiba kwa upande wa Maisha yote ya Mtume- Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾ [الأنعام: 162]

Sema,«Hakika Swala yangu na kuchinja kwangu wanyama, na uzima wangu na kufa kwangu zote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu muumba wa walimwengu wote" [Al an-am: 162] Na Historia huyaelezea maisha yake na sifa zake na mambo yake na huyafungamanisha na ujumbe wake na unabii wake na kuteuliwa kwake na Mwenyezi Mungu.

*Hakika Historia ya Mtume husimulia zama za mapinduzi ya kiulimwengu na kubadilisha maisha ya Mwanadamu, katika zama hizo za mapinduzi walihamishwa watu kutoka kwenye kuabudu

masanamu na kuhamia kwenye Tauhiid, na kutolewa kwenye shirki na kuelekea kwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu mmoja, na kutolewa katika zama za kabla ya uislamu na kupelekwa katika uislamu.

*Athari ya Historia ni kubwa kwa wenye kuisoma, na mchango wake ni mkubwa katika kuathiri tabia na kuisimamia na kuitakasa nafsi na tabia na kuilea katika kumpenda Mtume -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-**

*Kutoka katika Historia hufahamika mchango mkubwa wa maswahamba wa Bwana Mtume -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-** na kumnusuru kwao kwa nafsi na mali na watu, na mapenzi yao makubwa ya kumpenda Allah na Mtume wake, na kinachofuata ni kuwalinda na maadui zao wenye kuwadharau, na hao maswahaba ni vipenzi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wakwe zake, mfano Abuubakar na Omar, na Othman na Ally -Radhi za Allah ziwe juu yao, na Wamama wa waumini na wote waliobakia katika nyumba ya mtume na maswahaba ambao Allah amewaridhia na wao wamemridhia Allah.

Uzuri wa Historia ya Mtume na uhakika wake na ukamilifu wake na uhalisia wake na uzuri wa maisha ya mwenye Historia naye ni Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani.

*Hakika Historia ya Bwana Mtume ndiyo mapito sahihi ya kuifahamu Qur'ani tukufu, na Aya zilizoshuka kwa Bwana Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-** katika mapito ya maisha yake mbalimbali.

Hali za Waarabu katika zama zilizopo kabla ya uislamu.

Kutumwa kwa Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani kulichomoza Nuru na kufunika giza na ikapata hadhi Tauhidi elimu na maarifa, na pia haki na uadilifu, kwa hivyo ilitambulika kabla ya uislamu kwa kuitwa zama za ujinga ili kutofautisha zama za uislamu, na ili kujua ubora wa uislamu kwa ulimwengu wote na hasa kwa waarabu, ni lazima kuijua hali iliopo kabla kidogo ya uislamu katika nyanja zote, pale ambapo uislamu ulikuja kukusanya mambo yote ya kimaisha na siyo kwenda na mambo ya kidini peke yake, bali kwenda na mambo ya kidunia kwa kufuata tabia zake na miamala yake na Ada zake na sheria zake na mapito yake yote. Na kama ilivyokuwa kisiwa cha waarabu kwa ujumla ndicho kilichokuwa ni jukwaa la matukio ya kihistoria kwa daraja la kwanza, hivyo hapana budi kuzijua hali zake kabla ya kutumwa Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- Hivyo miji ya kiarabu kwa upande wa jografia ni visiwa vikubwa, ambavyo vinazungukwa na bahari pande zake tatu, upande wa magharibi kusini na mashariki, katikati yake kuna jangwa lisilozalisha chochote lenye uchache wa maji na chemchemu, na ikiwepo ndani yake sehemu zenye ukijani kibichi basi ni chache sana ukilinganisha na ukubwa wa eneo lake, lakini huzingatiwa ni sehemu yenye Rutuba yenye kuzalisha mazao, na hupatikana nchi ya Yemeni kwa upande wa kusini na nchi ya Oman, na hizo nchi mbili ziko katika sehemu za milima zenye kuzalisha mazao kwa kiwacho cha wastani yenye hali ya hewa iliyo nzito.

Upande wa Kidini:

Waarabu wengi walikuwa ni wapagani na ilienea kwao ibada ya kuabudu masanamu, na walikuwa wanavituo maarufu katika miji

yote ya kiarabu, wakienda katika miji hiyo kwa ajili ya ibada na kutoa sadaka na wakiyaomba hayo masanamu misaada kila mmoja kwa njia yake, na wala haukusalimika mji wowote katika miji ya waarabu mpaka Makka ambako ni sehemu ya utakasifu.

Walipatikana idadi kubwa ya mayahudi, wameweka makazi katika mji wa Madina uitwao (Yathribah) na katika mji wa Khaibar, ukiongezea na mayahudi wa Khaibar na Taimah na Fadaka na bonde la Quraa, ambao wanatengeneza mkusanyiko mkubwa.⁹

Kama ambavyo vilikuwepo baadhi ya vikundi vilivyokuwa vikijulikana kwa jina la (Al-mawaal) waislamu wasiokuwa waarabu, asili yao kwa kawaida inatokana na wasiokuwa waarabu, wakitokea katika sehemu mbalimbali zilizoendelea, na kwa hakika pasina kubagua yalishiriki makundi mengi kutoka kwa waarabu na mayahudi na waislamu wasiokuwa waarabu katika matukuio ya kihistoria ya mtume.

Kama vile ambavyo unaswara ulienea kwenye baadhi ya makabila ya waarabu, na ikawa mji wa Najrani ndiyo kituo muhimu katika miji ya kiarabu.¹⁰

Na walikuwa manaswara wa kiarabu ni kama manaswara wengine walipatwa na mtihani wa kwenda kinyume na mafundisho

⁹ Mtunzi Swaabir Twaima, Historia ya mayahudi kwa ujumla juzuu ya pili ukurasa 2/14.

¹⁰ Rejea kitabu cha Muhammad bin Iwadh Al-utaib, kiitwacho Najraan katika zama za mtume na makhalifa waongofu, na Reseach ya masters iliyotolewa na kitengo cha Historia na maendeleo, katika chuo kikuu cha kiislamu kiitwacho Muhammad bin Saud mwaka wa masomo 1430 H na bado Reseach hii haikusambazwa.

na wakageuka wakawa ni wapagani, wakimuabudu Nabii Issa mwana wa Mariamu na wakiwatukuza Makasisi wao na watawa, na wakizitanguliza amri zao kuliko za Mwenyezi Mungu.

Kwa hakika walijulikana Manaswara wa kiarabu kwa kuwa na elimu na maendeleo zaidi kuliko wenzao katika makundi, na wakabadilishana maendeleo yao na wa roma na waarabu wa Sham na Iraq na hasa hasa kizazi kitokanacho na kabila la Manaadhirat na Khasaasinat.¹¹

Maisha ya kijamii:

Kwa kawaida wengi huathiriwa na maisha ya kidini, na itikadi zilizotawala kwa hakika ilitawala kwa waarabu wote tabia ya unywaji wa pombe na kucheza kamari na kula Riba, kama ambavyo wanaume walikuwa hawawezi kuepukana na zinaa, Zinaa ambayo waungwana walikuwa wakiichukia.¹²

Kama vile ambavyo waarabu walikuwa wakichukia kuwarithisha watoto wa kike¹³ kama vile walivyokuwa na idadi kubwa ya wanawake pasina kuwa na kiwango maalumu, bali baadhi ya wanawake waliwa na wanaume wengi pia¹⁴

¹¹ Jawad Ally, Al-mufassswal katika Historia ya waarabu kabla ya uislamu juzuu 3/ukurasa 155, mpaka 387.

¹² Rejea Kitabu cha Mahmood Shukri al-aluusiy, Kitabu kiitwacho - Kufikia malengo katika kujua hali za waarabu, juzuu ya 2/uk 4.

¹³ Tafsiri Ibnu Kathiir. juzuu 1/uk 1116

¹⁴ Angalia kitabu kiitwacho Jawaadu Ally Al-mufassswal juzuu ya 539/5 na uangalie Hadithi ya Aisha katika Bukhariy, katika sahihi

Kama ambavyo walikuwa baadhi yao wakiwaoa wake za baba zao kwa kuwalazimisha, na walikuwa wakioa mtu na dada yake¹⁵

Na kwa hakika palikuwapo na baadhi ya tabia na tamaduni zilizokuwa nzuri kwa waarabu, miongoni mwazo ni Ushujaa, na upandaji Farasi na nguvu za asili na ujanja na kupenda uhuru.¹⁶

Ama kwa upande wa Lugha walikuwa waraabu wapo kileleni na ni mafasaha zaidi pamoja na kutofautiana mipaka ya Lahaja.¹⁷

Na ufafanuzi na ufasaha ni wa hali ya juu kwao.

Na kwa ajili hiyo umekuja muujiza wa Mtume -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, kikiwapa changamoto kwa upande ambao wana nguvu nao zaidi, kama ilivyokuwa ufasaha wa Bwana Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani katika mazungumzo yake ni yenye ufasaha wa hali ya juu, walishindwa kuleta mfano wake achilia mbali kuweza kuleta mfano wa hii Qur'ani au hata kuleta sura kumi mfano wake za kutunga) kama ilivyokuja katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

yake ,kitabu Nikaah, mlango usemao hakuna Ndoa bila walii juzuu 6/132

¹⁵ Angalia Tafsiri ya Ibnu Kathiir juzuu 1/453; Jawaadu Ally AL- Mufasswal juzuu5/529.

¹⁶ Jawaadu Ally AL- Mufasswal juzuu 5/402; Mahmood Shukri lalूसiy, Bulughul Maraam, juzuu 1/46

¹⁷ Shaukiy Dhaifu, Historia ya Adabu za waarabu katika zama za ujahiliya, ukurasa 123

﴿أَمْ يَقُولُونَ أَفْتَرَلَهُ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرِيَاتٍ وَادْعُوا مَنِ اسْتَضَعْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ﴾ [هود: 13]

"Au je, washirikina hawa, miongoni mwa watu wa Makka, wanasema kwamba Muhammad ameizua hii Qur'ani? Waambie basi, «Iwapo mambo ni kama mnavyodai, leteni sura kumi mfano wake za kuzuliwa, na muwaite mnaowaweza miongoni mwa viumbe wote wa Mwenyezi Mungu, ili wawasaidie kuzileta hizi sura kumi, iwapo nyinyi ni wa kweli katika madai yenu". [Hud: 13].

Hali ya ulimwengu kidini katika zama kabla ya uislamu.

Hapana shaka kuwa ulimwengu ni mkubwa na mpana na ni vigumu kuujua wote kwa ujumla, na kwa kutoa kipaumbele yawezekana kuzungumziwa sehemu zilizo karibu na miji ya kiarabu ambazo ziliathirika na zikaacha athari katika zama za Historia ya Bwana mtume na kwa hakika iliweka wazi Qur'ani tukufu na kwa ufupi hali ya ulimwengu kwa ujumla katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu

﴿ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ﴾ [الروم: 41]

(Uharibifu umedhihiri bara na baharini kwa sababu ya yale iliyoyachuma mikono ya watu ili awaonjeshe adhabu ya baadhi ya mambo waliyoyafanya huenda wakarudi) [Surat Ruum: 41]

Na kwa upande wa Dini ambao ndio msingi wenye kutoa hukumu kikawaida katika tabia za watu ambazo zilikuwepo katika dini mbili za mbinguni ambazo ni Uyahudi na Unaswara dini ambazo zilipewa elimu kitabu na Urithi.

Uyahudi:

Ni Dini ambayo waliichukua wafuasi wa Mussa -Amani iwe juu yake- ambaye anatokana na kizazi cha Yakobo -Israeil- pale alipoteremshiwa Taurati, na walikuwa kwenye Tauhidi na walipatikana kwao manabii katika wakati tofauti tofauti, na kwa hakika waliibadilisha Taurati na wakawauwa manabii wao pasina haki.

Na wakaenda kinyume na manabii wao na wakamkosea Mwenyezi Mungu adabu, na wakapata umaarufu wa kuwa wao ni watu waliopewa kitabu, kwakuwa walikuwa na Taurati na vitabu mbalimbali, vilivyokuwa karibu na haki kuliko upagani, na pamoja na hivyo walipata hasira za Mwenyezi Mungu kutokana na kumkosea Mwenyezi Mungu adabu.

Kama vile ambavyo waliwatukuza makasisi wao na wakatanguliza kauli zao kuliko kauli za Mwenyezi Mungu na Amri zake

Kama walivyoibadilisha Taurati kwa Makusudi.

Na pamoja na hayo walikuwa wakidai kuwa wakimsubiri atakaye kuja zama za mwisho ili wamfuata na waijue haki ambayo ametumwa nayo Muhammad-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Amani.

Unaswara:

Ni dini ya wafuasi wa Nabii Issa -Amani iwe juu yake- ni katika dini miongoni mwa dini zilizoenea katika zama hizi, nayo ni makundi mengi yalikuwa yameenea katika mji wa Shamu na Iraq Misri, Habash, na kusini mwa ulaya na mashariki, na ikisaidiwa na nguvu za kisiasa kijeshi na kimali kutoka kwa Roma.

Na ikapelekea taifa la Waroma kuingia katika Upagani na kuingiza ushirikina humo tangu karne ya Nne tangu kuzaliwa yesu kwa kupitia mikono ya {Costantin Mkubwa} walitoka katika kumuabudu Mungu mmoja na kuelekea kwenye kumuabudu Yesu, na ikawa

yeyote asiyemuabudu Yesu anakuwa katoka katika itikadi Rasmi ya Kanisa. Na nguvu za Kanisa kisiasa zinatokana na dola ya Roma na watumishi wake ni kutoka katika kabila la Ghasaasinah la kiarabu au wafale wa Ethiopia -Habash- na ikaingia kati ya Manaswara sintofahamu ya vipengele mbalimbali kuhusu Tabia ya Yesu na wakaanza wao kwa wao kukufurishana na wakipigana vita wao kwa wao na ukatokea mgongano kati ya Manaswara wa Roma na Manaswara wa Misri na kukawa na uadui kati yao.¹⁸

Na walikuwa Manaswara wa Kiarabu katika zama za ujinga wengi wao kutoka katika kizazi cha Yaaqiba¹⁹kama ambavyo walikuwa sehemu ya Manaswara wa Fursi na Waarabu hasa hasa katika nchi ya Iraki linatokana na taifa la Nestorian²⁰na wanatofautiana na Manaswara wa Roma.

Na kauli ya ujumla kwa kila wafuasi wa manaswara katika zama kabla ya uislamu -zama za ujinga- ni kuwa wao waliingia katika kuyaabudu masanamu kwa mlango mpana zaidi kabla ya kutumwa Mtume Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani.

Majusi - waabudu Moto:

Dini hiyo husimamishwa kwa kuabudu moto ndiyo kipaumbele chao cha mwanzo, na vyenye kuonekana kwa kawaida kama vile

¹⁸ Na kwa faida zaidi angalia Kitabu cha Historia cha Abuu Hassan al-Nadawiy kukurasa wa 26.

¹⁹ Kitabu kiitwacho Mausuuatu Muyassara fil adiyaan walmadhaahibu almuaasir, kimetolewa na Nad'wal aalamia lishabaabul islaamiy, mjini Riyaadh ukurasa 503.

²⁰ Tazama: Kitabu kiitwacho Mausuuatu Muyassara fil adiyaan walmadhaahibu almuaasir ukurasa 502

Nyota Jua na vinginevyo,²¹na walikuwa na majumba yao maalumu ya kufanyia ibada yaliyokuwa yameenea katika nchi ya Iran na miji yote ya kifursi, pale ambapo Dola ya kifursi inasimama na Majusi na ikuihami dini hii na kuisambaza katika pande zote za himaya ya Wafursi na wenye kunyenyekea wafursi, na kwa hakika dini ya Kimajusi iliingia katika miji ya kiarabu na ikaenea kwa kiwango cha juu katika maeneo ya Bahrain mashariki mwa visiwa vya kiarabu, pale walipopatikana kundi la wafursi ambao waliwaathiri wakazi wa sehemu ile, na zikaenea sehemu zao za kuabudia na vyenye kuendana na dini hiyo ikiwemo ngano za kale na Makuhani.

Na Zaraadishtia ilikuwa ni Dini ya kimajusi hapo zamani na kukasemwa kuwa Umajusi unatokana na Zaraadishtia²²

Budha:

Ni dini ya kipagani ya kuabudu masanamu inategemea zaidi kuabudu masanamu na wanayatengenezea mahekalu na majumba ya ibada na wanayatumia masanamu hayo Makuhani na wachawi na wafanyao mazingaombwe²³na dini hii ilienea katika nchi ya India na nyuma ya India kuanzia kusini na mashariki mwa Asia na China.

Na Dini huendeshwa kwa madai yao ya kuwepo kwa miungu wengi wenye kupingana. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَوْ كَانَ فِيهِمَا ءَالِهَةٌ إِلَّا لِلَّهِ لَفَسَدَتَا فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ﴾ [الأنبياء:

[22

²¹ Kitabu cha Historia cha Abul hassan An- nadawiy ukurasa wa 26

²² Kitabu Swafwat Siirat An-bawiy cha mtunzi Mahd Rizqullah ukurasa wa 51

²³ Kitabu cha Historia cha Abul hassan An- nadawiy ukurasa wa 28

"Lau mbinguni na ardhini kungelikuwa na miungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu, kutakata na sifa za upungufu ni Kwake na kutukuka ni Kwake, wenye kuyaendesha mambo yake, ungeliharibika mpango wake. Basi Mwenyezi Mungu, Bwana wa 'Arsh, Ameenpukakana na sifa za upungufu na Ametakasika na kila sifa ambayo wakanushaji makafiri wanamsifu nayo ya uongo, uzushi na kila aibu". [Al-anbiyaa: 22] Na kwa hakika Ubudha ulikuwa pamoja mahala pake na dini ya Kihindu, dini ambayo iliagamia kwa madai yake ya kuwepo kwa waungu wengi²⁴

Na pamoja ya kuwa upagani wa waarabu na Ibada ya masanamu ilikuwa imeenea katika sehemu mbalimbali katika miji ya waarabu, na hasa hasa katika mji wa Makka tukufu, ila mtazamo wa wa Falsafa haukuwa ni umekita kama ilivyokuwa kwa wengine wenye kuabudu masanamu, na waarabu hawakuwa na utamaduni ulioandikwa kuhusu miungu yao ya uongo, bali ilikuwa ni kawaida yao kufuata kibubusa tu kudai kuwa kufanya hivyo ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الخَالِصُ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ﴾
[الزمر: 3]

"Jua utanabahi kwamba ni haki ya Mwenyezi Mungu, Peke Yake, kutiwa utiifu uliyotimia uliosalimika na ushirikina. Na wale wanaomshirikisha mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu wakawafanya wasiokuwa Yeye kuwa ni wategemewa, wanasema, «Hatuwaabudu waungu hawa pamoja na Mwenyezi Mungu

²⁴ Kitabu cha Historia cha Abul hassan An- nadawiy ukurasa wa 29

isipokuwa wapate kutuombea kwa Mwenyezi Mungu na ili watukurubishe daraja Kwake.» Hivyo basi wakakufuru, kwani ibada na uombezi ni wa Mwenyezi Mungu, Peke Yake. Hakika Mwenyezi Mungu Atawapambanua, Siku ya Kiyama, baina ya Waumini wenye ikhlasi na wale wenye kumshirikisha mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, katika yale waliokuwa wakitofautiana juu yake kuhusu vile walivyoabudu. Hapo amlipe kila mmoja kwa anachostahiki. Hakika Mwenyezi Mungu hawaelekezi kuongoka kwenye njia iliyonyooka wale wenye kumzulia uongo Mwenyezi Mungu, wenye kuzikanusha aya Zake na hoja Zake". [Azzumar: 3].

Na walikuwa wakipinga kufufuliwa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ وَمَا لَهُم بِدَلِيلٍ مِنْ عِلْمٍ
إِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ ﴿٢٤﴾﴾ [الجاثية: 24]

"Na wanasema hawa washirikina, "Hakuna maisha isipokuwa haya maisha yetu ya duniani tuliyonayo; hakuna maisha mengineyo," kwa njia ya kukanusha kufufuliwa baada ya kufa. "Na hakuna kinachotuangamiza isipokuwa kupitiwa na masiku na michana na umri mrefu," wakikanusha kuwa wana Mola Anayewatowesha na kuwaangamiza." Na hawa washirikina hawana ujuzi wowote juu ya hilo, hawana lolote isipokuwa ni kusema kwa kudhania, kufikiria na kuwaza". [Al Jaathiya: 24].

Hali ya kisiasa katika zama zilizo kabla ya uislamu.

kwa inavyofahamika kwa kila mwenye akili, kuwa Mtume - **Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- alikuja na Dini ya upwekeshaji na kufanya Ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kuwa yeye alisimamisha Dola, akaiwekea utaratibu wa kuindesha kisheria na kidini, na akaisimamisha dola hiyo kwa uadilifu mpaka ikawa na misingi imara hadi mwisho wa maisha yake, dola hiyo iliweza baada ya kufa Mtume-**Rehema za Mwenyezi mungu ziwe juu yake na amani**-kuziangusha dola zilizoizunguka na baadhi yake kudhoofika na kutawala sehemu kubwa, ili kueneza tauhidi na kuwahuisha watu katika kumuabudu muumba wao baada ya kuwa waovu wamewaiba na wakawapoteza, na kinachofuata basi ni lazima kutilia umuhimu kwa haraka hali ya kisiasa ya miji ya waarabu na miji ya pembezoni mwake kabla ya kutumwa Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**.

Hali za Waarabu kisiasa:

Hapakuwepo na utaratibu maalumu uliokuwa wazi katika kisiwa cha waarabu na hasa hasa katikati ya kisiwa, na wala hapakuwa na dola inayotambulika kiasi kwamba palitawala tamaduni za kikabila, lakini pamoja na hayo palijulikana katikati mwa kisiwa cha waarabu uwepo wa kabila la Haniifat, japokuwa jina haliwekiwazi nidhamu yake, na kwa hakika Mtume-**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**- alimuandikia ujumbe mfalme wake alikuwa akiitwa Huudha Bin Ally Al-hanafiiy²⁵

²⁵ Angalia: Kitabu kiitwacho Ar-rasuul limuluukil Aalam (amekiandika Lahuudhah Bin Ally Al-hanafiy) baada ya kitabu hiki.

Kama ulivyojulikana utawala wa Bahrain mlengo wake haukuwa wazi vilevile, lakini kauli sahihi ni kuwa ilikuwa chini ya utiifu wa Kifursi na ushawishi wao kwa kiwango kikubwa,²⁶na kwa hakika Mtume -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-**alimwandikia mfalme wa wakati ule ambaye ni (Al-mundhir Bin saawiy Al-abdiy,) ambaye alisilimu na wakasilimu waliokuwa naye idadi kubwa ya waarabu na Wafursiy katika watu wa Bahrain.²⁷²⁸

Na wala hatuwezi - kwa maandalizi haya machache-kutibu hali ya Miji ya Waarabu kisiasa au nidhamu zake za kiidara pasina kutofautisha kati ya Wafalme waliokuwapo wakiisimamia miji hiyo - kama ilivyokuwa Yemen- na baadhi ya miji iliyokuwa na mlengo mdogo wa kisiasa na uchache wa Idara kama vile Makkah na Madinah kabla kidogo ya uislamu.

Waarabu - Mabedui.

Yapo katika miji ya kiarabu makabila mengi yaliyoenea, na lilikuwa kila kabila likigawika katika koo na matumbo yakikusanywa na kiunganishi muhimu nacho ni kiunganishi cha damu na ukaribu vikipewa kipaumbele, na kiunganishi hiki hiki ndicho chenye kuwafarakanisha vilevile.

Na lilikuwa kila kabila likiendesha mambo yake lenyewe, na likitatu mambo yake kupitia wakubwa wa makabila na mahakimu wao, na haya makabila kwa kawaida hayakubali kuwa chini ya nidhamu fulani ya kisiasa, isipokuwa kila kabila linakuwa na kiongozi

²⁶ Al-balaadhiri, Kitabu kiitwacho Futuuhul baladain ukurasa wa 89

²⁷ Angalia: Kitabu kiitwacho Ar-rasul limuluukil Aalam (amekiandika Al-mundhir Saawiy Al-abdiy) ni miongoni mwa kitabu hiki.

²⁸ Al-balaadhiri. Futuuhul baladain ukurasa wa 89-90.

maalumu ambaye wanakimbilia kwake wakati wa matatizo, na wakashauriana kati yao na wakatoa maamuzi ya pamoja katika kikao cha Kiongozi huyo,²⁹ na pamoja na hayo yote hapakuwepo na upande maalumu wa kiutendaji ambao unafuatilia madhaifu ya kiidara na upangiliaji na ufuatiliaji wa maamrishi, na ikitokea hali ya kabila moja kulivamia kabila lingine kama ilivyokuwa Ada ya waarabu katika zama za ujinga kabla ya uislamu, basi kabila lote hujiandaa kwa ajili ya kujilinda lenyewe na linafanya maandalizi kamili kwa ajili ya jambo hilo, na wala hatuwezi kugusa utaratibu wowote wa kisiasa wa makabila haya, na yawezekana ukaelekezwa kwa kina usukani wa mambo haya katika mambo ya kikabila.

Na kulipita majaribio mengi toka kwa baadhi ya makabila katika kisiwa cha Waarabu kutaka kusimamisha ufalme au nidhamu za kifalme, kwa njia ya kumvisha Taji la ufalme mtu mmoja katika kabila, na hata hivyo pamoja na majaribio hayo yaliyo mengi hayakufanikiwa.³⁰

Mji wa Makkah na Madinah:

Na hatuna budi kuifahamu hali ya kisiasa iliyokuwepo katika Mji wa Makkah na Madina kabla kidogo ya uislamu, na hali hii baada ya hapo iliacha athari katika kutekeleza baadhi ya taratibu za uislamu,

²⁹ Dokta Swalehe Ahmad Al-alii, Mihadhara katika Historia ya Waarabu, juzuu ya kwanza Kitabu kiitwacho (Dola ya Kiarabu kabla ya uislamu) 1960 A.D pasina kutaja sehemu iliyochapishwa, juzuu ya Kwanza/158. Doctor Subhi Swalehe, kitabu kiitwacho Nidhamu za uislamu kukua kwake na kuendelea kwako, chapa ya 5,Beirut, mwaka1980 A.D ukurasa 50.

³⁰ Doctor Swalehe Ahmad Alalii marejeo yaliyopita, juzuu ya kwanza/ukuraa wa 160.

na hasa ukizingatia mji wa Makkah na Madina ilikuwa ni ardhi ya kwanza ya uislamu.

Yalikuwa yakiishi kabla kidogo ya uislamu baadhi ya makabila katika mji wa Makkah na miji ya pambazoni mwake na kabila muhimu katika hayo ni kabila la kikuraishi³¹ na Makkah tangu zamani ni sehemu takatifu kwa Waarabu wote ikijiwa na mahujaji katika hao waarabu, kama ilivyo walikuwa waarabu ni wafanya biashara mahiri wakhama kwa ajili ya Biashara kati ya Yemeni na Hijaz na miji ya Shamu na Iraq na sehemu nyingine, kwa ilivyojulikana kwa misafara ya kusi na kaskazi, misafara ambayo imetajwa kwenye Qur'ani tukufu katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَا يَلْفُ قُرَيْشٌ ۝١ إِيَّالْفِهِمْ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ﴾ [قریش: 2-1]

(Kwa ajili ya kuzoea Makuraishi) (1) (Kuzoea kwao misafara ya kusi na kaskazi) (2) [Quraish :1-2]

Na wao kwa misafara hiyo wanapata uzoefu wa kisiasa na kijamii ambao unawatofautisha na wengine, licha ya kuwa tabia ya watu wa Makkah kwa ujumla inafanana na nidhamu ya kikabila, pale ambapo kinakosekana kituo maalumu cha serekali kinachohusika na uendeshaji na upangiliaji wa mji, na palikuwepo na nidhamu ijulikanayo kama (jumba la mashauriano) wanakusanyika humo wakubwa wa kabila la kikuraishi wakifanya uchunguzi kuhusu mambo muhimu ya kivita kijamii na biashara (37) kama ilivyokuwepo vikao vingine vya pembeni vikijadiliana kuhusu mambo

³¹ Al- masoudiy: Abul hassan Ally bin Hussain, kitabu kiitwacho muuza Dhahabu na madini ya Johari, aliyekipangilia kitabu hiki ni Yusuf As-ad Daaghir, chapa ya pili Daarul Andalus, Bairuut, mwaka 1973-1393H juzuu 2/33

haya kwa kawaida vikao hivyo vilikuwa vikifanywa katika mduara pembeni mwa Al-kaaba³² na wakati wa vita wanampa Bendera mtu au watu maalumu, kama ilivyokuwa palikuwepo na viongozi maalumu wa kuongoza misafara ya Kibiashara, ama ukiachilia mbali hayo, hatujafikia kugusa utaratibu maalumu wa kisiasa ambao unaendesha kikamilifu mambo ya mji, kama ilivyo kwa baadhi ya falme zenye kuizunguka miji ya kiarabu, bali kinyume chake tunawaona watu wa Makkah wakikataa kutawaliwa na mtu atokanaye na wao ambaye ametumwa na (Kaisari wa Roman) wakawa wakimdhihaki mtu huyo.³³³⁴

Na huenda hiyo ikawa ni sababu ya kuwepo Dhulma na ufisadi katika jamii ya watu wa Makkah.³⁵

Ama katika mji wa Makkah, hali ilikuwa ni tofauti na Makkah kwa kiasi fulani pale ambapo walikuwa wakiishi katika mji wa Madina mchanganyiko wa Waarabu watokanao na kabila la Ausi na Khazraji

³² Jawad Ally, Al-mufasswal katika Historia ya waarabu kabla ya uislamu juzuu 3/ukurasa ج4, mpaka 44

³³ Muuluwiy.) S.A.Husainiy Kitabu kiitwacho Idara ya kiarabu, ukurasa wa 28.

³⁴ Ibnu Hishaam, Historia ya Mtume juzuu1/244 maelezo ya chini ya ukurasa wa 2na Ibnu Habibu katika kitabu chake kiitwacho - Almunmiq Fii akhbaar Quraish, ukurasa154; Na Zuberi kitabu - Nasbu Quraishikurasa wa 210, Shibli Rauuf-katika kitabu kiitwacho Almujtamaa Al-arbiy kablal islaam, chapa ya Daarul kutub alhadiith Cairo, 1977, ukurasa137.

³⁵ mtunzi Mahmud Shaakir, Historia ya Mtume, ukurasa 33.

na makundi mbalimbali ya Mayahudi³⁶na huu mchanganyiko wa wakazi ulichangia sana mgongano wa mambo, na kuwepo kwa vita kati ya kabila la Ausi na Khazraji kila wakati³⁷kwa uchochezi utokanao na mayahudi wa Madina.

Ama mayahudi wa Madina wao wenyewe walikuwa wana utaratibu wa ndani kati yao, kinachojulisha hilo ni kuenea kwa ngome zao na mpangilio wake, na kupatikana viongozi wanaongea kwa jina lao.

Na kuhusu waarabu wa Madinah watokanao na kabila la Ausi na khazraji, walikuwa wakitegemea nidhamu ya ya kikabila ambayo ndiyo ilikuwa imetawala kwa Waarabu wa mashambani, licha ya kuwa ni wakazi wa vijijini lakini wapo kinidhamu wanajipamba na pambo la kikabila, na kwa namna hiyo ikawa ni wepesi kwa mayahudi kuwatawala³⁸na kuzusha matatizo baina yao, na hali ya mji wa Madinah ya kutokuwa na Idara au mpangilio wa kiujumla unaohusu mji na maslahi yake mbali mbali mpaka ukaja uislamu.

Kama ilivyokuwa utawala wa Al-manaadhira umejikita kabla kidogo ya uislamu katika mji wa Hiirat katika mji wa Iraq katika

³⁶ Mtunzi Jawaadu Ally, kitabu kiitwacho Al-mufasssal, juzuu ya 4/ukurasa131; Muhammad Al-kht-raawiy,kitabu kiitwacho Al-madinah fii Aswri Al-jaahiliyy ukurasa wa 55,68

³⁷ Jawaadu Ally, Al-mufasssal. juzuu 4/138; Sub-hi Swaalih.Al-nudhum Al-islamiyat, ukurasa48; Muhammad Al-eid Al-khatrawiy, Al-madinah fii Aswri Al-jaahiliyy ukurasa wa 146

³⁸ : Docta Muhammad Ammar, Uislamu na Falsafa ya Hukumu. chapa ya pili Taasisi ya kiarabu inayoshughulika na pekuzi na machapisho, Bairut 1979 AD,ukurasa 50.

sehemu zilizopo pambizoni mwa mto wa Furaat, wakikaa humo waarabu ukiongezea na baadhi ya wafursi na An-baat³⁹ isipokuwa utawala wake ulikuwa ni wa kabila la Manaadhirat na watawala wake, na walikuwa wakimtii Kisra wa Fursi utiifu kamili.

Utawala wa Ghasasinah katika mji wa Sham ulikuwepo kwa muda mrefu kabla ya uislamu,⁴⁰ na kwa hakika jina la utawala huu lilikuwa ni lenye kujirudiarudia katika vitabu, kwa mujibu wa mafungamano yake makubwa na matukio makubwa ambayo yaliambatana na ufunguzi wa kiislamu wa miji ya Sham, pale ambapo yalikuwa mafungamano ya huu utawala na nchi ya Roma yaliifanya Roma iwe ni yenye kuwahami mara nyingi kutokana na kuvamiwa na jeshi la kiislamu lenye kushinda katika vita vingi, sawa wawe peke yao au washirikiane na Waroma kwa mahakimu wa dini yao katika vita hizo, kama vile vita vya Yarmuuk na vinginevyo.

Na kulikuwa katika mji wa Yemen katika zama za ujinga kuna utawala wa kiarabu utawala wake ulikuwa mashuhuri kwa nguvu zake na wakawa wengi watawala wake, isipokuwa hali ya Yemen kabla kidogo ya uislamu imebadilika, pale ilipotawaliwa na wahabeshi kwa kupitia msukumo wa Waroma, na wakakosana na

³⁹ George Zaidan, kitabu kiitwacho Waarabu kabla ya uislamu, amekipitia na kuweka maoni Doctor Hussain Mu'unis, chapa ya Daarul hilaal Cairo, bila ya kuwekwa tarehe ukurasa 224. Doctor Swalehe Ahmad Al-alyi, Muhadhara katika Historia ya waarabu, juzuu 74/1

⁴⁰ Muhammad Ahmad Bashmiil, kitabu kiitwacho Al-arab fii shaam kabla la islaam, chapa ya kwanza, Daarul fikri Bairuut 1393 H1973 AD ukurasa 186.

wenye mji katika waarabu, ukiongezea wafursi na waliokuwepo kwa niaba yao.

Na katika mji wa Fursi paliwepo na dola yenye nguvu tangu zamani, dola ambayo ilipita mapito ya kimaendeleo endelevu katika masiku hayo, lakini cha muhimu kwetu tunachopaswa sisi kukijua kuhusu utawala wa Fursi ni miaka ya mwisho ulipotokea msuguanu kati ya dola ya kifursi na dola ya kiislamu.

Nidhamu ya hukumu katika utawala wa Fursi ulikuwa umesimamishwa kwa utaratibu wa kifalme kidhalimu utabakia ukiwatofautisha watu.

Na Roma⁴¹Ni Dola iliyoutawala mji wa Misri na Sham na kaskazini mwa Afrika na mashariki na katikakati mwa ulaya, na zilikuwa tawala nyingi zikifuata ufalme wa Roma, na mji mkuu wake ulikuwa ni Costantina -Uturuki ya leo- na alikuwa mtawala wa sheria wa kweli katika ufalme huu ni mfalme mwenyewe ambaye alikuwa ana haki ya kutoa maamuzi, akisaidiwa na kamati ndogo iliyokuwa ikifanya kazi pamoja naye,⁴²na Mamlaka hiyo ndiyo ile ambayo Qur'an iliizungumzia katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿الْمَغْلِبَةِ الرَّوْمِ﴾ فِي أَذْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَعْلَبُونَ ﴿[الروم: 3-1]

⁴¹ Imeitwa sura miongoni mwa sura katika Qur'ani kwa jina la Roma, na ikaashiria vita iliyokuwa ikizunguka kati yao na maadui zao wa kifursi.

⁴² Stiven Ronsiman, kitabu kiitwacho Al-hadhwarat Al-bizintia, kimefasiriwa na Abdul Aziz Taufiiq Jawiid, Aliyekipitia ni Zakiy Ally Maktabatul Nahdhwa Al-Masriyat, Cairo,1961, ukurasa wa 8.

Alif Lam Miim (1) Warumi wameshindwa (2) katika sehemu za karibu za ardhi ya Shamu kuelekea Uajemi. Na Baada ya kushindwa kwao watahinda (3) [Suratu Rum1-3] Na Dini kuu ya dola ilikuwa ni ukristo, kiasi kwamba viongozi wa dini walikuwa na nafasi maalumu katika Nchi.

Ulimwengu na kumngojea Mtume:

Alikuwa Nabii Ibrahim -Amani iwe juu yake- na watoto wake baada yake ni wenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu, na akamuomba Mwenyezi Mungu -kutakasika na machafu ni kwake- ya kuwa aifanye kuwa mpya Tauhidi kwa watoto wake, na wenye kukaa nyumba tukufu, na ilikuwa dua yake katika Qur'ani tukufu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾ [البقرة: 129]

“Ewe Mola wetu, mtume katika umma huu mjumbe miongoni mwa watu wa kizazi cha Ismāil, awesomee aya Zako na awafundishe Kitabu na Sunnah, awasafishe na ushirikina na tabia mbaya. Hakika Wewe Ndiye Mshindi asiyeshindwa na kitu, Ndiye Mwenye hekima Anayewiweka vitu vyote mahali pake.” [Suratul Baqara: 129]

MAYAHUDI:

Waliishi Mayahudi katika mji wa Madinah na Khaibar wakisubiri kutumwa kwa Mtume -**Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**-⁴³na alipotokea kutoka kwa asiyekuwa wao walimkufuru, na

⁴³ Angalia kitabu cha Bin Hishaam, Historia ya Bwana Mtume. juzuu ya 1/143. na Angalia Tafsiri ya Twabari akitafsiri aya hii.

Alama ziliashiria jambo hilo katika maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ وَكَانُوا مِن قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ﴾ [البقرة: 89]

"Na ilipowajia Qur'ani inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, ikisadikisha yale ambayo waliokuwa nayo kwenye Taurati, waliikanusha na kuukataa utume wa Muhammad, rehema na mani zimshukie. Na walikuwa, kabla ya kutumilizwa kwake, wakitumai kusaidiwa na yeye dhidi ya washirikina wa Kiarabu, na walikuwa wakisema, "Umekaribia wakati wa kutumilizwa Mtume wa zama za mwisho ambaye sisi tutamfuata na tutapigana na nyinyi tukiwa pamoja naye." Alipowajia huyo Mtume, ambaye walizijua sifa zake na ukweli wake, walimkataa na walimkanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu imshukie kila aliyemkanusha Nabii na Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad, rehema na amani zimshukie, na kukanusha Kitabu chake ambacho Mwenyezi Mungu alimletea kwa njia ya Wahyi". [Suratul Baqarat: 89]

Na zilikuja habari nyingi kutoka kwa mayahudi na wanazuoni wao katika zama za bwana Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani-zikibainisha kumjua kwao Mtume kikamilifu kwa sifa zake.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُم بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبَائِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ فَاَلَّذِينَ آمَنُوا بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَاتَّبَعُوا النُّورَ الَّذِي أُنزِلَ مَعَهُ أُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ﴾ [الأعراف: 157]

"Rehema hii nitawaandikia wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu na kujiepusha na mambo ya kumuasi, na wanaomfuata Mtume aliye Nabii, ambaye hasomi wala haandiki, naye ni Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani imshukie, ambaye wanazipata sifa zake na mambo yake yaliyoandikwa huko kwao katika Taurati na Injili; anawaamrisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtii na kila lijulikanalo kuwa ni jema, na anawakataza ushirikina na maasi na kila lijulikanalo kuwa ni baya, na anawahalalishia vizuri vya vyakula na vinywaji na kuoana, na anawaharamishia vichafu vya hivyo kama nyama ya nguruwe na vile ambavyo walikuwa wakijihalalishia miongoni mwa vyakula na vinywaji ambavyo aliviharamisha Mwenyezi Mungu, na anawaondolea wao mambo magumu waliokalifishwa nayo kama kukata mahali pa najisi, nguo kuzichoma moto ngawira, ulazima wa kisasi juu ya aliyeya kwa kukusudia au kwa kukosea. Basi wale ambao walimuamini Nabii asiyejua kuandika wala kusoma kilichoandikwa, Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani imshukie, na wakaukubali unabii wake, wakamheshimu, wakamtukuza na wakamuhami na wakaifuata Qur'ani aliyoteremshiwa, wakaufuata mwenendo wake kivitendo, hao ni wenye kufaulu kwa kupata yale ambayo Mwenyezi Mungu Aliwaahidi waja wake Waumini". [Al A'raf: 157]. Kama alivyotilia mkazo Mwenyezi Mungu namna wanavyomjua Mtume Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- kwa maneno yake:

﴿الَّذِينَ آتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ أَبْنَاءَهُمْ وَإِنَّ فَرِيقًا مِّنْهُمْ لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ

وَهُمْ يَعْلَمُونَ﴾ [البقرة: 146]

"Wale Tuliowapa Taurati na Injili miongoni mwa wanavyuoni wa Kiyahudi na wajuzi wa Kinaswara wanajua ya kwamba Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa sifa zake zilizotajwa katika vitabu vyao, kama vile wanavyowajuwa wana wao. Na hakika

kuna kundi kati yao wanaificha haki na wao wanaujuwa ukweli wake na kuwa sifa zake zimethibiti". [Suratul Baqara: 146]

Na walikuwa wapinzani wake wakimjua kiukweli kuwa yeye ni Nabii, na hasa kiongozi wao (Huyaiyi bin Ahtwab) na wengineo miongoni mwa viongozi wa mayahudi wa Madina ambao walimjua kuwa yeye ni mkweli na kuwa yeye ni Nabii wa zama hizi, na maadui wakaweka msimamo⁴⁴

Na kwa hakika mpaka sasa zimebakia ishara katika Taurati zikiashiria nyumba ya Mwenyezi Mungu na pia kutumwa kwa Mtume Muhammadi na kumfuata yeye ishara hizo zipo kwenye Zaburi (84: 5-6)

"Pongezi kwa watu wenye kuitukuza Makkah, kutufu nyumba yako kuko kwenye nyoyo zao, wakivuka kupitia jangwa la watu wa Makkah huku wakichimba visima.

Na Tamko kama lilivyowazi linaashiria Mji wa Makkah na Nyumba tukufu na kutufu nyumba tukufu.

Blessed is the man whose strength is in thee; In whose heart are the ways of them passing through the valley of (Baca) make it well"

⁴⁵(5-6-7- 89 Psalms)

⁴⁴ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 2/220.

⁴⁵ Angalia kitabu cha mtunzi Abul hasan An- Nadawiy, Historia ya Bwana Mtume, ukurasa wa 44, imenukuliwa toka kwa Jewish ENCYCLOPEDIA.y11.P 415

Na kwa hakika yamefahamisha maandiko katika Taurati ya kiarabu ni katika vitabu vilivyobakia ndani yake ukweli kuhusu kuwepo Nabii atokanaye na kizazi cha Ismail na katika Agano la kale (20-17) ambayo maneno yake yanasema:

"Ama Ismaili nilimsikia, na mimi hapa ninambariki na kumkuza na nitamzidishia sana kizazi, na atazaa viongozi kumi na mbili na nitakifanya kizazi chake kuwa Umma Mtukufu "⁴⁶

Na katika Agano jipya (15-18) "Mola wenu atawasimamishia Nabii atokanaye nanyi miongoni mwa ndugu zenu watu wa taifa lenu basi msikilizeni, Na atawasimamishia Nabii atokanaye na ndugu zao mfano wako, na nitayaweka maneno yangu kwenye mdomo wake kisha atawahamishieni yale nitakayo msemesha kwayo, na kila ambaye hatonisikiliza maneno yangu ambayo anayaongea kwa jina langu nitamtia makosani⁴⁷na makusudio ni kizazi cha Ismaili, nao ni ndugu wa Is-haq, na Mayahudi wanakiri kuwa wao wanabeba kitabu kilichobadilishwa, na wao wanafanya kazi ya kukirekebisha kutumia hekima zao na busara zao kama wanavyodai.⁴⁸

⁴⁶ Angalia ukurasa wa 19 katika kitabu kitukufu cha Agano la kale.

⁴⁷ Angalia ukurasa 237, Kitabu kitukufu; angalia Historia ya Mtume mtunzi Abul hassan an-nadawiy ukurasa 44; na kwa hakika alifananisha aliyoyanukuu An-nadawiy kwa kuchukua Maandiko ya agano la kale akakuta kuna tofauti katika baadhi ya matamshi ambayo yanapelekea kutofautiana kila chapa na chapa nyingine kwa mujibu wa chapa au matamano.

⁴⁸ Angalia kitabu cha Abul hasan An-dawiy kiitwacho Historia ya Mtume ukurasa wa 45 amenukuu toka katika Jewish Encyclopedia. Vol. 9P 589.

Kama ilivyopokelewa katika vitabu vya mayahudi "Na kisha nitautikisa kila umma na kisha atakuja (Hamduhu) kwa kila umma na kisha nitaijaza nyumba hii utukufu na hivyo hivyo amesema Mola wa siku ya mkusanyiko " Kitabu cha Hagai 9/7/9)⁴⁹

MANASWARA:

Walikuwa wanautawala katika nchi ya Misri na Sham na miji yote ya Roma, na ukaenea unaswara kati ya waarabu na hasa kaskazini mwa visiwa vya waarabu katika makabila ya tamimu na Qudhwaa na makabila mengine, na Mji wa Najrani ulikuwa kitovu cha manaswara kusini mwa kisiwa cha waarabu na kwa hakika Qur'ani imeeleza kuwa Issa -Amani iwe juu yake- aliwahadithia wafuasi wake kuhusu Muhammad - **Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani**-na akawataka wafuasi wake wamfuate kama ilivyokuja katika maneno yake Mtukufu:

﴿وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ
التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدُ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ
مُبِينٌ ﴿٦﴾﴾ [الصف: 6]

"Wakumbushe ewe Mtume, watu wako pindi Īssā, mwana wa Maryam, alipowaambia watu wake, «Mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenu, ni mwenye kusadikisha Taurati iliyokuja kabla yangu na ni mwenye kushuhudia ukweli wa Mtume atakayekuja baada yangu, jina lake ni Ahmad, naye ni Muhammad,

⁴⁹ Angalia maneno kwa ukamilifu wake kwa Abdul ahad Daud katika kitabu kitiwacho Muhammad kama alivyotajwa katika maandiko ya mayahudi, na kwa hakika kimeashiria uwepo wa jina Hamduhu: yaani Mtume Muhammad katika chapa na ikabadilishwa kuwa (Al-amniyat) katika baadhi ya chapa mpya ukurasa 37.

rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na ni mwenye kulingania watu wamuamini, basi alipowajia Muhammad, rehma ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kwa Aya zilizo wazi walisema, «Huu ni uchawi waziwazi.» [Surat As-swaffu :6]⁵⁰

Na kama ilivyo maarufu katika kisa cha kusilimu Salmaan Al-faarisiy kisa ambacho amekipokea Imamu Bukhariy katika sahihi yake ya kuwa Salmaan- Radhi za Allah ziwe juu yake- Hakika alimpa habari mmoja katika wanazuoni wa kinaswara akiwa Sham kuwa umekaribia muda wa kutumwa Nabii wa zama za mwisho, na akamuusia kumfuata, na hakika yeye Salmaan aliibiwa mpaka akawa mtumwa wa myahudi wa madinah, na aliposikia maneno ya Bwana Mtume-**Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie-** na akaona alama za utume ambazo aliambiwa na wanazuoni wa kinaswara Salman alimwamini Mtume na akamfuata.

Na kwa hakika wengi miongoni mwa walio ongoka katika manaswara wa zama hizi walifanya kazi ya kutafuta mambo yaliyotajwa kuhusu Muhammad **-Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie-**kutoka katika vitabu vya manaswara, na alikuwa pamoja nao kasisi wa Misri aliyemaliza muda wake (Ibrahim Khalil Ahmad) ambaye amesambaza kitabu kina anuani isomekayo"Muhammad katika Taurati na Injili" na akaegemea katika uandishi huo kitabu kitakatifu katika pande mbili Agano la kale na Agano jipya, na miongoni mwa aliyoyasema "Kinakusanya kitabu kitukufu maandiko yaliyo wazi sana kuhusu utume na utu wa mtume

⁵⁰ Angalia: mtunzi Mahdi Rizqullah, kitabu chake Historia ya Mtume katika mwanga wa machapisho ya asili, juzuu1/132

asiyeyua kusoma wala kuandika uwazi wenye kubainisha pasina kuwa na uficho ndani yake"⁵¹

Na yawezekana kutoa ushahidi kwa Alama zilizopokelewa toka kwa mayahudi kuhusu uyahudi kama ilivyokuwa kwa manaswara kama ilivyo katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ آبْنَاءَهُمْ وَإِنَّ فَرِيقًا مِنْهُمْ لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ﴾ [البقرة: 146]

"Wale Tuliowapa Taurati na Injili miongoni mwa wanavyuoni wa Kiyahudi na wajuzi wa Kinaswara wanajua ya kwamba Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa sifa zake zilizotajwa katika vitabu vyao, kama vile wanavyowajuwa wana wao. Na hakika kuna kundi kati yao wanaificha haki na wao wanaujuwa ukweli wake na kuwa sifa zake zimethibiti". [Suratil Baqarat: 146]

Na kwa hakika aliandika Abdul Ahad Daud mwenye kuitwa (David Benjamin Kaldan) -na alikuwa ni kasisi wa kinaswara na kisha akasilimu- kitabu kuhusu maudhui hii kwa Anuani isomekayo "Muhammad kama ilivyopokelewa katika kitabu cha mayahudi na manaswara"⁵²

⁵¹ Kitabu kiitwacho Taurati na Injili ,kilichotungwa na Ibrahim khalil Ahmad, chapa ya Daarul Manaar 1409 H,Ukurasa wa 30

⁵² Profesor Abdul Ahad Daud, Muhammad- Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie- Kama ilivyokuja katika vitabu vya mayahudi na manaswara. amekifanyia Tarjama Hamdu Faarouk Al-zain chapa ya kwanza Maktaba ya Ubaikan, Riyadh 1418 H.

Na kwa hakika waliandika wengi katika waislamu kuhusu Maudhui hii miongoni mwao ni Ahmad Diidat katika kitabu chake "Kina sema nini kitabu kitukufu kuhusu Muhammad -reheema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie- na zilisambazwa mamilioni ya kopi zake kwa lugha ya Kiingereza na kwa kiarabu⁵³ Na katika maandiko yaliyobakia mpaka sasa ni yaliyopo kwenye Injili ya Yohana (16-5) Na mimi ni mwenye kwenda kwa yule ambaye amenituma na wala asiniulize yeyote miongoni mwenu kuwa wapi ninakwenda? na sasa hivi nimewaambia na mioyo yenu ikajawa na huzuni nisadikisheni, ni kheri kwenu nyinyi nikienda, na ikiwa siendi hakutakujilieni mwenye kuwafariji"

Na vilevile ambavyo imekuja katika injili ya Matayo (21:42 na 43:44) Hivi hamkusoma katika kitabu kitukufu: chumba walichokikataa wajenzi kimekuwa kona ya uongozi? haya ndiyo aliyoyafanya muumba, ni ajabu iliyoje!

kwa hivyo ninawaambia: ALLAH atachukua ufalme wake toka kwenu na utapewa Taifa atalifanya nilenye kuleta matunda, atakayeanguka juu ya jiwe hilo atavunjika vipande vipande, na likimuangukia mtu yeyote litamponda.

Na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira- Radhi za aALLAH ziwe juu yake- kuwa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-amesema: (Hakika mfano wangu mimi na mfano wa Manabii

⁵³ Kinasema vipi kitabu kitukufu kuhusu Mtume Muhammad. kitabu kidogo kilisambazwa kwa lugha ya kiingereza mara nyingi na akakifasiri Khalil Ahmad kwa Lugha ya kiarabu, na yawezekana kwa yeyote kupata nakala ya kitabu na kuchukua toka internet kwa kuwa kinapatikana kwa wingi katika mitandao ya kiarabu na kiingereza(www.4shared.com)

waliokuwa kabla yangu ni kama mtu aliyejenga nyumba nzuri na akaipendezesha lakini akaacha sehemu ya tofali moja katika kona, ikawa watu wanaizunguka nyumba hiyo na kuishangaa huku wakisema: Kwanini usingeliweka tofali hilo? Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake akasema: Mimi ndiyo tofali hilo na mimi ni mwisho wa Mitume) ((188)).

Imepokelewa kutoka katika injili ya Yohana (16:7na 8) lakini nawaambia kweli kwamba kuondoka kwangu ni kwa faida yenu kwa maana nisipoondoka,yule msaidizi hatokuja kwenu lakini nikienda nitamtuma aje kwenu naye akija ataauthibitishia ulimwengu kuhusu dhambi,haki, na kwa hakika imepokelewa katika chapa nyingine ya injili ya matayo"Nilikwisha waambia mpaka muda utakapowadia muda wa kuja kwake, nimekumbuka kuwa nilikwisha wapa habari zake, nasikuwaambia haya tangu mwanzo kwa sababu nilikuwa nanyi,ama kwa sasa ninarudi kwa yule aliyenituma na wala hapatakuwa na yeyote miongoni mwenu anayeniuliza wapi unakwenda?" nilipowafahamisha hili nyoyo zenu zilijawa na huzuni, lakini mimi ninawaambia ukweli, ni bora nikaenda kwa sababu ikiwa sitoenda hatowaijieni msaidizi"(60)

Na cha kushangaza ni kuwa kitabu ambacho nimekirejea ni kitabu cha tafsiri ya Injili na Agano la kale, alipokuja kwenye maandiko alipotajwa Muhammad aliyaruka na wala hakuyafasiri Maalumu aliyetajwa katika maandiko akayapuuzia na akaongelea kuhusu maudhui nyingine ambayo ni kifo cha Yesu ili kufuta na kusamehewa madhambi ya watu.(61)

Na zinatilia nguvu pekuzi kuwa tamko la asili katika injili ya Yohana lilikuwa ni (Periglytos) yaani Ahmad au Muhammad na kwa hakika limebadilishwa kwa makusudi kilatini na kulifanya liwe (Paracletc) mwenye kufariji kwa makusudi ili kuwaweka watu mbali na jina la Muhammad ambalo ni la asili katika injili na kulibadilisha kutoka katika asili yake (62) kama ilivyokuja kwenye maandiko"Na

atakapokuja Roho wa kweli atawaongoza kwenye haki zote,kwa sababu hazungumzi kitu kutoka kwake,bali huongea vile avisikiavyo na kuwapeni habari kuhusu mambo yatakayotokea atanitukuza kwa kuwa yeye anachukua maneno yangu na anawaambieni nyinyi"(63) Yohana16:13)

Na huenda haya yanaafikiana na maneno ya ALLAH Mtukufu:

﴿وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ۖ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ﴾ [النجم: 3-4]

(Na wala haongei kwa matamano ya nafsi yake) Haikuwa Qur'ani isipokuwa ni ufunuo anao funuliwa MUHAMMAD. Surat Najm 3-4.

Na katika injili kuna maneno yanayo wafikiana na kutumwa kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na yaliyopokelewa katika injili ya Yohana (15:25): "Na atakapokuja mfariji aliyetumwa kwenu nyinyi kutoka kwa baba,ni roho wa kweli atokaye kwa baba ,na yeye ananishudilia mimi na nyinyi mtashudia kwa sababu nyie ni katika walioanza nami" na vilevile katika Yohana (16:15) "Na wakati atakapo kuja Roho wa kweli atawaongoza katika haki zote,kwani yeye haongei chochote toka kwake,bali anaongea kile alichokisikia na anawapa habari kwa kitakachotokea"

Na kwa hakika Qur'ani tukufu imetilia mkazo kuwa sifa za Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- na maswahaba zake zipo katika Taurati na Injili ni zinajulikana kwa Mayahudi na Manaswara na hayo yapo katika maneno yake ALLAH mtukufu:

﴿تَحْمَدُ رَسُولَ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءَ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءَ بَيْنَهُمْ تَرْتَعَا سَجْدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثَرِ السُّجُودِ ۗ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَةِ ۖ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْطَهُ فَفَازَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِ ۖ يُعْجِبُ الزُّرَّاعَ لِيغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ ۗ وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا﴾ [الفتح: 29]

"Muhammad ni Mtume wa ALLAH,na wale walio pamoja na yeye,ni wakali juu ya makafiri,wanahurumiana wao kwa wao, utawaona wakirukuu na hali wakisujudu,wakitafuta fadhila kutoka kwa ALLAH na kuridhiwa alama zao katika nyuso zao kutokana na athari za kusujudu huo ni mfano uliopo ndani Taurati na Injili ni kama mfano wa mmea uliotoa kijiti chake na tawi lake,ukashikana ukapata nguvu na ukasimama juu ya kigogo chake yanayowapendeza wakulima, amewaahidi ALLAH wale walio amini na wakafanya matendo mazuri miongoni mwao msamaha na malipo makubwa). (Surat Al-fath :29)

Na miongoni mwa maandiko yaliyopo katika kitabu cha isaya (21:13) kuna Anuani isomekayo"(Wajibu wa waarabu) na ndani yake kuna maneno haya"Laleni kwenye jangwa la waarabu enyi msafara wa Daedani, leteni maji kwa ajili ya wenye kiu enyi wakazi wa Taimaah,na jiandaeni kumpokea mkimbizi mwenye njaa kwa mkate, wao ni wenye kukimbia upanga ,upanga uliondaliwa na upinde ulio mkali na majanga ya vita"(64)

Na huenda maneno haya yanaashiria Wahyi ambao uliteremka kwa mtume muarabu muaminifu ambaye ni Muhammad-Sala na mani ziwe juu yake- nahili jambo kwa mtazamo wangu huu,ni mahala pajitihada,ndani yake kuna ishara ya mayahudi kukimbia vita kutoka katika miji ya waarabu mbele ya upanga wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-na panga na mapanga ya maswahaba wake baada yake ,ni ishara ya kuanguka kwao na kuondoka kwao baada ya hapo katika mji wa Haibari katika kipndi cha Omar na kuelekea Sham wakiptia mji wa Taimah,(65) hiyo ilikuwa kabla kidogo ya ufunguzi wa kiislamu wakati wa upanga ulioandaliwa na pinde zilizo madhubuti katika zama za ufunguzi wa kiislamu na Hisia ya maandiko haya kwa yaweza kuwa yanahitajia kuangaliwa vizuri. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Na vilevile twaweza vuta hisia ya mazungumzo yahusuyo waislamu kuitawala Baitul Maqdis wakati Omar Bin Khatwab na huenda miongoni mwa hayo ni yaliyokuja toka katika Injili ya Matayo (21:5) "mwambieni Binti Sayuni tazama mfalme wako anakuja kwako ni mnyenyekevu na amepanda punda mwanapunda mtoto wa punda" na inavyofahamika kwa viongozi wa kikristo yakuwa Omar alikuwa ni mnyenyekevu mwenye kupanda punda wake, na kwa hakika wasomi wa kikristo wakati wake kuwa wao wanazipata sifa zake katika vitabu vyao (66) na huenda haya ndiyo yanayoashiria maandiko yaliyopita- na hii ni Jitihada yangu.

Na kwa hakika nimeona kuwa katika walio yachambua maandiko,na miongoni mwao ni Abdul Ahad Daud, hakugusa mafungamano yake na Baitil maqdis katika masiku ya Omar Bin Khatwab -Radhi za Allah ziwe juu yake- (67) bali huenda baadhi yao wamefungamanisha na kuhama kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kutoka Makkah kwenda Madinah upande wa kaskazini, na jitihada hii inahitajia kutazamwa vizuri kwa mtazamo wangu.

Na hapana shaka hata kidogo kuwepo kitu katika mazungumzo yanayohusu waislamu kuifungua miji katika vitabu vilivyotangulia kwa mayahudi na manaswara,na huenda yenye kusadikisha hayo ni maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ﴾ [الأنبياء:]

[105

"Na hakika tumeandika ndani zabur baada ukumbusho kuwa ardhi watairithi waja wangu walio wema." Suratil Anbiyaa:(105), Na zaburi ni katika vitabu vilivyomtangulia Mtume Muhammad Sala na amani ziwe juu yake- ilishuka kwa Daudi na wakaisoma mayahudi.

Na imepokelewa katika kitabu cha Yohana .

Abdu rabbi "kitabu cha Yohana"(42:-8)

Tazama mtumishi wangu nitemgemezae,mteule wangu ambaye nafsi yangu imependezwa naye nimetia roho yangu juu yake nae atawatolea mataifa hukumu, hatolia wala hatatoa sauti yake barabarani Mwanzi uliochubuka hatouvunja,na mshumaa ufukao moshi hatouzima ataleta haki kwa uaminifu, yeye hatafifia wala kufa moyo hata atakapoimarisha haki duniani watu wa mbali wanaungojea uamuzi wake, hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu akazitandaza kama hema ,yeye aliyeiunda nchi na vyote vilivyomo yeye awapaye watu waliomo pumzi na kuwajaalia uhai wote waishio humo.

Mimi ni mola wako nimekuita kutenda haki,nimekushika mkono na kutenda haki,nimekushika mkono na kukulinda kwa njia yako nitaweka ahadi na kukulinda kwa njia yako nitaweka ahadi kwa watu wote, wewe utakuwa mwanga wa mataifa, utayafumba macho ya vipofu utawatoa wafungwa gerezani,waliokaa gizani utawaletea uhuru, jina langu mimi ALLAH.

Na kwa hakika yamekuja maandiko haya katika injili ya matayo (12:18) maneno hayo yananasibishwa na Nabii Isaya,na wakajaribu kuowanisha sifa zilizokuja kuhusu Issa -juu yake amani-

na huenda humo kukawa na viashiria vingi vilivyokuja toka kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake katika Qur'ani ya kuwa yeye ndiye mteule na Taa iangazayo.

Na kwa hakika yamepokelewa maandiko katika vitabu vya mayahudi kitabu cha St-Takla(33) yamekuja humo maneno haya " Na hizi ndizo Baraka ambazo amebarikiwa Mussa Mtu wa ALLAH Nabii wa wana wa Israeli kabla ya kufa kwake akasema: "Amekuja Mola toka mlima Sinai na akawachomozea kutoka katika mlima Sairir na akatokeza waziwazi toka Faaran) "na maandiko haya bado yapo kwenye agano la kale lilosambaa kila mahala na Faarin ni sehemu iliyopo Makkah,(69) pale ulipotoremka wahyi kwa Mtume Muhammad Sala na amani ziwe juu yake-na huenda maandiko haya

pamoja nakuwa ndani yake kuna mabadiliko yawezekana wakati wakuyasoma yanataja kilichopokelewa katika Qur'an tukufu katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَالرَّيُّنُونَ ﴿١﴾ وَظُورِ سِينِينَ ﴿٢﴾ وَهَذَا أَلْبَدَ الْأَمِينِ ﴿٣﴾﴾ [التين: 1-3]

(Na Apa kwa Tini na Zaitun)(1) Na kwa mlima Sinai (2) Na kwa mji huu wenye amani(3) Surat Tiin:1-3 Na katika Kitabu cha Mwanzo (21:8-20) kuna mkazo ya kuwa Faaran ni makao ya Hajira na mwanaye Ismail baada ya Ibrahimu kumchukua Hajira na kumpeleka kwenye Jangwa la Faaran. Na katika maandiko kuna ishara ya kisima cha zamzam na kunywa Humo Hajira na mwanawe.

KUFUKUZWA HAJIRA NA ISMAIL (21:8-21)

Mtoto alikuwa mkubwa na akaacha kunyonya, na Nabii Ibrahim akafanya Walima siku ile Is-haqa alipowacha kunyonya, na Sara akamuona mtoto wa hajira Mmisri ambaye amezaliwa na Ibrahim akicheza na mwanaye Is-haka,Sara akamwambia Ibrahim:" mfukuze huyu kijakazi na mwanawe ! "kwa kuwa mtoto wa huyu kijakazi hawezi kurithi na mwanagu Ish-haqa" maneno haya yalimuudhi sana Nabii Ibrahim kwa sababu Ismaili pia alikuwa ni mwanae, ALLAH akamwambia Ibrahim: "Yasikuudhi haya maneno yanayosemwa dhidi ya mwanao na kijakazi wako,sikiliza kila anachokuambia Sara, kwa sababu is-haqa ni kizazi chako na ni mtoto wa kijakazi wako,-vilevile- namfanya kuwa ni kiigizo chema kwa sababu anatokana na kizazi chako"

Basi akaamka Nabii Ibrahim Mapema kesho yake na akachukua mkate na kiriba cha maji, akawapa vyote viwili na Hajira akamuweka mwanae mabegani na akamwacha aende zake akaenda akiwa anatangatanga kwenye jangwa la Beersheba,na maji yakaisha katika kiriba, na Hajira akamtupa mtoto chini kwenye mti mmoja hivi, na akaenda na akakaa kwa kumuelekea mwanae kwa umbali wa kiasi cha kutupa pinde mbili,naye akisema moyoni mwake : "Sitaki

kumuona mtoto anakufa" na wakati alipokuwa amekaa mara akaangua kilio kwa sauti ya juu, na ALLAH akasikia sauti ya mtoto, na akaitwa na Malaika wa ALLAH kutoka mbinguni na akasema kumwambia Hajira :Una nini ewe Hajira? usiogope. amekwisa sikia Mwenyezi Mungu sauti ya mtoto huko aliposimama mchukue mtoto na mshike mkono wake, na nitamfanya kuwa ni umati mkubwa," na ALLAH akamfungua macho yake na akaona kisima cha maji akaenda mpaka kwenye maji na akajaza maji kwenye kiriba na akamnyweshwa mwanae"

Na akawa ALLAH pamoja na mtoto mpaka alipokua, akawa anaishi jangwani, alikuwa ni mrusha mishale, na alipokuwa anaishi katika Jangwa la Faaran-Makkah, mama yake alimuozesha mwanamke kutoka Ardhi ya Misri.

Na hapana shaka kuwa haya maandiko yalipata upinzani mkubwa, lakini pamoja na hayo zilibakia ishara zinazosadikisha yaliyopokelewa kuhusu Ismail na kuchimbuka maji kwa ajili yake katika jangwa la Faaran (Makkah) na yanatilia nguvu aliyoyasema Mtume wa ALLAH kuhusu Ismail katika maneno yake aliposema: "Tupeni mishale enyi watu wa Ibrahim kwa hakika baba yenu alikuwa ni mtupa mishale)). (70)

Na kwa kutilia mkazo ni kuwa hakuwahi tokea mtu yeyote hata mara moja katika mji wa Makkah kudai utume, wala katika zama zozote baada ya Issa -Amani iwe juu yake- ,bali Mwenyezi Mungu aliilinda sehemu hii asitokee yeyote mwenye kudai utume, pamoja na kutokea wenye kudai utume baada ya Mtume katika nchi ya Yemen na Najdi,na Yamamaah, lakini hakutokea yeyote mwenye kudai utume katika mji wa Makkah siyo kabla ya mtume wala baada yake, na hii nikutokana na ulinzi wa ALLAH.

Na kwa hakika imekuja katika injili ya Abakuki (3-6) nayo ni katika vitabu vya Agano la kale (Taurati) ambayo maaandiko yake yanasema hivi "ALLAH amekuja toka katika Temani Mungu

mtakatifu toka mlima parani, utukufu wake umetandaa kote mbinguni, nayo dunia imejaa sifa zake,mng'ao wake ni kama wajua miale imetoka mikononi mwake ambamo nguvu yake hudhihirishwa maradhi yanatangulia mbele yake nyuma yake yanafuata maafa ,akisimama dunia hutikisika akiyatupia macho mataifa hutetemeka milima ya milele inavunjwavunjwa, vilima vya kudumu vinadidimia, humo zimo njia zake za kale na kale,"

Na kwa hakika vyanzo vingi vimezungumza kuhusu mabadiliko yaliyokipata kitabu hiki katika chapa yake ya mwisho,na kuwa chapa hiyo imepunguzwa kutoka katika asili yake iliyochapishwa Beirut mwaka1884 A.D kwa mujibu wa maandiko yaliyokuja humo: "Na Ardhi ikajaa sifa za Ahmad aliyemiliki mikononi mwake ukombozi wa nyumati"na katika nakala iliyochapishwa mjini London mwaka 1848 A.D,na Makala ya Beirut ya mwaka 1988A.D:"na kwa hakika mbingu iling'aa kutokana na utukufu wa Muhammad ,na Ardhi ikajaa kutokana na sauti kali ya kusifiwa ikajaza mito,na ikatimbuka sauti yako mpaka Baharini,Ewe Muhammad njoo karibu,kwa hakika milima ilikuona ikapatwa na hofu "(72) huenda katika haya kuna usadikishaji wa maneno yake Mtume-Sala za ALLAH ziwe juu yake na amani: ((Nimenusurika na kuwekwa mbali na woga kwa masafa zaidi ya mwaka mzima))⁵⁴⁵⁵

kama ilivyopokelewa kutoka katika Injili ya Matayo (11-14) Habari njema kutoka kwa Issa kwa kuja baada yake kwa kauli yake :(Na

⁵⁴ angalia: Jarida la Al-bashaaraat, toleo la kwanza. limenukuliwa toka kwa (<http://www.hurras.org>), tarehe 27/11/2010 A.D

⁵⁵ Hadithi hii ameipokea Imamu Bukhari katika sahihi yake,katika kitabu cha Jihadi na Historia,mlango unaosema Nimenusuriwa na uoga kwa umbali wa mwezi,juzuu 4/12.

kama mko tayari kusadiki utabiri wao Basi Yohana Ndiye Eliya ambaye kuja kwake kulitabiriwa).

Na katika Injili ya Luka (1:14)" Nawe utakuwa na furaha kubwa moyoni wakati huo watu wengi watashangilia kuzaliwa kwake"na wanazuoni wanatilia mkazo ya kuwa hii tafsiri imebadilishwa nakuwa asili yake ni((Imekaribia kuja Amani Ardhini watu wengi watamshangilia Muhammad))(74)

Na miongoni mwa injili zilizokuwa mashuhuri ni injili ya Barnaba"(75)"Gospel of Barnaba" nayo ni injili mashuhuri iligunduliwa huko Vatcan mwanzo mwa Karne ya kumi na sita A.D (76) na baada ya hapo ilichapishwa katika lugha ya Kiitali na kiispaniola na Kiingereza katika karne ya kumi na saba na kumi na nane A.D.(77)

Na baadhi ya pekuzi zinaashiria ya kuwa Papa (Jiliasious) katika mwaka wa 492 A.D. kabla ya kutumwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alitoa ishara ya uwepo wa injili ya Barnaba na akaiweka miongoni mwa orodha ya injili zilizopigwa marufuku (78).

Na wanatamka waziwazi wengi katika washirika wa kanisa juu ya kupinga injili hii na yaliyopokelewa humo, na hii ni kutokana na uwazi uliyopo ndani yake kuhusu habari za Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kama itakavyokuja; licha yakuwa chapa yake ya kwanza ilikuwa katika lugha za kizungu kispaniola kiitaliano na kiingereza kabla ya miaka mia tatu takribani; na wala haikujulikana kwenye ulimwengu wa Waarabu na kwa waislamu isipokuwa kwa kupitia hizo chapa za kizungu, tangu karibia miaka mia.

Na kuna angalizo kwa mwenye kuipitia hii Injili ataona baadhi ya yaliyomo humo yanafana na yaliyokuja katika Qur'ani kuanzia Tauhiid na makatazo ya ushirikina na kuhusu uwanadamu wa Yesu- juu yake amani- na kukataa kwake kuabudiwa na kunasibishiwa kuwa ni mwana wa mungu na anatilia mkazo kuwa yeye ni mtume

mwanadamu mwana wa Maryamu (juu yake Amani) kutokana na nyama na damu.

Na kwa hakika ilikuja bishara ya wazi kuhusu Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake- katika injili ya barnaba, pamoja na kuweka wazi jina lake kama lilivyo Muhammad, na katika ishara ni kama ilivyokuja katika sura ya mia moja sitini na tatu:

"Na Yesu akaenda pamoja na wanafunzi wake mpaka katika msitu nyuma ya Jordani, na ilipomalizika swala ya mchana alikaa pembeni mwa mtende na wakakaa wanafunzi wake chini ya kivuli cha mtende, wakati huo Yesu akasema : "Enyi wanafunzi wangu kwa hakika kuteuliwa ni siri kubwa mpaka mimi nafikia kuwaeleza ukweli kwa hakika hakuna amjuae kikamilifu isipokuwa mtu mmoja tu, naye niyule ambaye umma unamtazamia ambaye siri za Mwenyezi Mungu zinamfunukia waziwazi, basi Shangwe kwa wale ambao watayasikliza maneno yake atakapokuja ulimwenguni. kwa sababu Mwenyezi Mungu atawafunika kama tulivyojifunika na hiki kivuli cha mtende, Kweli kama ulivyotulinda huu mti na joto la jua lilokuwakali, na hivyohivyo ndivyo rehema ya Mwenyezi mungu huwalinda waumini kwa jina hilo kutokana na Shetani.

Wanafunzi wakajibu: ewe mwalimu ni nani huyo ambaye huenda hata akawa ndiye mtu ambaye unamzungumzia kuwa atakuja ulimwenguni? Yesu akajibu kwa moyo mkunjufu: "Hakika huyo ni Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wakati atakapokuja ulimwenguni atakuwa ni sababu ya kutendwa matendo mema kwa watu kutokana na rehema kubwa atakayokuja nayo, kama ambavyo mvua inaifanya Ardhi itoe matunda baada ya kukatika mvua kwa muda mrefu, nayo ni mawingu meupe kwa huruma ya ALLAH anaisambaza ALLAH ikibubujika kwa waumini kama mvua"(79)

Na huenda maneno haya yanatukumbusha maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾ [الأنبياء: 107]

"Na hatukukutuma, isipokuwa uwe ni rehema kwa walimwengu wote" [Al Anbiyaai: 107]. na kwa maneno yake Mtukufu:

﴿وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ
الْتَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِن بَعْدِي أَسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُم بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ
مُّبِينٌ﴾ [الصف: 6]

Na pindi alipo sema issah mtoto wa Maryamu enyi wana wa israel hakika Mimi ni mjumbe wa Allah kwenu hali ya kuwa ni mwenye kusadikisha yale yalio mbele yangu kutokana na taurati na hali ya kuwa ni mwenye kutoa bishara kwa Mtume atakaekuja baada yangu jina lake ni Ahmad pindi alipo wajia kwa ubainifu walisema huu ni uchawi ulio wazi. {Surah As-Saff:6} Kama ilivyokuja katika sura ya mia ishirini na nne ambayo inasema: "Na iliipokuwa ALLAH ni mmoja haki pia ilikuwa ni moja basi kutokana na hilo nikuwa Mafunzo ni mamoja na maana ya mafunzo ni mamoja basi imani nayo ni moja kwa ukweli nawaambieni "Laukama haki iliyo kwenye kitabu cha Musa haikufutwa ,asingempa Mwenyezi Mungu Daudi baba yetu kitabu cha pili, na lau kama kisinge haribiwa kitabu cha Daudi asingetoa ALLAH ahadi ya Injili kwangu, kwa sababu ALLAH mola wetu habadiliki na kwa hakika ametamka ujumbe mmoja kwa watu wote, hivyo wakati wowote atakapokuja mtume wa ALLAH ili kutwahaisha kila walichokiharibu waovu kwenye kitabu changu wakati huo alitaka kujibiwa muandishi ,Ewe mwalimu Mtu anapaswa kufanya nini pindi sheria itakapokuwa imechafuliwa na akaongea Nabii anaedaiwa kuja? Yesu akajibu: "Hakika swali lako ni kubwa ewe Barnaba, hivyo basi nakupa faida kuwa wale ambao watakao kuwa wanafanya kwa moyo mtakasifu kwa wakati huo watakuwa wachache, kwa sababu watu hawafikirii malengo yao ambayo ni ALLAH, namuapia ALLAH ambaye

unasimama mbele yake, hakika Mafundisho yoyote mwanadamu hauyabadilisha malengo yake ambayo ni kumkusudia ALLAH basi hayo mafundisho ni ya Shari, kwa hivyo inakupasa wewe kuangalia mambo matatu katika mafundisho: yaani kupenda kwa ajili ya ALLAH na mtu kuwa mpole kwa ndugu wa karibu, na kuichukia nafsi yako ambayo imemkasirisha ALLAH na kuichukia kila siku, hivyo basi jiepusha na kila mafundisho ambayo yatakuwa ni kinyume na haya mambo matatu ya msingi kwa sababu hiyo ni shari kubwa".

Na miongoni mwa ushahidi katika Injili ya Barnaba katika sura ya mia mbili na Nane (80)

"Basi mwambie: huyu mwana wa Ibrahimu alikuwa ni nani? Yesu akajibu: "Hakika wivu wa utukufu wako ewe Mola wangu unanichagiza na wala siwezi kunyamaza, nasema ukweli: kwa hakika Ibrahiim ni Ismail ambaye ni lazima aje kutokana na kizazi chake Masihi aliye ahidiwa Ibrahim kuwa makabila yote yatapata baraka kuptia kwake".

Na kwa hakika kimekuja kitu ambacho ni maalumu kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- katika Injili ya Barnaba,na katika hicho ni kusimama kwake katika uombezi mkubwa wa kuwaombea viumbe siku ya kiama, pamoja ya kuwa kuna ukweli wa wazi kuwa kumebadilishwa maandiko, ndani yake kuna maneno tunayapitia ya kubakia haki yakuwa tusivuke mipaka zaidi ya vile ilivyopokelewa katika Hadithi sahihi zinazohusiana na Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake.

Barnaba anasifia kuhusu kisimamo hiki cha bwana Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akinukuu maneno ya Issa- juu yake amani- katika sura ya hamsini na nne na hamsini na tano katika maandiko marefu ambayo yanaendana madhumuni yake na hadithi inayozungumzia Uombezi, na yanatofautiana katika baadhi tu ya matamshi napo ni sehemu ya kutazama vizuri, na yaliyopokelewa yanatilia mkazo ujuzi wa wanafunzi wa Nabii Issa -juu yake amani-

na Barnaba ni miongoni mwao wanaojua utukufu huu na umaalumu wa bwana Mtume -rehema na mani ziwe juu yake- na kwa hakika yamekuja maneno katika injili yakisema (54:12:33) "kisha atawafufua ALLAH baada ya hapo watu wote walio wema ambao watakuwa wakipaza sauti zao kwa kusema: Tukumbuke ewe Muhammad,hivyo itaingia Huruma kwa mtume kutokana na kupaza kwao sauti, na ataangalia yale aliyoyafanya hali ya kuwa na hofu kwa namna gani atawakomboa, kisha Mwenyezi Mungu baada ya hapo atawafufua viumbe wote watakuwa kama walivyokuwa mara ya kwanza, na kila mmoja wao atakuwa na nguvu ya kuzungumza zaidi kisha atawafufua ALLAH baada ya hapo watu waliotengwa wote, ambao watakapo simama viumbe vyote vitawaaogopa kwa sababu ya muonekano wao mbaya, watapiga ukelele: Ewe Mlezi mola wetu usitusahau kwa rehema zako, na baada ya tukio hili atamsimamisha ALLAH Shetani ambaye atakuwa kila kiumbe akimtazama anamuona kama maiti kutokana ubaya wa muonekano wake wenye kutisha, kisha Yesu akasema: Natarajia ALLAH asinionyeshe fedheha hii katika siku hiyo, kwa hakika Mtume peke yake ndiye ambaye hatouogopa muonekano huu kwa sababu yeye hamuogopi yeyote isipokuwa ALLAH peke yake.)

Na atakwenda Mtume wa ALLAH ili kuwakusanya manabii wote ambao atawasemesha kwa kuwavutia ya kuwa waende pamoja naye wakanyenyekee kwa ALLH kwa ajili ya waumini, basi watatoa udhuru wote kwa khofu na kusema ninamuapia ALLAH hakika mimi sitokwenda huko kwa sababu mimi ninayajua ninayoyajua, na ALLAH atakapo liona hilo atamtajia mtume wake namna alivyoumba kila kitu kwa ajili ya mapenzi yake, basi hapo itaondoka khofu yake, na atasogea sehemu ya kukusanywa hali ya kuheshimiwa, na Malaika watakuwa wakisema kwa sauti nzuri: limetukuka jina lako tukufu ewe ALLAH mola wetu, na wakati atakapokuwa karibu na sehemu ya kukusanywa basi ALLAH atamfungulia kama kipenzi anapomfungulia ampendaye baada ya kupita muda mrefu bila

kukutana, ataanza kwanza Mtume kwa maneno akisema: Mimi kwa hakika nakuabudu wewe na ninakupenda mola wangu, na nina kushukuru kwa moyo wangu wote na nafsi yangu, kwa sababu wewe ulikusudia na ukaniumba mimi ili niwe mja wako na umeumba kila kitu kwa kunipenda mimi ili nikupende kwa ajili ya kila kitu na katika kila kitu na juu ya kila kitu, Basi na akushukuru kila kiumbe wako ewe mola wangu, wakati huo kila kiumbe cha ALLAH kitasema: Tunakushukuru ewe mola wetu limetukuka jina lako tukufu, kwaukweli nawaambieni :kwa hakika shetani na waliotengwa pamoja na shetani watalia wakati huo: mpaka mmoja wao jicho lake moja litabubujisha machozi zaidi ya mto wa Joradan, na pomaja na hivyo hawatomuona ALLAH, na ALLAH atamsemesha Mtume wake kwa kusema: karibu ewe mja wangu mwaminifu, Omba utakalo utapata kila kitu, basi Mtume Mwenyezi Mungu atamjibu: "Ewe mola wangu kwa hakika nakumbuka pale uliponiumba ulisema: hakika wewe ulikusudia kuumba ulimwengu na pepo pia Malaika na watu kwa mapenzi yako kwangu, ili wakitukuze kupitia kwangu. mimi ni mja wako kwa hivyo nanyeyekea kwako ewe mola wangu mola mwenye huruma na muadilifu ukumbuke ahadi yako kwa mja wako, basi ALLAH atamjibu kama vile anavyomjibu mtu akimfanyia mzaha kipenzi chake na atasema: je unamashahidi juu ya haya ewe kipenzi changu Muhammad? basi atasema kwa heshima: ndiyo ewe mola wangu, basi atasema ALLAH ewe Jibril nenda na uwaite, na atakuja Jibril kwa mtume na atamuuliza: Ni nani hao mashahidi wako ewe muheshimiwa? Mtume atajibu: Hao mashahidi ni Adam na Ibrahiim, na Ismail na Mussa na Daud na Yesu mwana wa Marayam basi Malaika wataenda kuwaita mashahidi waliotajwa ambao watahudhuria huko wakiwa na khofu.

Basi watakapo hudhuria tu atawaambia Mwenyezi Mungu: hivi mnayakumbuka aliyoyathibitisha mjumbe wangu? watamjibu ni jambo gani hilo ewe Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu atasema:

"kwa hakika mimi niliumba kila kitu kwa mapenzi yangu ili wanishukuru mimi kila kiumbe kwa mapenzi hayo, basi watajibu kila mmoja wao: kuwa tuna mashahidi watatu ambao ni bora zaidi kuliko sisi, Mwenyezi Mungu atawajibu: Na ni kina nani hao watatu? basi Mussa atasema ushahidi wa kwanza ni kitabu ambacho ulinipa mimi. Na atasema Daudi; Ushahidi wa pili ni kitabu ambacho ulinipa mimi, na anasema ambaye anakusemesheni: Ewe mola wangu hakika Shetani ameudanganya Umma wote akasema mimi ni mtoto wako(81) na ni mshirika wako, lakini kitabu ambacho ulinipa kimesema kweli kwa hakika mimi ni mja wako na kitabu kinakubaliana na alichokithibitisha mtume wako na wakati atakapokuwa anayasema haya mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atasema: "kwa hakika hiki nilichokifanya sasa hivi nilikifanya ili kila mmoja ajuwe Upeo wa mapenzi yangu kwako, na baada ya kuongea hivyo atampa Mwenyezi Mungu Mtume wake kitabu kilichoandikwa ndani yake majina ya kila wateuliwa wa Mwenyezi Mungu hivyo kila kiumbe kitamsujudia Mwenyezi Mungu kikisema: kwako wewe peke yako ewe Mola wangu kuna utukufu na ukarimu kwa sababu wewe umetupa mtume wako" (82)

Kama unavyopatikana ushahidi mwingi kwenye injili ya Barnaba kuhusu mazungumzo ya Masihi -Issa -juu yake amani- ambayo yanafanana na mazungumzo ya mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- na miongoni mwa mazungumzo hayo ni kuisifu pepo katika sura ya mia moja sitini na tisa miongoni mwa sifa hizo za pepo ni kuwa" jicho la mwanadamu halijawahi kuona wala masikio kusikia wala moyo wa mwanadamu haujawahi kufikiria walichoandaliwa na Mwenyezi Mungu katika vile wanavyovipenda"(83)

Na jambo hili linaafikiana na maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾ [السجدة: 17]

"Hakuna nafsi yeyote inayoyajua yale waliofichiwa kwa ajili yao ya kutuliza macho na kufurahisha moyo, yakiwa ni malipo yao kwa matendo yao mema." Surat Sajdah 17 Na hili linasadikisha maneno ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuhusu ALLAH Mtukufu: "Nimewaandalia waja wangu wema, mambo ambayo jicho halijawahi kuona wala sikio halijawahi kusikia wala hayajawahi kufikirika katika moyo wa mwanadamu" (84)

Kama inavyoafikiana Injili ya Barnaba na yaliyokuwamo kwa waislamu kwenye Qur'ani na Sunna kwa ujumla pasina kuchambua mafungamano ya Yesu mwenyewe na kuinuliwa kwake kwenda mbinguni, na hayo hupatikana kwenye sura ya mia moja na kumi na sita kwa maelezo yake yasemayo: "Na wakaja Malaika watakatifu na wakamchukua Yesu kupitia dirisha lililopo upande wa kusini, na wakambeba na wakamuweka katika mbingu ya tatu akiwa anaambatana na Malaika wanaomtaka ALLAH wakati wote (85) "

Na hili linaafikiana na kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿ وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِمَّنْهُ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾ [النساء: 157]

"Na wala wao hawakumuua 'Issa wala hawakumsulubu, bali walimsulubu mwanamume aliyefanana naye kwa kudhani kwao kuwa yeye ndiye 'Issa. Na yeyote aliyedai kwamba walimuua, miongoni mwa Mayahudi na pia wale waliomsalimisha kwao, miongoni mwa Wanaswara, wote hao wako kwenye shaka na kuchanganyikiwa; hawana ujuzi wowote isipokua ni kufuata dhana tu, na wala hawana yakini ya kuwa walimuua, bali wana shaka nalo hilo na wanalidhania tu". (Suratun nisaai: 157) Sisi hatuna shaka ya kuwa kuna mabadiliko yametokea katika vitabu vya mayahudi na manaswara wa asili na wanaotokana na hao wa asili

kwa kukiri kwao, wao pamoja na hayo kwa hakika ukweli uko wazi kwa baadhi yao, hasa hasa yakuwa Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- kwa hakika aliwalingania kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kuwaheshimu manabii waliotangulia na kuendana na misingi yao ya kumuheshimu ALLAH na kumtukuza, kwa sheria yake ambayo amekuja nayo na manabii waliotangulia, amesema ALLAH mtukufu:

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾﴾
[آل عمران: 64]

"Sema ewe Muhammad enye mayahudi na manaswara njooni katika neno la sawa baina yetu na nyie tusimuabudu isipokuwa ALLAH na wala tusimshirikishe na chochote na wala baadhi yetu wasiwafanye baadhi kuwa ni miungu kinyume na ALLAH kama wataenda kinyume basi semeni kubalini kuwa sisi ni waislamu."
Surat [Al-Imran: 64].

Na kwa hakika jambo lilikuwa wazi kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- katika ujumbe wake aliomwandikia Hirakli na wengineo miongoni mwa viongozi wa manaswara katika zama zake.

Wanautamaduni wa kimagharibi wa zama hizi na mtazamo wao kuhusu Mtume-Sala na amani ziwe juu yake:

Imeonekana kuwa idadi kubwa ya wanautamaduni wa kimagharibi katika kipindi cha karne mbili zilizopita walitoa ushuhuda kuhusu ukweli wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake au waliashiria jambo hilo kwa uadilifu kiwango fulani, na hata ikiwa tutatofautiana nao katika maandiko na madhumuni wakati mwingine, kwa hakika walikuwa wengi katika wasomi wa Ulaya siyo waadilifu katika kuuzungumzia utu wa mtume Sala na amani ziwe juu yake- (86) anasema Darmangham: "miongoni mwa masikitiko makubwa ni kuvuka mipaka kwa hawa wenye ubobezi wa

uchambuzi wakati mwingine na mpaka sasa vimebaki kuwa vitabu vyao ni michoro tu, na vilikuwa vitabu vyao ni nyenzo maalumu ya uangamizaji" (87)

Na kwa hakika tungo nyingi zilitilia kipaumbele maudhui hii na kuleta ushahidi wa hilo. (88)

Na huenda karne ya kumi na nane ndiyo karne ambayo kwa wingi kulidhihirika ukweli wa utendaji wa wamagharibi katika kumzungumzia mtume kwa uadilifu kwenye macho ya watu wa Ulaya, kama alivyotaja Rudensn Maxim katika maneno yake: "Kwa kuja idadi kubwa ya wana Historia wa Ulaya waliong'aa katika karne ya kumi na nane ulianza ukamilifu wa utambuzi wa taswira, nayo ni taswira ya Muhammad mwenye hekima mwenye kusamehe sana na ni hakimu na mweka sheria" (88)

Na anatoa ishara mwandishi wa Kiingereza aitwaye (George Bernard shaw) mwanzo wa watu wa ulaya kumfahamu Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- licha ya kujaribu kumchafua muonekano wake. katika kauli yake: "Kwa hakika Ulaya kwa sasa wameanza kutambua Hekima za Mtume Muhammad, na dini yake imeanza kupata uhai, na itatakasika Itikadi ya uislamu kutokana na walivyoituhumu kwa habari za uongo za watu wa ulaya katika zama za kati" (90)

Kama anavyo ashiria (Marcel Pourzar) kuhusu kudhihirika ukweli kuhusu Muhammad Sala na amani ziwe juu yake- na dini yake licha ya kuchafuliwa, hivyo anasema: "kulikwisha andikwa kila kitu kuhusu mtume wa uislamu-Sala na amani ziwe juu yake, hivyo mwangaza wa Historia ya maisha yake tunayajuwa kwa uwazi zaidi na mtazamo aliouacha mtume -Sala na amani ziwe juu yake- uko wazi, na hata kama mtazamo huo utachafuliwa kwa makusudi kiutaalamu kwa kiwango ambacho kinajulikana lakini mtazamo huo pamoja na kuchafuliwa bado unaunganisha jambo la uislamu

litokanalo na muonekano wa kidini na kutoa fursa ya kujua ukutufu wake wa kweli"

Na hakuwa Mtume Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake- Hakuwa kwa mtazamo wa Kihistoria ni mlinganiaji Dini peke yake, Bali alikuwa vilevile ni muanzilishi wa siasa ambayo alileta mageuzi ya mapito ya Historia, na ikawacha athari katika maendeleo ya ueneaji wa uislamu baada ya hapo katika uwanja mpana. (91)

Kwa hakika ilikuwa kuyasoma maisha ya Mtume -Sala na amani ziwe juu hake- ni yenye kuathiri kwa kiwango kikubwa kwa baadhi ya watu wa ulaya licha ya kuwa na ukomo fulani katika vyanzo vya masomo, na kuwepo na uchafuaji wa haki katika baadhi ya vyanzo, isipokuwa mwangaza wa haki utokanao na baadhi ya tungo ziliipa hisia yenye nguvu na ukweli kiasi kwamba ikaathiri mapito ya maisha yao kwa nguvu, na huyu Martin (Alphonse de Lamartine) anasema katika maneno yake: "Jambo kubwa katika maisha yangu ni kuwa mimi nilisoma maisha ya Mtume wa ALLAH Muhammad usomaji wa kufahamu, na nikakuta humo katika maisha yake utukufu wa kudumu, ni nani awezaye kuthubutu kumfananisha na watu wenye Historia na Mtume Muhammad?! na ni nani ambaye alitokea akawa mtukufu kuliko yeye, kwa kungalia vipimo vyote ambavyo hutumika kupimia utukufu wa mtu?! Hakika tabia yake ilikuwa ni kupenda ushindi ambao ulimfanya ajitolee kufikisha ujumbe na swala zake zilikuwa ni nguzo za Itikadi. Hakika Mtume ni Mzungumzishaji watu na mweka sheria na mwenye kufungua miji na mwenye kurekebisha Itikadi nyingine ambaye alianzisha ibada isiyotukuza mapicha mtume huyo ni Muhammad, kwa hakika aliangamiza Muhammad Itikadi ambazo zinafanywa kuwa ni muunganisho kati ya Mwenyezi Mungu na viumbe" (92)

Na anatalia msisitizo (Eduard Perroy) ya kuwa Mtume Muhammad-Sala na amani ziwe juu yake- ni Nabii wa Mwisho na kuwa sheria zake ni za ALLAH na ni zenye kukusanya sheria zote na

ni utaratibu wa tabia ya kijamii, hivyo anasema: Alikuwa Muhammad Bin Abillahi, mtume Muarabu na mwisho wa Manabi, akiwapa habari njema Waarabu na watu wote kuhusu dini mpya na akiwalingania kwa kauli ya kusema kuwa Mwenyezi Mungu mmoja wa pekee, na ilikuwa sheria katika kulingania kwake haitofautiani katika Itikadi au Imani na ni yenye kunufaisha kutokana na kulazimiana na utawala wa kiuungu, haipangilii mambo ya kidini peke yake, bali inapangilia mambo ya kidunia vilevile, kwa hivyo humlazimisha muislamu kutoa zaka na kupigana jihadi na maadui wa uislamu, na kuieneza dini ya uislamu tukufu, na ilipochukuliwa roho yake mtume Muarabu -Sala na amani ziwe juu yake Mnamo mwaka 632 A.D, alikuwa amekwisha maliza Kulingania kwake, kama ilivyokuwa alikuwa amekwisha maliza kuweka mpangilio wa kijamii ambayo ilivuka na kuwa juu zaidi ya nidhamu ya ukabila ambayo ilikuwa kwa waarabu kabla ya uislamu, na udugu wao ukawa katika umoja wenye nguvu, na hivi ndivyo ulitimia umoja kisiwa cha waarabu, ukawa umoja ulioshikamana kidini, ambao haukujulikana kabla ya hapo"(93)

Kama vile (Leitner) anavyomtetea Mtume -Sala na mani ziwe juu yake- na anavyotetea Wahyi ulioteremka na anatilia mkazo juu ya uwepo wa alama zinazojulisha juu ya ukweli wa utume wake katika maneno yake aliposema: "Kwa kiwango ninachokijua kuhusu dini mbili za mayahudi na manaswara nina sema; aliyemfundisha Muhammad -Rehema na amani ziwe juu yake- siyo Nukuu bali ni Wahyi (ufunuo) amefunuliwa na wala hakuna shaka katika hilo kwakuwa bado tunaamini kuwa umetujia wahyi kutoka kwa mwenye nguvu na mjuzi na mimi kwa hashima zote na unyenyekevu ninasema ikiwa kujitolea kwa wema na kwa dhati, na kuwa na makusudio ya kweli, na kuwa na imani na moyo thabiti, na mtazamo wa kweli wenye kupenyeza mpaka katika mambo madogo na makosa yaliyojificha na upotofu, na kutumia njia nzuri zaidi ya kuyaondosha, hizo zote ni alama zilizo wazi zenye kujilisha ya kuwa

Unabii wa Mtume Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake-, na kuwa yeye amepewa wahyi (Ufunuo)"

Kwa hakika dini ya kikristo ambayo alitamani Muhammad -Sala na mani ziwe juu yake- airudishe katika asili yake ya usafi ambayo Issa- juu yake amani- aliihubiri, inatofautiana sana na mafundisho aliyoyaeneza Paulo na mchanganyiko wenye kuleta Fedheha ambao umeingizwa na kundi la wakristo, na kwa hakika yalikuwa matarajio na matamano ya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- nikuwa Baraka za dini ya ibrahimu -juu yake amani- zisifanywe kuwa maalumu kwa watu wake peke yake, bali baraka hizo ziwe kwa watu wote na kwa hakika dini yake ilikuwa ni kiunganishi cha uongofu na Utamaduni wa mamilioni ya watu, na lau kama siyo dini hii wangebakia watu katika unyama na ushenzi, na wasingekuwa na huu udugu wenye kufanyiwa kazi katika uislamu. (94)

Na huenda katika mambo ambayo waliyatazama baadhi ya wataalamu wa Ulaya ni swala la Itikadi, nayo ni Kiini cha dini ambayo aliilingania Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na akaeleza Mtume kuwa hiyo ndiyo Daa'wa ya mitume wote, kama ilivyokuja katika aya nyingi za Qur'an na Hadihi za Bwana Mtume.

Anasema (Voltaire): Kwa hakika Itikadi ya Muhammad haina Mashaka wala kificho, na Qur'ani ni ushahidi mtukufu juu ya upweke wake ALLAH" (95)

Na anasema (Roma Landau) "Hajawahi Mtume kujinasibisha hata siku moja katika masiku sifa ya uungu au nguvu ya maajabu. kinyume chake alikuwa akipupia maandiko yakuwa yeye ni mtume tu, amemuandaa ALLAH ili kufikisha wahyi kwa watu" (96)

Na anatalia mkazo (Arnold Toyubee) kuhusu swala la Itikadi aliyonayo Mtume na yanayofungamana na sheria na mpangilio unaoendana na uwezo wa utekelezaji au nguvu ya kusimamia uadilifu, hivyo anasema: "Kwa hakika alijitolea Mtume uhai wake ili

kutekeleza ujumbe wake katika kusimamia hii mionekano miwili katika jamii ya waarabu nayo ni Fikra ya umoja wa kidini na Kanuni na Nidhamu katika hukumumu) na hilo lilitimia kiukweli kutoka na ubora wa uislamu wenye kuenea ambao ulijumuisha kati ya uwazi wa umoja na mamlaka ya utekelezaji kwa pamoja" (97)

Na anatoa ushahidi (Washington Irving) kwa tukio lake la ufunguzi wa Makkah ili kutilia mkazo ya kuwa Muhammad ni mwisho wa manabii na anasema katika maneno yake: "Alikuwa Muhammad -Rehema na mani ziwe juu yake- ni mwisho wa manabii na ni miongoni mwa mitume watukufu ambao Mwenyezi mungu aliwatuma ili kuwalingania watu kumuabudu Mwenyezi Mungu"

Na vilikuwa vitendo vya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- mwishoni mwa ufunguzi wa mji wa Makkah vilijulisha kuwa yeye ni mtume na siyo tu kuwa yeye ni kiongozi mwenye kutafuta ushindi. Kwa hakika alidhihirisha upole na huruma kwa wakazi wake licha ya kuwa yeye alikuwa katika kambi yenye nguvu lakini aliuvisha ushindi wake Taji la upole na msamaha" (98)

N anatilia mkazo (Edwad Ramsay) Ujumbe wa mtume -Sala na mani ziwe juu yake- na kutilia mkazo kwake jambo la Itikadi, hivyo anasema: "Alikuwa Muhammad ulimwenguni na ujumbe wa mmoja mwenye nguvu, ili kuwatoa watu kwenye giza na kuwapeleka kwenye Nuru, Hivyo ikachomoza Al-fajiri mpya iliyokuwa ikionekana angani na katika siku ambayo alirudisha mkono wa msuluhishi mtukufu ambaye ni Muhammad, haukukosa uadilifu na uhuru, ulikuja wahyi kutoka kwa ALLAH kuja kwa mtume mtukufu, Hoja zake za kiakili zilifungua vizibo katika macho ya umma wa waarabu wa zamani kabla ya uislamu, na wakahakikisha kuwa wao walikuwa wamelala katika matawi ya utumwa" (99)

Na anasema (Karen Armserong) na kwa namna hii Basi ikiwa ushindi wa kisiasa ndiyo utekelezaji wa kipekee wa Mtume Muhammad, basi ni haki yake kutushangaza, lakini kufaulu kwa kwa

Muhammad kumeegemea zaidi katika mtizamo wa dini ambao waliuchukua waarabu, na ambao waliukumbatia-kwa mchango wake- Raia kutoka katika mataifa yenye Himaya, na hivyo ni kwa sababu walikuwa na muitikio wa utashi wa kiroho, isipokuwa Muhammad na waislamu wa mwanzo hawakupata ushindi kwa wepesi kama wanavyofikiria baadhi, lakini wao walipambana kwenye vita vikali vyenye kukatisha tamaa, na lau kama isingelikuwa zingatia la kwanza la Mtume na jamaa zake wa ni Dini basi wasingekuwa ni wenye kubakia" (100)

Na wengi katika watu wa ulaya wanamsifu mtume -Sala na amani ziwe juu yake- yakuwa yeye ni msuluhishaji na mwenye maono na wakimsifia -japokuwa hawamwamini- anasema (Jowld Tasiir) "Na hapana shaka kuwa Muhammad bila shaka ndiye msuluhishi wa kwanza wa kweli katika taifa la kiarabu kihistoria na katika zama hizi tunamuona Muhammad anatumia uzoefu wake wenye kufikirisha na maono ya ndani na mtazamo wa hali ya juu "katika kupambana na maadui zake ambao walianza kupinga makusudio yake na malengo yake ndani ya makazi yake na nje".(101)

Na kwa hakika baadhi yao walichoshwa na watu wa ulaya kwa kutoamini unabii wa mtume Muhammad -Sala na mani ziwe juu yake-, na wakahesabu kuwa jambo hilo ni aibu kwao, anasema (Tomas Carlyle): "Kwa hakika imekuwa ni aibu kubwa kwa yeyote mwenye kuzungumzia zama hizi kusikiliza yasemwayo kuwa dini ya uislamu ya ni ya uongo, na kuwa Muhammad ni mdanganyifu mwenye kuzua mambo" (102).

Na huyu hapa mwana historia muamerika maarufu kwa jina la (Will Durant) ambaye anajulikana kwao kuwa yeye ni Baba wa Historia anasema: "Ni wazi kuwa hakuna yeyote aliyemsaidia Muhammad Rehema na mani ziwe juu yake- kusoma wala kuandika na wala haijulikani kuwa alishawahi kuandika kitu yeye mwenyewe, lakini hilo halikuwa ni kizuizi kilichomzuia kutokujuwa mambo ya

watu kiukamilifu, hakuna yeyote katika watu aliyemfikia kielimu, alikuwa ni kiongozi mwenye uzoefu, lakini yeye alikuwa kwenye siasa hii ni mzoefu, anajua namna ya kuunganisha mapigano kwa amani, na tukiwa tunataka kutaja watukufu, basi Muhammad ni katika watu watukufu kihistoria" (103)

Na baadhi yao wanatoa ishara kuhusu kupigiwa mfano ukamilifu wake Mtume -Sala na mani ziwe juu yake- ikilinganishwa na upeo waliokuwa nao watu wa ulaya kuhusu aliyokuja nayo mtume Sala na amani ziwe juu yake.

Anasema mwandishi wa kijerumani (Johann Wolf Gang Von Goethe): "Kwa hakika sisi watu wa ulaya kwa ufahamu wetu wote bado hatujaweza kufikia upeo alioufikia Muhammad, na wala hatomtangulia yeyote, na kwa hakika nilitafuta kwenye Historia mfano wa aliye na sifa za juu zaidi ya huyu mtu, nakuta ni kwa mtume muhammad, na kwa namna hii ni lazima haki iwe wazi na iwe ni yenye kushinda, kama vile ambavyo alifanikiwa Muhammad ambaye aliufanya ulimwengu wote kuwa wanyeyekevu kwa neno la Tauhiid (Kumpwekesha Mwenyezi Mungu).

Na anatoa ishara (Bernard Shaw) mwandishi wa kiingereza mashuhuri ishara ya mafungamano ya mafundisho ya mtume -Sala na amani ziwe juu yake- namna yanavyofungamana na zama hizi, na miongoni mwa hayo ni kuamini sheria zake na kufaa kwake katika kila zama, na hali yakuwa alikwisha eleza kabla ya miaka 1400, anasema: "Anapasa kuitwa mkombozi wa ubinadamu, na mimi na amini kuwa kama angesimamia sheria moja kwa moja mtu mwingine mfano wake katika ulimwengu huu wa sasa, angefaulu katika kutatua matatizo yake kwa njia ambayo inaleta suluhisho zaidi miongoni mwa amani na furaha."

Na ameashiria (Gustave Le Bon) Doctor mwanahistoria wa Kifaransa, ameashiria mwanzo wa wamagharibi kumfanyia uadilifu Mtume Sala na amani ziwe juu yake- anasema: "Ikiwa utapima

thamani ya watu kutokana na utukufu wa kazi zao anakuwa Muhammad ni katika watukufu zaidi kuwahi kujulikana katika historia, na wakawa wasomi wa kimagharibi wakimtendea haki Muhammad pamoja na kuwa ubaguzi wa kidini uliziba macho ya wanahistoria wengi kuto kukubali ubora wake"

Aliweza Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake- kuanzisha sifa ya hali ya juu yenye nguvu kwa mataifa ya kiarabu ambayo hayana mfano wake, na katika kuanzisha huko, kunadhihirisha utukufu maalumu wa Muhammad, na wala hawakusita wafuasi wake katika kujitolea nafsi zao katika kufuata sifa hizi za hali ya juu".

Hakuna kitu alichopatia zaidi Muhammad kama alivyopatia kwenye kuwakusanya watawala wa miji na wa vita na wa dini katika mkono mmoja, katika siku ambazo kisiwa cha waarabu kilikuwa ni machinjio hatukuweza kukadiria thamani yake kwa matokeo yake, kwa hakika warabu waliukomboza ulimwengu katika karne ya kwanza baada ya kuwepo makabila yenye kufanana na kabila la Barbar lililokuwa likipigana kabla ya kuja Muhammad" (106)

Na (Etienne Dinet) anamsifia Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- sifa zake na utofauti wake, hivyo anasema: "Kwa hakika sifa ambazo amezibeba Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake- zilizoandikwa kwenye kurasa zilikuwa zimevuka mipaka ya kawaida na zilikuwa na athari kubwa sana mpaka ikafikia hatua ya kuchapishwa sheria zake kwa namna yenye nguvu ambazo zilimfanya awe na roho ya ubunifu, na zikampa sifa ya kitu kipya."⁵⁶

Na kinaelezea kwa kina kitabu cha watu wa Ulaya kuhusu kushangazwa kwao na Mtume-Sala na mani ziwe juu yake, na

⁵⁶ Chanzo kilichotangulia ukurasa 127.

miongoni mwao ni (Jacques Augustin Berque), Anasema: "Na hapana shaka kuwa uislamu ambao muumba alimchagulia Muhammad ulikuwa unastahiki kwa Muhammad na alikuwa Muhammad anastahiki uislamu huo"⁵⁷

Anasema Mjerumani (Jacques Augustin Berque) Alikifanya mtume wa uislamu kisiwa cha waarabu kuwa ndiyo hatua ya kuanzia kufikisha ujumbe wake mtukufu ambao ulipigwa vita sana na haujaachwa kupigwa vita, lakini daima haki ni yenye kushinda, na hakuja muhammad isipokuwa ni kwa haki na ukweli"(109)

Na inadhihirika kwa baadhi ya wamagharibi kutosheka kwa utume wa mtume Muhammad -reheema na amani ziwe juu yake- bali wanatilia mkazo baadhi yao kuwa Muhammad ndiye nabii wa mwisho na yeye ndiye mwenye kustahiki utukufu huu, anasema mwanazuoni wa kifaransa aitwaye (Clement): "Hakuwa Muhammad ni Nabii wa kawaida, bali alipaswa na kustahiki kuwa ni Nabii wa mwisho na lau kama waislamu wangemfanya mtume wao kuwa ni kiigizo chema katika kusambaza Daa'wa ungekuwa ulimwengu wote ni waislamu" (110).

Kwa hakika wamagharibi wengi waliusifu msimamo wa Mtume Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake- miongoni mwao ni manaswara na dini zote zinazonasibishwa kuwa zinatoka mbinguni, na uadilifu wake kwa watu wake na kumuheshimu kwake Yesu -juu yake amani- na huyu hapa

⁵⁷ Chanzo kilichotangulia ukurasa wa 171.

(George Bernard show) anasema: "kwa hakika nilimsoma Muhammad kwa kumzingatia ni Mtu mwenye kushangaza, basi nikamuona yuko mbali na ugomvi na yesu, bali anapaswa kuitwa mkombozi wa uwanadamu, na watu wa ulaya wameanza katika zama hizi kufahamu itikadi ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu, na huenda wamekwenda mbali zaidi ya hapo, mpaka wakafikia hatua ya kukubali kuwa uwezo wa itikadi hii katika kutatua matatizo kwa njia ambayo italeta amani na furaha! na kwa madhumuni haya ni wajibu mfahamu Habari zangu"

Na tukimhukumu kwa upande wa utukufu kutokana na utukufu aliouacha kwa watu, tunasema kuwa hakika Muhammad mtume wa waislamu ni mtukufu katika watukufu katika historia, kwa hakika alizuia kundi lenye upendeleo na lenye kuzusha mambo, na akaiwekea mbadala dini ya kiyahudi na kikristo na dini ya makao yake ya zamani, akaiwekea Dini iliyokuwa wazi na yenye nguvu, iliweza kubakia mpaka leo hii ni yenye nguvu na hatari kubwa"

Haijapata kuwahi Historia kuandika kuhusu mtu asiyekuwa Muhammad, alikuwa ndiye mwenye ujumbe na mwenye kuujenga umma na mwanzilishi wa Dola, mambo haya matatu ambayo aliyafanya Muhammad yalikuwa ni mambo tofauti yaliyoshikanishwa, na dini ndiyo ilikuwa ndiyo nguvu iliyovishikanisha kwa muda wote kihistoria. (111).

Na waliashiria baadhi ya manaswara -wakristo- namna ulivyokuwa msimamo wa Muhammad kuhusu Issa -juu yake amani-, na kumheshimu kwake katika Hadithi na Qur'ani aliyoteremshiwa, anasema mustashriki wa kifaransa aitwaye (Louis-Pierre-Sedillot): "Kwa hakika umefika wakati ambao

mtazamo unaelekea kwenye historia ya ule umma ambao ulikuwa jambo lake halijulikani pembezoni mwa Asia kisha ukapanda katika nafasi ya juu zaidi, na likafanyiwa kazi jina lake katika pembe za dunia kwa muda wa karne saba, na chimbuko la huu muujiza ni mtu mmoja, ambaye ni Muhammad". Anasema (Lady E.cobold) ambaye alisilimu na akautembelea Mji wa Madina mwamke huyo aliandika kwa hisia zake kwa kusema: "Walikuwa warabu kabla ya Mtume Muhammad hawana lolote wala hawakuwa ni wenye kuyatilia umuhimu makabila yake wala umoja wake, na alipokuja Muhammad - **Rehema na amani ziwe juu yake**-aliufufua umma huu na ukawa mpya unaofaa kuwa karibu na miujiza, na ukaushinda umma huu ulimwengu na ukahukumu mpaka mwisho"(112)

ZAMA ZA BWANA MTUME -SALA NA AMANI ZIWE JUU YAKE.

Kwa hakika mazungumzo kuhusu Historia ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-yatupasa kuzungumzia mpaka zama zake na wakati alioishi kwa umakini, nao ndiyo muda ujulikanao kwa wachunguzi kwa jina la Nyakati, japokuwa yanayofungamana na ujuzi wa Historia ya Bwana mtume yanaanzia kabla ya kuzaliwa Mtume Sala na mani ziwe juu yake- kwa hivyo mwanzo wa wakati wa zama za bwana mtume kabla ya kuzaliwa kwake kwa muda kidogo ni ngumu sana kuthibitisha nyakati, kutokana na kufungamana kwake na maisha ya makuaraishi wa Makkah, na pia maisha ya wazazi wake Mtume wa ALLAH.

Na kuzaliwa kwake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ilikuwa ni siku ya Juma tatu katika Mwaka wa Tembo, na jambo hili limethibiti kwa tamko la hadithi ya Bwana Mtume Sala na amani ziwe juu yake- amesema: "Siku ya juma tatu ni siku niliyozaliwa", (113) Na maulamaa wengi wametaja kuwa kuzaliwa kwake ilikuwa ni tarehe 12 mfungo sita katika mwaka wa Tembo na inawafikiana na Mwaka 571 A.D.

Na ikiwezekana kuweka mpaka wa zama za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kwa umakini kuanzia kuzaliwa kwake mpaka kufa kwake, basi haiwezekani kumweka mbali na mambo yaliyomtangulia. (114)

Ama kuhusu mwisho wa zama za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ni mahala walipowafikiana maulamaa kikamilifu, pale ambapo ilikuwa kufa kwake **-reheema na amani ziwe juu yake-** ni mchana wa siku ya Juma tatu Tarehe 12 Mwezi wa Mfungo sita sawa na tarehe 8 Mwezi wa 6 mwaka 633A.D.(115)

Na huenda katikati mwa zama hizi palitokea tukio la kuhama ambalo nimeligawa kwenye makundi mawili makuu, na tukio hilo lilikuwa katika mwaka wa kwanza wa Hijiria ambao sawa na mwaka 622 A.D.(116)

Mji wa Bwana Mtume Sala na amani ziwe juu yake:

Ni mji wa Makkah au Ummul-quraa (117) ndiyo mji alipozaliwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na katika mji huo ndipo alipopewa utume, na katika mji huo ndipo alipolelewa na kukulia na kuoa, na kufanya kazi na maisha yake marefu yalikuwa humo, na kulelea kizazi chake na akachagua maswahaba wake.

Mji wa Makkah upo chini ya bonde mahala alipomuweka Nabii Ibrahim mke wake Hajira na mwanawe Ismail, Amesema ALLAH mtukufu:

﴿رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ فَاجْعَلْ أَفْئِدَةً مِنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ وَارْزُقْهُمْ مِنَ الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾﴾ [إبراهيم:

[37

"Ewe Mola wetu hakika mimi nimewekeza kutokana na kizazi changu ndani bonbe lisilokuwa na mimea kwenye nyumba yako tukufu Mola wetu ili waweze kusimamisha swala basi jalia mioyo ya watu iwe ni yenye kuelekea kwao na uwape riziki zitokanazo na matunda ili wapate kushukuru." [Surat Ibrahim: 37]

Makkah ulikuwa ni mji wa Tauhidi wa kwanza katika miji ya waarabu kuanzia wakati wa bwana wetu Ibrahim na mwanawe Ismail (juu ya wawili hao amani), pale ambapo Ibrahim alipoiomba Makkah na watu wake, na akajenga Al-kaaba na wakahiji nyumba hii tukufu manabii baada yake.

Amesema Allah Mtukufu:

﴿وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنَا وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَنَّ طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢٥﴾ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ مَنْ ءَامَنَ مِنْهُم بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ قَالَ وَمَن كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٢٦﴾ وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾ رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا إِنَّكَ أَنْتَ الرَّؤُوفُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾ رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ ءَايَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾﴾ [البقرة: 125-129]

"Na pindi tulipo ifanya nyumba (alkaaba) kuwa ni marejeo kwa hali ya kuwa ni amani na tukajalia kutokana na mahala alipo simamia ibrahimu kuwa ni sehemu ya kufanyia ibada na tukampa ahadi ibrahim na ismaili kuwa isafisheni nyumba yangu kwa wafanyao tawafu na wenye kukaa ndani ya msikiti na wenye kurukuu na kusujudu." Na pindi alipo sema Ibrahim ewe MOLA wangu ijalie nyumba hii iwe yenye amani na uwape watu wake kutokana na matunda atakaye muamini ALLAH miongoni mwao na siku ya mwisho akasema ALLAH na atakaye kufuru nitampa starehe kidogo kisha nitamsongesha mpaka kwenye adhabu ya moto na ni mafikio mabaya mno." Na pindi alipo nyanyua Ibrahimu nguzo za nyumba na Ismail ewe MOLA wetu tukubalie sisi hakika wewe ni msikivu mwenye elimu." (127) "Ewe Mola wetu, na utujaalie, sisi wawili, ni wenye kusimama imara juu ya Uislamu, ni wenye kukufuata kwa Imani. Utuonyeshe njia za kukuabudu. Utusamehe madhambi yetu. Hakika Wewe Ndiye Mwingi wa kukubali toba za waja wako, Ndiye mkunjufu wa rehema kwao. MOLA wetu watumie kwa wao mtume miongoni mwao awesomee juu yao aya zako na awafundishe Qur'ani na sunnah na awatacase hakika wewe ni mwenye nguvu mwenye hekima. Suratil Baqara: (129-125)

Ama tabia ya nchi ya mji wa Makkah kijiografia unatofautiana na kisiwa cha waarabu, kwa kuzungukwa na jangwa na milima katika kila sehemu.

Na wanaishi makuraishi na washirika wake katika mji wa Makkah, nalo ni kabila lililostaarabika lenye misafara ya kibiashara, na mahusiano mazuri ya nje, ukilinganisha na makabila na miji mingine. (118)

Makkah ilikuwa maarufu kutokana na uwepo wa Al-kaaba ambayo alijenga Ibrahim -Amani iwe juu yake- amesema ALLAH mtukufu:

﴿وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ﴾ [البقرة: 127]

"Na pindi alipo nyanyua Ibrahim nguzo za nyumba na Ismail ewe MOLA wetu tukubalie sisi hakika wewe ni msikivu mjuzi." Suratil Baqara: (127)

Ilikuwa Makkah imegawanyika mara Nne, kati ya mgawanyiko wa makuraishi na matawi yake mbalimbali, na yawezekana kupitia kabila hilo kuainisha makazi yao na majumba yao na mikusanyiko yao ndani ya Makkah, kama ilivyokuwa jamii hii ina wadhifa maalumu katika kabila, miongoni mwa nyadhifa hizo ni Kunyweshwa mahujaji, kutoa mali kusaidia mahujaji, na kushika hatamu za uongozi, (199) kama ambavyo kabila hili lilikuwa na wadhifa wa kupanga ushuru utokanao na kodi ya biashara ya wenye kuja katika mji wa Makkah.

Na ulipata umashuhuri mji wa Makkah kwa kuitwa jumba la makongamano (120) ambapo hukusanyika humo watu maarufu wenye maono katika kabila la kikuraishi, nao ni wakubwa ambao walikuwa wakifanya juhudi kulipa nguvu kabila la kikuraishi na kuutunza umoja.

Kama walivyokuwa wameshikamana na ujinga wao wakiuhami upotofu wa kikuraishi hali ya kuihifadhi tamaduni zao za kuabudu masanamu na vinginevyo, kama wanavyodhani kwa kila ujinga na upofu uliokuwa mbali na haki na ubaguzi wa batili. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ ءَاثِرِهِم مُّهْتَدُونَ﴾ [الزخرف: 22]

"Wakasema hahika sisi tumewakuta baba zetu wakiwa juu mila na hakika sisi juu ya alama zao ni wenye kuzifuata." (Surat Zukhruf: 22).

Kwa hivyo walikuwa na fikra dhaifu walizozirithi bila kutumia akili, wakiiga baadhi ya mambo fulani na wanakosa utoaji wa maamuzi katika mambo fulani. (121)

Walikuwa wakizini wakinywa pombe na wakila Riba na wakicheza miziki na kila aina ya matamano, yalikuwa yakiwashinda matamano kwa hoja yakuwa hawaamini kufufuliwa na kuhesabiwa,(122) Amesema ALLAH Mtukufu.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَاللَّبْسُ وَأَلْأَنصَابُ وَأَلْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ

﴿فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾ [المائدة: 90]

"Enyi mlio amini hakika ya pombe na kamari na mizimu na kuangalia ramli ni uchafu utokanao na shetani jiepusheni naye ili mpate kufaulu". (Suratul Maidah 90).

Ilikuwa Shirki imekithiri katika mji wa Makkah"(123)

NASABA YA BWANA MTUME SALA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:

Jina lake ni Muhammad Bin Abdillahi Bin Abdul muttwalib (Shaibah) Bin Hishaam Bin Abdi Manaaf, Bin Mudhir, Bin Kilaab, Bin Murra, Bin Kaa'ab, Bin Lua'i, Bin Ghaalib, Bin Fih'ri, Bin Maalik, Bin

Nadhwar, Bin Kinaanat, Bin Khuzaimata, Bin Mud'rikata, Bin Ilyasa, Bin Mudhir, Bin Nizaar, Bin maa'ad, Bin Ad'naan, Bin Adiiy, Bin Udad, Bin Muqawwim, Bin Naahuur, Bin Tairuh, Bin Yaa'ruba, Bin Yash-jab, Bin binThaabit, Bin Ismail, Bin Ibrahiim -juu yake amani- (124)

Na baada ya Adnaan kuna angalizo kwa maulamaa wengi isipokuwa kuungana kwake na Ismail, (125)

Na kwa hakika imepokelewa kuwa yeye Mtume Sala a na amani ziwe juu yake amesema: "Hakika ALLAH alimteua kutoka katika watoto wa Ibrahim Ismail, na akamteua kutoka kwa Ismail Kinanah, na akamteua kutoka kwa Kinanah, Quraish na akamteua kutokana na kabila la kikuraishi watu wa Hashim, na akaniteua mimi kutokana na Banii Hashim, na mimi natokana na aliye bora kutoka kwa aliyebora kutoka kwa aliyebora"

KUZALIWA KWA MTUME KIPENZI -SALA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:

Abdillahi Bin Abdulmuttwalib mzazi wa Bwana Mtume alimuoa Amina Bint Wah'bu Mama ya Bwana Mtume Rehema na mani ziwe juu yake, na akakaa naye muda mfupi na ikatokea mimba yake ya kumzaa Bwana Mtume -Sala na mani ziwe juu yake-, na mimba ikaendelea baadhi ya miezi, mara akafariki Abdullahi mzazi wa Bwana Mtume kabla ya kufikia muda wa mimba kuzaliwa (127) na akaruhusu Mwenyezi Mungu mtoto kuzaliwa katika viunga vya Makkah, kabla ya mama yake kumzaa aliota ndoto kama ilivyokuja kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake: "Hakika mimi kwa ALLAH ni Nabii wa Mwisho, na Adamu, kwa hakika Nabii Adam ameumbwa kutokana na udongo wake na nitakupeni habari kuhusu hilo, mimi ndiye dua ya Ibrahiim na bishara ya Nabii Issa, na ndiye ndoto ya mama yangu ambaye aliota na vilevile ndiyo Ndoto waliyoiona wamama wa manabii". (128)

Na Inasemekana kuwa mama yake aliota ndoto wakati wa kumzaa kwake kanakwamba Nuru ilitoka kwake na ikaangaza nuru hiyo Basra katika Ardhi ya Sham. (129)

Tarehe ya kuzaliwa kwake haijaacha kuwa na kutofautiana rai katika hilo (130) licha ya kuwa imethibiti kutoka kwake yakuwa amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake: "Siku ya juma tatu ni siku niliyozaliwa" ,(131)

Na katika hali ya kuzaliwa ilikuwa ni vigumu kudhibiti, kwa kuwa alikuwa wakati huo kwa watu ni mtoto wa kawaida kabisa aliyezaliwa yatima, lakini yeye kwa ALLAH alikuwa ni mteule katika watu, na ni mwisho wa Manabii na katika waja wake walio bora kabisa, na hapakuwa na kiumbe yeyote ajuaye muda wa kuzaliwa kwake au kujua wakati wa mimba yake, na ingekuwa si hivyo wangepanya bidii ya kumuudhi mashetani wa kibinadamu na kijini, Hivyo Mwenyezi Mungu akaficha siri yake na hakuweza yeyote kujua siri hiyo hata yeye mwenyewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakujua. Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا أَكْتُبُ وَلَا الْإِيْمَنُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ﴾ [الشورى:

[52

"Na kama vile tulivyowapelekea wahyi Manabii kabla yako wewe, ewe Nabii, tulikuletea wewe wahyi wa Qur’ani itokayo kwetu, hukuwa unajua kabla yake ni vitabu vipi vilivyotangulia wala nini Imani wala zipi Sheria zinazotoka kwa ALLAH, Lakini tumeifanya Qur’ani ni mwangaza kwa watu ambao kwao tunawaongoza waja wetu tunaowataka kwenye njia iliyolingana sawa. Na hakika wewe, ewe Mtume, unaelekeza na kuongoza kwa amri ya ALLAH kwenye njia iliyolingana sawa, nayo ni Uislamu" [Ash shura: 52].

Na kwa hakika walijitahidi Maulamaa kudhibiti siku aliyozaliwa, wakasema baadhi yao kuwa yeye alizaliwa tarehe 12 mfungo sita katika mwaka wa Tembo, (132) sawa na mwaka 571, tangu kuzaliwa yesu. (133) na hii tofauti ya siku ya kuzaliwa kwake haipunguzi Heshima yake -Sala na amani ziwe juu yake, hivyo yeye ataendelea kuwa ni Bwana atokanae na watoto wa Adam na hakuna shaka katika hilo, na wala haikutajwa kuwa yeye Mtume alihangaika kudhibiti siku ya kuzaliwa kwake.

Na ama sehemu aliyozaliwa Mtume -Sala na mani ziwe juu yake- ilikuwa ni katika nyumba ya Ami yake Abuu Twaalib ukoo wa banii Haashim, na ilikuwa nyumba hiyo kwa muda wa karne mbili mfululizo ni miongoni mwa nyumba zilizokuwa jirani mwa Al-kaaba nyumba hiyo ilihama kutoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mwingine mpaka alipohiji mama yake Harouna Rashiid aitwae Al-Khaizaraan katika utawala wa Harouna Rashiid akifanya nyumba hiyo kuwa msikiti, na nyumba hiyo ipo karibu na msikiti wa Makkah na kwa sasa sehemu yake inajulikana, napo ni pale ilipo Maktaba ya Makkah Tukufu kwa upande wa mashariki kutoka katika uwanja uliokamtana na sehemu ya kufanyia Saa'yi, na habari hizo zimepokelewa na kundi kubwa la wanawazuoni wa Makkah na pia watu wa Makkah.

Na baada tu ya kuzaliwa alinyonyeshwa na Kijakazi wa Abii Lahab Baba yake mdogo kijakazi aitwae Thuwaibat (134) na akamlea Barakatul Habashiyyat (Ummu Aiman) Kijakazi wa Baba yake mzazi Abdullah, na alikuwa Abdillahi akimtendea wema maisha yake yote, hapo akasilimu na akahama kwenda Madinah, na akashuhudia kufa kwa Mtume.

Jambo la kwanza alilolifanya mama yake Mtume na wanawake waliokuwa pamoja naye, baada tu ya kuzaliwa kipenzi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alimpeleka haraka kwa babu yake mzee Abdul muttalib akimpa bishara njema ya kuzaliwa mtoto huyo

yatima wa kipanzi chake ambaye ni mwanaye Abdullah, akampokea Abdulmuttwalib kwa haraka na furaha na akamkumbatia kifuani kwake, huku akikumbuka uyatima wake na na kumkosa mzazi wake Abdullah, na akamchukua mpaka Al-kaaba akamshukuru Mwenyezi Mungu na akamuomba Dua (135) na akamuita Muhammad, nalo ni jina Nadra sana bali linakaribia kutokuwepo kwa waarabu wakati ule.(136)

YATIMA ALIYELELEWA NA ALLAH:

Kabla ya kuzungumzia uyatima wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- inadhihirika katika akili upatilizaji wake ALLAH na kumchungwa kwake kwenye uyatima wake, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ﴾ [الضحى: 6]

"Hivi hakukukuta ni yatima akakupa mahala pazuri pa kukaa". (Surat Dhuha: 6). Na alikuwa Mama yake Mtume Amina Bint Wahab akimuonea huruma na kumfanyia upole, kuanzia pale alipomzaa baada ya kufa Baba yake Abdullah, na alikuwa babu yake Abdul muttwalib akisimamia nafasi ya mzazi wake akimlea na kumfanyia upole muda aliyobakia katika maisha yake, mpaka akafikia Mtume umri wa miaka minane akaacha kunyonya kwake kutoka kwa banii Saad.

Kwa hakika uyatima wake uliongezeka kutoka kwa baba yake kwenda kwa mama yake, pale alipofariki mzazi wake Amina Bint Wahab alipofikia Mtume -Rehema na mani ziwe juu yake- miaka sita na alikuwa safarini kuelekea madinah, na wakati wa kurudi alifia sehemu iitwayo Ab-waa na alizikwa huko.

Na kijakazi wake aitwae ummu Aiman akambeba na kumlea, na akaendelea na safari yake kwenda Makkah mpaka akamfikisha kwa Babu yake Mzee Abdul Muttwali, upole wake na uangalizi wake ukazidi kwake, na akaendelea Ummu Aiman kumlea akifuatilia hali

yake na wakati huo huo Babu yake anafuatilia maisha yake, na alikuwa Ummu Amani akimpenda sana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na akimuonea huruma na mtume alijua huruma hiyo na alikuwa akiuunga udugu katika mji wa Madinah baada ya kuhama Makkah (137) na akawa akisema kuhusu Ummu Aiman kuwa "Huyo ni Mama yangu baada ya kufa mama yangu".

UJANA WAKE MTUME-Sala na Amani ziwe juu yake.

Alikulia Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake katika uangalizi wa Babu yake Mzee Abdul muttalib, na akafariki hali yakuwa ana umri wa miaka Nane, akamlea na kumchungu Baba yake mdogo Abu Twaalib, na aliishi kwake- Sala na amani ziwe juu yake na amani- utoto wake wote kisha ujana wake, na Abuu Twaalib alikuwa anamafungamano naye akimpenda. Na kwa hakika zimejulisha Pokezi tofautitofauti kuwa Abuu Twaalib alikuwa pamoja naye katika safari yake ya kwenda Shamu (138) na kwa hakika zimeleta baadhi ya Riwaya kisha cha Bahira aliyekuwa ni Kasisi katika safari na Abuu twaalibu kwenda Sham, nayo ni Riwaya wametupilia mbali Maulamaa wengi pamoja na kuwa imepokelewa kwa Isnaad zenye kukubalika kutoka kwa Tirmidhiyy na wengineo, na kwa hakika Imamu Dhahabiy ameitilia shaka riwaya hiyo (139) na pia Bin Qayyim katika kitabu chake Zaadil Maad (140) na Maulamaa wengine wa zama hizi katika, Historia (141) Kwa hakika waliitumia fursa wengi katika Mustashrikiina kujaribu kubadilisha mafungamano ya mtume na uislamu kwa yale aliyokutana nayo toka kwa Kasisi, na kubadilisha mafungamano ya yake na Qur'an kwa alivyojifunza kutoka kwa Kasisi, wakijitoa ufahamu wa kutojuwa misingi midogo tu ya kielimu ijulikanayo kiakili na upimaji wa mambo, na udogo wa umri wa mtume kama Riwaya na safari aliyosafiri ingekuwa ni sahihi, kama anavyoeleza mtunzi, wako wapi na mpaka wasijue ufuatanaji wa kuteremka Qur'an kwa mujibu wa matukio ambayo Aya zimeyataja maisha yake yote -Sala na amani ziwe juu yake-mpaka mwisho mwa maisha yake, lakini upofu wa

kutoiona haki na kumchukia Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ndiyo kumewapelekea washikamane na hizi Riwaya wakijitoa ufahamu wa kutojuwa misingi midogo tu ya kielimu kwa kufuata matamano ya nafsi zao. (142)

Alikuwa Mtume Sala na mani ziwe juu yake akihisi kuwa anajukumu la kukutana na baba yake mdogo Abuu Twaalib, na akijitahidi kwa nguvu zote kumpa awezacho kwa ajili ya kusaidia kuondosha umasikini kwa watoto wake na kwa ajili hiyo, alishughulika mtume Sala na mani ziwe juu yake-katika kuchunga mbuzi akiwa na umri mdogo, na alikuwa akimsaidia Baba yake mdogo kwa kile anachokipata katika mali kutokana na malipo ayapatayo kwa ajili ya kazi hiyo, amesema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake: "Hakuwahi ALLAH kumtuma Mtume isipokuwa Mtume huyo alichunga Mbuzi, maswahaba wake wakasema na hata wewe Mtume wa ALLAH, akasema: Ndiyo nilikuwa nachunga kwa watu wa Makkah kwa malipo kiasi fulani" (144)

Kazi ilikuwa ni katika mlango wa chumo ambalo linaipa utukufu nafsi, na kutowategemea watu wengine, na kusaidia mahitajio ya Bwana mtume na Baba yake mdogo kutokana na chumo litokanalo na uchungaji mbuzi, na kwa hakika alikuwa mtume -Sala amani ziwe juu yake ni mwenye kujitahidi, akiwafundisha maswahaba kufanya kazi na kutafuta chumo na uzalishaji na kujiepusha na kuwategemea watu wengine, na kuishi maisha ya kupambania kipato.

Na alikwa Mtume tangu anaanza kupata ufahamu ni mwenye kuyachukia masanamu, na kuyakasirikia, wala hakuwahi kushuhudia yalipo.

Na ALLAH alimuhifadhi na kutomuasi kabla ya kutumwa kwake-Sala na amani ziwe juu yake- siyo katika udogo wake wala ujana wake na alimuhifadhi na kila jambo baya.(146).

Kama alivyokuwa Bwana Mtume Sala na amani ziwe juu yake anachukia pombe licha yakuwa pombe ilikuwa imeenea katika mji wa Makkah na wala haikufahamika kuwa yeye aliwahi kuinywa hata kidogo.

Ukweli na Uaminifu vilikuwa ni katika sifa za Mtume Sala na amani ziwe juu yake- kuanzia utotoni mwake mpaka ujana wake (147) na alikuwa mtaratibu mpole licha ya ututo wake na ni kweli kama alivyosema -Sala na amani ziwe juu yake-: "Alinifunza adabu Mola wangu na akaifanya adabu yangu kuwa nzuri zaidi"⁵⁸.⁵⁹

Ni kweli kwa hakika ALLAH alimchagua, na akamuhifadhi na kumlinda kabla ya kupewa utume na baada ya kupewa utume (149) Hiyo ilikuwa ni ngome ya ALLAH na haikuwa isipokuwa kwa Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake, na ni malezi ya ALLAH na mafunzo ya tabia toka kwa muumba aliyetukuka na aliye juu, na akasema Mtukufu:

﴿اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ﴾ [الأنعام: 124]

"ALLAH hujuwa zaidi wapi auwekapo ujumbe wake" (Suratul An-aam 124.)

Uanaume wake Mtume- Sala na amani ziwe juu yake:

Alipofikia Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- utu uzima alikuwa ni mwenye kuheshimiwa na watu na kukubalika, na hajawahi kujulikana mtu yeyote aliyekuwa mkweli kuliko yeye katika

⁵⁸ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/188.

⁵⁹ Yameshatangulia maelezo yake

mji wa Makkah wala mwenye uaminifu zaidi kuliko yeye, mpaka akajulikana kwa jina la Mkweli muaminifu. (150)

Alijulikana Rehema na Amani ziwe juu yake kwa kuunga undugu, na upole wake kwa mafukara na wenye mahitajio, na twaweza kufupisha kwa kutaja sifa zake muhimu katika zile alizozisema Khadija -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- na kwa hakika Khadija alimpa habari ya kukaribia kunyanyuliwa daraja. "Hakuwa ALLAH ni mwenye kukufedhehesha hata kidogo, kwa hakika wewe utaunga udugu, na utamkirimu mgeni na utawasaidia wasio jiweza, na utaleta visivyokuwepo, na utatoa msaada wakati wa matatizo" (151)

Alikuwa anabeba sifa za uanadamu na upole pamoja na Fadhila, ni mtakasifu zaidi na mwema kwa watu, na ni muadilifu na mwenye Tabia ya hali ya juu kuliko watu wote -Sala za ALLAH ziwe juu yake.

Kuanzia ujana wake mpaka na utu uzima wake kabla ya kupewa utume na baada ya kupewa utume ilikuwa kipaumbele chake ni uadilifu na usawa, na kutomdhulumu mtu yeyote na kwa namna hiyo ndiyo maana akashiriki uekeanaji ahadi na baadhi ya makuraishi na umri wake ukiwa ni miaka ishirini (25)⁶⁰(kiapo cha Fudhuul) pale kilipo fungwa katika nyumba ya Abdillahi Bin Jad-aan, na alikuwa ni katika watukufu wa Makkah, kiapo kilihusu kuwa wawe na nguvu ya pamoja na mwenye kudhulumiwa dhidi ya dhalimu mpaka atoe haki ya mwenye kudhulumiwa.⁶¹

Alikuwa Mtume ana marafiki wenye kujulikana na kutambulika kwa ukweli wao na tabia za hali ya juu katika kiwango hiki, na kiongozi wao alikuwa ni Abuubkar Swiddiq -Radhi za ALLAH ziwe juu

⁶⁰ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad ukurasa wa 128.

⁶¹ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad ukurasa wa 128.

yake- (154) ambaye alikuwa karibu na umri wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alikuwa amezoeleka kwa makuraishi, zaidi ya huyo alikuwa ana marafiki wengine waaminifu, imepokelewa kuwa mtume aliwasifia marafiki hao.

Ulikuwa uaminifu wake Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake- ni wenye kukodolewa macho, na makuraishi kulikuwa miongoni mwao na mwenye kuizungusha mali yake na atakayemfanyia Biashara atapampatia malipo maalumu, na alikuwa Bi Khadija Bint Khuwailid -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- ni katika matajiri wa kikuraishi, alikuwa hamuamini kila mtu anayefanya Biashara kwa mali yake, jambo ambalo wanaume wengi walitaka hivyo, lakini pamoja na yote hayo alikuwa akiuliza na kuchunguza na kutafuta mtu atakayekuwa muaminifu zaidi ili aifanyie kazi mali yake, na awe na uzoefu katika nyanja hii, Basi akamsikia Muhammad Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu ukweli wake na uaminifu wake, hivyo akafanya haraka kumuajiri ili aifanyie kazi mali yake malipo atakayompa itokanayo na faida, akakubali Rehema na amani ziwe juu yake- kufanyia kazi mali ya Khadija.

Basi akasafiri Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika Biashara ya Khadija kwenye masoko mbalimbali yanayozunguka mji wa Makkah katika miji ya Waarabu.

Alisikia Bi Khadija -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- kutoka kwa kijakazi wake aitwaye Maisara jambo lilotilia nguvu ukweli wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kutilia nguvu uaminifu wake na uzoefu wake, kwa hakika alikuwa ni mpole na mwenye muamala mzuri, akichunga haki za wengine, Khadija akapendezwa naye -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- akapendezwa na tabia za Mtume na uaminifu wake na kuipa kipaumbele heshima na tabia kuliko mali, na vyanzo vya habari vinatilia mkazo kuwa mali ya Khadija ilizidi kwa Baraka za Mtume na kuifanyia kazi mali hiyo kwa uaminifu.

Na hapana shaka kuwa safari za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- safari za biashara ya khadija na kuingia kwake masoko ya waarabu na kuchanganyikana kwake na watu na wakubwa wa kiarabu na kukutana na makabila matukufu kwa hakika kulimpa faida nyingi, na akaweza kukuza uzoefu wake na kuwajua watu na makabila na miji na habari za miji hiyo.

KUMUOA KWAKE KHADIJA -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- (155)

Khadija Binti khuwailid Bin Asad Bin Abdul Izah Bin Quswaiy, Bin Kilaab (156) alikuwa ni Bibi mwenye heshima akili na hekima, mzazi wake wa kiume ni Khuwailid Bin Asad ni katika watukufu wa Makkah, aliuliwa katika vita vya uovu, aliolewa kabla ya kuolewa na mtume kisha akajitenga, alikuwa ni mwenye mali nyingi alihesabika ni katika matajiri wa Makkah alikuwa akiwakodisha wafanya biashara ili kuizalisha mali yake na alikuwa Mtume ni miongoni mwa waliokodishwa na Khadija na akampa majaribio akawa ni muaminifu.

Kama ambavyo Khadija kwa hakika alijadiliana na mtume-Sala na amani zie juu yake na akamsikiliza na akafanya nae kazina akamuona kuwa ni mwenye tabia ya hali ya juu mwenye tabia nzuri basi khadija akampenda mtume na tabia nzuri ikampendeza na alikuwa khadija akiitwa kwa watu wake kwa jina la (msafi aliyeepukana na machafu)⁶²

Alikuwa Khadija katika umri wa miaka Arobaini na walipupia wakubwa wa kabila la kikuraishi kutaka kumposa na kumuoa lakini yeye khadija alikuwa akizirudisha posa kwa heshima (158) na

⁶² Siirat Nabawiyyat kutoka katika Twabakati cha Bin Saad juzuu ya 1/130, Bin asaakir Taarikha Dimashqi ukurasa wa 109; Bin Kathiir siirat Nabawiyyat juzuu ya 1/263.

alikuwa akijua kuwa baadhi yao walikuwa wakisukumwa na mali na vinginevyo, naye ni mwenye mali kila mmoja anazitamani.

Na wakati Mtume anamfanyia kazi khadija alijua kutokuwa na tamaa ya mali pamoja usafi wake na utwahara wake na tabia yake ya kiwango cha juu hivyo basi akavutiwa na kuolewa naye (159)

Na hapana shaka yakuwa ALLAH amemuandalia mtume wake yaliyo mema na akamchagulia mwanamke aliye mwema ambaye alipenda kuolewa na mtume kwa juhudi zake khadija na kwa hekima za ALLAH.

Na kwa heshima zote Khadija alimtumia miongoni mwa sahiba zake ambaye atamuanzishia jambo hilo na kumuashiria jambo hilo, basi yule swahiba wa khadija akamuanzishia Mtume na akambainishia mapenzi ya khadija kupenda kuolewa naye, pamoja na utukufu aliokuwa nao na heshima yake na katika Nasaba yae, na kuwa mapenzi yake kwa mtume yanatokana na uzuri wa tabia yake na ukweli wa maneno yake, na inasemwa kuwa Nafiisat bint Maniyyat alikuja kwa mtume naye ndiye mpeleka posa na akasema: ni kitu gani kinakuzuia kuo? akasema sina chochote ninachomiliki cha kuniwezesha kuo, akasemana ikiwa utapewa cha kuolea na ukaitwa kumuoa mwanamke mzuri mwenye mali na utukufu na akawa ni mwenye kutoshana nawe vipi hautokubali? basi akauliza Mtume ni nani huyo akasema ni Khadija, akasema mtume -**rehe**ma na amani ziwe juu yake- ni nani atakaye mfanya awe wangu, Nafisa akasema ni juu yangu mimi, (160) basi Mtume akapendezwa na kumuoa aliyetwahara msafi na mtu sahihi katika waliompenda na miongoni mwa walioandaliwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili yake na kumchagua.

basi akaenda haraka kwa baba zake wadogo, na akaenda pamoja nae baba yake mdogo Hamza na baadhi ya wakubwa wa kikuraishi wakaenda mpaka kwa baba mdogo wa Khadija aitwae Amru Bin Asad na wakampelekea posa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-

na ikatimia kwa Muhammad Bin Abdillahi kumuoa Khadija Bint Khuwailid- Radhi za Allah ziwe juu yake- ili awe mama wa waumini kipenzi cha mtume wa ALLAH ambaye ni mama wa watoto wake wa kiume na wa kike-Radhi za Allah ziwe juu yao- Mke wa duniani na peponi.

Ulikuwa Umri wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake- ni miaka 25, aliishi nae kwa muda wa miaka 24 na akamzalia watoto wote isipokuwa Ibrahimu, na kwa hakika alifariki Khadija Radhi za ALLAH ziwe juu yake- akiwa na umri wa miaka 65 na kwa hakika ndoa hii ilimpatia mtume raha ya moyo na malezi ya kiakili yaliyompambanua Mtume na kumpa heshima yake, ALLAH alimchagua Khadija na akamchagulia mtume wake katika wanaume wote kabla ya kupewa utume wake, alisimamia jambo la ALLAH na huruma zake pamoja na mtume wakati wa kuteremka wahayi, na akatumia akili yake na akampenda kwa kule kujua sifa na tabia, na huruma ya ALLAH kwa waja wake wema na dhana yake nzuri kwa ALLAH, na kuwa yeye hawafedheheshi walio wema, wanawazuoni wa zama zake kama vile (Waraqatun Bin Naufal) pale alipo mchukua mtume rehema na amani ziwe juu yake kumpeleka kwa mtu anayemjua na kumkubali, yote haya ni matunda ya katika matunda ya Ndoa hii yenye baraka.

TUKIO LA KUIJENGA AL-KAABA:

Al-kaaba kabla ya kutumwa mtume kwa kiasi cha miaka 25, ilikumbwa na matukio mawili yaliyosababisha kuporomoka jengo lake, pale ambapo makuraishi walikuwa wakiifunika kwa ngozi na sufi ambazo hutengenezwa kwazo mapazia ya Al-kaaba, huunganishwa baadhi yake na baadhi nyingine na ilikuwa ni Ada yao kabla uislamu waifukize Al-kaaba kwa kutumia mafusho, basi kaa la moto likaipata pazia za Al-kaaba hivyo ikaungua na kuporomoka, kisha ikakumbwa na amafuriko yakabomoa upande mmoja wa Al-kaaba, wakapitisha maazimio makuraishi kuijenga upya.(161)

Ulikuwa utaratibu wa ujenzi katika mji wa Makkah ni mwepesi, nguzo zake ni mawe na udongo, na paa linakuwa la mbao nyepesi, na kwa hakika ilipita safina ikija kutoka katika miji ya Italia ikielekea Ethiopia, na ilipofika karibu na Bandari ya Shuaibah (162) iliyopo magharibi mwa mji wa Makkah nayo ni Bandari yake ya zamani kabla ya uislamu safina ile ikakumbwa na Dhoruba, na ilikuwa imebeba mbao, na nahodha wake alikuwa mtu mmoja aitwae (Baquum) maarufu kwa Useremala na wakaja makuraishi wakazichukua mbao hizo, na wakamuita Fundi Seremala wa kabila la Qibtwiyyat ili atengeneze paa la Al-kaaba, na wakaanza Makuraishi kubomoa sehemu iliyobakia ya Al-kaaba ili waweze kuijenga upya (163) mpaka wakafikia msingi fulani ambao kwao ni maarufu hawawezi kuuvuka wala kuugusa (164)

Walitoa makuraishi mali ya halali kwa ajili ya ujenzi, na wakamtaka msaada (Baaquum)(165) toka katika kabila la Qib-twiya na wakagawana matumbo ya kikuraishi kona za al-kaaba pale ambapo kila watu wana upande wao wa kuujenga kwa vile wanavyoona kuwa ni heshima na ufahari, na ili heshima hiyo isiende kwa baadhi ya koo za kikuraishi bila koo zingine kuipata. (166).

Na walipo maliza kuijenga Al-kaaba walitofautiana kuhusu nani atakaeweka jiwe jeusi mahala pake mpaka wakakaribia kupigana.(167)

Kisha wakakubaliana kuwa ahukumu yule wa kwanza kuingia msikiti mtukufu, na akawa wa kwanza kuingia nyumba tukufu ni Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na walipo muona tu wakapiga ukelele wote kwa kusema "Huyu ni Mwaminifu Huyu ni Muhammad tumemridhia muaminifu" na huu ni ushuhuda wa moja kwa moja kutoka kwa watu wake mpaka wale waliokuwa wakimfanyia uadui baada ya hapo (168).

Na hapakuwa na kazi nyingine kwa Mtume isipokuwa ni kuiweka shuka yake na kuliinua jiwe jeusi na kuliweka katika shuka, na

akaamrisha kila kabila washike ncha za shuka yake na waibebe mpaka itakapo fika mahala pake katika sehemu ya Al-kaaba akaliweka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- jiwe kwa mikoni yake mitukufu, basi wakaridhia watu wote na zikaridhia nafsi zao⁶³.

Kwa hakika wamekata utata wanahistoria yakuwa wakati wanarudia kuijenga Al-kaaba Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alikuwa na miaka thelathini na tano (35)⁶⁴.

VIDOKEZO VYA KABLA YA KUPEWA MTUME:

ALLAH -Aliyetakasika na kutukuka-, amemchagua Mtume wake na akamfunza adabu na akamlea na kumfunza kabla ya kumpa utume bali kabla ya kuzaliwa na baada yake,⁶⁵na hajawahi kujua mtu yeyote hilo kwa Hekima ambayo anaijua Mwenyezi Mungu, japo kuwa wanadamu wote na hasa hasa watu wa dini nyingine za mbinguni walikuwa wakimsubiri Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- na kabla ya kupewa utume yalimtokea baadhi ya mambo ambayo yana julisha kukaribia kutumwa kwake, kama alivyokuwa akifuata Mtume -Sala na amani ziwe juu yake na amani- alifuata baadhi ambazo zilikuwa ni zenye kumzidishia kuwa karibu na ALLAH na kufikiria katika ufalme wake.

Kisha ilikuwa katika hivi viashiria ni ndoto njema kama ilivyokuja katika Hadithi za Aisha -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- "Kwa hakika

⁶³ Siirat An-bawiyat juzuu ya 1/197 ya Bin Hishaam, Musnad imamu Ahmad juzuu ya 3/425

⁶⁴ Bidayat wanihaya cha Bin Kathiir juzuu2/324, siirat ya Mtume cha imamu Dhahabiy ukurasa77.

⁶⁵ Angalia Siirat Nabawiyat kitabu cha Abuu hassan An-nadawiy ukurasa 109, na ASiirat An-nabawiyat As-swalaabiy juzuu 1/76.

jambo la kwanza ambalo alianza nalo Mtume -sala na amani ziwe juu yake katika Wahyi ni ndoto ya ukweli aliyoiona akiwa usingizini, na alikuwa haoni ndoto isipokuwa ndoto ile huonekana wazi mithili ya mawingu ya asubuhi" (172)

Kisha akawa Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake-akitoka katika miamba ya Makkah na mabonde yake akifikiria katika uumbaji wa ALLAH akikata mabonde huku akizingatia na kufikiria na akiwa anamtaja ALLAH Mtukufu akimpwekesha katika mila ya Ibrahim⁶⁶.

Pamoja na yaliyopita kwenye umri wa Bwana Mtume-Sala na amani zie juu yake- kabla ya kupewa Wahyi, kwa hakika hakuwa ni mwenye kuteremshiwa Wahyi haikuwa ni kwa kutaka kwake kama alivyosema ALLAH Mtukufu: Waambie, ewe Mtume,

﴿قُلْ لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُ عَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَأْتُكُمْ بِهِ ۗ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ﴾ [يونس: 16]

«Lau ALLAH Angelitaka, asingaliwasomea hii Qur’ani, wala ALLAH Asingeliwajulisha nayo. Basi jueni kuwa hiyo ni haki itokayo kwa ALLAH. Kwani nyinyi mnajua kwamba mimi nimekaa na nyinyi muda mrefu kabla Mola wangu Hajauleta wahyi wa hiyo (Qur’ani) kwangu, na kabla sijaisoma kwenu. Basi hamtumii akili zenu kwa kuzingatia na kufikiri?» [Surat Yunus 16:]

Kisha Mtume akapendezeshewa kujitenga pale alipokuwa ni mpwekeshaji katika mila ya Ibrahimu, akichukia mambo waliyokuwa nayo Makuraishi, hali yakuwa anamwamini Mwenyezi Mungu peke

⁶⁶ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/234.

yake hali ya kufikiria ufalme wake, hivyo akapendezeshewa kujitenga na akachagua kujitenga na kukaa katika pango la mlima Hiraa (174) uliopo upande wa mashariki mwa mji wa Makkah mlima ambao kwa sasa unajulikana kwa jina la Jabal Nuur uko upande wa kushoto kwa mtu anayetokea Twaaf kwa kutumia njia ya Sail- kwa sasa- Basi alikuwa Mtume Sala na amani ziwe juu yake- akifunga na akijitenga katika pango la Hiraa kwa idadi ya siku na michana kadhaa kwa ajili ya kujikurubisha kwa ALLAH Mtukufu, pale alipoongozwa kufanya jambo hilo na wala hakuamrisha kufanya hivyo lakini ni tabia tu ya kimaumbile inayomfanya awe karibu na ALLAH- Mtukufu- Tabia yake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- mpaka ikafikia kusemwa kuwa yeye alikuwa akikaa mwezi mmoja katika kila mwaka na kwa hakika alipendezeshewa jambo hilo kama ilivyokuja katika hadithi ya Aisha -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- amesema: Kisha akapendezeshewa kujitenga na akawa anajitenga katika pango la Mlima Hiraa akimwabudu Mola wake masiku mengi yenye idadi kabla ya kurudi kwa watu wake na alikuwa akichukua chakula cha akiba kisha akawa akirudi kwa Khadija kwa ajili ya kuchukua tena chakula kama hicho mpaka ghafla akajiwa na haki na ye akiwa katika pango la Hiraa"⁶⁷⁶⁸

Na alikuwa Mtume katika hatua hii bado hajapewa utume kama alivyosema ALLAH:

⁶⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/234.

⁶⁸ Ameipokea Imamu Bukhari ,katika kitabu kiitwacho Fathul Baari, juzuu ya 26/197. Na Muslim juzuu ya 1/139/140.

﴿وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا أَلَكِنَّا وَلَا الْإِيمَنُ وَلَا كِنٌ جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ﴾ [الشورى:

[52

"Na kama vile tulivyowapelekea wahyi Manabii kabla yako wewe, ewe Nabii, tulikuletea wewe wahyi wa Qur'ani itokayo kwetu, hukuwa unajua kabla yake ni vitabu vipi vilivyotangulia wala nini Imani wala zipi Sheria zinazotokana na Mwenyezi Mungu, Lakini tumeifanya Qur'ani ni mwangaza kwa watu ambao kwao tunawaongoza waja wetu tunaowataka kwenye njia iliyolingana sawa. Na hakika wewe, ewe Mtume, unaelekeza na kuongoza kwa amri ya ALLAH kwenye njia iliyolingana sawa, nayo ni Uislamu" [Ash shura: 52].

Mwezi mtukufu wa Ramadhani ndiyo mwezi aliokuwa Mtume akipenda zaidi kujitenga na kufunga Swaumu kabla ya kupewa kwake utume, na alikuwa Bi Khadija akisubiri uwepo mbali wa mtume wakati alipokuwa anajitenga, na alikuwa anajua kuwa ni mtu wa kheri na hakuna kitakachompata kutoka kwa ALLAH isipokuwa kila lilokuwa la kheri, na akimliwaza na kumpa hamasa, na alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akimaliza kujitenga kwake na akirudi Makkah anaanzia Haram (Msikitini)⁶⁹na akatufu pambizoni mwa Al-kaaba akijiepusha na masanamu.

⁶⁹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/235.

Lilikuwa pango la Hira'a mkao wake KiJografia likimpa fursa yenye nguvu ya kuona Anga kwa nje na kuona Ardhi akiwa juu kileleni na fursa ya kujua utukufu wa uumbaji wa ALLAH Mtukufu⁷⁰.

Na alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuanzia alipojitambua, ni mkarimu mtoaji na ulizidi utoaji wake na ukarimu wake na ukazidi msaada wake kwa wenye kuhitajia wakati ulipofikia umri wake miaka Arobaini, mpaka ikawa ni sifa miongoni mwa sifa zake ambazo alijulikana nazo Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na Khadija alimtaja kwa sifa hizo wakati wa kuteremka wahyi, na huenda sadaka zake zilikuwa zikitolewa zaidi katika mwezi wa Ramadhani kabla ALLAH ya kuteremshiwa Wahyi kama ilivyokuwa kabla ya kupewa utume (Wakati ambapo alikuwa ni mkarimu zaidi katika wakati huo wa Ramadhani)⁷¹

⁷⁰ Siirat An-Nabawiyat ,kitabu cha Muhammad Abuu Shuhbat ukurasa 256.

⁷¹ Angalia hadithi ya Imamu Bukhari katika sahihi yake, mlango wa usemao Vipi ulikuwa manzo wa kushuka Wahyi,(5) juzuu ya 1/4.

KUPEWA UTUME NA KUCHAGULIWAKUWA MTUME.

KUTEREMKA KWA WAHYI:

Wahyi kwa ufahamu wa kisheria ((Ni ALLAH kuwajua Manabii wake na mitume wake kwa anavyowafikishia wao Ufunuo utokanao na sheria au kitabu)):⁷²kupitia mjumbe au moja kwa moja, na hucusudiwa yale aliyoyateremsha ALLAH kwa manabii wake, na neno Wahyi kwa lugha ya kiarabu: linamaanisha Utambuzi wa siri na wa haraka.⁷³

KUTEREMKA KWA WAHYI:

Hakujulikana Mtume Sala na amani ziwe juu yake- kutajwa kwake wala maneno kabla ya kushuka kwa Wahyi.

Na wala hajawahi kusema japo neno lolote kutoka kwake, na wala hajawahi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuongea au kujifunza kitu kitokanacho na Wahyi ulioteremshwa kwa Manabii waliotangulia, au mfano wake kabla ya kupewa utume, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدَى إِلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾﴾ [الشورى:

[52

⁷² Mtunzi Sub-hi Swaleh Kitabu, Mabaahithi fii uluumil Qur'an ukurasa wa 23.

⁷³ Al-mad-khal lidiraasatil Qur'an al-kariimu kurasa wa 73, mtunzi Abuu shuhbat. Na Siiratul Nabawiyat,juzuu ya 1/267.

"Na hivyo hivyo tumekushushia ufunuo kwako kwa kupitia Malaika Jibrili ulikuwa hufahamu ni kipi kitabu wala imani isipokuwa tumeijalia Qur'ani kuwa ni nuru tunamuongoza kwayo tumtakaye katika waja wetu hakika wewe unaongoza kwenye njia iliyo nyooka". [Ash shura: 52]. Na katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani baada ya kufikia Mtume umri wa miaka Arobaini ulimteremkia Wahyi kwa mara ya kwanza akiwa katika pango la mlima wa Hiraa, katika mlima uitwao Jabal Nuur katika mji wa Makkah tukufu, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۚ فَمَن شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۖ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِيُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِيُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْكُم وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾ [البقرة: 185]

"Mwezi mtukufu wa Ramadhani ambao umeshuka ndani yake Qur'ani hali ya kuwa ni muongozo wa watu na yenye kutenganisha kati ya haki na batili, basi yeyote atakaye kuwepo wakati wa mwezi huo basi na afunge mwezi huo" [Al Baqara: 185]. Na amesema Allah Mtukufu:

﴿إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ﴾ [القدر: 1]

"Sisi Tumeiteremsha Qur'ani katika usiku wa cheo na utukufu", nao ni moja wa masiku ya mwezi wa Ramadhani. [Suratil Qadri :1.] Na amesema Allah Mtukufu:

﴿إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ مُبْرَكَةٍ ۚ إِنَّا كُنَّا مُنذِرِينَ﴾ [الذخار: 3]

"Sisi tuliiteremsha katika Usiku wa Cheo uliobarikiwa wenye kheri nyingi, nao unapatikana katika mwezi wa Ramadhani. Sisi ni wenye kuonya watu kwa kile kinachowanufaisha na kuwadhuru, nako ni kule kupeleka Mitume na kuteremsha Vitabu, ili hoja ya

ALLAH iwasi mamie waja Wake." Surat Dukhaan:6. Katika usiku huo wenye baraka ulikuja wahyi kwa Bwana Mtume-Sala na amani ziwe juuyake- katika hadithi yake mashuhuri ambayo ameipokea Imamu Bukhari kutoka kwa Ur-wa Bin Zubair kutoka kwa Shangazi yake Aisha Mama wa waumini-Radhi za ALLAH ziwe juu yake-kuwa yeye alisema: "Jambo la kwanza ambalo alianzishiwa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- katika kuteremshiwa Wahyi ni Ndoto nzuri akiwa usingizini, na alikuwa haoti ndoto isipokuwa ndoto ile humjia kama ilivyo panapo pambazuka asubuhi, kisha akapendezeshewa kujitenga, na akawa anajitenga kwenye pango la Hiraa akiabudu kwa masiku mengi ya kwenda kwa watu wake na akichukua akiba ya chakula kwa ajili ya ibada, kisha alikuwa akirudi kwa Khadija na akichukua akiba kama hiyo mpaka ikamjia haki naye bado yupo kwenye pango la Hiraa, basi akamjia Malaika, akamwambia: "Soma" akasema mimi siyo msomaji, akasema akanishika na akanikaba kwa nguvu mpaka nikaishiwa nguvu kisha akaniwachia kisha akasema: "Soma", nikasema mimi siyo msomaji basi akanikaba tena mara ya pili kwa nguvu mpaka nikaishiwa nguvu kisha akaniwachia na akasema: "Soma" nikamjibu kuwa mimi siyo msomaji, akanishika kwa mara ya tatu akanikaba kwa nguvu kisha akaniachia na akasema soma:

﴿أَقْرَأْ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ﴾ [العلق: 1]

"Soma, kwa Jina la Mola wako Aliyeumba". (Suratul Alaq: 1)⁷⁴

Basi akarudi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kwa Khadija akitetemeka mwili wake na akaingia kwa Khadija Bint Khuwailid-

⁷⁴ Kitabul Bad'al wahyi, Swahili Bukhariy hadithi 3; juzuu ya 1/3 na angalia Sherhi ya Bin Hajar katika Fat-hul Baar, na angalia Bin Kathiir katika Tafsiir yake juzuu ya 2/2010.

Radhi za ALLAH ziwe juu yake- akasema; Nifunikeni Nifunikeni, Basi wakamfunika mpaka uoga ukaondoka, akamsimulia Khadija aliyoyaona na kuyasikia na akamsimulia na kusema: kwa hakika nimeogopa katika nafsi yangu" Akasema Khadija: Si hivyo namuapia ALLAH (Hakuwa ALLAH ni mwenye kukufedhehesha hata kidogo, kwa hakika wewe unaunga udugu,na unamkirimu mgeni na unawasaidia wasio jiweza, na huleta visivyokuwepo, na unatoa msaada wakati wa matatizo, Basi akaondoka na Khadija mpaka wakafika ka Waraqatu Bin Naufal Bin Asad Bin Abdil Izzi mtoto wa baba yake mdogo Khadija na alikuwa ni mtu aliyeingia kwenye unaswara katika zama kabla ya uislamu, na alikuwa akiandika lugha ya Kiebrania na akiandika Injili kwa Lugha ya Kiebrania kiasi alichojaaliwa na Mwenyezi Mungu kuandika, na alikuwa ni mzee sana na nikipofu, basi khadija akamwambia; Ewe mtoto wa Baba mdogo msikilize mtoto wa ndugu yako, Waraqa akamwambia mtume: Ewe mtoto wa ndugu yangu umeona nini? Mtume -Sala na amani ziwe juu yake akampa habari ya alichokiona akamwambia waraqatu: kuwa huyo uliyemuona ni Naamuus alimteremsha ALLAH kwa Mussa natamani wakati huo ningekuwa kijana, pindi watakapokutoa watu wako, akasema Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- hivi wao watakuwa ni wenyekunitoa? akasema waraqa ndiyo, Hakuwahi kuja mtu yeyote na jambo kama ulilokuja nalo isipokuwa alifanyiwa uadui, na kama masiku yako hayo yatanikuta nikiwa hai basi nitakunusuru kwa nguvu zote", na wala hakuishi Waraqatu akawa amefariki na Wahyi ukakatika.⁷⁵

Na imepokelewa kuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake amesema:

⁷⁵ Angalia: Maghaazi kitabu cha Bin Abii shaiba ukurasa wa 103.

"Siku moja wakati mimi ninatembea nilisikia sauti kutoka mbinguni nikainua macho yangu, ghafla nikamuona Malaika amenijia kwenye pango, akiwa amekaa juu ya kiti kati ya mbingu na ardh, nikamuogopa na nikarudi nikusema nifunikeni nifunukeni basi wakanifunika, akateremsha Allah Mtukufu kauli yake: "Ewe uliojifunika Nguo!" Surat Mudathir: 1⁷⁶

Na kwa hakika Aya za mwanzo kuteremka kwa Bwana Mtume - Sala na amani ziwe juu yake- na aya zote vilevile ni Rehema toka kwa ALLAH Mtukufu zinafungua ujuzi wa ALLAH kwa wanadamu na aina zingine za elimu (kwa hakika aya hizo zinahusu kusoma, aliposema: 'Soma') na ni kusoma kwa aina gani? kwa jina la Mola wako na ninani Mola wako?, kwa hakika yeye ni muumba wako na viumbe wengine alipokea Wahyi wa ALLAH kwa amri ya ALLAH, na wala siyo kutoka kwake Mtume, na kwa hakika huo ulikuwa ni wahyi ambao uliteremshwa kwa mitume waliokuwapo kabla yake, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالْتَمِيزِ بْنِ مِنْ بَعْدِهِ وَأَوْحَيْنَا إِلَى إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَعِيسَى وَأَيُّوبَ وَيُونُسَ وَهَارُونَ وَسُلَيْمَانَ وَآتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا﴾
[النساء: 163]

"Hakika sisi tumekuletea wahyi, ewe Mtume, ili ufikishe ujumbe kama tulivyomletea wahyi Nūḥ na Manabii wengine baada yake. Na tumewapelekea wahyi Ibrāhīm, Ismā'īl, Is-ḥāq, Ya'qūb na Kizazi chake, nao ni Manabii waliokuwa katika makabila kumi na mbili ya wana wa Isrāīl wanaotokana na kizazi cha Ya'qūb, na pia

⁷⁶ Tafsiri Ibnu Kathiir, juzuu 1/uk1934

‘Īsā, Ayyūb, Yūnus, Hārūn na Sulaimān na tukampa Dāwūd Zaburi, nacho ni kitabu na kurasa zilizoandikwa". [An Nisaa: 163]. Na kwa hakika ilifuatana Qur'an baada ya hapo, na Wahyi ukawa wazi na aina zake na hali zake, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا أَلَكِ الْكِتَابَ وَلَا إِلَىٰ يَمَنُ وَلَا يَمِينُ
 جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدَىٰ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٥٢﴾﴾ [الشورى:

[52

"Na kama vile tulivyowapelekea wahyi Manabii kabla yako wewe, ewe Nabii, tulikuletea wewe wahyi wa Qur'ani itokayo kwetu, hukuwa unajua kabla yake ni vitabu vipi vilivyotangulia wala nini Imani wala zipi Sheria zinazotokana na ALLAH, Lakini tumeifanya Qur'ani ni mwangaza kwa watu ambao kwao tunawaongoza waja wetu tunaowataka kwenye njia iliyolingana sawa. Na hakika wewe, ewe Mtume, unaelekeza na kuongoza kwa amri ya ALLAH kwenye njia iliyolingana sawa, nayo ni Uislamu" [Ash shura: 52]. Na anasema ALLAH Mtukufu:

﴿قُلْ لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُمْ عَلَيْهِمْ وَلَا آذَنْتُكُمْ بِهِ ۗ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ
 أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦﴾﴾ [يونس: 16]

"Sema ewe MUHAMMAD laiti angependa ALLAH nisinge kusomeeni na wala nisingewajulisha kunako Qur'ani hakika nimeishi nanyi muda mwingi kabla ya hiyo Qur'ani hivi hamna akili." Surat Yunus 16, Na anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَمَا كُنْتَ تَتْلُوا مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُ بِيَمِينِكَ إِذًا لَّآزِتَابَ الْمُبْتَلُونَ ﴿٤٨﴾﴾ [العنكبوت: 48]

"Na miongoni mwa miujiza yako iliyo wazi, ewe Mtume, ni kuwa wewe huku soma kitabu wala hukuandika herufi zozote kwa mkono wako wa kulia kabla ya hii Qur'ani kukuteremkia, na hali

wao wanalijua hilo. Na lau ungalikuwa ni mwenye kusoma au kuandika kabla hujaletewa wahyi wangalilifanyia shaka hilo hao wapotofu na wangelisema, «Amejifunza hiyo (Qur’ani) au ameinakili kutoka kwenye vitabu vilivyotangulia.» Surat An-Qabuut: 48. Na anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٩١﴾ وَإِنَّهُ لَنَزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٩٢﴾ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٩٣﴾

عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٩٤﴾ [الشعراء: 191-194]

"Na kwa hakika Mola wako Ndiye Mshindi, Mwenye kuteza nguvu, Mwenye kuwatesa maadui Wake, Mwenye huruma kwa walioamini miongoni mwa viumbe Wake." "Na kwa hakika, hii Qur’ani ambayo ndani yake zimetajwa habari hizi za kweli imeteremshwa na Muumba viumbe na Mmiliki wa mambo yote". "ameshuka nayo Jibrili muaminifu." "akakusomea mpaka ukaikusanya moyoni mwako, kwa kuihifadhi na kuielewa, upate kuwa ni mmoja wa wajumbe wa ALLAH wenye kuwafanya watu wao waogope mateso ya ALLAH, upate kuwaonya, kwa Teremsho hili, binadamu na majini wote." Surat Shuaraai: 191:194 Na anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِنَّكَ لَلْقَائِي الْقُرْآنَ مِنَ لَدُنْ حَكِيمٍ عَلِيمٍ ﴿٦﴾﴾ [النمل: 6]

"Na kwa hakika wewe, ewe Mtume, unapewa Qur’ani kutoka kwa ALLAH, Mwingi wa hekima katika kuumba Kwake na upelekeshaji Wake Ambaye Amekizunguka kila kitu kwa kukijua." [An Nahli: 6]. Na anasema ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿١٩﴾ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٢٠﴾ مُطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ ﴿٢١﴾ وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُونٍ ﴿٢٢﴾ وَقَدْ رَآهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ ﴿٢٣﴾ وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَنِينٍ ﴿٢٤﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَجِيمٍ ﴿٢٥﴾ فَأَيْنَ تَذَهُبُونَ ﴿٢٦﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٢٧﴾﴾ [التكوير: 19-27]

"Hakika Qur'ani hii ni kauli ya mjumbe mkarim (jibriel)" (19) Mwenye nguvu anakuwa kwenye Arshi tukufu. (20) Mwenye kuheshimiwa kisha muaminifu. (21) Na hakuwa jamaa yenu (MUHAMMAD) ni mwenda wazimu. (22) Na hakika MUHAMMAD alimuona kwenye mawingu akiwa amedhihirika (23) Wala yeye hafanyi ubakhili katika kufikisha Wahyi. (24) Na haikuwa Qur'ani ni maneno shetani aliye laanika. (25) Basi mnakwenda wapi? (26) Haikuwa hii Qur'ani isipokuwa ni ukumbusho kwa viumbe. (27) [Surat Tak-wiir: 19-27]. Na anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَمَا تَنزَّلَتْ بِهِ الشَّيَاطِينُ ﴿٢٦﴾ وَمَا يَتَّبِعِي لَهُمْ وَمَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٢٧﴾ إِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ لَمَعَزُونَ ﴿٢٨﴾﴾ [الشعراء: 210-212]

Na Qur'ani haijateremshwa na mashetani. (210) Na hilo halifai kutoka kwao na wala hawaliwezi, (211) Na hakika wao ni wenye kuzuiliwa kuisikiliza Qur'ani hakika ni wenye kupigwa na vimondo. (212) [Surat Shuaraai: 210-212] Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾﴾ [النجم: 3-4]

"Na wala haongei kwa matamania ya nafsi yake (3) Haikuwa Qur'ani isipokuwa ni ufunuo alio funuliwa. (4) [Surat Najm: 3-4] Ilikuwa Shauku ya Bwana Mtume ni kwa ajili ya Qur'ani na kwa ajili ya kujifunza na kuihifadhi ni shauku ya hali ya juu pale mwanzo wa kuteremka wahyi, na katika maisha yake yote alikuwa na shauku Likateremka neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿١٦﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ﴿١٧﴾ فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ﴿١٨﴾﴾ [القيامة: 16-18]

"Usitikise ulimi wako kwa kuiharakia Qur'ani. (16) Hakika kwetu sisi ndio tunaikusanya na kukusomea. (17) Basi tunapokusomea basi fuata kusomwa kwake. (18) kisha ni wajibu juu yetu

kukubainishia (19) [Suratil Qiyamah: 16-19] Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿فَتَعَلَى اللَّهِ الْمَلِكُ الْحَقُّ وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ وَقُل رَّبِّ
زِدْنِي عِلْمًا﴾ [طه: 114]

"Ametukuka ALLAH mfalme wa kweli, na wala usiiharakie Qur'ani kabla hakuja maliziwa kufunuliwa juu yako, na sema MOLA wangu nizidishie maarifa". [Twaha: 114].

KUANZA KWAKE KUFIKISHA UJUMBE.

Wakati wa kuteremka suratil Mudathir ilikuwa jambo la kulingania Mtume kwa ALLAH lipo wazi na kuwaonya viumbe ambao mtume ametumwa kwao.

﴿يَأَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنْذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمْنُنْ
تَسْتَكْبِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾﴾ [المنثر: 7-1]

"Ewe uliojifinika nguo! (1) Simama na uonye (2) Na Mola wako umtukuze (3) "Na nguo zako uzisafishe" (4) "Na Masanamu uyahame".(5) Na usitamani kwa kutaka wingi. (6) Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira (7) [Suratul Mudathir: 1-7] Kwa hakika huo ni ujumbe na Ulinganiaji, na ujumbe unamtaka kutoa juhudi na kutenda na kuonya na kusubiri na kujitwahaisha kwa hakika hilo ni onyo kwa viumbe la kuwaongozea kwa Mwenyezi Mungu na kumpwekesha yeye, na kujiepusha na Ushirikina na kujiandaa kwa hilo kwa kujitakasa na kujisafisha na kujiweka mbali na ushirikina na kuwapendelea watu kheri, hakika kufanya hivyo ni kusimamia mambo ya ALLAH, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿قُمْ فَأَنْذِرْ﴾ [المنثر: 2]

"Inuka kutoka kwenye malazi yako owaonye watu adhabu ya ALLAH." [Suratul Mudathir: 2] Kwa hakika hiyo ni amri ya ALLAH kwa Mtume wake, kumtukuza pamoja na kumuabudu.

Na Khadija Mama wa Waumini ndiye wa kwanza aliyeingia katika uislamu na kumuamini Mtume -Sala na amani ziwe juu yake⁷⁷ hakuna aliyemtangulia kwenye hilo si mwanaume wala mwanamke kama vile yeye kahdija -Radhi za ALLAH ziwe juu yake-ndiye wa kwanza kuswali na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-⁷⁸

Kama walivyofanya haraka kuingia kwenye uislamu mabinti wa Bwana Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kwa hivyo wao walisilimu moja kwa moja pamoja na mama yao Khadija, na hasa wakubwa wao, wakimfuata mama yao na kumsadikisha baba yao, na huenda mama anamchango katika kusilimu kwao -Radhi za Allah ziwe juu yake-K wa hakika waliashiria baadhi ya maulamaa yakuwa Mtume (Mwenyezi Mungu alipomkirimu Mtume wake unabii, Khadija na Mabinti zake walisilimu)

Kama alivyokuwa katika nyumba ya Mtume Ally Bin Abii Twaalib-Radhi za allah ziwe juu yake- ambaye alikuwa katika malezi ya Mtume Rehema na amani ziwe juu yake- kwa kumpunguzia mzazi wake uzito wa utoaji wa Matumizi, basi ALLAH akamkirimu kwa hilo na alikuwa Ally ni miongoni mwa waliokubali moja kwa moja Da'awa

⁷⁷ Kitabu kiitwacho Siirat Nabawiyyat cha Bin Hishaam juzuu ya 1/240; Siirat Nabawiyyat Bin Kathiir juzuu ya 1/426.

⁷⁸ Kitabu kiitwacho Siirat Nabawiyyat cha Bin Hishaam juzuu ya 1/244; Siirat Nabawiyyat cha As-swalaabiy juzuu ya 1/126.

ya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na wala umri wake haukuwa umefikia miaka kumi.⁷⁹

Na kubakia kwa Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake- katika nyumba ya Mtume alipata maisha bora pamoja na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kabla ya kupewa kwake utume na akaweza kuona mambo ambayo hajawahi kuyaona mambo hayo yeyote, na kuna mtu mwingine alipata ubora wa kuamiliiana pamoja na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- naye ni kijakazi wake ambaye ni Zaid Bin Haarith -Radhi za Allah ziwe juu yake.⁸⁰ ambaye kubakia kwake pamoja na Mtume kulimuathiri kwa kutorudi kwa jamaa zake na akawaambia jamaa zake: kwa hakika nimeshuhudia toka kwake mambo ambayo yanarifanya mimi nisimuache, hapo ni pale walipotaka kumlipia gharama yake na waende naye, na alikuwa ni kijakazi wa bwana Mtume Sala na amani ziwe juu yake, na akajitahidi Mtume Sala na amani ziwe juu yake- kumuacha huru na akamuita kwa Ubini wa jina lake, alikuwa kila anayeishi katika nyumba ya Mtume wa ALLAH ni Mwenye kumuamini mtume, kuanzia Mke, Mabinti, na mtoto wa baba mdogo, na kijakazi, na walikuwa wakiunga safu nyuma ya imamu wao Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- wakisali wakimsadikisha na kumuamini,⁸¹ na hii ni katika Sala za ALLAH kwa Mtume wake na mwenye kumsadikisha

⁷⁹ Angalia: Maghaazi kitabu cha Bin Abii Shaibah ukurasa wa 130; na Siirat, juzuu ya 1/284; cha Muhammad Abuu Shaibah kitiwacho Siirat juzuu ya 1/137.

⁸⁰ Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 137.

⁸¹ Angalia Hadithi katika sahihi Bukhariy katika fadhila za maswahaba, namba 3661; na Bin Kathiir, Siirat An-nabawiyat juzuu ya 1/437.

yeye ,pale ambapo walimuamini wote waliopo kwenye nyumba yake.

Na wa kwanza aliyesilimu na akamuamini Mtume -Sala na amani ziwe juu yake kwa wanaume ni Abuu bakar Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- (190) naye ni swahaba wa bwana Mtume wa ALLAH tangu mwanzo walifunganishwa na mahusiano maalumu, kila mmoja wao alijua ukweli wa mwenzake na akamjaribu na kujua uaminifu wake⁸² na alikuwa ni mtu aliyebanikiwa alianza kuwa mlinganiaji tokea kusilimu kwake akilingania kwa ajili ya uislamu na kwa ajili ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, na alikuwa akiwachagua watu wakweli wenye akili ili awalinganie katika kumuamini Mtume wa ALLAH, na kwa hakika walisilimu kwenye mkono wa Abuubakar - Radhi za Allah ziwe juu yake-wengi katika waliobashiriwa pepo, na miongoni mwao ni Othman Bin Affan, na Zubeir Bin Awwam ,na Abdurahman Bin Aufiy, na Saad Bin Abii Waqqaas, na Miqdaad Bin As-wad na Twalha Bin Ubaidillah, na Ubuu ubaidah Bin Jarraah ,na Saidi Bin Zaid Bin Amrou Bin Nufail -Radhi za Allah ziwe juu yao wote-⁸³⁸⁴

Na kwa hakika uislamu ulianza kuenea kwa siri kwa Makuraishi, na idadi ya waislamu ikazidi, na walikuwa baadhi ya waislamu hawaujui uislamu wa wenzao na kila aliyesilimu alikuwa ikifanya kazi kama Da'ai (Mfikisha ujumbe) kwa ajili ya Mwenyezi Mugnu na

⁸² Angalia Maghaazi kitabu cha Bin Abii shaiba ukurasa wa 103.

⁸³ Angalia kitabu cha Fadhaail Swahaba kwa Bukhariy katika sahihi yake, mlango wa Manaacaqib Abubakar,juzuu ya 5/192.

⁸⁴ Al-maghaaz cha Bin Abii Shaibah ukurasa 125-138 Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/250.

Mtume wake na akiutangaza uislamu kwa anayemuamini katika wanao ishi pembeni yake.⁸⁵

Walikuwa waislamu wa mwanzoni ni katika watukufu wa Makkah na miongoni mwao walikuwepo wanyonge mfano Bilal Bin Rabaah, na Ammar Bin Yaasir na Khabbab Bin Al-Arat na Abdullahi Bin Masoud, na walikuwa waislamu wengi ni vijana.

Kama ilivyokuwa kati yao kuna idadi ya wanawake, miongoni mwao ni As-maa Bint Abuubakar As-swidiq ,na Fatma Bintul khattwab, na Fatma Bintul muhallal, na Fikiihat Bintu Yasaar, na Ramlatu Bintu Aufii, na Amina Bint Khalaf Mke wa Khalid Bin Said Bin Al-aass, Sumaiyyat Mama yake Yaasir -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote-na wengineo,⁸⁶na hapo ziligeuka nyumba na familia kuwa za kiislamu katikati ya jamii kubwa ya Makkah.

Walikuwa waislamu wa mwanzo wakishirikiana kuisoma Qur'ani na kuswali kwa kujificha kwenye makorongo na mapango na majumbani⁸⁷na kwa hakika walijua kupitia kuisoma Qur'ani na kuisikiliza kutoka kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-walijua kuwa wafuasi wa manabii wanapatwa na maudhi na hata kuuwawa.

Alikuwa Bwana Mtume akiwalea maswahaba wake katika Tauhiid na kuifanya ibada kwa ajili ya ALLAH, na kuvumilia matatizo ya

⁸⁵ kitabu kitiwacho Min Muiin Siirat cha Swalih Shaam juzuu ya 1/198.

⁸⁶ Al- siirat Nabawyyat, juzuu ya 1/256; angalia kitabu kitiwacho Sahihi Siirat cha Ibrahiim Al-Aliiyukurasa wa 54 na kitabu kitiwacho muiinu siirat cha swalehe Al-Shaamiyukurasa wa 38.

⁸⁷ Al-siirat Nabawiyat cha Bin Hishaam, juzuu ya 1/246, 263.

kibinadamu na kuyafungamanisha na muumba na kuyaepusha na kumshirikisha Mungu⁸⁸na kumuitikia ALLAH kikamilifu na kuzitakasa nyoyo, na kuwapendelea watu heri na kumuogopa ALLAH na kuwayapenda yaliyopo kwake, na kuitarajia nyumba ya Akhera na kufanya sababu na kutegemea kwa ALLAH.

Ilikuwa Nyumba ya Ar'qm bin Abi Arqam ndiyo sehemu ya kukutania waumini na Mtume wao -Sala na amani ziwe juu yake- na wengine kukutana na wengine, wakipata mafundisho kutoka kwa Mtume mwenye huruma moja kwa moja, wakawa hawa ndiyo chanzo cha umma wa kiislamu ulio mkubwa ambao ulipigwa katika kila pembe ya Ardhi mpaka leo hii, kwa hakika wao ni walinganiaji wa kweli walioboba majukumu kwa ajili ya watu wengine, Amesema, **ALLAH Mtukufu:**

﴿وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْعَدْوَةِ وَالْعَشيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الدُّنْيَا وَلَا تُطِيع مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَنْ ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا﴾ [الكهف: 28]

"Na uvumilie nafsi yako, ewe Mtume, pamoja na Masahaba wako miongoni mwa Waumini masikini wanaomuabudu Mola wao Peke Yake na kumuomba Yeye kucha na kutwa, wakiomba kupata radhi Zake, ukae pamoja nao na utangamane nao, na usiuepushe uso wako na wao kuwaangalia wasiokuwa wao miongoni mwa makafiri kwa kutaka kujistarehesha na pambo la uhai wa kilimwengu. Na usimtii yule tulioufanya moyo wake ughafilike kututaja na akafadhilisha kufuata matamania yake juu ya kumtii Mola Wake na mambo yake yakawa, katika matendo yake yote, yamepotea na kuangamia". [Al-Kahfu: 28] Baada ya kupita muda

⁸⁸ Al-siirat Al-nabawiyat cha Ally Al-swalaab juzuu 1/144.

unaokaribia miaka mitatu tangia kuanza Daa'wa ya kiislamu na kuenea kwake kwenye koo za kikuraishi, na waislamu kuificha da'wa kwa kiwango kikubwa mpaka ikafikia hatua ya kutojuana wao kwa wao,⁸⁹ yakamteremkia Mtume juu yake amani maneno yake Mtukufu:

﴿وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٢١٤﴾ وَأَخْفِضْ جَنَاحَكَ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢١٥﴾﴾ [الشعراء:

[215-214

"Na watahadharishe, ewe Muhammad, watu wako wa karibu, ukianza na wale walio karibu nawe zaidi, isije adhabu yetu ikawashukia". (214) Na uwe laini wa mwenendo na maneno, kwa unyenyekevu na huruma, kwa yule ambaye imekufunukia kutoka kwake kuitika wito wako. (215) [Surat Shuaraai: 214-215]. Ikaja amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mtume wake Sala na amani ziwe juu yake- yakuwa adhihirishe ujumbe wake na kuwaonya watu wake katika maneno yake Mtukufu:

﴿فَأَصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٤﴾﴾ [الحجر: 94]

"Na utangaze waziwazi ulinganizi wa haki ambao Amekuamrisha nao ALLAH, wala usiwajali washirikina, kwani hakika Amekutakasa Mwenyezi Mungu kutokana na hayo wanayoyasema." [Surat Hijri: 94]⁹⁰

Na akatoka Mtume kuelekea haram nayo ni sehemu ya wazi, na akapanda juu ya mlima Swafaa akapanda juu ya jiwe na akaiona

⁸⁹ Angalia kitabu kiitwacho Al-siirat sahihi cha Akram Ndhwiyaaul Amriy juzuu ya 1/140

⁹⁰ Tafsiir Bin Kathiirjuzuu ya 1/1053

haram (Msikiti Mtukufu) ulipo, na akaanza kuita watu (Ewe asubuhi yangu -Kumekuchaa!) na hii namna ilikuwa ikifuatwa na waarabu kualika mkutano na kumsikiliza muongeeji katika jambo atakaloliona ni muhimu na la hatari, na akawa Mtume akiwaita makuraish: "Enyi watu wa kabila la Fihri, Enyi watu wa Abdi mananfi, enyi watu wa Abdul Muttwalib, Enyi watu fulani mpaka watu wakakusanyika akasema Mwaonaje ikiwa nitawapa habari kuwa Farasi anakuja kutoka kwenye maporomoko ya mlima huu vipi mtanisadikisha?wakasema: "Hatukuwahi kukusikia ukisema uongo" na kwa hakika ushuhuda huo ulikuwa ni wa wote kuhusu ukweli wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akasema Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- Basi mimi ni muonyaji wenu kunako adhabu kubwa, na alikuwa katika waliohudhuria ni Ami yake Abuu Lahab, naye akamjibu kwa ukali na ususuwavu na kiburi: "Umepata hasara wewe leo hii, je ndiyo kwa jambo hili umetukusanya"⁹¹⁹²

Kisha akateremka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kwa hakika alifikisha Amri ya Mola wake waziwazi mbele ya watu wa Makkah wote, na yalikuwa majibu ya Abuu lahab ambaye ni baba yake mdogo na ni katika watu wa karibu yake zaidi kuliko yeyote, alimjibu majibu makali yasiyo huruma na ni majibu mazito, na akateremsha ALLAH kwa Mtume wake -Sala na amani ziwe juu yake- na ndani yake kulikuwa na Aya zisomwazo mpaka siku ya kiama. Amesema ALLAH Mtukufu:

⁹¹ Imepokelewa kutoka katika riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, kitabu tafsiir, mlango unaohusu surat Tabbatiyadaa Abii lahabin Watabba, juzuu: 6/94.

⁹² Angalia Bin Saadn,Siirat An-nabawiyat kutoka katika kitabu, Attwabaqaatul Kubraa, juzuu ya 1/200 Ibrahiim Al-alii swahihu Siirat ukurasa wa 56.

﴿ تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ۚ مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ۚ سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ۚ

وَأُمْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ۚ فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ۚ ﴾ [المسد: 1-5]

"Imehasirika mikono miwili ya Abu Lahab, na yeye mwenyewe ameangamia, kwa kumuudhi Mtume, rehema ya ALLAH na amani zimshukie. Hasara ya Abu Lahab ilithubutu." (1) Hayakumfalia kitu mali yake na watoto wake. Kwani hivyo havitamkinga na adhabu ya ALLAH pindi ikimshukia. (2) Atauingia moto wenye miale (3) Na mke wake mwenye kubeba mizigo ya kuni (4) katika shingo yake amefungwa kamba zitokanazo na kamba za motoni. (5) [Suratul masad: 1-5] Na haukuwa msimamo wa Abii lahab ni wa kwake peke yake bali alikuwapo mke wake ambaye aliendelea kumuudhi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake⁹³

Kama ambavyo Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alisema katika kulingania kwa mara ya kwanza " Enyi kongamano la makuraishi, zikomboeni Nasfi zenu siwezi kuwatosheleza kwa chochote toka kwa Mwenyezi Mungu, Ewe Abbas Bin Abdil-Muttwalib siwezi kukutosheleza kwa chochote kutoka kwa ALLAH, na Ewe Sofia Shangazi wa Mtume siwezi kukutosheleza kwa chochote toka kwa ALLAH, na Ewe Fatuma Bint Muhammad niombe chochote utakacho katika mali zangu siwezi kukutosheleza kwa chochote tokwa ALLAH⁹⁴" yalikuwa maneno ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- yapo wazi kabisa na yenye nguvu nae analingania kwa ALLAH, na yeye ni muonyaji na wala hakitomfaa

⁹³ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad juzuu 1/200.

⁹⁴ Tafsiri Suurat Shuaraai katika Sahihi Bukhariy, mlango usemao, Na uwaonye ndugu zako wa karibu juzuu ya 6/16, na uangalie Takhriij toka kwa Ibrahim Al- aliiy, swahili Siiratu kurasa 56.

mtu chochote isipokuwa mafungamano na ALLAH na kutafuta Radhi zake, nakuwa ukaribu wake Mtume na wao hautowafaa peke yake na wala Mtume hana mamlaka yoyote kwa yule ambaye hatofuata Radhi za ALLAH kwa kumuamini na kumpwekesha na kusadikisha.

Washirikina walimuudhi bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na yaliyomkuta kutoka kwao [203].

Ulikuwa mwanzo wa maudhi ni kutoka kwa Abuu Lahab na mke wake, na wakawa watu wake na hasa wakubwa madhalimu ni wenye kushiriki katika kumuudhi Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na masahaba zake, na alikuwa kiongozi wao ni Amru Bin Hishaam (Abuu Jahal) kama alivyomuita Mtume baada ya kujikita na kuendelea na ukafiri na kupinga, na alikuwa akiitwa kabla ya uislamu Abal hakam Bin Hisham.⁹⁵.

Ama mpinzani wa kike katika wenye kumuudhi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake na miongoni mwa wanawake alikuwa ni mke wa Abuu Jahal, na alikuwa akiitwa Jamiila Bint Harbi⁹⁶

kwa hakika maudhi ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake yaliendelea baada ya kulingania kwa wazi wazi miaka kumi, na huongezewa miaka minane baada ya kuhama mpaka kufikia kuukomboa mji wa Makkah, walikuwa wakibeba bendera ya maudhi watu madhalimu, na ikidondoka bendera kwa baadhi yao wanaibeba wengine kama ilivyokuwa katika vita vya Badri, mpaka akatoa ALLAH idhini ya kuukomboa mji wa Makkah kuimaliza kabisa

⁹⁵ Angalia Bin HabibAl- munmiqū fiiAkh-baar Quraish ukurasa 340,366.

⁹⁶ Tafsiir Bin Kathiir juzuu: 2/2045.

nguvu yake, na alikuwa Jamilah mke wa Abu Jahal mwanzo wa kuanza ulinganiaji wa wazi wazi ndiye miongoni mwa wenye maudhi makubwa kwa Mtume wa ALLAH, na kwa hakika walimuudhi Mtume Abu Lahab na mke wake Ummu Jamiil maishani mwao mpaka wakaangamia wakiwa katika ukafiri.

Walikuwa Makuraishi na makafiri wenzao wakimuelekezea Mtume wa ALLAH kila aina ya maudhi na walikuwa wakilenga kumtoa katika uislamu yeye na wale wanaomfuata, kama vile ambavyo walikuwa wakiwazuia watu kumsikiliza Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake - baada ya kuenea kwa ulinganiaji wake na wakawa wakiweka mikutao na wakisuka mipango ya kuwazuia watu wasiisikilize dini hii, kama vile ambavyo walikuwa wakimuelekezea Mtume wa ALLAH maudhi ya kila aina ya kihisia na kimwili ikiwa ni katika kujaribu kwao kumzuia katika njia ya ALLAH.

Na pamoja na maudhi yaliyompata Mtume wa ALLAH kutoka kwa watu wake, kwa hakika alikuwa Baba yake mdogo Abu twaalib akimzuilia asipatwe na maudhi kadiri ya uwezo wake, na alikuwa bado yupo katika dini ya makuraishi wakimzingatia umuhimu wake, na hasa hasa mwanzo wa kuanza Da'wa kwa matarajio yao kuwa atakuwa ni msaidizi wao dhidi ya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kama ilivyokuwa hali ya Abu Lahab, lakini yeye baba yake mdogo alikuwa ni msaada mkubwa kwa bwana Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na alikuwa ni mwenye kumtetea⁹⁷ na yakampata Mtume kwa kiasi kikubwa maudhi licha ya kutetewa na baba yake mdogo.

⁹⁷ Siirat Nabbawiyat ya Bin Hishaam juzuu ya 1/265; siirat nabawiyat kutoka katika Attwabaqaatul kubraa juzuu ya 1/201; angalia kitabu kiitwacho Swahihu siirat chaTwaharouniy juzuu1/464

Na inateremka Qur'ani hali yakuwa ni ujumbe kwa bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuhusu hali ya hawa wakaidi wapinzani, ikikusanya yote waliyoyasema na kuanza kuwajibu majibu toka kwa mwenye hekima na mjuzi, basi akivuta mwanadamu hisia ya kisa na majibu ya ALLAH kwa hawa, atatambua kuwa hii Qur'ani ni yenye Hekima imeteremshwa kwa Mtume wake, imepangiliwa kwa mujibu wa matukio, Aya zake ni zenye kusomwa mpaka siku ya Kiama, na kwa hakika alikuwa Abuu Jahal na wengineo miongoni mwa madhalimu wa kikafiri na wakubwa wa Makkah, wenye viburi, wakiwausia watu kutosikiliza kitabu cha ALLAH, Hivyo akataremsha kwa Mtume wake, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا لِهَذَا الْقُرْآنِ وَالْغَوْا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَعْلَمُونَ﴾ [فصلت: 26]

[26]

"Na makafiri walisema wakiambiana wao kwa wao wakiusia baina yao, «Msiisikilize hii Qur'ani wala msiiandame wala msizifuate amri zake. Na ziinueni juu sauti zenu kwa kelele, kupiga mbinja na kumfanya Muhammad achanganyikiwe anaposoma Qur'ani, huenda mkamshinda akaacha kusoma na kwa hivyo tukapata ushindi juu yake.» [Surat Fuswilat: 26]. Kama ambavyo walikuwa wakiisikiliza Qur'ani wanafanya kiburi, basi likateremka neno lake Mtukufu:

﴿وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِيْ أَكْتِمِ مِمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ وَفِيْ آذَانِنَا وَقْرٌ وَمِنْ بَيْنِنَا وَبَيْنِكَ حِجَابٌ فَاعْمَلْ

إِنَّا عَمِلُونَ﴾ [فصلت: 5]

"Na wanasema hawa wenye kukataa na kumkanusha Nabii Muhammad, rehema ya ALLAH amani zimshukie, «Nyoyo zetu zina vifuniko vyenye kutuzuilia tusielewe unayotambia, na masikizi yetu yana uziwi hatusikii, na baina yetu sisi na wewe, ewe Muhammad, pana pazia inayotuzuia kuitika wito wako. Basi fanya

kulingana na dini yako , kama ambavyo sisi tunavyofanya kulingana na dini yetu.» [Surat Fuswilat: 5]. Na wakajaribu kumcheza shere Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- na wakamtia kasoro uwanadamu wake na anayoyafanya kama wafanyavyo watu wengine, na yakawa kwao majibu ya Qur'ani yapo wazi, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَقَالُوا مَالِ هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ لَوْلَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُونُ مَعَهُ نَذِيرًا﴾ [الفرقان: 7]

"Na walisema washirikina, «Ana nini huyu anayedai kwamba yeye ni Mtume wa ALLAH (wakimkusudia Muhammad, Sala ya ALLAH na amani zimshukie), anakula chakula kama sisi na anaenda sokoni kutafuta riziki? Basi si angalimtuma Malaika awe naye ashuhudilie ukweli wake" [Suratil Fur'qaan:: 7] Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ وَاحِدٌ فَاَسْتَفِيمُوا إِلَيْهِ وَاسْتَغْفِرُوهُ وَوَيْلٌ لِّلْمُشْرِكِينَ﴾ [فصلت: 6]

"Sema ewe MUHAMMAD si vinginevyo mimi ni mtu mfano wenu nina shushiwa ufunuo hakika shani ya jambo la Mungu wenu ni Mungu mmoja kuweni na msimamo kwake na mumtake msamaha na adhabu kali kwa wafanyao shirki". [surat Fuswilat: 6] Majibu kwa mwenye kupinga kuwa ALLAH ni mwenye kumfufua Mwanadamu, wakasema lau angekuwa ni malaika basi ikawajibu Qur'ani katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَلَوْ جَعَلْنَاهُ مَلَكًا لَّجَعَلْنَاهُ رَجُلًا وَلَلَبَسْنَا عَلَيْهِم مَّا يَلْبَسُونَ﴾ [الأنعام: 9]

"Na kama tungelifanya mjumbe kuwa ni malaika hakika tungelimfanya kuwa ni mwanamume na tungeliwavisha utata juu yao katika yale wanayoyatia shaka". [Suratil An-aam: 9] Na

wakamtaka baadhi yao awe pamoja naye Malaika, hivyo ikaja Kauli yake Mtukufu:

﴿ وَقَالُوا لَوْلَا أَنْزَلَ عَلَيْهِ مَلَكٌ وَلَوْ أَنْزَلْنَا مَلَكَ لَفُضِيَ الْأَمْرُ ثُمَّ لَا يُنظَرُونَ ﴾ [الأنعام: 8]

"Wakasema laiti angelishushiwa MUHAMMAD malaika na kama tungeliteremsha Malika hakika jambo lingepitishwa kisha wasingelipewa muhula". [Surat An-aam 8] Na hao Wakaidi Madhalimu walimtaka alete alama, na si kwa sababu ya kutafuta haki lakini ilikuwa ni ukaidi na kiburi, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿ وَقَالُوا لَوْلَا أَنْزَلَ عَلَيْهِ آيَاتٍ مِّن رَّبِّهِ قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴾ [العنكبوت: 50]

"Na wakasema bora angeliteremshiwa aya kutoka kwa MOLA wake sema ewe MUHAMMAD hakika si vinginevyo aya zinatoka kwa ALLAH na hakika mimi ni muonyaji niliye wazi". [Surat An-qabuut: 50] Kama alivyotuhumiwa Mtume kuwa yeye anajifunza Qur'ani kutoka kwa baadhi ya manaswara katika mji wa Makkah au kutoka kwa watoto wao⁹⁸Qur'ani ikawajibu katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ وَلَقَدْ نَعَلِمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِّسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجِبِي وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ ﴾ [النحل: 103]

"Na hakika tunatambua wanasema anaye mfundisha ni kiumbe, lugha wanayo ipinga ni lughu isiyo ya kiarabu na hii ni lugha ya kiarabu iliyo wazi". [Al-Nahli: 103], Na kwa hakika walijaribu kuwafarakanisha waislamu wote na wakawatuhumu wafuasi wa Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- yakuwa wao ni

⁹⁸ Tazama: Tafsiir Bin Kathir juzuu ya 1/1077

madhaifu na wakamtaka aachane nao ili wakaye naye, Basi Qur'ani ikamkataza kufanya hivyo na ikawaamrisha kuwa imara, na ikamuamrisha Mtume kuwa Subira pamoja nao, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ مَا عَلَيْكَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِمْ مِنْ شَيْءٍ فَتَطْرُدَهُمْ فَتَكُونَ مِنَ الظَّالِمِينَ﴾ [الأنعام: 52]

"Na wala usiwafukuze wale wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni wakitafuta radhi za ALLAH hesabu yao haipo juu yako kwa chochote na wala hesabu yako haipo juu yao kwa chochote basi utakapo wafukuza utakuwa miongoni mwa watu waovu". [Al-an'aam: 52], Na inateremka Qur'ani hali ya kuwa ujumbe katika kila tukio ikiwajibu:

Na wakamtuhumu Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuwa yeye alikuja na ngano (Hadithi) za watu wa kale, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَقَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ اكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمْلَىٰ عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٥﴾ قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٦﴾﴾ [الفرقان: 5-6]

"Na wakasema hiyo Qur'ani ni maneno ya kale yaliyo andikwa maneno hayo huandikwa asubuhi na jioni". (5) Sema ewe MUHAMMAD ameiteremsha Qur'ani hii yule ambaye anafahamu siri za mbinguni na aridhini hakika yeye ni mfuta madhambi mpole. (6) [Al-furqaan: 5-6] Na wakamtuhumu kuwa na uwendawazimu, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ ﴿٦﴾﴾ [الحجر: 6]

"Na wakasema ewe ambaye uliye shushiwa utajo hakika wewe ni mwenda wazimu". [Al-hijri: 6] Na wakamtuhumu kuwa yeye ni mchawi, Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضِعُّ طَائِفَةً مِنْهُمْ يُدَبِّحُ أَبْنَاءَهُمْ وَيَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ﴾ [القصص: 4]

"Wakastaajabu kujiwa na muonyaji miongoni mwao na wakasema makafiri huyu ni mchawi tena muongo". [Swaad: 4], Na wakamtaka mambo mengine mbali mbali, Amesema ALLAH Mtukufu

﴿أَوْ يُلقَىٰ إِلَيْهِ كَنْزٌ أَوْ تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا وَقَالَ الظَّالِمُونَ إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَّسْحُورًا﴾ [الفرقان: 8]

"Au ateremshiwe hazina ya mali au awe na bustani ale kupitia bustani hiyo, na wakasema waovu hamna mnaye mfuata isipokuwa ni mtu aliye rogwa". [Al-fur'qaan: 8] Kama vile ambavyo Qur'ani ilivyomtetea na ikamtetea kutokana na kumcheza shere Mtume hivyo ikamkumbusha kuhusu manabii waliokuwa kabla yake, Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَقَدْ أَسْتَهْزِئُ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ﴾ [الأنعام: 10]

"Na hakika walifanyiwa mizaha mitume kabla yako ikawathibitikia wale ambao walio fanya mizaha miongoni mwao yale waliyo kuwa wakiyafanyia mizaha". [Al-anaam: 10] Na ilikuwa Qur'ani tukufu ikimkumbusha Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-yakuwa Manabii waliokuwepo kabla yake walipata fungu lao la kuudhiwa na kucheza Shere na jamaa zao.

WA MWANZO KUPATA MISUKOSUKO NA MASHAHIDI.

Na hawakutosheka washirikina na kumuudhi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake bali walimimina hasira zao zote kali kwa maswahaba zake ikiwa ni katika kujaribu kuwarudisha kutoka katika uislamu na kuizua dini ya ALLAH na kuwatia adabu makuraishi na

hasa vijana, na kuwaogopesha kwa kile ambacho chaweza kuwafika kama watasilimu kama vile yalivyowafika waumini na Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na yakawa mateso ya kimwili kwa kila atakaye mfuata Mtume Sala na amani-ziwe juu yake- hali yakuwa ni malipo ya kuzuia kutoepukana na njia ya ALLAH na kuwaweka watu mbali na dini yao, lakini hili halikuwaathiri na mashujaa wao walikita nakuwa na msimamo na wakawa ni mfano kwa waislamu wakati wote wakiigwa kwenye Subira na kuvumilia na kufa mashahidi katika njia ya ALLAH na kuwa na subira katika dini yake, na mfano wa hawa mashujaa kwa wanaume na wanawake ni Sumaiya na Yaasir na watoto wake Ammar na Bilal Muhabeshi -Radhi za ALLAH ziwe juu yao-.

Kama ambavyo kulikuwapo na wengi katika vijakazi walipata mateso kutoka kwa watawala wao wa kikuraishi miongoni mwao ni Humamaat ambaye ni mama yake Bilal Bin Rabaah na Mama Anis, na Zaniirat, na kijakazi wa Kabila la Muammal na An-Nahdiyyat na Mwanaye na walikuwa ni wajakazi wawili wa mwanamke kutoka katika kabila la Banii Abdi Daari katika makuraishi⁹⁹kwa hakika wote hao walipatwa na maudhi na kujaribu kuwabadilisha na kuwatoa kwenye dini yao, na kwa hakika alikuwa Abuubakar swiddiq -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- anamchango mkubwa katika kuwaokoa kwa kuwanunua kutoka kwa jamaa zao na akawaacha huru katika njia ya ALLAH.¹⁰⁰

⁹⁹ Siirat An-Nabawiyat, kitabu cha Muhammad Abuu Shuhbat Juzuu ya 1/346.

¹⁰⁰ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/319.

Na alikuwa Saad Bin Abii Waqaas ni miongoni mwa waumini wa mwanzo waliomuamini Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na alikuwa na mama yake naye alikuwa akimfanyia wema kuliko watu wengine kabla ya uislamu, na aliposilimu wema wake ukazidi na wala haukupungua, na alipojua juwa amesilimu nayeye alikuwa ana mtii alitaka -kujua hukumu ya wema wake na kumkubalia jambo lake akataka amtoe kwenye uislamu na kumuweka kwenye Taharuki, akasema Ewe Saad: Utaiwacha dini hii laa sivyo sitakula wala kunywa mpaka nife" Saad akamwambia mama yake: "Ewe mama yangu usifanye hivyo kwa kuwa mimi siwezi kuiacha dini hii hata kidogo", Na alipoona uthubuti wake akaanza kusita kula na kunywa, basi akakaa usiku na mchana hajala hivyo akadhoofika akaendelea hivyo mpaka siku ya tatu hajala na akawa akimuonyesha hali ya kuchoka kwake huenda akawacha dini yake na alipo ona hilo akasema: "Ewe mama yangu- Nina Apa kwa jina la ALLAH lau kama ungekuwa na roho mia moja na zikawa zinatoka moja moja nisingeweza kuwacha dini yangukwa ajili ya jambo hili, ikiwa utataka kula na ikiwa hautaki basi usile",¹⁰¹na alikuwa akimkumbusha dini yake na kuwafanyia wema wazazi wawili, na yeye anajua kuwa din ihaiachwi kwa ajili ya hilo, na ikateremka kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهَنًا عَلَىٰ وَهْنٍ وَفَصَّلْهُ فِي عَامَيْنِ أَنِ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ﴿١٤﴾ وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۗ وَصَاحِبُهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾﴾ [لقمان: 14-15]

¹⁰¹ Angalia Siyar Aalami Nubalaa juzuu ya 1/109; Bin Kathiir katikaTafsiri yake juzuu ya 2/1426.

"Na tumempa wosia mwanadamu kufanyia wema wazazi wawili mama yeke ameibeba mimba yake shida juu ya shida na kumuachisha ziwa ni baada ya miaka miwili, nishukuru mimi [ALLAH] na wazazi wako, kwangu mimi ndio marejeo. (14) Na kama watakulazimisha unishirikishe mimi -ALLAH- kwa mambo usiyo kuwa na ujuzi nayo basi usiwakubalie na kuwa nao karibu duniani kwa wema na ufuate njia ya yule aliye kuwa karibu yangu kisha kwangu mimi ndio marejeo yenu kisha nitakuelezeni kwa yale mliyo kuwa mkiyafanya. (15) (Luqmaan: 14-15)¹⁰².

KUHAMA MARA YA KWANZA KWENDA HABASHI [ETHIOPIA].[212]

Maudhi yalizidi kwa Mtume na Maswahaba wake na akawa Mtume akiwaliwaza maswahaba wake na akiwaamrisha kufanya Subira na akawa akiwapigia mifano kwa wafuasi wa manabii waliopita na Qur'ani ilikuwa ikiteremka mfululizo kwa Mtume -Sala na Sala ziwe juu yake- ikisimulia visa vya umma zilizopita na namna ALLAH alivyowapa Nusra, na alikuwa akiwaliwaza na akiwafungulia mbele yao milango ya matumaini liyomipana katika wakati ambao alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akiwabashiria kuwa wao watashinda -na kwa hakika ALLAH- kutakasika na machafu ni kwake- ataieneza dini hii kila mahali, na lilikuwa lengo lao katika hatua hii ni kuihifadhi dini na kuipa kipaumbele kabla ya kila kitu, hata kama jambo hili litapelekea kuuwacha mji wao wa Makkah (kwa kuikimbiza dini yao kuitoa katika mji wenye fitna na kuipeleka katika mji wenye amani) (213) Na alikuwa Mtume anawajua wafalme waliokuwa wakiishi pambizoni mwa miji ya waarabu, na hali ya wafalme hao kidini na kisiasa na upeo wa uadilifu wao baina ya ufalme wao na nidhamu zao na heshima yao kwa watu na

¹⁰² Angalia: Bin Kathiir Tafsiri yake juzuu ya 2/1462.

kuheshimu haki za watu, na pamoja na kufungamana Mtume na Mwenyezi Mungu na kumkubali kwake na kuegemea kwake, hakika alikuwa akichukua sababu na kuamrisha kupitia sababu hizo, na hii ni sehemu ya dini ambayo alikuja nayo, na kwa hivyo alifikiria Mtume Rehema na amani ziwe juu yake- kukimbilia sehemu ambayo watajihifadhi waislamu, na apate nyumba ya kuhamia inayomlinda sawa iwe nyumba ya kuhamia kwa muda au ya kudumu kwa kusuhubiana na maswahaba zake bwana Mtume Rehema na amani ziwe juu yake-na kwa hakika Qur'ani ilikuwa ikiteremka kwa Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- ikimuashiria kuwa Ardhi ya Mwenyezi Mungu ni pana na ikimuashiria kuwa awe na subira, na hayo yako kwenye maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قُلْ يٰعِبَادِ اللّٰدِيْنَ ءَامِنُوْا اَتَّقُوْا رَبَّكُمْۙ لِلَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا فِيْ هٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ وَّاَرْضُ اللّٰهِ وَّاسِعَةٌۭ اِنَّمَا يُوَفّٰى الصّٰبِرُوْنَ اَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿١٠﴾﴾ [الزمر: 10]

"Sema ewe MUHAMMAD enyi waja wangu ambao mlio amini muogopeni MOLA wenu kwa wale wafanyao mema katika hii dunia watapata mema, na ardhi ya ALLAH ni pana hakika watalipwa wafanyao subira malipo yao bila ya kuhesabiwa". [Az-mar: 10]¹⁰³Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿يٰعِبَادِىُّ اللّٰدِيْنَ ءَامِنُوْا اِنْ اَرْضِىْ وَّاسِعَةٌۭ فَاِيْنِىْ فَاَعْبُدُوْنِ ﴿٥٦﴾﴾ [العنكبوت: 56]

"Enyi waja wangu ambao mlio amini hakika ardhi yangu ni pana basi kwangu mimi niabuduni". [Al-ankaboot: 56]¹⁰⁴Kama

¹⁰³ Angalia Bukhariy katika sahihi yake kitabu cha Vita mlango wa Hijra kwenda Habashi juzuu 4/244.

¹⁰⁴ Angalia Bin Kathiir Tafsiri yake juzuu ya 2/1616.

ilivyoashiriwa katika kuhama kwa kuchelewa¹⁰⁵katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّيْنَاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنْتُمْ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضَ اللَّهِ وَسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا فَأُولَئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٧﴾﴾
[النساء: 97]

"Hakika wale wanao fishwa na Malaika hali ya kuwa ni waovu walisema-Malaika kuwauliza- mlikuwa na mambo gani? wakasema tulikuwa tumetenzwa nguvu katika ardhi, wakasema -Malaika- hivi haikuwa ardhi ya ALLAH ni pana mkahamia huko? basi hao mafikio yao ni motoni na ni mafikio mabaya mno". [An- nisaa: 97].¹⁰⁶

Na kwa hakika aliashiria Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake- ukimbizi huu na kutoka huku kwa jambo ambalo analijua kutokana na hali za Umati uliotangulia, akasema Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake- kuwaambia maswahaba wake: "Laiti mngetoka kuelekea Ardhi ya Habasha, kwa hakika huko kuna mfalme ambaye kwake yeye hadhulumiwi yeyote, nayo ni Ardhi ya haki mpaka awape faraja Mwenyezi Mungu kutokana na haya mazito mnayoyapitia"¹⁰⁷

Na maelekezo haya yalikuwa ni ya waislamu wote wenye uwezo, kwa kuwaogopea kupatwa na fitina na walikuwa wa kwanza kutekeleza amri yake ni watu wa nyumbani kwake waliokuwa

¹⁰⁵ Angalia Bin Kathiir Tafsiri yake juzuu ya 2/1441.

¹⁰⁶ Tafsiri Ibnu Kathiir. juzuu 1/uk522.

¹⁰⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/30.

waislamu na akawa wa kwanza kuhama ni Bint yake Rukia na mume wake Othman Bin Affan -Radhi za Allah ziwe juu yake-¹⁰⁸ na wengineo katika waislamu, na wala hawakuwa wanyonge peke yao, bali wale wabora na waheshimiwa ndiyo waliotangulia, na wakatoka wakinyata kwa siri, nao walikuwa ni kundi lililokamilika, miongoni mwao walikuwepo Mafukara na matajiri na watoto wadogo na vijana, wanaume na wanawake na ilikuwa idadi yao ni wanaume kumi na nne na mwanamke mmoja, na kwa hakika walifika hawa wahamiaji katika mji wa Habasha na akawapokea mfalme wa Habeshi Najashi AS-humat na kuwapa kila aina ya ukarimu na akawasikiliza na akawapa hifadhi na kuwalinda na maudhi, na hakika Najashiy alisilimu -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- na Mtume alimswalia alipokufa.¹⁰⁹

Na alikuwa ni katika wasomi wa kikristo, na bila shaka alijadiliana na waislamu kuhusu kuja kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kuhusu ujumbe wake, na yakawa matokeo yake ni akuingia katika uislamu na akauamini na kuusadikisha. Na kwa hakika alifungamanisha imamu Bukhari mlango wa kuhama kwenda Habasha na kitabu cha vita kuwa ni mlango mwingine akauita Mlango wa kifo cha Najashi ametaja humo hadithi tano zote zinazojulisha juu ya kusilimu An-Najashi:

Na kuhamia kwa waislamu wa kwanza Habashi ilikuwa ni mwaka wa Tano tangu kupewa Mtume utume¹¹⁰ na kwa hakika ilipita miezi

¹⁰⁸ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad Twabakaat juzuu ya 1/204.

¹⁰⁹ Sahihi Bukhariy mlango wa Mauti ya Najaashi na angalia yaliyokuja katika suala la Najashi na kisha cha kusilimu kwake kwenye Maghazi cha Bin Abii Shaibah ukurasa wa 165.

¹¹⁰ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad kutoka katika Twabaqaat 1/206.

mingi, na mwisho wake zikaja habari ambazo siyo sahihi yakuwa Makuraish wamesilimu, wengi wao wakarudi Makkah (221)¹¹¹

KUHAMA KWA MARA YA PILI KWENDA HABASHI (ETHIOPIA):

Na walipogundua waislamu kuendelea kwa maKuraish kumfanyia uadui Mtume na kuwaudhi maswahaba zake, na kuwa hakuna ukweli kwa kilichosemwa katika habari za kusilimu Makuraish, pakawa na haja ya kutoka idadi nyingine ya waislamu ambao idadi yao ilizidi katika mji wa Makkah, na hasa waliposikia kuwa wenzao wa mwanzo waliohama wapo salama, basi akatoka Jaafar Bin Abii Twaalib Bin mtoto wa baba mdogo wa Mtume wa ALLAH katika idadi ya waislamu mpaka ikafika idadi yao watu themanini na tatu (83) na wanawake kumi na moja¹¹² na inasemekana ni zaidi ya hao.

Na kwa hakika walifika Habashi na wakapata usalama na wakapokelewa zaidi ya walivyopokelewa kwa mara ya kwanza na akawadhihirishia ukweli wake na akawahifadhi na kuwalinda, na walijaribu makuraishi kuwarudisha Makkah, na Najashi akajadiliana nao na akamsikiliza Jafar na waliokuwa pamoja naye, na akatoa azimio la kuwahifadhi na akakataa matakwa ya makuraishi.¹¹³

Na baada ya hapo ulifika wakati wa kusilimu Hamza baba mdogo wa Mtume kisha kusilimu Omar Bin Khatwab -(Radhi za allah ziwe

¹¹¹ Kitabu kitiwacho Siirat Nabawiyat cha Bin Saad kutoka katika Twabakatul kubra juzuu ya 1/364; Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 1/205.

¹¹² Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad JUZUU 1/206.

¹¹³ Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu 1/334-338, na maelezo ni yake, na angalia: Bin abii Sheibah Al-maghaazi ukurasa wa 165-169 Bin Kathiir Siirat Nabawiyat juzuu ya 2/24.

juu yake) ambaye alikuwa na pupa tangu asilimu juu ya kumnusuru Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na kuwadhi makuraish, na alikuwa ni mwenye utu wenye ushawishi, mwenye heshima ya kweli.

Na kusilimu kwa Omari kulikuwa ni ushindi na nguvu kwa waislamu, anasema Bin Masoud: "Tuliendelea kuwa na nguvu tangu aliposilimu Omari",¹¹⁴. Na anasema vilevile ((Na kwa hakika tulijikuta hatuwezi kusali mpaka aliposilimu Omar, basi aliposilimu tu alipambana nao mpaka wakatuacha tusali))¹¹⁵

VIKWAZO VYA KIDHALIMU: [226]

Na walikuwa makuraishi wakitekeleza aina tofauti tofauti za adhabu kali zenye kuumiza na kumuudhi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kwa kila mwenye kumuamini Mtume au mwenye kumuhami na pia wafuasi wake, na kwa hakika walijaribu kila aina ya maudhi na waliazimia makuraishi kumuua Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akafanya bidii baba yake mdogo kumhami Mtume, na wakashirikiana pamoja naye kabila la Banii Haashimu na kabila la bani Muttwalib.

Na yaonekana wazi kuwa hayo ni matokeo ya shinikizo na hofu juu ya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na iliwalazimu wenye kumuhami Mtume kujikusanya katika mapango ya banii Haashim¹¹⁶ na katika wakati huu walijikusanya viongozi wa washirikina katika mji wa Makkah, na ulikuwa ni mwaka wa kumi

¹¹⁴ Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake Fathul Baari, juzuu ya 14/186.

¹¹⁵ At-twabaqaat juzuu ya 3/370.

¹¹⁶ Kitabu kiitwacho Raudhul Aniif: cha mtunzi Al-sihiliy juzuu ya 2/127.

baada ya kupewa utume (228) na wakakubaliana kati yao kuwa waandikiane mkataba, wakikubaliana kuwawekea vikwazo banii hashim na banii Muttwalib na watakao shirikiana nao katika kumuhami Mtume, na mkataba ulikuwa ndani yake kuna makubaliano ya kuwa wasiowe kwao wala wao wasiwaozeshe wao, wala wasiwauzie wao wala wasinunue kwao, na wala wasiwakubalie kupatana hata kidogo mpaka wamsalimishe Mtume ili wamuuwe, na kwa hakika waliyaandika hayo katika waraka kisha wakautundika katikati ya Al-kaaba, katika kujaribu kupata uhalali wa kisheria na kulipa nguvu ya upitishaji kati ya Makuraishi na waliowekeana kiapo nao, na vikwazo hivi viliendelea kwa muda wa miaka mitatu (229) na njaa na kiu vikazidi na mahitajioa ya waislamu na ndugu wa damu na bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na pia wale wenye kumuhami.¹¹⁷

Na kwa hakika walilazimika walioko kizuizini waliowekewa vikwazo kula majani ya miti na ngozi kutokana na kuhitaji kuliko kukubwa, na adhabu hii ilikuwa kwa Banii Muttwalib na Haashim kulindana kuliko wapelekea wakawa pamoja na Mtume na waumini katika kuzuiliwa huku, na kuwekewa vikwazo isipokuwa Abuu Lahab¹¹⁸

Na wakati wakiwa kizuizini walikuwa baadhi ya watu katika makuraishi miongoni mwa wenye udugu na waliokizuizini inawapata

¹¹⁷ Angalia kiatbu kiitwacho Al-siirat Nabawiyat cha Ak-ram Al-umariy ukurasa wa 182.

¹¹⁸ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 2/351.

huruma hivyo wanasimama na kujitahidi kupenyeza chakula cha njia ya magendo wakati wa usiku kwa siri.¹¹⁹

Na baada ya miaka mitatu tangu kukaa kizuizini walilaumiana baadhi ya wenye busara katika kikuraishi, na wakakubaliana kundi miongoni mwao kuwa waweke wazi kufuta vikwazo, na kuwataka makuraishi kuuchana waraka, na kuacha kuwawekea vikwazo Banii Hashim na wafuasi wa Mtume wa ALLAH, na aliyekuwa kiongozi wa hawa waliokataa uwekaji wa vikwazo na miongoni mwa wenye kutaka ufutwe ni Hisham Bin Amrou Bin Rabiia, na alikuwa ni katika wakubwa, basi akaenda kwa wakubwa wa kikuraishi kwa upole akawataka msaada na kuwaonyesha ubaya wa vikwazo (akawa ametibua mori wao na uwanadamu wao ili waupinge waraka, na kutoka kwenye haya makubaliano ya kidhalimu, na walipokuwa watano walikusanyika na wakakubaliana kuupinga waraka huu¹²⁰ na akasimama Zuhairi Bin Umaiyyat na mama yake Aitwaye Aatiqat Bint Abdul Muttwalib katika jangwa la makuraishi na akasema: "Enyi watu wa Makkah hivi tunakula chakula na tunavaa nguo na kabila la Banii Hashim wanaangamia hawauziwi wala kununuliwa toka kwao, namuapa Mwenyezi Mungu sitoki hapa mpaka uchanwe waraka huu wa kidhalimu"¹²¹

Na akajaribu Abuu Jahli kupambana kuzuia waraka usitenguliwe lakini wenye fikra nzuri walimshinda katika mazungumzo basi

¹¹⁹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/354.

¹²⁰ Kitabu cha Historia cha Abul hassan An- nadawiy ukurasa wa 139.

¹²¹ Angalia anuaniya kitabu Al-raudwul Muniif juzuu ya 2/127na Bin Saad Al-siirat Al-nabawiyat kutoka kwenye Twabaqaat juzuu 1/21.

akasema Abuu Jahal maneno yake mashuhuri: "Kwa hakika hilo jambo limepangwa usiku"¹²²

Na akarudi Mtume na waliokuwa pamoja naye kwenye maisha yao ya kawaida katikati ya jamii ya Makkah, na wakachangamkia Biashara ya kuuza na kununua na wakatajirika kwa kazi hiyo baada yakuwa walikuwa ni wenye kuzuiliwa kufanya hivyo, na wakafanyiwa mpango kabambe wa kuwaondoa kiuchumi na kijamii na kihisia kwa watu wa Makkah¹²³

KUFARIKI KWA KHADIJA -RADHI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE:- [236]

Alikuwa mama wa waumini Khadijah -Radhi za Allah ziwe juu yake - ni mke mwenye Neema na mwema na mwenye kumliwaza na kumsaidia Mtume -Sala na amani ziwe juuyake alimliwaza kwa mali yake na akamsaidia yeye mwenyewe, ni wa mwanzo aliyemwamini Mtume na kumkubali, ndiyo mke bora kwa mbora wa viumbe Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- Mtume alimsifu na akasema katika hadithi ambayo ameipokea Ally Bin Abii Twaalib -Radhi za Allah ziwe juu yake-: "wanawake walio bora ni Maryam bint Imraan na Bora ya wanawake ni Khadija Bint Khuwailid"

Alikuwa ni mke wake pekee mpaka alipofariki, na ni mama wa watoto wake na mabint zake, na ni mwanamke aliyekuwa na tabia njema na mweye kupendwa zaidi kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alimkinga sana na maudhi yeye mwenyewe na kwa maelekezo ya mabinti zake -Radhi za Allah ziwejuu yake- kama ambavyo walishiriki ndugu za Khadija kumkinga Mtume -Sala na

¹²² Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 1/374 na Siirat Nabawiyat, juzuu 2/45.

¹²³ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad Juzuu1/209.

amani ziwe juu yake- kwa kumridhisha khadija, kwa namna wanavyo mfahamu Mtume kwa khadija alivyo mkweli na uzuri wa muamala wake.¹²⁴

Na katika mwaka wa kumi tangu kupewa utume (239) alifariki dunia mama wa waumini Khadija Bint Khuwailid -Radhi za Allah ziwe juu yake - na alikuwa -Rehema na mani ziwe juu yake amemridhia na anampenda na akambashiria pepo katika sehemu zaidi ya moja na kwa hakika ilkuwa kufa kwake ni katika mwaka ambao alikufa baba yake mdogo Abuu Twaalib, na alikuwa mtetezi mzuri wa Bwana Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake na kwa hivyo ukaitwa mwaka huu ni mwaka wa huzuni.

KUFA KWA ABUU TWAALIBU:

Kabla kidogo ya kufa Abdul Muttwalib aliugua na akazidiwa katika mwaka wa kumi tangu kupewa utume (241) na alikuwa Mtume akimuonea huruma na akamlingania kuingia katika uislamu na kwenye kheri, tangu pale alipopewa utume, lakini hakuamini na kutangaza uislamu wake, na katika wakati huo huo hakuwacha kumsaidia Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na kumuwezesha na kuwa naye na kumlinda, amepokee Imamu Bukhariy ((Kuwa Abuu Twaalibu alipofikwa na maradhi Mtume aliingia kwake na mbele yake alikuwa Abuu Jahal, Mtume akasema: "Ewe Baba yangu mdogo sema laailaaha illa llahu neno ambalo nitakutetea nalo kwa ALLAH", Abuu Jahal akasema na Abdullahi Bin Umaiyat: "Ewe Abuu Twaalib, Hivi wataka kuiwacha Mila ya Mzee Abdul Muttwalib?" Na hawaja wacha kumsemesha mpaka mwishoni akasema neno la mwisho alilowaambia kuwa yuko katika mila ya Mzee Abdul Muttwalib,

¹²⁴ Angalia Kumuoja Mtume Khadija -Radhi za Allah ziwe juu yake- katika kitabu hiki.

akasema Mtume: "Nitakuomba madamu sijakatazwa", (242) likateremka neno lake ALLAH Mtukufu:

﴿ مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولَىٰ قُرْبَىٰ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴾ [التوبة: 113]

"Haitakikani kwa Nabii na wale walioamini wawaombe msamaha washirikina hata kama ni ndugu wa karibu baada ya kubainikiwa kuwa wao ni watu wa motoni". [Attauba: 113]. Na ikateremka kauli yake ALLH Mtukufu:

﴿ إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴾ [القصص: 56]

"Hakika wewe Muhammad humuongozi umpendaye isipokuwa ALLAH anamuongoza anaye mtaka na yeye ALLAH ndiye mjuzi wa walio ongoka". [Al-qaswas: 56]^{125, 126}

Na kwa hakika alikuwa akimpenda Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- baba yake mdogo hali ya kumuonea huruma anauona wema wake na anamshukuru kwa kuwa naye pamoja na anajua kuwa haiwezekani kuokoka na moto kwa namna yoyote isipokuwa kwa kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni ALLAH peke yake na alikuwa Mtume akipupia sana mzee Abuu Twaalibu ayaseme hayo, lakini kwa kuhudhuria Abu Jahal na mfano wake katika mashetani wakijini na kumsisitizia afe katika mila ya Abdul Mutwalib pale ambapo hawakuacha

¹²⁵ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad juzuu 1/211.

¹²⁶ Angalia sahihi Bukhariy kitabu cha manaaqib, mlango wa kisa cha Abii Twaalib juzuu ya 4/246.

kumsemesha mpaka mwisho akasema maneno yake ya mwisho kuwa yeye yupo katika mila ya mzee Abdul muttwalib.¹²⁷

Na akafa katika hali hiyo na akahuzunika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- huzuni kubwa, na kwa hakika waliona baadhi ya maulamaa kuwa Aya iliyokataza kutowaombea msamaha washirikina haikuwa maalumu kwa Abuu Twaalib, na pamoja na hayo katika aya hiyo kuna makatazo ya ujumla ya kuwaombea msamaha waliokufa hali yakuwa si waislamu na hata kama watakuwa ni watu wa karibu na Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake-** na jambo hili lipo wazi katika Aya.

Na kwa hakika alikuwa Abuu Twalibu ni mwenye kumsaidia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kwa kufa kwake ulipungua uwezeshwaji wa Mtume, na wakakosa nguvu waliokuwa wanamnusuru na likachanganyikana hilo na kufa kwa Bi Khadija hivyo ukaitwa mwaka huo ni mwaka wa huzuni.(245)

KISA CHA SAFARI YA USIKU NA KUPANDISHWA MBINGUNI (ISRAA NA MIIRAJI, MWAKA WA: 9 H)

Kwenda kwake masjidul Aq-swa (Palestina) na kupandishwa Mbinguni¹²⁸ni katika matukio muhimu na muujiza maalumu kwa ajili ya Mtume wetu -Sala na amani ziwe juu yake- na huenda kuitwa sura katika sura za Qur'an tukufu kwa jina la (Al-israa), na

¹²⁷ Inatoka katika hadithi ya Bukhariy mlango wa Kisa cha Abuu Twalib juzuu ya 4/247.

¹²⁸ Vimetungwa vitabu vingi na jumbe mbalimbali kuhusu tukio hilo zamani na sasa, na bado mpaka sasa kuna vitabu vingi sana vinaandikwa kuhusu tukio hili, angalia kitabu: Al-fahrisu shamil liturathil Arabii Islami, na: Al-Makhtuutu sira wal madaaihin nabawiyya, kilichotolewa na taasisi ya Ahlul Bait, Oman, Jordan.

kupokelewa idadi kubwa ya Hadithi kuhusu tukio hilo, ni alama juu ya umuhimu wa tukio na nafasi yake katika maisha ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na katika Unabii na Utume.

Hivyo basi Al-israai ni kwenda Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kutoka msikiti mtukufu wa Makkah tukufu mpaka kufika masjidi Al-aqswa (Palestina) katika nyumba tukufu katika sehemu ya usiku, na kurudi kwake katika usiku huo huo kwa njia ya muujiza na njia ya kipekee¹²⁹.

Na Miiraji ni kupanda kwake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kutoka nyumba tukufu palestina na kupanda mpaka mbingu ya saba na kuona kwake alama kubwa za Mwenyezi Mungu na kurudi kwake katika msikiti mtukufu katika usiku huo huo.¹³⁰

Na Israa ndani yake kuna mafungamano kati ya Nyumba ya ALLAH tukufu katika mji wa Makkah na msikiti wa Al-aqswa (Jerusalem) na kufungamana na Bwana Mtume- Daawa ya Tauhiid ambayo walikuja nayo waliomtangulia -**Rehema na amani ziwe juu yake**- hivyo basi ALLAH ni mmoja na Dini ni moja na asili ya wanadamu ni moja, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿ذُرِّيَّةً مَنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا﴾ [الإسراء: 3]

¹²⁹ Angalia Bin Kathiir ,siirat an-nabawiyat juzuu ya 2/95; Bin Hajar Fathul Baar juzuu ya 15/49 na mahdii Rizqullah ukurasa wa 233; Bin Saad Siirat Nabawiyat kutoka katika twabaqat juzuu ya 1/213.

¹³⁰ Angalia Al-maghaaziy ya Bin Abii Shaibah ukurasa 120, Bin Saad, Siirat Nabawiyat kutoka katika Twabaqat juzuu 1/213.

"Ni kizazi ambacho tulikibeba pamoja na Nuhu hakika yeye alikuwa ni mja mwenye kushukuru". [Al-israa: 3] Na lengo ni moja, na amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَأِلَىٰ عَادِ أَخَاهُمْ هُودًا قَالَ يَقَوْمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنِّ إِلَهِ غَيْرُهُ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿65﴾﴾
[الأعراف: 65]

"Na kwa watu wa Adi tulimtuma ndugu yao Hud akawaambia muabuduni ALLAH hamna nyinyi Mungu kinyume na yeye ALLAH, hamuogopi". [Al-aaraaf: 65] Na kwa hakika Aya zimeelezea tukio la Israa katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنَ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿1﴾﴾ [الإسراء: 1]

"Mwenyezi Mungu Mtukufu anajisifu na kujitukuza kwa uwezo Wake juu ya yasiyowezekana kwa yeyote isipokuwa yeye, hapana Mola isipokuwa yeye, hapana Mlezi isipokuwa yeye. Yeye Ndiye ambaye Aliyempeleka mja wake Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kipindi cha usiku, kwa mwili wake na roho yake, katika hali ya kuangaza na siyo ya kulala, kutoka msikiti Mtukufu wa Makkah, kwenda msikiti wa Aqṣā uliyoko Bayt al- Maqdis, ambao Mwenyezi Mungu Amezibariki sehemu zinazouzunguka kwa matunda, nafaka na vinginevyo, na Akaufanya ni mahali pa Manabii wengi, ili ajionee maajabu ya uweza wa Mwenyezi Mungu na dalili za upweke wake. Hakika Mwenyezi Mungu, Aliyetakata na kutukuka, Ndiye Mwenye kuzisikia sauti zote, Ndiye mwenye kukiona kila cha kuonekana, na atampa kila mmoja anachofaa kupata duniani na Akhera". [Surat Israa: 1].

Na ni wazi kuwa safari hii ya usiku (Israa) ilikuwa ni kwa mwili na roho yake -Sala na amani ziwejuu yake-

Mwanzo mwa Israa alipokuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alikuwa amelala nyumbani kwake katika mji wa Makkah, Jibrili -juu yake amani- akamjia akamchukua mpaka katika kisima cha zamzam na akampasua kifua chake na kumsafisha moyo wake na akaujaza imani na hekima, (249) na kupasuliwa huku hakupingani na kupasuliwa kwake katika matukio mengine, (250) na akamletea mnyama aitwaye Buraq, mnyama ambaye ana mwendo mkali na mwendo maalumu hakuna aujuaye isipokuwa ALLAH Mtukufu.

Na akampa mnyama huyo -Sala na amani ziwe juu yake- na akamfikisha haraka katika msikiti mtukufu wa Aq-swaa (Jerusalem)¹³¹

Na kwenye msikiti wa Aq-swaa Buraqu alifungwa katika kilinge ambacho Manabii walikuwa wakifunga wanyama wao¹³²

Na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- aliswali Rakaa mbili kisha Jibrili akamjia akiwa na vyombo viwili katika chombo kimoja kuna Maziwa na chombo cha pili kina Pombe, basi Mtume akachagua Maziwa, akasema Jibrili: "Umepatia kuchagua umbile (kinachoendana na akili salama)¹³³ ama lau ungechukua pombe ungepotea na ungepotea umma wako"

¹³¹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/397.

¹³² Kutoka katika Hadithi ya Muslim na kutoka katika Riwaya ya Bin Abii Shaibah, Al-maghaazi ukurasa wa 120.

¹³³ kutoka katika Riwaya ya Muslimu katika sihihi yake Angalia Bin Hishaam Siirat Nbawiyat juzuu ya 1/387.

Na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Bin Is-haqa kuwa yeye Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- alikuta kundi kubwa la manabii miongoni mwao ni Ibrahim kipenzi na Mussa na Issa katika kundi la manabii wamekusanyika kwa ajili yake na akawasalisha-Sala na amani ziwe juu yake-¹³⁴

Kisha akapanda Mtume mbinguni, Na ameweka imamu Bukhariy katika sahihi yake mlango ameuuta mlango wa Miiraj¹³⁵, amepokea humo hadithi ndefu kutoka kwa Anas Bin Maalik, ametaja ndani yake faida kwa ufupi kuhusiana na safari ya israa na Miiraj, licha ya kuwa ufafanuzi wake katika Riwaya nyingine ni mwingi.

Alikuwa Mtume Sala na amani ziwe juu yake akisimulia aliyoyaona wakati wa kupanda kwake kwenda mbinguni katika hadithi nyingi zilizopokelewa kutoka kwake, sawa ziwe hadithi hizo ni kuisifu pepo au moto, na kwa hakika alipewa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- hazina kubwa ya elimu na alama alizozishuhudia wakatiwa wakupandishwa kwenda mbinguni, na ukawa Umma unahadithia kisa hicho maisha yake yote kwa nyakati tofauti tofauti, kitu ambacho inakuwa ni vigumu kwake kuzungumzia alichokiona Mtume wa ALLAH wakati wa kupanda kwake katika hadithi moja.¹³⁶

Na kwa hakika wametolea ushahidi wengi katika maulamaa kwa kilichopokelewa katika suratu Najmi miongoni mwa aya na

¹³⁴ Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 1/398 na Siirat Nabawiyat ,juzuu 2/99.

¹³⁵ Sahihi Bukhari: 4/248.

¹³⁶ Angalia: Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/272 Bin Abii Shaibah Al-maghaazyi, ukurasa wa 120.

mafungamano kati ya Aya hizo na kupandishwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- Anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿١﴾ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾ وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾ عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ ﴿٥﴾ ذُو مِرَّةٍ فَاسْتَوَىٰ ﴿٦﴾ وَهُوَ بِالْأُفُقِ الْأَعْلَىٰ ﴿٧﴾ ثُمَّ دَنَا فَتَدَلَّىٰ ﴿٨﴾ فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٩﴾ فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ﴿١٠﴾ مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَىٰ ﴿١١﴾ أَفَتَمُنُّونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٢﴾ وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ ﴿١٣﴾ عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَىٰ ﴿١٤﴾ عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَىٰ ﴿١٥﴾ إِذْ يَغْشَىٰ السِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ ﴿١٦﴾ مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ ﴿١٧﴾ لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ ﴿١٨﴾﴾ [النجم:

[18-1

"Naapa kwa Nyota zinapoanguka" (1) Hakupotea jamaa yenu na wala hakukengeuka. (2) Na wala haongi kwa matamano ya nafsi yake. (3) Haikuwa hii Qur'ani isipokuwa ni ufunuo anao funuliwa. (4) Amemfundisha Malaika mwenye nguvu (5) Mwenye umbile kubwa kisha akalingamana (6) Na yeye akiwa juu ya wingu. (7) Kisha Jibrili akamkaribia Mtume (8) Akawa Mtume yupo karibu na Jibrili kama ukaribu wa upinde na mshale au zaidi. (9) kisha Jibrili akamfunulia mja wa ALLAH aliyo mfunulia (10). Moyo wa Mtume haukusema uongo uliyo yaona. (11) Je! mnabishana naye kwa yale aliyo yaona (12) Na Mtume akamuona Jibrili mara nyingine (13) Kwenye mkunazi wa kumalizikia mambo yote, (14) Kwenye Mkunazi huo ndipo kuna pepo yenye kila aina za neema (15) Kilipo ufunika Mkunazi huo kilicho ufunika. (16) Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka. (17) Hakika Muhammad aliona katika ishara kubwa kabisa za Mola wake Mlezi. (18). [An-naji: 1-18]

Kisha akarudishwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kutoka kupanda kwake mbinguni mpaka Masjid Aq-swa (Jerusalem) na kutoka masjidul Aq-swa akarudi mpaka Makkah katika usiku wake.

Na akawahadithia Mtume -Sala na mani ziwe juu yake- watu wa Makkah asubuhi ya siku iliyofuata, na akaamsha mshangao kwao.

Kwa hakika alikuwa Abubakar ni wa pekee -Radhi za Allah ziwe juu yake- katika ile asubuhi ya kupelekwa kwake masjidul Aq-swa kwa msimamo wake toka kwa Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake-** na walifurahia washirikina habari hii, na wao wanajua akili ya Abubakari na uchambuzi wake wa habari, lakini wao hawapimi mambo kama anavyopima yeye na upeo wa mtazamo wake kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-:

Basi wakaenda mbio washirikina wa Makkah kwa Abubakari - Radhi za Allah ziwe juu yake- na wakampa habari ya aliyoyasema kutokana na safari yake ya miiraji (usiku) -Sala na amani ziwe juu yake- Akasema -Radhi za ALLAH ziwe juu yake-: "Namuapia ALLAH ikiwa atakuwa amesema basi ni mkweli, na nini kinachowashangaza katika hilo?! Namuapia Mwenyezi Mungu hakika yeye huniambia habari inayomjia toka mbinguni katika wakati wa usiku na mchana na hii ni habari ya mbali zaidi ambayo mnaishangaa"¹³⁷Kisha Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- akamwendea Mtume ili akamuulize mbele ya watu ili amsadikishe, basi kila alivyokuwa akiongea Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na akataja kitu alimwambia: 'Umesema kweli' na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- anamwambia: "Na wewe Abubakari ni mkweli"¹³⁸

Na muda wa israa (safari hii ya usiku) kwa undani kuna hitilafu ya kauli za wasomi, kuna miongoni mwao wanaoona kuwa Israa ilikuwa

¹³⁷ Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 1/399 na Siirat Nabawiyat ,juzuu 2/97.

¹³⁸ Al-haakim Fil Mustadrak juzuu ya 3/63, na ameisahihisha Imamu Dhahabiy; Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/399.

ni mfungo sita, na kuna wanaoona kuwa ni katika mwezi wa Rajab na vinginevyo.¹³⁹

Na mazingatio hayako katika muda, lakini mazingatio yapo kwenye tukio na utukufu wa Mtume katika tukio hilo, na somo lenye faida kutokana na tukio hilo na kujua hali na matokeo yake.

KUJITANGAZA KATIKA MAKABILA [260]

Na yalikuwa yote hayo ni huruma ya ALLAH kwa Mtume wake Sala na amani ziwe juu yake- na alichomfanyia na kumlea na kumfundisha kwa kumuandalia chenye kumfanya kuyajua makabila na sehemu zao, kwa hakika Mtume alifanya kazi katika biashara ya Kahdija, na alikuwa Khadija ana heshimaka kwa watu wa Makkah na alikuwa akichanganyikana na watu waliokuwa wakija kwake kutoka katika makabila tofauti tofauti, kama alivyokuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ni miongoni mwa waliokuwa wakiyazungukia masoko ya warabu ambayo yalikuwa ni mengi, miongoni mwayo ni ya msimu wakati ambapo warabu walikuwa wakija katika soko la Ukaadh karibu na Taif¹⁴⁰kisha wanaondoka hapo wanaelekea Hijja unapo karibia muda wake kisha masoko yanaungana kwa kuelekea kwenye soko liitwalo Majannat na soko liitwalo Dhil majaazi¹⁴¹

¹³⁹ Angalia: Bin Saad Siirat Nabawiyat katika Twabaqaatul kubraa, juzuu ya 1/213 Bin Kathiri Siirat Nabawiyat juzuu ya 2/107, Muhammad Abuu Shaibah Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/418.

¹⁴⁰ Angalia: Nasor Al-Rashiid, soko la Ukaadhi kabla ya uislamu na baada ya uislamu, Historia yake na kukua kwake na mahala lilipo. Chapa ya kwanza: Daarul Answaar, Cairo, mwaka 1379H.

¹⁴¹ Rejea Saiidul Afghhaan, As-waaqul Arab fil Jaahiliyyat wal-islam chapa ya tatu Daarl fikri, Beirut 1394H.

Na alipotumwa bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake na akaiweka wazi Daawa yake walimpiga vita watu wake tangu mwanzo, na ilikuwa Daawa yake ni ya ulimwengu mzima na haikuishia Makkah na watu wake pekee, bali daawa yake ilikuwa ni ya viumbe kwa mjumbe kutoka kwao wenyewe na kwa ajili yao.

Na zilikuwa zikimteremkia Aya kuanzia mwanzo wa kutumwa zinazotia mkazo kuwa ujumbe wake ni wa ulimwengu mzima, na aya hizo ni:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾ [الأنبياء: 107]

"Na hatukukutuma, isipokuwa uwe ni rehema kwa watu wote"
[Al Anbiyaai: 107]. Nakuwa Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kutukuka Amesema:

﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾ [الفاحة: 2]

"Kila sifa njema ni zake ALLAH Mola mlezi wa walimwengu".
[Al-fat-ha: 2]

Na haikuwezekana abakie katika mji wa Makkah, na tangu mwanzo alikuwa akifanya Daawa katika masoko na kati ya waliokuwa wakija Makkah wakitokea nje ya mji wa Makkah.

Kama ambavyo Sala na amani ziwe juu yake alikuwa akiingia katika mikusanyiko ya makabila wakati wa Hijja, na akiwatangazia ujumbe na alikuwa Abuulahab akifuatia nyuma yake kujaribu kuwaweka watu mbali na kumsikiliza Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na alikwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- anasema: "Enyi watu wa kabila fulani hakika mimi ni Mtume wa ALLAH niliyetumwa kwenu nyinyi anawaamrisheni mumuabudu ALLAH na wala msimshirikishe yeye na chochote na muachane na mnavyoviabudu asiyekuwa ALLAH katika hii miungu, na kuwa mniamini mimi na mnisadikishe na mnihami, mpaka nibainishe

yatokayo kwa ALLAH yale aliyonituma kwayo, na alikuwa Abu Jahal akiwazuia watu wasimsikilize Mtume na akimweka mbali na akiwaambia Hakika yeye ni mwenda wazimu na wakawa baadhi yao wakimjibu majibu mabaya, na anasema kumwambia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa watu wako ni wajuzi kuliko wewe na wakimjibu majibu mabaya.¹⁴²

Na alikuwa Abuubakar swidiq- Radhi za Allah ziwe juu yake- akiwa pamoja na Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- wakati alipokuwa anayazungukia makabila na hasa wakati wa Hijja hivyo anaongeza uzoefu mwingine wa kuyajua makabila na kukaa nayo na kujua idadi yao na nguvu zake, na alikuwa Abuubakar akiuliza wakati mwingine: "Idadi yenu ni wangapi? na vipi kuhusu nguvu yenu?"¹⁴³

Na katika mwaka wa kumi tangu kupewa utume na mwaka uliofuata alizidisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kujitokeza yeye mwenyewe kwenye makabila na hasa baada ya kurudi safari yake ya Twaif¹⁴⁴ na vilinukuu baadhi ya vyanzo kwa uchanganuzi zaidi kuhusu huko kukutana na makabila.

Na katika makabila ambayo Mtume aliyatokea yeye mwenyewe ni kabila la Bani Aamir Bin Swa'aswaa, akasema mmoja katika

¹⁴² Angalia: Siira ya Bin Kathiir juzuu ya 2/185, Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/424.

¹⁴³ Musnad Imamu Ahmad, Bin Kathiir, Siirat Nabawiyat juzuu ya 2/166.

¹⁴⁴ Angalia majina ya makabila haya na kuyatokea kwake Mtume - Sala na amani ziwe juu yake- kwenye kitabu cha Bin Hishaam katika Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/424; na Rejea kitabu cha An-saabu cha Al-sam'aan.

wakuba wao naye Baiharat Bin Firaas: "Namuapia ALLAH lau kama ningemchukua kijana huyu wa kikuraishi ningewamaliza warabu kupitia kijana huyu", kisha akamwambia Mtume: "Waonaje ikiwa sisi tutakufuata kwenye jambo lako kisha ALLAH akakubadilishia na jambo likawa kwa mwenye kwenda kinyume nawe, je tutakuwa na mamlaka baada yako? Akasema: "Mamlaka ni ya ALLAH anayaweka atakapo" akasema: "Tujiangamize kwa Warabu kwa ajili yako, ikiwa atakuteua ALLAH basi Mamlaka yatakuwa kwa wengine wasiyokuwa sisi, hivyo, hatuna haja na jambo lako".

Na ukaja ujumbe wa watu wa Madinah katika mwezi wa Rajab kabla ya msimu uliofuata na wakakutana na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-¹⁴⁵

Na miongoni mwa waliokutana na Mtume katika makabila ni Banii Shaibaan Bin Tha'alaba katika kabila la bani Bak'ri Bin Waail.

Na yakawa majibu yao kwa Mtume: ikiwa utataka tukuhifadhi na tukunusuru na hawa warabu walio mbele yetu basi sisi twaweza hilo, akasema Mtume -Rehema na mani ziwe juu yake-: "Hamkukosea majibu kwenye majibu yenu mlipo ongea ukweli, na kwa hakika dini ya Mwenyezi Mungu -kutakasika na machafu ni kwake- hatoinusuru isipokuwa yule ambaye ataifahamu kikamilifu, mwaonaje lau mngelikaa muda kidogo ili Mwenyezi Mungu awarithishe Ardhi yao na majumba yao na awamilikishe wake zao, hivi ikiwa hivyo mtamtukuza na kumtakasa Mwenyezi Mungu?)) Akasema Nuuman: "Ewe Mola wetu wa haki, tumekubali hilo kutoka kwako ewe ndugu mkuuraishi" Basi Mtume akawasomea maneno yake ALLAH:

¹⁴⁵ Al-maghaaz cha Bin Abii Shaibah ukurasa 125- na tazama: Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/242.

﴿إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِيدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا﴾ [الفتح: 8]

"Hakika tumekuleta ili uwe shahidi na mtoaji wa habari njema na muonyaji" Kisha akainuka¹⁴⁶

Na kwa hakika alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake Daa'wa yake ni ya ulimwengu mzima hakukubali yeyote kumwekea mipaka ya kiJiografia au ya kibinadamu au mipaka ya wakati, na ndiyo maana hakuwakubalia banii Shaibaan isipokuwa kukubali kwa moja kwa moja pasina kuwawekea mipaka ya mji wa Fursi (Iran) au ya kisiasa.

Alikuwa Mtume Sala na amani ziwe juu yake- akiuwekea uislamu misingi yake ambayo itasambaa ulimwenguni kote, misingi ambayo haitabagua wakazi wala haitovunja makubaliano au kwenda kinyume na makubaliano ya mwanzo, kama ambavyo Mtume hataki kuweka masharti ambayo yatafanya utawala baada yake kuwa ni wa kabila fulani au kiongozi fulani, hivyo misingi hiyo ni Daa'wa na ni dola ya ulimwengu mzima, na kufanya kwa utakasifu na kukubali kwa ajaili ya ALLAH -Mtukufu- peke yake, na kana kwamba yeye Mtume Sala na amani ziwe juu yake- alijua kuwa Daa'wa hii itaingia katika vita na mfalme Kisra wa Fursi (Iran) katika siku za usoni, hivyo, ndiyo maana hakukubali kulivua kabila la Shaibaani.

KUKUTANA KWA MARA YA KWANZA NA ANSWAAR (WAKAZI WA MADINA):

Walikuwa Ausi na Khazraj ni wakazi wa wa mji wa Madina Munawwara [269]] na palitokea kati yao vita, na vita iliyokuwa

¹⁴⁶ Angalia: Bin Kathiir Al-bidayat wannihaayat juzuu ya 2/167na Al-swaalihi Al-shaamiy, Subul hudaa warrashaad juzuu ya 2/596, na Swallaabiy Siirat juzuu ya 1/443,444.

mashuhuri zaidi ni vita ya siku ya Buaath,¹⁴⁷na kwa hakika kila mmoja wao alikuwa akitafuta mshirika atakaye mpa nguvu na kumsaidia katika vita hii, yeye akawa wa kwanza kuwajulisha kuhusu uislamu.¹⁴⁸¹⁴⁹

Na ilikuwa vita hii ni sababau ya kumsikiliza Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- walipokuja Makkah kutaka msaada, kama ambavyo ilikuwa ni sababu iliyopelekea kuwa kitu kimoja nyuma ya Mtume-Sala na mani ziwe juu yake, na bila shaka vita iliwatafuna na wakabaini baada ya hapo kuwa misingi ya Mtume ni umoja na Amani.

Na walikuwa Mayahudi wakiishi katika mji wa Madinah na kabila la Ausi na Khazraj, na wakizungumzia kuhusu kukaribia kuja kwa Nabi wa mwisho wa zama hizi na wakiwatishia kuhusu Nabii huyo, Na kumesemwa kuwa Mayaudi ilikuwa ikitokea kati yao na jirani zao katika kabila la ausi na Khazraj mapigano, basi Mayahudi huwatishia na kuwaambia: "Hakika mtume wetu atatumwa hivi karibuni, bila shaka muda wake umefika na tutamfuata na tutawauwa tukiwa naye pamoja mauaji kama ya Adi na Iram". Basi na makabila ya Ausi na Khazaraj walipokutana na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-

¹⁴⁷ angalia Bin Kutaibah Al-maarif ukurasa wa 109; na Alnawawiy, nihaayat Al-rbi juzuu ya 1/311; Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/428 Bin kathiir Siirat An-nabiyat juzuu ya 2/172.

¹⁴⁸ Moja kati ya masiku mashuhuri ya vita kati ya Ausi na Khazraj kabla ya uislamu. Angalia: Jawaad Ally AL- MUFASWAL 4/140.

¹⁴⁹ Amepokea Imamu Bukhariy katika sahihi yake, kitabul manaaqibul Answaar, mlango wa Manaaqibul Answaar, juzuu ya 4/221.

alipojitokeza kwa makabila wakasema baadhi yao kuwaambia wengine: "Tunaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Hivi mnajua hakika huyu ni Nabii ambaye mayahudi walikuwa wakiwaahidi?, basi chungeni wasijekuwatangulia kwenda kwake"¹⁵⁰

Na walipokutana na Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- alisema kuwaambia: "Nye ni akina nani?" wakasema: "Ni watu kutoka katika kabila la Khazraj", akasema: "Mnatoka kwa mabwana wa kiyahudi?" wakasema: "Ndiyo", Akesema: "Hivi hamkai niwaelimishe?" wakasema: "kwa nini tusikae" basi wakakaa naye akawalingania katika njia ya Mwenyezi Mungu-kutakasika ni kwake na Mtukufu- na akawatangazia uislamu na akawasomea Qur'ani, wakasema baadhi yao kuwaambia wengine: "Enyi watu hivi mwajua tunakuapieni kwa jina la ALLAH hakika yeye nduye Nabii ambaye mayahudi walikuwa wakiwaahidi kuja kwake?, basi wasiwatangulieni kwenda kwake", hivyo wakamkubalia katika kile alichowalingania, wakamsadikisha na wakamkubalia kwa alichokitangaza katika uislamu, na wakamwambia: kwa hakika sisi tumewaacha watu wetu na wala hatutokuwa na uadui na shari kati yao, na huenda ALLAH akawakusanya kwako, basi tutawaenda na kuwaita katika jambo lako na tutawatangazia kile ambacho tumekuitikia katika dini hii, basi ikiwa ALLAH atawakusanya kwako hapatakuwa na mtu mtukufu kama wewe", kisha wakaondoka kwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- wakarudi kwenye miji yao wakiwa wameamini na kumsadikisha.¹⁵¹

¹⁵⁰ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/429.

¹⁵¹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/429.

Na walipofika Madina wakawatajia watu wao kuhusu kukutana kwao na Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- na akawalingania katika uislamu mpaka uislamu ukaenea kati yao, na haikubakia nyumba katika nyumba za Answaar isipokuwa utajo wa Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake -uliifikia.¹⁵²

KIAPU CHA KWANZA CHA UAMINIFU CHA AKABA.

(Akaba ni jina la eneo) Alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akiwapa habari maswahaba wake yakuwa imekaribia kuainishwa sehemu maalumu ambayo watahamia, sehemu ambayo watakusanyika pamoja nao mwenye kuhama, na walikuwa baadhi yao walikwisha hama kwenda Habashi (Ethiopia) kabla ya hapo, na bado wapo huko lakini wote walikuwa wakisubiri sehemu moja ya kukusanyika ambayo ALLAH atampa ruhusa Mtume wake ili wakutana naye huko au wamtangulie, na kwa hakika ukandamizaji wa makuraishi ulizidi ili kumtoa Mtume -Sala na mani ziwe juu yake- kutoka katika mji wa Makkah, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِنْ كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا وَإِذًا لَا يَلْبَثُونَ خِلافَكَ إِلَّا قَلِيلًا﴾

[الإسراء: 76]

"Na makafiri walikaribia kukutoa Makkah kwa kukukera, na lau wangelikutoa huko wasingalika huko baada yako isipokuwa muda mchache, hadi iwashukie adhabu ya ulimwenguni". [Al-Israa: 76]. Na kwa hakika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alitoa habari kuwa yeye aliiona sehemu hiyo ndotoni, na ndoto za manabii ni za ukweli, na amepokea Bukhariy katika kitabu chake sahihi kutoka kwa Abuu Musa kutoka kwa Mtume -Sala na amani

¹⁵² Bin Kathiri Assiratun- Nabawiyyat juzuu ya 1/176; Mahdi Rizqi Ilah, Al- siirat Al- Nabawiyyat kutoka kwenye vyanzo vya asili. juzuu ya 1/288.

ziwe juu yake- kuwa amesema: "Nimeona usingizi kuwa mimi nahama kutoka Makkah nakwenda kwenye Ardhi yenye mitende, na dhana yangu ikanipelekea kuwa Ardhi hiyo ni Al-yamamah au Hajar, mara ikawa ni Ardhi ya Madinah Yathriba"¹⁵³¹⁵⁴

Na walikuwa Mayahudi wameweka makazi katika mji wa Madinah na pambizoni mwa Madinah kwenye mitende na Ardhi ya Mawe meusi makali (Ardhi ambayo mawe yake meusi makavu) Kwa kujua kwao sehemu atakayohamia Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake-, na kumsubiri kwao.

Na katika mwaka wa pili tangu kupewa utume walifikiana kikundi miongoni mwa waliosilimu katika Answari, na walikua wamekwisha mtambua na wakajua ujumbe wake kabla ya tarehe hiyo kwa miezi mingi, kuwa wapange kukutana maalumu na Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-.

Walikuwa wanaume kumi na mbili¹⁵⁵ watu kumi ni katika kabila la Khazraj na wawili ni katika kabila la Ausi¹⁵⁶ kwa namna ilivyojulikana kwa jina la Baiatul Aqabah (kiapo cha uaminifu cha kwanza)

¹⁵³ Neno Wahliy: yaani Dhana yangu.

¹⁵⁴ Ameipokea Imamu Bukhariy, mlango wa kuhama kwa Mtume - Sala na amani ziwe juu yake- na Maswahaba zake kwenda Madinah juzuu 4/252.

¹⁵⁵ Bin Hishaam Saiirat Nabawiyat. Jambo la Aqabah ya Kwanza juzuu ya 1/292.

¹⁵⁶ Angalia: kitabu kiitwacho Al-siirat sahihi cha Akrim Al-Amriy juzuu ya 1/197

Na alishuhudia shahidi wa moja kwa moja miongoni mwa watu wa usiku wa Aqabah naye ni Ubadat Bin Swaamit -Radhi za Allah ziwe juu yake- "Kuwa Mtume Sala na amani ziwe juu yake amesema na pembeni yake walikuwepo kundi la maswahaba wake: "Njooi mchukue kwangu Ahadi yakuwa msimshirikishe ALLAH na kitu chochote na wala msiibe na wala msizini wala kuwauwa watoto wenu, na wala msilete uzushi mnaouzusha baina yenu kwa mikono yenu na miguu yenu wala msiniasi katika jambo jema, basi atakayetokeleza anamalipo yake kwa ALLAH, na yeyote atakayefanya katika hayo jambo lolote na akaadhibiwa kwa jambo hilo Duniani basi adhabu hiyo kwake humfutia kosa hilo, na yeyote atakayefanya chochote katika hayo kisha ALLAH akamsitiri basi jambo lake hilo litakuwa kwa ALLAH akitaka atamuadhibu na akitaka atamsamehe" tukachukua Ahadi kwa hayo.¹⁵⁷

Na ulikuwa uchukuaji Ahadi huu ni uchukuaji Ahadi ya ulinganiaji (Daawa) ulio salama na misingi yake ni Tauhiid na Utiifu, na hakukutajwa hapo vita, na kwa ajili hiyo waliita baadhi ya Maswahaba kwa jina la (Uchukuaji Ahadi wa wanawake).

Na watu walipoondoka kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- aliwatumia na wakaenda pamoja naye Mus'ab Bin Umair -Radhi za Allah ziwe juu yake- na akamuamrisha awasomeshe Qur'ani na awafundishe uislamu na awafundishe dini, na alikuwa msomaji

¹⁵⁷ Ameipokea Bukhariy, katika mlango wa Ujumbe wa Answaar juzuu ya 4/251.

katika mji wa Madinah anaitwa Mus'ab¹⁵⁸ na kama alivyokuwa Imam wa katika Swala -Radhi za Allah ziwe juu yake-¹⁵⁹

Na kukatimia kumpokea kwake -Radhi za Allah ziwe juu yake- katika mji wa Madinah na kumnusuru na kulindwa na waislamu wa mwanzo katika Maanswari.

Na alikuwa Mus'abu -Radhi za Allah ziwe juu yake- ni mwenye juhudi kubwa katika kuwasaidia watu wa Answari, katika kuueneza uislamu katika mji wa Madinah kwa wema na hasa baina ya wakubwa na vionozzi ambao wana ushawishi katika mji kwa wengine.

Na kwa hakika alijitahidi Mus'ab Bin Umair -Radhi za Allah ziwe juu yake- jitihada ya kila aina kwa ujumla na kikamilifu, na wakasilimu kwenye mikono yake idadi kubwa ya Answari, na akawaandaa kukutana na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake katika mji wa Makkah katika msimu wa Hijjah mwaka wa kumi na tatu tangu kupewa utume.

Na kwa hakika alisema ukweli Mus'ab bin Umair katika kazi hii na nyingine, naye ni miongoni mwa wale aliowasema Mwenyezi Mungu:

﴿مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُمْ مَّنْ يَنْتَظِرُ

وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا﴾ [الأحزاب: 23]

"Miongoni mwa Waumini kuna wanaume waliotekeleza ahadi zao walizomuahidi ALLAH, Aliyetukuka, na wakasubiri juu ya shida,

¹⁵⁸ Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/293; Angalia hadithi ya Bukhari juzuu ya 4/263.

¹⁵⁹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/293.

madhara na wakati wa vita. Kati yao kuna aliyetekeleza nadhiri akafa shahidi katika njia ya ALLAH au akafa juu ya ukweli na utekelezaji ahadi, na kati yao kuna anayengojea moja wapo ya mema mawili, ushindi au kufa shahidi, na hawakuigeuza ahadi ya ALLAH wala hawakuitangua wala hawakuibadilisha kama vile wanafiki walivyogeuza". [Al-ahzaab: 23]¹⁶⁰

AHADI YA UAMINIFU YA PILI YA AKABA:

Uislamu ulienea katika majumba ya Answaar katika mji wa Madinah na wakawa wakisomeshana Qur'anl na wakiswali nyuma ya Mus'ab huku wakisubiri kukutana na Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kulikuwapo na Uratibu kati ya Mus'ab na Mtume wakisubiria jambo hilo na kujiandaa kwa ajili yake.

Kama alivyokuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akisubiri mfano wa hawa waumini wa kweli, na inabainika kuwa yeye alipokuwa akikutana na baadhi ya waislamu wa Madinah walikuwa wakisema baadhi yao kuwaambia wenzio kama ilivyopokelewa kutoka kwa Jaabir Bin Abdillah: "Tunawezaje kumuacha Mtume wa Allah afukuzwe katika milima ya Makkah na kutishwa".¹⁶¹

Na amepokea Bin Is-haqa Riwaya Ndefu na yenye kutosheleza katika Historia yake kutoka kwa shahidi aliyeshuhudia moja kwa moja uchukuaji Ahadi wa akabah kwa mara ya pili na uchanganuzi wa ndani pale ilipo pokelewa kutoka kwa Kaab Bin Maalik Amesema:

¹⁶⁰ Tafsiri ya Twabariiy juzuu ya 10/280; Tasiir ya Bin Kathiir juzuu ya 2/1488.

¹⁶¹ Angalia kitabu kiitwacho As-siiratu sahihi cha Akrim dhwiyaaul Amriy juzuu ya 1/198

"Tulitoka kwenda Hijja na tukamuahidi Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- kukutana naye katikati mwa masiku ya kutanda nyama, akasema na tulipomaliza Hijja na ulikuwa ni usiku ambao ametuahidi Mtume katika usiku huo, na tulikuwa pamoja naye Abdullahi Bin Amrou Bin Haraam Abuu Jaabir bwana mkubwa katika mabwana wakubwa wetu na ni mtukufu katika watukufu wetu tulimchukua kwenda nasi, na tulikuwa tukimficha jambo letu yeyoto anayekuwa nasi katika watu wetu waliokuwa washirikina, hivyo tukamsemesha na kumwaambia: "Ewe Baba Jaabir hakika wewe ni Bwana mkubwa katika mabwana wakubwa wetu na sisi hatupendezwi na hayo uliyonayo ambayo yatakufanya kesho uwe kuni za moto, kisha tukamlingania katika uislam, na tukamfahamisha kuhusiana na ahadi yetu katika sehemu ya Akabah na bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-akasema: "Bsi Akasilimu na akashuhudia pamoja nasi uungaji mkono wa Akabah na akawa ni miongoni mwa Majemedari.

Akasema: Basi tukulala usiku ule sisi na watu wetu katika vipando vyetu, mpaka ilipopita theluthi ya usiku tulitoka kwenye vipando vyetu kwa ajili ya ahadi yetu ya kukutana, tukatembea tukinyata unyataji wa paka huku tukijificha, mpaka tukakusanyika kwenye makutano ya njia mbili kwenye Akabah, na sisi tulikuwa idadi ya watu sabini, na wapo pamoja nasi wanawake wawili katika wanawake wetu Nusaibah Bint Qaab na Ummu Ammara, mmoja miongoni mwa wanawake wa Banii maazin Bin An-najjar, na Asmaa Bint Amrou Bin Adiiy, mmoja wa wanawake wa Banii Salama, naye ni mama Maniiu.

akasema tukakusanyika kwenye pango tukiwa tunamngoja Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- mpaka akatujia akiwa pamoja naye (Baba yake mdogo) Abbas Bin Abdul Mutwalib, naye wakati huo alikuwa katika dini ya watu wake isipokuwa yeye alipenda kuhudhuria jambo linalomuhusu mtoto wa ndugu yake na kumpa matumaini, na alipokaa alikuwa wa kwanza kuongea ni

Abbas Bin Abdul Muttwalib, Akasema: "Enyi kundi la Khazraji, na walikuwa warabu wakikiita kijiji hiki cha Answaar kwa jina la (Khazraj) Kwa hakika Muhammad anatokana nasi kama mnavyojua, na tumlikatalia kuwa ni katika watu wetu ambao walikuwa wanamtazamo kama wetu, hivyo yeye yupo katika ya kutenzwa nguvu na ndugu zake na kuwekewa kizuizi katika mji wake, na yeye alikataa yote na akachagua kuwa nanyi na kukutana nanyi, ikiwa mnaona kuwa nyinyi mtakuwa ni wenye kumtekelezea kila mlichio muitia, na mtamlinda kutokana na mwenye kumpinga basi shikamaneni na mliyoyakubali kuyabeba, na ikiwa mnaona kuwa mtamsaliti na kumfedhehesha atakapokujieni, basi kuanzia sasa mwacheni, kwa hakika yeye yupo katika hali ya kutenzwa nguvu na watu wake na kuzuiliwa mji wake. Akasema Tukamwambia: kwa hakika tumesikia uliyoyasema, Basi sema ewe Mtume wa ALLAH, basi kwa ajili yako na kwa ajili ya ALLAH unachokipenda.

Akasema: Basi akaongea Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- na akasoma Qur'ani na akalingania kwa ALLAH, na akahamasisha juu ya uislamu, kisha akasema: "Nawatakeni Mniunge mkono kwa kunilinda kama ambavyo mnawalinda wake zenu na watoto wenu" Akasema Baraa Bin Maaruri akamshika kwa mkono wake kisha akasema: "Ndiyo, Numuapia yue ambaye amekutuma kwa haki kuwa (Mtume) tutakulinda vile ambavyo tunawalinda wenye kusaidiana nasi, hivyo tunamuunga mkono Mtume wa ALLAH, na ninamuapia ALLAH hakika sisi ni wana wa vita na watumiaji silaha tulierithi silaha hizo toka kwa Mababu na Mababu, Akasema zikapishana kauli, na Baraa anamsemesha Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na amani ziwe juu yake- na Abuu Haitham Bin Al-Tahayyaan, akasema: ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: "Hakika sisi na mayahudi tuna makubaliano kati yetu, na sisi tutayavunja, je ikitokea kuwa tumevunja makubaliano kisha ALLAH akakurudisha kwa watu wako vipi je utatuacha? akatabasamu Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- kisha akasema:

"Bali atakaye mwaga damu yenu hakika amemwaga damu yangu, na atakaye waangamiza nyinyi atakuwa ameniangamiza mimi, mimi natokana nanyi na nyie mwatokana na mimi. Nitapigana na mnayepigana naye, na ninajisalimisha kwa yule ambaye mnajisalimisha kwake"¹⁶²

Na walikuwa wenye kumuunga mkono ni katika Answaari -Radhi za Allah ziwe juu yao- walikuwa wakijua uhatari wa kuunga mkono na yanayotokana na uungaji mkono, pale ambapo masharti yake yanatofautiana na uungaji mkono wa mwanzo, na ilikuwa uungaji mkono katika vita unatofautiana na uungaji mkono wa wanawake¹⁶³na jambo hili lilikuwa wazi, na pamoja na hivyo Abbas Bin Ubaadah Al-answaariy alitaka watu wafahamu vizuri yale watakayoyafanya, Akasema: "Enyi kongamano la Khazrajy hivi mnatambua kuwa ni jambo gani ambalo mnamuunga nalo mkono huyu mtu? wakasema: "Ndiyo" Akasema: Hakika nyinyi mnamuunga mkono kupigana vita na watu weupe na weusi, basi ikiwa mnaona kuwa mali zenu zitaangamia na waheshimiwa wenu watauliwa, hivyo mkawa ni wenye kumsaliti basi kuanzia sasa Naapa kwa jina la ALLAH tambueni kuwa kufanya hivyo ni fedheha hapa Duniani na Akhera, na ikiwa mnaona kuwa mtamtekelezea kile mlichomuitia hata kama mali zitaangamia na kuuwawa waheshimiwa basi fanyani jambo hilo, na ninamuapia ALLAH hilo ni jambo la kheri hapa Duniani na kesho Akhera, wakasema: kwa hakika sisi twalichukua jambo hilo hata kama mali zitateketea na hata kama waheshimiwa watauawa sisi tutapata malipo gani ikiwa tutatekeleza hilo ewe Mtume wa ALLAH? Akasema: "Mtalipwa pepo", Wakasema:

¹⁶² As-siirat Nabawiyat cha Bin Hishaam, juzuu ya 1/440/-.442

¹⁶³ Angalia: Fiq-hu Siirat ya Al- Ghazaliy ukurasa wa 160.

"Nyoosha mkono wako", akanyoosha mkono, basi wakamuunga mkono.¹⁶⁴

Hakika walikuwa ni wakweli katika kumuunga mkono, wakasema kumwambia Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- Na Tunamwapia yule aliyekutuma kwa haki, ikiwa utataka tutawavamia kesho watu wa Minah kwa mapanga yetu, akasema Mtume -Sala na amani ziwe juu yake: "Hatukuamrisha kufanya hivyo, na rudini kwenye vipando vyenu"¹⁶⁵. Basi wakarudi kwenye vipando vyao, na Mtume Sala na amani ziwe juu yake aliwataka wamtotee majemedari wao wapatao kumi na mbili, basi wakawatoa Majemedari tisa toka upande wa kabila la Khazraji na watatu toka upande wa kabila la Ausi, na walikuwa ni viongozi wa watu wao.¹⁶⁶

Na baada ya watu kuondoka Minah Makuraishi walipata uhakika wa habari hii, wakajaribu kuwashika watu wa Madinah na wakaweza kumkamata Saad Bin Ubaadah -Radhi za Allah ziwe juu yake- na wakaifunga mikono yake kwenye shingo yake na wakamburuzza mpaka mjini Makkah, na wakaanza kumpiga -Radhi za Allah ziwe juu yake- na wakawa wakimuudhi na kumtukana.

Uungaji mkono ulihitajia kupangwa upya kwa Mus'abu Bin Umairi -Radhi za Allah ziwe juu yake- na wale walio amini pamoja naye miongoni mwa watu wa Madina.

¹⁶⁴ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/446.

¹⁶⁵ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/446.

¹⁶⁶ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 2/198.

Kama vile ambavyo jambo lilikuwa wazi kwa bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- yeye atasimama nao kama walivyo simama naye: "Atakaye mwaga damu yenu hakika atakuwa amemwaga damu yangu na atakaye waangamiza hakika atakuwa ameniangamiza mimi"¹⁶⁷

Na alikwisha wafundisha Mtume Utaratibu na mipangilio na majukumu na namna ya kushauriana kwa wakati mmoja kwa kuwataka (wao wenyewe) wamchagulie watu kumi na mbili katika majemedari ambao watakuwa ndiyo wasimamizi wa watu wao, Hatua inayofuatia siyo iliyopita na upangiliaji na kugawa majukumu na kushauriana na watu wengine ni katika mienendo ya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-¹⁶⁸

Na hivi ndivyo walivyojipanga watu wa Madina wakiwa tayari kumpokea bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika nyumba iliyochagulia katika mji wa Madina Nyumba ya watu wa Madina na wanaume wake.

Na ilikuwa uungaji mkono huu ni kutangaza mlango wa kuhama kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- wakati ujao na ni katika muda wa hivi karibuni- kwa Idhini ya ALLAH- na wakati huo huo kukafunguliwa mlango wa waumini kuhama ili wamtangulie Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- wamtangulie katika mji wa Madina ili waanzishe jamii ya kiislamu na dola yake ya Mtume na Nidhamu za mipango miji na nidhamu za kiaskari.

¹⁶⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Kathiir juzuu ya 2/198.

¹⁶⁸ Angalia: Fiqhu siirat ya Muhammad Alghazaal ukurasa wa 159.

Kwa hakika washirikina wa Makkah walizidi kuwakamata waislamu baada ya kujua mchanganuo wa makubaliano ya uungaji mkono, basi wakawabana maswahaba miongoni mwa waislamu wa kikuraishi na wengineo katika mji wa Makkah, na wakawa wakimtilia shaka Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na akawa akiwaamrisha kuhama kwa kuwaambia: "Kwa hakika ALLAH-kutakasika na machafu ni kwake- amewapeni ndugu na nyumba ambayo humo mtaishi kwa amani"¹⁶⁹

KUHAMA KWA MASAHABA WA MTUME REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:

Neno (Hijra) katika lugha ya kiarabu: maana yake ni kutoka katika Ardhi kwenda Ardhi nyingine,¹⁷⁰na matumizi ya neno hilo katika sheria ni Kuuacha Mji wa kishirikina na kuhamia mji wa kiislamu, na mji ambao atakuwa na amani katika dini yake¹⁷¹kutokana na kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿ وَمَنْ يُهَاجِرْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يَجِدْ فِي الْأَرْضِ مُرَاعًا كَثِيرًا وَسَعَةً وَمَنْ يَخْرُجْ مِنْ بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴾
[النساء: 100]

"Na yeyote mwenye kutoka kwenye ardhi ya ushirikina kwenda kwenye ardhi ya Uislamu kwa ajili ya kukimbia na dini Yake,

¹⁶⁹ kitabu kiitwacho Min Muiin Siirat cha Swalih Shaam juzuu ya 1/153.

¹⁷⁰ Kitabu Taajul Aruus cha Al-zubaidiiy, juzuu ya 3/611

¹⁷¹ Angalia Al- zubaidi kitabu Taajul Aruus juzuu ya 3/611; Abuu Faaris, muhammad Bin Abdul qaadir, Fii Dhwilaalil Siirat" Al-hijrat ila Nabawiyat chapa ya 1, Daarul furqaan, Oman 1402 hijiria.

akitaraji fadhila za Mola wake na akikusudia kuinusuru dini Yake, atapata katika ardhi mahali pa kuelekea ambapo ataneemeka, pawe ni sababu ya yeye kupata nguvu na maadui zake kuwa wanyonge, pamoja na kupata ukunjufu wa riziki na maisha. Na yeyote mwenye kutoka nyumbani kwake kwa lengo la kuinusuru dini ya ALLAH na Mtume Wake, Sala na amani za ALLAH zimshukiye na kulitukuza neno la ALLAH kisha akapatwa na kifo kabla ya kufikia lengo lake, basi malipo ya kitendo chake yameshathibiti kwa ALLAH, kwa fadhila Zake na wema Wake. Na ALLAH ni Mwingi wa msamaha, ni Mwingi wa huruma kwa waja Wake". [Surat Nisaa: 100].

Ama sababu ya kuhama ni kuihifadhi dini na kuitekeleza na kuinusuru na kukusanyika pamoja na Bwana Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na pamoja na maswahaba zake na kujiandaa kwa ajili ya kuieneza dini na kutoa mali na nafsi katika njia ya ALLAH, na kuwa na wepesi kwa waja wake katika kumuabudu ALLAH kwa kusimamisha nidhamu ambayo inaruhusu kufanya hivyo.

Na kwa hakika aliwaamrisha Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- Maswahaba zake katika mji wa Makkah na nje ya Makkah yakuwa wakutane na ndugu zao katika mji wa Madina na kwa hakika kama siyo kutiwa dhiki na Makuraishi wasingetoka wenye kuhama, na kilichofuata ni kuwa Muhaajiriina walitoka katika majumba yao kama anavyosema ALLAH Mtukufu:

﴿لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ﴾ [الحشر: 8]

"Kwa ajili ya mafukara wale ambao walio tolewa kwenye miji yao na mali zao wakitafuta fadhila za ALLAH na kuridhiwa na wakimnusuru Allah na Mtume wake hao ndio wakweli". [Surat Hashir: 8] Kama walivyokuwa Answaar watu wa Madina -Radhi za ALLAH ziwe juu yao- wakiwapenda hawa waliohama wakiwaliwaza

na wakitekeleza haki zao basi akawasifia ALLAH kwa hilo katika maneno yake matukufu:

﴿وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيْمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْتُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ﴾ [الحشر: 9]

"Na wale walio andaa nyumba na imani kabla yao wanawapenda wale walio hamia kwao na hawapati ndani ya vifua vyao mashaka kwa yale waliyo yatoa na wanawapendelea kwa kheri kabla ya nafsi zao hata kama wangelikua wao wanalihitajia na atakaye jizuilia ubadhili wa nafsi basi hao ndio walio faulu". [Suratil Hashir: 9] Na kwa hakika waliotangulia wa mwanzo na waliowanusu walikwenda na malipo makubwa kwa kule kutangulia kwao kuliko wengine, na imeashiria Qur'ani tukufu jambo hilo katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَالسَّبِقُونَ الْأُولُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾ [التوبة: 100]

"Na walio tangulia mwanzo miongoni mwa muhajirina (Waliohama kutoka Makka) na ansvari (waliowapokea Madina) na wale walio wafuatia kwa wema ALLAH amewaridhia na wao wamemridhia, na amewaandalia wao mabustani yapitayo mito pembezoni mwake, wataishi humo milele huko ndiko kufaulu kuliko kuwa kukubwa". [Surat Taubah:100]

Na wakafuatia wengine wenye kuhama na miongoni mwao Bin Umme Maktuum, na Omar Bini Khattwab na Twalha Bin Ubaidillah, na Ammar Bin Yasir na Saad Bin Abii Waqqas na Abdullah Bin masoud, na Bilal Bin Rabaah, na Zaid Bin Haaritha, na Hamza Bin Abdul muttwalib, na Abdulrahman Bin Aafi, na Abu Kabsha na

Ubaida Bin Haarith Bin Abdulmuttwalib, na Al-zubair Bin Al-awwaam na Abuu Hudhaifa Bin Ut-bah Bin Rabiia, na Ut-bah Bin Rabiyyat Bin Az-waan, na Othmaan Bin Affaan -Radhi za Allah ziwe juu yao- na wengineo¹⁷²

Na kwa hakika vyanzo vya habari vilizungumzia nafasi ya hawa waliohama kwa watu wao katika maanswari ambao ALLAH alisema kuhusu wao:

﴿وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْتُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ﴾ [الحشر: 9]

"Na wale walio andaa nyumba na imani kabla yao wanawapenda wale walio hamia kwao na wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa yale waliyo pewa (wahamiaji) na wanawapendelea kheri zaidi ya nafsi zao, hata kama ni wenye kuhitajia, na atakayeepushwa na uchoyo wa nafsi yake hao ndio walio fanikiwa". [Suratil Hashir: 9]

Baadhi ya vijana mabarobaro walikwenda kwa vijana wenzao kama walivyofikia kwa Saad Bin Khaithama Al-answari- Radhi za Allah ziwe juu yake-.

Na kwa hakika watu wa Madina walikuwa wakishindana katika kuwapatia malazi watu wa Makkah waliohama na kuwapa makazi na kuwaliwaza, mpaka wakawa wakipiga kura ya kuwapa makazi wenye kuwafikia katika watu wa Makka waliohama, (295) na Aya zilikuwa zikiteremka kwa Bwana Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- zikiwa

¹⁷² Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/329,331

zinawasifia waliohama na kuwapa ahadi ya kuwanusuru. Anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا ظَلَمُوا لَنُبَوِّئَنَّهُمْ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَلَا نُجْرُ الْأَخِرَةَ أَكْبَرُ
لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾ الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٤٢﴾﴾ [النحل: 41-42]

"Na wale walio hama kwa ajili ya ALLAH baada ya kudhulumwa tutawaandalia duniani mema na malipo ya akhera ni makubwa laiti wangelifahamu". (41) Wale walio subiri na kwa Mola wao wakategemea. (42) [Surat Nahli: 41-42]. Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ هَاجَرُوا مِنْ بَعْدِ مَا فُتِنُوا ثُمَّ جَاهَدُوا وَصَبَرُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ
رَّحِيمٌ ﴿١١٠﴾﴾ [النحل: 110]

"Na hakika Mola wako kwale walio hama baada ya kufanyiwa fitina kisha wakapigana na wakasubiri, hakika Mola wako baada ya hayo ni msamehevu mpole". [Surat Nahli: 110].¹⁷³¹⁷⁴

Na kwa hakika Aya nyingi zimezungumza kuhusu waliohama (Muhajiriina) Radhi za Allah ziwe juu yao.¹⁷⁵

WATU WA SUFA.

Nao ni idadi ya waliohama waliishi katika chumba kwenye msikiti wa bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- walijulikana kwa

¹⁷³ Siirat Nabawiya kitabu cha Twahmaaz kurasa wa 246.

¹⁷⁴ Angalia kitabu cha Siyar Aalaam Nubalaa, juzuu ya 2/21.

¹⁷⁵ Angalia kitabu kiitwacho Hijratu rasul wa swahaaabatihi fil Qur'an wa Sunnah ,chapa ya 1, Daarul wafaai ,Al- Mansoorat.1409 Hijiria .

jina la watu wa Sufa, na walikuwa ni vijana mafukara hawapati chochote cha kula (298) na Mtume ikimjia sadaka anaipoleka kwao (Watu wa Sufa ni wageni wa uislamu hawana ndugu wala mali ilikuwa Mtume akiletewa sadaka anaipoleka kwao na hachukui katika sadaka hiyo chochote, na ikimjia zawadi anawapeleka na huchukua katika zawadi hiyo kiasi na kushirikiana nao katika zawadi hiyo.¹⁷⁶¹⁷⁷

Na alikuwa Mtume akiwapitishia kila siku (pishi la Tende kati ya watu wawili)¹⁷⁸

Na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake akiwataka wenye uwezo miongoni mwa maswahaba kuwalisha watu wa Sufa, na walikuwa Answaar-Radhi za ALLAH ziwe juu yao- wakiwachukua baadhi ya watu wa Sufa na kwenda nao majumbani mwao wakiwalisha na kuwaliwaza: Kwa hakika watu wa Sufa walikuwa ni mafukara na Mtume Sala na amani ziwe juu yake- amesema: "Yeyote atakayekuwa na chakula cha watu wawili basi na aende na mtu wa tatu, na atakayekuwa na chakula cha watu wanne basi na aende na mtu wa tano na wa sita, na hakika Abubakar alichukua watu watatu na Mtume akaondoka na watu kumi"¹⁷⁹

¹⁷⁶ Abu Turaab kitabu Kitiwacho As-habu Suffah chapa ya Daarul Qibla ,Jeddah,1403 Hijiria .

¹⁷⁷ Ameipokea Imamu Ahmad katika Musndai yake juzuu ya /287.

¹⁷⁸ Ameipokea Imamu Ahmad katika Musndai yake juzuu ya /287.

¹⁷⁹ Abu Nuaimu Hiliyatul Auliyaai juzuu ya 2/22-33 Al-suuyaan ,Al-siiat Al- nabawiyat juzuu ya 2/32.

Hawa watu Sufa baadhi yao walikuwa wakibeba mizigo masokoni au wanakata kuni au hufanya chochote ambacho kitachompelekea mtu kupata kitu chochote cha kuuza au kununua kitu kidogo, na shughuli zao hazikua zikiwasaidia, lakini pamoja na hivyo alikuwa mtu akiuza kuni au kitu chochote basi anakuja na chakula kwa jamaa zake.¹⁸⁰

KUHAMA KWA MTUME -REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:

Abubakari Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- na familia yake na mchango wao katika kuhama:

Mtume -Sala na amani ziwe juu yake hakuwa ni Nabii wa kwanza kuhama, kwa hakika alitanguliwa kuhama na nabii Ibrahim -Amani iwe juu yake- amesema ALLAH Mtukufu:

﴿فَقَامَنَ لَهُ لُوطٌ وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّي إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾ [العنكبوت: 26]

"Nabii lutu akamuamini na akasema hakika mimi ni mwenye kuhamia kwenda kwa Mola wangu hakika yeye ni mwenye nguvu mwenye hekima". [Al-ankabuut: 26]. Kama ilivyokuwa uadui wa washirikina na uchochezi wao na kujaribu kwao kumzuia au kumfunga ulikuwa nyuma ya kuhama kwake kwenda Makka, nao ndiyo mji wa ALLAH wenye kupendeza zaidi kwa ALLAH na Mtume wake. Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرٌ الْمَكْرِينِ﴾ [الأنفال: 30]

﴿وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرٌ الْمَكْرِينِ﴾ [الأنفال: 30]

¹⁸⁰ Hilyatul aulyaa kitabu ha Abuu nuaimu juzuu ya 1/348.

"Na pindi walipo kufanyia vitimbi wale walio kufuru ili wakutie uzito au wakuue au wakutoe, wanafanya vitimbi na ALLAH anawafanyia vitimbi na ALLAH ndiye mbora wa wafanyao vitimbi". [suras Anfaal: 30]

﴿وَإِنْ كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا وَإِذًا لَا يَلْبَثُونَ خِلافَكَ إِلَّا قَلِيلًا﴾

[الإسراء: 76]

"Na walitaka kukukera ili wakutoe katika nchi. Na hapo wao wasingelibakia humo ila muda mchache tu". [Alisraa: 76]. Na hapana shaka kuwa watu wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake miongoni mwa makafiri wa kikuraishi walishikamana kumtoa kama alivyoeleza Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kauli yake:

﴿وَكَايْنٍ مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجْتِكَ أَهْلَكَنْتَهُمْ فَلَا ناصِرَ لَهُمْ﴾

[محمد: 13]

"Na ni miji mingapi yenye nguvu kuliko mji wako waliokutoa tuliwaangamiza na hawakupata wa kuwanusuru". [Surat Muhammad:13]. Na inatilia mkazo Aya hii kuhama na kufuatia waliokufuru kumtoa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na nusura ya ALLAH katika kauli yake Mtukufu:

﴿إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِي أَثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَّمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾ [التوبة: 40]

"Na kama hamtomnusuru basi hakika ALLAH amekwisha mnusuru pindi walipo mtoa wale walio kufuru, wakiwa wawili ndani ya pango pindi -Mtume- alipo mwambia jamaa yake-Abubakari- usihuzunike hakika ALLAH yupo pamoja nasi kisha ALLAH akateremsha utulivu na akamtia nguvu kwa askari ambao hamkuwaona, na ALLAH akalifanya neno la walio kufuru kuwa

chini na neno la ALLAH kuwa juu na ALLAH ni mwenye nguvu mwenye hekima". [Surat Taubah: 40]

Kama ambavyo Hadithi zinatilia mkazo kuwa yeye Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- aliondolewa katika mji wa Makkah, na alikuwa akiomba dhidi ya wale waliomtoa katika mji wa Makkah.

Na Mtume Sala na amani ziwe juu yake alikuwa akiipenda Makkah mapenzi ya hali ya juu, hapo Makkah ndipo alipozaliwa na kukulia na kuoja na kuruzukiwa watoto, ukiongezea yale anayoyafahamu Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na wanavyofahamu watu kuhusu utukufu wa Makkah na nafasi yake kwa ALLAH.

Na huenda ushahidi wa jambo hilo ni kauli ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alipoigeukia Makkah wakati wa kuhama kwake. "Namupia ALLAH hakika wewe ni Ardhi ya ALLAH ambayo yapendeza kwangu zaidi na kwa hakika wewe ni Ardhi ya ALLAH ipendezayo kwa ALLAH, na lau kama si watu wako kunitoa nisingelitoka kwako" (303)

Walihama maswahaba wa bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika kipindi kuanzia Uungaji mkono wa Akabah ambao ulitokea katika siku ya kumi na mbili katika mwezi wa Dul-Hijja mwaka (13 Hijiria) tangu kutumwa Mtume, Kuunga mkono kwa mwanzo kulikuwa kabla ya kuhama, na idadi yao ikaongezeka kidogo kidogo, na alikuwa Abubakari -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- amejiandaa kuhama kwa kutekeleza amri ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ya kuandamana naye wakati wa kuhama isipokuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alikuwa akimtaka Abubakari kuwa na uvumilivu katika jambo ambalo analijua ALLAH na Mtume wake na wala Abubakari mwenyewe halijui.

Na alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake akingojea amri kutoka kwa ALLAH Mtukufu na kumpa ruhusa ya kuhama kwa

mpangilio wake -kutakasika na machafu ni kwake- naye ndiye hufanya vitimbi kwa ajili ya Mtume na akimuandalia hilo -Sala na amani ziwe juu yake-.

﴿وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُنْبِتُوا أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٣٠﴾﴾ [الأنفال: 30]

"Na walipo kupanga mpango waliokufuru wakufunge, au wakuue au wakutoe. Na wakapanga mipango yao na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango" [Suratil Anfaal: 30]

Na alikuwa Abubakari Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake- akiandaa mahitaji ya Mtume katika kuhama na hasa hasa vipando atakavyokuwa navyo, kabla ya kujua kuwa yeye ndiye mwenza katika safari ya kuhama.

Na kwa hakika walijitahidi makuraishi kuweka mipango ili kuzuia kuhama Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na wakaweka mipango ya kumuua Mtume Sala na amani ziwe juu yake-

Basi akaja Jibrili -juu yake amani- akasema: "Usilale usiku huu katika kitanda chako ambacho huwa unalala", akasema: Na ulipofikia usiku wenye kiza kinene walikusanyika mlangoni kwake wakimvizia kuwa atalala wakati gani ili wamvamie, na Mtume alipowaona walipokuwa akamwambia Ally Bin Abii Twaalib lala kitandani kwangu na ujifunike kwa shuka langu hili la kijani la hadharami na ulale humo, na wala hutopatwa na maudhi yoyote toka kwao, na alikuwa Mtume akilalia shuka lake hilo wakati wa kulala.

Akasema: Basi akawatokea Mtume -Sala na amani ziwe juu yake na akachukua choto la mchanga katika mkono wake na wao hawamuoni na akawa anawanyunyuzia vichwani mwao na huku akisoma Aya hizi:

﴿يس ١﴾ وَالْقُرْآنِ الْحَكِيمِ ﴿٢﴾ إِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣﴾ عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٤﴾ تَنْزِيلَ الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٥﴾ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أُنذِرَ آبَاؤُهُمْ فَهُمْ غَافِلُونَ ﴿٦﴾ لَقَدْ حَقَّ الْقَوْلُ عَلَىٰ أَكْثَرِهِمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٧﴾ إِنَّا جَعَلْنَا فِيهَا آعْنَاقَهُمْ آعْنَاقًا فَهِيَ إِلَى الْأَذْقَانِ فَهُمْ مُقْمَحُونَ ﴿٨﴾ وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا وَمِنْ خَلْفِهِمْ سَدًّا فَأَعْشَيْنَهُمُ فَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ ﴿٩﴾﴾ [يس: 1-9]

(Yaasin)(1) Na ninaapa kwa hii Qur'ani tukufu (2) Hakika wewe Muhammadi ni miongoni mwa mitume (3) Na upo juu ya njia iliyonyooka (4) Ni uteremsho wa mwenye nguvu mwenye hekima. (5) Ili upate kuwaonya watu yale waliyo shushiwa baba zao na wao walikuwa ni wenye kughafilika. (6) Hakika limethibiti neno kwa wengi katika wao, kwa hiyo hawaamini. (7) Hakika sisi tumeweka vitanzi katika shingo zao navyo vikawafika mpaka kwenye videvu vyao, kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu. (8) Na tunaweka mbele yao kizuizi na nyuma yao kizuizi tukawafunika macho yao; kwa hivyo hawaoni. (9) [Surat Yasiin: 1-9] Mpaka akazimaliza Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- hizi aya zote, na hakubakia yeyote katika wao isipokuwa alimuwekea kichwani mwake udongo kisha akaondoka na kuelekea kule alipopakusudia kwenda, mara akawajia mtu ambaye hakuwa nao, basi akasema: "Mnangojea nini hapa? Wakasema: "Muhammad", akasema: "Amewatia hasara Mwenyezi Mungu, kwa hakika namuapia ALLAH Muhammad amekwisha watoka, kisha hakuna mtu aliyemuacha hivi hivi isipokuwa amemuwekea udongo kichwani mwake, na akaendelea na mambo yake, hivi hamjioni mlivyo? akasema: wakaweka kila mtu mkono wake kichwani akukuta ana udongo, kisha wakawa wakichungulia wanamuona Ally akiwa kitandani amejifunika shuka la bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na wakawa wanasema: hakika huyu ni Muhammad amelala, amejifunika shuka lake na hawajaacha kuwa hivyo mpaka kukakucha akainuka Ally kutoka kitandani -Radhi za Allah ziwe juu yake- wakasema: "Twamuapia ALLAH alikuwa mkweli yule bwana aliyetupa habari. Amesema Bin Is-haqa na ikawa

ndiyo tukio ambalo siku hiyo ilishuka Qur'ani na vile walivyokuwa wamepanga kwa ajili yake, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرٌ الْمَكْرِينَ ﴿30﴾﴾ [الأنفال: 30]

"Na walipo kupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuue au wakutoe. Na wakapanga mipango yao na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango" [Suratil Anfaal: 30] Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ تَتَّبِعُ بِهِ رَيْبَ الْمُنُونِ ﴿30﴾ قُلْ تَرَبَّصُوا فَإِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُرْتَبِصِينَ ﴿31﴾﴾ [الطور: 30-31]

"Au wanasema hao washirikina kuwa yeye ni mshairi, tunangojea ashukiwe na mauti?» (30) Waambie subirini hakika mimi nipo pamoja na wenye kusubiri. (31) [Surat Tuur: 30-31] (304)

Kama alivyokuwa Abubakar -Radhi za Allah ziwe juu yake- ni Rafiki bora wa Mtume katika safari ile, na yalimtokea matukio mbali mbali akawa akijitolea nafsi yake kwa ajili ya Mtume na miongoni mwa mambo hayo ni :

Ni kuwa pale Mtume alipoelekea kwenye pango liliopo kwenye Jabal Thaur ili aingie humo, Abubakari alimtaka angojee kwanza mpaka ahakikishe kufaa kwake na usalama wake kwa ajili ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-

Na wakati wa kukaa kwao hao wawili ghafla wakaona shimo basi Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yake akaliziba kwa mguu wake na akasema: "Ewe Mtume wa ALLAH ikiwa kutakuwa na kung'atwa au kugongwa na nyoka au nge basi inipate mimi" (305)

Alikuwa Radhi za Allah ziwe juu yake- ni mwenye kuogopa na kumuonea huruma Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-

walipokuwa wako pangoni, na katika Hadithi ya Anas aliyoipokea kwa Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yake-amesema Abubakari: nilikuwa na Mtume Sala na amani ziwe juu yake- katika pango nikainua kichwa changu nikajikuta nipo chini ya nyayo za watu nikasema: "Ewe Mtume wa ALLAH lau kama mmoja wao angeinamisha macho yake angetuona", Akasema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-: "Nyamaza ewe Abubakari watu wawili ALLAH ni watatu wao"¹⁸¹

Kwa hakika kutarajia huku na kuogopa na Mtume kuwa na imani na ALLAH, ni kumpa Matumaini Abubakari na kumtuliza. Limetajwa tukio hili kwenye Qur'ani katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ ۗ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾﴾ [التوبة: 40]

"Na kama hamto mnusuru hakika ALLAH amemnusuru pindi walipo mtoa wale walio kufuru hali ya kuwa wakiwa wawili ndani ya pango alipo mwambia rafiki yake usihuzunike hakika ALLAH yupo pamoja nasi kisha ALLAH akateremsha utulivu na jeshi ambalo hamkuliona na akajalia neno la wale walio kufuru kuwa la chini na neno la ALLAH ndilo la juu na ALLAH ni mwenye nguvu mwenye hekima". [Surat Taubah: 40] Ndiyo, aliteremsha ALLAH utulivu wake kwa Mtume wake.

¹⁸¹ Ameipokea Imamu Bukhariy ,mlango wa kuhama kwa Mtume- Rehema na amani ziwe juu yake- na Maswahaba zake kwenda Madinah juzuu 4/263.

Na Abubakari alimuhudumia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- wakiwa njiani.

Na kwa hakika alikuwa Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yake- ni msaidizi wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na alikuwa ni Maarufu sana kwa watu kwa wingi wa kwenda Sham, basi alikuwa akiwazuga wasimjue Mtume -Sala na amani ziwe juu yake. na yeye akiwa ni mwenye kufukuzwa. Amepokea Bin Abii Sheiba kuwa:

Walikuwa mabint wa Abubakari wana mchango mkubwa katika safari ya kuhama, Na imepokelewa kutoka kwa Asmaa -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Niliandaa chakula cha safari cha Mtume katika nyumba ya Abubakari pale alipotaka kuhama kwenda madina, na wala hatukuwa tumepata kamba ya kukifunga chakula chake wala kinywaji chake kamba ya kuvifungia, nikamwambia Abubakari, Namuapia ALLAH sijapata chochote cha kuvifungia vitu hivyo isipokuwa mkanda wa kiuno, anasema: akasema Abubakari upasue vipande viwili na ufunge kwa kipande kimoja kinywaji na kipande cha pili fungia chakula cha safari, na kwa ajili hiyo ndivyo akaitwa mwenye mikanda miwili".¹⁸²

Na kwa hakika Asmaa mwenyewe alipatwa na maudhi kutoka kwa washirikina wa Makkah baada ya kuondoka Mtume na kuhama, anasema Asmaa: "Alipoondoka Mtume walitujia watu katika makuraishi, miongoni mwao alikuwa Abu Jahali Bin Hishaam wakasimama mbele ya mlango wa Abubakari, basi Asmaa akawatokea wakamwambia yupo wapi baba yako ewe Bint ya

¹⁸² Bin Abii sheiba ukurasa wa 144; na ameipokea imamu Bukhari katika kitabu chake sahihi katika mlango wa kuhama kwa Mtume - Rehema na amani ziwe juu yake- na maswahaba wake, juzuu ya 4/258.

Abubakari? Akasema: "Nikasema, nakuapia ALLAH sijui alipo baba yangu" Akasema: Basi Abuu jahali akainua mkono wake na alikuwa mkorofi tena muovu basi akanipiga kofi la shavu, na akaangusha kwa kofi Hereni yangu"¹⁸³

Kama alivyokuwa Abdallah Bin biibakari swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake - akipeleka chakula kwa Mtume na Baba yake kwa nyakati tofauti tofauti na wao wakiwa pangoni,¹⁸⁴kabla ya kuanza kufuata njia ya kwenda Madina, kama ambavyo alikuwa akiwaletea habari.

Kama alivyokuwa Aamir Bin Fuhaira Mtumishi wa swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake -akiwapelekea mbuzi Abubakari swiddiq ili akamue maziwa kutoka katika mbuzi hao, na kwa hakika alifuatana na Mtume na Abubakari swiddiq katika safari yao ya kuhama Makkah kwenda Madinah.¹⁸⁵

ALLY -RADHI ZA MWENYEZI MUNGU ZIWE JUU YAKE- NA KUMLIPIA KWA MTUME REHAMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE NA KUREJESHA KWAKE AMANA ZA WATU.

Na pindi makuraishi waliposhauriana katika usiku wa kuhama Mtume kuwa kitu gani wamfanyie Mtume Sala na amani ziwe juu yake, wakakubaliana kumuwa kwa pamoja, alimfahamisha ALLAH Mtume wake kuhusu mpango huo, na Jibrili akamuamrisha kuwa asilale kitandani kwake, basi Mtume akamuita Ally Bin Abii twaalib - Radhi za Allah ziwe juu yake- na akauamrisha alale kitandani kwake,

¹⁸³ Angalia Bin Hishaam Siirat Nabawiyat juzuu ya 1/487.

¹⁸⁴ Al maghaazi ya Bin Abii Shaibah, ukurasa wa 150.na ameipokea Imamu Bukhari katika sahihi yake juzuu ya 4/256.

¹⁸⁵ Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 137.

na ajifunike Ally kwa shuka lake la kijani -Radhi za Allah ziwe juu yake -na Mtume akawatokea wale watu nao wakiwa mbele ya mlango wake na wala hawakumuona.

Kwa hakika walibakia washirikina wakiilinda nyumba ya Bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na wakawa baadhi yao wakikiona kitanda na Ally Radhi za Allah ziwe juu yake- akiwa amejifunika, basi wakadhani kuwa yeye ndiye Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na wakawa wakisubiri, jambo ambalo lilimpa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake fursa ya kutoka kwenda pangoni pamoja na Abubakari swiddiq- Radhi za Allah ziwe juu yake-¹⁸⁶

Na kazi hii ya kishujaa kutoka kwa Ally -radhi za Allah ziwe juu yake- na kujiandaa kwake kumkomboa bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kazi hii inakuja kuwa ni miongoni mwa kazi tukufu zenye heshima alizozifanya Mtoto wa baba mdogo wake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na pia ni mkwe wake aliyebashiriwa pepo na Mtume na kumuomba kwake, naye ndiye aliyelelewa katika imani kwenye nyumba ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kwa hakika zilichanganyika juhudi za Ally na juhudi za Abubakari na watu wake katika kumhudumia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- wakati wa kuhama, na juhudi hizo zilikuwa ni zenye kukamilishana zenyewe, na wala hakuna kupingana katika hilo nazo zilikuwa ni kukamilishana na kushindana katika mambo ya kheri, na kumpenda bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na kumhudumia na kumlinda.

Na kwa hakika Ally alichelewa kidogo katika kuhama kwa amri ya Mtume ili akabidhi Amana na vitu vya makuraishi vilivyowekezwa

¹⁸⁶ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/482.

kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ikiwepo katika hivyo vitu vya washirikina, na alikuwa Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake- ni katika watu wenye kutekeleza amana na yupo katika nafasi ya kuaminiwa na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- (312) na pia kuaminiwa na waumini na watu wote.

Na Ally alibakia katika mji wa Makkah kwa siku tatu baada ya kuondoka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akatekeleza amana katika siku hizo tatu kisha akaenda kukutana na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- katika mji wa Madinah. (313)

NJIA YA KUELEKEA MADINA [314]

Walikaa Mtume na Abubakari swiddiq katika pango la Hiraa katika mlima Thauri kusini Magharibi mwa mji wa Makkah kinyume na uelekeo wa njia ya kuelekea Madinah, kwa kuzidisha usiri na kujiweka mbali na kutafutwa.

Bila shaka Makuraishi waliweka zawadi inayokadiriwa kiwango chake kuwa Ngamia mia moja kwa atakaye mleta Mtume akiwa hai au amekufa¹⁸⁷ jambo ambalo liliwapa msukumo watu wengi kumtafuta Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kwa juhudi ya hali ya juu katika kila upande na kufuata njia iliyo karibu na Makkah.

Pamoja na washirikina kufika kwenye pambo zaidi ya mara moja, kwa hakika ALLAH alimlinda Mtume wake -Sala na amani ziwe juu yake-

Basi utafutaji na usakaji wa washirikina ulipotulia alitoka Mtume wa ALLAH- Sala na na amani ziwe juu yake- akatoka usiku kutoka

¹⁸⁷ Angalia sahihi Bukhari ,mlango unaohusu kuhama Mtume kwenda Makkah na maswahaba zake juzuu ya 4/256, kitabu cha Akrim Alumariy, swahihu siirat juzuu ya 1/211.

pangoni, akiwa pamoja naye Abubakar swiddiq, na wakakutana na Abdullahi Bin Uraiqitwi muongozaji njia wao akiwa pamoja na vipando viwili, akawapitisha njia iliyopo chini ya mji wa Makkah kisha akawatokezea katika pwani, kisha akapita nao msituni, barabarani na kwenye majangwa ambayo watu hawakuwa wakipita huko wakiwa wanaenda Madinah, (316) ili kuzidi kuwapoteza wenye kuwafukuzia.

Na katika visa mashuhuri katika njia aliyokuwa akipta katika kuhama kwake, ni kisa cha Ummu Maabad mmiliki wa Hema ambalo Mtume -Sala na amani ziwe juu yake alipitia hapo.

Na katika visa mashuhuri vilivyopokelewa wakati Mtume akiwa njiani kuelekea Madinah, ni kisa cha Suraka Bin Maalik -Radhi za Allah ziwe juu yake- kwa upokezi wa Abdurahman Bin Maalik Al-mudlajiy naye ni mtoto wa baba yake mdogo Bin Jaasham kuwa baba yake alimuhadithia kuwa yeye alimsikia Suraaka Bin Jaasham akisema: "Walitujia wajumbe wa makafiri wa kikuraishi wakiweka kwa Mtume Sala na aman ziwe juu yake na Abuubakar zawadi nono kwa kila atakaye wauwa, au kuwateka, na wakati mimi nikiwa nimekaa katika vikao miongoni mwa vikao vya watu wangu wa mudlajiy alitujia mtu tukiwa tumekaa akasema: Ewe Suraka kwa hakika mimi nimeona simba muda mchache uliopita huko ufukweni, nimemuona Muhammad na maswahaba wake, akasema Suraka: nikajua kuwa wao ndiyo wenyewe nikamwambia: hao siyo wao,lakini wewe umewaona fulani na fulani ambao walipotea kwenye macho yetu, kisha nikakaa kwenye kikao kile kama muda wa saa moja hivi kisha nikasimama nikaingia ndani nikamuamrisha kijakazi wangu atoke na farasi wangu aliyekuwa nyuma ya kilima na amfungue mbele yangu, na nikachukua mkuki wangu na nikatoka nao mbele ya nyumba yangu basi nikaweka fimbo yake chini na nikauinamisha upande wake juu, mpaka nikamfikia farasi wangu nikampanda nikamkazanisha ili anifikishe harak,a mpaka nikawakaribia mara akajikwaa farasi wangu nikaanguka

nikatumbukiza mkono wangu kwenye mfuko na kutoa vimishale vya ramli, Basi nikaangalizia kuwa ni wadhuru au nisiwadhuru, likatoka jibu ambalo si zuri, hivyo nikapanda farasi wangu na nikayaasi majibu ya vimishale, farasi akanisogeza karibu mpaka niliposikia kisomo cha Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- na hali ya kuwa hageuki, na Abubakar akigeuka mara kwa mara, ilizama mikono ya farasi wangu katika ardhi mpaka ikafikia kwenye magoti mawili nikaanguka kisha nikamkemea na kuinuka, ilikaribia mikono yake kutokutoka, na alipomaliza kusimama sawasawa ghafla mikono yake ikatifua vumbi lenye kuchomoza kutoka mbinguni kama mfano wa moshi, basi nikatazamia kwa mishale ya Ramli na yakatoka majibu yasiyo mazuri, Basi nikawaita kwa usalama wakasimama nikapanda farasi wangu mpaka nikawafikia na kukazuka katika nafsi yangu nilipopatwa na kilichonipata nacho ni kuzuiliwa kuwakuta, kuwa lifuchuke jambo la Mtume-**rehema na amani ziwe juu yake**-,hivyo nikamwambia Hakika watu wako wameweka Dau kwa ajili yako, na nikawapa habari ya namna watu wanavyotaka kuwafanyia, na nikawatolea chakula cha safari na bidhaa na wala hawakuchukua toka kwangu chochote wala hawakuniuliza isipokuwa waliniambia, tuondokee, basi nikamuomba aniandikie maandishi ya amani, basi akamuamrisha Aamir Bin Fuhaira akaandika kwenye kipande cha ngozi kisha akaenda zake Mtume **-Rehema na amani ziwe juu yake-**.¹⁸⁸

¹⁸⁸ Angalia: riwaya ya Bukhariy katika sahihi yake, mlango unaozungumzia kuhama kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na maswahaba wake juzuu ya 4/256; na Bin Abii Shaibah, Almaghaaziy, ukurasa wa 146.

Na imepokelewa habari inayofahamisha kuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alimpa habari Suraka ya kuanguka ufalme wa Kisra na kuwa yeye atavaa Bangili yake.¹⁸⁹

Na riwaya zinatilia nguvu utekelezaji wa Suraka aliyotakiwa kuyatekeleza na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na hakika yeye aliwageuzia muelekeo mwingine baadhi ya waliokuwa wakimtafuta Mtume na kuwaelekezea sehemu ambayo Mtume hakupita huko.¹⁹⁰

Kwa hakika mwanadamu anashangaa kuja Bishara hii ya Bangili ya kisra katika wakati ambao Mtume -Sala na amani ziwe juu yake amani- alikuwa ni mwenye kufukuzwa na washirikina wakimtaka sawa sawa akiwa hai au amekufa, pale ambapo waliweka zawadi nono kwa atakaye mleta.

Na pamoja na mambo hayo yote bado anamsimulia Suraka kuhusu kufunguliwa Fursi (Irani) miji ya kisra, na kuwa huyu mwarabu atavaaa vazi la Kisra ambalo linamsitiri, basi vipi kwa mchungu ngamia huyu alivae vazi hilo? Na Suraka alikutana na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alipokuwa akirudi toka Hunain na Twaaf katika mji wa Jurana akamtolea na kumuonyesha barua, akasema Mtume Rehema na amani ziwe juu yake-; Leo hii ndiyo siku

¹⁸⁹ Angali kitabu Al-iswaabat cha Bin Hajar juzuu ya 2/19.

¹⁹⁰ Angalia riwaya ya Bukhariy katika sahihi yake, mlango unaozungumzia kuhama kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na maswahaba wake juzuu ya 4/257; na Bin Abii Shaibah, Almaghaaziy, ukurasa wa 146.

ya kulipa wema na kutekeleza ahadi, soge, akasoge karibu na Mtume Sala na amani ziwe juu yake na akasilimu.¹⁹¹

Na kwa hakika kiukweli yalitokea aliyoyasema Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- Basi ukawa ni Muujiza miongoni mwa miujiza ya kiutumbe, na katika utawala wa Omari -Radhi za Allah ziwe juu yake- Ilifunguliwa miji na zikaletwa Ngawira na katika Ngawira hizo kulikuwepo na Bangili ya Kisra na Taji lake na Busati lake na vito vya thamani ya juu.

Anakumbuka Omari -Radhi za Allah ziwe juu yake- ahadi ya Kinabii na akamuita Suraka Bin Maalik na katika msikiti wa Mtume-Sala ana amani ziwe juu yake- na anamvisha bangili ya kisra, na akamwambia: "ALLAH ni mkubwa, Namshukuru ALLAH ambaye amemnyang'anya kisra Bin Hurmuz bangili na akamvisha Suraka Bin Juushum Mwarabu atokanaye na kabila la Banii Mudlajiy"¹⁹²

Na Omar akainua sauti kwa ajili ya bangili hiyo, kisha akapandishwa Suraka na akazungushwa katika masoko ya Madinah na watu wakiwa pembeni mwake, naye akipiga takbira na akirudia Kauli ya Omari, mpaka watu wa Madina wakashuhudia huo muujiza unakuwa kweli baada ya kupita miaka kumi na tano tangu Mtume kutoa ahadi kwa Suraka.

Na katika matukio mengine yaliyotokea wakielekea katika mji wa Madina ni kuwa msafara wa waislamu ulikuwa njiani ukielekea Sham wakiwa pamoja na Zubair Bin Awwam -Radhi za Allah ziwe

¹⁹¹ Dalaailu Nubuwwat juzuu ya 2/489, cha Imamu Baihaqiy na Al-iswaabah, juzuu ya 2/19.

¹⁹² Angalia: Bin Hajar, katika kitabu Al-iswaabah, juzuu ya 2/19, Bin Kathiir, kitabu Bidaaya na Nihaayat, juzuu ya 7/68.

juu yake- walikutana na Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- Zubair -Radhi za Allah ziwe juu- akamvisha Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na pia akamvisha Abubakar Nguo nyeupe.¹⁹³

Kama ilivyopokelewa kuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alipita kwenye Ngamia wa mtu wa kabila la Aslamiy katika sehemu za Juhfa, na kulikuwa na mtoto akichunga akasema hawa Ngamia ni wa nani? Mtoto akasema: ni wa mtu wa kabila la Aslamiy, basi akamgeukia Abubakari na akamwambia: "Umesalimika akipenda ALLAH", kisha akamwambia: jina lako nani? akasema Masoud, akageuka Mtume kwa Abubakari na akamwambia "Umekuwa Bwana kwa mapenzi ya ALLAH". (323) Na alikuwa -Sala na amani ziwe juu yake- akipenda kutoa matumaini mazuri.¹⁹⁴¹⁹⁵

KUFIKA KATIKA MJI WA MADINA.

Iliwafikia Muhaajiriina na Answaar habari ya kutoka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ((Na walikuwa wakiambia jangwani wakimsubiria huko mpaka linawarudisha joto la mchana, na siku moja walirudi baada kusubiri kwa muda mrefu, na walipoingia kwenye majumba yao, alipanda mtu miongoni mwa mayahudi katika kilele miongoni mwa vilelel vyao kwa ajili ya kuangalia jambo fulani, akamuona Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- akiwa na Abubakari wakionekana kama weupe weupe kutokana mangati yatokanayo na joto kali, hivyo Myahudi hakuweza kujimiliki

¹⁹³ Sahihul Bukhari Bin Hajar Fathul Baar, juzuu ya 7/1936.

¹⁹⁴ Siirat An-Nabawiyat, kitabu cha Muhammad Abuu Shuhbat Juzuu ya 1/495.

¹⁹⁵ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Kathiir juzuu ya 2/256.

isipokuwa aliinua sauti yake kwa kusema: Enyi kundi la waarabu huyu hapa Babu yenu ambaye mlikuwa mkimngojea, waislamu wakazikimbilia silaha wakakutana na Mtume wa ALLAH akapita nao upande wa kulia mpaka akafikia kwa watu wa banii Amru Bin Aafi, na hiyo ilikuwa ni siku ya Juma tatu, tarehe nane katika mwezi wa mfungo sita (325) sawa na tarehe 21 mwezi December mwa 622,(326) akasimama Abubakari kwa kuwaheshimu watu na Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akakaa mpaka jua likampata, basi Abubakari akamgeukia na akamfunika kwa shuka lake, basi hapo watu wakamjua kwa hilo Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-¹⁹⁶Na baadhi ya riwaya zimetaja kuwa wale waliompokea Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- wakati anaingia mji wa Madina walikuwa idadi ya Answar ni Mia tano (328) na kwa upande mwingine waliohudhuria upande wa Qubaa baada ya kufika Bwana Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- ili wampokee huenda idadi yao ikawa ni ile ile au inakaribiana na ile, pamoja na idadi nyingine ya waliokuwa wakihama huenda idadi yao haipungui mia moja, kama riwaya zinavyotufahamisha, na walimuunga mkono watu wa Makkah (Waliohama pamoja naye) na wakati huo wakitarajia hatari na vitisho ambavyo vilikuwa vikimzunguka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kutoka kwa maadui wake, na kilichofuata ni kuwa wao walikuwa wapo tayari kumhami na kumtii na kujitoa kwa ajili yake,na kwa hakika Answaar walimuunga mkono mara nyingine baada ya kufika Madina, kama inavyotoa habari

¹⁹⁶ Angalia Riwaya ya Imamu bukhari katika sahihi yake,mlango Unaohusu vita ,mlango unaohusu kuhama kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na maswahaba zake kuelekea Madina ,juzuu a 4/258.

Riwaya ya Imamu Bukhariy kutoka kwa Bin Umar -Radhi za Allah ziwe juu yake-¹⁹⁷¹⁹⁸

Na katika Riwaya nyingine kutoka kwa Anas Bin Maalik katika sahihi Bukhari riwaya iliyo bora zaidi katika jambo hili amesema: "Alipofika Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-katika mji wa Madinah alifikia upande wa juu ya mji wa Madina katika kijiji wakiitacho banii Amru Bin Aufi, akasema: akakaa hapo masiku kumi na Nne, kisha akatuma ujumbe kwa watu wakabila la Banii Najjar, akasema, wakaja wakiwa wameweka panga zao kwenye mabega yao, akasema: kana kwamba mimi namuangalia Mtume wa ALLAH akiwa kwenye kipando chake na Abubakari akiwa nyuma yake (wamepakizana) na umati wa kabila la Banii Najjar wamemzunguka pambizoni mwake"¹⁹⁹

Na mahala pa kufikia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika maeneo ya Qubaa ilikuwa ni kwa Kulthuum Bin Al-Hadam miongoni mwa Banii Umar Bin Aufiy na kwa Saad Bin Khaithama, na alikuwa akiwapokea watu katika nyumba ya Saad, nayo ni sehemu ya makazi ya idadi kubwa ya vijana waliohamia Madina²⁰⁰

¹⁹⁷ Angalia kitabu cha Tarmaniin, Azmat Taarikh al-islamiy, ukurasa wa 11.

¹⁹⁸ kutoka katika Riwaya ya Imamu Bukhar, mlango wa kuhama Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-na maswahaba wake juzuu 4/258; na tamko ni lake. na angalia Bin Hishaam siirat ya Mtume juzuu ya 1/343.

¹⁹⁹ Kutoka Riwaya ya Imamu Bukhariy Hadithi namba 3932.

²⁰⁰ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/343.

Na kwa hakika kufika kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-sehemu ya Qubaa katika mji wa Madina ni siku nyeti na maaalumu ambayo waliifanya waislamu ndiyo mwanzo wa tarehe ya Hijiria (kalenda ya kiislamu) ya kuhama kwa namna walivyokuwa wakiuona umuhimu wake.²⁰¹

Na imepokelewa kutajwa kwa siku hii ikifungamanishwa na mazungumzo kuhusu kuujenga msikiti wa Qubaa katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿لَا تَقُمْ فِيهِ أَبَدًا لَمَسْجِدٍ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَىٰ مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَنْ تَقُومَ فِيهِ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَنْ يَتَطَهَّرُوا وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُطَهَّرِينَ﴾ [التوبة: 108]

"Usisimame, ewe Nabii, kuswali katika msikiti huo kabisa. Kwani msikiti uliojengwa kwa misingi ya uchamungu kuanzia siku ya mwanzo, nao ni msikiti wa Qubā', unafaa zaidi kwa wewe kusimama humo kwa kuswali. Kwani katika msikiti huu kuna watu wanapenda kujisafisha na najisi na uchafu kwa maji, kama wanavyojisafisha kwa kujiepusha na mambo yanayopelekea kufanya mambo yaliyoharamishwa na kuomba msamaha kutokana na madhambi na maasia. Na ALLAH Anawapenda wenye kujisafisha". Na iwapo msikiti wa Qubā' ulijengwa juu ya misingi ya uchaji-Mungu, basi Msikiti wa Mtume wa ALLAH, rehema ya ALLAH na amani zimshukie, ni kama hivyo kwa njia ya ubora zaidi na ustahiki zaidi. [Attauba: 108]

kwa hakika hiyo ilikuwa ni ishara ya hiyo siku yenyewe, na huenda hiyo ndiyo ikawa sababu ya waislamu kuifanya ndiyo tarehe

²⁰¹ Angalia Omar Bin Shaiba Historia ya Madina juzuu ya 2/758. Angalia Mlango wa Historia kuanzia walianza kuweka tarehe, kwa Bukhari katika sahihi yake juzuu 4/67.

ya Hijiriya, pale walipotaja kuwa Qur'ani tukufu imeashiria hii siku yenyewe, na hivyo wakaona waifanye ndiyo siku ya kuanza tarehe ya Hijiriya, na wakaipa nguvu siku hii kuliko masiku mengine yaliyokuja kwenye riwaya, kama alivyosema Omari: Kuhama kumetenganisha kati ya haki na batili, hivyo basi iwekeeni hiyo Hijra tarehe²⁰²na kwa hivyo waliona maswahaba kuwa siku hiyo ndiyo siku ya kwanza ambayo uislamu ulipata nguvu .

Alibakia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- masiku kumi na Nne (334) alifanya baadhi ya kazi, ilikuwa kazi muhimu aliyofanya hapo ni kujenga msikiti wa Qubah -kama tulivyokwisha taja, nao ni msikiti wa kwanza uliojengwa katika uislamu, alishiriki katika kuujenga Mtume Sala na amani ziwe juu yake- yeye mwenyewe, na hakuna shaka kuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- aliwasalisha waislamu humo na alikuwa akihimiza kusali humo na akasema: "Kusali sala moja katika msikiti wa Qubah ni sawa na kufanya Umra" .²⁰³²⁰⁴

Na wala haimaanishi huku kufungamanishwa msikiti wa Qubaa na hii Aya kuwa wenyewe ni bora kuliko msikiti wa Mtume -Sala na

²⁰² Sahihi Bukhari, Mlango unaohusu tarehe kuanzia wapi walianzia kuweka tarehe katika kitabu kinachozungumzia Fadhila za Answaar juzuu ya 4/267, angailia kitabu Bidaayat wanihaayatjuzuu ya 2/253, naUmarBin Shaibat Historia ya Madina,juzuu ya 2/758.

²⁰³ Kutoka Riwaya ya Bukhariy,katika mlango unaohusu kufika kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na maswahaba wake katika mji wa Madina, juzuu ya 4/466.

²⁰⁴ wamekubaliana Bukhari na Muslim, angalia Tafsiri ya Bin Kathiir juzuu ya 1/908.

amani ziwe juu yake-,kwani yote miwili imeanzishwa kwa misingi ya uchamungu, na msikiti wa Qubaa ndiyo uliokusudiwa katika Aya hii, na sifa za wenye kujitwaharisha katika hadithi nyingi zinawahusu watu wa Qubah miongoni mwa Answaar na wao walikuwa wakifuatishia mawe kwa maji baada ya kujitwaharisha .(336).

Na kwa hakika aliswali Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-Ijumaa ya kwanza katika kijiji cha kabila la banii Saalim Bin Aufiy kabla ya kufika kwake Madina na ikawa ndiyo Ijumaa ya kwanza (337) na mpaka sasa msikiti huo haujaacha kuwa ni mashuhuri katika mji wa Madina nao ni miongoni mwa alama zake kuu²⁰⁵²⁰⁶

Hawakuwa tu peke yao Banuu Najjaar katika msafara bali na ulinzi na kudhihirisha nguvu pamoja na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-, bali Answare wote waliobaki na Muhaajiriina walikuwa kwenye maandamano makubwa, ambayo yalivuka idadi yake watu mia tano.(339)

Ilikuwa kufika kwa Mtume Madina ndiyo mwanzo wa kupata utulivu kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na waliokuwa naye miongoni mwa muhaajiriina ,na mwanzo wa furaha na kupata nuru watu wake ambao nyumba zao nyingi waliingia katika uislamu, na kwa hakika walitoka watu wa Madina mpaka vijakazi walikuwa juu ya nyumba wakionyeshana wakisema ni yupi kati yao ni

²⁰⁵ Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 1/493 na Siirat Nabawiyat ,juzuu 2/271.

²⁰⁶ Angalia: Abdul aziiz Kaa'ak, mkusanyiko wa picha za Alama mashuhuri za Madinatul Munawwara juzuu ya 1/148.

Muhammad? na hawajawahi kuona mandhari inayo fanana naye kwa uzuri.

Na walitoka Mabinti wa banii Najjar wakimkaribisha Mtume wa ALLAH wakirudia rudia kusema:

Sisi ni Mabinti wa Banii Najjaari.

Twatamani ikiwezekana Muhammad awe jirani.

Na imepokelewa kuwa yeye alisema kuwaambia Je mnanipenda: Wakasema: "Ndiyo Twaapa kwa jina la ALLAH akasema: "Na mimi namuapia ALLAH kuwa nawapendeni".(340)

Hakika huo ni wema wa hakika na mapenzi ya kweli kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- mapenzi kutoka kwa watu wa Madina wakubwa na wadogo, walidhihirisha furaha yao alipofika Madina akiwa njiani na kwenye majumba na walidhihirisha furaha watoto na watumishi. (Walikuwa wakisema Allahu Akbar- ALLAH ni mkubwa amekuja Mtume wa ALLAH, Allahu Akbar amekuja Mtume wa ALLAH (341)

Na katika riwaya imepokelewa kuwa alipoingia Mtume wa Mwenyezi Mungu- katika mji wa Madina walipanda wanaume na wanawake juu ya nyumba na watoto na watumishi wakatawanyika barabarani wakiita "Ewe Muhammad Ewe Mtume wa ALLAH, Ewe Muhammad Ewe Mtume wa ALLAH" (342) na baadhi yao walikuwa wakirudia rudia: ((Amekuja Mtume wa ALLAH, Amekuja Mtume wa ALLAH)) (343)

Na kwa hakika Baraa Bin Aazib alishuhudia- naye ni mtoto wa watu wa Madina- kuingia kwa Mtume katika mji wa Madina na akanukuu hisia za watu wa Madina kwa kusema maneno yake: "Sijapata kuona watu wa Madina wamefurahia jambo kuliko walivyofurahia kuja kwa Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- (244) na wakati wa kuingia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika

mji wa Madina walishindana Answaari watu wa Madina kumkaribisha Mtume na kutaka kila mmoja afikie makwao, kila mmoja anataka utukufu wa kufikia Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kwake, hivyo basi wakawa wanamsimamisha na wanamtaka afikie kwao na kila mmoja anadhihirisha utashi wake na uwezo wake kwenye kumkirimu na kumlinda na wanasema: Njoo palipo na maandalizi na Silaha na ulinzi, akitaka kila mmoja wao kuchukua Hatamu ya Ngamia wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- basi naye huwaambia "Muacheni Ngamia huyo kwani yeye ameamrisha", na akazunguka Ngamia mara kadhaa mpaka mwisho akapiga magoti sehemu ya msikiti wake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na ilikuwa ni sehemu ya kukusanyikia Ngamia nyuma ya nyumba, na ni ardhi ya vijana wawili wa kabila la Bani Najjar, na walikuwa baadhi ya Maswahaba wakisali hapo kabla ya kufika kwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- (345).

Na kwa wingi wa wenye kupenda kumkaribisha Mtume Sala na amani ziwe juu yake- Basi alijikuta akiwa katika wakati mgumu kwani alipenda kuwafurahisha wote, na wakati huo huo akiwa na mapenzi makubwa ya kufikia kwa watu kabila la banii Najjar nao ni Wajomba wa Babu yake ambaye ni Abdul Muttalib.

Mara ghafla akatokea Abuu ayub Al-Answaariy -Radhi za Allah ziwe juu yake- akitajihidi na kufanya bidii kubeba mizigo ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kutoka kwenye Ngamia wake na kuviingiza nyumbani kwake, na anasema Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**:- "Mtu huambatana na mizigo yake"²⁰⁷

²⁰⁷ Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 1/491 na Siirat Nabawiyat, juzuu 2/273.

Na akaondoka Abuu Ayoub Al-Answariy -Radhi za Allah ziwe juu yake- na utukufu wa kumkaribisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- (347)

MADINA NA WAKAZI WAKE:

Mji wa Madina katika zama kabla ya uislamu ulikuwa ukijulikana kwa waarabu kwa jina la (Yathriba).²⁰⁸na umetajwa katika Qur'ani tukufu kwa jina hili, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِذْ قَالَتْ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوا وَيَسْتَأْذِنُ فَرِيقٌ مِّنْهُمُ النَّبِيَّ يَقُولُونَ إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ إِن يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا﴾ [الأحزاب: 13]

"Na pindi lilipo sema kundi miongoni mwao enyi watu wa Yathriba (Madina) hamna makazi basi rudini na kuna kundi miongoni mwao linamtaka idhini nabii wanasema hakika nyumba zetu zipo tupu na hali ya kuwa hazipo tupu hawana wanacho kitaka isipokuwa ni kukimbia". [Suratul Ahzaab: 13]

Na alipokuja Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina alibadilisha jina lake ili uitwe mji wa Madina, na limekuja jina hilo katika Qur'ani mara Nne.

Na mji wa Madina una majina tofauti tofauti nayo ni Twaibah, na Twaabah na Mubaaraka Al-mushrifat, na Daarul hijra. Na kumetungwa vita vingi maalumu kwa ajili ya Madina na kuhusu yaliyotokea humo na Fadhila za mji huo²⁰⁹

²⁰⁸ Angalia upekuzi mrefu kuhusu maudhui hii kwa Bin Kathiir katika Tafsiri yake juzuu ya 1/908.

²⁰⁹ Angalia: hadithi zilizopokelewa kuhusu fadhila za Mji wa Madina hadithi zilizo kusanywa na kufanyiwa uchunguzi na dokta Swalehe Bin Haamid Al-rifaay, kutoka katika kituo cha kuhudumia Sunna

Na kwa hakika Madina ilipata utukufu kwa kuhamia Mtume hapo na kuiombea Dua, na miongoni mwa dua hizo ni maneno yake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**" "Ewe Mola wetu wa haki Tupendezeshee mji wa Madina kama tunavyoupenda mji wa Makkah au zaidi"²¹⁰

Na maneno yake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake: "Ewe Mola wetu wa haki tupe baraka katika matunda yetu na baraka katika mji wetu wa Madina na utupe baraka kwenye vipimo vyetu na kwenye viwango vyetu, Ewe Mola wetu wa haki hakika Ibrahim ni mja wako na ni kipenzi chako na ni mtume wako na mimi ni mja wako na ni mtume wako, na kwa hakika yeye alikuomba kwa ajili ya Makkah na mimi nakuomba kwa ajili ya Madina kama alivyokuomba kwa ajili ya Makka na mfano wake pamoja naye"²¹¹Na kwa hakika Mtume aliupenda mji wa Madina na akauwekea utukufu na ulinzi, na amepokea Bukhari kutoka kwa Anas Bin Maalik -Radhi za Allah ziwe juu yake- kuwa Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- Amesema: "Mji wa Madina kumeharamishwa kutoka sehemu fulani mpaka sehemu fulani, sehemu hizo hakukatwi miti yake wala haifai kuzusha uzushi wowote, na yeyote atakaye zusha humo uzushi wowote, atapata laana ya ALLAH na Malaika na watu wote".²¹²

kwenye chuo kikuu cha kiislamu kilichopo Madina, chapa ya 1, mwaka 1413 H.

²¹⁰ Al-Bukhariy katika kitabu cha Fadhila za Madina,juzuu ya 2/220.

²¹¹ Muslim kitabu cha Hijja,Fadhila za Madinah,juzuu ya 2/10

²¹² Swahihu Bukhariy, kitabu cha Fadhila za mji wa Madina,Hadithi Namba 1867.

Ulijivunia mji wa Madina sifa ya kuitwa mji mkuu wa Dola ya Kiislamu tangu alipoishi hapo Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na ukaendelea kuitwa hivyo mpaka wakati wa Makhalfi wake waongofu, na ukawa ni katika miji mitukufu yenye athari katika ulimwengu wote kuanzia wakati huo na baada ya hapo.

Na wanaweka kabila la Ausi na Khazraji mkusanyiko wa makazi yanayotengeneza matumbo ya makabila haya.²¹³

Na amani inatawala katika makabila haya mawili, kama ambavyo kuna kuoleana kati yao, isipokuwa kulikuwa na vita kati yao wakati mwingine, kama vile vita vya siku ya Buaath vita, iliyokuwa mashuhuri.²¹⁴

Kama ilivyo miongoni mwa vipengele muhimu vya makazi katika mji wa Madina yenye nuru pindi alipofika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ni mkusanyiko wa mkabila ya kiyahudi, na wala haikupungua nguvu na ushawishi kwa makabila ya Ausi na Khazraji.²¹⁵

Na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akiamiliana pamoja kuwepo hali hii kwa njia zilizokuwa bora zaidi ili apate matokeo mazuri na ili aanzishe kwa ajili ya jamii mji wenye amani itakayoenea kwa wote wenye kutaka maisha yenye utukufu, kama

²¹³ Al- nuwairiy, Nihaayatil Arab fii Funuunil Adab, juzuu ya 1/311.

²¹⁴ Swahihul Bukhariy, mlango wa kfika kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na maswahaba wake, juzuu ya 4/265.

²¹⁵ Angalia kitabu kiitwacho majibizano katika Historia ya Mtume, kitabu cha Al-hamdu, Muhammad Ibrahiim ,chapa ya wizara ya waqfu nchini Kuwait, ukurasa 187.

ambavyo alifanya mshikamano wa kiitikadi kati ya waislamu kuwa ni msingi wa kuaminiana, na katika wakati huo huo, alitanua kiunganishi cha kuishi pamoja kwa amani pamoja na wakazi wakiwemo ndani yake mayahudi, jambo ambalo lilijulikana baada ya hapo kwa jina la (Mkataba wa Madina).²¹⁶

Na alikaa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika nyumba ya Abuu ayoub Al- answaariy mpaka akajenga msikiti wake na vyumba vyake -Sala na amani ziwe juu yake.

Na kwa hakika Abuu Ayoub alijipatia ufahahari huu mtukufu na kubakia nao mpaka siku ya kiama, na walikuwa maswahaba -Radhi za Allah ziwe juu yao- wakimuonea wivu kwa hilo pale ambapo ilikuwa nyumba yake ndiyo makazi ya Mtume ALLAH- na ndiyo sehemu ya kuteremkia wahyi na ndiyo makutano ya waumini kukutana na mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu kwa miezi kadhaa.

Kwa hakika ukarimu aliopewa Mtume kutoka kwa Abuu Ayoub na watu wa Madina -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- na waliohama kutoka Makka kwenda Madina pamoja naye, jambo hilo lilikuwa ni Rehema kutoka kwa ALLAH, na ni mbadala kwa yale waliomfanyia washirikina wa Makka ikiwepo kuwafukuza watu wa Makka na kuzitawala nyumba zao na amali zao katika mji wa Makka, hawa hapa sasa watu wa Madina wanampokea Mtume na waliokuwa naye kwa namna nzuri na wanawaliwaza, na huu hapa Umma

²¹⁶ Al-shaabiy. Ahmad Qaaid, mkataba wa Madina wenye dhamana na muongozo, kitabu cha umma ni idadi toleo namba 110. toka wizara ya Waqfu, Doha, mwaka 1426 hijiria ukurasa wa 29.

mzima unamsifia Abuu Ayoub Al-Answaariy mpaka siku ya kياما kwa kumkirimu kwake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake.²¹⁷

KUJENGWA KWA MSIKITI WA MTUME:

Miongoni mwa kazi za mwanzo alizozifanya Mtume-Sala na mani ziwe juu yake- pindi alipofika Madina, ni kuweka mpaka wa sehemu ya msikiti wake, Na alipiga magoti Ngamia wake aliyeheshimiwa mbele ya sehemu ya msikiti wake -Sala na mani ziwe juu yake-(358) (pale ambapo walikuwa wakiswalia watu miongoni mwa waislamu na ilikuwa ni Ardhi ya kukaushia tende, ikiwa ni miliki ya Suhail na Sahli ambao walikuwa watoto wawili mayatima waliokuwa chini ya uangalizi wa As-ad Bin Zuraarat, akasema Mtume -Sala na mani ziwe juu yake-: "Alipopiga Ngamia huyu magoti hapo kwa mapenzi ya ALLAH ndiyo mafikio", kisha Mtume akawaita vijana wawili na akajadiliana nao kuhusu kiwanja cha kuanikia tende, ili akifanye kuwa Msikiti basi vijana hao wakasema: Bali sisi tunakupa bure wewe, basi Mtume akakataa-Sala na amani ziwe juu yake- kukichua bure kutoka kwao wawili hao mpaka akakinunua kisha akajenga msikiti.²¹⁸²¹⁹

²¹⁷ Angalia Bin Saad, Siirat ya Mtume, kutoka katika kitabu Twabaqaatul Kubraa juzuu ya 1/237, Bin Hajar Kitabu Kiiwachochi Al-iswaabah juzuu ya 1/402, Al-dhahabiy, Siiyar Aalaam An-nubalaa, juzuu ya 2/402.

²¹⁸ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad JUZUU1/237.

²¹⁹ Angalia Riwaya ya Imamu bukhari katika sahihi yake, mlango Unaohusu vita, mlango unaohusu kuhama kwa Mtume- Sala na amani ziwe juu yake-na maswahaba zake kuelekea Madina, juzuu a 4/254.

Na kwa hakika ilikuwa ni matarajio ya Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- kupata msikiti ambao ataabudiwa Mwenyezi Mungu humo yeye peke yake hana mshirika wake (360) na wala asichukue chochote kutoka kwa hawa mayatima wala mali kutoka kwa mtu yeyote, licha ya kuwa Mtume anachukua zawadi na vya kupewa bure lakini yeye mahala hapa hakukubali, bali Mtume aliamrisha kutolewa gharama katika mali yake na akawapa thamani ya sehemu ile, na huzingatiwa msikiti huu kuwa ndiyo Waqfu ya kwanza katika uislamu, na muweka Waqfu ni yeye Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-

Ilikuwa kazi ya kwanza aliyoifanya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-ni kuchagua sehemu ya msikiti wake, na jengo la kwanza katika kazi zake Mtume na watu wa Makka na Madina pamoja naye ni jengo la msikiti wa Qubaa katika njia ya Mtume ielekeayo Madina, kisha ujenzi wa msikiti wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina, na kwa hakika ulijengwa Msikiti wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- wakati wa Mtume mara mbili, mara ya kwanza ni katika mwaka wa kwanza tangu kuhama, haraka aliujenga alipofika Madina, na mara nyingine ni katika mwaka wa saba tangu kuhamia Madina, na lilikuwa jengo la kwanza ni dogo kuliko la pili kwa ukubwa, na kwa upande wa ubora wa jengo, na aliamrisha Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuisawazisha ardhi mpaka iwe yafaa kujenga, na alishiriki Mtume mwenyewe katika kuujenga msikiti na alikuwa akiimba pamoja na maswahaba wakati wakijenga na maswahaba wakiwa wanashirikiana naye katika ujenzi, na kakifanya Mtume Kibla chake msikiti huo ni Baitil maqdis (Jerusalem) katika ujenzi huu wa kwanza ambao ulijengwa kabla ya kugeuzwa kibla kuelekea Makka.

Na kwa hakika msikiti ulirudiwa kujengwa tena pamoja na kuupanua kidogo baada ya vita vya Khaibar.²²⁰

Na bado mipaka ya msikiti wa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-inajulikana na imewekewa alama za rangi ya kijani na zimeandikwa alama hizo na namna iliyokuwa wazi, mwenye kutembelea msikiti wa Mtume anaweza kuziona alama hizo na kuyasoma yaliyoandikwa katika alama hizo.

KUUNGA UDUGU [362]

Na alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akipupia kuweka mshikamano maalumu kati ya waislamu, wakiliwazana wao kwa wao na wakipeana badala wao kwa wao katika mali walizopoteza na wake na jamaa, hali ya kuwa ni matokeo chanya ya kuhama kwake au kusilimu kwake, na kwa hilo imepokelewa kuwa uungaji udugu wa kwanza ulikuwa Makka kabla ya kuhama Mtume kati ya idadi kubwa ya waislamu, miongoni mwao ni Omar na Abuubakar na Twalha Bin Ubaidillah na Zubair Bin Awwam na Abdulrahman Bin Aufiy na Othman Bin Affan na kuwa Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake- alimwambia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- wakati huo akiwa Makka: "Ewe Mtume wa ALLAH kwa hakika wewe umewaunganisha kati ya maswahaba wako basi ni nani ndugu yangu?", Akasema: "Mimi ni ndugu yako"²²¹

²²⁰ Siirat Nabawiyat Bin Kathiir juzuu ya 3/345,Al- waaqidiy,Alghaaz, juzuu 2/636.

²²¹ Angalia Muhammad Abuu shaiba Siirat Nabawiyat juzuu ya 5/52Al-balaaziriy .Nasaba za masharifu,juzuu ya 1/240,na kupanua zaidi elimu rejea kitabu cha Siirat Nabawiyat swahihi cha Doctor Akrim Dhwiyaahu Ulumariy juzuu ya 1/240.)

Na walipotulia waislamu katika mji wa Madina baada ya muda mfupi tangu kuhama Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- aliunganisha kuwa ndugu kati ya Answaar na Muhaajiriina, na wapokezi wamelitaja hilo kwa kila swahaba na yule aliyemuunganisha Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-** pamoja naye, na uungwaji undugu ulikuwa kwa kawaida ni kati ya Answaar na Muhaajiriina²²² Na palipatikana baadhi ya hali katika kuwaunganisha baina ya Answaar na Muhaajiriina, na baadhi ya Muhaajiriina na wengine ,na huenda jambo hili lilikuja katika hatua za mwishoni au kwa ajili ya hali fulani, isipokuwa kihakika kuunganishwa kulikuwa ni kati ya Muhaajiriina na Answaar.

Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kumingilia Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake-:

Ilikuwa kwa wake za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kumchagua Mtume ni huruma kwake na kwa umma mzima, na alikuwa Khadija -Radhi za Allah ziwe juu yake- ni mkubwa kiumri kuliko Mtume, katika wakati ambao alikuwa na haja ya kufanya hivyo, mpaka pale ulipoteremka wahyi kwake Mtume alikuwa Khadija ni msaidizi wake katika wakati ambao alikuwa na haja ya kusaidiwa, alimwamini Mtume na akamliwaza na akamsaidia, na akamuashiria kwa kumpa Rai zenye hekima na nyingi ya rai hizo zilikuwa ni msaada kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake, na hapana shaka kuwa huku ni kumtilia umuhimu ALLAH Mtume wake Sala na amani ziwe juu yake

²²² Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 1/505.

Ama Aisha -Radhi za ALLAH ziwe juu yake -alikuwa ndiye mwanamke pekee aliyekuwa Bikra katika wanawake wote wa Mtume, na alikuwa ndiye mdogo wa wote kiumri na ndiye aliyekuwa amehifahi zaidi, ALLAH kwa ajili ya Mtume wake na akamuamrisha Aisha pamoja na wanawake wengine miongoni mwa Mama wa Kiislamu jambo kubwa, na jambo lenyewe ni kuihifadhi sheria itokayo kwa Mtume wake na kuufikishia Umma, Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَأَذْكُرَنَّ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَالْحِكْمَةِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا﴾
[الأحزاب: 34]

"Na watajieni watu yasomwayo kwenye majumba yenu katika Aya za ALLAH na hekima, hakika ALLAH ni mpole na ni mjuzi wa mambo ya siri na ya Dhahiri" [Ahzab: 34]

Na ilikuwa kuchumbiwa kwa Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake-baada ya kufariki Bibi Khadija kwa muda mchache.

Na ilikuwa ndoa ya Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-ni katika mwezi wa Shawwal katika mwaka wa kumi tangu kupewa utume, na wala hakumingilia isipokuwa katika mwezi wa shawwali katika mwaka wa kwanza tangu kuhama, (365) na inasemekana kuwa ilikuwa baada ya hapo.

Na kutokana na udogo wake Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake-ulikuwa na mchango mkubwa wa kuendana tabia yake Mtume Sala na amani ziwe juu yake, na malezi yake kwake na pande nyingi, mpaka ikawa yeye Mtume akapendelea Aisha amuuguze katika maradhi ambayo Mtume alikufa kwa maradhi hayo, alipendelea kubaki kwa Aisha mpaka akafariki akiwa kwenye mapaja yake-Radhi za Allah ziwe juu yake- (366)

Alikuwa anahifadhi na kuifahamu zaidi elimu itokayo kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuliko yeyote- -Radhi za Allah

ziwe juu yake- na umri wake ukawa mrefu mpaka akawa amefundisha sunna za Mtume mataifa mengi katika Umma wakiwemo wanaume na wanawake.

Na alikuwa mwenye kupendwa zaidi katika wake zake, na wala hakujaaliwa kupata mtoto, aliitwa Mama Abdallah kwa jina la mtoto wa Dada yake Abullahi Bin Zubair -Radhi za Allah ziwe juu yake- na kwa kuwa yeye ni Bint wa Abuubakar -Radhi za Allah ziwe juu yake- alimpa ruhusa ya kuchukua kutoka kwa Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- na kuchukua kutoka kwa baba yake -Radhi za Allah ziwe juu yake- kwa wakati mmoja, kama vile ambavyo alimpa fursa ya kukutana na Abubakari na Mtume wa ALLAH katika nyumba yake Aisha na mbele yake na katika safari.

Na kama inavyofahamika kuwa Aisha, bali siyo yeye tu na familia ya Abuubakar swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- walipata utukufu kutokana na nasaba hii kama ambavyo yeye Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- (Alikuwa ni mke wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake hapa duniani na pia Akhera, kama ilivyopokelewa katika Hadithi Tukufu) (367)

KUUKUZA MJI WA MADINA NA JAMII YAKE.

Ulikuwa Uislamu katika jamii ya wanadamu ili uwapendezeshee kwa kumtii ALLAH na kumpwekesha kwanza, na ili kuunyanyua kwenye ngazi ya utukufu wake, na kuitukuza Nidhamu, na kuinua uzalishaji na kuyalinda mazingira na Ardhi kutokana na ufisadi, na kuujenga mji wa Madina kwa yanayofaa kibinaadaamu, na ukawa mji wa Madina ni mfano wa kuigwa kwa jambo hili, pale ambapo Mtume aliupanga mji kwa kuweka sheria mbali mbali na kuweka mpango kazi na utekelezaji kwa ngazi ya manispaa, jambo ambalo liliwafanya watu wote wakishindana katika uzalishaji na kuingiza kipato, badala ya kupata hasara na kuwategemea watu wengine jambo ambalo lilikuwa wazi kwa watu wa Madina, Madina ambayo

ilikuwa na kubadilika hali yake baada tukio la kuhama la kiutume lenye baraka.

Na mwanzo kulianzwa na vitu vya kinadharia ya akili vyenye umuhimu mkubwa, na jambo la kwanza ilikuwa:

Ni kubadilisha jina la mji wa Madina:

Mji wa Madina Ulijulikana kwa Waarabu kabla ya uislamu kwa jina la (Yathriba) maana yake Ubaya au Lawama.

Na kwa hakika alilichukia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- jina hili na akaamrisha libadilishwe na kuitwa Madina²²³ na ilivyo maarufu ni kuwa jina hilo lenyewe lina maana ya utamaduni na maendeleo na utulivu na chenye kufuatia miongoni mwa Elimu na Kazi na Nidhamu na uadilifu na mengineyo yanayo ambatana na Madina. Na hakika Mtume aliuita mji wa Madina kwa majina mengine mfano Twaabah, na Twaibah, na Al-mubaaraka, na Daarul Iman, na Ngome, na majina yote hayo yanapelekea kwenye matumaini na mtazamo mzuri na uzuri wa jina.(369)²²⁴

Kuupenda mji wa Madina na kuuwekea mipaka ya utukufu:

Alipupia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- juu ya kuweka mipaka ya utukufu wa Mji wa Madina, na akaweka mipaka na akauombea mji wa Madina -Sala na amani ziwe juu yake- kama ilivyopokelewa kutoka kwa Imam Bukhariy kwenye sahihi yake kuwa yeye -Sala na amani ziwe juu yake Amesema: "Hakika Nabii Ibrahim aliifanya Makka kuwa ni mji Mtukufu na akawaombea dua watu wa

²²³ Rejea Al-rifaai, Hadithi zilizopokelewa kuhusu fadhila za mji wa Madina ukurasa wa 301.

²²⁴ Rejea Swaaleh Al-rifaai ,Hadithi zilizopokelewa kuhusu fadhila za mji wa Madina ukurasa wa 301.

mji huo, na mimi nimeufanya mji wa Madina kuwa ni mtukufu sehemu iliyopo kati ya Milima yake" (370) Kama alivyoomba Dua Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- "Ewe Mola wetu wa haki Tupendezeshee mji wa Madina kama tunavyoupenda mji wa Makkah au zaidi" (371) Na hapana shaka kuwa kupaombea mahala, kunapelekea kwenye kuuhifadhi mji na wakazi wake na kupata makazi ya kudumu humo.

Kama ilivyo katika sheria aliyioweka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kwa ajili ya kuhifadhi mazingira na maisha ya uhalisia katika mji wa Madina ni kauli yake aliposema: "Kwa hakika Ibrahim aliufanya mji wa Makka kuwa ni mtukufu na mimi nimeufanya mji wa Madina kuwa ni mtukufu sehemu iliyopo kati ya vitongoji vyake viwili na mipaka yake ni sehemu tukufu, hivyo haikatwi miti yake wala kufukuzwa wanyama wake, wala hakuokotwi kilichopotea isipokuwa kwa nia ya kukitangaza, na wala miti yake haikatwi isipokuwa kama mtu atamlisha ngamia wake, na wala hakuruhusiwi kubeba silaha kwa ajili ya kupigana".²²⁵

Kama alivyosema Mtume Sala na amani ziwe juu yake "kumefanywa ni sehemu tukufu sehemu iliyopo kati ya vitongoji viwili vya Madina ni sehemu tukufu kwa kupitia ulimi wangu" Amesema na akawajia Mtume watu wa kabila la Banii haaritha na akasema: "Nina waoneni Enyi watu wa Banii Haaritha mmetoka katika mipaka ya sehemu tukufu" kisha akageuka na akasema: "Bali nyinyi mpo ndani ya mipaka ya sehemu tukufu"²²⁶

²²⁵ kutoka Riwaya ya Imamu Ahmad katika musnadi yake juzuu ya 1/119.

²²⁶ Ameipokea Bukhari, katika mlango wa Utukufu wa Mji wa Madina, juzuu ya 2/221.

Na kwa hakika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- aliwasifia watu wa Madina na wakazi wake humo na wenye kukimbilia humo na wenye kuhamia humo kama alivyosema -Sala na amani ziwe juu yake-: "Hakika Imani itapenyeza na kuingia katika mji wa Madina kama anavyopenyeza nyoka mwenye kuingia katika shimo lake" (374)

Na katika hadithi ndefu amesema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake: "Na mji wa Madina Bora kwao kama wangukuwa wanajua" (375.)

KUONGEZEKA KWA WAKAZI:

Alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake akipupia juu ya kuongezeka kwa wakazi katika mji wa Madina na kuzaana kwa waumini, na kwa ajili hiyo alifurahi Mtume na waliokuwa pamoja naye miongoni mwa waislamu kwa kuzaliwa mtoto wa kwanza kwa waliohama kutoka Makka kwenda Madina baada kuhama kwa Mtume naye mtoto huyo ni Abdallah Bin Zubair (376) na kwa hakika zimekuja Aya nyingi za Qur'ani zikiamrisha kuwachunga watoto na kutilia mkazo uwajibikaji wa baba zao kuwatafutia riziki katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ حَشِيَّةَ إِمْلَاقٍ نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ﴿٣١﴾﴾

[الإسراء: 31]

"Na mkijua kwamba riziki iko kwenye mkono wa ALLAH, kutakata na sifa za upungufu ni Kwake, basi msiwaue watoto wenu kwa kuchelea umasikini, kwani Yeye, kutakata na sifa za upungufu ni Kwake, Ndiye Mwenye kuwaruzuku waja Wake, Anawaruzuku wana kama Anavyowaruzuku wazazi. Hakika kuua watoto ni dhambi kubwa". [Al- israa: 31]

Kama yalivyokuja maamrishi tofauti tofauti kutoka kwa Mtume, yakitilia mkazo juu ya umuhimu wa kuongezeka kwa waislamu pamoja na kuhimiza malezi bora na kufanyia maandalizi, miongoni

mwa amri hizo ni maneno yake-Rehema na amani ziwe juu yake aliposema: "Oeni wanawake wazuri wenye kuzaa, kwa hakika mimi natarajia kuwa na watu wengi kuliko ummati mwingine siku ya kiyama"²²⁷

Na Sensa ya Kwanza ya wakazi kutambulika katika uislamu ilikuwa katika wakati wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na imepokelewa kuwa Mtume alisema: "Niandikieni kila mtu aliyetamka uislamu", anasema Hudhaifa Bin Yamaan: "Tukamuandikia watu Elfu moja na mia tano"²²⁸. Na huku ndiko kutilia umuhimu wa moja kwa moja, ili kujua uwezo wa watu, na alikuwa Salana amani ziwe juu yake- akimuelekeza mtu mmoja mmoja kwa lile ambalo linamfaa.

Na kwa ilivyokuwa maarufu kuwa Mtume alihimiza kuhama kwenda Madina, na pamoja na hivyo alikuwa akipupia kudhibiti mambo, na kutotoka kwenye mipaka ya mji wa Madina na kutochanganya utaratibu wake, na alikuwa anapupia vilevile kutotokea makosa katika upangiliaji wa makazi, na hivyo, pindi waliposilimu Baadhi ya makabila na wakataka kuhama moja kwa moja kwenda katika mji wa Madina aliwaamrisha Mtume-Sala ana amani ziwe juu yake-wabakie majumbani mwao na wajifunze wao kwa wao, wawe tayari kupokea Amri zake.(379)

Kama ambavyo alisimamisha kuhama baada ya kuufungua mji wa Makka (380) jambo ambalo linakusudiwa kuleta uwiano na usawa kwa watu wa Madina na miji mingine.(381)

²²⁷ Ameipokea Imamu Ahmad katika Musndai yake juzuu ya/245.

²²⁸ Al-khuzaaiy ,takhrij Dalaalat samiyyat,ukurasa wa 230.

Na si hivyo tu bali ilikuwa kuwagawa wakazi ndani ya mji wa Madina ilikuwa ni jambo muhimu, na hivyo, ndiyo maana alipojenga Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- msikiti wake Mtume, na baada ya watu wa Madina kujua utukufu wa msikiti huo na kuswalia hapo walitaka watu wa kabila la Banii Salama wayaache makazi yao yaliyopo pembeni mwa Madina na wasogeze makazi yao karibu na msikiti wa Mtume, basi hakupendezewa Mtume kwa wao kufanya hivyo, kama ilivyokuja kwenye mapokezi ya Anas. "Watu wa kabila la banii Salama walitaka wabadilisha makazi ili wawe karibu na msikiti, akalichukia hilo Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuuwacha mtupu mji wa Madina, na akasema: "Enyi watu wa Bani Salama hivi hamtaki kupata Thawabu kwa majumba yenu haya ya kale" (382)

Ukuaji wa Nadharia ya Kiakili:

Hakika kuzidi kwa idadi ya wakazi pasina kutilia umuhimu wa aina ya wakazi na kuwapambanua hakuna faida, na kwa hivyo hakika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alikuwa akipupia zaidi kwa kila mmoja kati ya waislamu ahisi utofauti wake na nafasi yake pasina kuwa na kiburi, akiambatanisha hilo na kuwa mnyenyekevu kwa ajili ya ALLAH na kujidhalilisha kwake na kuwa mlaini kwenye kuamiliiana na waislamu na kuwaonea huruma viumbe wote, na hilo lilipasa kuilisha roho chakula cha kimaana na kuiimarisha mbele ya kila mtu, na kujenga uaminifu katika nafsi ya mwanadamu kuanzia masiku yake ya mwanzo wa maisha, na kuiimarisha hali yake ya kinafsi, Kuanzia jina lake ambalo huitwa kwalo, pale ambapo alipupia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuita kwa majina mazuri, (383) akiachilia mbali majina mabaya nakuita kwa majina mazuri, na majina ya utani yaliyo mabaya na kuita kwa yaliyo mazuri, basi akashiriki kwenye kuwaita idadi kubwa ya watoto katika wakati wake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake, kwa mfano Abdallah Bin Zubair na Hassan na Hussain watoto wawili wa Ally bin Abiitwaalib - Radhi za Allah ziwe juu yao- na wengineo katika watoto waliozaliwa katika mji wa Madina baada ya kuhama .

Kama alivyobadilisha majina ya baadhi ya Maswahaba (385)

Kama livyokuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akiwapa vijana na watu wote msukumo wa kiakili wakati wa kuwaita kwa kutumia majina mazuri na majina ya utani yaliyo mazuri, na akawa akimuita mtoto mdogo ewe katoto kangu, na akiwaitania, basi humuita ndugu mdogo wa Anas Bin Maalik na husema; Ewe Baba Numair, yote haya alikuwa akiyafanya kwa mtu mmoja mmoja ,ama kwa watu wote wa umati wa Muhammad -Sala na amani ziwe juu yake-kwa hakika ALLAH-Kutakasika na machafu ni kwake amesema kuhusu umma huo:

﴿ كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ
وَلَوْ ءَامَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ مِّنْهُمْ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ ﴾ [آل عمران:
110]

"Mmekuwa ni Umma bora mlioteuliwa kwa watu" [Al-Imran: 110]. Kama ambavyo aliufundisha umma mzima kupendana wao kwa wao na ulimwengu mzima, na kukihurumia kila kiumbe hai.

UKUAJI WA KIELIMU:

Ilikuwa Uislamu tangu kuteremka kwa Qur'ani na Aya zake za Mwanzo kuteremka kwa Mtume asiyejua kusoma wala kuandika ili kukumbusha Elimu na kalamu, amesema ALLAH Mtukufu:

﴿ وَإِنَّكَ لَعَلىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾ فَسْتَبْصِرْ وَبُصِيرُونَ ﴾ [القلم: 4-5]

"Aliyewafundisha viumbe wake kuandika kwa kalamu". (4) Alimfundisha binadamu vitu ambavyo hakuwa akivijua. (5) Akamtoa kwenye giza la ujinga, Akampeleka kwenye nuru ya elimu. [Suratil Alaq: 4-5] (386)

Na katika wakati ambao waarabu walitwaliwa na ujinga na kutokujua kusoma wala kuandika na uzushi wa mambo mbali mbali na viganu vya kale, na wala hauwezi linganisha na miji mingine na

mataifa ya jirani na kulinganisha na jamii ya mayahudi na manaswara katika miji ya warabu.

Na alikuwa Mtume katika mji wa Madina akihimiza elimu na kujifunza (387) na hakuna shaka kuwa jambo hilo lilikuwa na athari yake kwa jamii ya Madina na ukuaja wake wa kielimu, na vilikuwa vikao vyake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ni vikao vya kielimu.

Walikuwa Maswahaba wakisoma kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوا فِي الْمَجَالِسِ فَأَفْسَحُوا يَفْسَحِ اللَّهُ لَكُمْ وَإِذَا قِيلَ أَنْشُرُوا فَأَنْشُرُوا يَرْفَعِ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ﴾ [المجادلة: 11]

"Enyi mliomuamini ALLAH na Mtume Wake na mkafuata Sheria Zake kivitendo! Mkitakiwa mpeane nafasi kwenye mabaraza basi peaneni nafasi, na mkifanya hivyo Mwenyezi Mungu Atawakunjulia nafasi duniani na Akhera. Na mkitakiwa kwenu, enyi Waumini, muinuke katika mabaraza yenu kwa jambo lolote lenye kheri kwenu, basi inukeni. Mwenyezi Mungu Anavipandisha vyeo vya Waumini miongoni mwenu, na Anavipandisha vyeo vya wenye elimu daraja nyingi kwa kuwapatia malipo mema na daraja za kupata radhi. Na ALLAH Anayatambua matendo yenu, hakuna chochote kinachofichikana Kwake katika hayo, na Yeye ni mwenye kuwalipa nyinyi kwayo". Katika aya hii pana kutukuza cheo cha wanavyuoni na utukufu wao na kutukuzwa daraja zao. [Al-Mujadilah: 11].

Alikuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ndiye mwalimu wa kwanza katika mji wa Madina akiwafundisha watu Qur'an na mambo ya dini na hiyo Qur'ani ni mfumo uliokamilika na ndiyo kanuni ya sheria za maisha.

Ameweka Imamu Bukhari katika sahihi yake kitabu amekiita kwa jina la: kitabu cha elimu (388) ameleta humo milango hamsini na tatu, katika hadithi nyingi na akafafanua Aya mabali mbali mfano maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿أَمَّنْ هُوَ فَنِيكَ ءَأَنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ﴾ [الزمر: 9]

"Je, kafiri huyu anayejistarehesha na ukafiri wake ni bora, au ni yule anayemuabudu Mola wake na kumnyenyekea, anatumia nyakati za usiku kusimama kwenye lbada na kumsujudia, anaogopa adhabu ya Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake? Sema, ewe Nabii, «Je, wanalingana wale wanaomjua Mola wao na dini yao ya haki na wale wasiojua chochote katika hayo?» Hawalingani. Kwa hakika wanaokumbuka na kujua tafauti ni wale wenye akili timamu. [Al- zumar: 9]

Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ ۗ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا﴾ [الإسراء: 85]

"Na makafiri wanakuuliza juu ya uhakika wa roho kwa njia ya ushindani, basi wajibu kwamba uhakika wa roho na hali zake ni katika mambo ambayo ALLAH Ameufanya ujuzi wake uweko Kwake. Na hamukupewa ujuzi, nyinyi na watu wote, isipokuwa kitu kichache". [Al-Israa: 85] Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَمِنَ النَّاسِ وَالْذَوَابِّ وَالْأَنْعَامِ مُخْتَلِفٌ أَلْوَنُهُ كَذَلِكَ ۗ إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ﴾ [فاطر: 28]

"Na miongoni mwa watu na kila kinacho tembelea miguu minne na wanyama ni wenye kutofautiana rangi hivyo hivyo si vinginevyo wanao muogopa miongoni mwa waja wake ni wanazuoni".

[Faatwiri: 28] Na kwa hakika amesema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake: "Hakuna Husuda inayoruhusiwa isipokuwa kwa watu wawili, mtu wa kwanza ni aliyepewa mali na ALLAH akaidhibiti mali ile kwa kuitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu, na mtu wa pili ni yule ambaye ALLAH amempa Hekima na akawa anahukumu kwayo na kuifanyia kazi"²²⁹

Na alikuwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- akumuamrisha mwenye kujifunza kuwafundisha wengine, na kwa hakika alihimiza Mtume -Sala na amani ziwe juu yake: ujumbe wa Abdul Qaisi kuwafundisha watu wao, akawaambia: "Rudini kwa watu wenu na muwafundishe".²³⁰

Na kuandika kulikuwa kunachukua Nafasi ya kwanza kwa mayahudi katika mji wa Madina, mayahudi ambao walikuwa wakijua kuandika na kusoma na wakiwafundisha watoto wao kwa utaratibu ujilikanao kwa jina la Shule²³¹na ilikuwa utiliaji mkazo wao kwenye herufi za kiebrania wakiandikia nacho Lugha ya kiarabu, na baadhi ya watu wa kabila la Ausi na Khazraji walijifunza toka kwa mayahudi²³².

²²⁹ Sahihi Bukhari, Hadithi namba: 73.

²³⁰ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 87.

²³¹ Rejea kitabu cha Muhammad Al-eid Al-khatwraawiy,kiitwacho Madina katika wakati wa zama za ujinga ukurasa wa 99.

²³² Angalia kitabu cha Mustwafa Al-aadhwamiy, kiitwacho Waandhishi wa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-; kutoka katika Maktaba ya kiislamu chapa ya 1/Bairuut ,1401 hijiria.

Na walijua waislamu umuhimu wa uandishi kabla ya kuhama kweda Madina, pale ambapo Fatuma Bint Al-khattwab na mume wake Said Bin Zaid katika mji wa Makka walikuwa hao wawili wakisoma Surat Twaha kutoka katika kurasa walizokuwa nazo mikononi mwao pamoja na Khabbab Bin Aratt, na hilo lilikuwa pale alipoingia Omar Bin Khattwab na akagundua kusilimu kwao²³³

Na kwa hakika alikuwa Ubaada Bin Swaamit akiwafundisha watu wa Suffah Kusoma na kuandika²³⁴

Na baada ya kuisha vita vya Badri kulikuwa na kundi kubwa la mateka watokanao na washirikina wa kikuraish ambao walikuwa wanajua kusoma na kuandika vizuri na walikuwa hawana Mali za kujikomboa kutoka kwenye utumwa Basi Mtume akakubali mmoja wao kufundisha kusoma na kuandika watoto kumi miongoni mwa watoto wa Madina, na malipo yake ni kuachwa huru²³⁵ basi wakati huo walijifunza kusoma na kuandika kundi kubwa katika watoto wa Answaar.

Na huenda pupa kubwa baada ya hapo ni kuandika Qur'ani na Sunna ambayo ilianza wakati wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuchukuliwa kuwa ni miongoni mwa sababu muhimu za watu wa Madina kuandika vizuri, na vile vile hali ilivyo kwa waandishi wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ambao walitoa michango yao katika kuandika barua zake kwenda kwa viongozi wake aliowateua

²³³ Al- siirat Nabawiyat ya Bin Hishaam juzuu ya 1/345.

²³⁴ Doctor Akram Dhwyahul Umar ,katika kitabu chake kiitwacho Almujtamaa almadaniyyu fii ahad Al- nubuwwat, al-qismul awwal ukurasa wa 96.

²³⁵ Angalia Vita vya Badri kutoka katika kitabu hiki.

na wafalme wa ulimwengu ambao walifikia idadi ya waandishi sitini.²³⁶

Na huenda kutokana na kuchunga haki za wengine na ulazima wa kufanyia uhakiki huchukuliwa kuwa kufanya hivyo ni kinga na utetezi muhimu sana kwenye kuandika, na namna hii ndivyo Aya ndefu katika Qur'ani ilivyoashiria, Aya ambayo inatambulika kwa jina la Aya ya Deni katika maneno yake ALLAH Mtukufu.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا تَدَايَنْتُمْ بِدِينٍ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى فَاكْتُبُوهُ وَلْيَكْتُب بَيْنَكُمْ كَاتِبٌ بِالْعَدْلِ وَلَا يَأْبَ كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللَّهُ فَلْيَكْتُبْ وَلْيُمْلِلِ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ وَلَا يَبْخَسَ مِنْهُ شَيْئًا فَإِن كَانَ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيهًا أَوْ ضَعِيفًا أَوْ لَا يَسْتَطِيعُ أَنْ يُمْلَلَ هُوَ فَلْيُمْلِلْ وَلِيُّهُ بِالْعَدْلِ وَاسْتَشْهِدُوا شَهِيدَيْنِ مِنْ رَجَالِكُمْ فَإِن لَّمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَامْرَأَتَانِ مِمَّن تَرْضَوْنَ مِنَ الشَّهَادَةِ أَن تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا فَتُذَكَّرْ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَىٰ وَلَا يَأْبَ الشَّهَادَةُ إِذَا مَا دُعُوا وَلَا تَسْمَعُوا أَن تَكْتُبُوهُ صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا إِلَىٰ أَجَلِهِ ذَٰلِكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ وَأَقْوَمُ لِلشَّهَادَةِ وَأَدْنَىٰ أَلَّا تَرْتَابُوا إِلَّا أَن تَكُونَ تِجَارَةً حَاضِرَةً تُدِيرُونَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَلَّا تَكْتُبُوهَا وَأَشْهِدُوا إِذَا تَبَايَعْتُمْ وَلَا يُضَارَّ كَاتِبٌ وَلَا شَهِيدٌ وَإِن تَفَعَّلُوا فإِنَّهُ فُسُوقٌ بِكُمْ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿﴾ [البقرة: 282]

²³⁶ Angalia Waandishi wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kitabu cha Mustwafa Al-aadhwami ukurasa wa 179; na Angalia pia Muhammad Humaidillah Uthibitisho wa kisiasa katika zama za mtume na utawala ulioongoka, na Kitabu cha Ahmad Abdulrahman Issa, kiitwacho Kitabu cha Wahyi, kimechapwa na Daarul liwaai, Riyaadh 1400 Hijiria na kitabu cha Jamaludiin Abuu Abdullah Muhammad Abuu Hadiidah, kiitwacho Al-Misbaah Al- mudhwiiu fii Kitabi Annabiyuu -Swalla Ilaahu alaihi wasallam-

"Enyi mlio amini mtakapo daiana deni mpaka muda fulani basi liandikeni na aliandike baina yenu muandikaji kwa uadilifu na wala asikatae muandishi kuandika kama alivyo fundishwa na ALLAH basi aandike na amuandikie yule mwenye haki na amuogope Mola wake na wala asimpunje kwenye haki yake chochote, basi kama itakuwa yule mwenye haki ni mjinga au mdhaifu au hawezi kuandika basi amuandikie msimamizi wake kwa uadilifu na muweke mashahidi wawili miongoni mwa wanamume wenu, kama hawatapatikana wanaume wawili basi apatikane mwanaume mmoja na wanawake wawili miongoni mwa wale mnao waridhia katika mashahidi, ikiwa atapotea mmoja wao basi mmoja wao atamkumbusha mwingine, na wala wasikatae mashahidi pindi watakapoitwa, na wala msipuuzie kutoandika dogo wala kikubwa mpaka muda wake, kufanya kwenu hivyo ndio uadilifu mbele za ALLAH na ndio ushahidi wa sawa na ni kidogo kutopata mashaka, isipokuwa kama itakuwa ni biashara uliyopo mnayo izungusha baina yenu basi hakuna ubaya kama mtaacha kuandika, na wekeni ushahidi pindi mnapo uziana, na wala asidhuriwe muandishi wala shahidi na muogopeni ALLAH na atakuelemisheni ALLAH na ALLAH kwa kila kitu ni mjuzi". [Al-baqara: 282].

Na ilifahamika kuwa baadhi ya wanawake walikuwa wanajua kuandika na wakiwafundisha baadhi ya wanawake katika wakati wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na huenda hilo lilitokana uhamasishaja toka kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**, na kwa hakika imepokelewa kuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**amesema kumwambia Shifaa Bint Abdallah naye ni katika kabila la banii Adii Bin Kaab katika makuraish, alisilimu na akahama kwenda Madina "Hivi haumfundishi Hafswa Ruqya (kisomo cha

Qur'ani) kwa ajili ya ugonjwa wa vidonda vya mbavuni kama ulivyomfundisha kuandika"²³⁷

Na walipatikana wanawake wengine waliokuwa wakiwafundisha wanawake kuandika na kusoma kwenye mji wa Madina katika zama za Mtume²³⁸nasi twajua kuwa himizo la kujifunza na kufundisha lilokuja katika Sunna za Mtume na kabla yake himizo lililokuja kutoka katika Qur'an tukufu haikuwa ni maalumu tu kwa wanaume bila kuhusisha wanawake, Bali lilikuwa ni himizo la Umma mzima kwa jinsia zote na umri wowote na makundi yote.

Na huenda Taswira ya idadi ya waandishi katika mji wa Madina kabla ya kuhama Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na kuzidi idadi yao baada ya kuhama Mtume kwa kipindi kinachokadiriwa miaka minne, hutupa hisia kuhusu upeo wa kuenea kwa Waandishi katika mji wa Madina baada ya kuhama Mtume, na kutokana na Athari ya moja kwa moja toka kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake, na ni matarajio kuwa idadi ilizidi mpaka kufikia zaidi ya mara tatu au Nne, na hapana shaka kuwa kusoma na kalamu ndiyo vitendea kazi vya mwanzo kabisa kupata elimu navyo ndivyo vilivyoashiriwa katika Aya za Mwanzo kabisa zilizo teremka kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿أَقْرَأْ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ﴿۱﴾ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ﴿۲﴾ أَلَمْ يَكُنْ الْأَكْرَمُ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ﴿۳﴾ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿۴﴾﴾ [العلق: 1-5]

²³⁷ Kitabu Zaadul Maad cha Bin Qayyim, juzuu ya 3/24.

²³⁸ Angalia Abdul Aziz Al-umariy katika kitabu chake kiitwacho Alharfu wa Swinaat fil Hijaz fii Asri Nabawiy,Al- qiraatu walkitaabat,ukurasa 35.

"Soma kwa jina la Mola wako aliye umba. (1) Amemuumba mwanadamu kutokana na pande la damu. (2) Soma na Mola wako ni mwenye ukarimu. (3) Aliyewafundisha viumbe wake kuandika kwa kalamu. (4) kamfundisha mwanadamu asiyo yafahamu. (5) (Surat Al-alaq: 1-5) Na pamoja na kutilia mkazo- wakati huo huo- Hali ya Bwana Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na kuwa kutojua kwake kusoma na kuandika ni muujiza kwake:

﴿وَمَا كُنْتُمْ تَتْلُوا مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّوهُ بِيَمِينِكُمْ إِذَا لَأْتَابَ الْمُبْطُونَ﴾

[العنكبوت: 48]

"Na miongoni mwa miujiza yako iliyo wazi, ewe Mtume, ni kuwa wewe hukusoma kitabu wala hukuandika herufi zozote kwa mkono wako wa kulia kabla ya hii Qur'ani kukuteremkia, na hali wao wanalijua hilo. Na lau ungalikuwa ni mwenye kusoma au kuandika kabla hujaletewa wahyi wangalilifanyia shaka hilo hao wapotofu na wangalisema, «Amejifunza hiyo (Qur'ani) au ameinakili kutoka kwenye vitabu vilivyotangulia.» [Surat An-kabuut: 48].

UKUAJI WA KIJAMII:

Ilikuwa jamii ya watu wa Madina kabla ya uislamu na kuhama kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kama jamii nyingine ya kiarabu ya zama za ujinga, imegubikwa na Tamaduni za kikabila, kulikuwepo na ujinga mwingi na baadhi ya makabila yalikuwa mazuri.

Na popote alipofikia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- aliyetumwa kuwa huruma kwa viumbe wote, aliacha tabia ya hali ya juu na sifa tukufu ambazo alikuja nazo, na akataka ALLAH kuzieneza kwa watu, na kilichofuatia yalianza kuenea mabadiliko ya kijamii katika jamii ya Madina.

Alihimiza kujitolea katika mshikamano na kuweka mipaka ya majukumu (399) na kueneza sadaka, na kuwaliwaza wenye kuhitajia

na mafakiri, na kuchangia uwezeshanaji kijamii, sawa iwe kati ya Answaar na Muhaajiriina, au wenye kuhitajia miongoni mwa waislamu, Bali kutoa sadaka na kutenda wema kwa waliokuwa waislamu, ukiongezea zaidi maelekezo ya kiutumbe ya kujihifadhi na machafu na kutotegemea watu wengine, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٥٤﴾ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٥٥﴾﴾ [المعارج: 24-25]

"Na wale ambao katika mali yao kuna fungu maalumu alilowafaradhia ALLAH, nalo ni Zaka" (24) Kwa wenye kuomba na wasioomba (25) [Al-maarij: 24-25]

Na kulikuwa na vyanzo vinavyopelekea uharibifu wa tabia na jamii, Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alivipiga vita, kama Zinaa ambayo ulikuja uislamu kuiharamisha moja kwa moja na kuiwekea adhabu kali, nayo zinaa ni katika mlango mkuu unaochangia kuharibu jamii, na kupoteza nasaba na kuchanganya mbegu za uzazi kuenea maradhi ya kisaikolojia, na kupoteza majukumu na kukata udugu, na yamekuja makatazo makali katika hilo, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ هُمْ لِأُزْوَجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٥٦﴾ إِلَّا عَلَىٰ أَرْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ

مَلُومِينَ ﴿٥٧﴾﴾ [المؤمنون: 5-6]

"Na wale ambao tupu zao huzihifadhi. (5) Isipokuwa kwa wake zao au vijakazi wao basi wao si wenye kulaumiwa. (6) [Al Mu'minun: 5-6].

Na kama ambavyo aliwawekea wanandoa haki maalumu, na akaamrisha kuheshimiana na kuamiliana vizuri kati yao na pia kupendana na kuoneana huruma na kutendeanan wema, na Mtume akalifanyia kazi jambo hilo kwenye kuamiliana na wake zake na akawa ni mfano ulio hai kwa upande huu. (400)

Kama ambavyo pombe ilikuwa ikichangia matatizo makubwa katika jamii, na ilikuwa ikizingatiwa kuwa ni chanzo cha ufahari kwa warabu, licha yakuwa huleta matatizo mengi katika jamii, basi ukaja uislamu ili kuiharamisha pombe kwa awamu mpaka ikawa ni katika madhambi makubwa (401) Basi kwa kuharamishwa pombe zilibadilika tabia za watu wengi.

Na kwa hakika uislamu ulikuja ili kufungamanisha jamii na ukafanya kuunga udugu ni katika mambo makubwa ya kujikurubisha kwa ALLAH Mtukufu, na kutafuta kuujua udugu wa damu na kufanyiana wema, na kuwapa matumizi ni katika milango ya thawabu zilizo tukufu zenye kuambatana na upwekeshaji wa ALLAH na kufanya uadilifu, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَايَ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُم لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾ وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْقُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَعْمَلُونَ ﴿٩١﴾ ﴾ [النحل: 90-91]

"Hakika ALLAH anawaamrisha kufanya uadilifu na wema na kuwapa ndugu wa karibu na anakataza uchafu na maudhi na ujeuri anakupeni wasia ili mpate kukumbuka". Na tekelezeni ahadi za ALLAH pindi mnapo ahadi na wala msitengue viapo baada ya kuvithibitisha na hali mmemfanya ALLAH kuwa kwenu ni mdhamini, hakika ALLAH anajua mambo mnayo yafanya". [Al-nahli: 90-91] Kama alivyofanya kuwa kuwatendea wema wazazi wawili ni wajibu kisheria, na kumeambatanishwa na kumtii ALLAH Mtukufu na kujikurubisha kwake, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا إِمَّا يَبُلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أَفٍ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ ﴾ [الإسراء: 23]

"Na amehukumu Mola wako msimuabudu isipokuwa yeye peke yake na wazazi wawili muwafanyie wema, ikiwa atafikia

mmoja wao utu uzima kwako wewe au wote wawili, basi usiwaambie hata neno 'Ah!' na wala usiwakemee na waambie maneno mazuri". [Al Israai: 23]. Na akafanya uhusiano mzuri na majirani kuwa ni wajibu kisheria, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۚ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ
وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ
أَيْمَانُكُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا﴾ [النساء: 36]

"Na muabuduni ALLAH na wala msimshirikishe na kitu chochote na wazazi wawili wafanyiwe wema, na ndugu wa karibu, na mayatima, na masikini, na jirani wa karibu na jirani wa mbali na rafiki wa ubavuni (Mtu mnayesafiri pamoja) na mpita njia, na vijakazi wenu hakika ALLAH hampendi kila mwenye kujikweza na kujifaharisha." [An Nisaai: 36]. Na akafanya kusaidizana katika wema na uchamungu ni katika alama za kijamii kwa watu wote, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَحْلُوا شَعِيرَ اللَّهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ وَلَا الْهَدْيَ وَلَا الْقَلَئِدَ وَلَا ءَأْمِينَ
الْبَيْتِ الْحَرَامِ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّن رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا وَإِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوا وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ
قَوْمٍ أَن صَدَّوْكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَن تَعْتَدُوا وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى
الْإِنْمِ وَالْعُدُوِّ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ﴾ [المائدة: 2]

"Enyi mlio amini msihalalishe alama za ALLAH wala miezi mitukufu na zawadi wala kuweka vidani shingoni-mwa wanyama-wala walio pewa amani ndani ya al-kaaba tukufu wakitafuta fadhila za Mola wao na kuridhiwa, na mtakapo kuwa halali (mtakapomaliza ibada ya Hija) basi windeni, na wala kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika msikiti mtakatifu wa Makkah kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na msaidiane katika wema na uchamungu na wala msaidiane katika dhambi na uadui. Na

mcheni Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu" [Al Maaida: 2]. Yote hii ni kazi ya kuzidisha mshikamano wa kijamii na kuirekebisha jamii katika mji wa Madina, na kuendeleza kujuliana hali wao kwa wao na kuwasamehe kwao watu wengine (402) anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٣٩﴾ وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾﴾ [الشورى: 39-40]

"Na wale ambao yakiwapata maonevu wanawalipiza wale waliowaonea bila kupita kiasi. Na wanaposubiri basi mwisho wa subira yao kuna kheri nyingi. (39) Na malipo ya ubaya ni ubaya mfano wake, basi atakaye samehe na akapuuzia basi malipo yake yapo kwa ALLAH hakika ALLAH hapendi madhalimu. (40) [Suratu Shuura: 39-40]

Ukiachilia mbali kuhusu wasia zingine za Ujumla na muamala uliokuwa mzuri na kuachana na wajinga, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٦٣﴾﴾ [الفرقان: 63]

"Na waja wa Al-Rahman (Mwingi wa rehema) ni wale wanaotembea aridhini kwa upole na wanapo semeshwa na wajinga, husema salam." [Al-furqaan: 63]. Na amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٧٢﴾﴾ [الفرقان: 72]

"Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uwongo na wanapo pita kwenye upuuzi hupita kwa heshima zao". [Al-furqaan:72] Kama alivyoamrisha kujihami kwa njia iliyokuwa nzuri wakati wa dharura, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تَسْعَوِي الْحَسَنَةَ وَلَا السَّيِّئَةَ ادْفَعِي بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَهٍ حَمِيمٌ﴾ [فصلت: 34]

"Na wala mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lililo jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako na yeye pana uadui atakuwa kama rafiki na jamaa wa kukuonea uchungu" [Fuswwilat: 34].

Na akafanya kuwa Tabia ya hali ya juu ndiyo lengo tukufu kwa kila mtu na jamii kwa ujumla.

Na amesema ALLAH Mtukufu:

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِّن نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِاللُّغَابِ بِئْسَ الْأِسْمُ الْفُسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ وَمَن لَّمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ﴾ يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَبَ بَّعْضُكُم بَعْضًا أَيُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ﴾ [الحجرات: 11-12]

"Enyi mlio amini lisipatikane kundi likawadharau kundi jingine huenda wanao dharauliwa wakawa bora kuliko wao, na wala wanawake wasiwadharau wanawake wengine huenda wanao dharauliwa wakawa ni bora kuliko wao, na wala msivunjiane heshima, na wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia majina mabaya baada ya kuamini, na yule ambaye hata tubia basi hao ndio madhalimu. (11) Enyi mlio amini jiepusheni na wingi wa kudhania hakika baadhi ya dhana ni madhambi na wala msipelelezane na wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi, hivi yupo katika nyinyi anayependa kula nyama ya ndugu yake aliyekufa? (Bila shaka) mnalichukia hilo! na muogopeni Mwenyezi Mungu, hakika ALLAH ni Mwenye kukubali toba, Mwenye kurehemu. (11-12) Na akawafanya watu wote kuwa sawa, kama vile meno ya kitana,

na wala hakuwatofautisha kati yao, na Qur'an ikatangaza kuwa asili ya wanadamu ni moja anasema ALLAH Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْوَمُ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾﴾ [الحجرات: 13]

"Enyi watu! Hakika sisi tumekuumbeni kutokana na mwanaume na mwanamke. Na tukawajalia mataifa na makabila ili mpate kufahamiana, hakika mbora wenu mbele ya ALLAH ni yule anaye muogopa, hakika ALLAH ni mjuzi Mwenye habari". [Al Hujrati: 13]. Na akaharamisha kiburi na kujikweza dhidi ya wengine anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تُضَعِّرْ حَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿١٨﴾﴾ [لقمان: 18]

"Na wala usiwabeue watu na wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika ALLAH hampendi kila mwenye kujivuna mwenye kujifakharisha. [Luqman: 18]. Na akafanya kutengamaa kwa jamii na nchi kwa ujumla ndiyo lengo la jumla la muislamu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَأَدْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾﴾ [الأعراف: 56]

"Na wala msifanye ufisadi katika ardhi baada yakuwa imekwisha tengenezwa. Na muombeni -ALLAH- kwa kuogopa na kutamani hakika huruma ya ALLAH ipo karibu na wafanyao mema". [Al A'raf: 56]. Na akafanya kupeana nasaha katika haki na kusubiri kuwa ni jambo la kibinadamu na ni jambo la wajibu, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿٣﴾﴾ [العصر: 3-1]

"Na apa kwa wakati wa laasiri" "Hakika mwanadamu yupo kwenye hasara. (2) Isipokuwa wale walio amini na wakatenda matendo mema, na wakahusiana ukweli na wakahusiana kuwa na subira. (3) [Al-asri: 1-3] Kama vile ambavyo lbada za Kiislamu zote zinachochea adabu na heshima na zinakataza machafu na maovu na miongoni mwayo ni swala, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿أَتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ وَأَقِمِ الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾﴾ [العنكبوت: 45]

"Wasomee yale uliyo funuliwa kutokana na kitabu (Qur'ani) na usimamisha swala hakika swala inakataza machafu na maovu na kumtaja ALLAH ni jambo kubwa na ALLAH anayajua mnayoyatenda. [Al-ankaboot: 45]

Na maadili haya ya kijamii yamekita katika mji wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake baada ya kuhama Mtume, na yakachochea ukuaji wa jamii hajaipata kutokea katika Historia ya Mwanadamu.

UKUAJI KATIKA SEKTA YA AFYA:

Na ulikuwa mji wa Madina kabla ya kuja Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ukiteseka na matatizo mengi ya kiafya kwa wakazi wake, miongoni mwa matatizo hayo yanamafungamano na Mazingira, na hasa hasa Homa ambayo ilikuwa imeenea kwa wakazi wake kwa sababu ya mashamba na yanayohusiana nayo katika madimbwi, basi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akauombea Mji wa Madina: "Ewe Mola wetu tujaalie tuipende Madina kama tunavyoipenda Makkah au zadi ya hapo, Ewe Mola wetu tutilie Baraka katika vipimo vyetu, na katika vyakula vyetu, na utufanyie kuwa mji wenye usalama wa afya, na uhamishe Homa ya Madina

kuipeleka Juhfa"²³⁹Na kinachoonekana wazi katika Dua ya Mtume, ni kutilia umuhimu-Sala na amani ziwe juu yake- Afya ya wakazi wa Madina

Kama ilivyokuwa Mtume aliugua kama wanavyouguwa watu wengine, (404) na akawahimiza watu kutumia dawa (405) na kutafuta matibabu pale aliposema Mtume: "Hakuwahi ALLAH kuteremsha Ugonjwa isipokuwa aliuteremshia dawa" (406)

Na alidumu kwenye kujitibu na alikuwa akitilia mkazo matibabu kwa kutumia vitu ya asili kama Asali na vinginevyo, na imepokelewa kutoka kwake-Sala na amani ziwe juu yake kuwa yeye amesema: "Tiba ipo kwenye mambo matatu Kunywa Asali, kupiga chuku (Hijama) na kuchoma kwa moto na ninaukataza Umma wangu kutibu kwa kutibu kwa moto".(407)

Kama alivyosimama Mtume katika msimamo usiyoyumba kutokana na uzushi ambao ulisababisha maradhi ya moyo na mwili miongoni mwayo ni mikosi, na akawawekea watu msingi imara wa kujibashiria mambo mazuri, na alikuwa akiamrisha kutumia baadhi ya mimea kama vile Habbat Saudaa na dawa zingine.(408)

Ama katika sekta ya matibabu na kinga kwa hakika ameweka misingi yake Mtume Sala na amani ziwe juu yake- katika maneno yake: "kiwa mtasikia Ugonjwa wa Tauni (kipindupindu) katika Ardhi fulani, basi msiingie humo, na ikiwa utazuka katika Ardhi nanyi mpo humo basi msitoke nje ya mji huo" (409)

Kama vile yeye alivyoweka misingi muhimu katika Afya na Tiba na kinga na matibabu, kupitia mlo kamili na kutofuja katika kula na kufunga funga ya Faradhi na kujikurubisha kwa ALLAH,na hayo

²³⁹ Al-Bukhariy katika kitabu cha Fadhila za Madina,juzuu ya 2/225.

yanatokana na kauli yake: "Hajawahi kujaza Mwanadamu chombo cha shari zaidi kuliko tumbo lake, kwani yamtosha Binadamu matonge kadhaa yawezayo kuusimamisha mgongo wake, na ikiwa ni lazima kujaza tumbo lake basi aache Theluthi kwa ajili ya chakula chake na Theluthi kwa ajili ya kinywaji chake, na theluthi nyingine kwa ajili ya kupumua kwake" (410)

Na alikuwa Mtume anakubali wito wa Madaktari wa kutibu wagonjwa, kama ilivyotokea kwa Saad Bin waqqas alipo ugua katika Hijja ya kuaga (411)

Na akakiri Mtume Ruqiya (Kisomo cha Qur'ani) ambacho ni sahihi kitokanacho na Qur'an na Dua.

Na katika masiku yake-Sala na amani ziwe juu yake- kuliwekwa Hospitali ya Kwanza katika Uislamu, pale alipoweka Rufaidat Bintul Aslamiyat- Radhi za Allah ziwe juu yake- katika vita vya Mahandaki, aliweka Rufaida Hema katika msikiti wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake- akiwatibu ndani ya msikiti huo majeraha, (412) na kwa hakika alimuweka humo Mtume wa ALLAH na amani ziwe juu yake- Saad Bin Muaadh baada ya kujeruhiwa katika vita vya Mahandhaki, hivyo akasema: "Muwekeni katika Hema la Rufaidah ili niwe namtembelea kwa ukaribu" (413) Kama ambavyo michango ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ilichangia katika usafi na kupupia usafi wa kuoga ikiwa ni katika kuzuia maradhi na kuenea kwake.

Na ulikuwa wasia wake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- katika usafi wa chakula na kukihifadhi na kukifunika kulikuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi afya ya mwanadamu kwa ujumla

Na akahimiza Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kutahiri na baadhi ya matendo ya usafi wa mwili ambao unachangia kuzuia maradhi na Bakteria katika maneno yake: "Mambo matano ni katika maumbile, kutahiri, na kunyoa nywele za sehemu za siri, na

kupunguza kucha, na kungo'a nywele za kwapa, na kupunguza masharubu" (414)

Na kwa hakika vimetungwa vitabu vingi vinavyohusu Tiba ya Mtume, vitabu vyote hivyo, vinatokana na yale yaliyopokelewa toka kwa Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- katika Sunnah zake (415)

Na kwa hakika mafundisho hayo yaliacha athari kwa ujumla katika mji wa Madina, na watu wa Madinah wakaathirika na wakayafanyia kazi katika maisha yao kwa ujumla na Binafsi, licha yakuwa ni maelekezo kwa umma wote, isipokuwa jamii ya watu wa Madina katika zama za Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- iliathirika nayo na kukatokea katika zama zake kuhamishwa kwenda kwa wengine na yakachangia maendeleo ya kiafya, maendeleo hayo yalianza muda mfupi tu baada ya kufika Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina, na mpaka sasa athari yake imebakia mpaka atakapo ichukuwa ALLAH Ardhi na vilivyomo ndani yake.

UKUAJI WA UCHUMI:

Na alikuwa Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- ni mchumi tangu udogoni mwake, kwa hakika alichunga Mbuzi za watu wa Makka kwa malipo kidogo ya Dinari, ili apate pesa na kumsaidia Baba yake mdogo ambaye ni AbuuTwaalib katika kuwalisha watoto wake, na amasema Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- "Hajawahi kutumwa Nabii yeyote isipokuwa alichunga Mbuzi", wakasema: Nawe pia ewe Mtume wa ALLAH? akasema: "Na Mimi nilikuwa nikichunga mbuzi kwa malipo kidogo ya dinari (416) kwa watu wa Makka" (417) na alipofikia Mtume umri wa utu uzima Bi Khadija alimuajiri ili afanye Biashara kwenye mali yake (418) na akawa na safari mbali mbali kwa ajili ya kufanya Biashara.

Na katika kauli za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-zenye kuhimiza kufanya kazi na kuzalisha faida "Hakuna chakula kilicho bora kuliko chakula anachokichuma mtu kwa mkono wake"²⁴⁰

Na alikuwa-Sala na amani ziwe juu yake- akiwapigia mfano maswahaba wa Manabii wenye kufanya kazi za mikono wenye kuzalisha kipato Akasema -Sala na amani ziwe juu yake- "Alikuwa Nabii Zakaria ni fundi Seremala" (420)

Na kwa hakika imekuja milango mingi toka kwa watu wa hadithi iliyojaa Hadithi za Mtume ambazo zinahimiza uchumi na kuzalisha mali na kufanya kazi, miongoni mwazo zipo kwenye sahihi Bukhari (Mlango unaohusu chumo la Mtu kutokana na mikono yake).(421)

Na kwa Bin Maajah katika Mlango (Mlango unaohimiza uchumi (422) na kwa Daaramiy (Katika Mlango unaohusu uchumi na kazi za mikono ya mtu)²⁴¹²⁴²

Na ilikuwa ni tabia ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-pamoja na wenye ujuzi na wanaofanya kazi katika mji wa Madina wakiwapa hamasa, naye anaitikia wito wa chakula kwa fundi nguo (424) na anamwacha mwanaye Ibrahimu kwa ajili ya kunyonyeshwa kwa mwanamke fundi vyuma (mhunzi). (425)

Na akawa kwa vitendo hivi na vinginevyo ana nafasi katika kuubadilisha mtazamo wa watu wa Madina na wengineo ambao

²⁴⁰ Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake, kwenye Mlango unaozungumzia mtu kuchuma kwa mikono yake namba 2027.

²⁴¹ Sunanu Ibnu Maajah juzuu ya 2/771

²⁴² Al-Daaramiy .katika Sunna zake juzuu ya 28/247.

wanadharau baadhi ya kazi kama vile kazi ya Fundi chuma na ufundi mwingine.(426)

Na kwa hakika sheria mbali mbali za uislamu ambazo Mtume alizifanyia kazi zilichangia Uzalishaji katika mji wa Madina, na ukuaji wake katika nyanja zote.

RUHUSA YA KUPIGANA:

Na kama inavyofahamika kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- anapokea Maamrishi na Ruhusa kutoka kwa ALLAH- kutakasika na machafu ni kwake- katika mambo yake yote na matendo yake yenye kufungamana na dini na sheria, na kupigana kwa jina la dini ni katika mambo hatari, nakwa hakika maswahaba wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-walipatwa na maudhi na maudhi mbali mbali tangu kuanza kwa daawa ya Mtume, na kwa hakika waliudhiwa kwa ajili ya ALLAH na wakanyang'nywa mali zao, na baadhi yao zikamwagwa damu zao, na wengine walifungwa na wakafukuzwa wengine kuacha nyumba zao na mali zao katika mji wa Makka na hatimaye kuhamia Habasha au Madina.²⁴³

Na pamoja na yote haya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alikuwa yupo Makkah akiwaombea maswahaba wake na kuwausia kusubri na kuvumilia, na kutarajia malipo kutoka kwa ALLAH, na kuwakumbusha waumini namna umma uliotangulia ulivyokuwa unawatesa na kuwaua waumini, na wakati huo huo anawafungua nyoyo zao kwa kuwa na matumaini na bishara njema ya kuenea uislamu na kutimiza jambo lake katika kila pande za Dunia na kuingia katika muda ujao (katika kila nyumba ya iliyojengwa kwa mawe au kwa udongo mgumu) (428) na kuwa amani kwa waumini ni yenyekuja "Na kwa hakika Mwenyezi Mungu atalitimiza jambo hili

²⁴³ Angalia kuhamia madina katika hiki kitabu:

mpaka aweze msafiri kusafiri kutoka San'aa (Mji mkuu wa Yeman) mpaka Hadharamauti (Iraq) awe hana amuogopaye isipokuwa ALLAH tu" (429)

Na Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kutukuka- aliinusuru dini yake, anasema ALLAH Mtukufu:

﴿هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ﴾ [التوبة: 33]

"Ni yeye ndiye aliye mtuma mtume wake kwa uongofu na dini ya kweli ili azishinde dini zote hata kama washirikina watachukia". [At-Taubah: 33.]

Na baada ya kuhama Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kwenda Madina walikuwa washirikina wakiwatishia na kuwafukuza maswahaba wake, achilia mbali kuendelea kuwaudhi wale waislamu waliokuwa Makka na mwenye kuutembelea mji wa Makka miongoni mwao sawa sawa awe ni Mkuraishi au wengineo wasiokuwa wao.

Na ilikuwa kuhama kwenda Madina ni hatua nyingine ya kupata nguvu na kujipanga kijeshi ili kuuhami uislamu na watu wake.

Na kwa hivyo miongoni mwa Sharti za kuunga mkono kwa mara ya pili kulikuwa hivi: ((Nina wataka mniunge mkono kwa kunilinda kama ambavyo mnawalinda wanawake wenu na watoto wenu)) kwani ulikuwa ni uungaji mkono wa ulinzi hata kama jambo litapelekea kuuana, na kwa hivyo Saad Bin Zurarat alilikuta suala hili na akawahadithia watu wa Madina kwa kuwaambia: "Kwa hakika nyinyi Mnamuunga mkono wa kuingia kenye vita Nyekundu na nyeusi toka kwa watu" (430)

Jambo lilikuwa wazi sana katika kupambanua hatua ya aina yake baada ya kuhama, na ndiyo maana walikuwa Muhaajiriina na Answaar kwenye maandalizi yaliyokamilika kujitoa kafara na fidia na

kupigana jihadi kabla haijafanywa Jihadi kuwa ni wajibu, wakawa ni wenye kupata matokeo yakuachwa kwao huru na matokeo yakutoa mali zao, kama vile ambavyo makuraishi wanavyopata matokeo ya hatua zilizopigwa, pale ambapo washirikina walikasirika sana baada ya kujua uungwaji mkono wa Aqabah, na wakajaribu kumzuia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuhama, kwani kuhama mwisho wake ni ishara ya vita ya waumini waliodhulumiwa baada ya kutengeneza nguvu zao. Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُبْسِتُوا أَوْ يُقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٣٠﴾﴾ [الأنفال: 30]

"Kumbuka pindi walipo kulia njama wale walio kufuru ili wakufunge, au wakutoe au wakuuwe, na wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango" [Suratil Anfaal :30]

Walikuwa washirikina wakijua kuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- hakupigana katika mji wa Makka wala hakuwaamrisha maswahaba wake kupigana.

Idhini ya kupigana na washirikina au (JIHAD) kama ulivyo msemu wa kisheria ni Sheria ya ALLAH kwa maandiko ya Qur'an ,na katika malengo yake ni kuwatetea wanaodhulumiwa, na kuwasikilizisha watu neno la hakina Dini, kwa kuwapiga vita wenye kuwafanyia Uadui walinganiaji wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-na wanaowazuia watu wote wasisikilize neno la Laailaha illallahu, au anaufanyia uadui mji wa waislamu na utukufu wao, na Jihadi imefungamanishwa kuwa kwake ni njia ya Mwenyezi Mungu na kuinua neno la ALLAH na katika njia ya ALLAH na katika njia yake hutolewa Mali na Nafsi na kila kitu.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿الَّذِينَ ءَامَنُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ الطَّغُوتِ فَقَاتِلُوا
أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا﴾ [النساء: 76]

"Wale walio amini wanapigana katika njia ya ALLAH, na wale walio kufuru wanapigana katika njia ya miungu inayo abudiwa kinyume na ALLAH basi waueni vipenzi wa shetani hakika vitimbi vya shetani vimekuwa ni dhaifu". [An-nisaa: 76] Na baada ya muda ulipatikana utulivu katika mji wa Madina, na ALLAH kuwajali waja wake waumini, na wao kuwa na subira na kushikamana na amri za ALLAH na kujizuilia na mapigano, iliteremka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Aya za Qur'an, ALLAH katika Aya hizo akimpa Ruhusa ya kupigana, Anasema ALLAH Mtukufu:

﴿قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأُزَيِّنَنَّ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَلَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ﴾ [الحجر: 39]

"Wameruhusiwa kupigana wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa, na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni muweza wa kuwasaidia". [Al-hajji: 39] (431)

Na kupitia aya hiyo inaonyesha kuwa idhini ya kupigana imekuja baada ya katazo, nakuwa idhini haimaanishi kuwa faradhi na ni lazima, bali ni ruhusa kutoka kwa ALLAH Aliyetakasika na kutukuka, na aya inazungumza wazi kuwa wao walidhulumiwa, kama ambavyo imeambatana na ahadi kutoka kwa ALLAH Aliyetakasika na kutukuka ya kuwanusuru naye ni muweza juu ya hilo, ama aina za dhulma walizokumbana nazo ziko miongoni mwake kama zilivyokuja katika kauli yake Mtukufu:

﴿الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ
بِبَعْضٍ لَهَلَكْتُمْ سَوَاعِدٌ وَبِيعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسْجِدٌ يُذَكَّرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ
يَنْصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ﴾ [الحج: 40]

"Wale ambao walio tolewa kwenye miji yao bila ya haki kwa kusema kwao Mola wetu ni ALLAH na kama sio ALLAH kuwazuia watu baadhi yao kwa baadhi hakika yangevunjwa majumba ya ibada za-mayahudi- na majumba ya ibada-za manaswara- na misikiti inayo tajwa jina la ALLAH zaidi ndani yake, na hakika ALLAH atamnusuru aliye mnusuru hakika ALLAH ni Mwenye nguvu Mtukufu." [Al Haji: 40] Huu ni ukweli endelevu mpaka siku atakapoirithi ALLAH Ardhi na wale waliomo, (kiyama) Amesema Mtukufu:

﴿فَهَرَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُدُ جَالُوتَ وَعَاءْتَهُ اللَّهُ الْمَلِكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ
 وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلَكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾﴾
 [البقرة: 251]

"Na lau asingeliwazuia ALLAH watu baadhi yao kupitia wengine basi hakika Ardhi ingeliharibika, lakini ALLAH ni mwenye fadhila kwa walimwengu" [Al Baqara: 251].

Alikuwa Sala na Amani ziwe juu yake akijua kuwa kupata nguvu na jihadi ni vitu vinahitaji nguvu, na kuwaandaa wanaume katika ngazi ya kwanza, kisha vifaa na kila kinachohusiana na vifaa.

Kupigana kulikuwa ni kwa sababu ya kuzuia dhulma na wala si kwa kuwafanyia watu uadui, na hapa ndipo iliteremka kauli yake Mtukufu:

﴿وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَقْتُلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿١٩٠﴾﴾
 [البقرة: 190]

"Na wapigeni katika njia ya ALLAH wale wanao kupigeni na msivuke mipaka hakika ALLAH hapendi wanao vuka mipaka." [Al-baqara: 190] Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا وَاجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا﴾ [النساء: 75]

"Mna nini nyinyi kutopigania katika njia ya ALLAH na wale walio tenzwa nguvu miongoni mwa wanaume na watoto ambao wanasema Mola wetu tutoe kwenye mji huu watu wake ni waovu na utujaliye sisi kutoka kwako msimamizi na utujaliye kutoka kwako wa kutunusuru." [An-saai: 75]

Maisha ya Mtume Sala na Amani ziwe juu yake yote yalikuwa ni kupambana na ushirikina, yamejaa Jihadi kwa maana yake kamili, na hasa hasa kuwapiga vita washirikina baada ya hatua ya kuidhinishwa kupigana, mpaka watu wengi waliotunga vitabu kuelezea maisha yake walilitilia umuhimu hilo kiasi kikubwa kinachoonyesha kuwa historia yake imejawa na jihadi na vita kuliko hata historia ya utume.

Walikuwa washirikina wakimpiga vita Mtume wa ALLAH Sala na Amani ziwe juu yake, basi ni kwanini yeye asipigane nao?, Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِي كِتَابِ اللَّهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرْمٌ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ وَقَاتِلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقَاتِلُونَكُمْ كَافَّةً وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ﴾ [التوبة: 36]

"Na wapigeni washirikina kabisa kabisa kama wanavyo kupigeni kabisa kabisa na tambueni kuwa ALLAH yupo pamoja na wachamungu". [Attauba: 36].

Na vilifikia vita vya Mtume Sala na Amani ziwe juu yake, na vikosi vyake alivyovituma zaidi ya vita na vikosi sitini (60) vikiwemo vita kumi na nane alivyoviongoza yeye mwenyewe, alipigana ndani ya vita nane miongoni mwa hivyo.²⁴⁴²⁴⁵

Na kuna tofauti kati ya wanachuoni katika idadi inayokuja katika kutofautisha kati ya vita na vikosi,²⁴⁶, wakati mwingine, au kulizingatia tuko kuwa ni kikosi au vita, au pengine tukio halikutokea kamwe.

Hakika Jihadi na upiganaji Vita katika maisha yake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ni miongoni mwa sababu zilizompa nguvu kwa ajili ya ALLAH na Mtume wake- Sala na amani ziwe juu yake-,na Mwanzo mzuri wa Ukombozi wa uislamu ambao malengo yake makubwa yalikuwa ni kuwakomboa watu na Dhulma na kuwapa fursa ya kusikiliza neno la haki pamoja na kutilia mkazo kuwa ((Hakuna kulazimisha katika Dini)) (435) na ahadi kwake kama ilivyokuja katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

²⁴⁴ Kitabu cha Bin Kathiri, katika Historia ya Bwana Mtume juzuu ya 2/353.

²⁴⁵ Tazama kitabu: Munaaqashatul Adad min khilalil maswaadiril mukhtalifa, cha Buraik Abuu Maila Al Omari, Vikosi na wajumbe wa Mtume pembezoni mwa Madina na Makka. Masomo yaliyochambuliwa, Uk. 58.

²⁴⁶ Buraiki Abu Maailat Al-umariy,kiitwacho As-saraaya wal-buuthu Nabawiyat haulal madinat wa Makkah ,ukurasa wa,Tazama riwaya ya ya Bin Abii Shaibah katika kuitabi chake Almaghaazyi,kikiwa cha Anuani " Fii Ghazawaatin Nabiiy Kam Ghazza"ukurasa wa 169.

﴿هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ﴾ [التوبة: 33]

"Yeye Ndiye Aliyemtumiliza Mtume Wake Muhammad, rehema ya ALLAH na amani zimshukie, kwa Qur'ani na dini ya Uislamu, ili Aifanye kuwa juu ya dini zote, ingawa washirikina wanaichukia dini ya haki-Uislamu- na kushinda kwake dini nyingine". [At-Taubah: 33].

Na amesema Allah Mtukufu:

﴿وَنُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ﴾ [القصص: 5]

"Na tunataka tuwaneemeshe wale walio tenzwa nguvu katika ardhi na tuwafanye kuwa viongozi na tuwafanye wao kuwa warithi". [Al-qaswas: 5]

Nayo ni sheria ambayo yatosheleza kuwa imekubalika toka kwa ALLAH Mola wa viumbe wote, na imetajwa kwenye Qur'ani tukufu, kwa kiwango kinachozidi mara ishirini, na zikateremka hukumu maalumu walizozifanyia uchunguzi wataalamu na umma ukazifuata, na kwa hakika alikuwa Mtume tofauti ukimlinganisha na mitume wengi waliotangulia kupigana Jihadi, na kushiriki kwake mwenyewe vita mbalimbali, na upangiliaji wake na uendeshaji wake (436) na kuitekeleza kwake jihadi ikiwemo nguvu na huruma na uadilifu na uhuru kwa wakati mmoja.(437).

Na hata kama watakosea ya baadhi wenye kukosea miongoni mwa wenye kuwafanyia uadui waislamu na wengine na wakatumia msemu huu kufanya matendo mabaya (Jihadi), kwa hakika hli kosa ni la kwao wao, kukosea hakumaanishi kuwa Jihadi ya kiislamu ya hakika na kisheria haitambuliki katika zama zote zilizopita pasina kutoa zama yoyote, na unatakiwa umma wote kujiandaa ili kujilinda

wenyewe na wawe ni wenye kukaa tayari kwa hilo, (Na hii ni kanuni ya kimataifa: If you want peace be prepare for war- Ukitaka amani jiandae kwa vita) kwa mujibu wa alivyo amrisha Mwenyezi Mungu - kutakasika na machafu ni kwake- na kama haitokuwa hivyo, watavamiwa na umma utadhoofika kutokana na maadui wake, maadui ambao tumewaona katika zama hizi namna gani walivyowafanyia waislamu kila mahala, kwa hakika kuihami dini na kuulinda mji na kuutunza mbele ya maadui, ni sehemu katika mambo yaliyowekewa sheria na ALLAH kutakasika na machafu ni kwake- katika maneno yake:

﴿الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَهْتِمَتْ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ﴾ [الحج: 40]

"Wale ambao walio tolewa kwenye miji yao bila ya haki isipokuwa kwa kusema kwao Mola wetu ni ALLAH na kama sio ALLAH kuwazuia watu baadhi yao kwa baadhi hakika yangevunjwa majumba ya ibada ya kiyahudi na makanisa na misikiti inayo tajwa ALLAH ndani yake kwa wingi na hakika ALLAH atamnusuru yule anaye mnusuru hakika ALLAH ni mwenye nguvu mwenye utukufu".
[Al Haji: 40]

Na yatupasa tuisahau ufahamu huu na kuwa maadui hawarudishwi nyuma isipokuwa kwa nguvu na kupigana jihadi, basi kwa kuitaja tu Jihadi huwatisha maadui wa uislamu.

Na watu wengi -kwa masikitiko makubwa- wanajaribu kuchafua ufahamu wa uislamu kwa kupitia neno Jihadi na kuliambatanisha na matendo ya nje yasiyohusiana na uislamu ili waung'oe ufahamu huu katika umma, bali huenda wamewafanya watoto wa kiislamu walichukie neno hilo wanapolisikia kwenye vyombo vya habari, pindi linapofungamanishwa neno hilo na uadui au (Ugaidi) .

FUNGA YA RAMADHANI:

Swaumu ilitambuliwa kwa Mayahudi na Manaswara kabla ya uislamu, na mpaka sasa kwa baadhi yao wanaijua funga pamoja na kubadilisha namna ya ufungaji wake na muda wake kinyume na ilivyowajia kutoka katika asili ya sheria.

Na katika mwezi wa Shabani mwaka wa pili tangu kuhama Makkah Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- iliteremka Faradhi ya kufunga Swaumu ya Ramadhani kwa waislamu katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾ أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ فَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُ وَأَن تَصُومُوا خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٤﴾ شَهْرَ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْءَانُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِيُكْمِلُوا لِّلْعِدَّةِ وَلِيُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَى مَا هَدَيْتُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٨٥﴾﴾ [البقرة: 183-185]

"Enyi mlio amini mmefaradhishiwa juu yenu kufunga kama walivyo faradhishiwa wale waliokuwa kabla yenu ili mpate kuwa wachamungu". (183) Mfunge siku zenye kuhesabika, basi yule atakaye kuwa mgonjwa miongoni mwenu au akawa safarini alipe kwenye siku zingine na kwa wale wanao weza kufunga-kisha wakala- watoe fidia ya kulishiza masikini, na atakaye jitolea basi kheri kwake na kama mtafunga ni bora kwenu ikiwa mnafahamu". (184) Mwezi wa ramadhani ndio iliteremshwa Qur'ani ndani yake hali ya kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi na uongofu na upambanuzi. Basi atakeye uona miongoni mwenu mwezi na afunge na atakaye kuwa mgonjwa au akawa safarini alipe katika siku zingine, ALLAH anakutakieni wepesi na wala hakutakieni uzito,

na mkamilishe hizo siku na mumtukuze ALLAH kwa yale aliyo kuongozeni ili mpate kushukuru. (185) (Al-baqara:183-185), Na ikawa ni Nguzo ya Nne miongoni mwa nguzo za uislamu (Kufunga)

Na zikafungamana sheria nyingi na sawaumu na sheria zake, na wakawa wakubwa na wadogo wakiupa kipaumbele mwezi mtukufu, na wakiuwekea Nembo yake maalumu, ikiwa ni kufunga na kusimama usiku na kusoma na kujishughulisha na elimu na masomo mbali mbali hadi hivi sasa.

Kama ambavyo imefungamana na kuwepo usiku wa lailatul Qadri (Usiku wenye cheo)²⁴⁷amesema ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ﴾ [القدر: 1]

"Hakika Sisi Tumeiteremsha Qur'ani katika usiku wa cheo na utukufu", Nao ni moja wa masiku ya mwezi wa Ramadhani. [Suratil Qadri :1] Na ukawa Umma unajipinda katika usiku huu kwa kufanya matendo mema ikiwepo kusimama na kutoa sadaka na kuunga udugu na kukaa Itikafu.

Na matokeo yakawa Funga ni yenye kuendana na kisimamo na kuisoma cha Qur'ani na ukawa Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa Kumtii Allah na kujikurubisha na kutoa sadaka na kufanya mambo mengine ya Kheri, na hivi ndivyo yatakikana katika umma wa kiislamu mpaka Mwenyezi Mungu atakapoichukua Ardhi na vilivyomo ndani yake.

Na mwenye kufuatilia hali za waislamu katika Mwezi wa Ramadhani, na mabadiliko yanayowatokea, na wema wa mtu

²⁴⁷ Angalia Bin Kathiir Tafsiri yake juzuu ya 2/2013.

mmoja mmoja na wote kwa ujumla, na namna wanavyotoa, atafahamu umuhimu wa nembo hii katika maisha ya umma .

KUGEUZWA MUELEKEO WA KIBLA:

Ulikuwa Muelekeo wa waislamu kabla ya kuhama Mtume na baada ya kuhama ni moja kwa moja unaelekea Baitil Maqdis (Jerusalem) -Palestina-, na kwenye mwezi wa Shaban katika mwaka wa pili tokea kuhama Mtume, Mwenyezi Mungu alibadilisha muelekeo wa waislamu, kutoka kuelekea Msikiti wa Aqswaa (Jerusalem) na kuelekea msikiti mtukufu wa Makka, (439) katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ
الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ وَإِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
رَبِّهِمْ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ﴾ [البقرة: 144]

"Hakika tunaona kugeuka geuka uso wako mbinguni, hakika tutakugeuza -kuelekea- Kibla utakacho kiridhia, basi elekeza uso wako upande wa msikiti wa Makkah na popote mtakapo kuwa elekezeni nyuso zenu upande huo, na hakika wale ambao walio pewa kitabu wanatambua kuwa ni ukweli kutoka kwa Mola wao na hakuwa ALLAH mwenye kughafilika kwa yale wanayo yafanya" [Al-baqara: 144]

Na kwa hakika walijaribu mayahudi na wenzao kuwafitinisha waislamu kwenye kugeuza Kibla, Mwenyezi Mungu -kutakasika na machafu ni kwake akawaita -Wapumbavu:

﴿سَيَقُولُ السُّفَهَاءُ مِنَ النَّاسِ مَا وَلَّيْتُمْ مَا وَلَّيْتُمْ عَنْ قِبَلَتِهِمُ الَّتِي كَانُوا عَلَيْهَا قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ
وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ﴾ [البقرة: 142]

"Karibu watasema wapumbavu miongoni mwa watu ni kipi kilicho wageuza kuacha kibla walichokuwa wanageukia, sema

upande wa Mashariki na Magharibi ni wa ALLAH anamuongoza amtakaye kwenye njia iliyo nyooka". (Al-baqara: 142) Na jambo la Kibla kwa waislamu siyo jambo la kulichukulia mzaha, hivyo katika kila zama na kila mahala wanajitahidi kuufuatilia na kujua muelekeo wake kabla ya kila swala, na msafiri katika miji tofauti wanakuta Mihirabu za kila msikiti zimeelekezwa upande wa Kibla ambacho ameamrisha Mwenyezi Mungu kuelekea huko.

﴿وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ فَلَا تَحْشَوْهُمْ وَاَحْشَوْنِي وَلَا تَمَّ نِعْمَتِي عَلَيْكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَبُونَ﴾ [البقرة: 150]

"Na popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande wa msikiti wa Makkah ili isiwe kwa watu hoja juu yenu isipokuwa kwa wale walio jidhulumu miongoni mwao basi msiwaogope niogopeni mimi na ili nitimize neema zangu juu yenu na mpate kuongoka". [Al-baqara: 150).

Na kwa hivyo tunakuta katika zama zetu hizi viashiria vya hiyo Alkaaba katika baadhi ya nyumba za kulala wageni na baadhi ya Viwanja vya Ndege na kwingineko katika nchi za kiislamu na nje yake, na kimekuwa Kibla ni nembo ya waislamu na ni takwa lao katika kila mahala.

MWANZO WA VIKOSI NA VITA:

Makuraishi hawakusimama na kuacha kuwaudhi waislamu baada ya kuhamia Madina, na walikuwa akiwafunga baadhi yao katika mji wa Makkan wakiwatisha Answar na wakiwazuia kuingia katika mji wa Makka, na wakiwaudhi wenye kutumbukia kwenye mikono yao, na vitisho vyao viliwafikia muhaajiriina katika mji wa Madina, pale walipo wanyakua baadhi ya watu wa Makka wakiwa Madina (440) na walikuwa wakitangaza mfululizo wa matukio hayo, na

wakiwatisha kuhusu Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na kila mwenye kumfuata.

Na katika hali hii iliteremka Idhini ya kupigana vita, na jambo likawa ni lenye kuhitajia maandalizi ikiwemo kuandaa Nafsi na silaha na wanyama na kuchukua mafunzo na ujuzi, kisha kukaanzwa jambo lijulikanalo kama Vikosi na Vita vya Mtume (441)

Na uadui wa makuraishi kwa waislamu ulikuwa wazi wazi, lakini waislamu hawakubakia kama waliofungwa mikono, kama makuraishi walivyowadhuru waislamu na wakayadhuru maslahi yao, kwa hakika waislamu walikwenda mbio baada ya kupata Ruhusa ya kupigana nao kuharibu maslahi ya makuraishi, pale ambapo zilikuwa Biashara zao zikipitishwa karibu na mji wa Madina, basi waislamu wakachagua kuweka mpaka njia wazipitazo na kuwatia dhiki njiani, na kuwaonyesha makuraishi uwezo wa waislamu kutia vizuizi ujanja na uwezo wa kuwadhuru maadui wao.

Vilikuwa Vikosi vimeandaliwa kijeshi, na kwa ujanja wa kijeshi kwa ajili ya kuwa Askari wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-ukiongezea malengo yake maalumu yaliyokusudiwa wakati huo.

Kama ilivyokuwa wakati huo huo, wakishughulishwa vijana na watu wazima kupata kazi kwa kutumia nguvu zao, na hasa hasa watu wa Makka ambao walifika Madina na wahakuwa baadhi yao na kazi maalumu inayowashughulisha, ukiongezea kushughulishwa na mafunzo kwa viongozi na wasiokuwa viongozi kwenye majukumu ya kiaskari, na machungu na safari na kubeba majukumu na kupigana na kujiandaa kwa hayo.

KIKOSI CHA KWANZA: (442)

Vinazingatiwa vikosi na Vita vilivyotangulia kabla ya vita vya Badri kubwa, ni vita vya utangulizi, vikafuatiwa na Idhini ya kupigana, na wala haikuonyesha ushindi wa waislamu, na ilikuwa ni mbinu za

kivita na harakati maalumu zilizoitangulia vita ya Badri, na miongoni mwa vikosi muhimu ni:

Kikosi cha Hamza Bin Abdil Muttwalib (Saiful Bahri):

Ilitokea katika mwezi wa Shawwal katika mwaka wa kwanza tangu kuhama Mtume baada ya miezi saba tangu kuhama kwa Mtume alimuweka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kiongozi wa kwanza wa jeshi la waislamu, kwa uongozi wa Hamza Bin Abdil Muttwalib, na walikuwa wafuasa wake ni watu wa Makka -Radhi za Allah ziwe juu yao-, (443) na kwa hakika Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- alilisindikiza jeshi yeye mweyewe, na lilikuwa lengo la jeshi ni kukatisha msafara wa Makuraishi uliokuwa ukija kutokea Sham kwenda Makkah, msafara huo ulikuwa na watu mia tatu katika makuraishi, akiwepo Abuu Jahal (Amrou Bin Hishaam) na inasemekana walikuwa wachache zaidi ya hapo, na hakika alielekea Hamza na jeshi lake upande wa chini katika sehemu za Juhaina, na wala hapakutokea vita yoyote kati ya pande mbili, kwa sababu ya kuingilia wakubwa wa makabila katika kitongoji na huenda katika hilo kulikuwa na maslahi. (444)

Kikosi cha Ubaida bin Haarith bin Abdil Muttwalib -Radhi za Allah ziwe juu yake-

Mtoto wa baba yake mdogo Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ni mmoja kati ya mashahidi wa vita vya Badri, baada ya hapo. Kikosi hiki kilikuwa katika mwezi wa shawwal mwaka wa kwanza tangu kuhama kwa Mtume.

Jeshi lake lilikuwa na wafuasi themanini na wote ni watu wa Makka-Radhi za Allah ziwe juu yao, (446) na akalikabidhi jeshi hilo Bendera nyeupe, na ulikuwa muelekeo wake ni upande wa Raabigh, (447) ili kuukinga msafara wa makuraishi msafara uliokuwa unaongozwa na Abuu Sufian Bin Harbi, na Ikrima Bin Abii Jahal, na wakashambuliana pande mbili na wakatupiana mishale, na wala

haikutokea vita ya moja kwa moja kati ya pande mbili, na kwa hakika alikuwa Saad Bin Abii Waqqas akitupa mikuki yake kwa weledi namna ambayo ilisababisha idadi kubwa ya washirikina wapatwe na majeraha, na alikuwa wa kwanza kutupa mkuki na akamwaga Damu katika njia ya ALLAH (448)

Na kulikuwa katika msafara wa washirikina kuna waislamu wawili, wakawakimbia makuraishi na wakakutana na Maswahaba wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake-²⁴⁸

Kikosi cha Abdullahi Bin Jahshiy kuelekea (Nakhlat) (450)

Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-aliwatuma watu kumi na mbili miongoni mwa watu wa Makka katika kikosi cha Nakhla wakiwa pamoja nao watu wa Makka wapatao themanini (451)

na akampangia muelekeo, na akampa waraka, na akamuamrisha kuwa asiufungue isipokuwa baada ya kwenda siku mbili katika upande aliompangia, na baada ya mwendo wa siku mbili, alitazama Abdullahi Bin Jahshi katika waraka wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ghafla akaona humo kumeandikwa: "Utakapoangalia katika waraka huu basi nenda mpaka ufike sehemu iliyopo kati ya Makka na Twaaf itwayo Nakhla, basi uwafuatilie huko makuraishi, na ujue kuhusu habari za huko" (452)

Na alipousoma waraka, akasema: Nimesikia na nimetii ewe Mtume wa ALLAH, kisha akawapa habari watu wake kile alichomuarisha Mtume wa ALLAH- Sala na amani ziwe juu yake- katika waraka wake, na akawaeleza kuwa Mtume wa ALLAH amemkataza kuwa asimchukie yeyote katika watu wake mwenye kwenda naye na akawaambia: "Yeyote miongoni mwenu mwenye

²⁴⁸ Tazama: Bin Saad Al-twabaqaatil Kubra, juzuu ya 2/7.

kutaka kufa shahidi na anapenda kufa shahidi basi na aende, na mwenye kuchukia hili basi na arudi, ama mimi ni mwenye kwenda kwa amri ya Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-, Basi akaenda na wakaenda waliokuwa pamoja naye, na wala hakukataa yeyote katika wao.(453)

Na Abdullahi Bin Jahshi na waliokuwa pamoja naye katika watu wa Makka walifuata njia kuelekea Nakhla. (454).

Na akafika Abdullahi Bin Jahshi mpaka Nakhla sehemu aliyoikusudia kwa amri ya Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- basi ukawapita msafa wa Makuraishi ukiwa umebeba Ngozi na Zabibu, na biashara ya makuraishi kutoka Twaif, na katika msafara huo kulikuwepo na Amru Bin Al-hadhramiy na walikuwa wapo mwisho wa mwezi wa Rajab na mwezi huo ni katika miezi mitukufu kwa warabu. Na kikosi kikashauriana kuhusu kuwaua au kuwaacha kwa kuogopea kupigana katika miezi mitukufu, na wakati huo huo waliogopa kutoingia msafara katika mipaka ya Haram nao walikuwa karibu na mji wa Makka, au wakaogopea kuwa makuraishi wangekabiliana nao kwa mashambulizi dhidi yao jambo lao likasimamia kwenye kuushambulia msafara wa makuraishi, wakakubaliana kuwapiga, wakaweza kumuua Abdullahi Binil Hadhramiy, (455) na wakatekwa watu wawili, na wakaswaga msafara na mateka wawili mpaka katika mji wa Madinat Munawwara, na walipofika katika mji wa Madina watu walizungumzia kuhusu kupigana katika mwezi mtukufu akasema Mtume -Sala na amani ziwe juu yake: "Sikukuamrisheni kupigana katika mwezi mtukufu" Basi wakatolewa mikononi mwa Abdullahi Bin Jahshi na waliokuwa naye miongoni mwa mateka na wakadhania kuwa wao wameshaangamia, na ndugu zao miongoni mwa maswahaba wakazidi kuwakemea, na wakaanza wanafiki na washirikina kusambaza habari hizo, na wakapiga kampeni dhidi ya msafara wa waislamu na kuwa waislamu wamehalalisha kupigana miezi mitukufu. Na katika hali hii ngumu kwa watu wa kikosi

iliteremka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ وَصَدٌّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفْرٌ بِهِ
وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ وَلَا يَزَالُونَ
يُقْبِلُونَكَ حَتَّى يَرْدُوكُمْ عَن دِينِكُمْ إِنِ اسْتَظَلُّوا وَمَن يَرْتَدِدْ مِنكُمْ عَن دِينِهِ فَمَا كَانَ مِن
كَافِرٍ فَأُولَئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢١٧﴾
[البقرة: 217]

"Wanakuuliza kunako kupigana ndani ya miezi mitukufu, waambie kupigana ndani ya miezi mitukufu ni jambo kubwa, na kuwazuia watu kuto ifuata njia ya ALLAH ni kumpinga ALLAH, na msikiti wa Makkah na kuwatoa watu wake ni jambo kubwa zaidi mbele ya ALLAH na fitina ni kubwa kuliko kuua na hawato acha kuwapigeni mpaka wakutoeni kwenye dini yenu kama wakiweza na atakaye ritadi -kuacha dini ya uislamu- miongoni mwenu akaacha dini yake kisha akafa hali ya kuwa ni kafiri basi hao yameporomoka matendo yao katika dunia na akhera na wao ni watu wa motoni wao wataishi humo milele". [Al-baqara: 217].

Na kwa hakika alifurahishwa, Mtume wa ALLAH -Sala na amani ziwe juu yake- na wakafurahishwa maswahaba kwa kuteremka hizi Aya, na kikaondoka kwa Abdullahi Bin Jahshi na wenzake mambo yaliyokuwa wakiyahisi miongoni mwa huzuni, (456) basi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akaichukua ngawira na akailekeza shemu husika, kisha akakubali fidia ya mateka wawili wa Kikuraishi.(457)

Kwa Angalizo ni kuwa ule msafara wa kwanza walikuwa vinara wa jeshi lake ni watu wa Makka waliohamia Madina, na wengi wao walikuwa ni makuraish na viongozi wake pia ni maquraish, ni miongoni mwa watu wa karibu kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, na wakaelekea ili kuudhuru msafara wa kibiashara wa makuraishi na kuwatia dhiki wafanya biashara na watu watokanao

na makuraishi, na hao ndio ambao waliwaudhi waliohama Makka na wakawatoa kwenye majumba yao pasina haki wakateka mali zao na majumba yao na wakapupia Muhaajiriina kushiriki katika hilo, na walikuwa ni vinara wa kile kikosi. (458)

Kwa hakika miongoni mwa walioshiriki katika waislamu ilikuwa ni kwa hiyari yao, na hakuna yeyote aliyewalazimisha kushiriki, na kwa kuongezea nikuwa Maanswari watu wa Madina hawakushiriki katika muda huu, na huenda Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alitaka kuwashughulisha watu wa Makka waliohamia Madina ambao ilizidi idadi yao, na wakati huo huo kuwafundisha na kuwajuzi njia na sehemu zinazouzunguka mji wa Madinat munawwara, na ambazo huenda sehemu zikawa ni ngeni kwa baadhi yao .

Kama ambavyo watu wa Madina walikua wakishughulisha na kilimo na jamaa zao, na wakati huo huo wanasimamia ulinzi wa mji wa Madina na ulinzi wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akiwa Madina, ikiwa ni kutekeleza ahadi waliyowekeana katika Uungaji mkono wa Aqaba ya mara ya pili.

Na hapana shaka kuwa hiki kikosi kilipata nguvu na mafunzo na ukakamavu, na kujua njia na makabila ikiwa ni maandailizi ya kinafsi na kiaskari ilikuweza kushiriki na Mtume kwenye vita zake.

Na kwa hakika mafanikio yalipatikana katika kuulenga msafara wa Makuraishi, na kuwaonyesha hatari ambayo inaweza kuwakuta ,na pia uwezo wa waislamu kuwaletea fujo kama vile Makuraishi walivyowafanyia fujo waislamu na wakazi wa Makka na wale wanaopita katika mji wa Makka, na kuizuia fitina kwenye dini yao.

Na kwa hakika walikutwa baadhi yao karibu na Makka sehemu iliyopo kati yake na mji wa Twaif, na baadhi yao kwenye pwani ya magharibi na kaskazini mwa mji wa Makka, na kuuzunguka mji wa

Makka katika kila upande, na hasa hasa kaskazini na mashariki na magharibi.

VITA VYA KWANZA:

Kabla ya vita vya Badri ambayo huzingatiwa kuwa ni kipambanuzi kati ya matukio mengi ya Historia ya Mtume, bali katika Historia ya ulimwengu wote, alisimama Mtume kupigana vita mbali mbali alizoziongoza yeye mwenyewe, ukiongezea na vikosi ambavyo vilivyotumwa vikiongozwa na aliyekiongoza miongoni mwa maswahaba -Radhi za Allah ziwe juu yao-na yalikuwa malengo yake katika awamu hii ni yenye kukaribiana, pamoja na kutilia umuhimu kukata biashara ya makuraishi kwenda nje, na kuikinga misafara yake ya kibiashara na watu wake, na kuwaonyesha makuraishi nguvu za waislamu na uwezo wao wakuzihami nafsi zao, bali na kuzirudisha mali zao zilizochukuliwa Makka.

VITA VYA AB-WAA: (459)

Na huitwa (Buwaat), (460) katika mwezi wa Swafar katika mwaka wa pili wa hjiaria karibia miezi kumi na mbili tangu kuhama Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**. Na kwa hakika alibeba bendera yake Mtume, Hamza Bin Abdul Muttwalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-(461)

Na akatoka na Muhaajiriina na ukawa muelekeo wake Mtume-Rehema na amani ziwe juu yaku-ili kuuzuia msafara wa makuraishi, nao msafara huo unapita upande wa Mlima Radh-wa (462) katika majumba ya Juhaina.

Na alikuwa kiongozi wa msafara wa Makuraishi ni Umaiyyat Bin Khalaf, naye ni katika maadui wakubwa wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-

Na wala hakukutana Mtume na vitimbi wala mapigano, na katikati ya vita Mtume -Sala na amani ziwe juu yake alikutana na

Dhwamrat kutoka katika kabila la Abdumanaat na akafunga nao makubaliano.(463)

Na alirudi Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- na wala hakupatwa na mitihani yoyote (464)

VITA VYAASHIRA :[465]

Nayo ni sehemu iliyopo pande za Yan-buu magharibi mwa mji wa Madina, ni sehemu ya kabila la banii Mudlaji, na mtume alitoka kwenda huko akiwa na mswahaba wake wapatao mia mbili, na akaibeba bendera yake Baba yake mdogo Hamza Bin Abdul Muttwalib-Radhi za Allah ziwe juu yake- na ilikuwa kutoka kwake ni katika mwezi wa Jumadal uula katika mwezi wa pili tangu kuhama Mtume, (466) na wala hakuna yeyote aliyechukia kutoka naye.

Na lengo la msafara lilikuwa ni msafara mkubwa wa makuraishi, msafara ambao ulikuwa umekusanya mali nyingi ukiwa unaelekea Sham, na kwa hakika msafara ulimpita, na akafika sehemu za banii Mudlaji nao ni washirika wa kabila la Dhwamrat na akawaaga Mtume-Sala na amani ziwe juu yake(467)

VITA VYASAF-WAN: (BADRI YA KWANZA): [468]

Wakati alipofika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kutoka katika vita vya Ushaira kwa masiku machache tu, Kurzi Bin Jaabir Al-fihri alivamia mifugo ambayo inatokea Madina kwa ajili ya malisho ya nje ya mji wa Madina huitwa mfugo huyo (Sarha), (469) na akapora, basi Mtume wa ALLAH kwa haraka akatoka nyuma yake akiwa na kundi la waislamu, na akaibeba bendera yake Ally Bin Abi twaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-na Mtume akakutana na Kurzi Bin Jaabir Al-fihriy, lakini akamchenga, na akafika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- Saf-waan upande wa Badri kisha akarudi Madina, na Kurzi alisilimu baada ya hapo na ukawa mzuri uislamu wake na akapigana vita pamoja na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na akauliwa shahidi wakati wa ufunguzi wa mji wa Makka.(470)

VITA VYABADRI (TAREHE: 17 RAMADHANI MWAKA 2H) [471]

Huzingatiwa viti hii ni katika vita kubwa katika Historia ya uislamu kwa ujumla, pale alipoiita Mwenyezi Mungu -Mtukufu- Siku ya Upambanuzi katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ
وَالْمَسْكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ إِن كُنْتُمْ ءَامَنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ التَّفَاقُ
الْجُمُعَاتِ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾ [الأنفال: 41]

"Na tuliyayateremsha kwa Mja wetu siku ya kipambanuzi siku ambayo yalikutana majeshi mawili ya waislamu na makafiri, na ALLAH juu kila kitu ni muweza" [Al-anfaal: 41] Na imepokelewa kuwa vita hiyo imetajwa kwenye Qur'an katika maneno yake Mtukufu:

﴿يَوْمَ نَبُطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرَىٰ إِنَّا مُنتَقِمُونَ﴾ [الدخان: 16]

"Siku tutakayoshambulia mashambulio makubwa, bila shaka sisi ni wenye kutesa". [Al- Dukhaan: 16]

Na miongoni mwa sababu ya vita hiii ni kuwa Mtume Sala na amani ziwe juu yake alikuwa akifuatiia msafara wa Makuraish na akiwavizia, kwani wao walimuudhi Mtume na wakamtoa na maswahaba wake kwenye majumba yao, na wakawapokonya mali zao na wakafungwa baaadhi yao na wakawaadhibu, basi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akajua kuwa msafara wa Makuraishi unakuja kutoka Sham kwa kufuata njia ya Makkana msafara huo upo karibu na mji wa Madina, basi Mtume akawaita waliopo karibu miongoni mwa maswahaba ili watoke pamoja naye, (472) na akatoka pamoja nao kwa haraka pasina kuwa na maandalizi kabla ya hapo, na walikuwa wakifuatana na Mtume (Watu mia tatu na kidogo (473) wengi wao walikuwa wakitembea kwa miguu, na hawakuwa isipokuwa na Farasi wawili na Ngamia sabini, (474)

walikuwa wakidhani kuwa watakuta msafara na kuwa hapatakuwa na mapigano, kwa hivyo wao hawakuwa wamejiandaa maandalizi yaliyokamilika kwa ajili ya vita.

Na alikuwa kiongozi wa msafara wa Makuraishi ni Abuu Sufiani Bin Harbi, kwa kuchukua tahadhari na kwa kuogopea mali zilizokuwapo kwenye msafara ambao ulikuwa pamoja naye, kwa hivyo alikuwa akitafuta habari kwa kuwaogopa waislamu, na kajua kuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ametoka kwa ajili ya kumtafuta yeye na Msafara aliokuwa nao, basi akabadilisha nia ambayo alikuwa akiifuata na akaenda na msafara kwa kupita karibu na pwani katika njia ambayo hawakuwa waislamu wanatarajia, na wakati huo huo alituma kwa Makuraishi wa Makka akiwahamasisha kuukomboa Msafara wake kutoka kwa waislamu, na likatoka jeshi la Mkquraishi ili kuuokoa msafara- Kwa madai yake- jeshi likiongozwa na Abuu Jahal Amrou Bin Hishaam, na wakatoka wakubwa wanaume wakikuraishi na mashujaa wake, na viongozi wa makafiri katika makuraishi (475) Na akafaulu Abuu Sufian kuuokoa msafara kutoka kwenye mikono ya waislamu, na wakakaribia Makka, akiwa na uhakika wa usalama wa msafara wake, na akatuma muwakilishi kwenda Makka, akiwapa habari juu ya kufanikiwa msafara, na akiwataka kurudi katika mji wa Makka.

Na akatamka wazi wazi Abuu Jahal kiongozi wa Makafiri wa Kikuraishi kushindana na kufanya Kiburi na majivuno, na akatangaza kuwa yeye hatorudi mpaka anywe maji ya Badri, na alishe Chakula na kunywa Pombe na kuimba nyimbo na warabu wasikie mwenendo wao, na hilo liitakuwa ni tishio kwao wakati wote, na hili ndilo liloashiriwa kwenye kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بَطْرًا وَرِشَاءَ النَّاسِ وَيَصُوتُونَ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ

وَاللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ﴾ [الأنفال: 47]

"Na wala msiwe kama wale walio toka kwenye miji yao kwa majingambo na kujionesha kwa watu na wakizuia watu katika njia ya ALLAH na ALLAH kwa wanayo yafanya ni mwenye kuyazingira" (Al- an-faal:47) Na wakaendelea na safari yao mpaka katika mji wa Badri kwenye lengo lilokusudiwa (476)

Alikuwa Abuu Jahli anajua ukweli wa Mtume-Sala na mani ziwe juu yake -na kwa hakika watu wake walimuambia wakati akienda kwa Mtume wa ALLAH-Sala na mani ziwe juu yake- katika siku ya Badri: "Hivi waonaje kwenda kwako kwa Muhammad hivi unajua kuwa yeye ni Nabii?" akasema: "ndiyo, najua lakini ni wakati gani tulishawahi kuwa wafuasi wa Abdu Manafi". (477)"

Alijua Mtume kuhusu kuondoka kwa makuraishi, basi akawakusanya maswahaba na kuwataka ushauri, na alikuwa Mtume-Sala na mani ziwe juu yake- kahifadhiwa na makosa akiwataka ushauri maswahaba wake wakati wote katika mambo muhimu, miongoni mwa mambo hayo ni mambo makuu mawili: Jambo la kwanza ni kutengeza safu ya waislamu na kuwa kitu kimoja, na kuzitegeneza fikra zao, nalo ni jambo muhimu sana hasa hasa pamoja na watu wa Madina katika ngazi hii, na wao ni wenyeji, na Jambo la pili kufikia maamuzi sahihi na ya Busara zaidi.

Mtume akatupa jambo kwa kikundi cha maswahaba zake waliokuwa wakifuatana naye huku akiwaambia: "Nitazameni mimi enyi watu", na wakaongea kundi la Muhaajiriina akiwepo Abuubakari na Omar-Radhi za Allah ziwe juu yao- na akawa miongoni mwa wenye kuongea ni Mikdad Bin Amrou amabaye alisma: "Ewe Mtume wa ALLAH nakuapia kwa ALLAH kuwa sisi hatusemi kama walivyosema wana wa Israil kumwambia mussa, amasema ALLAH Mtukufu:

﴿قَالُوا يَمُوسَىٰ إِنَّا لَن نَّدْخُلَهَا أَبَدًا مَّا دَامُوا فِيهَا فَأَذْهَبَ أَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَتِلَا إِنَّا هَهُنَا

قُلْعِدُونَ ﴿٤٧﴾ [المائدة: 24]

"Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane sisi tutakaa hapa".
[Al-maida: 24] ,²⁴⁹Lakini Nenda wewe na Mola wako mkapigane hakika sisi tupo pamoja nanyi tunapigana, Na tunamuapia yule ambae amekutuma kwa haki, lau ungetupeleka sehemu ya mbali tungepigana tukiwa pamoja nawe mpaka ufikie mafanikio" (479) Basi Mtume akumuomba Dua Abuubakari kisha akasema mara nyingine ((Nipeni ushauri enyi watu)) na alikuwa Mtume akikusudia Ushauri wa watu wa Madina kwa kuwa wao ndiyo wenyeji, na ndiyo wengi, na alikuwa Mtume anataka kuivuta mioyo yao na kuwakinaisha kwa ajili ya kuhifadhi safu ya waislamu, na huu ndiyo ulikuwa mwanzo wa kukutana Mtume na jeshi lake la watu wa Makka na Madina, na kati ya Makuraishi na viongozi wao wa kikafiri,akitangaza Mtume vita na kifo, basi akajitokeza Saad Bin Muadh-Radhi za Allah ziwe juu yake- akisema: "Kana kwamba unatukusudia sisi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Akajibu Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**:- "Ndiyo", basi Saad akajibu kwa kumsifu Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake, na akawakumbusha kuwa wao wapo kwenye ahadi yake na akasema: 'Ewe Mtume wa ALLAH pitisha ulilokusudia namuapia yule ambaye amekutuma kwa haki lau ungetuonyesha bahari kisha ukazamia katika bahari hiyo tungezamia bahari hiyo sisi pamoja nawe na asingepinga mtu yeyote kati yetu, na wala hatuchukii kukutana na maadui wetu kesho na sisi ni wenye kuvumilia katika vita, tutakuwa wakweli wakati wa mapambano huenda ALLAH

²⁴⁹ kutoka katika Aya (24) katika surat Al-maidah.

akakuonesha toka kwetu sisi jambo litakalo kuwa kitulizo cha macho yako, basi nenda kwa Baraka za ALLAH"(480)²⁵⁰

Basi akafurahishwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake na maneno ya Saad hivyo akamuomba Dua yeye Saad na akawaomba watu wa Makka na Madina, na akapata utulivu kutokana na msimamo wa jeshi lake katika kukutana na maadui.

Basi akaenda na akiwa pamoja na maswahaba zake, naye akiwaambia Nendeni na ninawapa bishara njema kwa hakika Mwenyezi Mungu amenipa ahadi ya moja kati ya makundi mawili, **na ahadi hiyo ni kwa kusadikisha kauli yake Mtukufu:**

﴿وَإِذْ يَعِدُكُمُ اللَّهُ إِحْدَى الطَّائِفَتَيْنِ أَنَّهَا لَكُمْ وَتَوَدُّونَ أَنَّ غَيْرَ ذَاتِ الشَّوْكَةِ تَكُونُ لَكُمْ وَيُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَيَقْطَعَ دَابِرَ الْكَافِرِينَ﴾ [الأنفال: 7]

"Na pindi ALLAH alipo wapa ahadi kuwa moja ya makundi mawili litakuwa kwenu nyinyi na mkapenda kundi lisilo kuwa na nguvu liwe upande wenu, na Mwenyezi Mungu anapenda ahakikishe haki kwa maneno yake, na aikate mizizi ya makafiri". [Al-anfaal: 7] Basi akaenda Mtume Sala na amani ziwe juu yake- na waliokua pamoja naye wakielekea upande wa Badri, na wao wakiwa na yakini kuwa wataukuta msafara wa Makuraishi au jeshi lake. Na waislamu wakafikia karibu na Badri nao wakiwa wanapeleleza habari kuhusu maadui zao, na Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake alijua kuwa watu hao idadi yao wapo kati ya mia tisa mpaka elfu moja, na wakapata taarifa ya uwepo wa majemedari wa kikuraishi katika jeshi, akasema Mtume-Rehema na amani ziwe juu

²⁵⁰ Tazama kuhusu Ushauri huu katika kitabu cha Siirat Annabawiyat cha Bin Hishaamjuzuu ya 2/215na linganisha na hadihi iliyopo katika kitabu cha Bukhari (Fahul Baar juzuu ya 15/151.)

yake-: "Hii ndiyo Makka imewaletea vigogo wake wote" Na akawa na yakini Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuwa makabiliano yatakuwa na jeshi la makuraishi wenye silaha na mashujaa wa Makka na wapanda farasi wake, nakuwa msafara umekwishawaacha.

Na akaja Hubabu Mundhir kwa Mtume Sala na amani ziwe juu yake na walikuwa waislamu wamefikia karibu zaidi na kisima cha maji kisha akasema kwa adabu kumwambia Mtume akimuekezea mtazamo ulio wa sawa "ewe Mtume wa ALLAH waonaje hii sehemu ndio amekuelekeza ALLAH ufikie hapa au ni mtazamo na mbinu kivita? Akasema Mtume Sala na amani ziwe juu yake: "Bali ni mtazamo na ni mbinu za kivita" Akasema: Ewe Mtume wa ALLAH hakika sehemu hii siyo pahala pa kufikia, watoe watu mpaka wasogee karibu na maji, kisha tuteremke na tuifunge sehemu ya nyuma ya mdomo wa kisima kisha tujengee juu yake birika na tulijaze maji na tunywe na wao wasipate nafasi ya kunywa, Mtume akamuomba dua na akasema: "Hakika umetoa mtazamo mzuri" {481} na ulikuwa huu ndio msimamo wa Mtume muongozaji ni somo kwa kila kiongozi kusikiliza mtazamo wa askari wake kufikia malengo mazuri na kuchukua sababu za kidunia na za kikawaida pamoja na kumtegemea ALLAH, na ndio msingi katika kila harakati zake Mtume Sala na amani ziwe juu yake.

Na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akitoa habari ya sehemu watakazofikia idadi kubwa ya wakubwa wa kikuraishi, na akiwaonyesha Maswahaba sehemu ambazo watafia wakiwa mashahidi (482) jambo ambalo liliwazidishia kuwa na uhakika na wao kupata ushindi kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Na Maswahaba walimjengea Mtume Sala na amani ziwe juu yake kijumba akijetenga humo baadhi ya nyakati kwa ajili ya kuomba Dua na kuswali (483) licha yakuwa kwakwe mwanzo wa Safu ya mapambano, kwa hakika alikuwa Mtume-Sala na amani ni shujaa.

Walifika makuraishi kabla ya vita kuanza, na walipowaelekea waislamu Mtume-Rehema na amani ziwe juu- yake- akasema: "Ewe Mola wangu hawa ni makuraishi kwa hakika wamekuja na viburi vyao, na ufahari wao, wanakufanyia wewe uadui na wanamkanusha mtume wako, hivyo naomba msaada wako uliyoniahidi, ewe Mola wangu Jaalia maangamizi yao yawe mapema asubuhi" (484)

Walijaribu baadhi ya Makuraishi wenye Busara kuwakatisha tamaa ya kupigana watu wao na wakiwakinaisha kurudi katika mji wa Makka, lakini Abuu Jahal na watu mfano wake miongoni mwa viongozi wa kikafiri waliwaharibu na wakawakinaisha Makuraishi kwa kuwapinga na kukabiliana nao kwa ukali. Na lilifanyika hili ili Mwenyezi Mungu apitische jambo lake ambalo alikuwa amelipanga liwe.(485)

Waislamu walilala usiku wa kuamkia vita vya Badri wakimuomba ALLAH na kunyenyekea kwake kwa kuomba nusura na kuwashinda Maadui, basi ALLAH akateremsha utulivu wake kwa juu yao, na wakawa ni watulivu na ukawapata usingizi, na ALLAH akateremsha Mvua nyepesi, na katika hilo anasema ALLAH Mtukufu:

﴿إِذْ يُغَشِّيكُمُ اللَّعَاسُ أَمَنَةً مِنْهُ وَيُنزِلُ عَلَيْكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لِيُطَهِّرَكُم بِهِ وَيُذْهِبَ عَنْكُم رِجْزَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَى قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ الْأَقْدَامَ﴾ [الأنفال: 11]

"Kumbukeni pindi ALLAH alipo wafunikeni kwa usingizi hali ya kuwa ni amani kutoka kwake na anateremsha kutoka mawinguni maji ili awasafisheni kwa maji hayo na ondoshe kwenu nyinyi uchafu wa shetani na afungamanishe juu ya nyoyo zenu na azithibitisha nyayo zenu". [Al-anfaal :11] Na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu- yake- katika usiku huo akiswali na akilia akinyenyekea kwa ALLAH kwa kuomba Dua ya kuwanusuru waislamu, na ilikuwa katika Dua yake aliyoiomba katika kile kijumba wakati wa usiku au asubuhi yake: "Ewe Mola wangu wa haki ninakumbushia ahadi yako na agano lako, Ewe Mola wangu wa haki

ikiwa utataka basi hautaabudiwa baada ya leo milele". Abubakari akamshika kwa mkono wake na akamwambia: "Inakutosha ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu umemsisitiza Mola wako vya kutosha" akatoka akiwa ameshika ngao huku akisema:

"Utashindwa mkusanyiko wa makafiri wa Makkah mbele ya Waislamu na watakimbia". (45) Na hili lilitokea siku ya vita vya Badri. "Bali saa kiyama ndio ahadi yao, na saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi"²⁵¹. [Alqamar: 45-46] (486)

Ama washirikina wa Kikuraishi walikuwa wakila usiku kucha na kunywa pombe na wakiimba nyimbo, na wakijifaharisha kwa nguvu zao, na vitu walivyokuja navyo na wakiweka wazi ukafiri wao na ushirikina wao na kumpinga kwao ALLAH na Mtume wake, na alikuwa Abuu Jahal akijiomba mabaya dhidi yake kwa kusema:

﴿إِنْ كَسَفَتْحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ وَإِنْ كَذَبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِنْ تَعُدُّوا نَعْدَ وَلَنْ تُغْنِيَ عَنْكُمْ فِئَتُكُمْ شَيْئًا وَلَوْ كَثُرَتْ وَأَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ﴾ [الأنفال: 19]

"Kama mnataka hukumu basi hukumu umekwisha kujieni. Na mkiacha (enyi makafiri) basi ni kheri kwenu. Na kama mtarudi na sisi tutarudi. Na jeshi lenu halitokufaeni kitu, hata likiwa kubwa. Kwani hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na waumini". (Al-anfaal: 19)²⁵²

Na asubuhi ya siku ya Vita Waislamu waliswali nyuma ya Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-,na baada ya swala

²⁵¹ Ameipokea Bukhari : (Fathul Baar) juzuu ya 18/254.

²⁵² Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 184.

aliwahutubia na akawahamasisha kupigana vita nakuwa na subira.(488)

Kisha akatoka mwenyewe Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwa ajili ya kupangilia Safu ya waislamu na kuwaelekeza, na alichowaambia kilikuwa hiki -Sala na amani ziwe juu yake-"Wakikukusanyikieni -yaani wakawa wengi- basi watupieni mishale na shindaneni kwenye kutupa mishale", (489) Na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alikuwa akipenda kutupa mishale na akihimiza kutupa mishale, na wakati Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-anapangila Safu yake mara ghafla akatokea (Suwaad Bin Ghaz-ya)-Radhi za Allah ziwe juu yake- (490) alikuwa amepinda kwenye safu, Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akamuweka sawa kwa kutumia mkuki wake ambao alikuwa nao mkononi mwake na akasema kumwambia: "simama sawa swa ewe Suaad", hapo Suad akamwambia: "Umeniumiza ewe Mtume wa ALLAH basi niache nikulipizie", Basi Mtume akamfunulia tumbo lake tukufu ili amlipizie mwenyewe, basi akalibusu tumbo la Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- na Mtume akamwambia: "Nini kimekufanya ufanye hivyo ewe Suaad?" Akasema: Ewe Mtume wa ALLAHkwa hakika yametokea hayo uliyoyaona nikataka iwe ahadi yangu ya Mwisho na wewe ni ngozi yangu kuigusa ngozi yako, basi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akamuombea Dua. (491)

Na watu wakangojea amri ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwa ajili ya kuanza vita, na Mtume akarudi kwenye kibanda na akaanza kuumuomba Mola wake: "Ewe Mola wangu wa haki ikiwa utaliangamiza kundi hili leo hii, basi hautoabudiwa, Ewe Mola wangu nitekelezee uliyoniahidi" (492) Na akaendelea kuomba na pembeni mwake alikuwepo Abubakar-Radhi za Allah ziwe juu yake-mpaka akamuonea huruma na akamwambia: Ewe Mtume wa ALLAH unatosha ukumbusho wako kwa Mola wako, kwa hakika yeye ni mwenye kutekeleza alichokuahidi" kisha akapitiwa na usingizi mwepesi, kisha akasema: "Furahi ewe Abubakari, imekuja Nusrua

ya ALLAH, huyu hapa Jibriil ameshika Hatamu ya Farasi wake akimuongoza, (493) Basi waislamu wakafurahia baada ya Mtume kuwatokezea na akiwa anasoma maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿سَيَهْرَمُ أَجْمَعُ وَيُولُونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾ بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَىٰ وَأَمَرٌ ﴿٤٦﴾﴾ [القمر]:

[46-45]

"Karibu litashindwa kundi na watakimbizwa kurudi nyuma". "Bali saa kiyama ndio ahadi yao, na saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi" (45) [Alqamar: 45-46] (494) Na akawa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akimuomba ALLAH na akiwahimiza watu kupigana vita na akiwakumbusha pepo na akiwapa bishara ya kuteremka Malaika pamoja nao. Nao ndiyo wale ambao umekuja utajo wao katika maneno ALLAH Mtukufu:

﴿إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُم بِآلِفٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُرَدِّفِينَ ﴿٩﴾﴾

[الأنفال: 9]

"Na pindi mlipo mtaka Mola wenu msaada akakujibuni kuwa mimi {ALLAH} ni mwenye kukuongezeeni Malaika elfu moja wanao kuja kwa kufuatana". (Al- Anfaal: 9) Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿إِذْ يُوحَىٰ رَبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَيِّ مَعَكُمْ فَتَبَيَّنُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا سَأَلْتَنِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ فَأَضْرِبُوا فَوْقَ الْأَعْنَاقِ وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿١٣﴾﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُّوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٣﴾﴾ [الأنفال: 12-13]

[الأنفال: 12-13]

"Pindi alipo washushia ufunuo Malaika kuwa mimi {ALLAH} nipo pamoja nanyi basi watieni nguvu wale walio amini karibu nitatumbukiza ndani ya mioyo za wale walio kufuru uwoga basi pigeni juu ya shingo na muwapige kwenye kila ncha za vidole." (12) Hayo ni kwakuwa wao wamekwenda kinyume na ALLAH na Mtume wake na atakaye kwenda kinyume na ALLAH na Mtume wake hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. (13) [Al- anfaal:12-13]

Na katika wakati huo huo Makuraishi waliandaa safu yao na wakijiandaa kwa ajili ya kupigana vita, na akatazama Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- kuwa huenda akapatikana mmoja wao mwenye akili, na miongoni mwao kulikua na mtu alikuwa juu ya Ngamia mwekundu, akijadiliana na jamaa zake, akasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**:- "Ikiwa miongoni mwao kutakuwa na mtu mwenye busara basi huenda akawa ni huyo bwana mwenye Ngamia mwekundu" Hamza akasema: Huyu Utba bin Rabi'a, alikuwa kawakataza kupigana lakini hakufanikiwa kwa hilo.²⁵³

Na kwa hakika alijaribu mmoja wa Makuraishi kupenya kwenye safu ya waislamu ili anywe maji, basi Hamza Bin Abdul Muttwalib akamshukia na kumuua. (496)

Kisha ukaanza mpambano wa mwanzo kabisa katika Vita kati ya Shaiba Bin Rabiia na Utbah Bin Rabiia na Ally Bin Abii twaalib, na Al-waliid Bin Ut-bah katika washirikina, na kati ya Hamza na Bin Abdul Munttwalib, na Ally Bin Abii Twaalib na UbaidatBin Al-haarith miongoni mwa waislamu-Radhi za Allah ziwe juu yao-na wote hao ni katika Ahlu Bait- watu wa nyumbani- kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-,na mapambano yakaisha kwa kuuawa washirikina watatu na kujeruhiwa Ubaida Bin Al-haarith-Radhi za Allah ziwe juu yake- kisha naye kuuliwa shahidi (497) Na kwa hakika walikuwa ahlu baiti ndiyo wa mwanzo kupigana na kutoka kwao ndipo alipatikana shahidi wa kwanza.

Kisha yakashikana makundi mawili na vita ikaanza na Mtume akachukua choto la changarawe na akawatupia wale watu na

²⁵³ Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 184.

akasema : "Nyuso zimepata hasara" (498) na katika hili liliteremka kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿ فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ رَمَىٰ وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءً حَسَنًا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴾ [الأنفال: 17]

"Na hamkuwauwa nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyeauwa. Na haukurusha pindi ulipo rusha isipokuwa ALLAH ndiye aliye rusha, ili awape majaribu waumini kutoka kwake hali ya kuwa ni mtihani mzuri hakika ALLAH ni msikivu mjuzi". [Al-anfaal : 17] Na vita vikapamba moto kati ya pande mbili, na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwenye safu za mbele mpaka Maswahaba wakawa wakimchunga Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na maswahaba wengi walikuwa na nafasi ya ushujaa katika vita hii.

Na ikadhihiri bishara njema ya ushindi kwa waislamu, na washirikina wakashindwa na wakauliwa mabwana wa kikuraishi mfano Abu Jahal (499) na Utbatu Bin Rabiia na Ummaiyyat Bin Khalaf na wengineo miongoni mwa makafiri wa kikuraishi ambao walifikia idadi yao watu sabini, na watu waliokuwa hai wakakimbia wakiwa wameshindwa na hawana cha kuongea. (500)

Na wakakaa waislamu na Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-kwa siku tatu katika mji wa Badri baada ya Vita, wakazikwa mashahidi hapo, ambao walifikia idadi yao mashahidi kumi na Nne.²⁵⁴

²⁵⁴ Tazama Majina ya Mashahidi wa kiislamu katika mji wa Badri: Bin Hishaam, Siirat Nabawiyyat juzuu 2/706,707, Tazama Bin Abii Shaiba Al-maghaziy, ukurasa wa 204,206. na Tazama Al-subhiy Muhammad Bin Abdullah Ghabaan, mashahid wa vita vikubwa vya

Na kwa hakika alimtuma Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Zaidi Bin Haarith kwa kutumia Ngamia wa Mtume akiwapa bishara njema watu wa Madina, basi walifurahi waislamu kwa kheri na wakakasirika mayaudi na wanafiki na wala hawakumsadikisha Zaidi. (502)

Na bada ya hapo alirudi Mtume- Sala na amani ziwe juu yake-pamoja na aliokuwa nao miongoni mwa mujahidiina mpaka katika mji wa Madina wakiwa salama na wenye kupata Ngawira, basi waislamu wakawapokea katika mji wa Madina wakiwa na furaha kubwa kwa kurudi kwake salama Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na kwa kushinda waislamu ushindi huu mkubwa.²⁵⁵

Na alikuwa Mtume na mateka sabini wa Kukuraish, Na kwa hakika aliwashauri maswahaba wake kuwa awafanyaje hawa mateka tuchukue fidia toka kwao na kujizidishia nguvu katika njia ya Mwenyezi Mungu (504) Akasema Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake-** "Nye ni Maskini hivyo basi asiachiliwe yeyote katika wao isipokuwa kwa kutoa fidia au kuuawa. (505)

Na kwa hakika waislamu waliwatendea wema mateka wao katika muamala, na wakawa wakiwalisha wanavyovila na wakiwavalisha wanachovaa, na kwa hakika walikuja ndugu zao wa karibu kutoka katika mji wa Makka na wakawa wakitoa fidia ikiwa ni malipo ya kuwaachia huru (506) Na hawa mateka waliathirika kwa kubakia

Badri ,Aljumuiyyat Taarikhiya AL- Suudia ,Riyadh,silsilatu Buuthi Taarikhiyat Al-iswdaaril Khaamis Ashara,Rabiul Awwal1424 Hijiria.

²⁵⁵ Siirat Nabawayyat ya Bin Hishaam juzuu ya ج26434;Al-waaqidiy: Al-maghaaziy juzuu ya 1/144.

kwao Madina na kushuhudia kwao ukweli wa waislamu, na uzuri wa uislam, Basi wakasilmu wengi wao katika muda uliokuja.

Na kwa hakika ziliteremka baadhi ya Aya katika Tukio la vita vya Badri, na miongoni mwake ni maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ كَمَا أَخْرَجَكَ رَبُّكَ مِنْ بَيْتِكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ فَرِيقًا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ لَكَاهُونَ ﴾ ٥ يُجَدِّدُونَكَ فِي الْحَقِّ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ كَأَنَّمَا يُسَاقُونَ إِلَى الْمَوْتِ وَهُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٦﴾ وَإِذْ يَعِدُكُمُ اللَّهُ إِحْدَى الطَّائِفَتَيْنِ أَنَّهَا لَكُمْ وَتَوَدُّونَ أَنَّ غَيْرَ ذَاتِ الشُّوْكَةِ تَكُونُ لَكُمْ وَيُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَيَقْطَعَ دَابِرَ الْكَافِرِينَ ﴿٧﴾ لِيُحِقَّ الْحَقَّ وَيُبْطِلَ الْبَاطِلَ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨﴾ إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُمْ بِالْفِئَةِ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُرَدِّفِينَ ﴿٩﴾ وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِ قُلُوبُكُمْ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾ إِذْ يُعَشِّيكُمُ النَّعَاسَ أَمَنَةً مِنْهُ وَيُنزِلُ عَلَيْكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لِيُطَهِّرَكُمْ بِهِ وَيُذْهِبَ عَنْكُمْ رِجْسَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَى قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ الْأَقْدَامَ ﴿١١﴾ إِذْ يُوحَىٰ رَبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَنِّي مَعَكُمْ فَثَبِّتُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا سَأَلَتْنِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ فَأَضْرِبُوا فَوْقَ الْأَعْنَاقِ وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿١٢﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٣﴾ ذَلِكَ فَذُوقُوهُ وَأَنَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابَ النَّارِ ﴿١٤﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحَفًا فَلَا تُولُوهُمُ الْآدْبَارَ ﴿١٥﴾ وَمَنْ يُؤْلَمْ يَوْمَئِذٍ دُبْرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّرًا إِلَىٰ فِتْنَةٍ فَذُوقْ بَأْسَ الْعَذَابِ مِنْ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٦﴾ فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ رَمَىٰ وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءً حَسَنًا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٧﴾ ذَلِكَمْ وَأَنَّ اللَّهَ مُوهِنٌ كَيْدِ الْكَافِرِينَ ﴿١٨﴾ إِنْ تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ وَإِنْ تَنْتَهُوا فَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ وَإِنْ تَعُودُوا نَعُدْ وَلَنْ تُغْنِيَ عَنْكُمْ فِئَتُكُمْ شَيْئًا وَلَوْ كَثُرَتْ وَأَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٩﴾﴾ [الأنفال: 5-19]

"Kama alivyo kutoa Mola wako nyumbni kwako kwa ukweli na hakika kundi miongoni mwa waumini ni wenye kukarahika. (5)

Wana kujadili katika ukweli baada ya kubainikiwa kana kwamba wanapelekwa kwenye kifo na wao wanatazama. (6) "Na pindi ALLAH alipo wapa ahadi kuwa moja ya makundi mawili litakuwa kwenu nyinyi na mkapenda kundi lisilo kuwa na nguvu liwe upande wenu, na Mwenyezi Mungu anapenda ahakikishe haki kwa maneno yake, na aikate mizizi ya makafiri". (7) Ili ahakikishe haki na auvunje upotovu hata kama waovu watachukia. (8) "Kumbukeni mlipo mtaka msaada Mola wenu akakujibuni hakika mimi (ALLAH) ni mwenye kuwaongezeeni Malaika elfu moja wenye kushuka kwa kufuatana." "Na ALLAH hakujalia jambo hilo isipokuwa ni bishara kwenu na ili ipate kutulia mioyo yenu na haukuwa ushindi isipokuwa unatoka kwa ALLAH hakika ALLAH ni mwenye nguvu mwenye hekima. (10) "Pindi alipo wafunikeni kwa usingizi hali ya kuwa ni amani kutoka kwake na akiwateremshia kutoka mawinguni maji ili apate kuwasafisha kwa maji hayo na ili awaondoshee uchafu wa shetani na kuzipa nguvu nyoyo zenu na kuitia imara miguu yenu" (11) Pindi Mola wako alipo wafunulia Malaika kuwa mimi [ALLAH] nipo pamoja nanyi basi watieni nguvu wale walio amini, karibu nitaingiza ndani ya nyoyo za wale walio kufuru uwoga kisha muwapige juu ya shingo na muwapige kwenye kila nchi za vidole. (12) Hayo ni kwakuwa wao wamekwenda kinyume na ALLAH na Mtume wake na atakaye kwenda kinyume na ALLAH na Mtume hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. (13) Adhabu hiyo basi ionjeni, na kwa hakika makafiri wana adhabu ya moto. (14) Enyi mlio amini mtakapo kutana na wale walio kufuru vitani basi kukimbia basi msiwageuzie migongo (kwa kukimbia). (15) Na atakaye kimbua kwa kurudi nyuma, isipokuwa kwa (mwenye lengo la) mbinu za vita au kuungana na kikosi, hakika huyo atakuwa amestahiki ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Na mafikio yake ni motoni wa Jahanamu, na huo ni mwisho muovu. (16) Hamkuwauwa nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewauwa. Na wewe hukutupa (mshale) lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupa, ili awajaribu waumini majaribio mema yatokayo

kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye msikivu na Mjuzi. (17) Ndiyo hivyo! Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kudhoofisha vitimbi vya makafiri (18) Kama mnataka hukumu basi imekwisha kujieni. Na mkiacha itakuwa ndio kheri kwenu. Na mkirejea sisi pia tutarejea. Na jeshi lenu halitokufaeni chochote, hata likiwa kubwa. Kwani hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na waumini. (19) Al-anfaal:5-19 Na anasema Allah Kutakasika namachafu ni kwake kuhusu matukio ya hii vita katika sehemu nyingine katika sura hiyohiyo.

﴿وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ
وَالْمَسْكِينِ وَأَبْنِ السَّبِيلِ إِن كُنْتُمْ ءَامَنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أُنزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ التَّقَىٰ
الْجُمُعَاتِ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾ (٤١) إِذْ أَنْتُمْ بِالْعُدْوَةِ الدُّنْيَا وَهُمْ بِالْعُدْوَةِ الْقُصْوَىٰ وَالرَّكْبُ
أَسْفَلَ مِنْكُمْ وَلَوْ تَوَاعَدْتُمْ لِاحْتِلَافْتُمْ فِي الْمَيْعَدِ وَلَكِن لِّيَقْضَىٰ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا لِّيَهْلِكَ
مَنْ هَلَكَ عَن بَيْتِهِ وَيَخِيَّ مَنْ حَىٰ عَن بَيْتِهِ وَإِنَّ اللَّهَ لَسَمِيعٌ عَلِيمٌ﴾ (٤٢) إِذْ يُرِيكُهُمُ اللَّهُ فِي
مَنَامِكَ قَلِيلًا وَلَوْ أَرَأَيْتَهُمْ كَثِيرًا لَّفَشِلْتُمْ وَلَتَنزَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَلَكِنَّ اللَّهَ سَلَّمَ إِنَّهُ عَلِيمٌ
بِذَاتِ الصُّورِ﴾ (٤٣) وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ إِذِ الْتَقَيْتُمْ فِي أَعْيُنِكُمْ قَلِيلًا وَيُقَلِّلُكُمْ فِي أَعْيُنِهِمْ لِيَقْضَىٰ
اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ﴾ (٤٤) [الأنفال: 41-44]

Tambueni ya kwamba chochote mlichote kipata kwenye ngawira basi moja kati ya mafungu matano ni kwa ajili ya Allah na mtume wake na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na mpita njia ikiwa nyinyi ni wenye kumuamini Allah na yale tuliyo yateremsha juu ya mja wetu siku ya kipambanuzi siku yaliyo kutana makundi mawili na Allah kwa kila kitu ni muweza. Pindi mlipokuwa kwenye bonde karibu na mji wa madina na wao wakiwa kwenye bonde la mbali karibu na makkah na msafara ukiwa chini yenu na laiti mngepeana ahadi na wao hakika mnetofautiana katika utekelezaji isipokuwa Allah alipitishie jambo likawa ni lenye kupitishwa ili aangamie mwenye kuangamia kwa ubainifu na aishi

mwenye kuishi kwa ubainifu na hakika Allah ni msikivu mjuzi. Pindi Allah alipo kuonesha kwenye usingizi wako kuwa wao ni wachache na kama angekuonesha kuwa wao ni wengi mngefeli na mngelitatizana katika jambo nakini Allah akipitisha kwa usalama hakika yeye ni mjuzi kwa yale yaliyomo ndani ya vifua. Na pindi alipo kuonesheni wao pindi mlipo kutana kwenye macho yenu kuwa ni wachache na Allah anakuonesheni kwenye macho yenu kuwa ni wachache ili Allah apate kupitisha jambo limekuwa ni lenye kufanywa na kwake Allah ndiko kunarejea majambo. Al-anfaal:41-44.

Na ilikuwa Vita ya Badri ndiyo ya kwanza kwa waislamu kuwashinda washirikina wa Makka na kwa hakika waarabu walisambaza habari zake,na baadae watu walitambua kuwa waislamu wamekuwa na nguvu yenye kutambulika kisawasawa.

KATI YA BADRI NA UHUDI.

Vita vya Badri vilibadlisha hali nyingi katika mpambano kati ya maquraishi na washirika wao na kati ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-,mtume ambaye alikuwa anapupia Amani ya Mji wa Madinah na watu wake,na ili hali iwe nzuri kwa waislamu,kama vile ambavyo alikuwa akipupia juu ya ufahamu wa ulipizaji wa walichofanya maquraishi na wengineo miongoni mwa maadui kwa ajili ya kuwanusuru waislamu katika vita vya Badri,na pasiwepo huko na udhaifu,na ilikuwa ni jambo la wazi kuwa maquraishi hawatonyamaza kwa kushindwa na kuuwawa watu wake na mateka wake,na jambo hili linahitajia ufuatiliaji wa kila wakati kutoka kwa Mtume na nakuendelea kazi za Kijeshi yanayofungamana na kazi za Kijeshi ikiwa miongoni mwa kutma vikosi na kupigana vita na,kwa ajili ya kuuhifadhi mji wa Madina na watu wake na kazi zilizopata Umaarufu baada ya vita vya Badri na kabla ya vita vya Uhud ni:

Vita Vya Watu wa Qainuqaa:

Walikuwa Mayahudi wa Banii Qainuqaa ni miongoni mwa kabila na kikundi cha mayahudi, walikuwa wakiishi Madina kabla ya kufika Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na wakati wa kuhama kwake aliwaaga wao pamoja na wengine miongoni mwa Mayahudi katika mkataba wa madina ,na kulikuwa ni miongoni mwa kuaga kulikotoa ushirikiano wa kuulinda mji wa Madina yenye nuru,na kuwalinda watu wake.

Na mayahudi walikuwa wakijuwa ukweli wa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na ziliteremka aya nyingi na sura nyingi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu katika mji wa Madina walijadiliana mayahudi na wakazungumza kuhusu Manabii wao na Historia yao na kundakwa kwao kinyume.

Na alikua Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-Mara nyingini mwenye kujadiliana na wanazuoni wao na akaiwatembelea katika sehemu zao za mafundisho akijaribu kuwakinaisha kwa dini ya Mwenyezi Mungu na hawakusilimu isipokuwa idadi chache miongoni mwao Abdiullahi Bin Salaam-Radhi za Allah ziwe juu ya-. (508)

Na baada ya kwisha vita vya Badri jambo la waislamu kuwashinda maquraishi lilikuwa wazi,na hii inamaanisha kuwa waislamu walikuwa ni wenye nguvu katika mji wa Madina,kwa kusadikisha ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuwanusuru waja wake walioamini,na aliikuwa Mtume ni Mwenye huruma kwa Myahudi na akiwa na pupa ya wao kuongoka na wao ni watu waliopewa kitabu wanaijuwa haki.

Na vilevile baada ya kurudi kwao kutoka katika vita vya Badri((Kwa hakika Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-aliwakusanya katika soko la Banii Qainuqaa,kisha akasema:Enyi kundi la Mayahudi chukueni tahadhari yasije yakawapata yaliyowateremkia maquraishi katika Adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mjisalimishe kwa hakika mmekwisha juwa kuwa mimi ni

Nabii niliyetumwa,mtapata ahadi ya Mwenyzi Mungu kwa hilo,wakasema "Ewe Muhammad hakika wewe unaona kuwa sisi ni watu wako,usidanganyike kwa kuwa wewe umekutana na watu wasiokuwa na ujuzi wa kivita,kwa hakika sisi twamuapia ALLAH tutaamua kukupiga vita utatujua kuwa sisi ni watu gani"(509)

Na katika wakati ambao Mtume -Sala na amani ziwe juu yake akiwafanyia upole banuu Qainuqaa na kutaka kuwaongoa na akiwakumbusha yaliyowapata maquraishi,walikuwa wakimjibu kwa vitisho vya waziwazi nakujiandaa kumpiga vita nakumpa somo ambalo walilitambuwa watu wa vita na majemedari-Kama walivyodai-Na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Bin Abbas - Radhi za Allah ziwe juu yake na baba yake- Kuwa ALLAH kutokana na wao kumtishia mtume,Allah aliwateremshia Aya hii:

﴿قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا سَعْتٌ لَّيْسَ لَهُمْ شُرَكَاءُ فِيهِمْ وَهُمْ عَلَيْكَ عَذَابٌ عَظِيمٌ﴾ [آل عمران: 12]

Waambie wale walio kufuru karibu mtashindwa na mtafufuliwa kwenye moto wa jahannama nani mafikio mabaya. Al-imran:12)(510)

Hivi vitisho vya waziwazi kutoka kwao,unahesabiwa kuwa ni uvunjaji wa waziwazi wa ahadi iliyowekwa kati yao pamoja na Mtume- Sala na amani ziwe juu yake-((Na wakawa ndiyo Mayahudi wa kwanza kuvunja makubaliano yaliyopo kati yao na Mtume wa Mwenyezi Mungu))(511)

Na kukazuka tukio lililochochea uadui mkubwa kati pande zote mbili,na tukio hilo ni kuwa alikuja mwanamke akiwa ameleta bidhaa yake,akaiuza katika soko la banuu Qainuqaa na akakaa kwa sonara,na wakawa wanamtaka afunuwe uso wake,basi akakataa,basi Sonara kwa makusudi akachukua ncha ya nguo yake na akaifunga nyuma ya yule mwanamke,na aliposimama ukafunuka uchi wake,wakamcheka mwanamke yule,basi akapiga ukelele mara ghafla Muislamu akamrukia Sonara na akamuwa,na alikuwa ni

Yahudi,basi mayahudi wakambana muislamu mpaka wakamuuwa ,basi watu wa yule muislamu wakawapigia kelele waislamu dhidi ya Yahudi,hivyo waislamu wakakasirika,na yakazuka mapigano kati yao na watu wa Qainuqaa.(512)

Na kumesemwa kuwa Aya hii imeteremkaka kwa ajili yao:

﴿وَأَمَّا تَخَافَنَّ مِنْ قَوْمٍ خِيَانَةً فَأَثْبِدْ إِلَيْهِمْ عَلَى سَوَاءٍ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِبِينَ ﴿٥٨﴾﴾ [الأنفال:

[58

Basi ikiwa utaogopa khiyana kwa watu ambao umechukuwa pamoja nao Ahadi basi watupie Ahadi yao kwa usawa kwa hakika Mwenyezi Mungu hapendi wafanyao khiyana. Al-anfaal:58/(513)

Na kwa hakika alifanya haraka mtume -Sala na amani ziwe juu yake-kukusanya jeshi la waislamu na kuwazuia Banuu Qainuqaa katika ngome zao kwa nyusiku kumi na tano (514)ALLAH aliwatia uwoga katika nyoyo zao basi wakajisalimisha kwa amri ya Mtume - **Rehema na amani ziwe juu yake-** na wakaingia katika hukumu yake,na walikuwa ni washirika wa baadhi ya watu wa Madina hivyo waislamu wakawaachia,na kiongozi wao ambae Ni Ubaadat Bin Swaamit-Radhi za Allah ziwe juu yake-ambaye alijitenga nao kwa ajili ya ALLAH na Mtume wake,na wanafiki wakawaogopea na wao ni wasaidizi wao katika kumuudhi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kwa hivyo alisimama Abdullahi Bin Ubaiyyat Bin Saluul,alipo watawalishia ALLAH Mtume atokanae na wao Akasema :Ewe Muhammad wafanyie wema washirika wangu na walikuwa ni washirika wa kabila la Khazraj,akasema,akawa mzito mtume wa ALLAH akasema:wafanyie wema washirika wangu,akasema akampa mgongo,basi akaingiza mkono wake katika tundulililopo kwenye Ngao ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Amesema Bin Hishaam:hilo tundu lilikuwa linaitwa Dhaatul Fudhuul.

Amesema Bin Ishaqa:Basi mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- akamwambia Niwachilie(Taratibu),na akachukia Mtume

wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-mpaka wakaona usoni mwake weusi,kisha akasema una nini wewe!niwachilie,akasema hapana namuapia ALLAH sikuwachii mpaka uwatendee wema washika wangu na wala usiwauwe,mateka mia nne na Ngao mia tatu wao wamenihami mimi nakila watu waarabu na waajemi,unawakusanya na kuwauwa wakati mmoja,kwa hakika mimi ni mtu naogopea ikiwa itatokea misiba namatatizo sitakuwa na wakuninusuru,akasema:amesema mtu mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-,"nimekuwachia wao"(515)

Na yalikuwa matokeo nikuwasamehe na kutowauwa,na kuwatoa katika mji wa Madina,pale ambapo waislamu walichukua Ngawira kutoka kwenye mali zao na majumba yao,na wakatoka ndani ya siku tatu na wakaelekea katika miji ya Sham.

Na katika hali aliyokuwa nayo Abdullah Bin Ubaiya Iliteremka kauli yake ALLAH :

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴾ ﴿٥١﴾ فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يُسْرِعُونَ فِيهِمْ يَقُولُونَ نَخْشَىٰ أَنْ تُصِيبَنَا دَآئِرَةٌ فَعَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِندِهِ فَيُضْبِحُوا عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي أَنْفُسِهِمْ نَدِيمِينَ ﴿٥٢﴾ وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَهَؤُلَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ إِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ حَبِطَتْ أَعْمَلُهُمْ فَأُضْبِحُوا خٰسِرِينَ ﴿٥٣﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَن دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٌ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٌ عَلَى الْكٰفِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَآئِمٍ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ وَسِعَ عَلَيْهِمْ إِنَّمَّا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ ﴿٥٤﴾ وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهُ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٥٥﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُوعًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَالْكَفَّارَ أَوْلِيَاءَ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٥٦﴾ [المائدة: 51-57]

Enyi ambao mlio amini msiwafanye mayahudi na wakristo kuwa ni vipenzi wapendane wao kwa wao na atakaye nayeyote miongoni mwenu atakaye wafanya kuwa ni vipenzi atakuwa miongoni mwao hakika ALLAH hawaongozo watu madhalimu. Utaona kwenye nyoyo za wale ambao wana maradhi wanafanya haraka kuwaendea wanasema tunahofia tusipatwe na mwisho mbaya karibu ALLAH ataleta ushindi au jambo kutoka kwake hakika watakuwa kwa yale waliyo ya ficha ndani ya nafsi zao ni wenye kujuta. Na watasema wale ambao walio amini hivi hao ndio ambao walio muapia ALLAH kwa viapo vyao vya uhakika hakika wao wapo miongoni mwenu yameporomoka matendo yao na wakawa ni wenye hasara. Enyi ambao mlio amini atakaye acha dini yake karibu ALLAH ataleta watu ALLAH anawapenda na wao wanampenda ALLAH wenye kujishusha kwa waumini na ni wenye hasira kwa makafiri wanapigania katika njia ya ALLAH na wala hawaogopi lawama ya mwenye kulaumu hiyo ni fadhila kutoka kwa ALLAH anampa amtakaye na ALLAH ni mwenye fadhila nyingi na mjuzi. Si vinginevyo kipenzi chenu ni ALLAH na mtume wake na wale ambao walio amini wale ambao wanasimamisha swala na wanatoa zaka na hali yakuwa ni wenye kunyenyekea.(55) Na atakaye fanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walio amini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda. (56) Enyi mlio amini msiwafanye wale ambao walio ifanya dini yenu ni upuuzi na mchezo kutokana na wale ambao walio pewa kitabu kabla yenu na makafiri kuwa ni wasimamizi[wenu]na muogopeni ALLAH ikiwa ni wenye kuamini.(57) Al- maaida: 51-57

Na ilikuwa kuondoshwa kwa kabila la Banii Qainuqaa ni pigo la nguvu kwa amyahudi wa Madina,ambao walishindwa mara hii kuwanusuru ndugu zao Mayahudi pale ambapo ALLAH aliwapa pigo la udhalili na Khofu.(516)

Kama ilivyokuwa walichokichukuwa waislamu kama ghanima kutoka kwa Banuu Qainuqaa kulikuwepo na silaha nyingi na vifaa vya kutengenezea Dhahabu na mali mbalimbali,walinufaika nazo waislamu,na kwa hakika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alizigawa kwa waislamu na akatoa Moja ya tano(517) na walipata faida ya kuzitumia silaha hizo katika vita zilizofuata.

Kuowana Ally na Fatma -Radhi za allah ziwe juu yao hao wawili-(518)

Fatma Bint ya Mtume wa ALLAH,Mtume alisema kuhusu Fatma: ((Fatma ni Mheshimia wa wanawake wa peponi))(519) Na alisema: ((Fatma ni sehemu itokanayo nami,na yeyote atakaye mkasirisha amenikasirisha mimi)) (520)

Mdogo zaidi katika mabint wa Bwana mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na mwenye kupendwa zaidi kwake pamoja nakuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- aliwapenda wote -Radhi za Allah ziwe juu yao-naye Fatma ndiye Bint wa pekee aliyebakia mpaka mwisho wa uhai wake katika mabinti wa Mtume-Sala na amaniziwe juu yake-alibakia baada yake kwa miezi kadhaa,na kutoka kwake zilipokelewa Hadithi nyingi,na kwa ajili hiyo akili za umma zilikuwa na mafungamano naye zaidi kuliko yeyote katika mabinti wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,kama ambavyo ili uwa kukatika kwa kizazi cha mtume-Sala na amani ziwe juu yake-isipokuwa kizazi cha Fatma kulimfanya akumbukwe zaidikuliko mwingine yeyote.

Alizaliwa Fatma-Radhi za Allah kabla ya kutumwa mtume kwa miaka miwili,(521)na alikuwa ni miongoni mwa wenyekumuhami mtume-Sala na amaniziwe juu yake-katika mji wa Makka wakati walipomuudhi watu wake,alibeba kondo la uzazi la Ngamia ambalo watu walimtupia kichwani mwake na akawatukana na akawafukuzia mbali na mtumewa ALLAH-Sala na amaniziwe juu yake-.(522)

Zimepokeewa Fadhila zake kutoka kwa mama wa Waumini Aisha katika hadithi mbalimbali na alikuwa Aisha akisema: ((Sijawahi kumuona hata mara moja mtu aliye bora kuliko Fatma isipokuwa Baba yake tu))(523)

Amepokea Aisha -radhi za Allah ziwe juu yake- ((Kuwa Fatma alikuwa akija huku akitembea ilikuwa kutembea kwake ni kama alivyokuwa akitembea Mtume-Sala na amaniziwe juu yake-basi akasema: Karibu ewe Binti yangu,kisha akamkalisha upande wake wa kulia kisha akamnong'oneza akalia Fatma kisha akamnong'oneza akacheka,basi nikasema:sijawahi kukuona kama nilivyokuona leo furaha iko karibu zaidi kuliko huzuni,basi nikamuuliza kuhusu nini alichosema?akasema,siwezi kufichua siri yake mtumena alipokufa nilimuuliza ,basi akanipa habari kuwa yeye amesema:Malaika Jibril alikuwa akinisomesha Qur'an kila mwaka mara moja,na kwa hakika yeye amenifundisha mwaka huu mara mbili,na sioni isipokuwa mauti yangu yamekaribiana kwa hakika wewe nimtu wangu wa kwanza kukutana nae na bora ya watangulizi wako ni mimi,nikaliaakasema:hivi hauridhiki kuwa wewe ni muheshimiwa wa wanawakewa ulimwenguni basi nikacheka.))(524)

Na kwa hakika Fatma alikutana na Mtume-Sala na amaniziwe juu yake-akiwa anahamia Madina na alikuwa Fatma ni kijana,(525)

Na alikuwa Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake-nikijana mwenye kuhama pamoja namtume kuelekea Madina,naye ni mtu wa karibu zaidi kwa Mtume wa ALLAH kwa upande wa Nasaba kiroho na kiimani,na kwa hakika alilelewa katika nyumba ya Mtumewa ALLAH-Sala na amaniziwe juu yake-na alikuwa muumini wa kwanza kwa upande wa vijana,na mweye kujuwa zaidi kuhusu ukweli wake,alimuokoa mwenyewe siku ya kuhama,ana nafasi kubwa kwa mtumewa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-na ana nafasi kubwa kwa waislamu nafasi ambayo yeyote hana nafasi hiyo.

Na katika Mwezi wa Muharram mwaka wa pili tangu kuhama mtume,alipenda Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake-kumchumbia Fatma toka kwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake- isipokuwa Ally alikuwa na haya na kumuogopa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-zaidi ya hayo ni kuwa yeye alikuwa ni kijana hana uzoofu kwenye haya mambo.

Na kwa hakika walijaribu baadhi ya Maswahaba kumchumbia Fatma -Radhi a Allah ziwe juu yake-isipokuwa Mtume alirudisha kwa upole ,kana kwamba alikuwa anamsubiri Ally-Radhi a Allah ziwe juu yake-ili amchumbie,na kwa hakika baadhi ya mabinti wa Kianswari walimuhamasisha kufanya hivyo.(526)

Amesema Ally Radhi za Allah ziwe juu yake- Na nilipo kaa mbele yake niliishiwa na maneo namuapia ALLAH sikuweza kuongea basi akasema: nini kimekuleta?basi nikanyamaza,akasema:Huenda umekuja ili umchumbie Fatma?nikasema:Ndiyoakasema:je unachochochote cha kumuhalalisha nacho?Basi nikajibu :sina na ninamuapia ALLAH ewe Mtume wa ALLAH Basi akasema:ile Ngao niliyokupa kama silaha uliifanyia nini,nikasema nipo nayo akasema: Basi Mpe Fatuma hiyo Ngao.)) 527.

Na inasemekana kuwa mtume aliinga kwa Fatma na akampa habari ya anachokitaka Ally basi akanyamaza basi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akatambuwa kuwa huko kunyamaza ndiyo kukubali kwake.

Na kwa hakika ilikuwa ni uowaji mwepesi na wakinyenyekevu,Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake alitoa kile alichokuwa na uwezo nacho.

Na kwa hakika imepokelewa kuwa yeye alikuwa ni mwenye kubebe kuni na akileta kwa kwa mmoja wa mafundi sonara wa Madina anasema Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake-: ((Na pindi nilipotaka Kuingia kwa Fatma Bint ya Mtume-Sala na amani ziwe juu

yake-nilimuahidi mfua Dhahabu kutoka katika kabila la Banuu Qainuqaa aende nami na tuje na mali niliyokuwa nimeihifadhi niiuze kwa wafuwa dhahabu na inisaidie katika walima wa Harusi))(528) Na kwa hakika walichangia baadhi ya watu wa Madina na wa Makka katika huu walima na wakinyenyekevu wenye baraka.

Na kwahakika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alimuandaa maandalizi madogo na akaanda mitungi miwili ya maji(529) na kwa hakika imepokewa kuwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alimwambia Ally usiku wa kuingia kwa Fatma: usifanya kitu chochote mpaka ukutane nami,basi akaagiza maji kisha akatawadha kisha akawamwagia maji yake,na akasema Ewe Mola wangu wa haki wape baraka wote wawili na uwabariki juu yao wawili na ubariki vizazi vyao.(530)

Na kwa hakika alipupia Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kumpa Makazi Ally na Fatma -Radhi za Allah ziwe juu yao-karibu yake,na kwa hakika Haarithat Bin Nuuman Al-answaariy alilijuwa hilo,na akabadilisha chumba chake kilichopo pembeni mwa msikiti wa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-ambacho kipo upande wa kaskazini mwa chumba cha Aisha,na akamtaka Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-akichukuwe kwa ajili ya Ally na Fatma na akasema:Namuapia ALLAH ambacho anachukuwa ni chenye kupendeza zaidi kwangu kuliko anacho kiwacha,akasema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-umesema kweli,akabadilisha na wakaishi Ally na Fatma Sehemu yake.wakawa wao wawili wakiishi pembeni mwa Mtumewa ALLAH akiwa anawatembelea na akizungumza nao na akawaombea na akiwaongoza.(531)

Na kwa hakika kumepokelewa Hadithi nyingi kuhusu hizi ziyara zenye baraka za kuitembelea nyumba yenye baraka ambayo ametoka humo mabwana wawiwili wa vijana wa peponi nao ni Hassan na Hussein -Radhi za Allah ziwe juu yao-na Ummu Kulthuum

na Zainab na Mabinti watokanao na Fatma-Radhi za Allah ziwe juu yao.(532)

Na kwa hakika alikuwa Fatma-Radhi za Allah ziwe juu yake-akiishi pamoja na Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake-katika maisha magumu na ya shida,na haikuwa Dunia ndiyo lengo lao,na pamoja na hayo walikuwa wakiumia kutokana na wingi wa kazi,na kwa hakika imepokelewa kutoka katika musnadi wa Imamu Ahmad((Ally alimwambia Fatma siku moja namuapia ALLAH kwa hakika nimekuwa mtu mzima nafanya kazi ya kuvuta maji toka kisimani mpaka nafsi yangu inakachoka Akasema:na ALLAH amemletea baba yako mateka wa kike,basi mtake atupe mateka mmoja.akasema Fatma Mimi namuapia wenyezi ALLAH kwa hakika nimesaga nafaka kwa kutumia jiwe mpaka mikono ikatia sugu hivyo nikamuendea Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akaniuliza((Ni jambo gani lilokuleta ewe Binti yangu))akasema Fatma nimekuja ili nikusalimie nikaona aibu kumuomba,hivyo tukaenda wote.akasema Ally.Namuapia ALLAH kwa hakika nafanya kazi ya kuvuta maji toka kisimani mpaka nafsi yanguna Fatma akasema:kwa hakika namuapia ALLAH kwa hakika nimesaga nafaka kwa kutumia jiwe mpaka mikono ikatia sugu na ALLAH amekujaalia mateka na uwezo,basi twaomba tuwekee mtumishi,Basi akasema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-((Namuapia ALLAH kuwa siwezi kuwawekea mtumishi kisha niwawache watu wa suffa yakijikunja matumbo yao na nisiweze kupata cha kuwapa,lakini mimi hao watumishi nawanunuwa na ninatoa gharama zao))(533)Basi wakarudi wote wawili Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akawajia na wa hakika walikuwa wameshaingia kwenye kashuka kao amabcho wakijifunika vichwa vya inafunuka miguu yao,na wakifunika miguu yao vinafunuka vichwa vyao,basi mtume akainua sauti na kusema (Bakieni hivyo hivyo.kisha akasema((Hivi sikupeni habari juu ya kile mlíchoniomba?))wakasema kwanini usitupe basi akasema:((Ni maneno alinifundisha malaika Jibriil-juu yake amani-basi alisema

Mtamsabbih ALLAH mwisho wa kila swala mara kumi,na mtamuhimidi mara kumi,ni mtaleta Takbira mara kumi,na mnapolala kitandani kwenu basi mumsabbihii ALLAH mara thelathini na tatu,na muhimidi mara thelathini na tatu na mlete takbira mara thelathini na tatu))(534)

kama walivyo wanadamu wengine,ilikuwa inatokea wakati mwingine yale yanayotokea kwa baadhi ya wanandoa,na alaikuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-akiwasuluhisha kati yao,mpaka Ally akafikia kumwambia Fatma Wallah sitofanya tena jambo ambalo linakuudhi.Amepokea Bin Hajar akasema ilikuwa kati ya Ally na Fatma mzozo-Radhi za Allah ziwe juu yao-hivyo akaingia mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-na mzozo haukusimama mpaka akawasuluhisha,kisha akatoka akaambiwa uliingia ukiwa na hali tofauti na umetoka ukiwa na hali tofauti na sisi twaona furaha kwenye uso wako,akasema Mtume,ni kitu gani kitakacho nizuia na hali ya kuwa nimewapatanisha wawili niwapendao (535)

Na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Ummu Salama kuwa amesema:(Katika nyumba yangu paliteremka Aya tukufu katika maneno yake mtukufu)

﴿وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَىٰ وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتَيْنَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا﴾
[الأحزاب: 33]

Na mtulie kwenye majumba yenu na wala msitoke mkiwa mmejipamba kujipamba kwazama za ujinga wa mwanzo na msimamisha swala na mtoe zaka na mumtii ALLAH na mtume wake si vinginevyo anataka ALLAH awaondoshee uchafu watu wa nyumbani kwa -mtume-na akusafisheni kweli kweli. Al-ahzab:33

Akasema basi akatuma mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- akawaita Fatma na Ally na Hassan na Hussein kisha akasema

hawa ndiyo watu wa nyumba yangu(536) na pamoja na hivo,Aya hii inawaenea Watu wote wa nyumba ya mtume na miongoni mwao ni wamama wa uislamu,ambao Aya ilianza kuwazungumzia,na wala haingii akilini kama walivyofanya hawa wenye chuki kuwagawa wamama wa waislamu na wanaiona Aya imekuja maalumu kwa Ally na Fatma na watoto wao-Radhi za Allah ziwe juu yao wote-kuthibitisha kwao hakumaanishi kupinga wasiokuwa hawa waliotajwa,,hivyo basi wake za Mtume wote ni katika watu wa nyumba ya mtume kama walivyo watu wengine,hivyo hawavuliwi wake za mtume katika Aya,kwani mwanzo imewazungumzia wao,bali aya hiyo inaelekezwa kwao.

Na huenda Mtume-Sala na mani ziwe juu yake- alifanya hivyo pamoja na Ally na Fatma na watoto wao,ili kukata njia ya wenye kutilia mashaka ya wao kuingia na kuwa miongoni mwa watu wa nyumba ya Mtume na hapana shaka kwa ni aya imeshathibitisha kuwa wake zake mtume-Rehema na mani ziwe juu yake-ni miongoni mwao.

Vita Vya Uhud(Mwezi Shawwal Mwaka 3 hijiria)(537)

Na maquraish hawakunyamaza baada ya kushindwa katika vita vya Badri,na wakaanza kufanya mandalizi ya kuwapiga vita waislamu katika mji wa Madina ,na kafanya kila mmoja kwa bidiiyake,basi wale ambao Baba zao waliuliwa au watoto wao au mmoja wa familia yao walikuwa wakiwapitia watu nawakiwaahamasisha kuwa dhidi ya Mtume na waliokuwa pamoja nae,(538) na walikuwa mayahudi wa Makkah wakishirikiana katika kuwahamasisha viongozi wao,na wanafiki waliopo katika mji wa madina wakiwaandaa Maquraishi na wakiwataka misaada ikiwa watafika Madina kwa ajili ya ili kumng'oa Muhamad na wenzake miongoni mwa waislamu,na wagharamikie maandalizi ya hali na mali kwa ajili ya hilo,na kwa wao iliteremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ لِيَصْنُؤْاَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ فَسَيُنْفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ يُحْشَرُونَ﴾ [الأنفال: 36]

Hakika wale walio kufuru wanatoa mali zao ili wazuie kunako njia ya ALLAH basi watazitoa kisha itakuwa ni majuto juu yao kisha watashindwa na wale ambo walio kufuru kwenye moto wa jahannama watakusanywa. Al-anfaal:36(539)

Nawalijiandaa maquraishi na washirika wao watokanao na kabila la Tihama na wengineo,na jeshi lake likaelekea na nguvu zake na watu wake na watumwa wake,na baadhi ya wanawake wakiwa wanaukusudia mji wa Madina,na kwa hakika ilifikia idadi yao inayozidi wapiganaji (540)

Katika wakati huu habari zilikuwa zinamjia Mtume -Rehema na mani ziwe juu yake- kutoka kwa wapelelzi wake wa Makka kuhusu kuondoka kwa watu kwa ufafanuzi .(541)

Aliwakusanya Mtume Waislamu-Rehema na amani ziwe juu yake na akawashauri katika jambo hilo kama kawaida yake,na zikatofautiana Rai zao,basi miongoni mwao kuna waliokuwa na rai ya kutoka na kukutana na maadui nje ya mji wa Madina na waliokuwa na rai ya kutoka walikuwa ni wengi ,na kuna waliokuwa na rai ya kubakia ndani ya mji wa Madina ,na kupambana na washirikina akiwa ndani ya mji ikiwa watakusudia kuja madina,na Mtume -Rehema na mani ziwe juu yake-alikuwa enaelemea kwenye rai ya pili ya kubakia ndani ya mji wa Madina.(542) na walikuwa watu wenye rai ya kusema tutoke ili tukutane ni katika mashujaa wa kiislamu na vijana wake nawakajaa kwa Mtume-Rehema na mani ziwe juu yake- basi akaingia nyumbani kwake kisha akawatokea akiwa amevaa Ngao na ameshika silaha na akajiandaa ma mapambano,basi wale amabao walikuwa wamejaa kwake wakimshinikiza kutoka walijuta na wakasema:Ewe Mtume wa ALLAH tumekulazimisha na hatukuwa twatarajia hilo,ikiwa utataka basi

usitoke,Akasema Mtume-Sala na mani ziwe juu yake-((Haikuwa kwa Mtume pindi anapovaa mavazi yake ya kivita ayavuwe mpaka apigane)) (543)

Na kwa hakika mtume alikuwa ameona ndoto aliisimulia kwa maswahaba zake,na miongoni mwahizo ndoto kama alivyopokea Bukhari maneno yake: ((Nimeona katika ndoto hii kuwa mimi nimetikisa upanga ukakatika ncha yake ,basi ikawa taafsiri yake ni yale yaliyowapata waumini siku ya vita vya Uhud,.kisha nikautikisa tena ukarudi upanga na kuwa mzuri kuliko ulivyokuwa mwanzo,basi ikawa ni matokeo aliyokuja nayo Mwenyezi mungu katika Ufunguzi wa Makka na kukusanyika waislamu,na katika ndoto hiyo niliona Ng'ombe ,namuapia Mwenyezi Mungu kuwa ndoto hiyo ni kheri,na ikawa tafsiri yake ni waislamu siku ya ya Uhud.))(544)

Na walikuwa maquraishi wamefikia katika moja ya majangwa yaliyopo karibu na mji wa Madina akatoka mtume akiwa pamoja na aliokuwa nao miongoni mwa watu wa Madina wapatao Alfu moja,na wakati wakiwa njiani wakielekea Uhudi alirudi kiongozi wa Wanafiki aitwae Abdullahi Bin Saluul,akiwa pamoja nae Theluthi moja ya jeshi wakijivua kutomnusuru mtume-Sala na mani ziwe juu yake- na akadai Bin Ubaiyyat kuwa yeye hakufanya hivyo ila kwasababu yeye alikuwa anaona katika rai ni kubakia Madina na wakaendelea waumini pamoja na Mtume wa ALLAH-Sala na mani ziwe juu yake- (545)

Ilikuwa Uhud ndiyo mafikio ya Mtume na waliokuwa pamoja nae katika waumini,na akachagua Mtume sehemu yake mwenyewe,na akaipanga safu ya waislamu mahala hapo,akapanga kituo cha waislamu wakae katikati ya milima miwili,na akaupa mgongo mlima wa Uhud,na akachagua kilima kidogo kilichopo mbele ya watu na akachaguwa watupoa mishale wakukaa kwenye kilima hicho na akawachagulia kiongozi wao aitwae Abdullahi Bin Jubair-Radhi za Allah ziwe juu yake-na akawausia kuwa wabakie sehemu yaompaka

iwajie amri ya Bwana mtume-Rehema na mani ziwe juu yake-na wawatawanishe washirikina ili wawe mbali na waislamu kwa kuwatupia mishale,ili wasije wakawatokea waislamu kwa nyuma,na akawausia kubakia pale kwa hali yoyoteVita itakavyokuwa na wasubirie maelekezo yatakayotolewa kutoka kwa Mtume-Rehema na mani ziwe juu yake-.Amepokea Bukhari katika sahihi yake kutoka kwa Baraa Bin Aazib-Radhi za Allah ziwe juu yake-amesema-((Tulikutana na washirikina siku moja na Mtume akalikalisha Jeshi la watupa mishale na akawawekea kiongozi wao ambaye alikuwa ni Abdullah,na akasema:Msiondoke hata mkiona tumewaelemea Msiondoke mkauwacha mlima,na mkiwaona wametuelemea basi msije kutusaidia)).Al-hadith.(546)

Na akamchaguwa Mtume-Rehema na mani ziwe juu yake-Mus'ab Bin Umair -Radhi za Allah ziwe juu yake- ili kubeba Bendera ya waislamu ,na mtume akasimamamia upangiliaji Safu wa Maswahaba wake wenye kupigana jihad pamoja nae,na akawaahidi Ahadi ya ALLAH ya kuwalipa pepo,na kuwa Subra na msimamo wakati wa kukutana na maadui,kisha akawarudisha Madina baadhi ya waliokuwa ni wadogo kiumri.(547)

Na kwa upande wa washirikina alisimama kiongozi wao Ambaye ni Abuu Sufiani Bin Harbiy -Radhi za allah ziwe juu yake- kusajili wapiganaji,na walikuwa kiasi cha kinachokaribia wapiganaji Elfu tatu maradufu ya wapiganaji wa upande wa waislamu na Abuu Sufiani akawapangilia,akamuweka upande wa kulia Khalid Bin Al-waliid-Radhi za allah ziwe juu yake- na akawachukua wenye umashuhuri na wenye sauti miongoni mwao wakiwahamasisha watu kupigana,kumtokomeza Muhammad -Rehema na mani ziwe juu yake- na waliokuwa pamoja nae,na wanawake wakiquraishi wakasimama kuwahamasisha wanaume juu ya kupigana ,na wakawakumbusha kuhusu waliouliwa miongoni Mwa watu waokatika vita vya Badri katika mwaka uliopita.(548)

Vita vilianza na kila mmoja akawa amekaa sehemu yake,na akatoa Mtume Upanga wake aliokuwa nao kisha akasema nani atakae uchukua upanga huu kwa kuupa haki yake? Basi akasimama swahaba aitwae Abuu Dujaanah Bin Sammaaki Bin kharsha -Radhi za Allah ziwe juu yake- na akasema :Ewe Mtume wa ALLAH ni ipi haki ya huu upanga? Basi Mtume-Sala na mani ziwe juu yake-akamwambia kuwa haki yake ni kumpiga nao Adui mpaka uwajeruhi kisawasawa,basi akauchukuwa upanga huo Abu Dujaanah,na akatoa kwenye mfuko wake mkanda mwekundu na akaufunga kwenye kichwa chake na akanza kutembea na upanga huo kwa maringo,basi akasema Mtume-Sala na mani ziwe juu yake-((Hakika utembaji huu anauchukia ALLAH na Mtume wake isipokuwa yafaa kwenye sehemu kama hii)) (549) Na mapigano yakaanza ,na Abuu dujaana akapambana na upanga wa Mtume-Sala na mani ziwe juu yake-,upambanaji wa kishujaa (550)kama alivyopambana Hamza-Radhi za Allah ziwe juu yake- kwa ushujaa mkubwa usiokuwa na mfano,na wakapambana pia mashujaa wengine wa kiislamu,mpaka kukadhihiri kushindwa katika safu ya makafiri,na kuanza kuonekana Ushindi wa waziwazi waislamu,na washirikina wakakimbia na kutoka uwanjani,na wakawafuatilia waislamu nyuma yao wakiwauwa na wakaanza waislamu kukusanya Ngawira ,watupa mishale walipoona hilo wakiwa juu ya kilima waliondoka sehemu zao,na akajaribu Abdullahi Bin Jubair-Radhi za Allah ziwe juu yake -kuwazuia kuuwacha mlima huku akiwakumbusha Amri ya Mtume-Sala na mani ziwe juu yake-lakini wao walimuasi na wakaondoka na wala hakuna aliyebakia nae isipokuwa watu wachahche wasiozidi watu kumi.(551)

Alikuwa Khalid Bin Al-waliid-Radhi za Allah ziwe juu yake- akiwa pamoja na wapanda Farasi wa kiquiraishi wakiifuatilia sehemu ile kwa ukaribu,na alipoona Khaalid kuwa watupa mishale wamepunguwa na kuwa wachache hawawezi tena kuwazuia Farasi kuwavamia basi wakashambulia na kiongozi wao,kisha

wakawashukia waislamu kwa Farasi ,wao wakiwa wazi wazi wanaonekana wakawajia kwa nyuma ,hivyo basi jeshi la maquraishi likarudi uwanjani kuwasaidia wapanda farasi,na hivyo ukabadilika mwenendo wa vita na mambo yakawa mazuri kwa upande wa Makafiri.(552)

Na wakajaribu kufika kwa Mtume wa ALLAH wamfikie yeye mwenyewe ili wamuuwe,na wakashindana mashujaa wao katikahilo.

Na akakita mtume wa ALLAH na akapambana mapambano ya kishujaa,na akamuuwa kwa mkono wake (Ubaiyya Bin Khalaf) ambae alikuwa ni mpingaji na alikuwa akijaribu kumuuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na akirudiarudia kumtaja Muhammad!! siwezi kusalimika ikiwa atasalimika ,basi mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akakataa asimuwahi yeyote katika maswahaba wake ila yeye,pale alipo mkabili mwenyewe kwa kumchoma na Singe ilompata shingoni mwake na akafa baada ya pigo hilo.(553)

Kisha Mtume akawa ameangukia katika moja ya mashimo hivyo akajeruhiwa paji lake la uso na kuvunjwa meno yake ya mbele na akapasuliwa mdomo wake.(554)na kikajikita kikundi cha maswahaba pamoja nae Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na wakachaguwa kufa kwa ajili ya kumuhami mtume,miongoni mwao ni Abuu Twalha Al-answaariy-Radhi za Allah ziwe juu yake- na Sahli Bin Haniif,na Mus-abu Bin Umair mbeba bendera ya waislamu-ambaye aliuliwa mbele ya MtumeSala na amani ziwe juu yake-na Ally Bin Abii Twalib na Abuu Dujaana na Saad Bin Abii Waqqaas-Radhi za Allah ziwe juu yao- wote,na akasema Mtume Sala na amani ziwe juu yake,kumwambia Saad wakati huo Saad anatuma kwa ajili ya kumuhami mtume:((Tupa mishale kwa hakika nakutolea kikomboleo chako Baba yangu na Mama yangu.))(555) kama alivyokuwa pamoja naokwenye kumuhami Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Mama yake Ammaar -Radhi za Allah ziwe juu yake-.(556)

Walivumisha washirikina kuwa wamemuuwa Mtume wa ALLAH jambo hilo likadhoofisha nguvu ya waislamu basi akasimama Swahaba Anas Bin Nadhri-Rdhi za Allah ziwe juu yake- akasema ni kitu gani kinawafanya mkae? wakasema Ameuliwa Muhammad mtume wa ALLAH akasema:sasa nini mtakachofanya baada ya maisha haya Simameni na Mfe kama alivyokufa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-kisha akawageukia watu akapigana mpaka akauliwa -Radhi za Allah ziwe juu yake-na akakutikana siku hiyo na majeraha Sabini yakuchomwa na mishale nahakuna aliyemjuwa isipokuwa Dada yake kupitia vidole vyake.(557.)

Na wakauliwa Mashahidi miongoni mwa Maswahaba wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-ilifikia idadi yao maswahaba sabini,miongoni mwao ni Hamza Bin Abdul Mutwalib -Radhi za Allah ziwe juu yake-alimuuwa Hamza ni Wahshiiy naye ni kijana toka Habash (558) Na Saad bin Rabiyy (559) na Mus-aab Bin Umair(560)Na Abdullahi Bin Jahshiy (561),na Han-dhwala muoshwaji na wengine-Radhi za Allah ziwe juu yao wote,na akaelekea Mtume na aliyokuwa nao kwenye sehemu iliyopo kati ya milima miwili,na akapanda Abuu Sufiyani mlima akawa juu ya mtume na aliokuwa nao,basi akasema Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-Ewe mola wetu wa haki haiwapasi wao kuwa juu yetu,basi akapambana Omar Bin Khatwab na baadhi ya Maswahaba na wakawatupia mawe mpaka wakawateremsha,akasema Abuu Sufiani je katika hawa watu waliobakia Muhammad yupo? Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akaambiwa kuwa msimjibu,kisha akauliza katika hawa watu waliobakia je yupo Bin Abii Quhaafah?kisha akasemakatika hawa watu kuna kuna Omar Bin Khattwab? kisha Abuu Sufianiakasema kwa hakika hawa watu wameuliwa kama wangukuwa wapo Hai wangejibu,basi Omar hakuweza kujizuia nafsi yake -Radhi zaAllah ziwe juu yake-akamjibu kwa kumwambia umesema uongo ewe Adui wa mwenyezi Mungu,amembakisha Mwenyezi Mungu kwa ajili yao ili

ufedheke,kisha akasema Abuu Sufiani Hubali aliyejuu Mtume akasema mjibuni wakasema maswahaba tumjibu vipi akasema mtume mwambieni kuwa Mwenyezi Mungu aliye juu ndiyo mtukufuBasi akasema Abuu sufiani ;sisi tunae Uzza na nyie hamna Uzza akasema Mtume mjibuni wakasema tumjibu vipi?akawaambia mwambienikuwa Mwenyezi Mungu ndiye mola wetu na nyie hamna Mola kisha akasema Abuu Sufiani;tumelipizia siku hii kwa sikuya BadriBasi wakamjibuna wakasema :hakuna ubaya wafu wetu wapo peponi na wafu wenu wapo motoni kisha akasema Abuu Sufiani: kwa hakika ahadi yenu itakuwa katika viwanja vya Badri mwaka ujao.

Na kwa hakika walishiriki wanawake wa kiislamu katika vita: walikuwa wanawake siku ya Uhudi wakiwatibu majeruhi wa washirikina ,na wakiwanyweshwa maji na wakiwapa dawa majeruhi))(563)

Waliondoka maquraishi kutoka katika Ardhi ya vita ,baada ya kuangamia watu Ishirini na Nne kwa kuuwawa,na waislamu wakawatibu majeruhi wao,na miongoni mwao alikuwepo Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na Mtume akawaswalia mashahidi ambao walifikia idadi yao mashahidi sabini na wakawazika.(564)

Kisha akarudi mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na waliokuwa pamoja nae na wakauingia mji wa Madina na wanawake wakililia waliouwawa,basi Mtume wa ALLAH macho yake yalibubujisha machozi(565)

Na alikuwa mtume ni mwenyekuchukua tahadhari ya kutorudi makuraishi katika mji wa Madina, Basi akawatokea katika siku iliyofuata ili kuwasaka maadui na kuwafukuza maadui ili wasirudi katikamji wa Madina, na akasema -Sala na amani ziwe juu yake: ((Asitoke nasi isipokwa yule ambaye alihudhuria pamoja nasi jana.))(566)

Na waislamu wakafika sehemu iitwayo Hamraaul asad,(567) sawa na mwendo wa maili kumi kutoka Madina ,na wakabakia huko zaidi ya siku tatu,na habari zao zikafika kwa maquraishi,na walikuwa maquraishi wamefikiria kurudi madina na kuvamia mji madina mara nyinginena wakafahamu katika habari hiyo kuwa wanafuatiliwa na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-jambo ambalo liliwafanya warudi haraka katika mji wa Makkah.

Na kwa hakika ziliteremka Aya katika Qur'an tukufu zikizungumzia yaliyojiri kwa waislamu katika vita vya Uhud na mongoni mwa hizo Aya ni maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ إِذْ تَحُسُّونَهُم بِإِذْنِهِ ۗ حَتَّىٰ إِذَا فَشِلْتُمْ وَتَنَزَّعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَعَصَيْتُمْ مِمَّن بَعْدَ مَا أَرْسَلَكُمْ مَا تُحِبُّونَ ۚ مِنْكُمْ مَن يُرِيدُ الدُّنْيَا وَمِنْكُمْ مَن يُرِيدُ الْآخِرَةَ ۗ ثُمَّ صَرَّفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ ۗ وَلَقَدْ عَفَا عَنْكُمْ ۗ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥٢﴾ ۝ إِذْ تُصْعِدُونَ وَلَا تَلْوُونَ عَلَىٰ أَحَدٍ ۚ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ فِي أُخْرَانِكُمْ فَأَتَيْتُمُ عَمَّا لِكَيْلًا تَخْرَنُونَ عَلَىٰ مَا فَأْتَكُمْ وَلَا مَا أَصَبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٥٣﴾ ۝ ثُمَّ أَنْزَلَ عَلَيْكُم مِّن بَعْدِ الْغَمِّ أَمَنَةً نُّعَاسًا يَغْشَىٰ طَآئِفَةً مِّنْكُمْ ۗ وَطَآئِفَةٌ قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِاللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ الْأَمْرِ مِن شَيْءٍ قُلْ إِنَّ الْأَمْرَ كُلَّهُ لِلَّهِ يُخْفُونَ فِي أَنفُسِهِم مَّا لَا يُبْدُونَ لَكَ يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَّا قُفِلْنَا هَهُنَا قُلْ لَوْ كُنْتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقَتْلُ إِلَىٰ مَضَاجِعِهِمْ ۗ وَلِيَبْتَلِيَ اللَّهُ مَا فِي صُدُورِكُمْ وَلِيُمَحِّصَ مَا فِي قُلُوبِكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٥٤﴾ ۝ إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ إِنَّمَا اسْتَزَلَّهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا ۗ وَلَقَدْ عَفَا اللَّهُ عَنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٥٥﴾﴾ [آل عمران: 152-155]

Na hakika alikuthibitishieni ALLAH ahadi yake pindi mlipo wauwa kwa idhini ya ALLAH mpaka mlipo shindwa na mkatatizana katika jambo na mkaenda kinyume baada ya ALLAH kuwaonesha yale mnayo yapenda kuna miongoni mwenu wanataka dunia na kuna miongoni mwenu wanataka akhera kisha ALLAH

akawaondoshea ili wape mtihani na hakika amekusameheni na ALLAH ni mwenye fadhila kwa waumini. Pindi mlipo panda na wala hamgeuki kwa yeyote na mtume akiwaita kwa wenzenu kisha ALLAH akawatia uzito tabu juu ya tabu ili msihuzunike juu ya yale yaliyo wapiteni wala kwa yale yaliyo wapateni na ALLAH ni mwenye kueleza kwa yale mnayo yafanya. Kisha akateremsha juu yenu baada tabu usingizi ulio wafunika kikundi miongoni mwenu na kundi likapupia juu ya nafsi zao wakimdhania ALLAH bila ya ukweli dhana za kijinga wanasema hivi sisi tuna lolote katika jambo sema hakika mambo yote ni lake ALLAH wanayaficha katika nafsi yao yale wasiyo yadhahirisha kwako wanasema laiti tungekuwa sisi na chochote katika jambo tusinge uwawa hapa sema hata kama mngelikuwa ndani ya majumba yenu wangefikiwa wale ambao wamepangiwa kufa wakiwa kwenye vitanda vyao na ili apate ALLAH kuyajaribu yaliyo ndani ya vifua vyenu na apate kupembua yale yaliyo ndani ya mioyo yenu na ALLAH ni mjuzi kwa yaliyo ndani ya vifua. Hakika wale walio kimbua siku yaliyo kutana makundi mawili si vinginevyo shetanindiye aliye walelezsha kwa baadhi waliyo yachuma na hakika ALLAH amewasamehe wao hakika ALLAH ni msamehevu mpole. Al- Imraan:152-155 Kisha anasema ALLAH kutakasika na machafu ni kwake katika sehemu nyingine katika sura hiyohiyo:

﴿أُولَٰئِكَ أَصَابَتْكُم مُّصِيبَةٌ قَدْ أَصَبْتُمْ مِثْلَيْهَا قُلْتُمْ أَنَّىٰ هَٰذَا قُلْ هُوَ مِنْ عِندِ أَنْفُسِكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٥٢﴾ وَمَا أَصَابَكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ فَيَٰذَنَّا لِلَّهِ وَلَيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥٣﴾ وَلَيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا وَقِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا قَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ ادْفَعُوا قَالُوا لَوْ نَعْلَمُ قِتَالًا لَّاتَّبَعْنَاكُمْ هُمْ لِلْكَفَرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِمْ مَا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يَكْتُمُونَ ﴿١٥٤﴾ الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قَاتَلُوا قُلْ فَادْرَءُوا عَن أَنْفُسِكُمُ الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٥٥﴾ وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قَاتَلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرَزَقُونَ ﴿١٥٦﴾ فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِمْ مِنْ

خَلْفِهِمْ إِلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٧٤﴾ ۝ يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةِ مِنَ اللَّهِ وَقَضَىٰ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٧٥﴾ الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا مِنْهُمْ وَاتَّقُوا أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿١٧٦﴾ الَّذِينَ قَالُوا لَهُمْ الْتَأْسُ إِنَّ الْتَأْسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ ﴿١٧٧﴾ فَأَنْقَلَبُوا بِنِعْمَةِ مِنَ اللَّهِ وَقَضَىٰ لَمْ يَمَسَّ لَهُمْ سُوءٌ وَأَتَّبَعُوا رِضْوَانَ اللَّهِ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَظِيمٍ ﴿١٧٨﴾ [آل عمران: 165-174]

Hivi yalipo kupatani matatizo hakika mlipatwa mfano wake mkasema yametoka wapi haya sema yametokana na nyie wenyewe hakika ALLAH kwa kila kitu ji muezwa. Na hakuwapatani siku yalipo kutana makundi mawili nai kwa idhini ya ALLAH na ili apate kutambua waumini. Na apate kuwatambua wale walio kuwa ni wanafiq na wakaambiwa njooni mpigane katika njia ya ALLAH au zuieni wakasema laiti tungelitambua mapigano tusingekufuatani wao kwenye ukafiri wapo karibu zaidi kuliko imani[uislamu]wanasemakwa vinywa vyao yale yasiyo kuwa ndani mioyo yao na ALLAH ni mjuzi kwa yale wanayo yaficha. Wale ambao walisema kuwaambia ndugu zao[wanafiq]na wakakaa laiti tungewasikiliza tusingeuwawa sema zuieni nafsi zenu kifo mkiwa ni wakweli. Na wala msiwadhanie wale walio uwawa kwenye njia ya ALLAH kuwa ni wafu isipokuwa wapo hai mbele ya MOLA wao ni wenye kuruzukiwa. Ni wenye kufurahiya yale waliyo pewa na ALLAH katika fadhila zake na ni wenye kuwapata bishara kwa wale ambao hawajakutana nao baada yao wasiwe na khofu juu yao na wala hawata huzunika. Ni wenye kufurahiya neema za ALLAH na fadhila zake na hakika ALLAH si mwenye kupoteza malipo ya waumini. Wale ambao walio muitikia ALLAH na mtume baada ya kupatwa na majeraha kwa wale walio fanya mema miongoni mwao na wakamuogopa ALLAH wana malipo makubwa. Wale ambao waliambiwa na watu kuwa watu wamejikusanya kwa ajili ya -kuwapiga-basi wagopeni ikawazidishia imani na wakasema ALLAH anatutosha na ndio mbora wa kutegemewa. Basi

wakageuka kwa neema za ALLAH na fadhila haikuwapata ubaya na wakafuata radhi za ALLAH na ALLAH ni mwenye fadhila kubwa. Al-imraan:165- 174.

na hivi ndivyo ilivyokuwa vita hii ni mtihani kwa waumini na uchanganuzi aliwachagua ALLAH katika vita hiyo baadhi ya Mashadi na akawafedhehesha wanafiki katika vita hiyo,na akawasamehe waislamu,na ikawa ni katika vita muhimu za mtume kuwahi kupigana aliishuhudia yeye mwenyewe na yakampata na kuwapata maswahaba zake matatizo na balaa,na ALLAH akamchagulia katika vita hivyo idadi kubwa ya mashahidi katika uhai wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-

Watu wa Rajii:(569)

Al-Rajii ni jina la sehemu katika miji ya Hudhail uliopo kati ya makkah na Ghusafaan.(570)katika mwezi wa Swafar katika mwaka wa Nne tangu kuhama mtumewalikuja watu watokanao na Hudhal na Qaarat watokanao na Al-huun watokanao na Mudhwir,walikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu katika mji wa madina,wakasema:Ewe Mtume wa Mwenyezi mungu hakika kwetu tunawaislamu hivyo basi tuma watu miongoni mwa maswahaba wakowatufundishe dini,na watufundishe sheria za uislamu((Basi akatuma Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kikosi makini,na akawawekea kiongozi wa kikosi ambae ni Aaswim Bin Thaabit naye ni Babu yake Aaswim Bin Umar Bin Khattwab (571)na wakaenda mpaka walipofika kati ya Ghasafaani na Makkah walikumbushwa kijiji cha kabila la Hudhail liitwalo Banuu Lahyaan wakawafuatilia wakiwa karibia watupa mishale mia moja wakafuata nyayo zao mpaka wakaja sehemu waliofikia wakapata kokwa za Tende ambazo walibeba kama chakula kutoka Madina basi wakasema,hizi Tende ni za Yathriba ,basi wakafuata nyayo zao mpaka wakawakuta,na alipomaliza Aaswim na watu wake,walikimbilia Fad Fad))(572) Na wale watu wakawajia nawakawazingira na wakawaambia kuwa nyie mna ahadi na makubaliano ikiwa mtafikia kwetu kuwa tusimuuwe

mtu yeyote kati yenu,basi Aaswim akasema: ama mimi siwezi kujishusha nakuingia kwenye Dhima ya makafiri,Ewe mola wangu wa haki mpe habari zetu Mtume wako,basi wakapigana nao mpaka wakamuuwa Aaswim kwa mishalewatu wapatao saba,na akabakia Khubaib na Zaid na mtu mwingine,(573)hivyowakawapa Ahadi na makubaliano na walipowapa tu ahadi na makubaliano,waliwashukia na walipoweza kuwadhibiti tu walifunguwa kamba zao za upinde na kuwafunga nazo,akasema mtu wa tatu ambaye alikuwa na hao wawili,Huu ndiyo mwanzo wa usaliti,basi akakataa kwenda nao basi wakamshindwa na kumkokota ili waende nae lakini hakufanya hivyo basi wakaondoka na Al-haarith na Zaid na wakawauza katika mji wa Makkah,Khubaibu akanunuliwa na Banuu Haarithi Bin Aamir Bin Naufal,na alikuwa Khubaib ndiye muuwaji wa wa Al-Harithi siku ya Badri,basi akabakia kuwa mateka wao mpaka watakapokubaliana kumuuwa,aliazima kisu kwa baadhi ya mabinti wa Banii Haarithi alitaka akinowe basi yule binti akampatia,akasema yule mwanamke nikaghafilika na na kumwacha mtoto wangu akatambaa mpaka akamfikia basi Khubaibu akamchukuwa na kumuweka mapajani mwake,basi nilipomuona nilifadhaika sana na wakati huo kisu kipo mkononi mwake,basi akasema Khubaibu,je waogopea kuwa mimi nitamuuwa hapana mimi siwezi kufanya hivyo-kwa kutaka kwake ALLAH Mtukufu-na akawa yule mwanamke akisema sikuwahi kumuona hata mara moja Mateka mwenye kheri kama Khubaibu kwa hakika nimemuona akila vikonyo vya zabibu,na hali yakuwa Makkah kwa wakati huo hapakuwa na Matunda,na yeye wakati huo amefungwa kwenye vyuma,na hakuwa anapata riziki isipokuwa ile riziki ambayo ALLAH alikuwa anamruzuku,basi wakamtoa nje ya mji wa makka ulio mtukufu ili wamuuwe,basi akasema:Niwacheni niswali Rakaa mbili,kisha akawaendea,basi akasema Laukama msingeona kuwa ninaogopa kifo ningezidisha rakaa,na akawa yeye ni wakwanza kufanya kuwa ni sunna kuswali rakaa mbili kwa mwenye kutaka kuuliwa kisha akasema:Ewe mola wangu wa haki idhibiti idadi yao.kisha akasema:

Na sijali ninapouliwa hali yakuwa mimi ni muislamu.

kwa upande wowote utakaokuwa basi mauti yangu ni kwa ajili ya mwenyezi Mungu

Na hilo lipo kwenye Dhati ya ALLAH pamoja na akitaka

atavibariki viungo vilivyokatwakatwa vipande

Kisha akamwendea Uq-batu Bin Al-haarith akamuwa,Na Maquraishi wakawa wanamtafuta Aaswim ili waulete sehemu ya mwili wake kwa ajili ya kuutambua,na alikuwa Aaswim amemuwa mkubwa miongoni mwa wakubwa wao siku ya vita vya Badri,basi Mwenyezi Mungu akamtumia mfano wa kundi la nyuki likamlinda na waluo tumwa kumchukuwa,na hawakuweza kuchukuwa chochote katika mwili wake)(571)>

Na kwa hakika walikufa hawa Maswahaba wote wakiwa wanampenda mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- nakutoa kikomboleo kwa ajili ya uislamu kwa roho zao kwa kuihifadhi uislamu kwa gharama zozote,imepokelewa kuwa walipokuja kwa ajili ya kumuwa Zaid,Abuu Sufiani Bin Harbi alikuwa mshirikina,akamwambia:Ewe Zaid hivi unampenda Muhammad kwa sasa? Una nafasi yako kwetu ikiwa utamuwa hali yakuwa wewe upo kwa watu wako,akajibu Zaid-Radhi za Allah ziwe juu yake-Namuapia ALLAH sipendi hivi sasa huko alipo kwake umpate japo mwiba utakao muudhi na hali yakuwa mimi nimekaa kwa watu wangu !! Basi Abuu Sufiaya akasema:Sijahi kuona yeyote katika watu,mtu anayependa mtu mwingine kama maswahaba wa Muhammad wanavyompenda Muhammad!!(575) Kama lilivyokuwa tukio la Khubaib Bin Adiy -Radhi za Allah ziwe juu yake- pindi alipo penya mtoto mpaka akamfikia na alaikuwa kwenye chumba chake akiwa na kisu,ni wazi alikuwa nimwenye kuzuia kumwaga damu za wasio na makosa,pale ambapo mama aliogopea mtoto wake,na akatetemeka na kuingia woga na haikuwa kwa Khubaib isipokuwa ni

kuwahi kumuuliza yule mama:vipi je unamwogopea mwanao? kuwa nitamuuwa,na akajibu wakati huohuo,mimi siwezi kufanya hivyo kwa maenzi ya ALLAH na alikuwa ni mtu mwenye msingi na mlinganiaji,na hakuwa ni mtu wa kulipiza visasi na kwa namna hiyo kwa hakika tukio lake hili lilimuathiri sana huyu mama,na likabakia tukio hilo kwenye Nafsi yake akiwahadithia watu tukio hilo.

Yalikuwa haya matatizo ni makubwa na mazito kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na Maswahaba wake,lakini matatizo hayo yalikuwa ni Daawa na huu msafara ndiyo ulikuwa miongoni mwao ni mashahidi-Radhi za Allah ziwe juu yao wote-

Tukio la Biiru Maaunat:

Katika Mwezi wa Safar katika mwaka wa Nne tangu kuhama Mtume ulikuja ujumbe kutoka katika kabila la Bani Aamir ujumbe huo ukiongozwa na Aamir Bin Maalik(mtu shujaa) Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akamtangazia Uislamu(hakusilimu wala hakuukataa) na akamtaka Baraa amtume Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-akiwa pamoja nae baadhi ya Wasomi miongoni mwa maswahaba ili kuwalingania watu wa Najdi kuingia kwenye uislamu,Mtume akahofia maswahaba wake lakini Baraa akasema mimi nitawanusuru,mtume akaondoa hofu na akamwandikia barua kwenda kwa Aamir Bin Tufail,Na akamtuma Hiraam Bin Malhaan mjomba wake Anas-Bin Maalik-Radhi za Allah ziwe juu yake-na watu sabini miongoni mwa Answar na Muhaajiriina miongoni mwao ni Aamir Bin Fuhairat.(576)

Na kwa hakika walikwenda mpaka wakafika Biiru Maaunat pande za Najdi,na Hiraam Bin Malhaan akakutana na Aamir Bin Tufail,na akampa Barua ya Mtume ALLAH-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na kabla Aamir hajaisoma Barua alimuamrisha mmoja kati ya watu wake akamchoma na mkuki mgongoni mwa Hiraam,mkuki ukawa umempata sehemu inayo sababisha kufa basi akasema Hiraam,kwa nimefaulu namuapia ALLAH mola wa Alkaaba!! kisha

Aamir Bin Al-Tufail alipigia ukelele Banii Aamir wakakataa kuwahami majirani wa Abii Baraa ambao aliwafanya kuwa jirani zake, naye ni miongoni mwa watu wao, basi akaipiga tena ukelele waliokuwa jirani zao miongoni mwa Banii Saliim (Rual, Zakawaan, na Uswaibah) basi wakatoka pamoja nae kwa haraka mpaka wakamzunguka Aamir Bin Tufail na waliokuwa pamoja nae na makabila yaliyobakia wakawazunguka maswahaba wa mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na wakawauwa na wala hakusalimika katika wao isipokuwa watu wawili walikuwa kwenye kutafuta chakula cha mchana nao ni Amru Bin Umaiyat Al-Dhwamriy na Mundhir Bin Muhammad Bin Uq-bah, kisha akauliwa Mundhir Bin Muhammad na akachukuliwa Umar Bin Umaiyat akiwa mateka. Na watu walipojuwa kuwa yeye anatokana na kabila la Mudhiriyu Aamir Bin Al-Tufaili alimuwacha huru baada ya kumvuta nywele zake za utosi basi akaelekea kwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina, na alipofika njiani alikutana na watu wawili wa kabila la Banii Aamir watu hao wawili wana Ahadi na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akawauwa na hali yakuwa hajui kama wana ahadi na Mtume, alifanya hivyo kwa kulipiza kisasi kwa ajili ya watu wake waliouliwa katika sehemu ya Biiri Maauun. Na alipofika wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake- alimfahamisha yaliyotokea kwa maswahaba waliokuwa wasomi wa Qur'an, na akamfahamisha kuhusu kuwauwa watu wawili basi mtume akamwambia (kwa hakika umeuwa watu wawili nami nitatoa Dia kwa ajili yao) (577) Ama Abuu Baraa ambaye aliwaweka karibu maswahaba wa mtume wa ALLAH, alitilia mashaka kitendo cha mtoto wa ndugu yake ambaye ni Aamir, alimtilia mashaka kwa wale aliowaweka karibu miongoni mwa maswahaba wa mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- hivyo basi mwanae aitwae Rabiiyat akaenda kulipiza kisasi kwa Aamir Bin Tufail ambaye alivunja makubaliano na na kumnusuru baba yake, basi akamchoma na mkuki na wala hakumuweza hivo akamuwa. na kwa hakika Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- aliwaombea dua mbaya hawa wasaliti kwa muda wa mwezi

mzima((imepokewa hadithi kutoka kwa Anas Bin Maalik -Radhi zaAllah ziwe juu yake- amesema:Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-aliwaombea wale waliowauwa watu wa Biir Maaun siku Thalathini wakati alipokuwa akiwaombea Ra'al Walah-yaan wa Aswiyat waliomuasi ALLAH na Mtume wake)) (578) Kama alivyomuomba Aamir Bin Tuafail moja kwa moja na ALLAH akampa Tezi,na akauguwa katika nyumba ya Mwanamke atokanae na kabila la Banii Saluul,basi akachukua kupatwa na maradhi hayo na,na akawa anasema " Nimepatwa Tezi kama Tezi la Ngamia kwenye nyumba ya Mwanamke wa kabila la Saluul" Basi akapanda Farasi wake na akatoka kisha akafia mgongoni mwa farasi na akaliwa na wanyama wa mwituni na ndege,(579) na kwa hakika ilipokelwa kutoka kwa Bukhari yakuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alipopata habari za mbali za kuuliwa kwa wataalamu alisema: (Kwa hakika watu wenu wameuliwa,na hakika wao walimuomba mola wao na wakasema Ewe Mola wetu tufikishie habari kwa ndugu zetu kwa lile ambalo tumeliridhia kwako,hivyo akawapa habari kuhusu wao,basi Mwenyezi Mungu akaeremsha Aya kuhusu wao ikawa inasomwa " yakuwa wafikishie watu wetu yakuwa tumekutana na mola wetu na akatuidhia nasi pia tukamridhia") (580) Na ka hakika alihuzunika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-huzuni uliokuwa mkubwa kwa kuuliwa mashahdi katika tukio la Biiru Maaunkama alivyohuzunika kwa mashaidi wa Rajiiu,pindi ilipowafikia habari yao wakiwa katika vita vya Uhud,na ulikuwa umetokea msiba mzito,kwa haijawahi kufikia mfano wa hii idadi ya waliouwawa miongoni mwa Maswahaba katika vita ,na kwa hakika waliuwawa hawa Maswahaba kwa usaliti na hali ya kuwa wao walikuwa ni watu walioibeba Qur'an na ni walinganiaji katika njia ya ALLAH katika hatua za mwanzo kabisa,na huku kujitolea muhanga ni kwa ajli ya kujitoa fidia kwa ajli ya dini,kwenye mikono ya hawaWasaliti kitendo hiki kinatupa somo ya kuwa nikiwango gani walichokitowa maswahaba wa Mtume wa ALLAH katika kuubeba ujumbe wake na kulingania katika uislamu.

Kama amabavyo ilivyokuwa tukio la Hiraam Bin Mal-haan alipochomwa ilikuwa ni wazikuwa yeye japo alikuwa ni muhanga basi yeye alikuwa ndiye aliyenusurika,na kwa hakika amesema kweli ALLAH.

﴿قُلْ هَلْ تَرَبُّصُونَ بِنَا إِلَّا إِحْدَى الْحُسَيْنَيْنِ وَنَحْنُ نَتَرَبَّصُ بِكُمْ أَنْ يُصِيبَكُمْ اللَّهُ بِعَذَابٍ مِّنْ عِنْدِهِ أَوْ بِأَيْدِينَا فَتَرَبَّصُوا إِنَّا مَعَكُمْ مُتَرَبِّصُونَ﴾ [التوبة: 52]

Waambie ewe MUHAMMAD hivi mnatungojea tupatwe na moja kati ya mazuri mawili na sisi tunawasubiri ALLAH awapatilize kwa adhabu kutoka kwake au kwa mikono yetu basi subirini hakika sisi tupo pamoja nanyi kwenye kusubiri. Al- Taubah:52. Na kwa hakika alikuwa-Radhi za Allah ziwe juu yake- anajuwa maana ya Shahada ,na kauli yake aliyoisema Kwa hakika nimefaulu ilikuwa na Athari kubwa kwenye nafsi za waliomkuta,wkijiuliza inakuwa vipi mwenye kuuliwa kwa kusalitiwa na mwenye matatizo wakati huohuo awe ni mwenye kufaulu,kwa maneno hayo yana maana kubwa ambayo anaifahamu Hiraam Bin Mal-haan na aliyekuwa pamoja nae miongoni mwa maswahaba wa mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-

Vita vya Banii Nadhiir vilivyotokea katika mwezi(Rabiiul Awwal 4Hijiria)

Walikuwa Banii nadhiir ni miongoni mwa makabila ya kiyahudi waliokuwa wakiishi katika mji wa Madina kabla mtume hajahamia katika mji huo,na wao ni miongoni mwa mwa makabila ambao walisuluhishana katika mabila ya mayahudiwa Madina,na akaandikishiana nao mkataba katika Gazeti la madina mkataba ambao umekusanya ndani yake kusuluhishana na kuutetea mji wa Madina na kusaidiana katika kuuhami mji huo na utoawaji wa Diyat kwa mauaji ilikuwa ni miongoni mwa makubaliano.(581)

Na kwa hakika alitoka mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-mpaka kwenye majumba yao Banii Nadhiir pambizoni mwa mji

wa madina ikatafuta msaada wa Diyat kwa ajili ya watu wawili alio wauwa Amrou Bin Umaiyat Al-Dhwamriy ,baada ya kutoka salama kwenye tuko la Biiri Maaun-kama ilivyo tanguliwa kutajwa-na alaikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- amekaa kwenye moja ya kuta za majumba yao,basi wakakubaliana mayahudi wa Bnii Nadhiir kumuua kwa kujaribu kumwangukia jiwe kubwa kutoka juu ya ukuta wakijitahidi kutumia hiyo fursa,basi Malaika Jibriil akampa habari Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-walichokikusudia na walipopanda tu ili wamuangukie jiwe Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akasimama Mtume kama vile alikuwa na haja fulani na wala hakumpa habari yeyote miongoni mwa waliokuwa nao katika maswahaba,basi wakadhani kuwa atarudi ili akae sehemu ile,na ulipokuwa mda wa kumsubiri umerefuka Maswahaba walisimama na wakaanza kumtafuta na walipokutana nae Madina alawahadithia Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-usaliti wa Mayahudi na kudharia kwao kumuua,Basi Mtume akamtuma Muhammad Bin Maslamat kwa hao mayahudi awape habari kuwa mtume alishauona usaliti wao,na anawataka wahame kutoka katika mji wa Madina ndani ya siku kumi na wasipotoka watapatwa na maangamivu,na akapamba nao Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na wakapatwa na uwoga mkubwa na mkanganyiko wa hali ya juu,na wakajuwa kuwa Usaliti wao ALLAH mtukufu ameudhihirisha (583)Basi wakaanza kuwasiliana na wanafiki wa Madina na kiongozi wao mkubwa alikuwa ni Abdullahi Bin Ubaiyyat Huenda wakapata kutoka kwao utatuzi na msaada ,basi Wanafiki wakawapa matumaini nawakawataka kufanya Subra na wasitoke na wakawa ahidi kushiriki mapigano pamoja nao ikiwa watahitajia kufanya hivyo.(583)na kwao wao ndipo iliteremka kauli yake ALAH mtukufu:

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ بَشِيرٌ إِنْتُمْ

لَكَذِبُونَ ﴿١١﴾ لَيْنٌ أُخْرِجُوا لَا يَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِن فُوتِلُوا لَا يَنْصُرُونَهُمْ وَلَئِن نَّصَرُوهُمْ لَيُوَلِّنَنَّ
 الْأَدْبَرَ ثُمَّ لَا يُصَرُّونَ ﴿١٢﴾ [الحشر: 11-12]

Je umepata kuwaona wale ambao wali kuwa wanafiki wanasema kwa ndugu zao wale ambo walio kufuru miongoni mwa mayahud na manaswara kama mtatolewa hakika tutatoka na nyie na hatuta mtii kwenu nyinyi yeyeto milele na kama mtauwawa tuta wanusuru na ALLAH anatambua kuwa wao ni waongo. Na kama watatolewa hawatatoka pamoja nao na kama watauwawa hawata weza kuwanusuru na kama wata wanusuru watakimbia kurudi nyuma kisha hawatanusuriwa. Al-hash-ri 11-12.

Na alipotambua mtume-ALLAH na amani ziwe juu yake- upingaji wao na maandalizi yao ya kupigana ,na kile walichokidhihirisha wanafiki katika kuwanusuru,Mtume aliliamrisha jeshi lake la maswahaba kujiandaa,na wakamuwacha katika mji wa Madina Abdullahi Bin Umme Maktoum na akaibeba Bendera yake mtume Ally Bin Abii Twaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake- (584) nawatia kizuizini kabila la Banii Nadhiir kwa muda wa masiku kumi na yaliendelea mapigano kati yao,na Akaanza Mtume kukata mitende yao kwa Idhini ya ALLAH ili wakate tamaa na na wapate hasara na waingiwe na uwoga katika nafsi zao,na iwe ni msukumo wa kuingia kwao kwenye kujisalimisha haraka,hivyo banii Nadhiir wakasema:Muhammad anakataza ufisadi na yeye anaangamiza na kukata mtende yetu,basi lkaja nenolake,ALLAH Mtukufu:

﴿مَا قَطَعْتُمْ مِّن لِّينَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَىٰ أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْرِجَ الْفَاسِقِينَ﴾

[الحشر: 5]

Hamkuyakata matunda na hamkuyaacha yakiwa yamesimama juu ya matawi yake isipokuwa kwa idhini ya ALLAH na ili awalipe watu waovu. Al-hashiri :5/585. Na mtume-Sala na amani ziwe juu yake-aliwawekea kizuizi kikali na wanafiki wakawa

wamewadanganya na wala hawakuwanusuru,hivyo basi Mayahudi wakajuwa matokeo ya Usaliti wao,na mtume akawa amewashinda na ALLAH akatia uoga kwenye uoga licha ya kuwa walikuwa wamejiandaa,basi wakamuomba Mtume wa ALLAH awaachie watoke na asimwage damu zao na kuwaruhusu kuchukuwa kiasi kidogo akiwezacho ngamia kukibeba miongoni mwa mali zao isipokuwa Silaha ,(586) basi wakajisalimisha kwa sharti hili,na wakapewa masiku maalumu ya kuondoka.

Na amesema ALLAH Mtukufu:

﴿هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ مَا ظَنَّتُمْ أَنْ يَخْرُجُوا وَظَنُّوا أَنَّهُمْ مَانِعَتُهُمْ حُصُونُهُمْ مِنَ اللَّهِ فَأَتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ يُخْرِبُونَ بُيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ الْأَبْصَارِ﴾ [الحشر: 2]

Ni yeye ALLAH ndiye aliye watoa wale ambao walio kufuru miongoni mwa mayahudi na manaswara kwenye miji yenu mwanzo mwanzoni mwa sham,hamkudhania kuwa hawatatoka na wao wakadhania kuwa wao matarajio yao ni kinga kutoka kwa ALLAH kisha ALLAH akawajilia kwa namna wasiyo tarajia na akaingiza ndani ya nyoyo zao uwoga wakivunja majumba yao kwa mikono yao na mikono ya waumini basi pateni mazingatio enyi wenye maono(2). Al-Hashri:2,587. Kisha wakatoka wakiwa kundi kubwa lenye ushupavu na wakipeana moyo wakusubiri wakiandamana pasina kujali chochote basi wakatoka ((Wakiwa na wanawake na watoto ,na pamoja nao wakiwa na Madufu na Mazumari,na mapambo wakisongamana nyuma yao kwa mapambo na kujifaharisha ,haijapata kutokea kuonekana kabla ya hapo katika zama zao watu wengi kama hao))(588) Na kwa kuondoka kwao ALLAH aliwapumzisha waislamu kutokana na shari zao,na kuzuia maudhi yao,Na hivyo walisilimu miongoni mwao watu wawili basi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akaziwachilia mali zao(589)Na

kwa hakika iliteremka kwa Banii Nadhiir Suratil Hash-ri yote,(59) mwanzo kabisa sura hio ilihusisha mazungumzo kuhusu mayahudi katika maneno yake:

﴿سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾ هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ مَا ظَنَّتُمْ أَنْ يَخْرُجُوا وَظَنُّوا أَنَّهُمْ مَا يَعْتَمِدُونَ خُصُونَهُمْ مِنَ اللَّهِ فَأَتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا وَقَدَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ يُجْرِبُونَ بَيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ الْأَبْصَارِ ﴿٥﴾ وَلَوْلَا أَنْ كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْهِمُ الْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٦﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَمَنْ يُشَاقِ اللَّهَ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٧﴾ مَا قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْتَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَى أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْزِيَ الْفَاسِقِينَ ﴿٨﴾ وَمَا آفَاءَ اللَّهِ عَلَى رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْحَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ وَلَا كِنٍ اللَّهُ يُسَلِّطُ رَسُولَهُ عَلَى مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٩﴾ [الحشر: 6-1]

Vina mtakasa ALLAH viumbe wa mbinguni na viumbe wa aridhini na yeye ni mwenye nguvu na mwenye hekima. ni yeye ambaye aliye watoa wale ambao walio kufuru miongoni mwa mayahudi na manaswara kwenye majumba yao mwanzo mwa mji wa sham,hamkudhaniakuwa watatoka na wao pia wakadhani kuwa wao matarajio yao ni kinga kwao kutoka kwa ALLAH kisha ALLAH akawajia kwa namna hawakutarajia na akaingiza ndani ya mioyo yao uwoga wakivunja majumba yao kwa mikono yao na mikono ya waumini basi zingatieni enye wenye muono. Na kama si ALLAH kuwaandikia kifo juu yao hakika angwapa adhabu duniani na wanayo wao siku ya mwisho adhabu ya moto. Hayo waliyo yapata ni kwakuwa wao walikwenda kinyume na ALLAH na mtume wake na atakaye kwenda kinyume na ALLAH na mtume wake hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. Na hakukata matunda na hamkuyaacha yakiwa yamesimama kwenye mashina yake isipokuwa ni kwa idhini ya ALLAH na ili apate kuwalipa watu wachafu. Na yale ALLAH aliyo mpa mtume wake miongoni mwenu

na wala hamkuifanyia haraka ya wanyama kutokana na farasi wala misafara isipokuwa ALLAH anamsalitishia mtume wake kwa anaye mtaka na ALLAH kwa kila kitu ni muweza. [Al-hashri 1-6]²⁵⁶²⁵⁷

Kama ambavyo sura nyingine zilizobakia kuna ndani yake yanayo usiana na Ngawira na hukumu zake,na ikawa ni Nidhamu ya mali na ni hukumu ya kisheria ya kuamiliana na kile kinachiochumwa kutoka kwa maadui pasina kuwepo mapigano,na hayo yamesemwa katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿مَا آفَاءَ اللَّهِ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ
وَأَبْنِ السَّبِيلِ كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ
عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥﴾ لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ
وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ﴿٦﴾
وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً
مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شَحْنًا فَلْيُكْفِمْ هُمْ
الْمُفْلِحُونَ ﴿٧﴾ وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ
وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٨﴾﴾ [الحشر: 10-7]

Mali aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa mtume wake kutoka kwa watu hawa wa hivi vijiji basi ni kwa ajili ya ALLAH na mtume na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na wapita njia ili isibakie ni yenye kuliwa baina ya matajiti miongoni mwenu

²⁵⁶ Na alikuwa bin Abas akiita sura hiyo kuwa ni sura ya Banii Nadhiir,sahihi Bukhariy,Kitabu Tafsiir,mlango wa Tafsiir,suratil Hashir,Hadithi 4882;Na Bin Kathiir ,Tafsiir yake juzuu ya 2/1844.

²⁵⁷ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 3/192.

atakacho kupeni mtume chukueni na kile atakacho kukatazeni kiacheni na muogopeni ALLAH hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. Basi na wapewe mali hiyo mafukara wa kimuhajirina ambao walio tolewa kwenye miji yao na mali zao wakitafuta fadhila za ALLAH na kuridhiwa na wakimnusuru ALLAH na mtume wake hao ndsio wakweli. Na wale ambao walifanya Maskani yao hapa na wakautakasa uislamu wanawapenda wale walio hamia kwao na wala hawapati ndani ya vifua vyao mashaka kwa yale waliyo yatoa na wanawapendelea ndugu zao zaid ya nafsi zao hata kama ni wenye kuhitajia na atakaye jizuilia ubakhili wa nafsi yake basi hao ndio walio faulu. Na pia wapewe mali hiyo wale walio kuja baada yao wanasema MOLA wetu tusamehe sisi na ndugu zetu walio tutangulia katika imani na usitujaliye ndani ya nyoyo zetu kinyongo kwa wale ambao walio amini MOLA wetu hakika wewe ni mrehemevu mpole. Al-Hashri: 7-10. Na kwa hakika Aya zimesheheniSifa za kuwasifia Muhaajiriina na Answaar ,na kuzungumzia ufakiri wa Muhaajiriina na kujitolea kwao.na kwa hakika amesema Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- Ikiwa mtapenda nitaigawanya kati yenu na Muhaajiriina kile alichu nipa ALLAH kutoka kwenye kabila la banii Nadhiir,na walikuwa Muhaajiriina wakimiliki walivyokuwa navyo miongoni mwa Makazi katika majumba yao na Mali zao,na ikiwa mtapenda nitawapa na watatoka kwenye majumba yenu)) Basi Saad Bin Ubaadah na Saad bin Muaadh wakasema-Wakubwa wa Answaar-Ewe Mtume wa ALLAH,twachagua uzigawanye kati yetu na sisi Answaar na Muhaajiriina na wabakie kwenye majumba yetu kama walivyokuwa,na Answaar nao wakajibu kwa kusema Tumeridhia na kujisalimisha ewe Mtume wa ALLAH,Basi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akasema:((Ewe Mola wangu warehemu Answaar na waoto wa Answaar),(592) na akagawanya Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-Mali na nyumba kati ya Answaar na Muhaajiriina,na akampa mtum mmoja katika mafukara wa Kianswaar na alikuwa Mukhairrki mmoja miongonimwa matajiri wa kabila la banii Nadhiir

amesilimu kabla ya vita vya Uhud na kapigana kwa kushirikiana na waislamu,na akasema ikiwa nitauwawa basi mali yangu ni Muhammad afanyie atakacho,na kisha akauliwa na alikuwa mashamba saba Mtume aliyatowa kuwa wenye kuhitajia katika waislamu(593) na ikathibitika kuwa Answaar wao ni ndiyo wakusudiwa kwa vile alivyowasifia ALLAH.

﴿وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْتُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ﴾ [الحشر: 9]

Na wale ambao walifanya maskani yao haoa kwa utakaso wanawapenda wale walio hamia kwao na wala hawapati ndani ya vifua vyao tabu kwa yale waliyo yatoa na wanawapendelea wenzao zaidi ya nafsi zao hata kama watakuwa ni wenye kuhitajia na atakaye jizuilia ubakhili wa nafsi yake basi hao ndio walio faulu. Al-hashir:9)

Na alipotaka Omar Bin Khattwab-Radhi za Allah ziwe juu yake- (594) kuweka kodi ya Ardhi na kuanzisha mafaili wakati wa utawala wake aliwakusanya Maswahaba -Radhi za Allah ziwe juu yao- miongoni mwa wenye kuchuliwa rai zao katika watu wa Madina na akajadiliana nao kuhusu kugawanya ardhi kwa walioukombowa mji wa makka au kuwacha kuigawa na kuiwekea kodi,kisha wafaidi waislamu wote kutokana na mapato kwa kutumia njia ya faili,na kwa hakika alitaka Omar-Radhi za Allah ziwe juu yake- kukumbushia tukio la Banii nadhiir na akatolea ushahidi kwa Aya zilizokuja kuhusu tukio hilo,na kuwa watakao kuja katika Kizazi cha waislamu wawe na haki katika mali hii kwa kutumia chanzo kitokanacho namaneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ﴾ [الحشر: 10]

Na wapewe pia mali hiyo wale walio kuja baada yao wanasema MOLA wetu tusamehe sisi na ndugu zetu walio tangulia katika imani na wala usitujalie ndani ya nyoyo zetu vinyongo kwa wale walio amini MOLA wetu hakika wewe ni mrehemevu mpole. Al-Hash-ri:10)

Na kwa hakika amaepokea Abuu Yusuf katika kitabu chake kiiitwacho "Al-Kharaaj"(Kuwa Omar Bin Khattwab -Radhi za Allah ziwe juu yake- aliwashauri watu kuhusu Ardhi walipoufungua mji,basi wote wakaona kuwa igaiwe ,na alikuwa Bilali Bin Rabaah nimwenye kutilia mkazo kuhusu hilo,na akaona Omar -Radhi za Allah ziwe juu yake- aiwache na wala asiigawe,basi akasema: Ewe mola wangu niepushe na rai ya Bilal na watu wake,na wakabakia kwenye jambo hilo kwa muda wa siku mbili au tatu au chache kuliko hizokisha akasema Omar,-Radhi za Allah ziwe juu yake- kwa hakika mimi nimepata Hoja ,amesema ALLAH Mtukufu katika kitabu chake:)

﴿وَمَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ وَلَكِنَّ اللَّهَ يُسَلِّطُ رُسُلَهُ عَلَى مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾ [الحشر: 6]

Na Mali aliyoleta ALLAH kwa mtume wake miongoni mwenu basi hamkuyaendeshea mbio farasi wala misafara isipokuwa ALLAH anamsalitishia mtume wake kwa anaye mtaka na ALLAH kwa kila kitu ni muweza. Al- hashir:6 Mpaka akamaliza jambo la Banii Nadhiir,hoja hii ni yenye kuenea katika Ngawira zote kisha akasema:

﴿مَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٧﴾﴾ [الحشر: 7]

Yale aliyo yatekeleza ALLAH kwa mtume wake kutokana na watu wavijiji basi ni kwa ajili ya ALLAH na mtume wake na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na wapita njia ili isiwe ni chakula chenye kuliwa baana ya matajiri miongoni mwenu na atakacho kupeni mtume chukueni na atakcho kukatazeni kiacheni na muogopeni ALLAH hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. [Al-Hashr 7] Kisha akasema :

﴿لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ﴿٨﴾﴾ [الحشر: 8]

Basi na wapewe mali hiyo kwa ajili ya mafukara wa kimuhajirina wale ambao walo tolewa kwenye miji yao na mali zao wakitafuta fadhila za ALLAH na kuridhiwa na wana mnusuru ALLAH na mtume wake hao ndio walio wakweli. Al-hashri:8. Kisha hakuishilizia hapo tu na akawachanganya na wangineo na akasema:

﴿وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْتُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾﴾ [الحشر: 9]

"Na wale walio andaa makazi na imani kabla yao, wanawapenda wale walio hamia kwao na wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa yale wanayo yatoa na wanawapendelea zaidi ya nafsi zao hata kama ni wenye kuhitajia na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake basi hao ndio walio fanikiwa". Al-hashir:9) Na haya ndiyo yaliyotufikia - Mwenyezi Mungu ndiye

Mjuzi zaidi- walikuwa Answaar wana chao maalumu kisha hakuishia hapo mpaka akawachanganya na wengineo basi akasema:

﴿وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ﴾ [الحشر: 10]

Na wale walio kuja baada yao wanasema MOLA wetu tusamehe sisi na ndugu zetu walio tangulia katika imani na usijalie ndani ya mioyo yetu vinyongo kwa wale walio amini MOLA wetu hakika wewe ni msamehevu mple. Al-Hash-ri:10) Basi ikawa ni ya wote haki kila aliyekuja baada yao,kwa imekuwa hii Ngawira na hawa wote,vipi tuwagaie hawa na twaache waliokuja baada yao wasigaiwe,basi akagawanya kilichobakia na akakusanya Kodi yake,amesema Abuu Yusuf: Alichokiona Umar-Radhi zaAllah ziwe juu yake-kwenye kuzuia kuzigawa Ardhi kwa wale walioifunguwa ni pale ambapo Allah alimfahamisha kilichopo kwenye kitabu chake yakuwa jambo hilo ni Taufiiq kutoka kwa ALLAH ndiyo maana likawa lile alilofanya,na katika hilokuna khaeri kwa Waislamu wote ,na katika jambo aliloliona la kukusanya kipato na kukigawa kwa Waislamuwote kuna kuenea manufaa kwa umma wote,kwa sababu jambo hili kama lisengekuwa limeegemezwa kwa watu kwenye kupewa na kuapatiwa rizki,madeni yasingelipwa wala majeshi yasingekuwa na nguvuya kwenda katika Jihad.(595).

Nakwa hakika zimamilizia Aya za Surat Al-Hashri na kutaja habari za Wanafiki na ikawafungamanisha na mayahudi katika maneno yake Mwenyezi mungu Mtukufu:

﴿أَلَمْ تَر إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِن أُخْرِجْتُمْ لَخُرُجْتُمْ مَعَهُمْ وَلَا تَطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِن قُوتِلْتُمْ لَنَنصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١١﴾ لَئِن أُخْرِجُوا لَا يَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِن قُوتِلُوا لَا يَنْصُرُونَهُمْ وَلَئِن نَّصَرُوهُمْ لَيُوَلِّنَنَّ الْأَدْبَرَ ثُمَّ لَا يُصَرُّونَ ﴿١٢﴾﴾ [الحشر: 11-12]

umepata kuwaona wale ambao walikuwa wanafiq wanasema kuwaambia ndugu zao walio kufuru miongini mwa mayahudi na manaswara kama mtatolewa hakika tutatoka pamoja nanyi na hatuto mtii miongoni mweni yeyote milele na kama mtauwawa hakika tutawanusuru na ALLAH atafahamu hakika wao ni waongo. Kama watatolewahawatatoka pamoja nao na kama watauwawa hawata wanusuru na kama wata wanusuru watakimbia kurudi nyuma kisha hawatanusuriwa. Al-hash-ri 11-12. Kama vile ambavyo Aya hizi ziliweka wazi kuhusu Tabia za Mayahudi na uoga wao na mbinu zao za kivita katika maneno yake Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿لَا يُقْتَلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرَى مُحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ جُدُرٍ ۚ بَأْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ تَحْسَبُهُمْ جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ﴾ [الحشر: 14]

Hawata pigana nanyi pamoja isipokuwa ndani ya miji iliyo zingirwa au nyuma ya ukuta ubaya ulopo baina yao ni mkali utadhani wapo pamoja na mioyo yao ipo tofauti hayo yaliyo wapata ni kwakuwa wao ni watu wasio kuwa na akili. Al-hashri:14)

Na hayakuwa Mahandaki ambayo mayahudi wanayajenga huko Palestina isipokuwa ni nikusadikisha kilichokuja kwenye hizi Aya kutoka kwa Bani Nadhiir na haswa mayahudi wote katika kila mahala na kila zama.

Vita vya Makundi(Al-Han-Ndaki) katika mwezi Shawwal mwaka wa 5):(596.)

Na sababu ya kupiganwa vita ni kuwa kundi miongoni mwa wakubwa wa kiyahudi katika mji wa Madina walikwenda Makka,na wakawa wakwahimiza maquraish kumpiga vita mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-katika mji wa Madina,na wakawa ahaidi kuwa wao watawasaidia Maquraish mpaka wamtokomeze Muhammad-Rehema na amani ziwe juu yake-pamoja na waliokuwa nae,na wakawapa Fat-wa kuwa dini ya Maquraishi ni bora kuliko Dini ya

Muhammad -**Rehema na amani ziwe juu yake**-na kwa hao mayahudi na kauliyao iakateremka kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu

﴿أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْجِبْتِ وَالطُّغُوتِ وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ
كَفَرُوا هَؤُلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا سَبِيلًا﴾ [النساء: 51]

Umepata kuwaona wale walio pewa fungu miongoni mwa kitabu wanaamini mizimu na miungu inayo abudiwa kinyume na ALLAH na wanasema kuambia wale walio kufuru kuwa je hawa ndiyo wapo kwenye njia iliyonyooka zaidi kuliko walioamini) (Al-Nisaai 51)(597) basi maquraishiwakajibu kwa madai ya Abuu Sufiani katika hilo.

Kisha hilo kundi la Mayahudi walielekea Ghat-faan na makabila mengine miongoni mwa makabila ya Najdiwakawaita waende kupigana na waislamu wa Madina na wakawaahahidi na wakawatamanisha kama walivyofanya pamoja na maquraish,na wakaweza Mayahudi kutengeneza makundi ya kumpiga vita Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na waliokuwa pamoja nae.(598)

Na alikuwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kama kawaida yake akifuatilia habari za maadui wake miongoni mwa Maquaishi na wengine,na kwa hakika wapelelezi wake walimjia na habari kabla ya watu kuondoka,na kilichofuata aliwakusanya Maswahaba na kuwataka ushauri wa kuwa ni jambo gani linampasa yeye kulifanya ili kukabiliana na uadui ujao,na haswahaswa ukizingatia kuwa maadui wamekuwa wengi katika mji wa Madina ,na huenda wasiweze watu wa Madina kukabiliana na hizo nguvu za maadui.

Na ikawa moja ya Rai iliyotolewa kutoka Salmaan Al-faarisiy-Radhi za Allah ziwe juu yake-alichimba Handaki pembeni mwa mji wa Madina ,akiwazuia wapanda farasi na watembea kwa miguu kuparamia ,na wakati huohuo,akiwawezesha waislamu kuilinda na haswa hali ya Kijiografia ya mji wa madina ilikuwa inafaa sana

kufanya hivyo,na kwa hakika alipendezesha Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-hiyo fikra,(599)na akachora sehemu zilizochaguliwa kuchimba mahandaki,na akagawanya kazi kwa maswahaba wake,na kikawa kiwango cha uchimbali kwa kila watu kumi ni Dhiraa Arubaini,na mtume akafanya kai na maswahaba wake kwenye kuchimba,pale ambapo alikuwa akipiga Sururu na akaibeba Udongo kwa mikono yake mitukufu.

Alikuwa Mtume akihamisha Udongo siku ya Han-dak mpaka tumbo lake likajawa na vumbi,na akawa anarudiarudia maneno ya maswahaba :

Twamuapia Mwenyezi mungu lau kama siyo Mwenyezi mungu tusinge ongoka.

Na wala tusinge toa swadaka wala tusinge swali.

Basi tuteremshie Utulivu juu yetu.

Na ututhibitishie pindi tutakapo kutana na maadui

hakika wale ambao wametufanyia dhulma na uadui.

wakitaka kutufitinisha kwenye Dini yetu tuwe niwenye kukataa hilo.(600)

Kutoroka kundi la wanafiki wakikimbia kutekeleza wajibu waliopewa,nao ni wale ambao amewataja Mwenyezi mungu mtukufu katika maneno yake:

﴿لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَسْتَلُونُ
مِنْكُمْ لَوْأَدَّأً فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾
[النور: 63]

Msilinganilishe mnavyo muita mtume kama jinsi mnavyo itana baadhi yenu kuwaita wengine hakika ALLAH amewajua wale

ambao wanao toka kwa kunyata miongoni mwenu basi wachukue tahadhari wale wanao kwenda kinyume kunako jambo lake wasije patwa na fitna au wakapatwa na adhabu kali. [An Nur 63] Na walikuwa waislamu akitaka mmoja wao kuiendea haja fulani walikuwa hawaondoki mpaka wapatiwe ruhusa na Mtume,basi Mwenyezi Mungu akawasifia katika maneno yake:

﴿إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ء وَإِذَا كَانُوا مَعَهُ عَلَىٰ أَمْرٍ جَامِعٍ لَّمْ يَذْهَبُوا حَتَّىٰ يَسْتَأْذِنُوهُ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ فَإِذَا أَسْتَأْذَنُوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأَذَنَ لِمَن شِئْتَ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ ۗ إِنَّ اللَّهَ ۖ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿62﴾﴾ [النور: 62]

Si vinginevyo waumini ni wale ambao walio muamini ALLAH na mtume wake na wanapo kuwa pamoja naye kwenye jambo la pamoja hawaondoki mpaka wamtake idhini hakika wale ambao wanao kutaka idhini hao ndio ambao wanao muamini ALLAH na mtume wake basi watakapo kutaka idhini kwa baadhi ya mambo yao mpe idhini umpendaye miongoni mwao na uwaombee msamaha hakika ALLAH ni mfuta madhambi mpole. [An Nur 62](601)

Na wakati wa kuchimba Handaki waislamu walikutana na mwamba mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akasimamaili kuupasua mwamba huo na alipoupiga ukatoka mwanga katika ule mwamba basi Mtume akapiga Takbira na waislamu pia wakafuatishiakwa kuleta Takbira kisha akaupiga mwamba kwa mara ya pili mwamba ukatoa mwanga kisha akapiga Takbira na waislamu wakapiga Takbira pamoja naena kwa hakika alisema Mutme baada ya pigo la kwanza:(Allahu Akbaru nimepewa Funguo za Sham ,namuapia ALLAH kwa hakika mimi ninaona Majumba mekundu hapa hivi sasa,kisha akapiga mara ya pili akasema Allahu Akbar Nimepewa funguo za Fursi Namuapia ALLAH ninaona majumba yamiji meupe,kisha akapiga mara ya tatuna akasema Allahu Akbar nimepewa funguo za Yemeni hakika mimi ninaona

Milango ya ya Sana'a hapa nilipo hivi sasa)) (602) Hivyo wakafurahi waislamu kwa habari hii nzuri,na kwa tukio hili alipata Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-matumaini na waislamu pia wakapata matumaini kuwa wao watawashinda hao wafleme na wataifungua wataikomboha miji yao na wakasadikisha kile alichwa wa ahidi Mweyezi mungu na Mtume wake.

Ama wanaafiki wakaanza kukejeli aliyoyataja Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kwa yanayohusiana na aahadi ya ALLAH:

﴿وَإِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ إِلَّا غُرُورًا ﴿١٢﴾﴾

[الأحزاب: 12]

Pindi walipo sema wanafiq na wale ambao kwenye nyoyo zao kuna maradhi ALLAH na mtume wake hawajatupa ahadi isipokuwa ni udanganyifu. Al- Ahzaab:12

Na Maquraish pamoja na makundi wakafika na ilikuwa idadi yao ni wapiganaji Eflu Kumi,na wakaweka kambi pambizoni mwa Madina,na wakashangaaa kuyakuta Mahandaki,pale ambapo waarabu hawakuwa ni wenye kuchimba mahandaki,na akaweka kambi mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na waliokuwa pamoja nae,karibia wapiganaji Jihad Eflu tatu,baada ya kuwa wamekwisha wakusanya wanawake na watoto katika Ngome ya Answaar.(603)

Na wakati ulikuwa ni mgumu sana pale ambapo waislamu hawakuwa na amani kwenye Nafsi zao siyo usiku wala mchana,na ukizingatia kuwa Mayahudi wa Banii Quraidhwa walikuwa upande wa Madina (604) na waislamu walikuwa wamewapa ahadi ya kushiriki kuulinda mji wa Madina ,lakini pamoja nahivyo walikuwa hawana imani na Mayahudi kuendelea na ahadi zao,na kilichofuata Waislamu walihisi kutokea hatari ambayo itawagusa kila upande,kama alivyosifia Mwenyezi Mngu hilo:

﴿إِذْ جَاءُوكُم مِّن فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونًا ﴿١٠﴾ هُنَالِكَ ابْتُلِيَ الْمُؤْمِنُونَ وَزُلْزِلُوا زِلْزَالًا شَدِيدًا ﴿١١﴾﴾ [الأحزاب: 10-11]

"Pindi walipo kujieni kwa juu yenu na chini yenu na pindi yalipo kodoka macho na nyoyo zikapanda kooni na mkamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali. (10) Hapo ndipo walipo jaribiwa waumini na wakatikiswa mtikiso wa nguvu. (11) Al-hzaab 10-11(605).

Na vikosi vya makundi vikaanza kupeleleza mahandaki huenda wakapata upenyo watakaopitia humo,na wakaweza kundi lao moja la wapiganaji kubombo Handaki katika sehemu moja ,lakini jeshi la kiislamu wakiwa na kiongozi wao Ally Bin Abi Twaalib -Radhi za Allah ziwe juu yao-waliweza kuwazuia na kuwauwa baadhi yao,basi akaamrisha Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuwasalimisha Wafu wa kiquiraish,na wala hakuridhia kuchukuwa mbadala katika hilo.(606)

Na kwa hakika waislamu waliendelea usiku na mchana wakililinda Handaki na wakiwazuia watu kutoyaharibu mahandaki,na Mtume alikuwa yeye mwenyewe akitilia umuhimu katika kulinda sehemu zilizokuwa Dhaifu,na kwa hivyo Makundi yalijaribu ili wapate Mbinu nyingine ya kuharibu ngome ya waislamu,na walikuwa pamoja na makundi palikuwepo na Mayahudi na kiongozi wao ni Huyaiy Bin Akh-twab,ambae alielekea kwa Mayahudi wa Banii quraidhwa kwenye Ngome yao,na akatoa Juhudi mbalimbali zitokanazo na vitimbi na hila mpaka wakaweza kumkinaisha kiongozi wa Banii Quraidhwa kwa kuvunja makubaliano ambayo yalikuwa kati yao na waislamu,na kwa hakika walikuja wapelelezi wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-wakimpa habari kuhusu Ziara ya Huyaiy Bin Akh-twab kwa Banii Quraidhwa na kuvunja kwao makubaliano na waislamu,na ahadi yao kwa maquraishi ya kushirikiana dhidi ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-pamoja nae waislamu,na

Mtume akahuzunika kutokana na habari hii,na akataka kuhakikisha kuhusu habari hiyo yeye mwenyewe,na wakati huohuo alijitahidi asijue suala hilo yeyote miongoni mwa waislamu ili isiwavunje nguvu na kuathiri Dhamira yao. Na kwa hivyo Mtume aliwatuma watu wa Nne wa Madina ambao walikuwa na mahusiano na ushirika pamoja na Banii Quraidhwa,miongonimwao ni Saad Bin Muaadh na Saad Bin Ubaadah,Mabwana wa Ausi na Khazraj,na akawaamrisha kuwatembelea Banii Quraidhwa katika Ngome zao,na kuhakikisha habari,nakuwaficha watu jambo la kuwa watu wameshasaliti,na wamfikishie mtume maneno ambayo kwa maneno hayo utajulikana msimamo,basi wakatoka watu mpaka kwa Banii Quraidhwa na wakakutana nao,wakalichunguza jambo kwa pamoja ,basi mayahudi wakamtukana sana mtume na maswahaba wakena wakasema,kutoka kwa Mtume sisi hatuna makubaliano wala mkataba basi Saad Bin Muaadhi akawapa Nasaha na akawaogopesha kutokana na matokeo ya kufanya Khiyana-na alaikuwa ni mshirika wao-basi wakamjibu majibu machafu,basi ujumbe ukarudi kwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-wakamwambia:hakika mayahudi wamesaliti kma walivyosaliti (607) nayo ni makabila mawili ambayo yaliwasaliti watu wa Rajii(608)na Balaa likazidi kwa waislamu,na mayahudi wakashirikiana na washirikina na wanafiki katika kufikisha habari za usaliti wa Mayahudi,na Unafiki na wanafiki ukatokeza waziwazi kwa nguvu zote.

﴿وَإِذْ قَالَتْ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوا وَيَسْتَأْذِنُ فَرِيقٌ مِّنْهُمُ النَّبِيَّ يَقُولُونَ إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ إِن يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا ﴿١٣﴾﴾ [الأحزاب: 13]

Na pindi ilipo sema kundi miongoni mwao enyi watu wa madina hamna nyinyi sehemu rudini na wanamtaka idhini mtume kikundi miongoni mwenu na wanasema hakika miji yetu ipo tupu na hali ya kuwa haipo tupu hawana wanacho kitaka isipokuwa ni kukimbia. Suratul Ahzaab:13 Na ikazidi mitihani kwa waislamu,pale

ambapo makundi yalipata nguvu kwa kujiunga Banii Quraidhwa,na wakajaribu baadhi ya Mayahudi kuwafanyia uadui wanawake wa kiislamu wakiwa katika ngome,basi wakajitetea wao wenyewe utetezi wa kishujaa ,na wakiwa na kiongozi wao ambae ni Safiyyat Bint Abdul Mutwalib Shangazi yake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-(609)

Na katika hali hii ngumu Nuaimu Bin Mas'ud Al-ashjaini -Radhi za Allah ziwe juu yake alikuja kwa Mtume akitokea Ghatfaan na alikuwa amekuja na makundi basi akakutana na Mtume Rehema na amani ziwe juu yake na akasema-Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hakika mimi nimesilimu na watu wangu hawajui kusilimu kwangu basi niamrishe jambo lolote utakalo,basi mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akataka kufaidi kutoka kwa huyu mpiganaji vita asiyejulikana kwa kadri awezavyo, basi akamwambia hakika wewe ni mtu mmoja tu basi tufanyie udanganyifu kwa maadui kiasi uwezavyo,kwani kwa hakika vita ni kudanganyana(610) basi akatoka Nuaimu Bin Masoud-Radhi za Allah ziwe juu yake- na kwa hakika alipokea maelekezo kutoka kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-mpaka akawajia banii Quraidhwa,na alikuwa anawajuwa tangu kabla ya uislamu basi akawaambia: kwa hakika mnajuwa fika mapenzi yangu kwenu nyinyi,basi wakasema wewe kwetu hauna tuhuma,akasema kwa hakika mliandamana maquraishi na Ghatfaan kwa kumpiga vita Muhammad,na wao siyo kama nyinyi,mji ni mji wenu,kwenye mji huo kuna mali zenu watoto wenu na wake zenu,na wala hamuwezi kuuhama mkatoka humo,na kwa hakika maquraishi na Ghatfaan,wakiiona fursa na Ngawira wanaichukuwa,na wakiwa wataona visivyokuwa hivyowatarudi kwenye mji wao na watawacheni nyinyi na Muhammad,na wala hamna nguvu ya kupambana nao. Kisha akaendeleza mazungumzo yake pamoja nao,akasema mimi naona kuwa msipigane nao mpaka mchukuwe toka kwao Rehani kutoka kwa mabwana wakubwa

wao,mpaka muweze kumpiga vita Muhammad na wala wasiwawache peke yenu.

Kisha Nuaimu akawajia yeye mwenyewe Maquraishi,na akamwambia kiongozi wao ambaye ni Abuu Sufiani Bin Harbi na waliokuwa pamoja nae,kwa hakika mnatambuwa mapenzi yangu kwenu nyinyi na kutofautiana kwangu na Muhammad,na kwa hakika ilinifikia habari kuwa Banii Quraidhwa walijutia kitendo chao na Muhammad ,na kwa hakika walituma ujumbe kwa Muhammad na wakamwambia: Je unaturidhia tukuchukulie kutoka kwa Maquraishi na Ghatfaan watu kutoka kwa watukufu wao kisha tukupeni ili muwauwe,kisha tuwe pamoja nawe na waliobakia?akawajibu ndiyo.

Kisha akaendelea Nuaimu na maneno yake akijifanyisha kuwa ni mwenye kuwatahadharishaMaquraishi hali yakuwaambia: ikiwa Banii Quraidhwa watawatakeni muwape watu kwa ajili ya Rehani,basi msiwape mtu hata mmoja,kisha akatoka mpaka Ghatfaanna akasema mfano wa aliyoyasema kuwaambia Maquraishi na kuwatahadharisha na banii Quraidhwa.(611) Na lilikuwa kabila la Ghatfaan na Quraidhwa na maquraishi,wamejiandaa kesho yake waanze mapambano,na hiyo ilikuwa ni siku ya Juma mosi,basi Maquraishi wakatuma kwa Banii Quraidhwa ujumbe ili washirikiane kwenye vita katika hiyo siku,wakasema;hakika siku ya leo ni siku ya juma mosi,na sisi hatuwezi kushirikiana mapigano nanyi mpaka mtumpe Rehani,kwani sisi tunahofia kuwa mtarejea kwenye miji yenu na mtatuwacha na huyu mtu,wanamkusudia mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-Basi Maquraishi na Ghatfaan wakasema: Twamuapia Mwenyezi mungu kwa hakika amewaambia kweli Nuaimu Bin Masoud,tunawaapia hatuwezi kuwapa mtu hata mmoja naQuraidhwa wakasema kwa hakika amewaambia kweli Nuaimu bin masoud,na yakafeli makubaliano ya watu na wote wakadhaniana vibaya.(612)

Basi akawajia usiku na wala hawakufanya chochote na waislamu na katika wakati wa Usiku ALLAH aliwatumia watu wa vikundi upepo wenye baridi kali, ukawa upepo huo unapeperusha mahema yao na kupindua vyungu vyao, na ndyo upepo ambao Amezungumzia ALLAH:

﴿يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءَتْكُمْ جُنُودٌ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا وَجُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا﴾ [الأحزاب: 9]

Enye ambao mlio amini kumbukeni neema za ALLAH juu yenu pindi walipo kujieni majeshi kisha tukatuma juu yao upepo na wanajeshi nyie hamkuwaona na akawa ALLAH kwa wanayo yafanya ni mwenye kuoana. Al-Ahzaab :9. Basi kambi ya washirikina ikatikisika na kukasikika kelele za manung'uniko kutoka kwao(613)

Mtume akamtuma Hudhaifa Bin Al-yamaan -Radhi za Allah ziwe juu yake-ili aweze kufuatilia habari za watu, na kwa hakika alimuamrisha asiansishe chochotewala asifanye chochote isipokuwa upelelezi hata kama itamjia Fursa ,Basi akaenda Hudhaifa na akaingia kambi ya Maquraishi, na akakaa na kundi miongoni mwao waliwa wamejifunika majoho wakiwa pembeni mwa moto, na akapenya kati ya opasina pasina yeyote kumjuwa, na baridi ilikuwa kali na upepo ukiwavuruga , na alikuwa Abu Sufiani kwenye kundi la watu akikikisha kuwa hakuna mpelelezi wa Muhammad-Sala na amani ziwe juu yake-kati yao, akawaambia watu kabla ya kuanza mazungumzo, amtambue kila mtu mwenzake, na hakuwa Hudhaifa na kazi nyingine zaidi ya kufanya haraka kumuuliza mwenzake ambaye alikuwa upande wake wa kulia , ni nani wewe? kisha akawahi kugeuka kwa aliyekuwa kushotoni mwake na akamuuliza ni nani wewe? Na kwa namna hiyo alilikwepa swali na hakuna aliyemtambua katika wale watu, na kwa hakika alizungumza na akasema: Enyi kundi la maquraish kwa hakika nyinyi mmekuwa

kwenye nyumba ya utukufu, Ngo'mbe wameangamia na mbuzi na pia Ngamia na wametuwacha banii Quraidhwa na tumekutana na upepo mkali kama mnavyoona upepo hauwachi vyungu vikatulia wala kuwacha moto uwake, na wala majengo hayatulii, hivyo ondokeni namimi ni mwenye kuondoka, kisha akapanda Abuu sufiyani Ngamia wake akitaka kuondokabasi watu wakamsimamisha ili waondoke pamoja nae, basi wakajitoa Maquraishi na wakabakia baadhi ya wapiganaji ili kuzuia kutoondoka kwake Maquraishi, kisha yakafuatia baadhiya makabila ya vikundi.

Na akaja Hudhaifa-Radhi za Allah ziwe juu yake-ili ampe habari njema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-habari ya kuondoka hayo makundi, baada ya kuwa waliwaweka kizuizini kwa muda wa nyusiku Ishirini na tano.(614)

Na vikosi vilipoisha katika mji wa Madina mtume aliwaambia waswahaba wake "Sasa hivi tunawafuata kuwapiga vita na wala hawatatupiga vita, sisi tunawaendea(615)" na ukawa muelekeo ni kama alivyosema Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na baada ya hapo mtume aliwaruhusu wapiganaji vita kurudi nakushika Doria pembeni mwa mahandaki mpaka kwenye majumba yao na akasema kweli ALLAH:

﴿وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَظِيمِهِمْ لَمْ يَنَالُوا خَيْرًا وَكَفَى اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ وَكَانَ اللَّهُ قَوِيًّا

عَزِيزًا﴾ [الأحزاب: 25]

Na ALLAH akawarudisha wale walio kufuru kwachuki zao na wala hawakupata kheri na ALLAH akawazuia na kupigana vita na akawa ALLAH ni mwenye nguvu mshindi. AI-AHZAAB 25: Na kwa hakika Waislamu waliwapoteza mashahidi Sita,(616) kama walivyoliwa washirikina watu watatu.(617) Na kwa hakika iliteremka kuhusu hii vita, Suratil Ahzaab, ambayo iliitwa kwa jina

hilo na ikawa miongoni mwa aya zilizokuja katika hilo ni neno lake mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءَتْكُمْ جُنُودٌ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا وَجُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ﴿١٥﴾ إِذْ جَاءَكُمْ مِنْ فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنْكُمْ وَإِذْ رَأَيْتُمُ اللَّيْلَ مُغْشًى بِسُحُوبٍ مُدْبِرَةٍ تَلْمِذَةٍ لِيُظْهِرُوا أَفْعَالَهُمْ فِي مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾ إِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ مَّا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ إِلَّا غُرُورًا ﴿١٧﴾ وَإِذْ قَالَت طَّائِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوا وَيَسْتَأْذِنُ فَرِيقٌ مِّنْهُمُ النَّبِيَّ يَقُولُونَ إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ إِن يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا ﴿١٨﴾ وَلَوْ دُخِلَتْ عَلَيْهِمْ مِنْ أَقْطَارِهَا ثُمَّ سُئِلُوا الْفِتْنَةَ لَا تَوَّهَا وَمَا تَلَبَّوْا بِهَا إِلَّا يَسِيرًا ﴿١٩﴾ وَلَقَدْ كَانُوا عَاهَدُوا اللَّهَ مِنْ قَبْلُ لَا يُولُونَ الْأَذَىٰ وَلَئِن لَّمْ يَنْفَعَكُمُ الْفِرَارُ إِن فَرَرْتُمْ مِنَ الْمَوْتِ أَوِ الْقَتْلِ وَإِذًا لَا تُمْتَعُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢٠﴾ قُلْ مَنْ ذَا الَّذِي يَعْصِمُكُمْ مِنَ اللَّهِ إِن أَرَادَ بِكُمْ سُوءًا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٢١﴾ ۞ قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الْمُعَوِّضِينَ مِنْكُمْ وَالْقَائِلِينَ لِإِخْوَانِهِمْ هَلُمَّ إِلَيْنَا وَلَا يَأْتُونَ النَّبَأَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢٢﴾ أَشِحَّةً عَلَيْكُمْ فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَىٰ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ إِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوكُمْ بِالسِّنَةِ حِدَادٍ أَشِحَّةً عَلَى الْخَيْرِ أُولَٰئِكَ لَمْ يُؤْمِنُوا فَأَخْبَطَ اللَّهُ أَعْنَاهُمْ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٢٣﴾ يَحْسَبُونَ الْأَحْزَابَ لَمْ يَذْهَبُوا وَإِن يَأْتِ الْأَحْزَابُ يَوَدُّوا لَوْ أَنَّهُمْ بَادُونَ فِي الْأَعْرَابِ يَسْأَلُونَ عَنْ أَنبِيَائِهِمْ وَلَوْ كَانُوا فِيكُمْ مَّا قَتَلُوا إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢٤﴾ لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢٥﴾ وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٢٦﴾ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَّن قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُمْ مَّن يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَلُوا تَبَدُّلًا ﴿٢٧﴾ لِيَجْزِيَ اللَّهُ الصَّادِقِينَ بِصِدْقِهِمْ وَيُعَذِّبَ الْمُنَافِقِينَ إِن شَاءَ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٢٨﴾ وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَنَالُوا خَيْرًا وَكَفَى اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ وَكَانَ اللَّهُ قَوِيًّا عَزِيمًا ﴿٢٩﴾﴾ [الأحزاب: 9-25]

Enye ambao mlio amini kumbukeni neema za ALLAH juu yenu pindi walipo kujieni majeshi kisha tukatuma juu yao upepo na majeshi nyie hamkuyaona na akawa ALLAH kwa wanayo yafanya ni mwenye kuona. Pindi walipo kujieni kwa juu yenu na chini yenu na pindi yalipo kodoka macho na mioyo ikafikia kwenye mturinga na mkamdhania ALLAH kumdhania hasa. Hapo ndipo walipo jaribiwa waumini na wakatikiswa kutikiswa kuliko kukali. Pindi walipo sema wanafiq na wale ambao kwenye nyoyo zao kuna maradha ALLAH na mtume wake hawakutupa ahadi isipokua ni uwongo. Na lilipo sema kundi miongoni mwao enye watu wa madina hamna makazi rudini na linamtaka idhini mtume kundi miongoni mwao wanasema hakika majumba yetu yapo tupu hali ya kua hayapo tupu hawana wanacho kitaka isipokuwa kukimbia. Na laiti ukiingia kwenye miji yao kisha wakaulizwa fitna hakika wataijia na hawata isubiri isipokuwa muda kidogo. Na haki walikuwa wamemuahidi ALLAH kabla ya hapo hawata kimbia kurudi nyuma na ikiwa ahadi ya ALLAH ni yenye kuulizwa. Sema haita wasaidia kukimbia kama mtakimbia kifo au kuuwawa na wakati huo hamta pata starehe isipokuwa kidogo.» Sema ni nani ambaye atakaye kuingeni kutokana na ALLAH kama atawakusudia ubaya au akawakusudia huruma na wala hawata pata wao kinyume na ALLAH msaidizi wala wa kuwanusuru. Hakika amefahamua ALLAH wale wenye kutia uzito miongoni mwenu na wale wenye kusema kuwaambia jamaa zao njooni kwetu na wala hata leta ubaya isipokuwa kidogo. Ugumu upo juu yenu basi itakapo ondoka hofu utawaona wakikutazama wakizungurusha macho yao kama yule ambaye anaye hofiwa kifo basi ikisha ondoka hofu watakutoleeni ndimi kali hali ya kuwa ni ugumu juu y kheri hao hawakuamini kisha ALLAH akaporomosha matendo yao na likawa hilo kwa ALLAH ni jepesi. Wanadhania kuwa makundi bado hayajaenda na kama yatakuja makundi watatamani laiti wao wangukuwa wapo jangwani na mabedui wakiulizana kunako khabari zenu na laiti wangelikuwa pamoja nami wasingepigana ila

kidogo tu. Hakika mmekuwa na kiigizo kizuri kwa mtume kwa yule anaye mtarajia ALLAH na siku ya mwisho na akamtaja ALLAH sana((21)), Na pindi waumini walipo yaona makundi walisema hivi ndivyo alivyo tuahidi ALLAH na mtume wake na amesema ALLAH na mtume wake na haikuwazidishia isipokuwa imani na kujisalimisha. Kuna miongoni mwa waumini wanaume walio sadikisha yale walio muahidi ALLAH juu yake basi miongoni mwao wapo waliotekeleza ahadi yake na kuna miongoni mwao wapo wanasubiri na hawakubadilisha chochote. Ili ALLAH awalipe wakweli kwa ukweli wao na awaadhibu wanafiq akitaka au awasamehe hakika ALAH amekuwa ni msamehevu mpole. ALLAH akawaweka sawa wale walio kufuru kwa chuki zao hawakupata kheri na ALLAH akawatoshleza waumini vita na akawa ALLAH ni mwenye nguvu mshindi. Al-ahzaab:9-25(618)

Licha ya kuondoka makundi kwa hakika mzunguko wa kivita ulikuwa haujaisha bado,kabla ya kurudi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- nyumbani kwake na kutua silaha yake akawa amemjia Jibriil-Juu yake amani-akamwambia mtume: ((Kwa hakika umetwa Silaha yako! namuapia ALLAH sisi hatukutuwa silaha,watokee,akasema Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-tuendewapi?akasema hapahapa na akaashiria kwa kabila la Banii Quraidhwa Basi Akawatokea Mtume))(619) Basi mtume -Sala na amani ziwe juu yake-alijuwa kuwa kuwapiga vita hawa wafanya Khiyana watokanao na kabila la Banii Quraidhwa ni amri itokayo kwa Sala-Tukasika na machafu ni kwake- bisi akampa bendera yake Ally Bin Abii Twalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-, (620) na akaamrisha kuwa watangaziwe kuwa (Asiswali swala ya alaasiri yeyote isipokuwa kwa Banii Quraidhwa kisha akaondoka mtume yeye mwenyewe ili kukutana na maswahaba wake,na akakita kambi mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na pamoja nae maswahaba zake pambizoni mwa ngome za Banii Quraidhwa", (621) na wakaanza kuwawekea kizuizi ambacho kilidumu kwa masiku kumi-ALLAH

akaweka uwoga kwenye nyoyo za mayahudi,na ALLAH akawatikisa,na khofu ikazidi,mpaka wakawa wakiwatafuta baadhi ya washirika wao wa kabila la Ausi,lakini wao walikuwa ni wanajuwa zaidi usaliti wao na vitimbi vyao kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na adhabu ambayo inawafaa,mpaka ikawa wao wakati wa kuwekwa kuzuizini wanaipata adhabu kutoka kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**)(622)

Na kutiwa kizuizini kwa mayahudi wa banii Quraidhwa kulipozidi,na wakawa na yakini kuwa hawawezi kuepukana na kuangukia kwenye mikono ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** kuna waliokuwepo pamoja nae miongoni mwa waislamu,na Mwenyezi Mungu akatikisa mionyo yao,wakatangaza kujisalimisha kwenye Hukumu ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**na likaja kabila la Ausi kwa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**wakiwaombea msamaha(Basi akarudisha hukumu kwa Saad Bin Mua'adh na akasema:mimi nawahukumu kuwa wapiganaji wao wauliwe na wanawake wao watekwe,(623) Akasema-**Rehema na amani ziwe juu yake:**Nimehukumu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu,(624) na alikuwa Saad amewasiliana nao wakati walipowekwa kwenye kizuizi cha Handaki na yeye ni katika waliokuwa wakijuwa usaliti wa Mayahudipale mtume alipomtuma pamoja naeujumbe wa walijadiliana nao,basi akakubaliana Saadi na wote yakuwa wakubali hukumu yake basi wakakubali kisha akatangaza hukumu kali dhidi ya mayahudi wa banii Quraidhwa walivunja makubaliano na wakamfamnyia mtume na waislamu Khiyana nawakawa wameufanyia khiyana sehemu wanayoishi,na hukumu yenyewe ni kuwa wapiganaji waowauwawe na wanawake wao watekwe na watoto waona mali zao zigaiwe,na wakatekelezewa hukumu hii,na hali yakuwa wao wanajuwa kuwa wanastahiki adhabu hiyo,na kasalimika katika adhabu hii moja miongoni mwa kiongozi wa kabila la banii Quraidhwa ambaye alikuwa amewakosoa watu wake kwa kuvunja makubaliano na

Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-na akasema kwa hakika mimi siwezi kushirikiana nanyi kwenye usaliti,na wakashirikiana nae kwenye kujiweka mbali na Khiyana kundi lingine la watu kutoka katika kabila la Banii Quraidhwana kiongozi huyo alikuwa bado yupo kwenye uyahudi wake,isipokuwa kukataa kwake kuvunja makuliano kulimuokoa yeye na wenzake mfano wake kutokana na Adhabu.

Na ilikuwa vita vya Ahzaab na vita vya Banii quraidhwa ni Nusra kwa waislamu,Mwenyezi Mungu aliyashinda makundi,hawakuwaweza waislamu,na ALLAH akawadhihirishia Mayahudi ukweli wao ,na akautwahararisha mji wa Madina kutokana na kabila la Banii Quraidhwa na waislamu wakaziteka mali zao na mashamba yao.na kwa hakika iliteremka kwa kabila la Banii Quraidhwa Aya miongoni mwazo ni maneno yake ALLAH mtukufu:

﴿وَأَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ صَيَاصِيهِمْ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا ﴿٢٦﴾ وَأَوْرَثَكُمْ أَرْضَهُمْ وَوَدَارِهِمْ وَأَمْوَالَهُمْ وَأَرْضًا لَمْ تَطَّوْهَا وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٢٧﴾﴾ [الأحزاب: 26-27]

Na ALLAH akateremsha juu yale walio wasaidia miomgoni mwa mayahudi na manaswara kutokana na ngome zao na akaingiza ndani ya nafsi zao hofu hali ya kuwa kundi mnalipiga na kundi mnaliteka. Na ALLAH akawarithisha ardhi zao na miji yao na mali zao na ardhi hamkuikanyaga na amekuwa ALLAH kwa kila kitu ni muweza. Al-hzaab:26-27.

Vita vya Banii mustwaliq(Al-uraissiy): (Shaaban mwaka 6Hijiria)

Iliitwa vita hii kwa jina la kabila la Banii mustwaliq,nao wanatokana na tumbo la Khuz'zaa kutoka katika kabila la Qah-twaan,kama ambavyo vita hivyo viliitwa vita vya Al-muraisiyy,(626)imenasibishwa na sehemu na maji amabyo walikuwa wameyakusudia wapiganaji nayo ni sehemu ya baniiAl-mustwaliq

sehemu iliyopo kati ya Makka walmadinah,iko karibu na mji wa Usafaani na Qudaidi na pambizoni mwake.

Na hili kabila lilikuwa katika sehemu inayotenganisha kati ya Maquraishi na makkah,na lilikuwa likiwapa Maquraishi mahusiano yenye nguvu,na wala msimamo wao haukuwa wa wazi msimamo wao kuhusu uislamu hapo mwanzo,pamoja nakuwa walikuwa na ushirika na makabila mengine ya Ghuz'aa pamoja na Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-,isipokuwa banii Mus-twaliq waliwahalifu watu wao,pale ilipobainika kuwa wao walituma msaada kwa maquraishi kabla kidogo ya kuanza vita vya Uhud(627) na alipopata uhakika wa wamukusudio ya kuwa wanataka kuushambulia mji wa Madina aliandaa Jeshi ambalo lilikuwa idadi yake ni wapiganaji mia saba na wakamuacha katika mji wa amadina Abuu Dharri Al-Ghifariy-Radhi za Allah ziwe juu yake-na akatoka kwenda kwenye kabila la Banii Mus-twaliq kwenye Mwezi wa Shaaban katika mwezi wa sita tangu kuhama mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-(629)na ilikuwa idadi ya Jeshi la Muhaajiriina ambao wanabeba Bendera yao ni Abuubakar Al-swiddiq-Radhi zaAllah ziwe juu yake-na vilevile Answaar ambao anaibeba bendera yao Saad Bin Ubaadah-Radhi za Allah ziwe juuyake.

Na kwa hakika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-sehemu waliokusanyika ((Na akamuamrisha-Radhi za Allah ziwe juu yake-Basi akawaita watu kuwa waseme Lailaha illa llahu,mtaziokoa Nafsi zenu na mali zenu basi wakatupiana mikuki,kisha Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akawaamrisha waislamu wakawavamia mara moja)),(630) basi watu wakasongamana na wakauwana ,basi Mwenyezi Mungu akawashinda Banii Mus-twalika na wakauliwa waliouliwa miongoni mwao,na waislamu Mateka wengi,miongoni mwa hao mateka ni Juwairiyat Bintul Haarithi-Radhi zaAllah ziwe juu yake-

Na kwa hakika ulidhihirika ushujaa wa wengi katika maswahaba-Radhi za Allah ziwe juu yake-katika vita hivi,miongoni mwao ni Ally Bin Abii Twalib na Abdurahmaan Bin Aufi-Radhi zaAllah ziwe juu yao wao wawili- na wengine.(632)

Na kwa hakika mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kwa shambulio hili aliwatia adabu hiki kizazi kitokanacho na kabila la Khuz'aa,nao ndiyo ambao waliwasaidia Maquraishi na wakataka kuuvamia Mji wa Madina.

Na Sehemu ya Khuz'aa ilikuwa ipo kati ya makkah na madina,na kwa kuwa walikuwa ni sehemu yenye kupinga na kuwafanyia uadui maadui watokanao na kabila la Khuz'aa,katika wakati ambao vizazi vyote vya Khuz'aa ni washirika wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,basi yakawa makabila yote walikuwa wakiujuwa ushindi wa mtume -Sala na amani ziwe juu yake-kwenye kuwapiga Maadui wake,na ikawa hii vita ni yenye kuondoa shaka ya jambo hili.

Tukio la kusingiziwa -Uongo.

Lilikuwa tukio la Uongo ni katika matukio muhimu yaliyotokea katika vita vya Banii Mus-twaliqa.(633)tukio hili ambalo liligusa heshima ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-lilitwaharisha heshima ya mwanamke kipenzi zaidi kwake na kwa umma mzima,na huenda Hadithi kuhusu tukio inatoka kwa mwenye tukio naye ni Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake-Riwaya iliyokuwa sahihi zaidi ndani yake kuna uchambuzi wa kina.nayo ni Hadithi inayozingatiwa kuwa ni katika Hadithi Ndefu,ipo katika Sahihi Bukhariy na yenye upambanuzi mwingi wakina kwa kutumia Riwaya ya mtoto wa Dada yake Ur-wat Bin Al-Zubair-Radhi za Allah ziwe juu yake- Na kwa hakika nilifanya bidii ya kukinukuu chote: (Hadithi ya kusingizia na kusingizia ni sawa na Najisi husemwa If-kuhum wa if-kihim,na mwenye kusema Af-kahum anasema amewageuza kutoka Kwenye Imani na kukadhibisha kwao,kama alivyosema:Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa,hugeuzwa kuepokana nayo mwenye

kugeuzwa, imepokelewa kutoka Bin Shahaab amesema: Amenihadithia Ur-wat Bin Zubair na Said Bin Musayyab na Al-Qamat Bin waqqaas na Ubaidillahi Bin Abdullahi Bin Ut-bat Bin Mas'uud, kutoka kwa Aisha, -radhi za Allah ziwe juu yake- Mke wa mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- pindi watu wa uzushi walipomwambia ambacho walikisema, na wote hao walinihadithia kikundi kutoka kwenye mazungumzo yake, na baadhi yao walikuwa wakifahamu zaidi tukio lake kuliko wengine na wakalithibitisha tukio hilo kwa kuhadithia, na kwa hakika nilifahamu mazungumzo ya kila mmoja wao alivyonihadithia kutoka kwa Aisha, na baadhi ya simulizi ni zenye kusadikidisha zingine, japo kuwa baadhi yao ni wenye kufahamu tukio hilo zaidi kuliko wengine, wakasema, amesema Aisha: Alikuwa mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- akitaka kusafi hupiga kura kati ya wake zake, na yeyote mshale wa kura utakapomtokea, basi mtume hutoka pamoja nae, akasema Aisha basi mtume akapiga kura kumchaguwa baina yetu katika vita aliyopigana, basi mshale wangu ukatokezea, basi nikatoka na mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake- wakati huo ilikuwa Aya ya Hijabu imeshateremka, na nilikuwa nikibebwa kwenye kijumba changu, na hushuswa humo, na tukaenda mpaka mtume akamaliza vita yake hiyo kisha na akarudi, tulikaribia mji wa Madina tukirudi akatoa idhini ya kurudi wakati wa usiku, basi nikasimama wakati ule alipotoa idhini ya kuondoka basi nikatembea mpaka nikalipita jeshi, basi nilipomaliza jambo langu nilirudi mpaka kwenye kipando changu, basi nikagusa kifua changu ghafla nikabaini kuwa kidani changu cha shingoni kimekatika, basi nikarudi kukitafuta kidani changu, kule kukitafuta kukanizuia kwa muda. akasema wakaja wale waliokuwa wakinisafirisha na wakabeba kijumba changu, na wakakihamishia kwenye Ngamia wangu ambaye nilikuwa nampanda na wao wakidhania kuwa mimi nimo ndani ya kijumba, na wanawake wakati huo walikuwa wepesi nawembamba na siyo wazito na hawajajazia nyama, na hawakuwa wakila chakula isipokuwa ni chache tu chenye kuwatosheleza na wala

hawakushangazwa kutokana na wepesi wa kijumba walipokiinua na kukibeba,na nilikuwa Bint mwenye umri mdogo basi wakawaamrisha Ngamia na wakaondoka na nikakipata kidani changu baada ya kuwa jeshi limeshaondoka,basi nikaja walipokuwa wamefikia nahapakuwepo kati yao mwenye kuita wala mwenye kuitikia,basi nikakusudia kwenda ile sehemu ambayo nilikuwepo,nikadhania kuwa wao watanikosa hivyo watanirudia,basi wakati nimekaa sehemu yangu ghafla nikapitiwa na usingizi,na hivyo nikalala,na alikuwa Swaf-waan Bin Muattwal Al-sulamiy Al-Dhakwaaniy alikuwa nyuma ya Jeshi akaja mpaka nilipokuwa nimekaa,basi akaona weusi wa mtu aliyekaa na kanijuwa aliponiona,na alikuwa ameniona kabla yakushuka Aya ya Hijab,basi nikaamka ili kumjibu baada yakunijuwa,hivyo nikajifunika na Jilbaab yangu,Namuapia ALLAH,namuapia hatujaongea neno lolote wala sikusikia kutoka kwake neno lolote zaidi ya kurudi kwake na akainama mpaka kikapiga magoti kipando chake akamkanyaga mikono yaje nikasimama na kumpanda,basi akaondoka akiniongozea kipando mpaka tukalifikia jeshi wakati wa mchana wa jua kalinawao walikuwa wamefikia sehemu maalumu,akasema Aisha,basi akaangamia kwa ajili yangu aliye angamia,na alikuwa yule ambaye ni mshika Dau mkubwa wa uongo ni Abdullahi Bin Ubayyat Bin Saluul,akasema ur-wat nilipewa habari kuwa habari hiyo ilikuwa ikisambazwa na ikiongelewa kwake,na akiidhinisha na kusikiliza na kuyapamba.na akasema Ur-wat vilevile:na hawakutajwa yeyote katika wasingizaji isipokuwa Hassan Bin Thaabit ,na Mis-twah Bin Athaathat,na Hamna bint Jah-shiy na watu wengine nisiowajuwa,isipokuwa wao ni kikundi,kama alivyosema ALLAH mtukufu.na kwa hakika mkubwa wao anaitwa Abdullahi BinUbaiyyat bin Saluul.

Amesema Ur-wat ,alikuwa Aisha akichukia kutukanwa Hassan mbele yake,na anasema kuwa yeye ndiye ambaye amesema:

Kwa hakika Baba yangu na mzazi wake na Heshima yangu.

kwa Heshima ya muhammad kwenu ni kinga.

Alisema Aisha tulifika Madina nikawa na uchovu kwa muda wa mwezi mmoja nilipofika madina,na watu wanaendelea kusambaza kauli ya watu wenyekusingizia,na nilikuwa sifahamu chochote katika hilo naye mtume akawa ni mwenye kuniulizia kuhusu uchovu niliokuwa nao na mimi wakati sioni tena ile huruma na upole toka kwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake huruma ambayo nilikuwa nikiiona kwake wakati nilipokuwa na maumivu na uchovu,na kwa hakika alikuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-anaingia kwangu na kunisalimia kisha husema:vipi hali zenu? kisha anaondoka,basi akawa anaulizia hali yangu na wala sikuwa nanihisi kuwepo na ubaya wowote,mpaka nilipotoka baada ya kupata nafuu,basi nikatoka na Mama Mis-twaha kwenda upande ulipojengwa sehemu za kukidhia haja(634),na nisehemu iliyokuwa ya wazi,na tulikuwa hatutoki isipokuwa usiku kwa usiku,na wakati huo ilikuwa kabla ya kujengwa Vyoo karibu na majumba yetu,akasema kuwa suala la kukidhi kwetu haja lilikuwa ni kama suala la waarabu wengine walivyokuwa wakikidhi haja zao porini kabla ya kuwa na vyoo,na tulikuwa tukichukia kuweka sehemu za kukidhi haja kwenye majumba yetu,akasema:basi nikaondoka mimi na Mama Mis-twah naye ni mtoto wakike wa Abii Rahmi Bin Muttwalib Bin Abdi Manaaf,na mama yake ni Mtoto wa Swakhri Bin Aamir Shangazi yake Abuubakar,na mwanae anaitwa Mis-twah Bin Athathat Bin Abaad Bin Al-muttwalibBasi mimi na mama Mis-twaha tuakelekea upande wa nyumba yangu,pale tulipokuwa tumeshamaliza jambo letubasi akajikwa Mama Mis-twaha kwenye kwa Kanga yake,akasema:amepata hasara Mis-twah,basi nikamwambia nini hiki unachosema,hivi unamtukana mtu ambaye ameshiriki vita vya Badri,akasema:wewe hujui hivi hukisikia aliyoyasema Mis-twah?akasema:nikamwambia amesema ninibasi akanipa habari ya watu wa tukio la uongo-akasema-basi yakazidi maradhi juu ya maradhi,na niliporudi nyumbani kwangu akaingia

kwangu Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-akasalilimia na akasema:"Habari yako"basi nikamwambia je unaniruhusu kwenda kwa wazazi wangu akasema nikataka kupata uhakika wa habari kutoka kwao,akasemabasi akaniba ruhusa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-nikamwambia ewe mama yangu ni jambo gani watu wanalizungumza? Basi akasema ewe mwanangu mimi nakujali,Na ninamwapia Mwenyezi Mungu kuwa ni mara chache sana kwa Mwanamke mwenye kupendeza kwa mume wake ampendaye mume wake isipokuwa watazidisha kumsema.akasema: nikasema:-Kutakasika na machafu ni Mwenyezi Mungu- hivi ni kweli watu wameyaongelea mambo haya? akasema basi nikalia usiku ule mpaka nikawa sitokwi tena na machozi na yamekauka, na wala siupati usingizi,kisha nikaamka nikiwa ninalia,akasema :kisha Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-akamuita Ally Bin Abii Twaalib na Usamat Bin Zaid,pale Wahyi ulipochelewa kuteremka, akawa anawauliza na anawataka ushauri wa kuwachana na mke wake,akasema Aisha:Ama Usama alimshauri mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-jambo ambalo analijuwa kuwa mkewe yuko mbali na anayosingiziwa,na jambo ambalo anawajuwa kwalo jambo hilo yeye mwenyewe,basi Usama akasema:Mke wako hatuna tunachokijuwa kuhusu yeye isipokuwa mema.Ama Ally Akasema:Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu hajakubania ,na wanawake ni wengi siyo huyo tu,na muulize kijakazi atakwambia ukweli,akasema Aisha:Basi Mtume waMwenyezi Mungu akamuita Barira na Akasema:Je umeona jambo lolote lenye kutia mashaka?"AkasemaBarira akamwambia:Namuapia yule ambaye amekutuma wewe kwa haki sijaona kwake jambo lolote hata nilifiche,isipokuwa ninachojuwa katika madhaifu yake ni kuwa yeye ni Msichana mdogo wa umri analala mbali na chakula alichokianda kwa ajili ya watu wake bila kukifunika na wanakuja kuku na wanakula Akasema:basi akasimama Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-siku hiyo akamuomba msamaha Abdullahi Bin Ubaiyyat akiwa juu ya

Membari Akasema: "Enyi kongamano la waislamuni nani atakae niomba mimi msamaha kwa ajili ya mtu ambaye habari zake za kumuudhi mke wanguzimenifikia", Namuapia Mwenyezi Mungu sina mambo niyajuwayo kwa Mke wangu isipokuwa ni ya Kheri, na mtu huyo hakuwa anaingia kwa mke wangu isipokuwa twaingia pamoja" akasema Aisha; Akasimama Saad Bin Muaadh Ndugu atokanae na kabila la Abdul Ash-hal na akasema mimi ewe mtume wa Mwenyezi Mungu ninakuomba msamaha, basi akiwa huyo mtu ni katika kabila la Ausi basi nitamuuwa, na kama atakuwa anatokana na kabila la ndugu zetu wa Khazraj basi tuamrishe tutekeleze amri yako. akasema Aisha basi akasimama mtu wa kabila la Khazraj, na alikuwa Mama Hassan Bin Thaabit ni baba yake mdogo atokanae na ukoo wake, nae alikuwa mtu huyo ni Saad bin Ubaadah, nae ni muheshimiwa wa kabila la Khazraj Akasema: na alikuwa kabla ya hapo ni mtu mwema lakini aligubikwa na ubaguzi, basi akamwambia Saad Bin Ubaadah: umesema uongo namuapia Mwenyezi Mungu mtu huyo tutamuuwa, kwa hakika wewe ni mnafiki unawajadili wanafiki akasemabasi wakachemka makabila mawili ya Ausi na Khazraji mpaka wakadhamiria kuuwana, na **Rehema na amani ziwe juu yake**- akiwa amesimama juu ya Membari Akasema Aisha: mtume akaendelea kuwatuliza mpaka wakanyamaza naye pia akanyamaza, akasema Aisha: nikalia hiyo siku nzima, machozi hayanikauki, wala usingizi siupati, Akasema Aisha: wakawa wazazi wangu wapo kwangu, na kwa hakika nililia nyusiku mbili na mchana mmoja machozi hayanikauki wala kupata usingizi mpaka nikadhania kuwa kilio kitapasuwa Ini langu na wakati wazazi wangu wamekaa kwangu nikiwa naendelea kulia, mara ghafla akabisha Hodi mwanamke wa Kianswaar ni kamuitikia, basi akakaa na akaanza kulia pamoja nami Akasema Aisha: basi wakati sisi tupo kwenye hali hiyo mara akaingia kwetu Mtume wa Mwenyezi Mungu- **Rehema na amani ziwe juu yake**- kisha akasalimia na akakaa kisha akasema Aisha na hajawahi kuka kwangu tangu paliposemawa yaliyosemwa, na palitulia kwa muda wa Mwezi mzima hapateremki wahyi kwake

unaohusu jambo langu Akasema Aisha: Basi akatamka Mtume Shahada alipokaa kisha akasema Ama Baada ya tamko hilo, Ewe Aisha kwa hakika zimenifikia habari hizi na zile kuhusu wewe, na kama utakuwa hauusiki nazo basi Mwenyezi mungu atakutakasa na ikiwa umekutikana na makosa, Basi mtake msamaha mwenyezi mungu na utubie kwake, kwa hakika mja akikosea na kakiri kisha akatubia basi Mwenyezi Mungu humsamehe "Akasema Aisha basi alipomaliza mtume kusema maneno hayo yalikauka machozi mpaka nikawa si hisi kuwepo hata tole la machozi, basi nikamwambia baba yangu nijibie Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hayo anayoyasema basi Baba yangu akasema :naapa kwa jina la Mwenyezi mungu sina jibu la kumjibu Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**-, basi nikamwambia mama yangu, nisaidie kumjibu mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hayo anayoyasema .akasema mama yangu, namuapia Mwenyezi Mungu sijui cha kumjibu mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**-basi nikasema na mimi ni msichana mwenye umri mdogo, na Qur'an sijui sana :hakika mimi naapakwa mwenyezi Mungu kwa hakika mimi ninajuwa kuwa mumesikia mazungumzohaya mpaka yakakita kwenye nafsi zenu na mkayasadikisha, na hata nikiwaambia kuwa mimi sihusiki hamtoniamini, na ikiwa nitakubali kosa basi mwenyezi mungu anajuwa mimi sihusiki ikiwa nitakubali basi mtanisadikisha, namuapia Mwenyezi mungu sina mfano wa kuwapa isipokuwa wa baba yake Yusufu aliposema "Kusubiri ni jambo zuri na mwenyezi Mungu ndiy mwenye kutakwa msaada kwa hayao muyasemayo kisha nikageuka na nikaegemea kitanda changu, na wakati huo mwenyezi mungu anajuwa kuwa mimi siyo mkosaji na kwa hakika mwenyezi mungu atanitakasa kwa utakaso wake, lakini namuapia Mwenyezi Mungu sikujuwa kama Mwenyezi Mungu angeteremsha Aya kwa ajili yangu na ikawa inasomwa, na lilivyokuwa jambo langu katika moyo wangu lilikuwa ni jambo dhalili sana kuongelewa kwangu na Mwenyezi mungu lakini nilikuwa natarajia kuwa mwenyezi Mungu atamuotesha mtume ndoto

itakayonitakasa nayo mwenyezi mungu hakuondoka mtume sehemu aliyokuwa amekaa wala hakuna yeyotekatika watu wa nyumbani alitoka mpaka akawa Mwenyezi Mungu ameteremsha kwake,basi ikampata tabu ambayo ilikuwa ikimpata mpaka linamtoka jasho mfano wa lenye kung'aa kama lulu na wakati huo yupo kwenye msimu wa masika,kutokana na uzito wa kauli ambayo ameteremshiwa kwake,Akasema basi mtume akafurahishwa na akawa anacheka ,na likawa neno lakwanza alilosema lilikuwa ni "Ewe Aisha na muapia Mwenyezi Mungu hakika amekutakasa Mwenyezi Mungu akasema:Akaniambia mimi mama yangu simama umwendee nikasema siwezi kusimama kwa ya kumuendea namimi sina wa kumshukuru isipokuwa Mwenyezi Mungu-mwenye nguvu na utukufu-Akasema Aisha :na akateremsha Mwenyezi Mungu mtukufu

﴿إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ﴾ [النور: 11]

((Kwa hakika wale walioleta habari za uzushi)) (Surat Nuur kuanzia Aya ya 11 jumla ni Aya kumi) kisha Mwenyezi Mungu akateremsha aya hizi kwa ajili ya kunitakasa .akasema Abuubakar swiddiq na alikuwa amlea Mis-twah Bin Athath kutoka na ukaribu waliokuwa naona kutoka na ufakiri aliokuwa nao namuaia Mwenyezi Mungu sitotoa matumizi kwa ajili ya Mis-twah hata mara moja baada ya kumsema Aisha hayo aliyoyasema.basi Mwenyezi Mungu akateremsha

﴿وَلَا يَأْتِلُ أُولَؤُا الْفَضْلِ مِنْكُمْ﴾ [النور: 22]

(Na wale miongoni mwenu wenye wasaa wasiape kutowapa jamaa zao wakaribu) surat Nuur kuanzia Aya ya 22 mpaka kwenye kauli yake

﴿وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾ [النور: 22]

(Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa Maghafira na mwenye huruma) akasema Abuubakar swiddiq-Radhi zaAllah ziwe juu yake Ni kweli hakika mimi napenda anisamehe Mwenyezi Mungu.

Basi akarudisha matumizi ya Mis-twaha ambayo alikuwa akimtolea ,na akasema namuapia ALLAH sitawacha kumtolea hata mara moja, Amesema Aisha:na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alimuuliza Zainab Bint Jahshiy kuhusu jambo langu,akamwambia Zainab ulifanya nini au uliona nini? ewe Mtume wa ALLAH ninayalinda masikio yangu na uoni wangu,namuapia ALLAH sina ninachokijuwa isipokuwa Kheri,akasema Aisha:naye Zainab alikuwa akinikweza miongoni mwa wake za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- basi Mwenyezi Mungu akamuhifadhi kwa uchamungu Amesema na Dada yake ambaye anaitwa Hamna akaanza kumpiga vita,basi akaangamia alaiyeangamia ,amaesema Bin Shihab: habari hii ndiyo iliyonifikia kutoka katika hadithi ya hiki kijikundi,kisha akasema Ur-wat Amesema Aisha : Namuapia Mwenyezi Mungu hakika mtu ambaye anasemwa dhidi yake kilichosemwa anasema Kutakasika kwa machafu ni kwa Mwenyezi Mungu,namuapia yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake sijawahi kumtowa Mwanamke nguo hata mara moja ,akasemakisha akauliwa katika baada ya hapo katika njia ya Mwenyezi Mungu)(635)

Na huenda mapokezi haya hutoka kwa muhusika wa jambo lenyewe ndiye mfikishaji mzuri zaidi wa hili tukio.

Na kwa hakika iliteremka katika hili tukio Aya nyingi ambazo zinasomwa mpaka siku ya kiyama ndani yake kuna mafunzo makubwa kwa Umma katika maneno yake ALLAH Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنْكُمْ لَا نَحْسَبُهُمْ شُرَكَاءَ لَكُمْ بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ لِكُلِّ أَمْرٍِ مِّنْهُمْ مَا أَكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٠﴾ لَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بِأَنفُسِهِمْ خَيْرًا وَقَالُوا هَذَا إِفْكٌ مُّبِينٌ ﴿١١﴾ لَوْلَا جَاءُوا عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ

فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا بِالشَّهَادَةِ فَأَوَّلِيكَ عِنْدَ اللَّهِ هُمُ الْكَذِبُونَ ﴿٣٧﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِي مَا أَفَضْتُمْ فِيهِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٣٨﴾ إِذْ تَلَقَّوْنَهُ بِأَلْسِنَتِكُمْ وَتَقُولُونَ بِأَفْوَاهِكُمْ مَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّبًا وَهُوَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمٌ ﴿٣٩﴾ وَلَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُمْ مَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَتَكَلَّمَ بِهَذَا سُبْحَانَكَ هَذَا بُهْتَانٌ عَظِيمٌ ﴿٤٠﴾ يَعِظُكُمُ اللَّهُ أَنْ تَعُودُوا لِمِثْلِهِ أَبَدًا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٤١﴾ وَبَيَّنَّ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٤٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ ءَامَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٣﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ رَؤُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٤٤﴾ بِأَيِّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّبِعُوا خُطُوتِ الشَّيْطَانِ وَمَنْ يَتَّبِعْ خُطُوتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٤٥﴾ وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَى وَالْمَسْكِينِ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلِيَعْفُوا وَلِيَصْفَحُوا أَلَا نُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٤٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ لَعُنُوا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٤٧﴾ [النور:

[23-11

Hakika wale ambao walio kuja na urongo ni kkundi miongoni mwenu msiwahesabu ni shari kwenu isipokuwa ni kheri kwenu kila mtu miongoni mwao ana alichu kichuma katika madhambi na wale walio walio simamia jambo hilo miongoni mwao ana madhambi makubwa. Bora mliposikia jambo hilo wangedhania waumini wa kiume na wa kike kwenye nafsi zao kheri na wakasema huu ni uwongo ulio wazi. Bora wangeleta mashahidi wanne basi wasipo leta mashahidi basi hao ndio waongo. Na kama si fadhila za ALLAH juu yenu na rehema zake duniani na akhera ingekupateni kwa yale mliyo yaendea adhabu kali. (14) Pindi mlipo yasema kwa ndimi zenu na mnasema kwa midomo yenu mambo msiyo kuwa na ujuzi nayo na mnayadhandia ni mambo mepesi na mbele ya ALLAH ni makubwa. Bora mlipo sikia mngesema haipendezi kwetu sisi kuzungumza haya utakasifu ni wako ewe

ALLAH huu ni uwongo ulio mkubwa. ALLAH anakukanyeni msije rudia mfano wa hilo kabisa kabisa ikiwa kweli ni waumini. Na anakubainishieni alama[zake ALLAH]na ALLAH ni mjuzi mwenye hekma. Hakika wale ambao wanapenda kueneza uchafu kwa wale ambao walio amini wana wao adhabu chungu duniani na akhera na ALLAH anajua na nyinyi hamjui. Na kama si fadhila za ALLAH na rehema zake na hakika ALLAH ni mrehemevu mpole. Enyi mlio amini msifuate hatua za shetani na atakaye fuata hatua za shetani basi yeye shetani atamuamrisha uchafu na mambo yenye kuchukiza na kama si fadhila za ALLAH juu yenu na huruma yake asinge takasika yeyote miongoni mwenu kabisa kabisa na lakini ALLAH anamtakasa amtakaye na ALLAH ni msikivu mjuzi. Na wasiache kusaidia wale wenye uwezo wa kusaidia kuwapa ndugu wa karibu na masikini na walio hama katika njia ya ALLAH pasi wasamehe na wapuuizie hivi hampendi ALLAH akusameheni na ALLAHni mfuta madhambi mpole. Hakika wale ambao wanawatupia zina wanawake walio jihifadhi walio ghafilika na uzinifu wamelaaniwa duniani na akhera na wanayo wao adhabu kubwa. Al-Nuur 11-23. Na kwa hakika Umma mzima ni wenye kuguswa kwa tabia zake,basi ikiwa atatuhumiwa Mtume wa ALLAH-Rehema na amani ziwe juu yake-na pia wakatuhumiwa watu wake katika tabia zao na heshima zao,basi kwa hakika itakuwa nyumba zote za ulimwenguni hazipo salama,na kwa ajili hiyo Qur'an ikaweka wazi kuwa haya matendo yalikuwa ni katika malengo yao amesema ALLAH kuhusu wao:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ ءَامَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ﴾ [النور: 19]

Hakika wale ambao wanapenda uene uchafu kwa wale walio amini wana wao adhabu chungu duniani na akhera na ALLAH anajua na nyie hamjui. An-nuur:19. Na akawatahadharisha wale ambao wanawakokota watu kuwapeleka kwenye kufuata

mwenendo wa Shetani na kwa hakika ALLAH amewakataza kufanya hivyo.

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ وَمَنْ يَتَّبِعْ خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴾ [النور: 21]

Enyi mlio amini msifuata Nyayo za shetani na atakaye fuata Nyayo za sheta basi yeye shetani atamuamrisha uchafu na mambo yenye kuchukiza na kama si fadhila za ALLAH juu yenu na huruma yenu asinge takasika miongoni mwenu kabisa kabisa lakini ALLAH anamtakasa amtakaye na ALLAH ni msikivu mjuzi. . Al- nuur:21. Na hapana shaka kuwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-na Bwana wa watu wema na wamama wa waislamu ni wema wa wanawake wote walio wema:

﴿ الْحَبِيبَاتُ لِلْحَبِيبِينَ وَالْحَبِيبُونَ لِلْحَبِيبَاتِ وَالطَّيِّبَاتُ لِلطَّيِّبِينَ وَالطَّيِّبُونَ لِلطَّيِّبَاتِ أُولَٰئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴾ [النور: 26]

Wachafu wa kike kwa wachafu wa kiume na wachafu wa kiume kwa wachafu wa kike na wasafi wa kike ni kwa wasafi wa kiume na wasafi wa kiume ni kwa wasafi wa kike hao ndio walio wekwa mbali kwa yale wanayo yasema wana wao msamaha na rizq nzuri. Al- nuur :26. Na ye Mtume ni mwema wa wema wote Sala za ALLAH na amani yake ziwe juu yake,na ALLAH amemchagulia wanawake Wema na miongoni mwao niyule ambaye alisifiwa na Hassan Bin Thaabit-Radhi za Allah ziwe juu yake-kwa maneno yake aliposema:

Aliye jihifadhi msafi mwenye akili Timamu asiyetuhumiwa na watu

Na siyo msengenyaji mwenye njaa ya kula nyama ya wasiyoyajuwa maovu(636)

Ni mke mwema mkarimu atokanae na na kizazi cha Luaiy Bin Ghaalib,

Mwenye juhudi na heshima, utukufu wao siyo wenye kuondoka

Aliyefunzwa heshima na kwa hakika Mwenyezi mungu ameifanya asili yake kuwa ni njema

Ame mtwahaisha na kila baya na mambo yasiyo faa

Na miongoni mwa maneno yake:

Kwa hakika Baba yangu na mzazi wake na Heshima yangu.

Heshima ya muhammad kwenu ni kinga. (637)

Na kwa masikitiko makubwa wanaleta baadhi ya Maadui kwa lengo la kusema maneno machafu kuhusu Mwema Aisha-radhi za Allah ziwe juu yake-Mke wa mwema wa walio wema Baba wa mwema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-, na mtu mwenye wema na mwenye kulingania mema.

Na ametakasika Mwenyezi Mungu unakuja utiliaji mkazo katika sura hiyohiyo juu ya kuinamisha macho kwa wanaume na wanawake ilikuchukua somo katika usafi kwa umma uliokuwa msafi nao ni umma wa mtume Muhammad-Rehema na amani ziwe juu yake-kwa kumfuata yeye na wake zake na wamama wa uislamu.

﴿ قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَعْضُوا مِنْ أَبْصَرِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴾ وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَعْضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ
ءَابَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنَاتِ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ
نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوْ التَّبَاعِينَ غَيْرِ أُولِي الْأَرْبَابَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوْ الْوَالِدِ الَّذِي لَمْ

يُظْهِرُوا عَلَىٰ عَوْرَتِ النِّسَاءِ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِن زِينَتِهِنَّ وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ
جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣٠﴾ [النور: 30-31]

Waambie waumini wa kiume wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao hivyo ndio usafi kwao hakika ALLAH mwenye kueleza kwa yale wanayo yafanya. Na waambiye waumini wakike wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao na wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa yale yalio onekana kutokana na hayo mapambo,na wajishushie shungi zao juu ya shingo zao,na wala wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa kwa waume zao au baba zao au baba wa waume zao au watoto wao au watoto wa waume zao au kaka zao au watoto wa kaka zao au wanawake wao au watumwa wao au wanao wafuatia wanamume wasio na matamano au watoto wadogo ambao wasio fahamu tupu za wanawake na wala wasipige miguu yao ikajulikana yale waliyo yaficha katika mapambo yao na ombeni msamaha kwa ALLAH nyote kwa pamoja enye waumini ili mfaulu. An-nuur:30-31 Na ni wazi kuwa Abuubakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake- alikuwa ndiyo mlengwa pamoja na Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-katika tukio la kusingizia ambalo lilimpitia Mama wa waumini Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake- kama ambavyo aliathirika kutokana na maneno ya watu waliongelea jambo hilo katika wakati ambao mtume-Radhi za Allah ziwe juu yake-akiwafanyia wema na na akiwapa sadaka na kuwapa matumizi yatokanayo na mali yake maalumu,kwa hivyo alisikitishwa kwa kitendo chao hicho nakupinga kwa mazuri mbasi akataka kusimamisha matumizi kwa Mis-twah Bin Athath naye ni mtoto wa mama yake mdogo Abuu Bakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake-,na lilipoteremka neno lake ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولِي الْقُرْبَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ عَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [النور:

[22

Na wala wasiache kusaidia wale wenye uwezo zaid miongoni mwenu kuwapa ndugu wa karibu na masikini na walio hamia katika mjia ya ALLAH na wasamehe na wapuuizie hivi hampendi ALLAH akusameheni na ALLAH na mfuta madhambi mpole. An-nuur:22,Amesema Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake:-Kweli namuapia ALLAH sisi tunapenda atusamehe Mwenyezi Mungu na akarudisha matumizi aliyokuwa anayatowa kwa mis-twah na akasema Namuapia ALLAH sitomundolea matumizi hata mara moja.(638)

Na lilikuwa miongoni mwa matukio yaliyokuwa mashuhuri zaidi katikaVita vya Banii Mustwaliq,na lilotokea kati ya Wanafiki haswahaswa Abdullahi Bin Ubaiyyat Bin Saluul,na wenye kufanana naye katika zama za mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-na hapana shaka kuwa wanao wafuasi katika kila zama,na zinawahusu Aya za Qur'an zilizoteremka kwa hao wanafiki.

Kwa hakika walipigania maji watu wawili ,mmoja wao ni anatokana na kabila la Ghifaar na muajiriwa wa Umar-Radhi za Allah ziwe juu yake- na mtu mwingine alikuwa ni mshirika wa moja wa kabila la Answaar,basi muajiriwa wa Umar akapiga ukelele kwa kusema Enyi kundi la Muhaajiriina: na akapiga ukelele mshirika wa Answaar:Enyi kundi la Answaar na ikakaribia kutoke Shari kati ya waislamu.na alaiposikia Mtume-jambo hilo-Rehema na amani ziwe juu yake akasema: ((Hivi mwaitana kwa mambo ya zama za kijinga na mimi nipo kati yenu,wacheni tabia hiyo kwa hakika tabia hiyo inanuka)).(639)

Na alikuwa Abdullahi Bin Ubaiyyat yupo kati ya watu wa Madina na pamoja nao alikuwa yupo Zaid Bin Ar-qam-Radhi zaAllah ziwe juu

yake Swahaba aliyekuwa na umri mdogo, akisikiliza yanayoendelea basi akasema Bin Ubaiyyat hali ya kuamsha hasira za watu: nawakaziamsha hasira zao, kwa hakika waliamia kwetu na wakajazana kwetu katika mji wetu, namuapia Mwenyezimungu haukuwa mfano wetu na mfano wa watu wa makka isipokuwa kama walivyosema waliotangulia (Mnenepeshe Mbwa wako ili akufanye wewe kuwa chakula) na ninamuapia ALLAH ikiwa tutarudi katika mji wa Madina wenye utukufu watawatowa walio wanyonge, kisha akawageukia na kuwalaumu waliokuwa pembeni yake miongoni mwa Maanswaar kwa kusema Namuapia ALLAH lau mngewazuilia vilivyomo mikononimwenu wangekwenda majumba mengine.

Kisha akaenda Zaidu Bin Arqam -Radhi za Allah ziwe juu yake- naye akiwa mtoto mdogo, na akamsimilia mtume- Rehema na amani ziwe juu yake- alichokisema Abdullahi Bin Ubaiyyat Bin Saluli na alai kuwa Umar Bin Khattwab yupo akasema Mtume: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu- Rehema na amani ziwe juu yake- niruhusu nimuuwe, akasema mtume- Rehema na amani ziwe juu yake- ((Waonaje ewe Umar ikiwa utafanya hivyo kisha watu waseme Muhammad anawauwa watu wake?)). (640)

Na akaja Abdullahi Bin Saluli kwa mtume akiapa kuwa yeye hakusema hayo aliyoyanukuu Zaid Bin Arqam, mpaka ambao hakuwepo wakawa na mashaka kuwa huenda Abdullahi Bin Ubaiyyat alikuwa mkweli, na wakamlaumu Zaidu Bin Arqam mtoto mdogo, na Mtume akamuamrisha aondoke katika muda ambao hakupaswa kuondoka katika muda huo, basi akaja Usaid Bin Hadwair-Radhi za Allah ziwe juu yake- akitaka kujuwa kutoka kwa Mtume wa ALLAH- Sala na amani ziwe juu yake- sababu ya kuondoka kwake katika muda huu ambao hakupaswa kuondoka katika muda huo akasema mtume- Sala na amani ziwe juu yake- ((Hivi jee haikukufikia habari aliyoisema jamaa yako? akasema jamaa yupi? akasema Abdullahi Bin Ubaiyyat akasema kwa nini kasema? akasema- Sala na amani ziwe juu yake- amedai kuwa ikiwa watarudi

Madina wenye utukufu watawatoa waliodhalili)) Akasema -Radhi za Allah ziwe juu yake- kwa hakika wewe ndiye mwenye utukufu na wao ndio madhalili sisi tutawatoa kwenye mji wa Madina ikiwa utataka,na akaenda mtume wa ALLAH- Sala na amani ziwe juu yake-siku yake hiyo na kaunganisha usiku wake na katikati ya siku iliyofuata mpaka watu wakachoka na walipotuwa mizigo yao walilala kutokana na kuchoka ,na hapakuwa na nafasi ya kujadiliana na maongezi kuhusu yaliyojiri kwani watu walishughulishwa mpaka wakachoka na kutaabika.(641)

na katika kipindi hiki Iliteremka hii Sura ya Wanafiki kwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-na ndani ya sura hiyo palikuwapo na usadikishaji wa maneno aliyoyasema Zaidu Bin Arqam,(642)naye ni kijana mwenye umri mdogo basi akamshika masikio hali kumbembeleza na akasema((Huyu ndiye ambaye Mwenyezi mungu ameyatekelezea masikio yake))(642) ni zikawa miongoni mwa Aya zilizoteremka kwa Abdullahi Bin Ubaiyyat Bin Saluli kwa maneno yake na wanafiki wenzake ikateremka kauli yake mtukufu:

﴿سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ﴾ هُمْ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنْفِقُوا عَلَيَّ مَنْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ حَتَّىٰ يَنْفَضُوا وَيَلَّهِ خِزَائِينَ
[المنافقون: 6-7]

Ni sawa juu yao umewatakia msamaha au ukaacha kuwatakia msamaha ALLAH hata wasamehe hakika ALLAH hawaongozi watu wachafu. Wao ndio ambao wanasema msitoe kuwapa wale walio pamoja na mtume mpaka waondoke na ni vya ALLAH hazina za mbinguni na aridhini na isipokuwa wanafiq hawafahamu. Al-munafikuuna: 6-7)

Na alikuwa Abdullahi Bin Ubaiyyat Bin Saluli ana mtoto mwema anayetwa Abdullahi ,na nimiongoni mwa maswahaba wa Mtume - Sala na amani ziwe juu yake-na alipojuwa yaliyotokea kwa baba

yake akaja kwa mtume- Sala na amani ziwe juu yake-akisema: kwa hakika zimenifikia habari kuwa wewe unataka kumuua baba yangu ,basi ikiwa ni kweli unataka kufanya hivyo basi nitume mimi namimi nitakuletea kichwa chakenamuapia ALLAH kuwa mimi nawajuwa zaidi watu kabila la Khazraj na hapakuwa na mtu mwema zaidi kwa mzazi wake kuliko mimi ,na mimi nachelea ikiwa utamuamrisha mtu mwingine asiyekuwa mimi akamuua baba yangu kisha nafsi yangu ikanishinda kumuangalia mtu ambaye alimuua baba yangu anatembea kwa watu hivyo nikamuua nami nikauwawa nikiwa muislamu anauliwa kwa ajili ya kafiri na nikaingia motoni akasema mtume- Sala na amani ziwe juu yake- ((siyo hivyo bali tupo naye na tunasuishi na kwa wema muda wakuwa bado tupo naye))(644)

Na hadithi hii inatubainishia hatari ya wanafiki na utumiaji wao wa sababu,ili kuleta fitna na na mashaka baina ya waislamunakuvunja haki zao na kuudhoofisha umoja wao,nakutumia mwanja wa ukabila katika hilo,kama vile ambavyo Ibnu Saluli alivyomtishia Mtume na maswahaba zake kwa kuwatoa katika mji wa madina lilikuwa ni jambo ambalo lipo wazi na wakawa wakingojea fursa ili kuwadhuru waislamuna kumdhuru mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake,kama ambavyo ilivyokuwa kurudi kwake nyuma kwa yale aliyoyasema na kuyapinga kunaweka wazi udhaifu wa wanaafiki,na kwa hakika ALLAH alimfedhehesha katika Qur'an ambayo inasomwa kila siku mpaka kiyama.

Na kwa msimamo wa mwanae Abdullahi kuna ukweli na kutekeleza ahadi na maandalizi ya kujitolea kwa kila kitu kwa ajili ya Mtume- Sala na amani ziwe juu yake- japokuwa ni mzazi wake,naye nikatika watenda wema zaidi kwa baba yake,na katika majibu ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kuituliza akili ya mtoto wa kiislamu,kuna Hekima na upole na muamala mzuri katika maamuzi kama haya yaliyo magumu ,kama ambavyo Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Sala na amani ziwe juu yake-aliliamrisha jeshi

kuondoka na akawa akiwafuatilia mfululizo katika kwenda kwao jambo ambalo lilipelekea wao kuchoka ili kuwazuia wasijadiliane na kugawanyika ,ni utukufu ulioje wa muongozaji ambaye ni Mutme-Sala na amani ziwe juu yake-na mwenye hekima zaidi katika maamuzi ambayo yanahitajia msimamo na hekima

Na miongoni mwa matokeo ya vita vya Banii mustwaliq ni Mtume kumuoa Juwairiyat Bintul Haarith,na kwa hakika alikuwa ni Mtoto wa Haarithi Bin Abii Dhwiraar muheshimiwa kwa watu wake ,na kwa hakika alikuwa ameuliwa mzazi wake na Mume wake katika Safu ya jeshi la Banii Mustwaliqa wakati walipokuwa wanapambana na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kama walivyotekwa wanawake na waoto wa Banii mus-twaliqa ,kwa hakika aliangukia kwenye umiliki wa Thabit Bin Qais Bin Shamman Al-answariy -Radhi za Allah ziwe juu yake-basi Juwairiyat wakaandikishiana kuikomboa nafsi yake,na alikuwa anajuwa Upole wa Mtume na ihsani zake kwa watu ,basi akaja kwa mtume na akasema: ((Ewe Mtume wa ALLAH Mimi Ni Juwairiyat Bintul Haarith Bin Abii Dwiraar Bwana wa watu wake,na kwa hakika nimepatwa na balaa ambayo kwako haifichikani,nimetumbukia kwenye umiliki wa Thanit Bin Qais Bin Shimaas,nikajiandikishia mkataba mimi mwenyewe ,hivyonimekuja ninakuomba msaada katika huu mkataba wangu,basi mtume akamkombowa kutokana na hali yake na akamuwekea wazi kuwa atamlipia na atamuoa ili amuinuwe na ampe badala ya alivyovipoteza ikiwa miongoni mwa utukufu na ubora))(645) Basi Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-akafanya hivyo na akamuoa ,na akawa kiuhalisia ni mtukufu kwa watu wake na kuwaondoshea matatizo,na haikuchuwa muda kuanzia pale alipomuoa mpaka waislamu wakaanza kuwaacha huru waliokuwa mikononi mwao miongoni mwa mateka wabanii Mus-twaliqi,na wakawa wanawaita wakwe wa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu-na akawa ni mwanamke mwenye baraka kwa watu wake,Anasema radhi za Allah ziwe juu yake- ALLAH akawaacha huru

kwa ajili yake watu mia moja wa nyumba watokanao na kabila la Bani mus-twaliq na hapakuwa na mwanamke aliyejulikana mwenye baraka kwa watu wake kama yeye).(646). Na kwa hakika alipata mafunzo kutoka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na akawa ni mtu wa Ibada na mwingi wa kufunga,na kwa hakika zimepokelewa kutoka kwake hadithi nyingi,na ilikuwa kufa kwake mwaka wa Khamsini tangu kuhama mtume.(647).

Na jambo lenye uhakika ni kuwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuoa kwake ilikuwa ni sababu ya kupatika mafungamano na Bani Mus-twaliq,kizazi hicho kitokanacho na kabila la Khuzaa ambalo lilimpiga vita Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- katika muda ambao walikuwa wamebakia baadhi ya watu wakabila khuzaa ambao ni washirika wa mtume-Sala na amani ziwe juu yake- basi kuowa huku kukachangia kuwafanya wawe karibu na waislamu na kuwasaidia dhidi ya maquraishi katika vita yao waliopigana na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake.

Vita vya Hudaibiyat(Shawwal 6 Hijiria)(648)

Alitanga Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- makusudio yake ya kwenda kufanya Umra.na akaelekea katika mji wa Makkah ili kuitekeleza ibada hiyo kwa amani,na kawaita watu kwa ajili ya hilo na akatoka na watu wa Makkah na wa Madina na baadhi ya waliojiunga na kwao miongoni mwa waliokubali Daawa ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-mpaka ikavuka idadi yao na kuwa zaidi ya watu elfu moja mia Nne(649) na katika sehemu litwayo Dhul hulaifa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Alihirimia kufanya ibada ya umra na akawa ameswaga kichinjwa,(650) ili awafundishe maquraishi kuwa yeye ametoka akikusudia kufanya ziara ya Umra ikiwa ni kuitukuza nyumba tukufu na hakikusudia kuwapiga vita watu wa Makkah.

Na katika mapokezi ya Bin Abii sheiba katika Maghaaziy kutoka kwa Hishaam Bin Ur-wat Bin Zubair Binil Awwam ni miongoni mwa

Riwaya zilizoelezea kwa uchambuzi kuhusu matukio haya,na kwa hakika imepokelewa katika riwawa hiyo: Alitoka mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- kwenda katika sehemu iitwayo Hudaibiya katika mweziwa Shawwal,akasema basi akatoka Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-mpaka alipofika Asafaan akakutana na mtu atokanae na kabila la Ka'ab,na akasema:Ewe Mtume wa ALLAH kwa hakika tumewaacha makuraishi wamewakusanya watu wa aina mbalimbali wakiwalisha vipande vya Nyama vilivyochanganywa na unga(651) wanaktaka kukuzuia usifike Nyumba tukufu,basi akatoka mtume wa ALLAH mpaka alipotokezea sehemu ya Usafani walikutana na Khalid Bin Al-waliid kiongozi wa kundi la Kiquraishi,basi wakampokea njiani basi mtume akasema:Karibia huku basi akakamata baina miti miwili na akafuata njia mpaka akatua sehemu iitwayo Ghamiim(652)Basi akawahutubia watu na akamshukuru ALLAH kwa kile anachostahiki,kisha akasema:ama baada ya kusema hayo,kwa hakika m,aquraishi wamewakusanyia watu mbalimbali jinsia tofauti na wanawalisha nyama na wakikusudia kutuzuia na kutofika Nyumba tukufu nishaurini vile muonavyo,kuwategema watu wa Makka au kuwategemea wale waliowategemea na walowasaidia wakawageuka na kuchukwa wanawake wao na watoto wao,na ikiwa watakaa tu watakuwa wamekaa mkao wa kushindwa,na ikiwa watatutaka msaada basi utakuwa ni msaada wa kinyonge hivyo atawadhalilisha ALLAH,basi akasema Abuubakar:Ewe Mtume wa ALLAH-Rehema na amani ziwe juu yako-ikiwa utawategemea watu wa Makka kwa hakika ALLAH atakuwa ni mwenye kukupa msaada na kwa hakika ALLAH atakunusu natakudhihirisha,basi akasema Miqdaadi Bin As-wad akiwa kwenye kipando chake ,kwa hakika sisi ewe mtume wa Mwenyezi hatwezi kukuambia wewe kama wana wa Israeli walivyomwambia Mtume wao

﴿قَالُوا يَمْوَسِيٰٓ اِنَّا لَنْ نَّدْخُلَهَاۗ اَبَدًا مَّا دَامُوۡا فِيْهَا فَاذْهَبْ اَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَتِيْلًاۗ اِنَّا هُمْۚنَا

قَلْعِدُوۡنَ ﴿٢٤﴾ [المائدة: 24]

((Wakasema ewe Musa kwa hakika sisi hatutoingia katika huo mji hata kidogo muda yakuwa wapo humo,Hivyo nenda wewe na Mola wako mkapigane sisi tupohapa tumekaa)) Al-maidah (24)lakini sisi twakwambia nenda wewe na mola wako mkapigane,nasisi tupo pamoja nanyi tukipigana,basi akatoka Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-mpaka akafika sehemu tukufu na kaingia mpaka sehemu walipokuwa wakitolea kafara Ngamia akapiga magoti,basi wakasema Ngamia amegoma kwenda,basi akasema mtume namuapia Mwenyezi Mungu Ngamia hakugoma kwenda wala siyo tabia yake lakini amezuiwa na kilichomzuia Tembo kutofika Nyumba tukufu,hawataniomba maquraishi jambo ambalo wanalitukuza isipokuwa nitawakubalia ,njooni hapa -Aliwaambia maswahaba wake-basi akaenda upande wa kulia katika upande uitwao Dhaatu Handwala,mpaka akatuwa Hudaibiyat ,na walipofika watu walitaka kunywa katika kisima wakakuta maji yamekauka na wala hayatoki,basi wakamshitakiakuhusu hali hiyo,basi akawapa mkuki alioutoa kwenye ala yake,na akawaambia ukiteni kisimani basi wakaukita kwenye kisima,basi yakaruka maji yake mpaka watu wakanywa mpaka wakatoshaka na kulala kwenye sehemu za mapumziko ya Ngamia,maquraishi waliposikia habari hiyo walimtuma ndugu atokanae na kabila la Banii Hulaisi ambao wanatukuza vichinjwaakasema tumeni kichinjwa ,na walipokiona kichinjwa hawakumsemesha hata neno mojabasi akaaondoka mpaka kwa maquraishi na akawaambia enyi watu wanyama waliondaliwa,Ngamia na zawadi !basi akawatahadharisha na akawakuzia jambo,basi wakamtukana na kumshambulia ,na wakasema kwa hakika wewe ni bedui usiyekuwa na adabu na mpumbavu hatukushangai ,lakini tunajishangaa sisi ambao

tulikutuma wakamwambia kaa chini kisha wakamwambia Ur-wat Bin Masoud: Nenda kwa Muhammad nasi tutakufuata nyuma yako,basi akatoka Ur-wat mpaka akamfikia mtume:akasema:Ewe Muhammad sijawahi kumuona mtu katika waarabu ametembea kama ulivyotembea wewe umepeleka mchanganyiko wa watu kwenye familia yako na kwenye asili yako ambayo ilikuwa imesambaratika ili kulikusanya kundi kubwa,tambua kuwa mimi nimekuja kwako natokea kwenye kabila Ka'ab Bin Luaiy na Aamir Bin Luaiy,kwa hakika wao wamevaa ngozi ya chui watakapotoka wakiwa na wanawake wao na watoto wao ili wawe imara kwenye mapambano(653)naapa kuwa hawatokwazwa na jambo lolote isipokuwa watajibiza kwa kinachoumiza zaidi,Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-akasema sisi hatukuja kwa ajili ya kupigana ,bali tunataka tutekeleze Umra yetu na tuchinje wanyama wetu,kwani haukuja na watu wako kwa hakika ni watu wadogo sana ,na kwa hakika vita imewaogopesha ,na kwa hakika wao hawana salama vita itawale bila kuwaacha kama ilivyotala,mpaka wataniacha mimi nifike nyumba tukufu natutatekeleza Umra yetu na kuchinja wanyama wetu nawa weke kati yangu na wao muda,watazunguka humo wanawake wao na watapata amani kwenye kutembea kwao ,na waniwache mimi na watu ,kwa hakika mimi nitapiganakwa ajili ya hili jambo na watu wote mpaka anidhihirishe mwenyezi mungu au wanaokuja nyuma yangu watengane,basi ikiwa watu watanipata kwa hakika nahilo ndilo wanalolitaka,na ikiwa atanidhihirisha kwao Mwenyezi Mungu watachaguwa ima wapigane wakiwa wamejiandaa au waingie kwenye kujisalimisha kwa kutekeleza masharti,akasema kwa hakika namuapia Mwenyezi Mungu kuwa mnatambuwa kuwa hakuna watu ninaowapenda kuliko nyinyi,kwa hakika nyinyi ni ndugu zangu na watu wenye kupendeza zaidi kwangu,na kwa hakika niliwatafutia usaidizi kwa watu kwenye majumba ya ibada,na walipokataa kuwapa msaada mimi niliwajia na watu wangu mpaka nikashuka pamoja nanyi kwa lengo la kuwaliwaza,namuapia Mwenyezi Mungu

sina nikipendacho katika maisha baada yenu,na kwa hakika mtajuwa kuwa huyu mtu amewatangazia nusu kwa nusu basi mkubalieni,mnajuwa kuwa mimi nilishakwenda kwa wafalme mbalimbali nanimeshawaona watu wenye vyeo,na ninamwapia Mwenyezi mungu sijaona mfalme wa muheshimiwa atukuzwae zaidi kwa watu wake kama yeye,na wala hakuna yeyeto katika wao anaweza kuongea bila ruhusa yake,ikiwa atapewa Idhini ataongea na ikiwa hatopewa ruhusa basi hunyamaza,kisha akitawadha wanashindania kukinga maji anayotawadhia na kisha hupaka kwenye vichwa vyao na wanamfanyia upole,na waliposikia kauli yake walimtuma Suhail Bin Amrou na Mukrizu Bun Hafsi ,wakasema:Nendeni kwa Muhammad ikiwa atawapa aliyoyataja Ur-wat,basi na wamuhukumu arudi mwaka huu na wasije kwetuna wala wasifike kwenye Nyumba tukufu,mpaka asikie mwenye kusikia miongoni mwa waarabu kuwa tumemzuia kwenda,basi akatoka Suhail na Mukriz mpaka wakamjia na wakamtajia jambo hilo,basi akawapa walichokiomba akasema andikeni((Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu))wakasema :twamuapia Mwenyezi Mungu hatuwezi kuandika hata kidogo,akasema:itakuwaje?tunaandika((kwa jina lako ewe mola wetu wa haki))akasema maneno haya yaandikeni maneno haya yandikeni,kisha akasema andika((hivi ndiyo alivyohukumu mtume wa ,Mwenyezi Mungu hilowakasema:twamuapia Mwenyezi Mungu sisi hatutofautiani isipokuwa katika hili,akasema je niandike nini?wakasema andika nasaba yako,na uandike Muhammad Bin Abdillah akasema na hili pia ni zuriliandikeni ,basi wakaliandika,na likawa sharti lao ni kuwa kati yetu na kati yao kuna chanzo cha makubaliano ya kutekeleza tulichokubaliana katika maandishihivyo hakuna kuvunja makubaliano wala kusalitiana ,akasema Baba Usama haya makubaliano ni pingu kwakubaliana kuwa yeyote atakae wajieni katika sisi mtamrudisha kwetu,na wenu akitujia hatumrudishi kwenu,basi akasema mtume wa Mwenyezi Mungu yeyote atakae ingia basi atakuwa amefuata masharti kama

niliyofuata mimi basi maquraishi wakasema atakae kubaliana nasi basi atakuwa ni katika sisi atakuwa amefuata masharti mfano wa masharti yetu,basi wakasema watu wa kabila la banii Qa'ab sisi tupo pamoja nawe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ,na Bani Bakri wakasema sisi tupo pamoja na maquraishi,na wakati wao wapo kwenye kuandikishiana mara ghafla akaja Bin Jandal (654) akitembea hali yakuwa amefungwa ,basi waislamu wakasema :huyu ni Abuu jandal ,akasema mtume-Rehema na amani ziwe juu yake kuwa huyu ni mtu wangu ,na Suhail akasema ni mtu wangu na akasema Suhail Soma andiko mara ghafla ni maandiko ya Suhailbasi Abuu jandal ewe mtume wa Mwenyezi Mungu !enyi kundi la waislamu ! je mwaniacha narudishwa kwa washirikina! chukuweni upanga huu huyu ni mtu mmoja ,basi akasema Suhail hivi hunisaidii ewe Umar? basi akasema MtumeSuhail nipe zawadi mimi,akasema hapana,akasema mtume nikodishie mimi,akasema hapana,akasema Mukriz kwa hakinimekukodishia ewe Muhammad na hatafaulu))(655)

Kwa hakika matukio ya Sul-hu ya Hudaibiyat yalijawa na matukio makubwa ambayo yameelezewa baadhi yake katika Qur;an tukufu,na miongoni mwa hayo matukio ni uungaji mkono wa maridhiano,na kisa chenyewe ni kuwa Mtume Alimtuma Uthman Bin Affan -Radhi za Allah ziwe juu yake- kwa watu wa Makkah ili awape habari kuwa mtume amekuja kufanya ziara kwenye Nyumba tukufu kwa kuitukuza na kufanya ibada ya umra na na wala hatukujakwa ajili ya mapigano,basi akaingia Uthaman katika mji wa Makkah pambizoni mwa Said Bin Aaswi-Radhi za Allah ziwe juu yake- basi akawafikishia wakubwa wa kiquiraishi yale aliyoamrisha na mtume wa ALLAH-Radhi za Allah ziwe juu yake-na wakamtaka atufu katika nyumba tukufu basi akakataa-Radhi za Allah ziwe juu yake-kinyume chake akataka aruhusiwe mtume wa ALLAH kufanya hivyo-Radhi za Allah ziwe juu yake-basi wakajaribu kumzuia Uthman huko kwao-Radhi za Allah ziwe juu yake-(656) Na ikamfikia Mtume-

Sala na amani ziwe juu yake-kuwa Uthmani ameuliwa huko kwa maquraishi kisha mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akawakusanya watu chini ya mti kwa ajili ya kumuunga mkono(657)na kwa hakika waislamu walishindana katika kumuunga mkono mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-mpaka Salamat Binil Auqa'a akamuunga mkono Mtume zaidi ya mara moja,kwa kutamani kurudiarudia kugusanisha mkono wake na mkono wa Mtume wa ALLAH,na wala hakwenda kinyume na uungaji mkono isipokuwa mmoja wa wanafiki naye ni(Al-jaddu Bin Qais),na alikuwa amejificha chini ya Ngamia wake,na kwa hakika ALLAH-kutakasika na machafu nikwake-Aliwasifia waumini waliomuunga Mtume mkono katika maneno yake:

﴿لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا﴾ [الفتح: 18]

Hakika ALLAH amewaridhia waumini pindi walipo kupa kiapo cha utiifu chini ya mti akajua yale yaliyo ndani ya nyoyo zao kisha akateremsha utulivu juu yao akawapa ahadi ufunguzi upo karibu. (Suratil fat-hi 18) Na kwa hakika Mtume aliwasifia watu wa uungaji mkono wa maridhiano akasema: ((Nyinyi leo hii ni watu bora kuliko wote katika ulimwengu)),(658) Na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- amemuunga mkono Uthman akapiga moja ya mkono wake juu ya mkono mwingine(659)

Na kwa hakika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alikuwa ni mlaini kwenye kuamiliiana na maquraishi,na katika sulhu yake kwa kiwango ambacho akawa Umar Bin Khatwab akapatwa na mfazaiko mkubwa kwenye jambo hili na akashangaa na akamwambia Ewe mtume wa ALLAH,hivi kiukweli wewe siyo ALLAH?Akasema Kweli mimi ni mtume wa ALLAH,akasema hivi sisi hatupo kwenye ukweli na wao wapo kwenye Batili? akasema kweli,akasema Umar,basi kwa nini tumpe fursa mwenye hali duni katika dini yetu?akasema

Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-mimi ni mtume wa ALLAH na siwezi kumuasi.Umar akasema hivi haukuwa wewe ni mwenye kutuhadithia kuwa sisi tutaijia nyumba tukufu na tutatufu,akasema kweli,hivi mimi nilikuambia kuwa ni mwaka gani tutakuja akasema Umar hapana ,akasema mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-na kwa hakika yatakwenda na utatufu nyumba tukufu,kisha Umar akaelekea kwa Abuubakar na akasema mfano wa maneno ya mwanzoakisema:Ewe Umar kwani tunampa mtu dhalili nafasi katika dini yetu?basi Abuubakari akamjibu majibu ya mjuzi mwenye akili:Ewe Umar kwa huyo ni mtume wa ALLAH,na wala hawezi kumuasi mola wake basi kamatana mizizi yake,namuapia ALLAH kwa hakika yeye yupo kwenye haki

Na jambo lilipomalizika kwa kukubaliana kuwa Mtume asifanye Umra katia safari hii,bali aje mwaka unaokuja ,akasema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuwaambia maswahaba wake((Simameni mchinje kisha mnyoe)) na akrudia kauli hiyo kuwaambia maswahaba,na wala hawakufanya haraka katika hilo ,kwa kuwa baadhiyao walikuwa wanamatumaini kufanya Umra ,basi akahuzunika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-katika nafsi yake akamwambia suala hilo Ummu salama,akasema Ummu salama-Radhi za Allah ziwe juu yake- toka na wala usimzunguzishe yeyote katika wao kisha chinja kichinjwa chako na unyoe kichwa chako,basi akafanya hivyo mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-,na maswahaba walipoona kuwa mtume kafanya hivyo walisimama haraka,basi wakachinja vichinjwa vyao na wakafanya haraka kunyoa.(661

Na akaelekea Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akiwa anarudi Madina munawwarat,na wakati akiwa njiani ilimteremkia surautl Fathi basi akafurahi furah iliyokuwa kubwa kwa kuteremka sura hiyo Amepokea Imamu Bukhariy katika sahihi yake kutoka kwa zaidi Bin As-lam:kuwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-alikuwa akitembea katika baadhi ya safari zake na Umar Bin Khattwab

akitembea pamoja nae wakati wa usiku,basi Umar akamuuliza Mtume kuhusu jambo fulani na Mtume hakumjibu,kisha akamuuliza na hakumjibu,kisha akamuuliza na wala hakumjibu,Umar akesema yeye mwenyewe Akukose mama yako ewe Umar,nimefanya haraka kumuuliza mtume mara tatu ,mara zote hizo hakujibu akasema Umar:

basi nikamuharakisha Ngamia wangu kisha nikatangulia mbele ya waislamu ,nanikaogopa isije ikaniteremkia Qur'an ,na nikamjia Mtume wa ALLAH-Rehema na amani ziwe juu yake-nikamsalimia kisha akasemamtume)) kwa hakika Imeniteremkia usiku huuSura nayo ni sura ipendezayo zaidi kwangu mimi tangu kuchomoza kwa jua))kisha akasoma

﴿إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا﴾ [الفتح: 1]

(Kwa hikika sisi tumekupa ushindi ulio wazi)(al- Fat-hu:1)(662)

Na kwa hakika Aya imetilia mkazo na pia Riwaya za Hadithi kuwa Sulhu ya Hudaibiyat ilikuwa ni tukio la ushindi uliokuwa mkubwa, ALLAH kwa kupitia tukio hilo alifungua fursa za Da'awa katika miji yote ya kiislamu na pia katika ulimwengu wote,pale ambapo ilifuatia baada ya tukio hilo kujiunga baadhi ya makabila na mkataba wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kama ambavyo tukio la Hudaibiyat lilifuatiwa moja kwa moja na ujumbe wa Mtume kwenda kwa wafalme wa hapa ulimwenguni,(663) na huko kukawa kama alivyokuita Mwenyezi Mungu ushindi mkubwa ,ALLAH mola wa waja alifunguwa kwa waja wake kuweza kusikiliza wito wa ALLAH,na kwa hakika imepokelewa kuwa Abu bakar Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- alisema((hapajawahi kupatikana ushindi mkubwa katika uislamu kama ushindi wa Hudaibiyat,lakini watu lakini watu mtazamo wao uliishia kwa yaliokuwapo kati ya Muhammad na na Mola wake,na watu kawaida ni wenye kuwa na haraka ,ninamwapia ALLAH kuwa ALLAH hana hafanyi haraka kwa mja wake

kuharakisha,ni mpaka mambo yafikie pale atakapo))(664) Na lilikua chumo na faida ka waislamu ni kubwa katika hii Sulhu kwa kiasi kisichweza kuhesabika,na faida yenyewe ilikuwa waziwazi haifichikani ALLAH aliitambua na akaiita (Ushindi mkubwa) Sulhu hii ilikuwa ni kuwatambuwa waislamu na Dola yao na kiongozi wao mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kama ambavyo makubaliano yaliwapa waislamu fursa ya kutanua wigo wa Da'awa na kurudi tena mwaka ujao wa pili kutekeleza suala la kuhama.

Na ama kuhusu masharti yaliyokuja ya kumrudisha kwa waislamu yeyote miongoni mwa maquraishi pasina idhini ya walii wake,kwa hakika ilikuwa wazi ni jambo gumu kwa waislamu,ama katika kulifanyia kazi kukatokea sintofahamu mwanzo wa utekelezaji wa hilo.

Na kwa hakika lilikuja kundi la waislamu katika mji wa Madina wakitokea Makkah pasina Idhini ya watu wao,na alikuwa miongoni mwao Abuu Buswair Ur-watu Bin Asad Al-Thaqafiy -Radhi za Allah ziwe juu yake-na akawatuma Maquraishi wawatafute kwa mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- basi mtume akamkabidhi kwa watu wawili wa kiquraish ,na alikuwa ni mwenye Imani Thabiti,na mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akamwambia: ((Ewe Abuu Buswair hakika sisi tumeweka na hawa watu Ahadi,na wala haifai katika Dini yetu kuwa wasaliti na kwa hakika ALLAH atakupa wewe na na walio pamoja nawe miongoni mwa wanaonyongeshwa faraja na suluhisho))(665) Basi akatoka hali yakuwa ni mateka akiwa pamoja na watu wawili,na walipokuwa njiani aliweza kuupokonya upanga wa mmoja wao na akamuua,na yule,mwingine akakimbia akiwa na Khofu na akaingia katika mji wa madina akiwa na khofu ,basi akampa habari Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-yaliyotokea basi mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akamtuliza kisha akaja Abuu Buswair na akasema:Ewe Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-kwa hakika ALLAH Deni lako kwa hakika ulinirudisha kwao kisha Mwenyezi Mungu akaniokoa kutoka kwao basi Mtume-Sala na

amani ziwe juu yake-akasema: ((Lau angekuwa pamoja nae mtu wa kumsaidia wangewasha moto wa vita))(666) Kisha akatoka Abuu Buswair mpaka pande(Al-aiswi) (667) kwenye njia ya biashara ya Maquraishi pande za pwani,na akakutana na na waliotoka miongoni mwa waislamu katika Maquraishi,na walikuwa miongoni mwao kundi linalokaribia wapiganaji Sabini,wakavamia njia ya maquraishi na Biashara zake,basi Maquraishi wakatuma kwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake wakimtaka awahifadhi kwake,(668)na wakatangaza sharti la kurejea nyuma na hili sharti likawa ni Ushindi kwa waislamu,na ALLAH akampa Abuu Buswair na watu mfano wake suluhisho na utatuzi,kama alivyotoa habari Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- utelezaji wake wa Ahadi.

Ujumbe wa Nabii kwenda kwa viongozi wa ulimwenguni(669)

Alitumwa mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- kwa ulimwengu mzima,amesema ALLAH mtukufu:

﴿ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴾ [الأنبياء: 107]

Na hatujakutuma asipokuwa rahma kwa watu wote [Al Anbiyaa: 107]. Anawaita Muumba kwenye kumuabudu muumba ,na kuwatowa kwenye giza na kuwapeleka kwenye Nuru kwa idhini ya mola wao,na kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka ,amesema ALLAH Mtukufu:

﴿ قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ الْكَذِبِي الَّذِي يُوْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَتِهِ وَأَتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴾ [الأعراف: 158]

Enyi watu hakika mimi ni mtume wa ALLAH kwa wote ALLAH ambye ni wake ufalme wa mbinguni na ardhini hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye na toa uhai na anafisha basi muaminni ALLAH na mtume wake nabii asiye jua kusoma wala kuandika anamuamini ALLAH na maneno yake na mfuateni ili mpate kuongoka. [Al A'araf: 158]. Na jambo hili haliitajii ujuzi mkubwa ,kwani ulimwengu na hali za wanaadamu waishio humo ni hali moja kwa mtazamo wa muumba:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْوَمُ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ﴾ [الحجرات: 13]

Enyi watu hakika sisi tumekuumbeni kutokana na mwaume na mwanamke na tukawajalia kuwa mataifa na makabila ili mtambuane hakika mbora wenu mbele za ALLAH ni mchamungu wenu hakika ALLAH ni mjuzi muelezaji. [Al Hujrati: 13]. Basi Uislamu na Mtume wa uislamu unawaita watu kwa Mwenyezi Mungu na unawafanya kuwa kitu kimoja chini ya kumuabudu Mwenyezi mungu,na kuondoa makundi kujiona bora

﴿لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْوَمُ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ﴾

(Ili mpate kujuwana ,kwa hakika mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni wachamungu wenu,kwa hakika mwenyezi mungu ni mjuzi na ni mwenye habari wa mambo yote)hakuna mbora wa mwekundu kwa mweupe, ((Watu wote wapo sawa kama meno kitana)) Na hapa twafahamu kuwa ujuzi wake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-wa kuufahamu ulimwengu na vyenye kuuzunguka ulimwengu na watawala wake na nidhamu zake,na kuyajuwa makabila na viongozi wake,na kujuwa Dola mbalimbali na hali zake zilizo wazi,na haikuwa kuchaguwa kwake Nchi ya Habash kwa ajili ya kuhamia maswahaba wake licha yakuwa nchi hiyo ipo nyuma ya Bahari katika Bara lingine yote hayo yamefanyika kwa

mtume kujuwa hali ya nchi hiyo na Nidhamu zake ,na kiwango cha uadilifu katika Nidhamu,na upeo wa utekelezaji kwa wafalme wake"Kwani humo kuna Mfalme Hadhulumiwi kwake mtu yeyote"(670)

Baada ya Sulhu ya Hudaibiyat aliandika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Ujumbe kwenda kwa idadi kubwa miongoni mwa wafalme wa ulimwengunina akalitilia umuhimu jambo hilo ,na akachaguwa miongoni mwa maswahaba wake katika kila upande mwenye kufaa upande huo miongoni mwa waliokuwa na uzoofu na wenye kuzijuwa sehemu hizo,na akawausia na kuwapa hisia za majukumu,amesema Bin Hishaam Imenifikia habari kuwa Mtume wa ALLAH-Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- aliwatokea maswahaba wake siku moja baada ya kutoka Umra yake ambayo alizuiliwa kwenda siku ya Hudaibiyat,basi akasema: (Enyi watu kwa hakika ALLAH amenituma hali ya kuwa ni Rehema kwa watu wote,basi msitofautiane kwa ajili yangu kama walivyo tofautiana wafuasi wa Issa Bin Maryam,basi wakamuuliza maswahaba zake na nivipi walivyotofautiana ewe mtume wa ALLAH?Aliwalingania katika lile ambalo ninawalingania kwalo,basi yule ambaye alitumwa sehemu ya karibu aliridhika na akasalimu amri,ama yule ambaye alituma sehemu ya mbali alikunja uso na kuwa mzito,basi Isaa akashitakia kwa ALLAH basi wakawa wale walioona uzito na kila mmoja wao anaongea lugha ya Umma ambao ametumwa kwao,basi Mtume wa ALLAH-Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-wajumbe miongoni mwa maswahaba wake na akawaandikia ujumbe kwenda kwa wafalme akiwalingania kwenye ujumbe huo kuingia katika uislamu)(671)

Ujumbe wake kwenda kwa Mfalme wa Roma:

Roma ilikuwa ikizingatiwa ni Dola yenye nguvu zaidi katika zama za Mtume-Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kwa hakika Qur'an tukufu iliizungumzia Nchi ya Roma katika sura iliteremka Makka na ikaitwa kwa jina la Roma .

﴿الْمَ غَلَبَتِ الرُّومُ ﴿١﴾ فِي أَذَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٢﴾ فِي بضعِ سِنِينَ لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلِ وَمِنْ بَعْدُ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٣﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٤﴾﴾ [الروم: 1-5]

na imekuja humo ALLAH ndiye mjuzi wa maana yake Walishindwa wa ROMA katika sehemu za karibu za ardhi ya Shamu kuelekea Uajemi. Na Baada ya kushindwa kwao watashinda(3) Kwa kipindi cha miaka isiyo zidi kumi jambo lote ni lake ALLAH kabla na baada na siku hiyo watafurahi waumini. Kwa nusra ya ALLAH anamnusuru amtakaye na yeye ni mwenye nguvu mpole. Aal-ruum:1-5.

Na ilikuwa Vita ikizunguka wakati huo kati ya Roma na Fursi katika pande za Palestina na Jordan,na ulimwengu mzima ulikuwa kiiizungumza vita hiyo

Na inavyofahamika kuwa mjni wa Misri na Sham na Africa ya Kaskazini zilikuwa ni wilaya zenye kufuata utawala wa Roma ya kiyunani na alikuwa mtawala wa kweli wa hukumu katika huu utawala ni mfalme mwenyewe (Mfalme) ambaye aliifanya Costantino ni mji mkuu wake(672) na hakimumu na wenye kuhukumiwa walikuwa wote ni manaswara .(673)

Na kwa hakika katika kipindi hicho palidhihiri Nizamumu ya Wenye kulazimiana,ambao walikuwa wakifanya kazi ya kuleta kodi zao wenyewe kwa malipo yakutoa kiwango fulani cha pesa wanazozitoa kwenye Serekali,na matokeo yake wakazidisha kodi kwa watu,na dhulma ikazidi mpaka yakapita malipo yao ambayo walikubali kuyatoa kwenye serekali.(674)

Na kwa hakika yalikutikana madhehebu mbalimbali ya kikristo katika ufalme wa Roma,na kukazidi khitilafu za kiitikadi ambazo zilipelekea magomvi yaliyofikia kwenye ngazi ya hali ya juu ya uadui

baina ya Kanisa,na kilichofuata kukatokea aina ya uadui baina ya baadhi ya Wilaya na baadhi ya mataifa pamoja na Dola ya Roma.

Na kwa hakika Utawala wa Roma ulipitisha Madhehebu ya Thiolojia ndiyo yenye kuenea katika mji Costantino kuliko baadhi ya Wilaya,na haswa katika mji wa Misri,jambo ambalo lileta uadui na wakazi wa zamani wa Misri.(675)

Alikuwa mfalme wa Roma na mtawala wao na utawala wao katika wakati wa Mtume ni Hiraqli(610 -641) hijiria naye anatokana na familia ya Kiyunani,alizaliwa Qur-taabah ambapo kwa sasa ni nchi ya Tunusia,na alikuwa mzazi wake ni mtawala wa Yunani,na kwa hakika aliitwa Hiraqli kwenda katika mji mkuu wa Costantino,na akamilikishwa mji wa Roma katika kipindi cha mapambano na Fursi,na kwa hakika alifaulu katika kuishinda Dola ya Fursi na akarudisha nguvu ya Roma na heshima yake kwa mara nyingine

﴿الْمَ عُلَيْتِ الرُّومُ ﴿١﴾ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٢﴾ فِي بَضْعِ سِنِينَ لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ بَعْدُ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٣﴾﴾ [الروم: 1-4]

Alifu laam miim Walishindwa wa ROMA (2) katika sehemu za karibu za ardhi ya Shamu kuelekea Uajemi. Na Baada ya kushindwa kwao watashinda(3) Kwa kipindi cha masiku yasio zidi miaka kumi na jambo mi lake ALLAH kabla na baada na siku hiyo watafurahi waumini. Al- ruum:1-4) Na hiyo ilikuwa mwaka 616 tangu kuzaliwa kristo,na alaikuwa Hiraqli ni kiongozi wa kikristo,aliweza kuurudisha msalaba mtukufu kwao,msalaba ambao wanaamini kuwa Masihi alisulubiwa kwenye huo msalaba,basi wakafurahi wakiristo wote kwa jambo hilo na wakafanya mahafali katika kila sehemu,(676)na haswahaswa katika katika Qudsi,pale ambapo ulimfikia ujumbe wa mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-na ikawa miongoni mwa yaliyokuwemo humo kama ilivyothibiti katika sahihi mbili kuwa aliandika ujumbe kwenda kwa Hiraqli: Bismillahir Rahmanir Rahiim kutoka kwa Muhammad

Mtume wa ALLAH kwenda kwa Hiraqli Mkubwa wa Wa Roma, Amani iwe juu ya mwenye kufuata uongofu, ama baada ya kusema hayo, kwa hakika mimi nakuita kwa kukutangazia uislamu, Silimu utasalimika ALLAH atakupa malipo yako mara mbili, na ikiwa utakwenda kinyume kwa hakika utakuwa na madhambi ya wanyonge.

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾﴾

[آل عمران: 64]

Sema ewe-MUHAMMAD-kuwaambia mayahud na manaswara njooni kwenye neno la sawa sawa baina yetu na nyie tusimuabudu isipokuwa ALLAH na wala tusimshirikishe na kitu chochote na wala usiwafanye baadhi yetu kuwa ni miungu kinyume na ALLAH basi kama mtaenda kinyume semeni shuhudieni kuwa sisi ni waislamu. Surat [Al-Imran: 64]. Al-arsiyuuna ni waajiriwa na na wafanya kazi na wakulima na watu wasiokuwa na ujuzi miongoni mwa watu na wenyekunyongeshwa kwa ujumla, ambao Hiraqli anawawekea kizuizi cha kutousikiliza uislamu.

Na kwa hakika Mtume alimtuma Dahiyat Bin Khalifah na ujumbe kwenda kwa Hiraqli, na alikuwa Dahiyat ni miongoni mwa watu waliokuwa wakisimuliwa na warumi katika mji wa Sham, pale ambapo kabila lake lipo sehemu iitwayo Kalbu kwenye Ncha ya kusini mwa miji ya Sham, (678) na huko hujulikanwa namna ya kuufikia ufalme wa Hiraqli na kuzunguza nae.

Na ujumbe wa Mtume wa ALLAH ulipomfikia Hiraqli alifadhaika sana, naye nikatika wanawazuoni wa kikristo wenye kutegemewa kwao, pamoja na kuwa yeye ni mfalme wao, na alitilia umuhimu Ujumbe na akajaribu kupata Elimu ya kiwango cha juu, basi akataka aletewe mmoja miongoni mwa watu wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na awe ni miongoni mwa wanaomjuwa, na

alikuwa Abuu Sufiyani Bin Harbi-kabla ya kusilimu-katika pande za Nyumba tukufu akiwa katika Biashara za Maquraishi baada ya Sulhu ya Hudaibiyat basi akaletwa pamoja na alikuwa nao miongoni mwa wafanyabiashara wa kiquaish wakaletwa kwa Hiraqli akawa anamuuliza kuhusu Mtume ,na walipokuwa mbele ya Hiraqli aliuliza na kujadili kuhusu namna ya kufanya ukalimani,na kwa hakika Bukhariy ameleta suala hilo na akasema: (Alituelezea Abuu Al Yamama Al Hakam bin Naafi'i alituelezea Shuaybu kutoka kwa Zuhri alisema: Alinieleza Ubeydi LLahi bin Abdillahi bin Utbah bin Mas'ud ya kwamba Abdillahi bin Abas alimueleza kuwa Abaa Sufiyani bin Harbi alimueleza ya kwamba Hiraqli alimtumia mjumbe Abuu Sufiyani katika msafara wa Maqureshi na walikuwa ni wafanya biashara katika Mji wa Sham katika muda ambao Mtume rehman na amani za Allah ziwe juu yake, alikuwa amefanya mapatano ya Sulhul Hudaibiyah baina ya Abuu Sufiyani na makafiri wa Kiqureshi - na mkataba huo ulikuwa ni wa miaka kumi na ujumbe huo ulifika katika mwaka wa sita tangu Mtume kuhama kutoka Makka kwenda Madina, rejea Fathul Baar , V.1, Uk. 34 – wakamwendea Hiraqli wakiwa katika Mji wa Iliyaai (6792)), (ni Mji katika Miji ya Sham), Hiraqli akawaita katika kikao chake (majlisi) akiwa amezungukwa na viongozi wakubwa wa Kiroma na akamwita mtu wa kutafsiri maneno yake akasema: Ni nani mwenye nasabu ya karibu na mtu huyu ambaye anadai kwamba yeye ni Mtume? Abuu Sufiyani akasema: Nikajibu mimi ndiye mwenye nasabu ya karibu, Hiraqli akasema: Msogezeni karibu yangu na wasogezeni ndugu zake karibu mgongo wangu, kisha akamwambia mfasiri wake: Waambie mimi namuuliza huyu Abuu Sufiyani kuhusu mtu huyu (Mtume) akinidanganya basi mkadhibisheni, Abuu Sufiyani akasema: Namuapia Allah lau ingekuwa siyo aibu wao kunijua mimi ni muongo basi ningesema uongo kuhusu Mtume rehman na amani za Allah ziwe juu yake, kisha ikawa swali la kwanza aliloniuliza kuhusu Mtume rehman na amani za Allah ziwe juu yake alisema hivi: Vipi nasabu yake kwenu? Nikasema: Yeye ana nasabu tukufu kwetu, Hiraqli akauliza: Kuna yeyote

aliyedai Utume miongoni mwenu kabla yake? Nikasema: Hapana, Hiraqli akauliza: Katika Baba zake kulikuwa kuna Mfalme? Nikasema: Hapana, akauliza: Watu watukufu wanamfuata au ni madhaifu tu? Nikasema: Wanaomfuata ni watu madhaifu, akauliza: Hao wanaomfuata wanazidi kila siku au wanapungua? Nikasema: Wanazidi kila siku, akauliza: Je! Kuna mtu anaritadi miongoni mwao kwa kuchukizwa na Dini yake baada ya kuwa ameshaingia? Nikasema: Hapana, akauliza: Je! Mlikuwa mnamtuhumu uongo kabla hajasema hayo aliyo yasema? Nikasema: Hapana, akauliza: Je! Anafanya khiyana? Nikasema: Hapana, anasimulia Abuu Sufiyani: katika hali ambayo sisi tupo kwa Mfalme Hiraqli hatukujua ni nini atakacho tufanya baada ya hayo maswali, na sijaweza kusema chochote zaidi ya neno ndiyo au hapana. Hiraqli akaendelea kuuliza: Je! Mlilimpiga vita? Nikasema: Ndiyo, akauliza: Vita vyenu kwake vilikuwaje? Nikasema: Vita baina yetu na yeye ilikuwa ni kushindana mara anatumu na sisi tunampiga, akauliza: Anawaamrisha nini? Nikasema: Anasema muabuduni Allah Mmoja na msimshirikisha na chochote, na acheni yanayosemwa na Baba zenu, na anatumu amrisha kuswali na kuwa wakweli na kujiepusha na mambo machafu na kuunga udugu. Hiraqli akamwambia mfasiri wake: Mweleze nimekuuliza kuhusu nasabu yake ukasema kuwa ana nasabu tukufu, vilevile Mitume wanatumwa katika nasabu ya watu wake, na nimekuuliza kuna yeyote miongoni mwenu aliyewahi kusema maneno kama yake, ukasema hapana, lau kama kungelikuwa na yeyote aliyewahi kusema maneno kama yake kabla yake ningelisema mtu huyo anafuata kauli iliyosemwa na mtu kabla yake, na nimekuuliza kwamba katika Baba zake kulikuwa na Mfalme, ukasema hapana, nasema: Katika Baba zake kama kungelikuwa na Mfalme ningesema mtu huyo anatafuta Ufalme wa Baba yake, na nimekuuliza je! Mlikuwa mnamtuhumu uongo kabla hajasema hayo aliyoyasema, ukasema hapana, kama angeliwahi kusema uongo tungejua kwamba hawezi kuacha kudanganya watu na kumsema uongo Mwenyezi Mungu, na nimekuuliza watu watukufu ndio

wanaomfuata au ni watu madhaifu, ukasema kuwa watu madhaifu ndio wanao mfuata, na watu madhaifu ndio wanaofuata Mitume, na nimekuuliza je! Wanazidi au wanapungua, ukasema kwamba wao wanazidi, hivyo ndivyo linavyokuwa jambo la imani mpaka litakapo timia, na nimekuuliza hivi anaritadi yeyote kwa kuichukia Dini yake baada ya kuingia, ukasema hapana, vilevile imani pindi furaha yake inapoingia moyoni haiwezi kutoka, na nimekuuliza je! Anafanya khiyana, ukasema hapana, vilevile Mtume hawafanyi khiyana, nimekuuliza nini anakuamrisheni, ukasema kwamba anakuamrisheni juu ya kumuabu Allah na msimshirikishe na chochote na anakukatazeni kuabudu mizimu na anakuamrisheni kuswali na kutoa sadaka na kujizuia na mambo machafu, ikiwa kama unayoyasema ni kweli mtu huyo atamiliki sehemu nilipoweka miguu yangu miwili, na nilikuwa najua kuwa mtu huyu niwa nje sikuwa najua kama ni miongoni mwenu, lau ningekuwa najua kuwa ndiye ninaye mtakasia niya basi ninge weka uzito wa kuonana naye, na laiti ningekuwa kwake basi ningemuosha miguu yake, kisha akaitisha barua ya Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake ambayo Mtume rehma na amani za Allah ziwe juu yake alimpa Dihiyah aipeleke kwa Mfalme wa Buswriy akampa Hiraqli akaisoma ikawa yaliyomo ni: Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, kutoka kwa Muhammad ambae ni mja wa Allah na Mtume wake kwenda kwa Hiraqli Mfalme wa Roma, amani iwe juu ya mwenye kufuata uongofu, baada ya hayo, mimi nina kulingania kwa ulinganio wa Kiislamu, silimu utasalimika na ALLAH atakupa malipo mara mbili, na ukikataa utakuwa na madhambi sawa na wanaoabudu moto (3قال)).

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿١٥٠﴾﴾

[آل عمران: 64]

Na enyi Watu wa Kitabu! Njooi kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila ALLAH, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Miungu badala ya ALLAH. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudi eni ya kwamba sisi ni Waislamu) [Al-Imran: 64]).

Na kuna simulizi tofauti zenye kuonyesha kuwepo kwa malumbano maalimu baina ya Hiraqli na Dahiyat Al-kalbiy wakiwa peke yao, maneno yalipita kuhusu uislamu na mtazamo wake kuhusu Masihina na mwenye kuombewa na masihi, na khafu yake kwa ALLAH na mwisho mbaya juu yake na kwa ufalme wake na Akhera yake.

Na kwa hakika Hiraqli alifanya ujanja na akaandika ujumbe kwenda kwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na akamtuma Dahiyat na Zawadi kumpelekea Mtume, basi mtume aliigawanya zawadi ile kwa waislamu, na akasema kuhusu Hiraqli: Amesema uongo Adui wa yeye bado yupo kwenye ukiristo wake (681)

Na licha yakuwa wana Historia walitilia shaka mfano wa riwaya mfano wa hii ambayo haikuja kwa Sanad iliyokuwa wazi kwa watu wa hadithi na wala haikuchambuliwa, ila ni jambo la kawaida kwa Hiraqli kukaa na Dahiyat mbeba ujumbe na kujadiliana nae, na kuhusu huo ujumbe, imekuja wazi katika sahihi ya Bukhari na sahihi nyingine ikionesha Hiraqli kutilia umuhimu ujumbe jambo ambalo linajulisha juu ya kukinai kwake ukweli wa Mtume - **Rehema na amani ziwe juu yake** - ijapokuwa hakuweka wazi uislamu wake.

Na kwa hakika hiraqli kuujuwa ukweli wa mtume lilikuwa ni jambo ambalo lipo wazi, nakujuwa kuwa mtume halinganii isipokuwa katika haki, na kuwa yeye ni Mtume, na kuwa yeye ni mtume wa waliotabiriwa, ni Nabii wa zama za mwisho, na alikuwa na uhakika wa kunusuriwa na ALLAH, na kuwa ALLAH atamtimia aliyomuahidi ikiwa miongoni mwa kuenea dini yake na kushinda Daawa yake, na kwa hivyo Abu Sufiani alisikia kutoka kwake aliyoyasikia katika

kipindi ambacho bado alikuwa kwenye ushirikina na akiwa ni kiongozi wa maquraishi na mwenyekumpiga vita Mtumewa ALLAH-Rehema na amani ziwe juu yake-na kilichotokea ni kupatwa Khofu Abuufufiani ya kumuogopa Mtume-ALLAH na amani ziwe juu yake-na pia kukatokea katika nafsi yake ujuzi wa kujua haki alipoona Khofu ya Hiraqli na mazungumzo yakebasi akasema:(Huyu Mfalme wa Banii Asfar anamuogopa)na alikuwa Abuufufiani mpaka wakati huo ni Adui wa Mtume-ALLAH na amani ziwe juu yake-akajikuta kuwa ni adui ya mwenye kuogopwa na wafalme wakubwa wa ulimwenguni katika kipindi chake.

Na alikuwa Hiraqli ni mwenye huzuni na mwenye kutangatanga baina ya kumwamini Mtume na nakufuata maamrifo ya masihi ya kuamini mtume wa Mwisho,nakilichofuata ikawa ni kuutekeleza uislamu pamoja na ukiristo uliopita,au kuwacha kuwa na imani na badala yake kumuasi ALLAH na Mtume wake na kuyapa kipaumbele Maisha ya Dunia kulioko Akhera,na kuipaka mafuta siasa ya ya Kiroma,na kuwanyenyekea wao kwa ajili ya kubakia kwenye nguvu ya uongozi,na kwa hivyo basi alitaka kuwapa mtihani viongozi wa Roma ikiwa je watafuata pamoja nae imani ya kumuamini Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kwa hakika alizuka mmoja miongoni mwa Maaskofu wa kikristo wa Sham alikuwa akiitwa Bin Naatuur na alikwa ni miongoni mwa wafuasi wa Hiraqli akasema: Kisha Hiraqli akaandika kwa mtu wake Baruumiyat,na alikuwa ni mpinzani wake katika Elimu na akaenda Hiraqli mpaka Himsi Na hakufanikiwa kufika Himsi mpaka ukawa ujumbe kutoka kwa mtu wake umemfikia ukiwa unakubaliana na Rai ya Hiraqli ya kutoka Mtume,na kuwa yeye ni Mtume Basi Hiraqli akawapa ruhusa wakubwa wa Roma katika jengo lake la Diskara katika mji wa Himsi(682)kisha akaamrisha milango kufungwa kisha akachungulia,akasema:Enyi kundi la watu wa Roma hivi mtakuwa ni wenye kufaulu na kuongoka naufalme wenu utadumu kwa ajili hiyo mnamuunga mkono huyu Mtume? basi wakatimua mbio za punda milia mpaka kwenye milangona

wakaikuta imefungwa,na Hiraqli alipoona ukimbaji wao na kukata kwao tamaa ya kutokuwa na imaniakasema:warudisheni kwangu,na akasema:hakika mimi nimesema maneno yangu hivi karibu ninawajaribu kwa maneno hayo ili kujuwa msimamo wa Dini yenu,kwa hakika nimeona basi wakamsujudia na wakamridhia) (683)

na hivi ndivy Qur'an ilisadikisha maneno ya Hiraqli katika sura Rum

﴿بَلِ اتَّبَعَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَهْوَاءَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ فَمَنْ يَهْدِي مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿٢٩﴾
فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَةَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَلِكَ الدِّينُ
الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾﴾ [الروم: 29-30]

Isipokuwa wale walio dhulumu nafsi zao walifuata matamano bila ya maarifa basi hakuna wa kumuongoza yule atakaye potezwa na ALLAH na hawata pata wao wa kuwanusuru. Basi simamisha uso wako kwenye dini hali ya kuwa ni mpwekeshaji maumbile ya ALLAH aliyo waambia watu kwayo hakuna wa kubadilisha uumbaji wa ALLAH hiyo ndio dini ya sawa isipokuwa watu wengi hawafahamu. Al-ruum 29-30. Na kauli ya Allah katika surat Ruum:

﴿فَإِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتَىٰ وَلَا تُسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلُوا مَدْبِرِينَ ﴿٥٢﴾ وَمَا أَنْتَ بِهَادٍ الْعُمَىٰ عَنْ
ضَلَّالَتِهِمْ ۗ إِنْ تُسْمِعُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٥٣﴾﴾ [الروم: 52-53]

Na hakika wewe huwezi kuwasikilizisha wafu wala huwezi kumsikilizisha kiziwi maombi wanapo kimbia kurudi nyuma. Na hukuwa wewe-muhammad- ni mwenye kumuongoza kipofu kunako upotevu wao huna unaye msikilizisha isipokuwa yule mwenye kuamini aya zetu basi wao ni waislamu. Al- Ruum:52-53) Na katika maneno yake mwenyezi Mungu mtukufu katika surat Rum

﴿فَيَوْمَئِذٍ لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَعذِرَتُهُمْ وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٥٧﴾﴾ [الروم: 57]

Basi siku hiyo haita wanufaisha udhuru wale ambao walio dhulumu na wala wao hawata laumiwa. Al-rum:57

Na huenda mwanadamu akatafakari kidogo ushuhuda wa Qur'an katika surat Al-rum ,na aone kuwa kuja huu ushahidi katika Surat Rum ni kama unaashiria msimamo wa falme waona wakubwa wao katika suala hilo kubwa kwa mwenye kulizingatia.

Na kwa hakika Hiraqli alizungumza kwa uwazi kabisa kuhusu kupata ushindi kwa waislamu huko baadae katika masiku ya karibu,na kukunjuliwa kwao vilivyopo chini ya miguu yake,na akaikusudia katika hilo mji wa Palestina na miji mingine ya Sham iliyobakia.

Na ukawa msuguano wa kwanza wa kijeshi ni kati ya wa Roma na waislamu katika vita vitwavyo Muu'ta.vita ambavyo aliviongoza Zaid Bin Haaritha Mshirika wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na ni swahaba wake na ni miongoni mwa vipenzi wakubwa kwake kulikwe watu wengi,na yakawa matokeo ya yale makabiliano ya kwanza ni kuuliwa shahidi idadi kubwa ya maswahaba wa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-miongoni mwao ni Zaid Bin Haarith,na Jaafar Bin abii twaalib,na Abdullah Bin Rawaah,na uwoga wa Hiraqli wakuwafuata waislamu na kupigana nae ulikuwa wazi ,pamoja na nguvu alizokuwa nazo na kuwafuatilia kwake wafursi mpaka kufikia kuvamia miji yao,ila yeye hakupupia kusuguwana na Mtume na jeshi lake na kuwakabili,na huenda Qur'an tukufu katika Surat Ruum iliashiria na kutahadharisha watu madhalimu wenye nguvu kwa ujumla,na miongoni mwao ni wa Roma katika Sura iliyoitwa kwa jina lao katika maneno yake mtukufu:

﴿أَوْ لَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ كَانُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَأَثَارُوا الْأَرْضَ وَعَمَرُوهَا أَكْثَرَ مِمَّا عَمَرُوهَا وَجَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ

وَلَكِنَّ كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٩﴾ ثُمَّ كَانَ عِقَابَ الَّذِينَ أَصْحَابُ السُّورَةِ أَنْ كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَكَانُوا
بِهَا يَسْتَهْزِئُونَ ﴿١٠﴾ [الروم: 9-10]

Hivi hawatembezi duniani kisha wakatazama namna gani ilikuwa mwisho mbaya kwa wale walio kuwa kabla yao walikuwa ni wenye nguvu kuliko wao waliitifua ardhi na wakaimarisha ndani ya ardhi zaidi kuliko walivyo imarisha wakajiwa na mitume wao hakuwa ALLAH ni mwenye kuwadhulumu isipokuwa nafsi zao walizifanyia dhulma. Kisha ikawa mwisho mbaya kwa wale walio fanya uwovu wakapinga aya zetu na wakawa wakizifanya utani. Al-Rum:9-10

Kwa hakika mimi nihisi kuwa hizi Aya kana kwamba zimelekezwa kwa watu wa Roma wa mwanzo na wa Mwisho ambao waliitawala Dunia, na walipozipinga Alama za Mwenyezi mungu mwisho wao ukawa mbaya, walipozidhulumu nafsi zao basi ALLAH akawarithisha waislamu Ardhi zao, baada ya wao kuzipinga alama za ALLAH, na likarudi jeshi la Mtume ALLAH-Rehema na amani zite juu yake kutoka katika vita vya Mu'uta, wakakutana na vijana wa madina kwa kuwaambia: Enyi mliokimbia, hapo akawatetea mtume kwa kusema siyo wenye kukimbia bali ni wenye kupanga mashambulizi kwa mapenzi ya ALLAH (684) basi wakati anarudi Khalid baada ya kupita miaka ili aliongoze jeshi la waislamu katika vita yao kubwa na waroma katika sehemu iitwayo Yarmouk, na alikuwa ni upanga miongoni mwa panga za ALLAH kama alivyosimilia Mtume-ALLAH na amani zite juu yake- (685) na Hadithi hiyo kutoka kwa mtume-Sala na amani zite juu yake- ilikuwa ikihusiana na upande wao kwenye muda ujao katika sehemu ya Yarmouk na sehemu zingine na kutokea huo muujiza miongoni mwa miujiza ya mtume -Sala na mani zite juu yake- na miujiza ya mtume ni mingi kiasi gani kwa mwenye kutafakari.

Kisha ukaja msugurano wa kijeshi kwa mara ya pili katika masiku ya mtume -Sala na amani zite juu yake- katika vita vya Tabuk, vita

amabavyo aliviendesha Mtume yeye mwenyewe-Sala na amani ziwe juu yake-,na alikuwa pamoja na jeshi kubwa ambalo waislamu walilijuwa jeshi hilo katika enzi zake,na lengo la jeshi hilo lilikuwa ni kuwapiga waroma na pembe za Dola yao ya upande wa kusini,kwakuwa Tabuuk ilikuwa kwenye mipaka ya miji ya Sham,kule alipoweka kambi mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kwa takriba siku kumi na tano,alieneza wakati huo karibia ujumbe wa kijeshi katika sehemu zilizopambizoni,na akawasiliana na idadi kadhaa ya viongozi wa miji na makabila yaliyopo pambizoni na yaliyokuwa ndani ya mipaka ya Roma,na akafunga nao makubaliano maalumu mbele ya masikio ya Hiraqli na macho yake,pale ambapo Riwaya zilielezea kuwa hapakuwa na misuguwano kati ya jeshi la Roma na jeshi la Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake,pale waliposhindwa kiukweli,licha ya nguvu za kijeshi na uwezo wake wa makabiliano.

Na kwa hakika imepokelewa kuwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-alimuandikia Hiraqli ujumbe akiwa Tabuuk akimpa Hiyari ya kuchagua jambo moja kati ya matatu;Ima asilimu na atabakiwa na ufalme wake ,na Ima atoe kodi,Na Ima atoe idhini ya kupigana vita,Hiraqli akawakusanya wataalamu wake na makasisi wake katika Jumba lake na akawafungia mlango na akawaambia:Hakaika Muhammad ametuma kwangu ujumbe ananipa habari ya kuchagua moja kati ya mambo,Ima nisilimu nanibakie na ufalme wangu au nimtumie kodi,au nitoe idhini ya kupigana vita,na kwa hakika mtakuta kwenye ujumbe mliopewa kuwa yeye atamiliki kila kilicho chini yangu miongoni mwa ufalme wangu basi wakaguna kwa pamoja na mpaka baaadhi yao wakatoa kofia zao na wakasema: Sisi tunatuma Kodi kwa mtu atokanae na waarabu amekuja na mashuka yake mawili na na makobadhi ?! Hiraqli akasema:Nyamazeni kwa hakika nilitaka kujuwa msimamo katika dini yenu na mapenzi yenu katika hiyo dini.(686)

Na huenda huu ukawa ni mtihani wa pili toka kwa Hiraqli katika kujaribu kwake kuweza kuwajibu viongozi wa Waroma kwa niaba ya

Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na alipoona wamekataa akawazindua wafalme na ulimwengu juu ya Amri ya ALLAH na Dini yake.

Na Riwaya zitaja kuwa matokeo ya hayo yaliyojiri ,alifika mjumbe wa Hiraqli kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-wakati wa kukaa kwake kwenye kambi yake huko Tabuuk ,na kwa hakika amaepokea Imam Ahmad katika Musnadi yake Hadithi ndefu kutoka kwa Naswara wa Kiarabu ambaye alitumwa na Hiraqli kwenda kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- katika mji wa Tabuuk Anuani ya Ujumbe ilikuwa ((Hadithi ya Tanuugh kutoka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- amesema mpokezi katika hadithi hiyo:)) Nilimkuta Tanuukh mjumbe wa Hiraqli kwa mtume wa ALLAH-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na alikuwa jirani yangu na ni Mzee amefikia ukongwe(687) au kakaribia ukongwe ,basi nikamwambia:hivi hunipi habari kuhusu ujumbe wa Hiraqli kwenda kwa mtume na ujumbe wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwenda kwa Hiraqli?akasema kwanini nisikupe;alifika Mtume Tabuuk na akamtuma Dahiyat Al-kilabiy kwa Hiraqli,na ulipo mjia ujumbe wa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-aliwaita makasisi wa Roma na washauri wake kisha akajifungia pamoja nao mlango na akasema: kwa hakika huyu mtu amefikia sehemu ambayo mumeiona ,na kwa hakika amenitumia ujumbe akiniita kwenye mambo matatu:amaeniita kwenye kuifuata dini yake ,au tumpe mali yetu itokanayo na Ardhi yetu na Ardhi ibakie kuwa yetu,au tuingie nae vitani,Namuapia Mwenyezi mungu hakika mnajuwa kwa mujibu mnavyosoma vitabu kwa hakika atachukuwa kilakilicho chini ya umiliki wangu,basi fanyeni hima njooni tumfuate katika dini yake,au tumpe mali yetu itokanayo na Ardhi yetu,basi wakaguna kwa sauti ya pamoja mpaka wakatoa kofia zaona wakasema ,na wakasema : hivi unatulingania tuuwache unaswara wetu na tufuate dini ya unaswara ili tuwe watumwa wa Bedui aliyekuja kutoka kutoka Hijaz,na alipodhani kuwa wao wakitoka kwake watakuwa

wameichafua Roma akawa mpole na kuwatuliza (688)na akasema kwa hakika mimi nimewaambieni hilo ili ni juwe msimamao wenu katika jambo lenu ,kisha akamwita mtu miongoni mwa waarabu atokanae na kabila la Kindat,alikuwa mkristo wa kiarabu,akasema:Niitie mtu ambae anaweza kuhifadhi maneno mwenye kujuwa lugha ya kiarabu ili nimtume kwa huyu mtu na majibu ya ujumbe wake,basi akaja nami na akanipa Hiraqli ujumbe,na akasema:nenda na ujumbe huu kwa huyu mtu na wala usipotezechochote katka maneno yake na unihifadhie kutoka kwake mambo matatu,je atataja chochote kilichokuwa kimeandikwa kwenye ujumbe wake?na angalia atakapo soma ujumbe wangu je atautaja usiku? na angalia mgongoni mwake je kuna kitu chochote kinachokutia mashaka? basi nikaondoka na ujumbe wake mpaka nikafika Tabuuk mara nikamkuta yeye akiwa amekaa baina yao amekaa kitako kwenye maji na akasema: yuko wapi mtu wenu,yule pale ndiyo yeye,nikageuka nikimwendea mpaka nikakaa mbele yake basi nikampa ujumbe wangu na akauweka kwenye mapaja yake kisha akasema :wewe umekuja kutoka kwa nani? nikasema mimi ni mmoja wa miongoni mwa kabila la Tanuukh,akasema:Je wewe katika uislamu unaitakasa mila ya babayako Ibraahim,nikasema mimi ni mjumbe wa watu wangu nipo kwenye dini ya watu wangu na siwezi kutoka katika dini ya watu wangu mpaka nirudi kwao,basi akacheka Mtume na akasema:(Kwa hakika wewe huwezi kumuongoa umtaka lakini Mwenyezi Mungu humuongoza amtaka nayeye ni mwenye kuwajuwa waongofu,)Ewe Ndugu ya Tanuukh kwa hakika mimi niliandika ujumbe kwenda kwa Kisra na akauchana ujumbe,na mwenyezi mungu atauchanachana ufalme wake,na nikamuandikia Najashiy Gazeti akaliteketeza na mwenyezi Mungu akamteketeza(689) na akautekeza ufalme wake ,na nikamwandikia mtu wako gazeti akalichukuwa basi watu hawatopatwa na ubaya wowote muda wa kuwa kwenye maisha kuna Kheri)ni kasema haya ndiyo moja ya mambo matatu ambayo aliniusia mtu wangu na nikachukuwa mshale na kwenye Ala yake nikayaandika maneno

hayo kwenye ngozi ya upanga wangu,kisha hakika yeye alimpa mtu aliyekuwa upande wake wa kushoto ,nikasema:Ni nani mwenye kuwasomea ujumbe wenu wakasema:Ni Muawiya mara Ghafila nikaona katika ujumbe wa mtu wangu;ujumbe uki niita kwenye pepo ambayo upana wake ni mbingu na Ardhi imeandaliwa kwa ajili ya wacha mungu ,uko wapi Moto?Basi akasema mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-Sub-haanallah ,utauona wapi usiku ikiwa mchana upo?akasema nikauchukuwa mshale wangu kutoka katika Ala yake nikaandika katika ngozi ya upanga wangu na alipomaliza kuusoma ujumbe wangu akaniambia: hakika wewe upo katika haki na wewe ni mjumbe,Na lau ningepata zawadi ningekupa lakini sisi ni wasafiri tumeishiwa na matumizi ya safari,akasema:Basi kuna mtu mmoja kati yao akasema:mimi ninampa zawadi,basi akafunguwa mizigo yake mara akaja na pambo kutoka Palestina basi akaliweka juu ya mapaja yangu nikasema:(690)

Na kwa inavyofahamika ni kuwepo kwa idadi kubwa ya ujumbe uliokuwa ukitumwa baina ya Mtume na Hiraqli,na lilikua mashuhuri jina la Dahiyat Al-kalbiy kama mbebaji wa ujumbe wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na mwenyekujibu Hiraqli(691)na kumetajwa kuwa Dahiyat alibeba ujumbe kwenda kwa Hiraqli kwenye mwisho wa uhai wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na alaikuwa Hiraqli ni mwenye kuzingazinga katika kumjibu mtume mpaka ikamjia habari ya kifo cha mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-(692)

Na kwa hakika aliishi Hiraqli baada ya hapo mpaka akaona yeye mwenyewe sehemu kubwa ya ufalme wake unaangukia katika mji Sham na katika mji wa Palestina na baitil Maqdis na haswa kwenye mikono ya waislamu,na akasadikisha maneno yake kuwa atamiliki yaliyokuwa chini ya miguu yangu hii,basi mwanzo ukawa ni katika utawala wa Abuubakar ,na ukakamilika katika utawala wa Omar baada yake-Radhi za Allah ziwe juu yao- pale ambapo Hiraqli aliipata hasara akiwa anatoka katika Ardhi ya Sham hali ya kuuwaachia ardhi

hiyo waislamu ambao waliichukuwa Ardhi hiyo kwa nguvu hali ya kuiaga moja kwamoja "Amani iwe juu yako ewe Ardhi ya Sirya,pokea sauti ya kuagwa kwa hataonana tena baada ya leo'(693)

na kwa hakika kumetajwa kuwa Hiraqli aliuhufadhi ujumbe wa Mtume-Rehema na mani ziwe juu yake-na akausia kuuhifadhi huo ujumbe baada yake ,na mpaka sasa wafalme wa Roma hawajaacha kupeana kwa kila karne,na walikuwa wakiuonyesha kwa baadhi ya waislamu katika wajumbe wa makhalifa na Watawala,(694) na kwa hakika ilipatikana Nakala halisi ya huu ujumbe wa mtume na ukafanyiwa Uchunguzi na ikapitishwa kuwa ni Nakala Asili.(695)

Ujumbe wake kwenda kwa Kisra:(696)

Fursi ni Dola yenye nguvu,imeshikana na Miji ya kiarabu iliweka utawala wake katika baadhi ya sehemu ndani ya Kisiwa cha waarabu,katika nyakati tofauti tofauti,na haswa katika mji wa Yemen na Bahrain,

Na kwa hakika dola hiyo ilipitia Awamu tofautitofauti za kimaendeleo ,Hapa kinachotuhusu zaidi ni miaka ambayo imetangulia kusuguana na hii Dola ya kiislamu kwa njia ya Daawa na ukombozi na kupigana Jihad,na zilikuwa Dini ni zenye nguvu katika Dola ya Kifursi na sehemu ambazo zilikuwa chini ya utii wake nazo ni za kimajusi,nazo ni Dini ambazo zilizo simamishwa kwa kuabudu Moto na kuutukuza, kama ambavyo palikuwa na Dini Nyingine kama vile Uyahudi na Unaswara,dini ambazo zilienea baina ya Waarabu waliokuwa chini ya hizo Dini katika miji ya Iraq na Bahrain na miji mingine.

Na ilikuwa hii Dola ikiitawala mji waFursi na khurasan na Iraq na baadhi ya sehemu katika pembe za Uarabuni kwa upande wake mwa mashariki na Magharibi.

Na kwa hakika ilisimama nidhamu ya Hukumu ya Fursi kwa Nidhamu ya kifalme na kidhalimu,ikisimamia kuwatofautisha watu

na kuwagawa kwa matabaka mbalimbali,kila tabaka lina mipaka maalumu katika haki,Ubora na Majukumu.(697)

Na Kisra ambaye aliishi zama za Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na akamuandikia Ujumbe ni Kisra aitwae(Abrawiiz) na anakusudiwa Al-mudhaffar naye ni mtoto wa Hurmuz wa Nne mjukuu wa Kisra wa Kwanza ajulikanae kwa jina la (Anu Sharawan) alifika hatua ambayo waliopita hawakufikia hatua hiyo ya kuitetemesha dola ambayo inashindana na Roma (Bizintwiin)ulifikia ushindi wake na utukufu wake kwenye mwaka wa 615 miladia.

Na baada ya Sulhu ya Hudaibiyat ulikuwa miongoni mwa ujumbe ambao aliutuma Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-kwa wakubwa na wafalme ni ujumbe kwenda kwa Kisra,ujumbe uliopelekwa na Abdillah Bin Hudhaafah Al-suhamiy,(698)akamuamrisha aupeleke kwa mtukufu wa Bahrain,basi akaupeleka mtukufu wa Bahrain kwa Kisra,na umekuja ujumbe wake mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwa Kisra ukisema: ((Kwa jina la ALLAH mwingi wa huruma Mwenye Kurehemu,kutoka kwa Muhammad kwenda kwa Kisra Mtawala wa Fursi Amani iwe juu ya wenye kufuata uongofuna akamwamini ALLAH na Mtume wake,na akashuhudia kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika wake ,na kuwa Muhammad ni Mja wake na amtume wake,Ninakuita kwa tangazo la ALLAH,kwa hakika mimi ni Mtume wa ALLAH niliyetumwa kwa watu wote ili kumuonya kila aliye hai na wapate onyo makafiri kwa kauli hii,Ingia katika uislamu utasalimika,na ikiwa utakataa basi wewe una dhambi walizonazo Majusi))(699) Na ulipofika ujumbe wa wa Mtume kwa Kisra Abruwiiz na akasomewa kilimpata kiburi na majigambo,na akamchukia Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na akauchana ujumbe wake,na ikawa dua ya mtume dhidi yao ni (awaangamize kila aliyechana ujumbe).(700)na hakuishia hapo kwenye kufanya kibri na kujigambakwake.bali akafikia hatua ya kumuandikia Baadhaan

mtumishi wake aliyopo Yemen-Na Dola ya Fursi ilikuwa na mamlaka katika Nchi ya Yemen tangu mwaka 575 miladia,-(701);(Watume watu wako wawili kwenda kwa huyu mtu huko Hijaz).kwa lengo la kumteka mtume na kuja nae ili amuadhibu anavyotaka,basi Baadhan akatuma kwenda Yemen watu wawili wenye Nguvu kwenda kwa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na walipokutana nae akawaambia:nendeni na mje kwangu kesho akasema:na ikamjia Mtume Habari kutoka kutoka Mbinguni:kwa hakika ALLAH amemtenza nguvu kisra kupitia mwanae Shairuwaih na akamuuwa.(703)

Akasema basi akawaita na akawapa habari ,wakasema wote wawili:je wayajuwa uyasemayo?kwa hakika sisi tumekufichia mambo ambayo ni mepesi kuliko haya ,je tuandike kutoka kwako hayo uyasemayo?na tumueleze mfalme Baadhaan?akasema;Ndiyo:mpeni habari kuhusu mimi na mumwambie yeye: hakika Dini yangu nauatawala wangu utafikia kiwango alichofikia Kisra na utaishia kwenye vita vya farasi na Ngamia"na mumwambie:hakika wewe ikiwa utauukubali uislamu nitakupa kila kilicho chini ya mikono yako na umilikiwa watu wako katika vijana kisha nitampa Kharkhara sehemu ambayo ina Dhahabu na Fedha sehemu ambayo alikuwa amepewa na Baadhi ya Wafalme basi wakatoka kwake mpaka wakafika kwa Baadhan wakampa habari basi akasema:Namuapia ALLAH kuwa haya siyo maneno ya Mfalme na mimi naona haya maneno ni ya Nabii kamawanavyosema na yatakuwa mambo kama walivyosema basi na haya yakiwa ni kweli basi huyu ni Nabii aliyetumwa ,na ikiwa kinyume na ilivyosemwa basi tutatoa maoni yetu,na wala hakukaa muda mrefu Baadhani mpaka kuletewa ujumbe kutoka kwa Shairuwaihi:Ama baada ya hayo,kwa hakika mimi nimemuuwa Kisra nasikumuuwa kwa sababu yoyote isipokuwa ni kwa ajili ya kuichukua Fursi,pale alipo halalisha kuwauwa watawala wao na kuwawauwa wakiwa kwenye sehemu zao,na utakapo kujia ujumbe wangu huu

basi Nitiikama ulivyokuwa unamtii aliyetangulia kabla yako,na uende mpaka kwa mtu ambaye Kisra alikuwa amemwandikia ujumbe na wala usimsemeshe chochote mpaka ikujie Amri yangu katika hilo.

Na ulipofika ujumbe wa Shairuwaihi kwa Baadhan akasema:Kwa hakika huyu mtu ni Mtume wa ALLAH basi wakashilimu watoto wa kifursi miongoni mwa waliokuwa Yemen ,akasema na kwa hakika Baadhawaihi alimwambia Baadhan ,sikuwa kumsemesha yeyote nakawa namuogopa kama yeye,akasema kwa kumuuliza vipi ana askari? akasema hapana (704)

(705)Mwaka wa Tisa Hijiria.

Na kwa hakika imepokewa kuwa MtumeRehema na amani ziwe juu yake- amesema: ((Ikiwa ataangamia Kisra basi hakuna Kisra baada yake,na akiangamia Qiswar basi hapatakuwepo na Qaiswar baada yake,namuapia yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake watatoa hazina zao katika njia ya Mwenyezi Mungu)(706) Kama anavyotoa ishara Mtume ya kuanguka kwa Madaain mji mkuu wa Fursikwenye mikono ya waislamu katika maneno yake aliposema: Kundi la waislamu lizifungua Hazina za Kisra katika jumba jeupe)(707)

Zilikuja habari kwa Baadhan na waliokuwa pamoja nae katika wafursikatika mji wa Yemen kwa ajili ya kumuwa Abruwiiz katika usiku ambao aliuelezea Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- imepokelewa kuwa Baadhan alisilimu na akasema(kwa hakika huyu ni Mtume)(708)na ikiwa ni jambo la kweli basi asije akanitangulia kwenye kumuamini mtume yeyote katika Wafalme)basi akasilimu nawakashilimu watotowaliokuwa pamoja naemiongoni mwa wafursi wa Yemen.(709)

Na zinataja Riwaya kuwa yeye alipeleka baadhi ya wajumbe kwenda kwa mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-katika mji wa Madina mwisho wa uhai wake(710)kama ambavyo walikuwa watoto wa Baadhaan na wengine miongoni mwa viongozi wa Fursi katika mji wa Yaman walikuwa na mchango mkubwa katika kuwapa

nguvu viongozi wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Muaadh bin Jabal-Radhi za Allah ziwe juu yake- na wengineo wakati wa kutawala kwao nchi ya Yemen wakimuwakilisha Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**

Kamwa amabavyo walishirikiana kwenye kummaliza murtad Aitwae Al-as-wad Al-isiy Muongo mwenye kudai utume,katika Ukhalifa wa Abuubakar-Radhi zaAllah ziwe juu yake- na wakasimama wao na wanawake zao kwenye kumuua Al-as-wad Al-isiy Muongo,na alikuwa Baadhan ni kiongozi wa hawa watoto.(711)

Na kwa hakika waislamu ukomboaji wao wa miji ya Fursi wakati wa utawala wa Abuubakar swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake-na zilikuwa vita kali zaidi kwao ni vita vya Qaadisiyyat.

Na katika zama za Ukhalifa wa Omar Bin Khatwab-Radhi za Allah ziwe juu yake na kabla ya vita vya Qaadisiyyat Rustum alitaka ujumbe wa waislamu ili aje awasikilize na kufanya nao mjadala,na ili awasikie yeye mwenyewe moja kwa moja,na akawa miongoni mwa wajumbe ni Rib-iyyu ambaye alipata umaarufu kama mjumbe aliyewawakilisha waislamu katika moja ya vikao,pale ambapo Rustum alijiandaa kukutana nae ,na akaandaa sehemu yake ya kifahari kwaajili ya kukutana na akaipamba kwa mito na yenye rangi za Dhahabu na Hariri na akatowa mapambo na vito vya thamani,na akaweka mapambo mbalimbali,na akatandika busati lilodariziwa kwa Dhahabu na na Fedha ,basi akakaa Rustum katika juu ya kitanda chake kilichotengenezwa kwa Dhahabu,basi Rib-iyyu Bin Aamir akafika kwenye kikao cha Rustum akiwa amevaa mavazi yaliyochakaa na yenye viraka na akiwa amaebeba silaha kwa unyenyekevuna amepanda Farasi mdogo,na alaihofika katika sehemu ya Rustum ya kufanyia kikao akaingia na Farasi wake sehemu ya kikao na akakanyaga mapambo na hariri,kisha akang'oa sehemu ya ile Hariri na akamfungia nayo Farasi wake,na akamgeukia

Rustum akiwa na silaha yake,waFursi wakamwambia weka chini Silaha yako,akasema:Mimi sikuwajieni mwenyewe bali nyinyi ndiyo mlioniita ,na ikiwa mtaniacha hivi nilivyo basi ni vizuri lakini ikiwa tofauti na hivyo mimi nitarudi,basi Rustum akawaamrisha wamuwache alivyo,basi akamwelekea Rustum akiwa ameegemea mkuki wake juu Busati na mitompaka akatoboa sehemu katika hilo Busati,Rustum akamwambia:mmekuja na jambo gani?Rib-iyuu akasema kwa hakika Mwenyezi Mungu ametutuma tuwatowe awatakao kwenye kuabudu waja na badala yake wamuubudu mwenyezi Munguna kuwatoa kwenye dhiki ya Dunia ya kuwaweka kwenye sehemu iliyo pana,na kuwatoa kwenye dini za kijeuri na kuwaweka kwenye dini ya uislamu yenye uadilifu,basi akatutuma na dini yake ili tuwalinganie katika dini hiyo,basi yule atakae kubali dini hiyo nasisi tutamkubalia na tunamuacha,na atakae kataa tutapigana nae milele mpaka tupate kile alichotuahidi Mwenyezi Mungu,akasema Rustum,na Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni nini?akasema Rib-iyuu Ni Pepo kwa yule aliyekufa kwa ajili ya kupambana na aliyekataa ,na ushindi utakuwa kwa yule aliyebakia.Akasema RustumJe mwaweza kulichelewesha jambo hili mpaka tumalize kushauriana?akasema Rib-iyuu naam inawezekana tuwasubiaria siku tatu,basi Rustum akataka wazidishiwe masiku akasema ,hajatuwekea Mtume utaratibu wa kumsubiria Adui zaidi ya siku tatu adui tukisha kutana naye, Rustum akamwambia je wewe ndiye mkubwa wao?akasema hapana,lakini waislamu ni kama mwili mmoja wa chini wanawahami walio juu,basi Rustum akawakusanya majemedari wake baada ya hapo na wakajadiliana kuhusu jambo hili,na wakakubaliana kupigana vita na waislamu,na wasikubalie kuwatangazia uislamu wala kutowa Jiz-ya,basi makundi mawili yakajiandaa kupigana,na kwa hakika viliumana vita baina ya waislamu na wafursi kwenye vita iliyokuwa chungu,vita vikaisha kwa waislamu kushinda (712) kilichofuata ni kuanguka kwa mji mkuu wao(713)

Na yakatokea yale aliyoyatolea habari mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuanguka utawala wa Kisra na dola yake pamoja na Hazina zake,baada ya kufanya jeuri zake na kukataa kwake ujumbe wa mtume na kuuchana kwa takriba miaka tisa ,kama amabvyo Salman Al-Farisiy-Radhi za Allah ziwe juu yake- alikuwa ni kiongozi wa miji baada ya kuikombowa katika kipindi cha Omar-Radhi za allah ziwe juu yake-na alikuwa akiuwakilisha uislamu mbele ya waFursi kwa unyenyekevu wake na uchamungu wake na muamala wake ulio mzuri na watu,na akawa yeye na wenzake miongoni mwa maswahaba wana Athari kubwa katika kuenea uislamu baina ya wafursi.

Ujumbe wake kwenda kwa muqauqis(mtawala wa kabila la Qibtwiya katika Nchi za Misri):

Mji wa Misri ulikuwa Mash-huur kimaendeleo tangu zamani,na kwa hakika utajo wake umekuja kwenye Qur'an tukufu zaidi ya mara moja ,miongoni mwa kutajwa kwake ni katika kisa cha Yusuf-Juu yake Amani-katika maneno ALLAH Mtukufu:

﴿وَقَالَ الَّذِي اشْتَرَاهُ مِنْ مِصْرَ لِمَرْأَتِهِ أَكْرِمِي مَثْوَاهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا
وَكَذَٰلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ وَلِنُعَلِّمَهُ مِن تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ وَاللَّهُ غَالِبٌ عَلَىٰ أَمْرِهِ وَلَكِنَّ
أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢١﴾﴾ [يوسف: 21]

Na akasema yule aliye mnunua-nabii yusuph-kutoka misri kumwambia mke wake heshimu nafasi yake huwenda akatufaa au tuta mfanya kuwa mtoto na hivyo ndivyo tulivyp mueka yusuph katika ardhi na ili tumfundishe kutoa tafsiri ya ndoto na ALLAH ni mshindi wa jambo lake isipokuwa watu wengi hawafahamu. Yusuf :21 Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَىٰ يُوسُفَ ءَاوَىٰ إِلَيْهِ أَبَوَيْهِ وَقَالَ ادْخُلُوا مِصْرَ إِن شَاءَ اللَّهُ ءَامِنِينَ ﴿٩٩﴾﴾
[يوسف: 99]

walipo ingia kwa yusuph aliwapokea baba zake na akasema ingieni misri akipenda ALLAH mtakuwa ni wenye amani. Yusuf:99 Kama ilivyokuja kwa urefu mazungumzo kuhusu maisha ya Nabii Mussa-juu yake Amani-na kisa chake pamoja na Firauni na akatajwa kwa jina lake katika Qur'an tukufu kwa ulimi wa Firaun.

﴿وَنَادَى فِرْعَوْنُ فِي قَوْمِهِ قَالَ يَا قَوْمِ أَلَيْسَ لِي مُلْكُ مِصْرَ وَهَذِهِ الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِن تَحْتِي ۗ أَفَلَا تُبْصِرُونَ﴾ [الزخرف: 51]

Na firauni akawaita watu wake akasema enyi watu hivi ufalme wa misri sio wangu na hii mito inayo pita chini yangu hivi amuoni. Al-Zukhrufu:51) Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ وَأَخِيهِ أَنْ تَبَوَّءَا لِقَوْمِكُمَا بِمِصْرَ بُيُوتًا وَاجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قِبْلَةً وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ﴾ [يونس: 87]

Na tukamfunulia musa na ndugu yake ya kwamba jengeni kwa watu wenu kwenye mji wa misr majumba na mukeke kwenye majumba yenu qibla na msimamishe swala na uwape bishara njema waumini. Yunus:87), Kama ilivyokuja simulizi kuhusu yeye kwenye Aya nyingi pasina kumtaja jina lake moja kwa moja (714)

Na kwa Hakika imethibiti kuwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-alitoa habari zaidi ya mara moja kluwa Masri itakombolewa kwa ajili ya waislamu,na miongoni mwa kauli yake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ((Kwa hakika mtaufunguwa mji wa misri nayo ni Ardhi huitwa Qiiraatwi,Basi ninawausia muwafanyie watu wake wema,kwani wana Amana walizo nazo na wana Nasaba))(715)

Na alikuwa akiongoza Misri Al-Muqauqis (Cyrus) kwa warum,naye alikwa mtu wa Dini kwenye Madhehebu ya Costantino,mwenye asili ya Yunani,alikuwa kiongozi wa Misri kwa upande wa Hiraqli,na ni Askofu wa Alexandra wakati huohuo.(716)

walikuwa wakazi wa Misri wakati wa kutumwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ni katika kabila la Qitwiya na wao ndiyo wenye mji wa asili,wanachanganyikana na kundi kubwa litokanalo na warumi(717) na miongoni mwao ni muqauqisi na wao walikuwa kwenye madhehebu moja na Wakiristo,na ilikuwa madhehebu ya Qibtwi ndiyo madhehebu ya(Monotheloma) Unaswara na wanatofautiana na madhehebu iliyoenea katika mji wa Costantino na baina ya Roma ,nayo ni madhehebu yaitwayo (Monophusitai)(718)

Na kuna jambo lipo tofauti kati ya madhebu mbili ,jambo ambalo lilipelekea waroma kuwadhikisha Idadi kubwa ya watu wa Dini ya Qibtwiya na kuwaweka mbali(719)na wakati aliporudi mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kutoka katika Sulhu ya Hudaibiyat aliandika ujumbe kwenda kwa Al-muqauqis mtawala wa Qibtwiya,naye alikuwa ni Hakimu wa Misri na Askofu wake kwa upande waa Roma,na ikaja kwenye ujumbe imeandikwa hivi((Kwa jina la ALLAH mwingi wa Rehma Mwenye Kurehemu,ujumbe kutoka kwa Muhammad mja wa ALLAH na Mtume wake kwenda kwa Muqauqis mtawala waQibtwia,Amani iwe kwa mwenye kufuata uongofu,Ama baada ya kusema hayo:Kwa hakika mimi nakulingania kwa wito wa uislamu,Jisalimishe utasalimika atakupaa ALLAH malipo yako mara mbili,na ikiwa utakengeuka basi una madhambi waliokuwa nayo Waqtwiya))

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾﴾

[آل عمران: 64]

Enyi mayahud na manaswara njooni kwenye neno la sawa sawa baina yetu na nyie tusimuabudu isipokuwa ALLAH na wala tusimshirikishe na kitu chochote na wala tusiwafanye baadhi kuwa ni miungu kinyume na ALLAH basi mkienda kinyume semeni

shuhudieni kuwa sisi ni waislamu. Surat [Al-Imran: 64]. Na kwa hakika Mtume alimchaguwa Haatib Bin Abii Baltah aubebe ujumbe(721) na kwa hakika aliweza kufika kwa Muqauqis na akampa ujumbe wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,na akamkirimu,na alikuwa ni Askofu basi akawakusanya viongozina wakajaribu kujadili na kumpa hoja Hatwib Bin Abii Bal-tah,na kwenye hilo kauli yake ikawa,ikiwa yeye ni Nabii basi kwa nini watu wake hakuwaombea dua mbaya walipomtoa kwenye mji wake kwenda mji mwengine,basi Hatwib akamjibu akamwambia:Na Issa ilikuwaje pale watu wake walipomchukuwa na wakataka kumsulubisha kwanini hakuwaombea Dua mabaya ili ALLAH awaangamize kabla hamja mnyenyuwa kumpeleka katika uwingu wa Dunia,basi akamwambia,wewe ni hakimu,kwa hakika amekuja kutoka kwa hakimu,kisha akajibu ujumbe wa mtume hakutaja ndani ya ujumbe huo kusilimu kwake,pamoja na kuwa yeye alifahamu kitu ambacho Mtume alichomlingania kwacho na kimemekuja kwenye ujumbe wake: Ujumbe wa Muhammad kutoka kwa Muqauqis mtawala wa Qib-twiw Amani iwe juu yako,Ama baada ya hayo,kwa hakika nimeusoma ujumbe wako na nimeelewa kilichotajwa humo na unacholingania ,na kwa hakika nimetambua kuwa Mtume kwa hakika yupo,na nilikuwa nadhania yupo Sham ,na kwa hakika nimemkirimu mjumbe wakona nimekutumia Mabinti wawili ambao wana vyeo katika kabila la Qibtiya,napia nimekuzawadia Nyumbu utakaekwa unampanda na amani iwe juu yako).(722) Na kama ilivyo wazi ni kuwa majibizano ya Muqauqis kwa Haatwib yalikuwa ni zaidi ya mara moja,na kumkinaisha kuhusu Unabii wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na kuwa maswahaba wake watakika Misri na watautangaza huo Unabii.(723)

Na miongoni mwa vilivyotumwa pamoja Haatib Bin Baltah miongoni mwa Zawadi kwenda kwa Mtume wa ALLAH ambaye ni Maria Al-Qibtwiyyat ambaye alikuja akawa Mama ya Ibrahiim Mtoto

wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-pamoja na Binti mwingine(724)na vilevile kijna mweusi na Khafu mbili na viatu.

Na ilivyo wazi inaonyesha katika ujumbe wa Muqauqis ni heshima yake kwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kumtambuwa kuwa Nabii wa Mwisho na wa mwisho wao,na wala ujumbe haukuonyesha uislamu wake pamoja na yeye kuijuwa haki na huenda yeye alifadhilisha maisha ya dunia na vyeo na ufalme kuliko Dini na Akhera,na akafuata njia ya Hiraqli kwenye kuijuwa haki na kuipinga,na alikuwa na uhakika kuwa waislamu wataichukuwa Misri na kuikombowa,kama walivyokuwa na yaqini na jambo hilo,na hayo ndiyo yaliyotokea kwenye maisha ya Muqauqis mwenyewe.

Na katika mwaka wa 20Hijiria,Aliondoka Amrou Bin Al-Aaswi.(725)

katika hali ya kuikomboa nchi ya Misri,na Muqauqis alipomuuliza Al-muqauqis kuhusu tabia za waislamuakamwambia,hawa waislamu lau wangetaka kupambana na mlima wangeweza kuuondoa.(726)

Na akahisi nguvu za waislamu na nusura ya ALLAH kwaobasi akasuluhishana nao na akatoa Jiz-ya.(727)

Jumbe zake kwa wafalme wa Habasha :

Habasha ni sehemu iliyopo Afrika mashariki ikielekeana na pwani ya Yemen ,na kwa hakika mipaka yake imekuwa ikitofautiana kutoka zama kwenda zama nyingine ,na sahihi ni kuwa Habasha ilikuwa katika zama za Mtume inakusanya sehemu za Somalia na Sudan na miji mingine na zamani ilikuwa ikiitwa(Apyssinia) nakwa sasa inaitwa (Ethiopia) na Dola ilikuwa ikijulikana tangu zama za Nabii Sulaiman-juu yake amani-nakwa hakika umeenea humo Ukiristo katika karne ya Nne tangu kuzaliwa kwa masihi,na wakaweza kuitawala nchi ya Yemen mwaka 525.kwa muda ambao unakadiriwa miaka khamsin na ulikuwa mji wake mkuu(Axum).(728)

Na mausiano ya watu wa Makkah na Habasha yalikuwa kabla ya kutumwa Mtume-Sala na amni ziwe juu yake-pale ambapo ilikuwa ni sehemu ya Biashara ya maquraish walikuwa wakileta na kuchukuwa Bidhaa,na kwa hakika wahabashi waliuteka mji wa Yemen na wakautawala na wakauhukumu Kabla kidogo ya kuzaliwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na wakawa wanagombania kuutawala wao pamoja na wafursi,na alikuwa Abrahah ni Muhabesh alikuwa ni kiongozi Mashuhuri katika mji wa Yemen,na yeye ndiye alikuwa mwenye msafara wa Tembo waliotaka kuibomoa Al-kaaba na ambaye iliteremka kwake neno la ALLAH mtukufu:

﴿أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ۗ أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي تَضْلِيلٍ ۗ وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ۖ تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ۗ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ﴾ [الفيل: 1-5]

Je umepata kuona namna MOLA wako alivyo wafanya watu wa ndovu. Hivi akujalia vitimbi vyao kuwa ni katika upotevu "Na Aliwapelekea makundi ya ndege yaliyofuatana," wakiwatupia wao vijiwe vya udongo mkavu mgumu." Akawafanyani kama majani makavu yaliyoliwa na wanyama na halafu kutupwa." AL-FIL: 1-5(729)

Na alipoudhiwa Mtume na maswahaba wake katika mji wa Makka ,aliwaelekeza maswahaba wake wahamie Habasha,(730)na akawapa habari ya uadilifu wa mfalme wa Habasha,ambae alikuwa akiitwa kwa Waarabu kwa jina la Najaashiy ,nalo ni jina la kila mfalme wa Habasha,na Mfalme wa wakati huo alikuwa ni Asw-hamat,na walikuwa wa kwanza kuhamia Habash ni JaafarBin Abii Twaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-na kwa hakika Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- alituma ujumbe kwenda kwa Najaashiy mfalme wa Habash ujumbe ambao ndani yake kulikuwa na maneno haya: ((Kwa jina la ALLAH mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu,kutoka kwa Muhammad mtume wa ALLAH kwenda kwa Najaashiy Al-asw-hamat mfalme wa Habasha Amani iwe juu

yakoKwa hakika mimi namshukuru ALLAH aliyekupa Neema mwenye kumiliki mtakatifu mwenye amani mwenye kutawalia mambo yote,na naninashuhudia kuwa Issa Bin Maryam ni Rehema ya ALLAH na nineno lake ambalo aliliweka kwa maryam aliyekuwa Bikra Msafi mwenye kujihifadhi,basi Akamzaa Issa na akamuumba kwa kumpa uhai utakao kwake,na kumpulizia kwake,kama alivyomuumba Adam kwa mikono yake na kumpulizia roho itokayo kwakwe,kwa hakika mimi nakulingania kwa ALLAH peke yake hana mshirika wake ,na kumpenda kwa ajili ya Kumtwii yeye,na kunifuata mimi na nakuamini yale ambayo yameletwa kwangu,kwa hakika mimi ni Mtume wa ALLAH,na kwa hakika nimeemtuma mtoto wa Baba yangu Mdogo pamoja nae kuna kundi la waislamu,basi wakikufikia wapokee na usiwe mwenye kiburi,kwa hakika mimi nakuita wewe na Jeshi lako kwenye moto wa ALLAH-mwenye nguvu na utukufu-kwa hakika nimefikisha na nimetoa nasaha,basi kubali nasaha zangu na Amani iwe juu ya kila mwenye kufuata uongofu.))

Na inavyofahamika ni kuwa Barua za Mtume zilikuwa zinatofautiana usulubu wake na Barua ambazo zilikuwa zikitumwa kwa watawala,pale ambapo ilibainika ndani ya Barua hizo kulikuwa na usemeshwaji maalumu kwa mtu mwenye Imani kwa kile alichokuja nacho Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kwa hakikani kuwa Najashiy Asw-hamat alijadiliana na JaafarBin Abii Twaalibna-Radhi zaAllah ziwe juu yake-mara nyingi miongoni mwazo ni pale alipofika na Ujumbe utokanao na Maquraishi wakimtaka kumrudisha Jaafar Bin Abii twalib na waliokuwa pamoja nae miongoni mwa muhaajiriina basi Asw-hamat akaweka kikao cha kujadiliana na akawasikiliza na pia akausikiliza ujumbe wa Maquraish,na matokeo ya Mjadala ukaonyesha kulemea Najaashiy kwenye haki na Uislamu(732) na kujiandaa kwake kuwahami Muhaajiriina miongoni mwa maswahaba,na kwa hakika Najaashiy alipokea Barua ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na

akautangaza uislamu wake kwenye mikono ya Jaafar bin Abii twaalib na miongoni mwa yaliyokuja kwenye barua ya Najaashiy ni haya:

Kwa jina la ALLAH mwingi wa Sala mwenye kurehemu kwenda ka Muhammad mtume wa ALLAH,kutoka kwa Najaashiy Asw-hamat,Amni iwe juu yako ewe mtume wa ALLAH kutoka kwa ALLAH na Sala na Baraka zake,ALLAH ambaye hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila yeye,ama baada ya kusema hayo,kwa hakika umenifikia ujumbe wakoewe mtume wa ALLAH katika mambo uliyoyataja kuhusu Issa ,uliyoyataja yapo sambamba kama ilivyo kokwa ya tende ilivyoshikana na ngozi yake(733)kwa hakika ni sahihi kama ulivyotaja,na tumefahamu ulichotumwa nacho kwenu na kwa hakika tulikuwa karibu na mtoto wa baba yako mdogo na wenzake,basi mimi nashuhudia kuwa wewe ni Mtume wa ALLAH uliye mkweli mwenye kusadikishwa,kwa hakika nimekuunga mkono,na nimemuunga mkono mtoto wa Baba yako mdogo,na nimesilimu kwenye mikono yakekwa ajili ya ALLAH mola wa viumbe vyote)(734)

Na walikuwa maswahaba kwa mfalme wa habash ni wenye kukirimiwa na wenye kupendwa kwa mfalme,na imepokelewa Riwaya mbalimbali zinazo julisha kuwa yeye Najaashiy aliingia katika Uislamu,na alikuwa yeye na Maswahaba wana vikao vingi katika vikao hivyo waliona kila jambo la kheri.

Na kwa hakika Imethibiti kuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alituma Barua kwa mfalme wa Habasha Asw-hamat,na huenda huyo ni wa pili,na anatofautiana na wa kwanza ,na alibeba ujumbe Amrou Bin Umaiyyat Al- Dhwamriy kwenye mwaka wa sita tokea kuhama mtume na ujumbe ulikuja na ndani yake kuna haya: ((Kwa jina la ALLAH mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu,kutoka kwa Muhammad mtume wa ALLAH kwenda kwa Najaashiy Al-asw-hamat mfalme wa Habasha Amani iwe juu yakoKwa hakika mimi namshukuru ALLAH aliyekupa Neema mwenye kumiliki mtakatifu

mwenye amani mwenye kutawalia mambo yote,na naninashuhudia kuwa Issa Bin Maryam ni Rehema ya ALLAH na nineno lake ambalo aliliweka kwa maryam aliyekuwa Bikra Msafi mwenye kujihifadhi,basi Akamzaa Issa na akamuumba kwa kumpa uhai utakao kwake,na kumpulizia kwake,kama alivyomuumba Adam kwa mikono yake na kumpulizia roho itokayo kwakwe,kwa hakika mimi nakulingania kwa ALLAH peke yake hana mshirika wake ,na kumpenda kwa ajili ya Kumtwii yeye,na kunifuata mimi na nakuamini yale ambayo yameletwa kwangu,kwa hakika mimi ni Mtume wa ALLAH,na kwa hakika nimemtuma mtoto wa Baba yangu Mdogo pamoja nae kuna kundi la waislamu,basi wakikufikia wapokee na usiwe mwenye kiburi,kwa hakika mimi nakuita wewe na Jeshi lako kwenye wito wa ALLAH-mwenye nguvu na utukufu-kwa hakika nimefikisha na nimetoa nasaha,basi kubali nasaha zangu na Amani iwe juu ya kila mwenye kufuata uongofu.))

Na baada ya Najaashiy kuusoma ujumbe yaliendelea baina ya Najaashiy na Amrou Al-dhumairiy mjadala kuhusu Issa -juu yake amani-na Daawa ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,na yalikuwa miongoni mwa haya majadiliano(Omar alimwambia:Ewe Asw-hamat,mimi nina neno nataka kukwambia ni wajibu juu yako kusikiliza Hakika wewe kama vile una upole kwetu sisi na kana kwamba sisi tunamatumaini na wewe kutoka kwako,kwa sababu sisi hatujawahi kukudhania jambo la kheri hata mara moja isipokuwa tuliipata,na wala watukuwahi kuogopea kwakokitu hata mara moja isipokuwa tulikitafutia usalama,na kwa hakika tumechukua hoja dhidi kutoka kwenye mdomo wako,Injili ipo baina yetu wewe ni Ushahidi tosha na Hakimu asiyedhulumu,na hilo ni jambo la lazima na haki kwa hakika wewe kwa mtume huyu asiyejuwa kusoma wala kuandika ni kama Yahudi kwenye kumuamini Issa Bin Maryam,na kwa hakika mtume-Sala na amani ziwe juu yake-aliwatawanya wajumbe wake kwa watu,akawa na matumaini nawe kuliko alivyokuwa na matumaini nao,na akakuamini kwa jambo ambalo

alipata khofu kwao kutokana na wema uliotangulia na na malipo yanayotarajiwa,basi akasema Najashiy: Nashuhudia kwa ALLAH kuwa yeye ni mtume asiyejuwa kusoma wala kuandika ambaye mayahudi na manaswara wanamgojea,na kuwa Bishara ya Mussa ya mwenye kupanda Punda ni kama Biashara ya Issa kwa mpanda Ngamia(737)na kuwa kushuhudia jambo siyo kama kupewa habari,kisha Najaashiy akaandika jawabu la Ujumbe wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-(737)

Na ujumbe ulielezea na Riwaya zilizobakia zinatila mkazo kuwa kusilimu kwa huyu Najaashiy kulikuwa kwenye mikono ya amrou Bin Umayyat Al-dhwamriy,na kauli yenye nguvu kwangu mimi na kwa wengi kuwa yeye siyo Najaashiy wa Kwanza ambaye Jaafari Bin Abii Twaalib na aliokuwa nao walihamia kwake,na Riwaya zanajulisha kuwa Najaashiy huyu jina lake ni Asw-hamat Bin Ab-hat,na kwa hakika mtu alimuandikia ujumbe akimuamrisha amuozeshe Ummu Habiba Bint Abii sufiyan,pale ambapo Mtume alimchumbia akiwa Habasha wakati ambao mume wake alikuwa ameritadi na amekufa,basi Asw-hamat akafunga Ndoa kwa niaba ya mtume na akatoa mahari yake kwa niaba ya mtume(738)na Riwaya Mbalimbali zinajulisha kuwa Mfalme wa Habasha alituma kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** katika mwaka wa 8 Hijiria,alituma watu kutoka Habasha ,na hao watu waliangamia katika Bahari kabla ya kufika katika mji wa Madina.(739)

Na Kwa hakika Amrou Bin Ummaiyat Al-dhwamriy aliwabeba maswahaba wa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-mpaka Habasha kwa kutumia Safina ,na akarudi madina wakati wa vita vya Khaibar kwenye mwaka wa Sita wa Hijiria,na wakiwa pamoja nae Jaafar Bin Abii Twaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-Basi akawa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-anasema:(Sijui ninafurahishwa na jambo gani,nafurahishwa kwa kuukomboza mji wa haibar au kuja kwa Jaafar?) na hapana shaka mpangilio wa safari yao ya kwenda na kurudi kwao ulikuwa ni wa Mtume-Sala na amani ziwe

juu yake- na Dhamana ya safari ilikuwa kwa Najaashiy,na kwa hakika Bin Hishaam aliwahesabu hawa Wahamiaji na majina yao na akaandaa kwa ajili hiyo Maudhui maalumu akaiita(Kutaja ujio wa Jaafar Bin Abii twalib kutoka Habasha na mazungumzo ya muhaajirina kwenda Habasha)(740)

Na zimejulisha Riwaya nyingi zilizo sahihi kwa Bukhari na Muslimna wengineo kuwa mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alimswalia Najaashiy swala ya Mbali alipo fariki,(741) pamoja na kutofautiana wakati wake,na hili tukio linajulisha kusilimu kwake,na ilivyo sahihi kwa maulamaa wengi,ni kuwa yeye alikuwa akiuficha uislamu wake ,na kuenda huyu ndiye Najaashiy wa kwanza ambaye alimpokea Jaafar Bin Abii twaalib na aaliokuwa nao miongoni mwa muhaajiriina.

Na wanataja baadhi ya wana Historia kuwa Hiraqli alijuwa kusilimu kwa Najaashiy,na alikuwa akiimpa msaada wa Mali kila mwaka,kwa kuangalia mafungamano yakeya kidini na kiidara kwenye Dola ya Roma,Basi Hiraqli akaukata hiyo misaada.(742)

Ujumbe wake kwenda kwa Huudhat Bin Ally Al-Hanafiy katika mji wa (Yamaamah):

Al-Yamaamah Ni mkoa maarufu katika mji wa Najdi,na huuitwa Al-Uruudh au Al-Aaridh,na msingi wake ni jiwe mpaka upande wa Magharibi kutokea Bahrain,na nimashuhuri kwa vijiji vingi katika Bonde la Hanafiyat ambapo ni Riyaadh ya sasa na pambazoni mwake kwa sasa-nayo ni sehemu ambayo una uzalishaji utokanao na kilimo,na katika wakati wa Mtume ilikuwa nisehemu ambayo huzalishwa Ngano na kuzipeleka Makkah na sehemu nyingine.(743)

Palikuwa katika mji wa Yamaamah watu mbalimbali wa mjini na wakuu tofauti tofauti,na makabila yenye vyeo,na Al-yamaamah ilikuwa mashuhuri kwa chemchem zake na miti yake ya Mitende.(744)

Na lilikuwa kabila lake maarufu ni Banii Haniifah na mipaka ya jiwe lake la msingini Aqribaa, (Karibu na Uyainah) (745) na katika watu Mashuhuri waliosilimu miongoni mwa wakubwa wake, (Thumaamat Bin Athaal) katika kisa mashuhuri, (746) na alikuwa miongoni mwa viongozi wake Mash-huur (746) pale alipozuilika kuzalisha Ngano na kuzipeleka kwa Maquraish baada ya kusilimu kwake, basi watu wa Makkah wakataka uombezi wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ili warudishiwe biashara ya Ngano, na alikuwa mkubwa wao ambaye alikuwa mash-hurni Haudhat Bin Ally Al-Hanafiy ambaye mtume alimuandikia Ujumbe, na alikuwa upande wa anga za Hadhara mauti (Al-kharju) nalaikuwa ni mtawala kwenye kabila la Banii Haniifat, basi mtume -Sala na amani ziwe juu yake- akamwandikia ujumbe kwenye mwaka wa Sita tangu kuhama mtume, ni miongoni mwa walioandikiwa ujumbe miongoni mwa wafalme na viongozi, na ukaja katika ujumbe Kwa jina la ALLAH mwingi wa Mwenye kurehemu, Kutoka kwa Muhammad Mtume wa ALLAH kwenda kwa Haudhat Bin Ally, Amani iwe juu ya Mwenye kufuata uongofu, najuwa ya kuwa Dini yangu itaenea kila sehemu mpaka wapitapo Ngamia na Farasi, Basi silimu utasalimika na nitakumilikisha kila kilichopo chini yako, Na Saliitwi Bin Amrou Al-aamiriy na alipomfikia na Ujumbe uliopigwa Muhuri wa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- alifikia kwake na akamsalimia na akamsomea, akajibu baadhi ya na akaacha baadhi, na akaandika kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ni uzuri ulioje wa unachokilingania, na mimi ni Mshairi wa watu wangu na Khatwiibu wao na waarabu wanakitukuza cheo changu, basi ni baadhi ya maamrishi ili niyatekeleze, na akamuandalia Saliitwi Zawadi na akamvisha Nguo iliyofumwa kifahari, akaenda nayo kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na akampa habari, na akamsomea mtume ujumbe wake, na akasema lau angeniomba kipande kidogo cha Ardhi ni singempa ameangamia na kimeangamia kilichopo mikonono mwake (747) Na kwa hakika (Sulaitwi Bin Amrou Al-aamiriy) aliubeba ujumbe naye ni Swahaba mtukufu ni miongoni

mwa waliohamia Habasha katika Waislamu wa Mwanzo na aliibeba familia yake katika kuhamia Habasha na akapata mtoto akiwa huko.(748)

Na ulipofika Ujumbe kwa Huudhat Bin Ally mbele yake alikuwepo kiongozi wa manaswara wa Damascas ya Sham,basi akamuuliza kuhusu Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na akamuelezea kuhusu ujumbe uliomjia kutoka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na Haudhat akamjibu kuwa yeye anaogopea ufalme wake basi akamwambia: (Ikiwa utamfuata basi atakumilikisha na ilivyo bora kwako ni wewe kumfuata ,kwa hakika yeye ni Nabiiwa Kiarabu ambaye amebashiriwa na Nabii issa ,na kwa hakika yeye ameandikwa kwetu katika Injili kwa jila Muhammad Rasulullah)(749)

Na ilivyowazi ni kuwa msisitizo wa Haudhat Bin Ally wa kutokuukubali uislamu licha ya kutumiwa ujumbe na Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na alipoweka masharti na kuwacha kusilimuMtume akamuomba dua ya maangamivu(Amengamia na vimeangamia alivyovimiliki)na haya ndiyo yaliyotokea baada tu ya kuondoka mtume kutoka katika vita Kwenye Ufunguzi wa Makka((Jibril alimjia Mtume juu yake amani-na kumpa habari kuwa Haudhat amekufa basi akasema Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-ama kwa sasa katika mji wa Yamaamah atatokea Nabii wa uongo atauliwa baada ya kuondoka kwangu)) akasema msemaji:Ewe mtume wa mwenyezi mungu ni nani atakaemuwa? basi mtume akamwambia ni wewe na watu wako))(750)

Na ulipokuja ujumbe wa Banii Haniifat katika mwaka wa tisa tangu kuhama mtume(751) walikuwa pamoja na Musailamatil Kaddhab,ambaye alisema(Ikiwa Muhammad atanipa mamlaka baada yake basi nitamfuata na akawafikishia wengi katika watu wake,akamjia mtume wa ALLAH akiwa pamoja nae Thabit Bin Qais Bin Shimas,na mkonoi mwa Mtume wa ALLAH tawi la mti,mpaka akasimama mbele ya Musailamat akiwa na watu wake

akamwambia:lau ungeniomba kipande hiki cha Tawi nisingekupa na sitokupa kilounachokitaka katika mambo ya ALLAH,na ikiwa utakwenda kinyume basi atakuadhibu ALLAH,na mimi ninakuona kama nilivyokuona ndotonina huyu hapa Thabit atakujibu kwa niaba yangu kisha akaondoka)(752)

Na kwa hakika aliritadi Musailamatul kaddhab na waliokuwa pamojanae katika kabila la banii Haniifat mwisho wa wakati wa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-na akadai utume,na akawa anawahimiza watu kwa maneno yasiyokuwa na maana na akidai kuwa maneno hayo ni Qur'an na akawafitinisha watu kwa maneno hayo na wakamfuata kwa upendeleo wa kikabila mpaka baadhi yao wakawa wanasema(Uondo wa kabila la Rabiit ni bora kuliko ukweli wa kabila la Mudhwar)(753) pale alipodai kuwa yeye wameshirikiana kwenye amri,na akaandika kwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-ujumbe na ndani yake umeandikwa: Ujumbe kutoka kwa Musailamatul mtume wa ALLAH kwenda kwa Mtume Muhammad Mtume wa ALLAH:Amani iwe juu yako,ama baada ya kusema hayo kwa hakika mimi nimeshirikiana mambo pamoja nawe ,na kwa hakika nina haki ya nusu ya Ardhi na Maquraishi wana haki ya Nusu iliyobakia laini maquraishi ni watu wenye kupituka mipaka)(754) Basi Mtume akamjibu na kitika majibu yaliyokuja humo ni haya: ((kwa jina la ALLAH mwingi wa Rehma na mwenye kurehemu,ujumbe kutoka kwa Muhammad,Mtume wa ALLAH,kwenda kwa Musailamatul Kaddhab:Amni iwe juu ya mwenye kufuata uongofu,ama baada ya kusema hayo,nakufahamisha kuwa Ardhi ni ya ALLAH anamrithisha amtakee katika waja wake na mwisho mwema ni wa wacha Mungu))(755)

Kuritadi kulizidi ,na Musailamatu akaandaa jeshi la kupigana na waislamu na kuuvamia mji wa Madina na lilikuwa jeshi la kwanza kutumwa kwake ni kutoka kwa Abuubakar ,jashi likiongozwa na (Ikrimat Bin Abii jahal)-Radhi za Allah ziwe juu yake- na hawakuweza kufanikiwa kukutana na amusailamat kwa mara ya kwanza ,na hivyo

Abuubakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake- akamuelekza (Shurah-bil Bin Hassan) Radhi za Allah ziwe juu yake- kisha Khalid Bin Waliid-Radhi za Allah ziwe juu yake- na akamuamrisha Shurah-bil kuungana na Khalid Bin Al-waliid ,(756) na wakampa nguvu Muhaajirina na wakiwa na Abuu (Hudhaifat) Waziri wa Omar Bin Khattwab -Radhi za Allah ziwe juu yao wawili- na anaebeba Bendera yao ni Salim Mtumwa wa Abuu Hudhaifa-Radhi za Allah ziwe juu yake- na Answaar na wakisaidiwa na Thabit Bin Qais Bin Shimaas - Radhi za Allah ziwe juu yake-na lilipokaribia Jeshi la waislamu ,alijuwa Musailamat na akatoka na majeshi yake kwenda (Aqribaah) na akawaweka Kambini nawakaweza waislamu kulivamia kundi la musailamat,na linakadiriwa kundi hilo kuwa linafikia kati ya watu Arubain mpaka sitini,kisha kakutana na Musailamat na wanajeshi wake.

Na waislamu walikaribia kushindwa ,basi wakaitana waislamu kuwa imara,na mapigano yakawa makali, na mara ya kwanza mapigano yakawa na manufaa kwa upande wa Banii Hanifa kisha kukawa na ushindani na ikaangukia bishara ya ushindi kwa waislamu,watu wa Musailamat wakamwambia,kiko wapi kile ulichotuahidi? akasema:piganieni utukufu wenu,na wakafanikiwa waislamu kumuwa Musailamatul Kaddhaab,na kwa hakika walishirikiana kwenye kumuwa mmoja wa ma Answaar na Wah-shiy ambaye alimuuwa Hamza Bin Abdul Muttwalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-

Ujumbe wake kwenda kwa Al-Mundhir Bin Saawiy Al-abdiy kayika mji wa Bahrain:

(Baharaini ni mji unaokusanya sehemu zilizopo baina ya Oman na na Basra kwenye Pwani ya Bahari) na miongoni mwa miji yake mikuu ni Hajar wa Jawaatha na Qatwiif na mkoa wote wa Ahsaa,na miongoni mwa watumishi wake wa kifursi ni Saibakhut na miongoni mwa Waarabu ni Al-Mundhir Bin Saawiy Al-Abdiy,(758)Ambaye alikuwa chini ya utawala wa Fursi.

Na Kwa hakika imepokelewa kuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-aliandika ujumbe kwenda kwa Al-Mundhir Bin Sahaawiy aliwasomea watu wa Baharain basi wakashilimu baadhi yaona baadhi yao wakauchukia uislamu,basi akaandika kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kuhusu tukio hilo,basi Mtume akamjibu kwa ujumbe ambao ndani kulikuwa na haya: ((Kwa jina la ALLAH mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu,kutoka kwa Muhammad mtume wa ALLAH kwenda kwa Mundhir Bin Saawiy,Amani iwe juu yakoMimi namshukuru Mwenyezi kwa Neema alizokupa,ALLAH ambaye hapana mola isipokuwa yeye na ninashuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye tu,na kuwa Muhammad ni Mja wake na Mtume wake,Ama baada ya kusema hayo kwa hakika mimi nakukumbusha kuhusu Mwenyezi Mungu-mwenye nguvu na utukufu-kwa hakika mwenye kutoa nasaha kwa hakika anatoa nasaha kwa maslahi ya Nafsi yake,na kwenye kuwatii wajumbe wangu na kufuata amri zao kwa hakika amenitii mimi,na mwenye kuwapa Nasaha kwa hakika ametoa nasaha kwa ajili ya nafsi yake,na kwa hakika wajumbe wangu,kwa hakika wajumbe wangu wamekusifia kwa mambo ya kheri,na kwa hakika mimi nimewaomba watu wako kwako basi waache waislamu na jambo lao la kusilimu,na nimewasamehe wenye madhambi,basi wakubalie,na kwa hakika wewe utakapokuwa mwema basi kamwe hatutaweza kukutoa kwenye kazi yako,na mwenye kuishi akiwa ni Myahudi au Majusi basi ni wajibu wake kutoa Jizia)) (759)

Na alikuwa mbeba ujumbe ni Alaa Bin Al-hadhramiy-Radhi za Allah ziwe juu yake-na huo ulikuwa ni mwaka wa Nanetangu kuhama mtume,na kwa hakika ulienea uislamu kwenye Mji wa Bahrain,na wakawa baadhi ya watu wake wakitoa Zakka na Baadhi ya wengine miongoni mwa manaswara na Majusi wakitoa Jizya.(760)

Na kwa hakika imekuwa Baharain ni sehemu katika Dola ya kiislamu mwisho wa zama za Mtume ,na kwa hakika alituma huko baharain mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- kundi la watawala

kwa mtazamo wa kuwepo kwa vijiji vyingi huko,na katika watawala waliokuwa maarufu katika zama za mtume ,noi swahaba mtukufu(Al-ala Bin Al-Hadhramiy)(761)na kwa hakika mtume alimtuma pamoja nae baadhi ya maswahaba miongoni mwao ni Abuu Hurairat-Radhi za Allha ziwe juu yake-(762)

Ujumbe wake kwenda kwa Farwat Bin Amrou Al-Judhaamiy:

Alikwa ni Kiongozi wa sehemu za Sham sehemu inayofuatana na miji ya waarabu,na alikuwa na mafungamano na na waroma na makao yake makuu ni kuanzia upande wa Jordan.(763)

Alisilimu na akaandika ujumbe kwenda kwa Mtume wa ALLAH-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na akapeleka zawadi kwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-,Basi mtume akamuandikia ujumbe na ndani yake kulikuwa na haya Kutoka kwa Muhammad Mtume wa ALLAH kwenda kwa Far-wat Bin Amrou,Ama baada ya kuyasema hayo,nakufahamisha kuwa ametufikia mjumbe wako,na amefikisha ulichomtuma na katoa habari kuhusu hali mliyokuwa nayo kabla,na ametujia na habari ya kusilimu kwako,na kwa hakika ALLAH amekuongoa kwa uongofu wake ikiwa utakuwa mwema na utamtii ALLAH na Mtume wake,na ukasimamisha swala na ukatoa Zakka basi akamuamrisha Bilali akampa mjumbe wake aitwae Masoud Bin jumla ya Dir-ham 60,akasema,na zikamfikia habari za kusilimu Far-wat,basi akamuita na akamwambia ,Rudi tukupe ufalme ,akasema: siwezi kuiwacha Dini ya Muhammad,na wewe kwa hakika unajuwa kuwa Issa amembashiria ,lakini wewe umenga'nga'nia ufalme wake,basi akamfunga kisha akamtoa na kumuwa kisha kumsulubisha(764) Pamoja na kujaribu kumridisha na kumtoa kwenye uislamu wake lakini alikuwa imara na akauwawa hali yakuwa shahidi,na kwa hakika alisema Beti ambazo zinajulisha juu ya kubakia kwake kwenye uislamu kabla ya kuuwawa kwake,miongoni mwa kauli yake:

imewafikia waislamu Furaha kwa kuwa mimi

nimeusalimisha mwili wangu kwa Mola wangu mtukufu

Na huenda kuuliwa kwake kuna mchango mkubwa kuanza vita vya Mu'uta pamoja na sababu zingine(766)na kwa hakika baada ya hapo ilijulikana uwepo wa idadi kubwa ya wakoma ambao wamejikita kwenye uislamu walimuhami Dahiyyat Bin Khaliifat Al-kilabiy pindi msafara wake ulipovamiwa na baadhiya makabila,(767) na imekuja habari kuwa yeye alimpa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alimzawadia Farasikabla ya kuuwawa na watu wa Roma.(768)

Jumbe zake kwenda kwa Mfalme wa Oman:

Oman ipo upande wa kusini mwa bara Arabu,kwenye pwani ya nyanda za juu za bahari ya uarabuni(Khalij Oman) na mipaka yake katika zama za Mtume ilikuwa ipo karibu na mipaka maarufu ya Oman ya sasa(769)na kwa upande wa magharibi inapakana na Hadhara Mauti na kwa upande wa kaskazini inapakana na Bahrain ni maarufu kwa kilimo cha mitende uzalishaji toshelezi wa Bidhaa zitokanazo na wanyama,na kulikuwepo humo dola waliyoirithi Al-Julnadiy na mji wake mkuu ni Suhaar,na kabila lake mashuhuri ni Al-azdiya na miongoni mwao walitokea wafalme.

Na ilikuwa waabudu masanamu wameenea katika mji wa Oman kama miji mingine ya Waarabu,pamoja na kuwa na baadhi ya waabudu Jua na baadhi ya Manaswara hawakuwa na athari yoyote ambayo yaweza kutajwa kwa hakika habari za uislamu zilijaaOman Mapema(770) kwa njia ya kusuguwana na makabila ya Waaraabu,vilevile Baharain au katika mji wa Yemen na Hadhara Mauti,na baada ya kurudi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kutoka katika Umra ya Qadhwau kwenye mwaka wa saba tangu kuhama makkah alimuandikia ujumbe Jaifar wa Ibbaad Watoto wawili wa Al-jalandiy akiwalingania kuingia kwenye uislamu na akamtuma Amrou Bin Aaswi(771)na imekuja kwenye ujumbe huo: Kwa jina la ALLAH mwingi wa Sala na mwenye kurehemu,kutoka kwa Muhammad Bin Abdillahi kwenda kwa Jaifarna Abbad watoto

wawili wa Al-Julaindiy,amani iwe kwa kila mwenye kufuata uongofu,ama Baada ya kusema hayo,kwa hakika mimi nakuiteni kwa wito wa uislamu Ingie nyote wawili katika uislamu mtasalimika,kwa hakika mimi ni mtume nilietumwa kwa watu wote ili ninuonye kila aliyekuwa hai na niHoja dhidi ya makafiri,kwa hakika nyi wawili kama mtaukubali uislamu,nitawapa ufalme wenu,na ikiwa mtakataa kuukubali uislamu kwa hakika ufalme wenu utaondoka na Farasi wangu watashuka kwenye viwanja vyenu,na utume wangu utadhihiri kwenye utawala wenu))(772)

Na anasimulia Amrou Bin Aaswi kufika kwake Oman na namna alivyokutana na wafalme wote wawwili na yaliyo jiri kati yao wawili hivyo anasema: (Amesema Amrou nilipofika Oman nilikusudia kufika kwa Abbad na walikuwa ni watu wapole sana na tabia nzuri basi nikasema: kwa hakika mimi ni Mjumbe wa Mtume wa ALLAH nilietumwa kwako na kwa ndugu yako,basi akasema Ndugu yangu aliyenitangulia kwa umrina Ufalme,nami nitakufikisha kwake ili ausome ujumbe wako ,basi nikakaa kwake masiku mengi kisha akainiita nikaingia kwake na niakampa barua iliyokuwa ina muhuri,na akaifunguwa barua na akaisoma mpaka mwisho wake kisha akampatia ndugu yake naye akaisoma ila mimi nimeona kuwa ndugu yake ni mpole kuliko yeye akaniambia niwache leo hii na unijie siku ya kesho,na ilipo fika hiyo kesho nilimrudia akasema :akasema kwa hakika mimi nimefikiria hiki ambacho umenilingania kwacho nikajigunduwa kuwa mimi ni mtu mwarabu Dhaifu zaidi ikiwa nitammiliki Mtu ambaye yupo mikononi mwangu,nikamwambia:mimi naondoka kesho,na alipokuwa na uhakika wa kuondoka kwangu aliamka na na akanitumia ujumbe na nikaingia kwake,basi akaukubali Uislamu yeye na ndugu yake wote,basi wakatowa Sadaka kumpa Mtume na waniwacha mimi na Sadaka na wakaniwachia niwahukumue baina yao,na walikuwa wawili hao ni msaada kwangu kwa mwenye kupingana nami,basi

nikachukujwa sadaka kutoka kwa matajiri wao na nikairejesha kwa mafukara wao(773)

Na ni wazi kuwa kulikuwapo na majibizano marefu yaliyoduru baina ya Amrou Bin Aaswi na hao Wafalme wawili,yalijikita zaidi kuhusu msimamo wa wafalme wengine kutokana na Barua za Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-na kutoka na Daawa yake,na kuhusu watu wake ambao ni Maquraish na alichokipata toka kwao,pale Amrou alipowapa habari kusilimu kwa Najaashiy na kukubali kwake Daa'wa yake na kuhusu msimamo wa Hiraqliy kutokana na kusilimu Najaashiy.kama ambavyo yalijiri majadiliano kuhusu Sadaka Ulazimwa wa Zakah na wenye kustahiki kupewa,na kiini cha Daawa ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-

Na kwa kawaida Wafalme wawili walikinai na kutosheka na uislamu na wakamuachia Amrou Bin Aa'sw atekeleze jukumu lake la Zakkah ,kwa kuzichukuwa Zakkah kutoka kwa matajiri na kuzirudisha kwa mafukara ilikuwa hivyo katika maisha yake yote mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,na ni wazi kuwa mtume alikuwa akimshirikisha Abuu Zaid Al-Answariy(774) katika mambo muhimu,pale ambapo alijitolea katika kufundisha watu Qur'an na Sunna za Mtume Salana amani ziwe juu yake-,kama ilivyokuwa kwa Alaau Bin Bin Al-hadhramiy Kiongozi wa Bahrain anamahusiano fulani na baadhi ya watendaji wa nchi ya Oman(775) na kwa hakika Abbad na Jaifar waliendelea kuitawala Oman katika Uhai wote wa mtume-Sala na amani ziwe juu yake-

Na kwa hakika palizuka kuritadi katika mji wa Oman baada ya kufariki kwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-Akaweza Abuubakar-Radhi za Allah ziwe juu yake-kwa msaada wa Jaifar na Abbad wafalme wawili wa Oman kuwasanbaratisha ,baada ya vita nyingi ambazo aliziongoza Hudhaifa Bin Mihswan na Ikrimat Bin Abii Jahal kwenye pande za Dub'aa(776)na watu wengi wa Oman walimkubali Abuu bakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake- pale

mwanzo wa Ukhalifa wakewakimuunga mkono na wakibakia kwenye uislamu,basi akawasifia na kubakia kwao licha ya hali ya misukosuko iliyowapata baada ya kufariki kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-(777) na lilikuwa kabila lake lina mchango mkubwa katika ukombozi wa kiislamu katika zama za waongofu na Haswa katika mji wa Iraq na Fursi.

Ujumbe wake kwenda kwa Haarith Bin Abii Shamriy Al-Ghassan:

Alikuwa Al-Haarith ni Kiongozi upande wa Al-Balqaau katika Ardhi ya Shaam na Baadhi ya pande za Damascas(778)na alikuwa ni mfuasi wa Roma na mwenye mwenye kuung'nga'nia Unaswara.

Na kwa hakika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alimuandikia Ujumbe na ndani yake kulikuja maneno haya: ((Kwa jina ala ALLAH Mwingi wa Sala na Mwenye Kurehemu,kutoka Muhammad Mtume wa ALLAH Kwenda kwa Al-haarith Bin Abii Shamri Amani iwe kwa kila mwenye kufuata uongofu na akamwamini Mwenyezi munguna akasadikisha,Hakika mimi nakuita umuamini Mwenyezi mungu peke yake hana mshirika wake na ukifanya hivyo Ufalme wako Utabakia))(779) Na kwa hakika Al-haarith alikasirika,na akamtupia ile Barua ,na alikuwa mbeba Risala ni Shujaau Bin Wah'bi Al-Asadiy (780),na akamtisha na kuumpa ahadi ya vitisho,na akaandika Ujumbe kwenda kwa Qaiswar akimtaka Ruhusa ya Kumvamia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-katika mji wa madina,basi Qaiswar akamkataza kufanya hivyona akasema hapana usimuendee na achana nae.(781)

Ujumbe wake kwenda kwa Haarith Bin Abii Shamriy Al-Ghassan:

Alikuwa Jabalatu Bin Aiham ni Mfalme wa Mwisho wa Ghasaasinah waliokuwa Maarufu kwenye mji wa Sham kabla ya uislamu.(782) na alikuwa mtu muhimu kwa Waarabu na ni mshairi wao katika zama za kabla ya uislamu,na akiwafungamanisha na Ausi

na Khazrajiy mafungamano ya ukaribu,walikuwa wakimtembelea Hassan Bin Thaabit na wengineo miongoni mwa washairi wa Yathriba Kabla ya uislamu hivyo wakawa wakiwasifia na wakipata kutoka kwao vipato.

Na walikuwa ni wafuasi wa Wa Roma,isipokuwa wao walikuwa wakiwaongoza Manaswara wa kiarabu katika Mji wa Shamu,na kwa hakika Mtume Aliandika Ujumbe kwenda Jabalatu Bin Al-Aiham Mfalme wa Ghassan akimlingania kwenye uislamu.(783)

Na kwa hakika aliubeba ujumbe Shujaau Bin Wah'bu Al-Asadiy,na alikuwa akijulikana kwa kuunganisha Nasaba baina ya Answar na Ghasaasinah ,na yakapita kati yao mazungumzo baina ya Shujaau na Jalabatu,nayo nikuwa Shujaa alimwambia: Ewe Jabalah kwa hakika watu wako wamemuamisha mtume huyu kumtoa kwenye mji wake na kumpeleka kwenye mji wao-Yaani watu wa Madinah-wakamuhifadhi wakamtetea na wakamnusuru,na kwa hakika hii Dini Ambayo wewe upo humo,siyo Dini ya Baba yako lakini wewe umetawala Sham na umepakana na Roma na lau ungepakana na Kisra basi ungefuata Dini ya Fursi,basi ikiwa utasilimu Basi Sham Nzima Itakutii na Roma itakuogopa,na ikiwa hawatafanya hivyo,basi wao watakuwa na Dunia nawe utakuwa na Akhera,na kwa hakika ulikuwa umebadilisha misikiti kuwa Makanisa na Adhana kuwa kengele na mikisanyiko kuwa ni siku ya kukusanyika manaswara(784)na yaliyo kwa ALLAH ni bora na yenye kubakia.akasema Jabalatu,Namuapia ALLAH kwa hakika mimi natamani wawe watu wote wangekusanyika kwa mtume huyu na kuwe kukusanyika kwao ni kwa ajili ya yule ambaye ameumba mbingu na Ardhi,na kwa hakika nimefurahishwa na watu wangu kwa kukusanyika kwa ajili yake,na kwa hakika aliniita Qaiswar kwenda kuwauwa wafuasi wake siku ya Mu'uta Basi nikamkatalia,lakini mimi sioni haki wala Batili na nitatazama wapi nielekee.)(785)

Na uislamu wake haukuwa wazi wakati wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-lakini inavyofahamika wazi kwake yeye ni kuufahamu uislamu na kukinaika nao wakati alipokuja nao Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-ijapokuwa hakuutangaza uislamu wake na kwa hakika watu wake walishiriki katika vita vya Yarmouk na yasemekana yeye alikuwa pamoja nao (786)katika mapigano

Na kwa hakika aliweka wazi uislamu wake na akaja Madina wakazi wa Omar Bin Khattwab-Radhi za Allah ziwe juu yake- akiwa pamoja nae wapanda Farasi miongoni mwa watu wake na wakuingia mji wa Madina wakiwa katika Vazi na mapambo yenye kufanya wakodolewe macho(787)na kwa hakika Omar alifurahishwa kwa kuja Jabalatu na aliokuwa pamoja nae miongoni mwa waislamu,nakwa hakika kulitokea tukio lilopelekea kuritadi kwake na kukimbia kwake kwenda Roma.

Ujumbe wake kwenda kwa Yahinnat Bin Ru'uyat na viongozi wa Ailat:

Ailat ,ni Bandari iliyopo upande wa Mgharibi mwa Al-aqbah kwa upande wa Palestina(788) nayo ni sehemu ya Bandari ya lilaat katika mji Palestina iliyokaliwa kwa mabavu,na ulikuwa ni mji wa uliondelea wanakaa humo wakazi mchanganyiko wa Mayahudi na wakiristo,na anawatawala Yahinnat Bin Ru'ubah naye ni miongoni mwa viongozi wa Wakiristo katika sehemu ile

Na alip[ofika mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Tabuk wakati wa vita yake alichaguwa ujumbe akautuma Ailat,wakibeba ujumbe kupeleka kwa kiongozi wake Yahinnat Bin Ru'baat na imekuja katika ujumbe ulioelekezwa kwake na kwa viogozu wa Ailat: ((Ujumbe kwenda kwa Yahinnat Bin Ru'ubat na Sarawaat Watu wa Ailat nyinyi mmesalimika,hakika mimi ninamshukuru ALLAH kwa neema zake kwenu nyinyi,ALLAH ambaye Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila yeye ,na mimi siyo mwenye kupigana nanyi vita mpaka niwe nimekwisha watumia Ujumbe,basi Ingieni kwenye uislamu au mtoe

Jizia na Mtiini ALLAH na Mtume wake na wajumbe wa Mtume wake na muwakirimu na muwavishe mavazi yaliyo mazuri na yasiyo mavazi kama vazi livaliwalo mwilini,na mumvisheZaidi vazi zuri,kwa namna yoyote watakavyokuwa wajumbe wangu wameridhika basi namimi nitakuwa nimeridhika na kwa hakika Jizya itakuwa imejulikana ,na ikiwa mnataka amani Bara na visiwani basi mtiini ALLAH na Mtume wake na mtaachiwa kila mali ambayo ilikuwa ikichukuliwa na Waarabu na wasiokuwa Waarabu isipokuwa Mali ambayo ni haki ALLAH na haki ya Mtume wake,na ikiwa wewe utawarudisha na hutawaridhia sitochukuwa kutoka kwenu chochote na nipigane nanyi vita ,na niwateke watoto wenu na kuwauwa wakubwa ,kwa hakika mimi ni Mtume wa Haki wa ALLAH Ninamwamini ALLAH na Mitume wake na Vitabu vyake na nina Muamini Issa Mwana wa Maryam kuwa yeye ni neno la ALLAH,na mimi ninamuamini kuwa yeye ni Mtume wa ALLAH basi kuweni watiifu kabla haijawajia Shari,kwa hakika mimi nimewausia,kwa hakika mimi nimewausia wajumbe wangu kwenu nyinyi ,na mumppe Harmalat kilo 112 za Shairi,na kwa hakika Harmalat ni miongoni mwenu na kwa hakika mimi kama isingekuwa Mwenyezi mungu kisha utiifu wa wajumbe nisingetuma kwenu chochote isipokuwa Jeshi,na nyinyi ikiwa mtawatii wajumbe wangu kwa hakika ALLAH atawalipa na Muhammad na yeyote atakaeyekuwa ni mwenye kufanya hivyo,na kwa hakika Mjumbe wangu Shurah-biil na Ubaiyyat na Harmilat,na Hariith bin Zaid Al-Twaai,kwa hakika wao vyovyote watakavyokuhukumu basi uwaridhie,na kwa hakika mna Dhima ya ALLAH na Dhimma ya Mtume wa ALLAH,Na amani iwe juu ya yenukiwa mtatii,na waandaeni watu wa Maq-na (789)kwenye Ardhi yao)) (790)

Na kwa hakika Mazungumzo haya yalikuwa ndani yake usalama wa waziwazi kwa Ailat na watu walipopenda jambo hilo,na ndani yake kulikuwa na matisho ya waziwazi kwa wao na Biashara zao za Bara na Visiwani watakapokuwa wame wamepinga,pale ambapo mji

wao ndiyo ulikuwa makutano ya Meli kutoka Yemen na sehemu zingine na ni kituo cha kukutania ili kuelekea Sham,Hivyo Yahinnat akaogopea matokeo mabaya,na akaja kwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-katika mji wa Tabuuk akiwa pamoja na watu wa Sham na watu wa Yemen na msafara wa Baharini na wafanya Biashara wak,na alikuwa Yahinnat anavaa mavazi ya Kinaswara na yana Msalaba uliotengenezwa kwa Dhahabu na Madini Mengine.(791)

Na kwa hakika mtume-Sala na amani ziwe juu yake-alimpokea yeye na waliokuwa pamojanae,na wakafunga mkataba na ndani ya mkataba kuna maelezo kuhusu usalama wa Safina ,na hili linaonesha ufahamu wa ndani zaidi wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kutambuwa harakati na Biashara za Baharini na umuhimu wa kuwapa Usalama.

Na hizi Barua zilikuwa ni Dalili kubwa zinaonyesha Pupa kubwa ya Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- ya kufikisha ujumbe,na kuwa Amani na Daawa kwa njia nzuri ndiyom msingi wa kwanza wa Daawa,na kuwa Propoganda za kuwa uislamu ulienea kwa upanga haina usahihiu hata kidogo.

Na kama zilivyoweka wazi hizi Jumbe na kilichofuata miongoni mwa matukio,ziliweka wazi namna gani viongozi wa Manaswara na majemedari wake walivyotilia umuhimu Uwito wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,na haswa kiongozi wao Hiraqliy,na ujumbe uliweka wazi kuwa hawa viongozi walijuwa Utume wake na ukweli wake,na kuzinduka kwao kwa kuenea dini ya Uislamu kwenye Ardhi zao na Sehemu zao na katika Dini zao,na haya ndiyo yaliyotekea katika zama zaona wakayashuhudia kwa macho yao sawa awe ni Hiraqliy au Muqauqis au Kisra na wengineo.

Kama ambavyo Ujumbe unajulisha juu ya Imani ya mtume- **Rehema na amani ziwe juu yake-** kuwa ALLAH ni mwenye kuinusuru dini yake licha ya kuwa na uwezo mdogo na uchache wa watu wake

kwa kipimo cha uwezo wa kimali,na ahadi ya ALLAH na Mtume wake ikatimia.

Kama ilivyo kwa hakika Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- alichaguwa watu wenye uwezo zaidi ndiyo wenye kubeba ujumbe wake ili kutimiza malengo ya ujumbe,na kuufikisha kwa yule aliyekusudiwa na alichaguwa watu wenye kuweza kuongea nae,na wenye kujuwa tabia na Itikadi za Jamii ambazo ujumbe umetumwa kwa viongozi wakekama walivyojipamba kwa kwa ushujaa na Subra na Hekima,na ulikuwa usulubu wa Barua zake Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-ni kufupisha na kuweka wazi nakuhakiki malengo ya ujumbe,na kutolea ushahidi kwa Aya za Qur'an zilizoelekezwa kwake mtume na kwa watu wote,haswa kwenye mazungumzo yake na viongozi wa Wakiristo,kama ambavyo alikuwa akizitoa barua hizo kwa kuanza na Jina la Sala,na akitilia mkazo ndani yake juu ya kumuabudu ALLAH peke yake hana mshirika wake.

Na kwa hakika mtume alijuwa kuwa Wafalme hawakubali Ujumbe isipokuwa uwe na muhuri,basi akatengeneza Muhuri kwa ajili ya kutekeleza jambo hilo na ndani yake kuna Heshima ya kumuheshimu ALLAH,pale alipoweka jina la ALLAH Mtukufu Katika mstari wa Kwanza na jina la Mtume kwenye Mstari wa pili na Jina Muhammad akaliweka katika mstari wa watatu yaani kwa utaratibu huu.

Allahu

Rasuul

Muhammad

Imepokelewa kutoka kwa Anas-Radhi za ALLAH ziwe juu yake- amesema alipotaka Mtume kuandika Ujumbe kwenda kwa Waroma aliambiwa kuwa hao wa Roma hawasomi Barua ambayo haina

Muhuri basi akatengeneza Pete mviringo kwenye mkono wake na ukatiwa Nakshi kwa kuandikwa (Muhammad Rasuulullah)(792)

Na wa hakika huu Ujumbe uliutoa uislamu na kuupeleka nje ya ya Miji ya Waarabu kwenda kwenye mataifa ya yasiyokuwa ya Kiarabu.

Ujumbe huu na vilivyomo ndani yake unazingatiwa kuwa ni miongoni mwa misingi ya namna ya kuamiana kimataifa na kutilia mkazo kuwa ni ujumbe wa kiulimwengu,na ni mwanzo wa mabadiliko katika Dola ya Kiislamu katika zama za Mtume na pia ni mwanzo wa mahusiano yake na ulimwengu mzima.

Na baadhi ya uchunguzi unaonesha kuwapo kwa asili ya hizi Barua kwenye Ngozi Miongoni mwa Ujumbe huo ni Ujumbe wa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kwenda kwa Muqauqis Mtawala wa Qibtwiyat na ujumbe wake -Sala na amani ziwe juu yake-kwenda kwa Mundhir Bin Sa'awiy Al-abdiy Mfalme wa Bahrain na ujumbe wake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwenda kwa Najaashiy mfalme wa Habasha na Ujumbe wake Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Kwenda kwa Kisra,na ujumbe wake kwenda kwa Qaiswar Mtawala wa Roma(793)

Na licha ya machapisho ya Mustash-rikiina kuhusu hivi vyanzo na kufanya Uchunguzi maalumu katika baadhi ya majumba ya ukumbusho Ulimwenguni isipokuwa yapasa kutolichukulia Uhakika kwa hayo yaliyotajwa mpaka ufanywe upembuzi yakinifu na uhakiki na ulinganishaji kutoka kwa wataalamu waliobobea kwenye mambo hayo

Na kuna vitabu vingi na Barua nyingi kutoka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kwenda kwa wakubwa na wafalme na huenda umuhumu wa kuwataja ukawa siyo muhimu kamatulivyotangulia kuwataja ,kama ambavyo alielekeza barua kwenye makabila fulani ambayo inakuwa ni vigumu kuyazungumzia yote ,na kwa hakika

kulitoka uchunguzi maalumu wenye mfumo wa kielimu uliokuwa wazi.

Na hapanashaka kuwa kuyafungamanisha matukio ya Historia na Zama za Makhalifa waongofu,na yaliyopita wakati huomiongoni mwa ukombozi wa kutumia Barua za Mtume kwenda kwa viongozi na watawala wa hizi sehemu zilikuwa na umuhimu maalumu,kama ambavyo kuzihusisha Barua za Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na hizo sehemu na kuingia watu wa sehemu hizo kwenye uislamu na kubakia Mataifa yao kwenye uislamu paka leo hii wakiwa chini ya Umma wa Kiislamu na kuendelea kuwa wafuasi wa Mtume,Muhammad-Sala na amani ziwe juu yake-kuziihusisha kuna umuhimu mkubwa kwa kila mwenye kusoma Historia na kuenea kwa uislamu baina ya watu wa sehemu zile,na Historia za hizi Sehemu kwa sasa.

Ukombozi wa Khaibar(ilikuwa ni mwezi Rabiul Awwal mwaka wa 7Hijiria)(795)

Na ulikuwa ujumbe wa mayahudi ambao waliwachochea makundi ju ya kuivamia Madina kwa hakika walikuwa wakuja kutoka Khaibar,na kama ilivyo Mayahudi wa Khaibar walikuwa wanaweka mipango ya kuuvamia mji wa Madina,na kwa hakika waliwasiliana na baadhi ya makabila ili kutekeleza lengo hili pale walipo kubaliana kuweka ushirika wa pamoja na Ghatfana ,na wakawa wanawakusanya Mayahudi wa Khaibar na wa Bonde la Qur'aa na Taimaau na waliokuwa pambizoni mwao ili Kuupiga mji wa Madina(796)

Na kwa hakika waislamu walipata uhakika kuhusu hiziz taarifa baada ya kurudi kwao kutoka Vita ya Sulhu ya Hudaibiyat ,pale ambapo ilikuwa ni kawaida ya Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-kupokea habari za Maadui wake kisha kuzifuatilia,na mji wa Haibari ulikuwa ndiyo sehemu ya kukusanyika maadui wapya,basi wakajiandaa waislamu kwa ajili ya jambo hili na wakati huo huo

Mayahudi wa Haibar walikuwa wakieneza Propaganda za nguvu zao,na wakieneza habari kuwa wao wanajeshi la wapiganaji linalo karibia Eflu kumi ambao wameandaliwa kwa ajili ya kumpiga vita Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-nakuwa wao wana ngome Imara,kama vile ambavyo walianza kuwatishia waislamu na kuwaahidi kwa njia ya moja kwa moja na isiyokuwa ya moja kwa moja kwa kupitia Mayahudi waliobakia katika mji wa Madina na baadhi ya Wanafiki walikuwepo humo.

Na kwa hakika hali iliyokuwa ikiwakabili Maquraishi inanasibiana na Sulhu ya Hudaibiyat,Sulhu ambayo waislamu walikubaliana na Maquraishi kusimamisha vita baina yao kwa muda wa miaka kumi,na haikuwa kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake wala kwa waumini isipokuwa ni kuliwahi jeshi la mayahudi Khaibar kabla ya wao hawajawawahi,pale ambapo waislamu walianza maandalizi yaona wakawakabili wakiwa pamoja na mtume-Sala na amani ziwe juu yake-,na walikuwa idadi yao ni wapiganaji Eflu moja na mia Nne.(798)

Na wakati waislamu wanaelekea Haibari,waliondoka wanajeshi wa Ghat-faan wakitokea Najdi ili kuwasaidia Mayahudi wa Haibar,basi waislamu wakawadanganya pale walipowapenyezea habari kuwa baadhi ya Waislamu wamekwenda kuvamia majumba yao ya kale,basi watu wa Ghat-faan wakawa wameikubali habari hiyo,na wakarudi kwenye majumba yao wakiwaacha mayahudi wa Khaibar kwenye mafikio yao(799) na wakati huohuo Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alikuwa amekusudia kufikia Khaibar kwa upande wa Sham (800) yaani katika sehemu iliyopo Baina yake na baina ya majumba ya Ghat-faan ili apate kuzuia uwezeka no wowote wa Ghat-faan au Mayahudi wa kaskazini mwa Hijaaz kufika kwenye uwanja wa Vita,au kupata Msaada wa Mayahudi wa Khaibar.

Walifika waislamu usiku katika mji wa Khaibarna wakakita Kambi na wala hawakupatwa na tatizo lolote Usiku(801) na Asubuhi

Mayahudi walipoenda mashambani mwao walishtukizwa na waislamu na wakarudi haraka kwenye Ngome zao wakirudia maneno haya (Muhammad Wal-khamiis) wakikusudia Muhammad na Jeshi lake,na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- akawa amesema: ((Niatakuwa nimeiharibu Khaibar ikiwa sisi tutafikia kwenye uwanja wa watu,basi atakuwa ni asubuhi mbaya na yenye shari kwa makafiri walionywa kuwa watapata adhabu))

Zilikuwa ngome za Mayahudi ni nyingi,na kwa hakika waislamu walijigawa ili kuzidhibiti,na walikuwa wakitupiana mishale na mayahudi wa Khaibar mpaka wakapatwa na mishale wengi katika waislamu kufuatia tukio hilo(803)

Alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-anapupia kujuwa hali za Ngome zilizodhibitiwa(804) na Ngome ya Al-Nutwaat nayo ni moja kati ya Ngome za Khaibari ilikuwa ina idadi ndogo ya walinzi ,na alijuwa Mtume kuwa imejaa silaha na vifaa vya kivita,na ndani yake kuna makombeo ya kurusha mawe na mapipa ya kivita-vifaru-akajuwa kuwa kama waislamu watafungua ngome ile watapa vifaa vitakavyo wasaidia kufungua Ngome zilizobakia ,basi waislamu wakatilia mkazo kwenye kuwazuilia na kuwashambulia kwenye hii Ngome mpaka wakaweza kuifungua Ngome ile,basi wakauta humo vyakula na vifa vilivyo wasaidia dhidi ya Maadui zao,kama ambavyo wao walifaidika na salaha silaha mbalimbali walizozikuta humo,ziliwasaidia kuwashambulia Maadui zao kwenye Ngome zilizobakia(805)

Na kwa hakika waislamu walifunguwa Ngome moja baada ya nyingine,na miongoni mwa hizo Ngome kulikuwa na Ngome Rahisi kuzifungua na pia kulikuwa na Ngome Ngumu.(806)

Kwa hakika ilikuwa Ngumu Ngome ya (Al-qamuus) kwa waislamu,basi mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akatoa Bishara ya kuifungua katika Riwaya iliyopokelewa kutoka kwa Sahli Bin Saad-Radhi za Allah ziwe juu yake-kuwa mtume wa ALLAH-Sala

na amani ziwe juu yake-alisema siku ya Khaibar: ((Nitampa hii Bendera kesho mtu ambaye ALLAH atafunguwa kupitia mikono yake,Mtu amabaye anampenda ALLAH na Mtume wake na ALLAH na mtume wake wanampenda)) Basi watu wakalala wakizungumzia usiku kucha kuwa nani miongoni mwao atakaepewa hiyo Bendera.

Basi watu walipoamka asubuhi wakaamkia kwa mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-wote wakitarajia kupewa bandera hiyo,basi mtume akasema yuko wapi Ally bin Abii Twaalib,kukasemwa kuwa ewe mtume wa ALLAH Ally anaumwa macho,akasema mtume-Sala na amani ziwe juu yake- basi mfikishieni ujumbe basi akaletwa ,basi Mtume akamtemea kwenye macho yake na akamuomba kisha akapona akawa kama vile hakuwa na maumivubasi akampa Bendera na Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake- akasema:Ewe Mtume wa ALLAH,nipigane nao mpaka wawe kama sisi.akasema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-Nenda polepole mpaka ufike katika viwanja vyao kisha walinganie kuingia katika uislamu,na uwape habari kuhusu jambo ambalo ni wajibu juu yao miongoni mwa haki za ALLAH,namuapia ALLAH,ikiwa ALLAH atamuongoza mtu mmoja tu kupitia kwako,jambo hilo ni bora kuliko kumilika Farasi Mwekundu))(807)

Na kwa hakika Sala alileta ukombozi kupitia mikono ya Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake-kama alivyotoa habari mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-na ngome za Khaibar zilizobakia zikaanguka moja baada ya nyingine,jambo lilopelekea mwisho wake kulazimika mayahudi kutaka mazungumzo ya kufikia muwafaka na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na wakajisalimisha kwa waislamu kwa lengo la kuzuia umwagaji wa damu zao,na ili waruhusiwe kutoka katika mji wa Khaibar(808) Na baada ya kukubaliana na waislamu kuhusu kuondoka kwao,walikubaliana waislamu pamoja nao kuwa Mayahudi wa Khaibar wafanye kazi kwenye Mitende na Mashambani,na malipo yao yatakuwa ni nusu ya matunda yatakayopatikana,na kuwa ni haki ya waislamu kuwaacha au

kuwaamisha wakati wowote watakapotaka(809)na yakawa matokeo ya hii vita ni kuuliwa Mashahidi Ishirini miongoni mwa Maswahaba wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kuuwawa mayahudi wa Khaibar wapatao tisini na tatu na kwa hakika kuzuiliwa na kuuwawa mayahudi wa Khaibar kuliendelea kwa zaidi ya siku kumi.(810)

Na baada ya mayahudi wa Khaibar kupatana na Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-alijaribu Mwanamke wa Kiyahudi kumuwekea Mtume Sumu kupitia Nyama ya Mbuzi iliyopikwa amabto alimpa kama zawadi,lakini ALLAH akamsalimisha (811)

Na imesemwa kuwa kufa kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-baada ya kula nyama hiyo kwa miaka kadhaa ,ilikuwa ni Athari ya ile Sumu,kwa hakika amepokea Bin Hishaam: ((N akwa hakika alaisema mtume akiwa katika maradhi ambayo alikufa kwa ajili yake,na aliingia Ummu Bishri Bint Al-Baraa Bin Ma'arouru akimtembelea:Ewe Ummu Bishri hakika hivi sasa nahisi kuwa unakaribia kukatika mshipa ambao unakwenda kwenye moyo kwa sababu ya kula ile nyama niliyokula na ndugu yako kule Khaibar.akasema,basi waislamu wanamshuhudia mtume wa mwenyezi mungu amekufa Shahidi pamoja na mwenyezi mungu kumkirimu kwa kumpa utume)) (812)

Na baada ya waislamu kuukomboa mji wa Khaibar na wakawa wameshapangilia mambo yao,alielekea Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-na waliokuwa pamoja nae miongoni mwa mujaahidiina mpaka Bonde Qur'aa Basi wakawapokea waislamu kwa kuwarushia mishale,na akapatwa Mshale mtumishi wa Mtume kutokana na urushaji wao mishale,basi waislamu wakapigana naona wakaukomboa mji wao kwa nguvuna mtume akawaacha waendeleo kufanya kazi katika Mitende kwa malipo ya Nusu ya kipatikanacho,kama alivyofanya kwa watu wa Khaibar(813) na Habari za Khaibar na za Waadil Quraa na sehemu zingine zilizobakia

zilipowafikia upande wa Kaskazini mwa Hijaaz ,wakafanya haraka kutafuta Sulhu na Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na haswahaswa watu wa Fadki na Taimaau na Ailat na Sehemu nyingine.(814)

Umra ya kulipa iliyopita:(815)

Na huitwa Umra ya Sulhu,na ilikuwa miongoni mwa Sulhu Hudaibiyat ni kurudi Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- mwaka wake huo(Na utakapofika mwaka wako ujao,tutatoka tukuwache uingie,basi wewe utaingia na waswahaba zako na kukaa humo siku tatu ukiwa umeweka silaha kwenye ala zakena wala usiingie na silaha nyingine yeyote)(816)Na alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-ameawapa ahadi maswahaba wake kuwa wataingia Mji wa Makkah atakapokwenda nao katika vita vya Hudaibiyat kwa mujibu wa Ndoto aliyोजना Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-na kwa ALLAH mtukufu:

﴿لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّعْيَا بِالْحَقِّ لَتَدْخُلَنَّ الْمَسْجِدَ الْأَحْرَامَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ ءَامِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٢٧﴾﴾

[الفتح: 27]

Hakika ALLAH amemthibitishia mtume wake ndoto kwa ukweli hakika mtaingia msikiti wa makkah akipenda ALLAH hali ya kuwa ni wenye amani wenye kunyoa vichwa vyenu na wenye kupunguza hamuogopi basi ALLAH akatambua mambo ambayo hamkuyafahamu kisha akajalia kinyume na hayo kuwa ufunguzi upo karibu. Al-Fathu:27. Alikuwa kwa ujuzi wa ALLAH na Amri yake kutanguliza ukombozi wa karibu ambao ni ukombozi wa Khaibar(817) kabla ya kuingia kwa Makkah kwa ajili ya Umra.

Katika mwezi wa Shaaban katika mwaka wa saba tangu kuhama mtume baada ya kukamilisha mwaka mmoja tangu kutoka kwenye Sulhu ya Hudaibiyat,aliamrisha mtume kutoka pamoja nawale ambao walishuhudia Vita vya Hudaibiyat kwenda nao Umra,basi

wakato walikuwa wakiishi pamojanae na wakato na wenginempka wakafika idadi yao wafanya Umra Alfu mbiliisipokuwa waliokuwa wana wanawake na watoto,na mtume akabeba Silaha nyepesi iliyotajwa kwenye Sulhu,na akaswaga vichinjwa na akahirimia yeye na maswahaba wake ,na wakaongozana akiwa pamoja na farasi mia moja wa Akiba ,na apakuwa na ishara yoyote ya mapigano,bali ilikuwa kutoka ni njia ya amani,na kulikuwa kunaletwa Talbiyat na Takbiira za kuhirimia.

Na mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akamtanguliza Muhammad Bin Maslamat akiwa na Farasi kwenda Al-Dwaharan na walipomuona maquraish walijuwa kuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-anakuja,na alipofika Mtume aliwacha Silaha katika bonde lilokuwa karibu na Tan-iim-Sala na amani ziwe juu yake(819)na maquraish wakamuachia Mji wa makkah na wakapanda juu ya milima wakimuangalia Mtume -Sala na amani ziwe juu yake Na alikuwa Abdullah Bin Rawaah amemshika Ngamia wa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- huku anaingia Makkah akiwa na muonekano unajulisha juu ya heshima ya waislamu na kuheshimu kwao na kumlinda kwao Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na wakikariri Shairi lisemalo:

Makafiri wamejiweka mbali na wamemwachia njia yake

wamepawacha wakakaambali na kila heri ipo kwa Mtume wake.

Ewe Mola wangu hakika mimi nimwenye kuamini maneno yake

Naijuwa haki ya Mwenyezi Mungu ni kumkubali yeye

Sisi tuliwapiga kwa maandiko ya Mwenyezi mungu

Kama tulivyo wapiga kwa kuteremka Qur'an tukufu

Pigo lenye kuondoa lenye kuondosha vichwa kwenye usingizi wa mchana(Kailula)

Na humuweka mbali mpenzi na kipenzi chake(820)

Na kwa hakika maquraishi walieneza kuwa Mtume ni Mdhaifu,Akafanya makusudi ili kuwaonyesha afya yake na ya Maswahaba wake na nguvu za miili yao kwa namna ambayo inachukiza maadui zao.

amepokea Bukhar kutoka kwa Bin Abbas amesema; walipanga mstari kwa ajili yake mbele ya Daaru Nad'wa ili wamuangalie yeye na maswahaba wake,na alipoingia Mtume wa ALLAH Msikitini alipandisha shuka yake na akatoa Msuli wa mkono wa kulia ,kisha akasema:ALLAH amrehemu aliwaonyesha msuli wake leo hii kisha akagusa kona ya upande wa kulia na akatoka akikimbia na maswahaba wake wakikimbia pia pamoja nae,mpaka wakafika nyuma yake kwenye Kaaba na akashika kona ya kulia akatembea mpaka akashika kona liliopo jiwe jeusi,kisha akakimbia tena vilevile Twawafu tatu,na akatembea katika Twawafu zilizobaki,na akawa Bin Abbas anasema kuwa :watu walikuwa wakidhani kuwa twawaafu hazikuwa ni wajibu juu yao,na kuwa mtume alitufu vile kwa sababu ya kijiji hiki cha maquraish kutokana na habari zilizomfikia kuhusu wao,mpaka alipo hijji hijja ya kuaga akafanya kutukufu kuwa ni lazima ,basi ikapita Sunna ya kutufu)(821)

Na baada ya kutekeleza Mtume Ibada yake ya Umra Alimuoa Maimuna Bint Harith na wala hakumuungilia na akakaa makka siku tatu na mwisho wa hizo siku tatu alimjia Huwaitib Bin Abdul Izzi na watu kadhaa kutoka viongozi wa Makkah na wakamtaka atoke basi akasema Mtume-Sala na amani ziwe juu yake Kwani kuna ubaya gani kwenu ikiwa mtaniwacha nikafanya Harusi kwenu ,na tukawaandalia Chakula na mkahudhuria kwenye chakula hicho,wakasema hatuna haja na chakula chako na uondoke kwetu,basi mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-akatoka akamuacha Maimuna kwenye uwangalizi wa Abuu Raafiy ambaye ni muachwa huru wake akaja nae mpaka sehemu iitwayo Sirfin,basi

huko ndipo mtume akamuingilia kisha Mtume wa ALLAH akarudi Madina"(822)

Na wakati mtume anatoka makkah alikutana na Binti ya Baba yake mdogo ambaye ni Hamza na alikuwa ni Yatima Ally akamshika mkono wake-Radhi za Allah ziwe juu yake-akampa Fatma na akamwambia Mchukue Bint ya Baba yako mdogo na mbebe basi wote kina Jafar na Zaid Bin Haritha wakawa wanapupia wamchukuwe mpaka wakapishana Ally Bin Abii Twalib -Radhi za Allah ziwe juu yake-kila mmoja anataka amchukue na amuhudumie kwa matumizi,basi wakapeleka ugomvi wao kwa Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- kila mmoja anataka malipo ya wema yake na kumlea ,basi mtume akampa haki Jaafar kwa kuwepo Mama yake Mdogo kwa Jaafar,na akasema "Mama Mdogo yupo katika nafasi ya Mama "(823)

Na huenda katika hili ni Ishara yakuwa mapenzi ya Mama mdogo yapo karibu sana namapenzi ya Mama,na atakuwa mtoto mdogo kwa mama yake mdogo ana raha zaidi na utulivu.

Vita vya Mu'uta (Jumaadatul Uula mwaka wa 8 Hijiria):(824)

Sambamba na kuukombowa mji wa Khaibar,Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- aliandika ujumbe kwenda kwa wafalme na viongozi akiwafikishia wito wa ALLAH na ilikuwa moja ya hizi Risala nizenyekuelekezwa kwa mtawala wa (Basra)katika mji wa Sham na kwa hakika mtume-Sala na amani ziwe juu yake-huu ujumbe kwa Haarith Bin Umair Al-azdiy ili aipeleke kwa mfalme wa Basra kwa upande Hiraqli (Al-Haarith Bin Abii Shamri Al-Ghassan) akakamatwa mjumbe wa Mtume-Sala na amni ziwe juu yake-na alipojuwa kuwa amebeba ujumbe kutoka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-basi akamuuwa pamoja na kuwa Mjumbe kwa kawaida hauwawi.(825)

Na alipojuwa Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- kuuliwa kwake alichukia na akakusanya jeshi lake idadi yake ni elfu tatu

miongonimwa waislamuna akawawekea kiongozi mwachwa huru wake ambaye ni Zaid Bin Harithat ,na ikiwa atauliwa basi ni Jaafar Bin Abii Twalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-na ikiwa atauliwa basi atashika uongozi Abdullah Bin Rawaahat -Radhi za Allah ziwe juu yake-(826) na ikiwa atauliwa basi waislamu waridhiane kati yao mtu mmoja na wamfanye kuwa ni kiongozi wao.(827)

Na alikuwa Khalid Bin Abii Twalib -Radhi zaAllah ziwe juu yake-pamoja na jeshi ni mgeni katika Uislamu ni mwanajeshi katika safu ya Mujaahidiina ,na Mtume -Sala na amani ziwe juu yake-akaliamrisha jeshi lielekee Pande za Sham ili kuwatia adabu na kuyatisha makabila ya kinaswara ya kiarabu,na kuonyesha nguvu za waislamu na kurudi tena mara nyingine katika mji wa Madina ,na kabla ya jeshi kuondoka Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake- alikutana nao na akawaamrisha kumcha ALLAH,na kawakumbusha kuhusu mafundisho ya dini yao wakiwa vitani,kisha akaikabidhi Bendera kwa Zaid Bin Haaritha-Radhi za Allah ziwe juu yake- na kawasindikiza na kuwaaga.(828)

Na jeshi lakafuata njia yenye kuelekea sehemu za Mji wa Sham(829)na jambo hili linamaanisha uchokozi wa moja kwa moja wa mara ya kwanza kwenye Falme za Roma na mipaka yake na kwa hakika Roma na Ghasasina walijuwa kuondoka kwa Jeshi basi wakandaa jeshi lingine la kukabiliana nalo,walishiriki katika jeshi hilo wasaidizi wao wa kiarabu miongoni mwa koo za Lughamiy na Bahraau na Judhaam na Baliy na jeshi hilo lilikuwa na wanajeshi wanaozidi idadi yao wapiganaji Laki moja na kwa hakika walikita kambi jeshi la Roma katika ardhi ya Balqaa ambayo ni Jordan ya sasa,na kwa hakika jeshi la waislamu lilijuwa mkusanyiko huo,basi wakataka wamuandikie mtume-Sala na amani ziwe juu yake-huenda akawaongezea ziada ya wapiganaji(830)lakini muda ulikuwa ni mfupi na maadui wapo karibu na hawatoweza kuwachelewesha,na wakati huo wanajeshi wa kiislamu wanahimizana wao kwa wao juu ya kupambana,basi wakakutana na

waroma katika sehemu iitwayo Mu'uta(831)basi wakapambana kishujaa na alikuwa mbeba Bendera ni zaid Bin Haarith-Radhi za Allah ziwe juu yake-((Basi akachukuwa Bendera Zaid akauliwa kisha akachukuwa Jaafar,akauliwa kisha akachuwa Abdullah Bin Rawaah akauliwa))(832) basi akachukuwa Bendera mmoja miongoni mwa Answaar kisha akawaita ili wakusanyike sehemu moja kisha akampa Bendera Khalid Bin Al-waliid(833)ambaye aliweza kwa msaada wa ALLAH kisha kwa uzoefu wake wa kijeshi kuirudisha safu ya waislamu,na kuwaongoza katika mapiganona kulirudishia jeshi nguvu na kuwaweka katika mpango kabambe ((Kisha akachukuwa Bendera Upanga miongoni mwa upanga wa ALLAH mpaka ALLAH akawapa ushindi))(834) na kwa hakika waislamu waliokoa hasara,liche ya tofauti kubwa iliyopo baina ya jeshi la maadui na jeshi la waislamu,ukipima kwa kipimo cha nguvu katika vita na kwa hakika alikuwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-akiwasifia hao mashahidi kwa sifa zilizokuwa nzuri na anasema kuhusu wao((Kinachonifurahisha mimi au kinachowafurahisha wao ni kuwa wao ni wa kwetu))(836)

Na kwa hakika Jeshi baada ya hapo lilirudi madina likiwa chini ya uongozi wa Khalid Bin Al-waliid-Radhi za Allah ziwe juu yake- pale ambapo ilikuwa hii ni vita ya kwanza ya jihadi kwake katika safu ya waislamu baada ya kusilimu kwake,na kwa hakika alitoa habari mtume Sala na amani ziwe juu yake-kwa watu wa Madina yalijiri kabla ya jeshi kufika,kwa hakika amepokea Al-bukhariy kutoka kwa Anas Bin Maalik-Radhi za Allah ziwe juu yake -(Kuwa mtume aliwatangazia watu msiba wa mbali wa kifo cha Zaid na Jaafar na Bin Rawaah kabla ya kuja habari zaobasi akasema:alichukuwa Bendera Zaid akauliwa kisha akachukuwa Jaafar akauliwa kisha akachukuwa Bin Rawaah akauliwa -hali yakuwa macho yake yakibubujika machozi-kisha akachukuwa Bendera Upanga miongoni mwa panga za ALLAH mpaka akawapa ushindi)(837)nao ni ushindi kama alivyouta Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-

Na kwa hakikaalihuzunika sana mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kwa kufa Jaafar na wengine na akawaombea Dua wote. ((Ewe mola wangu wa haki muwekee Jaafar Mbadala kwa watu wake kwa kitakachokuwa bora kuliko ulivyoweka mbadala kwa waja wako wema))(838) Basi baada ya hapo Abuubakar Swiddiq akamuowa Asmaa Bint Umair Mke wa Jaafar na akawalelea watoto wake baada ya kufa kwake ,kisha Asmaa akaolewa na Ally baada ya kufa Abu bakar -Radhi za Allah ziwe juu yake-na akawalelea watoto wake watokanao na Jaafar na Abuubakar.(839)

na amani ziwe juu yake-aliwasikia baadhi yao wakisema kuwaambia wao: Enyi wenye kukimbia hivi kweli mmekimbia hali uakuwa mpo kwenye njia ya ALLAH? Mtume akawajibu siyo wakimbizi haw bali wao ni wapambanaji kwa mapenzi ya ALLAH.(840) walikuwa ni washambuliaji popote wawao ni washambuliaji ,na mashambulizi hayo yalikuwa katika kuikomboa Sham katika vita vya Yarmouk kupitia mikono ya Khalid Bin Al-waliid na mfano wake-Radhi za Allah ziwe juu yake-ni miongoni mwa walioshiriki vita vya Yarmouk na kuboia nguvu za Roma ,na kuikomboa Damascas na Baitil Maqdis na miji mingine miongoni mwa miji ya Sham yenye Baraka.

alisema Mtume-Rehema na amni ziwe juu yake- kuhusu Ubora wa Mashahidi wa Mu'uta,na alikuwa akimuona Usaamat baada ya kufa baba yake Ambaye ni Zaid ,basi umuonea huruma na macho yake hutoka machoz ,vilevile wakati wanapokuwa anawaona watoto wa Jaafar Bin Abi twalib-Radhi za Allah ziwe juu yake- na kwa hakika alisema Mtume kuwa hao ni mashahidi,ni miongoni mwa watu wa peponi,na akasema kuwa Jaafar ana mbawa mbili peponi,basi akajulikana hivyo katia umma kwa sifa hiyo(841)

Fat-hu Makkah (Ramadhan 20 mwaka 8 Hijiria)

Yalikuwa miongoni mwa masharti ya Sulhul Hudaubiyat ((Kuwa mwenye kutaka kuingia kwenye mkataba wa Muhammad anaingia

na mwenye kutaka kuingia kwenye mkataba wa wa Maquraish anaingia)) basi wakaingia kabila la Khuzaa katika mkataba wa Mtume Sala na amani ziwe juu yake-na ukoo wa bani Bakri wakaingia kwenye mkataba wa maquraish(842) basi ukoo wa Bakri wakawafanyia Khuzaa uadui na maquraish wakawasaidia katika hilo,kitendo hicho kikazingatiwa ni kuvunja makubaliano kwa upande wa Maquraish,na kwa hakika alikuja mmoja wa viongozi wa Khuzaa naye ni Amrou Bin Saalim Al-Khuzaiy Akamsomea Mtume Beti akiwa anamuhimiza kupitia Beti hizo kuhusu makubaliano na kuwataka awasaidie kwa mujibu wa mkataba walioandikiana ,na haswa maquraish waliwasaidia washirika wao,na huu ni uadui dhidi ya washika walio pamoja na waislamu

Na alichokisema ni hiki:

Ewe Mola wangu hakika mimi nimwenye kumnasihi Muhammad.

Ushirika wa baba yetu na wa Baba yake ni watangu na tangu(843)

Basi nusuru hivi sasa na akuongoze ALLAH.

Na waite waja wa ALLAH waje na nguvu.

Mpaka mwisho wa Qaswidah.

Basi Mtume akasema nimenusuru ewe Amrou Bin Salim (844)kisha ukaja ujimbe mwingine kutoka katika kabila la Khuzaa wakitaka Nusura kutoka kwa Mtume-Sala na amani ziwe juu yake-hivyo akawapa ahadi,kisha Maquraish wakawa wamehisi hatari,na akaja mkubwa wao ambaye ni (Abuu Sufiani Bin Harbi) mpaka Madina ili kuweka upya makubaliano na mtume-rehema na amani ziwe ju yake-basi akaingia kwenye Nyumba ya Binti yake ambaye ni mama wa Waumini (Habibat Bint Abii sufian) hapo akiwa ni mkwe wa Mtume -Rehema na amni ziwe juu yake- na alipoingia chumbani kwa Bint yake Mama wa waumini Ummu Habibah akataka kukaa kwenye tandiko la Mtume basi Ummu Habibah akamwondolea lile

tandiko Basi Abuu Sufiyani akasema:Ewe bint yangu Sitambui hiviUmenichukia mimi ndiyo ukaniondolea tandiko au umelipenda tandiko kuliko ulivyonipenda mimi basi Ummu Habibah akasema:hapana bali ni Tandiko la Mtume wa ALLAH-Sala na amani ziwe juu yake-akasema:Namuapia ALLAH hakika utapatwa na jambo baya baada ya kuondoka kwangu,kisha Abuu Sufiani akamjia Mtume akamsemesha wala hakumjibu (845) Kisha akaja kwa Abuubakar ili amunganishe na Mtume akasema:mimi siwezi kufanya hivyo kisha akamsemesha Omar Bin Khattwab Radhi za ALLAH ziwe juu yake-akasema: mimi niwaombeeni kwa mtume wa ALLAH? namuapia ALLAH kama ingekuwa sina isipokuwa punje ningepigana nanyi kwa punje hiyo,kisha akamjia Ally akiwa na Fatma-Radhi za allah ziwe juu yao wawili- akasema kwa hakika Mtume ameazimia jambo ambalo siwezi kumsemesha kuhusu jambo hilo akamwambia Fatma -Radhi za Allah ziwe juu yake-Ewe Bint Muhammad je waweza kumuamrisha mwanao huyu (yaani Hassan) achukuwe dhamana ya kuondosha ugomvi ulokuwepo baina ya watu na atakuwa ni Bwana wa watu?akasema Fatma mwanangu huyu hakufikia umri wa kuweza kuchukuwa Dhamana ya kuweza kuamua ugomvi,na jambo lilipomuwia ugumu akamwambia Ally je unanishauri nini? Ally akamwambia:wewe ni mkubwa kwenye kabila la kinanah basi simama na uzunguke baina ya watu ukichukuwa Dhamana ya kuzuia magomvi baina yaokisha Rudi kwenye Ardhi yako,akasema je waonaje je hilo litaninufaisha chochote,Ally -Radhi za Allah ziwe juuyake akasema hapana ,lakini sioni njia nyingine itakayokufaa zaidi ya hiyo,basi Abuu Sufiani aksimama msikitini mbele ya watu na akasema:kwa hakika mimi nimechukuwa Dhamana ya kuzuia magomvi baina ya watu,na alipofika Makkah watu wake wakamwambia:Ally hakukuzidishia isipokuwa ni kukucheza Shere tu(846)

Kisha Mtume Sala na amani ziwe juu yake akawaandaa watu kwa ajili ya vita, na alikuwa na pupa kubwa kuwa makuraishi wasijue

habari za kutoka kwake, na akatuma moja kati ya vikosi vyake vya uchunguzi upande usiokuwa Makka, ili watu wadhania kuwa anakusudia kujiandaa kuelekea upande huo, na katika wakati huo huo aliwaeleza baadhi ya watu wake maalumu kuwa anakusudia kuelekea Makka akawataka waifiche habari hii akasema Ewe ALLAH wazuie majasusi wote na habari zote zisiwafikie Makuraishi ili tuwavamie.

Na katoka Mtume Sala na AMani ziwe juu yake kuelekea Makka ndani ya mwezi wa ramadhani akiwa na watu elfu tano katika muhajirina (Waliohama kutoka Makka) na Aswari (Waliowapokea katika mji wa Madina) na yakaungana naye makundi mengi mengi katika kabila la Muzaina na sulaim na Ghifari, na Juhaina, na Tamim, na Asadi, mpaka ikawa idadi ya jeshi lake alipokaribia Makka takribani wapiganaji elfu kumi (10,000) akashuka nao Mtume Sala na Amani ziwe juu yake eneo la Marru dhwharan.

Na Abbasi bin Abdil Muttwalib Radhi za allah ziwe juu yake akakutana na Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake naye akiwa njiani kuelekea Makka, akatangaza uislamu wake, na inasemekeana kuwa alikuwa akificha uislamu wake kabla ya hapo kwa muda mrefu, na ana baadhi ya matukio pamoja na Mtume Sala na Amani ziwe juu yake tangu tukio la baiatul akaba ya pili yakionyesha hivyo, na alikuwa Abbasi anapupa ya kutaka watu wake wasilimu, baada ya hapo akapanda nyumbu wa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake, na akaanza kutafuta wa kumtuma kwenda kwa Makauraishi Makka huenda wanaweza kumfuata Mtume Sala na Amani ziwe juu yake wakamuamini na wakasilimu, na alikuwa amewaamrisha waislamu wawashe mioto kwa wingi -na ulikuwa ni wakati wa usiku- ili wawahofishe watu wa Makka ili wasipigane nao, basi ikawashwa mioto takribani elfu kumi kwa wakati mmoja, Makuraishi walipoiona mioto hiyo, alitoka Abuu Sufiani ili apate habari na yeye ndiye alikuwa kiongozi wao, akakutana na Abbasi Radhi za ALLAH ziwe juu yake- Ami yake na Mtume Sala na Amani ziwe juu yake akamtuliza,

kisha akamuendea Mtume Sala na Amani ziwe juu yake naye akathibitisha amani aliyoisema Abbasi, na waislamu hawakumfanyia baya lolote, palipo pambazuka alikuja naye Abbasi Radhi za ALLAH ziwe juu yake- kwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake naye katangaza uislamu wake, kisha Abbasi akasema kumwambia Mtume Sala na Amani ziwe juu yake; Hakika Abuu Sufiani ni mtu anapenda ufahari kwa watu wake, laiti ungempa amani kila atakayeingia katika nyumba yake.

Alikuwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake anapupa kubwa sana yakuwa iwe kuingia kwake katika Mji wa Makka ni kwa amani, na asimwage damu, na ndiyo maana wakati wa kuingia kwake Makka aliligawa jeshi lake katika sehemu nne liingie katikapande zote nne za Makka, likionyesha nguvu yake, na kwa ajili ya kuwazuia watu, ili wajisalimisha watu wa Makka kulingana na hali halisi iliyopo na wajisalimisha kwa amani, na muda huo huo akatangaza Mtume Sala na Amani ziwe juu yake Yakuwa: Atakayeingia nyumba ya Abuu Sufiani basi huyo atakuwa na amani,, na atakayejifungia ndani kwake basi naye kasalimika, na atakayeingia msikitini basi naye kasalimika"²⁵⁸. Na kwa ajili hiyo alitoa fursa kubwa ya amani anayetaka kuingia katika uislamu, na akaingia Mtume Sala na Amani ziwe juu yake katika mji wa Makka kwa amani, na ikasimikwa bendera yake katika Mlima Hujuni²⁵⁹

²⁵⁸ Tazama: Fat-hul baari: juzuu 16/122, Bin Hisham, Siratun nbawiyya, juzuu 4/403, bin Kathiri, Siratu nabawiyya, Juzuu 3/549, Asswaalihi Shami, Subulu hudaa warrashaadi, Juzuu 5/330; bin Abii shaiba, Al Maghaazi, uk. 344.

²⁵⁹ Tazama Bukhariy (Fathul Baariy)juzuu ya 6/118

Na kilikutana kikosi cha Khalidi bin Walid -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- na kikosi cha Musailama kwa baadhi ya mashambulizi kutoka kwa wapiganaji wa kikuraishi washirikina kikosi ambacho haraka sana kilidondoka,²⁶⁰na washirikina wakakimbia kuelekea majumbani mwao au nje ya Makka. Na kulikuwa kuingia kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake ni kwa unyenyekevu kwa kutaka radhi za ALLAH, kwani alikuwa kainamisha kichwa chake, akiwa kamnyenyekea ALLAH Mtukufu,²⁶¹na alikuwa akisoma suratul fatihi,²⁶²kisha akaelekea katika Al-kaaba na akatufu katika nyumba hiyo mizunguko saba kisha akasema: "Hapana Mola isipokuwa ALLAH yeye pekee asiye na mshirika, ahadi yake imekuwa ya kweli,na kamnusuru mja wake, na kayashinda makundi yeye peke yake, tambueni kuwa kila damu au kisasi basi hivyo viko chini ya miguu yangu hii isipokuwa wahudumu wa Al-kaaba na watoa huduma ya maji kwa Mahujaji, kisha akasema: "Enyi jamii ya kikuraishi, mnadhani mimi nitakufanyeni nini? Wakasema tunataraji kheri kwani wewe ni ndgu mkarimu na mtoto wa ndugu mkarimu. Akasema Sala na Amani ziwe juu yake kauli yake mashuhuri: "Haya

²⁶⁰ Tazama Al Bukhari juzuu ya 16/119 na bin Hisham, Assiratun nabawiyya, Juzuu ya 4/407, bin kathiri, Assiratun nabawiyya, juzuu 3/560; bin Abii shaiba, Al maghazi, Uk. ص329.

²⁶¹ Tazama: Bin Hisham, Siratun nbawiyya, juzuu 4/405, bin Kathiri, Siratu nabawiyya, Juzuu 3/555, Asswaalihi Shami, Subulu hudaa warrashaadi, Juzuu 5/342.

²⁶² Al Bukhari, Fat-hul Baariy, 16/123; Bin Kathiri, Assiratun Nabawiyya, 3/555

nendeni kwani nyinyi mko huru²⁶³. Kisha akamuita muhudumu wa Al-kaaba akachukua funguo toka kwake, akafunguliwa Al-kaaba,²⁶⁴ akakuta ndani yake kuna mapicha akaamrisha yakafutwa, kisha akayazungukia masanamu katika nyumba tukufu, na yalikuwa masanamu mia tatu na sitini, kwa kuendana na idadi ya siku za mwaka mzima, na alikuwa akiyaashiria huku akisoma:

﴿وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَرَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا﴾ [الإسراء: 81]

Sema ewe-MUHAMMAD-ukweli umekuja na uwongo umeondoka hakika uwongo umekuwa wenye kuodoka. [Al Israai: 81]. Akayaporomosha yote, na akaamrisha yakavunjwa vunjwa.²⁶⁵ Na hakuacha Mtume Sala na Amani ziwe juu yake chochote katika masanamu ila kilivunjwa, wala picha yoyote isipokuwa ilifutwa.²⁶⁶

Na imepokelewa kutoka kwa bin Abii Shaiba kwa isnadi sahihi yakwamba Mtume Sala na Amani ziwe juu yake aliingia Makka kwa ajili ya ibada ya Umra akiwa amevaa shuka nyeusi, akatufu katika Al-kaaba akiwa juu ya mnyama wake aitwaye Al-kas-waa, na katika mkono wake kukiwa na mkongojo akizielekea nguzo, hakuchukua

²⁶³ Bin Hajari Al Asqalaaniy: Fat-hul Baari, 16/129; bi Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/411,412, bin Kathiri, Al Bidaaya wan nihaaya, 3/570; Asswaalihi shami, subulu hudaa warrashaadi, 5/364

²⁶⁴ Al-Bukhariy, Fathul Baariy juzuu ya 16/128; Tazama Bin Abii Shaibah ukurasa wa 323.

²⁶⁵ Al-Bukhariy, Fathul Baariy juzuu ya 16/127 Tazama Bin Abii Shaibah ukurasa wa 333.

²⁶⁶ Bin Abii shaibah, Al Maghaazi, uk 334, 341.

muda mrefu ngamia wake akapata mahala pa kutua katika msikiti mpaka akashuka katika mikono ya wanaume, kisha wakamtoa ngamia huyo mpaka wakamsimamisha katika bonde, kisha Mtume Sala na Amani ziwe juu yake akawahutubia watu, akamhimidi ALLAH na akamsifia kwa sifa anazostahiki, kisha akasema: "Enyi watu hakika ALLAH amewafutieni yale makosa ya aibu ya zama za ujinga na kuyatukuza kwa sababu ya kuwafuata baba zenu", watu ni aina mbili, kuna mwema mkarimu kwa ALLAH, na kafiri muovu dhalili kwa ALLAH, enyi watu hakika ALLAH anasema:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾﴾ قَالَتِ الْأَعْرَابُ ؕ آمَنَّا قُلْ لَمْ نُؤْمِنُوا وَلَكِنْ قُولُوا أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الْإِيمَانُ فِي قُلُوبِكُمْ وَإِنْ تُطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ لَا يَلِتْكُمْ مِنْ أَعْمَالِكُمْ شَيْئًا إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٤﴾﴾ [الحجرات: 13-14]

Enye watu hakika sisi tumekuumbeni kutokana na mwaume na mwamke na tukawajalia mataifa na makabila ili muweze kutambuana hakika mbora wenu mbele ya ALLAH ni mchaji mungu wenu hakika ALLAH ni mjuzi muelezaji. Wamesema mabedui tumeamini sema-ewe MUHAMMAD-hamja amini isipokuwa semeni tumejisalimisha na bado haijaingia imani ndani ya nyoyo zenu na kama mtamtii ALLAH na mtume wake hakuna chochote kitakacho pungua katika malipo yenu. [Hujurat: 13-14] Ninasema maneno haya na ninamuomba Allah msamaha kwangu na kwenu, kisha akavuka mpaka kando ya msikiti, akachukua ndoo ya maji ya Zamzam akaosha uso wake na hakuna tone la maji isipokuwa lilidondoka katika mkono wa mtu, na yakidondokea kwenye mtungi wa maji basi walikuwa wakiwanywa na wakati mwingine walikuwa maswahaba wakijifuta kupitia mtungi huo, na washirikina wakitazama, wakasema: Hatujawahi kuona Mfalme kama huyu katu hata siku moja, na hatujawahi kuona watu wapumbavu kama hawa, kisha akamuamrisha Bilali akapanda juu ya Al-kaaba, akaadhini kwa

ajili ya swala, na watu wakasimama wakatoa vikoi na ndoo zikachukuliwa wakaelekea katika Zamzam kuchota maji wakiiosha Al-kaaba nje na ndani yake, hawakuacha alama yoyote ya washirikina isipokuwa waliifuta au waliiosha kwa maji²⁶⁷.

Na katika riwaya hii kumetajwa sifa za ndani sana za vitendo vya Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na hotuba yake baada ya ufunguzi wa mji wa Makka.

Kisha wakampa ahadi ya utiifu (Baiya) wale walioweza kumpa ahadi hiyo miongoni mwa wanaume juu ya uislamu, kisha wakachukua ahadi wanawake juu ya uislamu na juu ya sharti zingine ambazo ni maalumu kwa ajili yao,²⁶⁸na ilifika swala ya adhuhuri akanyanyua Bilali sauti ya haki (Adhana) juu ya Al-kaaba akitangaza kwa kusema 'Allaahu Akbar' ALLAH Mkubwa, Ninashuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH, Ninashuhudia kuwa Muhammadi ni Mtume wa ALLAH. Na walichukia baadhi ya wageni katika uislamu miongoni mwa Makuraishi walipoona na wakasikia hivyo (asiye mwaarabu kupewa nafasi kubwa), kisha wakajuta kwa maneno waliyoyasema baada yakuwa wameufahamu vizuri uislamu wao.²⁶⁹Hivi ndivyo Makka ilivyosafishika kutokana na ushirikina, na ikamalizika nguvu yake ya kupingana na uislamu, na ikawa ni moja kati ya miji ya kiislamu, bali

²⁶⁷ Bin Abii Shaiba Al-maghaaz ukurasa 341.

²⁶⁸ Al-swaalihiy, Al-shaamiy,Subulul hudaa wa Al-rashaad juzuu ya 5/371.

²⁶⁹ Tazama: Bin Hisham, Siratun nbawiyya, juzuu 4/413, bin Kathiri, Siratu nabawiyya, Juzuu 4/575, Asswaalihi Shami, Subulu hudaa warrashaadi, Juzuu 5/372.

ni mji muhimu zaidi, kiasi ambacho aliupangilia Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na akamteua Itaaba bin Asiid kuwa kiongozi²⁷⁰

Alitoa kipaumbele kikubwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kwa watu wa Makka kuwafundisha uislamu, kiasi kwamba alibakia kwao siku kumi na tisa,²⁷¹ baada ya hapo aliondoka kwenda kukutana na makabila mawili, kabila la Thakifu na Hawazin, ambayo yalikuwa yamejiandaa kupigana na Mjumbe wa ALLAH Sala na Amani ziwe juu yake baada ya ufunguzi wa Mji wa Makka, na ufunguzi wa Makka ulikuwa ni sababu kubwa ya kupunguza makali ya waarabu katika kuupiga vita uislamu, kiasi kwamba baada ya hapo watu waliingia katika uislamu makundi kwa makundi,²⁷² baada ya Makuraishi kuingia ndani yake (uislamu) na kuporomoka kwa nguvu kubwa ya ushirikina iliyokuwa ikiupiga vita uislamu. Na amesema kweli ALLAH Mtukufu:

﴿إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿۱﴾ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿۲﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿۳﴾﴾ [النصر: 1-3]

Pindi itakapo kuja nusra ya ALLAH na ushindi. Na ukawaona watu wanaingia ndani ya dini ya ALLAH kwa makundi. Basi tukuza kwa sifa za MOLA wako na umtake msamaha hakika yeye amekuwa ni mkubali tauba. [An Nasri: 1-3]

²⁷⁰ Bin sa'd, Atwabaqaatil kubraa, 5/446; na bin Hajar, A iswaaba, 2/452 na Twabarii, taariikh yake, 3/162.

²⁷¹ Sahihi Bukhari (Fat-hul Bari) 16/132

²⁷² Sahihi Bukhari ,Fat-hul Baar,ujzuu ya 16/134.

VITA VYA HUNAINI NA TWAIF (SHAWAL MWAKA 8H): [867]

Lilijipanga kabila la Hawazin, na hasa hasa kabila la Thakif, kukutana na waislamu baada yakuwa wameukomboa mji wa Makka, na likatoka pamoja nao kabila la Ghat-fan na makabila mengine, na wakatoka pamoja na watoto wao na vizazi vyao ili wajizaatiti katika mapambano na kukabiliana na Mtume Sala na Amani ziwe juu yake yeye pamoja na wale alionao katika waumini,²⁷³ na akafuatilia Mtume Sala na Amani ziwe juu yake ili kujua ukweli wa taarifa hizo, akatoka na jeshi lililofanya ufunguzi, nao walikuwa ni wapiganaji elfu kumi (kama ambavyo pia walitoka pamoja na Mtume Sala na Amani ziwe juu yake watu elfu kumi katika wale aliowaacha huru)²⁷⁴ wale waliosilimu wakati wa ufunguzi, mpaka ikafikia baadhi yao wakadanganyika kwa wingi wao na wakasema: Hatutoshindwa leo kwa sababu ya uchache, na akaazima Mtume Sala na Amani ziwe juu yake silaha kutoka kwa Ya'la bin Umaiya kwa kuweka rehani kitu, na alikuwa huyu bwana ni katika wageni katika uislamu, kisha akamrejeshea baada ya vita na akamshukuru kwa hilo.²⁷⁵

Na lilikuwa kabila la Hawazini limejikusanya katika eneo la Hunaini likiongozwa na Maliki bin Aufu, na aliwaamrisha watu wake wabebe wake zao na mali zao ili kitendo hicho kiwe ni msukumo kwa wao kuwa imara wakati wa mapambano, na Duraidi bin Sumat alimdhalilisha Maliki na yeye alikuwa pamoja na kabila la Hawazini, (ukweli nikuwa huyu) mzee hawezi kusaidia lolote lakini alikuwa ni

²⁷³ Tazama: Al Bukhari, Fat-hul Bari 16/172; bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 3/438

²⁷⁴ Sahihi Bukhari (Fat-hul Bari) 16/172

²⁷⁵ Tazama: Uchambuzi riwaya hiyo kwa: Rizqullah, Assiiratun nabawiyya, uk 583

mtu mwenye hekima, na ilikuwa miongoni mwa maneno aliyoyasema kumwambia: 'Hakika mapigano haya kama utashinda hakutokuwa na faida yoyote kwako isipokuwa kumuua mtu yeye na upanga wake na mshale wake, na ikiwa utashindwa utafedheheka kwa watu wako na mali zako.²⁷⁶

Na wakaingia waislamu katika bonde la Hunaini, na hawakujua kuwa wale watu walijificha, na hiyo ni ilikuwa ni wakati wa mapambazuko ya asubuhi, na jeshi la waislamu lilikuwa kubwa, na ndani yake kulikuwa na makabila mengi na wale walioachwa huru na wengine wengi wakiwemo Muhajirina (waliohama kutoka Makka) na Maanswari (watu wa Madina), na lilivamiwa jeshi la waislamu kwa mashambulizi ya ghafla kutoka katika kabila la Hawazini, wakasambaratika wale waliokuwa mbele hasa hasa kabila la Tamim, na wale walioachwa huru katika watu wa Makka, na safu za jeshi zikaparaganyika, akasimama imara Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akiwa pamoja na baadhi ya Muhajirina na Maanswari, akiwemo Ammi yake Al-Abbas na Abuubakar na Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao, na akageuka Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake upande wa kulia na akaanza kuita kwa sauti: "Akaita mara mbili bila kuchanganya kati ya wito na wito, aligeuka kuliani kwake na akasema: Enyi kongamano la maanswari, wakasema Labeka (Tumekuitikia) ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kuwa na matumaini sisi tuko pamoja nawe. Naye Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akiwa juu ya nyumbu mweupe, akashuka akasema: "Mimi ni Mja wa Mwenyezi Mungu na ni Mtume wake,²⁷⁷Enyi watu njooni kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mimi ni

²⁷⁶ bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 3/438; Asswaalih Shami, subulul Huda warrashad 5/460.

²⁷⁷ Sahihi Bukhari ,Fat-hul Baar,ujzuu ya 16/172.

Muhammadi bin Abdillah, kisha akamuamrisha Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake Ammi yake Abbasi na alikuwa ni mtu mwenye sauti kubwa anadi kwa sauti, Enyi kundi la Maanswari, enyi watu wa samra, na alikuwa akinadi Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake "Jamani mimi ni Mtume wala si uongo, mimi ni mtoto wa Abdul Muttwalib",²⁷⁸, Muhajirina na Maanswari walipousikia wito walijibu Tumekuitikia Tumekuitikia, wakakusanyika kwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake, akawaelekea maadui kupitia maswahaba. Na mapambano yakapamba moto kati ya waislamu na kabila la Hawazini, mpaka akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Hivi sasa mapambano yamepamba moto",²⁷⁹Yeye ndiye mtu wa kwanza kusema neno hilo.²⁸⁰Na wakapigana waislamu wakiwa pamoja na Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake mapigano ya mashujaa, na akachukua Mtume choto la mchanga akawamwagia hao watu huku akisema: "Macho yamekodoka",²⁸¹ Wakaelemewa. Na baada ya muda mfupi kukathibitika kushindwa katika safu ya maadui na waislamu wakarudi na mateka na ngawira,²⁸²Na wakauawa katika

²⁷⁸ katika riwaya za Bukhari, Fat-hul Bari 16/143; N atazama bin Hisham, Assiratun nabawiyya 3/444, 445; Asswalihi shami, Subulul hudu warrashadi 5/471, bin Abii shaiba, Al-Maghazi, uk. 378

²⁷⁹ Bin Hisham, Assiratun nabawiyy, tazama: Rizqullah, Assiratun nabawiyya, uk 58.

²⁸⁰ Tazama: Assuhailiy, Arrraudhul anif, 4/138

²⁸¹ Kaipokea Muslim, tazama: Rizqullah, Assiratun nabawiyya, 589.

²⁸² Sahihi Bukhari ,Fat-hul Baar,ujzuu ya 16/172.

maadui zaidi ya wanaume sabini (70), na wakafa mashahidi kundi katika waislamu.²⁸³

Na akatuma Mtume vikosi kwa ajili ya kuwafuata wale walioshindwa vita, ili wawamalize au wausambaratishe umoja wao, na wakafaniiwa wajumbe wa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake, na akaamrisha Sala na Amani ziwe juu yake ngawira na mateka vikakusanywa katika eneo la Jirana.²⁸⁴ Na baada ya mambo kutulizana aliendelea na safari Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kuelekea Twaif, ambako ndiko makao makuu ya kabila la Thakifu ambalo ndilo kabila lililokusanya kabila la Hawazini kwa ajili ya kumpiga vita Mtume Sala na Amani ziwe juu yake.

Na mji wa Twaif ulikuwa umetiwa ngome ya uzio inayouzunguka na ndio sababu ya kuitwa hivyo,²⁸⁵ na ndio maana hakuweza Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kuuvamia, akauzingira takribani siku ishirini,²⁸⁶ na akatundika kombeo aliloshauri Salman Al Farisi, na

²⁸³ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/449.

²⁸⁴ Tazama: Bin Hajari, Fat-hul bari 16/162, bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/488: (Na Jirana ni eneo lililoko mashariki mwa Makka njia ya Twaif ya mwendo kasi, njia ya pembeni iko wazi kwa mwenye kutazama barabarani) kitabu Al-bilad, Mujamul Ma'alim Al Joghrafia katika Siratun nabawiyya, uk 83.

²⁸⁵ Yaaqut Al-hamawiy, Mu'jamul buldan 4/9, na tazama: Dr. Abdul jabbar Munsiy Al-ubaidiy, Attwaaif wa dauru Qabiilat Tha'qif Al-Arabiya, uk 16.

²⁸⁶ Na wako katika wanahistoria waliona mtazamo tofauti na huo katika muda wa kuzingirwa Twaif, Tazama: Asswaalih Shami, subulul

akalirusha lakini halikuleta madhara kwa wakazi wake,²⁸⁷na wakafa mashahidi kundi la maswahaba kwa sababu ya mishale waliokuwa wakirushiwa waislamu kutoka kwa watu wa Twaif na wengineo.

Na walijaribu baadhi ya waislamu kuivamia ngome kwa kutumia kitu mfano wa vifaru walivyovitengeneza kutokana na mbao na ngozi, walivamia ndani na wakaukaribia uzio, wakavirushia mishale watu wa Twaif ya vipande vya vyuma vilivyochocheo kwa moto, vikaunguza zile ngozi, na vikaziathiri zile mbao, wakatoka waliokuwemo ndani miongoni mwa wapiganaji wa kiislamu, wakawarushia mishale juu ya uzio wakaua mtu mmoja.²⁸⁸Na wakashuka baadhi ya watumwa wa watu wa Twaif kwa waislamu na wakatangaza uislamu wao Mtume Sala na Amani ziwe juu yake akawaacha huru.²⁸⁹Kisha Mtume Sala na Amani ziwe juu yake baada yakuwa wamewazingira kwa muda mrefu akawaeleza Maswahaba kuwa yeye hajapewa idhini ya kuifungua Twaif, na akaondoka na akaiacha si kwa sababu ya kukata tamaa, bali ni kwa sababu ya ya kutamani watu wa Twaifu waje hali yakuwa ni waislamu kwa hiyari

huda warrashadi, 5/565, Dr. Akram Al Omariy, Assiratu sswahiiha, 2/507, Rizqullah, Assiratun nabawiyya, uk. 596

²⁸⁷ bin Hisham Assiratun nabawiyya, 4/483, Tazama: Asswaalih Shami, subulul hudā warrashadi, 5/560, Dr. Akram Al Omariy, Assiratu sswahiiha, 2/509, Rizqullah, Assiratun nabawiyya, uk. 596

²⁸⁸ bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/483; Asswaalih Shami, subulul Hudā warrashad 5/561

²⁸⁹ Tazama sahihi Bukhari (Fathul Baari, juzuu ya 16/161; Bin Hisham ukurasa wa 4/485) As-waalihiy, Al-shaamiy, Subulul hudā wa Al-rashad juz 5/562.

yao toka ndani ya nafsi zao, kiasi kwamba aliwaombea na akasema: "Ewe ALLAH waongoze watu wa kabila la Thaqif" Na akaelekea Makka Mtume Sala na Amani ziwe juu yake na akasimama katika barabara ya Ji'ranan, palipokuwa na ngawira na mateka kutoka katika kabila la Hawazini na jamaa zao, na hapo Ji'rana alikaa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kusubiri mawasiliano kutoka kwa watu wa kabila la Hawazini au watubie na kuomba msamaha kwa yale yaliyotokea kati yao na waislamu, baada ya kupita siku kadhaa za kusubiri aliamua Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kugawa ngawira na mateka kwa waislamu. Kisha ukaja msafara kutoka katika kabila la Hawazini ukatangaza uislamu wake na toba yake kutokana na yale yaliyojitokeza kutoka kwao dhidi ya Mtume wa ALLAH na wale aliokuwa nao katika waislamu na wakamtaka Mtume Sala na Amani ziwe juu yake awarudishie mali zao na watoto wao, na akasema mmoja kati ya washairi wao ubeti katika wimbo mrefu akiomba utetezi na msamaha kutoka kwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kipande chake ni:²⁹⁰

Tuneemeshe ewe Mjumbe wa ALLAH katika ukarimu.

Kwani wewe ni mtu tunayetaraji mazuri kwake na kuwekeza²⁹¹

Akawapa hiyari Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kati ya kuchukua mali zao, au watoto wao na wake zao, wakachagua kuchukua watoto wao na mali zao Akasema Sala na Amani ziwe juu yake: "Wako nami hawa mnaowaona, na mazungumzo

²⁹⁰ Tazama: Uchambuzi riwaya hiyo kwa: Rizqullah, Assiiratun nabawiyya, uk 596

²⁹¹ Tazama kasida nzima: Katika kitabu cha Assalihi Shamiy, Subulul Huda warrashadi 5/571

yanayopendeza zaidi kwangu ni yale ya kweli, na nilikuwa nimekusubirieni", na alikuwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake amewapa muda takribani siku kumi pindi alipokuja kutoka twaif, walipofahamu kuwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake hana haja nao isipokuwa anahitaji moja kati ya makundi mawili, wakasema: Hakika sisi tunachagua mateka wetu, akasimama Mtume Sala na Amani ziwe juu yake akamsifia ALLAH kwa sifa anazostahiki, kisha akasema: "Ama baada ya hayo, hakika ndugu zenu wamekujieni huku wakitubia, na mimi nimeona niwarudishie mateka wao, yeyote litakayempendeza hilo basi na afanye, na atakayependa miongoni mwenu kuendelea kubaki katika miliki yake mpaka tumpe katika mali ya fai (ngawira ya bila vita) atakayotupa ALLAH basi na afanye, watu wakasema: Tumeridhika toka kwako ewe Mjumbe wa ALLAH"²⁹².

Na walifanya haraka waislamu kujivua katika mafungu yao kuanzia katika mateka kwa kumuiga Mtume Sala na Amani ziwe juu yake, kisha akawausia Mtume Sala na Amani ziwe juu yake watu wa kabila la Hawazini, na akasema kuwaambia: "Muelezeni Maliki bin Auf (Yaani mkuu wa kabila la Hawazini) ikiwa atakuja kwa lengo la kuwa muislamu basi nitamrudishia familia yake na mali zake na ziada ya ngamia mia moja", akatoka Twaif kwa siri na akaja kwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake akasilimu na ukawa mzuri uislamu wake, na Mtume akamteua kuwa kiongozi wa yeyote atakayesilimu katika makabila yanayoizunguka Twaif, na akaanza kuwabadilisha katika viuga vya washirikina wa kabila la Thakif mpaka akawabana wakakosa njia.²⁹³.

²⁹² Ni katika hadithi za Bukhari (Fat-hul Bari), 16/145-147.

²⁹³ Siirat Nabawiyat Bin Hishaam juzuu ya 4/491 na bin kathiri Siirat Nabawiyat, juzuu 3/683

Na alipogawa ngawira Mtume Sala na Amani ziwe juu yake aliyapa baadhi ya makabila sehemu katika ngawira hiyo na wageni katika uislamu kuanzia wale waliosilimu wakati wa ufunguzi wa Makka na wengineo, na hakuwapa chochote Maanswari (watu wa Madina) wakaingiwa na kitu baadhi yao ndani ya nafsi zao, akawakusanya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake wao peke yao, na akawahutubia: Na ilikuwa miongoni mwa yale aliyoyasema: "Enyi maanswari, hivi sikuwakuteni wapotevu akakuongozeni ALLAH kupitia mimi? Na mlikuwa hamuelewani akakuunganisheni ALLAH kupitia mimi? Na mlikuwa masikini akakutajirisheni ALLAH kupitia mimi?" Akawa kila anaposema jambo wanasema: ALLAH na Mtume wake ndio wenye neema. Akasema: "Ni kipi kinachokuzueni kumjibu Mjumbe wa ALLAH? Akasema: "Na laiti mngetaka basi mngesema kadhaa wa kadhaa. Hivi hamridhii nyinyi watu waondoke na mbuzi na ngamia na nyinyi muondoke na Nabii katika majumba yenu? Lau kama isingekuwa kuhama basi mimi ningekuwa ni katika maanswari, na laiti kama watu wangepita katika bonde na wakapita njia za milimani basi mimi ningepita bonde na njia ya maanswari, maanswari ni nembo na watu nembo yao ni vazi"²⁹⁴. Maswahaba wakalia mpaka wakalowanisha ndevu zao na wakasema: "Ndivyo hivyo, tumeridhika kwa mgao wa Mjumbe wa ALLAH na fungu alilogawa, na wakasambaa"²⁹⁵Kisha akatia nia Mtume Sala na Amani ziwe juu yake ya umra hapo hapo Ji'rana, na akaingia Makka, na akabaki huko kwa siku kadhaa, baada ya hapo akaondoka kwenda Madina, na baada miezi kadhaa uislamu ukawa mwingi pembezoni

²⁹⁴ Sahihi Bukhari,(Fat-hul Baar) juzuu ya 16/196.Tazama Bin Abii Shaibah,Al-Maghaaziy ukurasa 387.

²⁹⁵ Tazama Al bukhari: (Fathul bari) 16/171, na sherhe ya bin Hajari katika hadithi, na bin Athiri, Al-kaamil, 4/272.

mwa Twaif na kwa watu wake. Kisha ukaja msafara katika wao kwa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake, na akayasikiliza Mtume Sala na Amani ziwe juu yake mazungumzo yao, na yakamalizika mazungumzo hayo kwa watu kuingia katika uislamu, na mji wao wote kuingia katika uislamu na wakayavunja vunja masanamu²⁹⁶.

Na kwa kusilimu Twaif miji yote ya Hijazi ikaanza kuinyenyekea serikali ya Utume, ikiongozwa na viongozi aliowateua Mtume Sala na Amani ziwe juu yake.

Na ziliteremka baadhi ya aya zikizungumza kuhusu vita vya Hunaini, miongoni mwake ni kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَصَافَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحَبَتْ ثُمَّ وَابَّتْ مُدْبِرِينَ ﴿٢٥﴾﴾ [التوبة: 25]

Na hakika alikunusuruni ALLAH katika sehemu nyingi na siku ya -vita-vya hunaynipindi ilipo kuwastaajabisha wengi wenu na wala hakuwasaidia chochote na ikawabana ardhi juu yenu kwa ule upana wake kisha mkakimbia kurudi nyuma. (Attauba: 25)

VITA VYA TABUK: (RAJAB: MWAKA 9H) [892].

Yalikuwa matukio ya vita vya Muuta vilivyotokea kati ya waislamu na warumi na wasaidizi wao miongoni mwa Wakristo wa kiarabu Mwaka (8H) Ndio mwanzo wa kichocheo kati ya waislamu na warumi, kikabakia kimekita katika akili ya Mtume Sala na Amani ziwe juu yake, kwani walikufa mashahidi kundi kubwa la maswahaba.

²⁹⁶ Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 3/537, 541, na tazama Dr. Akram Al-Omari, Assiratu sswahiha, 2/512, Dr Rizqullah, Assiratun nabawiyya uk 659, na tazama: Msafara wa Twaif katika kitabu hiki

Na akaazimia Mtume Sala na Amani ziwe juu yake kupigana na warumi kulingana na kauli yake Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَاتِلُوا الَّذِينَ يَلُونَكُمْ مِنَ الْكُفَّارِ وَلْيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً وَأَعْلَمُوا أَنَّ
اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ﴾ [التوبة: 123]

Enye ambao mlio amini wapigeni wale ambao wanao kufuateni miongoni mwa makafiri na wapate kutoka kwenu dhiki na tambueni kuwa ALLAH yupo pamoja na wenye kumuogopa. [Attauba: 123] Na ndiyo maana vita hivi vilielekezwa tangu mwanzo moja kwa moja na kwa uwazi dhidi ya warumi, na ndiyo maana Mtume Sala na Amani ziwe juu yake alipowahamasisha waislamu kwa ajili ya vita hivi aliwaeleza wazi kuwa mashambulizi hayo yanaelekezwa pande za miji ya warumi.²⁹⁷Na alikuwa anajua wazi kuwa warumi wana majasusi miongoni mwa wanafiki wa mji wa Madina, kama ambavyo alitaka jeshi lake lijiandae, kwani safari ni ndefu, na hali ya hewa ilikuwa joto sana, na miji ina ukame, na watu wako na hali ngumu, na matunda ya Madina kama tende na zabibu yamekaribia kuvunwa,²⁹⁸na watu walikuwa wakiyasubiri mwaka mzima, na kwa ajili hiyo kutoka kwenda Tabuk ilikuwa ngumu sana.

Lakini pamoja na hivyo wanafiki walitumbukia katika dimbwi la uongo, kwani walianza kutoa nyudhuru za kuto kutoka pamoja na Mtume Sala na Amani ziwe juu yake za uongo na uzushi.

²⁹⁷ Tazama: Hadithi aliyoipokea Bukhari kutoka kwa ka'bu bin Maliki: Al-Bukhari (Fat-hul Bari) 16/242.

²⁹⁸ Anwani ya Bukhari kwa vita hivi (Mlango wa vita vya Tabuk navyo vita vya wakati mgumu), Fat-hul bari 16/237, na tazama: bin Abii shaiba, Al Maghaazyi, uk 398.

﴿وَمِنْهُمْ مَّنْ يَقُولُ أَذِّنْ لِّي وَلَا تَفْتِنِّي ۗ أَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ

بِالْكَافِرِينَ﴾ [التوبة: 49]

Na kuna miongoni mwao wapo wanao sema nipe idhini na wala usinifitinisha sikilizeni kwenye fita wameporomoka na hakika moto wa jahannama hakika ni mwenye kuwazingira makafiri. [Attauba: 49],²⁹⁹Na walihamasishana wanafiki kupingana na Mtume Sala na Amani ziwe juu yake na kuto kutoka pamoja naye katika kipindi cha joto kali,ALLAH anasema kueleza habari yao.

﴿فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ بِمَقْعَدِهِمْ خِلَافَ رَسُولِ اللَّهِ وَكَرِهُوا أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ﴾ [التوبة: 81-82]

Wamefurahi wanao kwenda kinyume na mtume wa ALLAH na wamekarahika kuto pigania kwa mali zao na nafsi zao katika nji ya ALLAH na wakasema msitoke kwenye joto sema-ewe MUHAMMAD-moto wa jahannama ndio wenye joto kali. Basi wacheke kidogo na walie sana ni malipo kwa yale waliyo yachuma. [Attauba: 81-82]³⁰⁰

Na akawaita Mtume Sala na Amani ziwe juu yake maswahaba zake kwa ajili ya kujitolea katika vita hivi, wakaenda mbio matajiri katika maswahaba kulitekeleza hilo na wa kwanza wao ni Abuubakari na Omari na wengineo -Radhi za ALLAH ziwe juu yao- na akatoa Othman -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- Sadaka kubwa

²⁹⁹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/516.

³⁰⁰ Tafsiir Bin Kathiir juzuu2/898.

ambayo ndani yake kulikuwa na ngamia mia tatu na dinari elfu moja, mpaka Mtume Sala na Amani ziwe juu yake akasema: "Hakitomdhuru Othman chochote atakachokifanya baada ya leo". Na akasema kuhusu yeye: Kama alivyosema Sala na Amani ziwe juu yake: Kama alivyosema Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- "Ewe ALLAH mridhie Othman kwani mimi niko radhi naye"³⁰¹Na walikuja watu katika waislamu kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- nao wakiwa ni watu wenye uhitaji, na wakiwa na hamu ya kutoka pamoja na Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- lakini shida zimewazuia na kutopata kipando. wakaeleza shida zao kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, akasema kuwaambia: "Sina kipandwa cha kukubebeni", Wakarejea huku macho yao yakibubujika machozi,³⁰² na wakaja wenye kutaka udhuru katika waarabu ili watoe udhuru.³⁰³

Na maswahaba watatu wakakwepa kwa sababu ya uvivu, na huku wakitaka kuungana na Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, lakini walikuwa wakweli katika kueleza hali zao, ALLAH akawasamehe³⁰⁴.

Amesema ALLAH Mtukufu:

³⁰¹ Ni katika hadithi za Bukhari (Fat-hul Bari), 14/195

³⁰² Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 3/518.

³⁰³ Tafsiir Ibnu Kathiir juzuu 1/uk902

³⁰⁴ Tazama: Hadithi ya Ka'b bin Maliki kwa Bukhari (Fat-hul Bari), 16/241; na kwa bin Abii Shaiba katika Maghaaziy, uk 398.

﴿لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى التَّيِّبِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ مِنْ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبَ فَرِيقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ إِنَّهُ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٧﴾ وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خَلَقُوا حَتَّىٰ إِذَا ضَاقَّتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنْفُسُهُمْ وَظَنُّوْا أَنْ لَا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١١٨﴾﴾ [التوبة: 117-118]

Hakika ALLAH amemsamehe mtume na muhajirina na maanswar na wale walio wafuata katika kipindi kizito baada ya mioyo kukaribia kupondoka kikundi miongoni mwao kisha ALLAH akawasamehe hakika yeye kwa wao ni mrehemevu mpole. Na wale-maswahaba-watatu ambao walicheleweshwa kukubaliwa Toba mpaka ardhi ikawa dhiki kwao pamoja na upana wake na nyoyo zao zikadhikika na wakadhani hakuna makimbilio kutoka kwa ALLAH isipokuwa ni kwake kisha akawasamehe ili waweze kutubia hakika ALLAH ndiye mwenyekukubali msamaha na nimpole. [Attauba: 117-118].

Vita hivi vilikuwa ni mtihani kwa jamii ya kiislamu kwa matajiri wao na masikini wao waumini na wadhaifu wa imani miongoni mwao, kama walivyokuwa baadhi ya wanafiki na wengineo katika mayahudi na nafasi kubwa ya kukwamisha, na kila safu ilikuwa na msimamo wake na matukio yake, na vita hii ilikuwa ndio vita ya mwisho katika vita vya Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na umri wake ulikuwa umesogea, kwani alikuwa kavuka miaka sitini katika umri wake Sala na Amani ziwe juu yake, lakini pamoja na hivyo alikuwa na pupa ya kuviongoza vita hivi yeye mwenyewe, kwani inachukuliwa chanzo cha vita hivi vya waislamu ni miji ya Roma, na katika ulimwengu mzima wa kiislamu.

Walikusanyika katika waislamu wapiganaji elfu thelathini alitoka nao Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- walikuwa miongoni mwao

wapanda Farasi elfu kumi,³⁰⁵Na jeshi hili linahesabika kuwa ndio jeshi kubwa la waislamu kuwahi kukusanyika katika uhai wa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, na waislamu wakaanza kutembea kuelekea katika njia ya Tabuk, na wakapita katika miji ya Swaleh (Nabii),³⁰⁶akawaamrisha Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kutembea haraka na wasiingie katika nyumba zao ila wakiwa wanalia au wakijiliza.

Na aliendelea Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na safari mpaka alipofika Tabuk, akakaa hapo zaidi ya siku kumi, alikuwa ndani ya siku hizo akituma vikosi na majasusi wake ili kujua habari za warumi, kama ambavyo alikuwa akituma katika maeneo jirani. Na walikuwa viongozi wa makabila na mahakimu wa vijiji vya karibu wakija kwake. Na alimkamata mateka Khalidi bin Walid mmoja kati ya mateka wake Ukaidi bin Abdil Maliki kiongozi wa Doumatul Jandal akaja naye mpaka kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, akaingia mkataba wa kuchukua dhima yake yeye na watu wake, na akakubali kulipa Jizia akamuacha huru Rehema na Amani ziwe juu yake,³⁰⁷Kama alivyokuja Yohana Robot kiongozi wa Aila akalipa jizia

³⁰⁵ bin Hajari, Fat-hul bari, 16/242, bin Hisham, Assiratun nabawiyya 4/520.

³⁰⁶ Kaipokea Bukhari kutoka kwa bin Omari -Radhi za ALLAH ziwe juu yao- amesema: "Alipopita Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika jiwe akasema: "Msiingie makazi ya wale waliozidhulumu msijekupatwa na yale yaliyowapata. Isipokuwa muwe mnalia. Kisha akainamisha kichwa chake na akatembea haraka mpaka akavuka bonde hilo" (Fat-hul Bari, 16/255).

³⁰⁷ Siirat Nabawiyyat Bin Hishaam juzuu ya 4/526 na bin kathiri Siirat Nabawiyyat, juzuu4/30

kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, na akachukua mkataba wa dhima ya watu wake, na wakaja watu wa Adh-rah na Jarba, Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-akawapa amani wote na akafunga nao mkataba wa dhima na akawapa barua.³⁰⁸

Na inaonekana kuwa waroma walikuwa wanajua safari ya Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-na wale aliokuwa nao na kufika kwao Tabuk na kuonyesha kwao nguvu zao katika miji ya kando ya Roma, bali baadhi yake inahesabika iko ndani ya mipaka ya Roma.³⁰⁹na pamoja na haya nguvu zao hazikuwatisha waislamu au kujaribu kuwashtukiza au kuwatia kwenye matatizo pamoja nakuwa wanauwezo wa kufanya hivyo,na huenda kinachotia mkazo juu ya warumi kufuatilia kwao tukio hilo kwa umakini nikuwa mfalme wa Ghasan alimtumia ujumbe (Kaabu bin Maliki),naye ni mmoja kati ya watu waliokwepa kwenda vitani waliosamehewa na ALLAH,akimtaka aende kwao huko Sham, baada ya vita vya Tabuk naye akiwa

³⁰⁸ Tazama: bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/525, 526, bin kathiri, Assiratun nabawiyya, 4/29. (Tazama: Barua za Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kwenda kwa Hiraklu wa Roma ndani ya kitabu hiki).

³⁰⁹ Amenukuu Imam bin Kathir kutoka kwa Imam Ahmad riwaya ya kufika kwa mjumbe wa mfalme Hiraqlu kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-katika mji wa Tabuk na kuufikisha kwake ujumbe nacho ni kisa cha ajabu sana, amesema kuhusu isnadi yake haina tatizo (Tazama: Bin Kathiri Assiiratun nabawiyya 4/27-29) Na tazama riwaya hiyo kwa Imam Ahmad katika Musnad, 3/442, na tazama: Ujumbe wa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-kwa Hiraqlu ndani ya kitabu hiki)

Madina.³¹⁰ ikiwa habari zilifika kwa mfalme wa Ghasan ambaye ni katika viongozi wa Roma mpaka akafikia kujua hali ya kila mmoja katika waislamu katika vita hivi, na msimamo wa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kwake, basi ana haki zaidi awe na taarifa nzima za kutembea kwa jeshi la Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- kutoka Madina mpaka Tabuk,na maandalizi mazima ya jeshi hili kabla halijatoka,kwani muelekeo wa jeshi hili ulitangazwa,na majasusi wa warumi walikuwa wakifika Madina,na huenda mfalme wa warumi alikuwa na uhakika kamili kabisa juu ya ukweli wa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-hili lilichangia kutokudhuria jeshi hili,kwa hofu na kwakujuwa kuwa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-lazima atawashinda ima kwa wakati huo au wakati ujao,kiasi kwamba Mfalme Hiraqlu pindi alipoipokea barua ya Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-na akasikiliza habari zake kwa wale wanaomjua,mpaka akamwambia aliyekuwa akizungumza naye: Wallahi(Namuapia ALLAH) kama utaniamini kwa haya ninayokueleza: "Huyu bwana anakaribia kumiliki kilichoko chini ya miguu yangu hii,"³¹¹Na mfalme huyu aliishi baada ya hapo mpaka akashuhudia waislamu wakimiliki kilicho chini ya miguu yake.³¹²

Na baada ya kuthibitisha Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-nguvu ya waislamu katika kisiwa cha Arabuni alirejea mara nyingine katika mji wa Madina. Akiwa njiani alikutana na maudhi kutoka kwa baadhi ya wanafiki, kiasi kwamba walijaribu kundi miongoni mwao

³¹⁰ Tazama: Hadithi ya ka'b bin Maaliki kwa Bukhari (Fat-hul Bari), 1/242.

³¹¹ Katika tamshi la Bukhari (Fathul bari) 12/71.

³¹² Tazama: Ujumbe wa Mtume kwa Hiraqlu wa Roma; na tazama: Attwabari, Taarikh yake, 4/38, Na Azdiy, Futhu Sham, Uk 236.

linalokadiriwa kuwa na watu kumi kumuua Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, alipokuwa akitembea katika njia nyembamba ya kati kati ya milima ili aivuke, na akaamrisha mwenye kunadi aite kwa sauti kuwa: Hakika Mjumbe wa ALLAH amepita katika njia nyembamba basi asipite yeyote njia hiyo (Njia hiyo ni ngumu sana kupita kwa sababu ya wembamba wake) na aliyekuwa akimuongoza Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- ni Hudhaifa bin Yamani naye alikuwa akiongozwa na Ammari bin Yasiri -Radhi za ALLAH ziwe juu yao-.

Wakamfuata kundi la wanaume wakiwa wamefunika nyuso zao (kininja) wakiwa juu ya vipandwa vyao mpaka wakamvamia Ammari-Radhi za ALLAH ziwe juu yake-huku naye akipiga nyuso za wanyama wao ili awafukuze kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- Akasema Sala na Amani ziwe juu yake kumwambia Hudhaifa: "Tulia,Tulia, na aliposhuka Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- akasema kumwambia Ammari-Radhi za ALLAH ziwe juu yake-: "Je,hao watu umewafahamu? Ammari akasema: Nimevijua vipando ila hao watu wamejifunika:Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- akasema kumwambia:"Hivi unajua nini lilikuwa lengo lao?" Ammari-Radhi za ALLAH ziwe juu yake akasema:ALLAH na Mtume wake ndio wajuzi, Akasema:"Walitaka kumkwapua Mjumbe wa ALLAH ili wamdondoshe".³¹³.

Na alirejea Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina, alipofika alisema: "Hii ndiyo Twaaba(Madina), na huu mlima Uhudi unatupenda na tunaupenda" ³¹⁴ Na wakatoka

³¹³ Tazama: Imam Ahmad bin Hanbal, Al Musnad, 5/390, Asswalihi shami, subulu hudaa warrashad, 5/669

³¹⁴ Al-Bukhariy,Fathul Baariy juzuu ya 16/256 Tazama Bin Abii Shaibah ukurasa wa 397.

wanawake na watoto kwa ajili ya kuwapokea waislamu, na watoto walikuwa wakiimba:

Mwezi umechomoza kwetu sisi

Kutoka lango la Wadaa

Ni wajibu juu yetu kushukuru

kwa muda wote atakaoendelea kulingania kwa Allah

Vita hivi vilikuwa ni malezi kwa jamii nzima ya kiislamu kwa makundi yake yote kwa kushiriki katika kupigana vita kwa nafsi na mali, na kuulea umma wote kuwa na mtazamo wa mbali na matarajio ya juu, kiasi kwamba Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kabla ya kuuaga umma wake na kuelekea kwa rafiki wa juu (Allah) mtazamo wake ukawa katika miji ya Roma, katika harakati ya vita kwa vitendo ili umma usimamie ufunguzi wa miji katika pande zake zote, na baada ya hapo swala la vita halikumalizika kwa kufika Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina, bali liliambatana na swala la msikiti wa madhara (Masjid Dhirari), na vile vile swala la waliokwepa kwenda vitani wale waliokuja kuomba udhuru kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na hao waliokwepa ni watu watatu na kiongozi wao ni Ka'bu bin Maaliki, akawatenga Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kwa muda kadhaa, kisha ALLAH Mtukufu akawasamehe kupitia Qur'ani ambayo inaendelea kusomwa mpaka siku ya kiyama.³¹⁵ Na zimezungumza baadhi ya aya za Qur'ani tukufu kuhusu vita vya Tabuk katika kauli yake Mtukufu:

³¹⁵ Tazama: Ufafanuzi wa hali ya waliotoa udhuru katika hadithi ya Ka'ab bin Maliki tuliyotangulia kuitaja katika (Fat-hul bari), 16/242; na bi Abii shaiba, Al Maghazi, kwa isnadi muttaswil, uk 398

﴿يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَتَأْقِلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرْضَيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَّعَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٣٨﴾ إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَيَسْتَبْدِلَ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّهُ شَيْئًا وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٩﴾ إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى ۗ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾ أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾ لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا وَسَفَرًا قَاصِدًا لَاتَّبَعُوكَ وَلَٰكِن بَعُدَتْ عَلَيْهِمُ الشُّقَّةُ وَسَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَوِ اسْتَطَعْنَا لَحَرَجْنَا مَعَكُمْ يُهْلِكُونَ أَنْفُسَهُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٤٢﴾ عَفَا اللَّهُ عَنْكَ لِمَ أَذْنَتْ لَهُمْ حَتَّىٰ يَتَّبِعَ لَكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَتَعْلَمَ الْكَذِبِينَ ﴿٤٣﴾ لَا يَسْتَفِذُكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَن يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ ﴿٤٤﴾ إِنَّمَا يَسْتَفِذُكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَآرْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِي رَبِّهِمْ يَزِيدُونَ ﴿٤٥﴾ وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ لَأَعَدُّوا لَهُ عُدَّةً وَلَٰكِن كَرِهَ اللَّهُ لَشِقَاعَتِهِمْ فَنَبْطَهُمْ وَقِيلَ اقْعُدُوا مَعَ الْقَاعِدِينَ ﴿٤٦﴾ لَوْ خَرَجُوا فِيكُمْ مَا زَادُوكُمْ إِلَّا خَبَالًا وَلَا وُضِعُوا لِللَّهِمْ جَلَالِكُمْ يَبْغُونَكُمْ أَلْفِئَةً وَفِيكُمْ سَمْعُونَ لَهُمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾ لَقَدْ ابْتَغَوْا أَلْفِئَةً مِنْ قَبْلِ وَقَلْبُوا لَكَ الْأُمُورَ حَتَّىٰ جَاءَ الْحَقُّ وَظَهَرَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَاذِبُونَ ﴿٤٨﴾ وَمِنْهُمْ مَن يَقُولُ أَتَذَن لِّي وَلَا تَفْتِنِي ۗ أَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا ۗ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٤٩﴾ إِنْ تُصِيبَكَ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ وَإِنْ تُصِيبَكَ مُصِيبَةٌ يَقُولُوا قَدْ أَخَذْنَا أَمْرَنَا مِنْ قَبْلِ وَيَتَوَلَّوْا وَهُمْ قَرِحُونَ ﴿٥٠﴾ قُلْ لَنْ يُصِيبَنَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَانَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾ قُلْ هَلْ تَرَبَّصُونَ بِنَا إِلَّا إِحْدَى الْحُسَيْنِيَيْنِ ۗ وَنَحْنُ نَتَرَبَّصُ بِكُمْ أَنْ يُصِيبَكُمْ اللَّهُ بِعَذَابٍ مِّنْ عِنْدِهِ ۗ أَوْ بِأَيْدِينَا فَتَرَبَّصُوا ۗ إِنَّا مَعَكُمْ مُّتَرَبِّصُونَ ﴿٥٢﴾ [التوبة: 38-52]

Enyi mlio amini mna jambo gani pindi mnapo ambiwa tokeni katika njia ya ALLAH mnakuwa wazito kubakia kwenye miji,mnaridhia maisha ya dunia kuliko ya akhera,lakini starehe ya

maisha ya dunia kulinganisha na ya akhera ni kidogo. Kama hamta toka ALLAH atakuadhibuni adhabu chungu na atawaleta watu wengine wala nyinyi hamta mdhuru ALLAH kwa chochote na ALLAH kwa kila kitu ni muweza. Kama hamta mnusuru-Muhammad-basi ALLAH ameisha mnusuru pindi walipo mtoa wale walio kufuru,naye ni wa pili katika pango,pindi alipo mwambia rafiki yake usihuzunike hakika ALLAH yupo pamoja nasi,kisha ALLAH akateremsha utulivu na akampa nguvu kwa askari nyie hamkuwaona na ALLAH akajalia neno la wale walio kufuru kuwa chini na neno la ALLAH ndio la juu,na ALLAH ni mwenye nguvu mwenye hekima. Tokeni kwa wepesi na uzito na mpiganiae kwa mali zenu na nafsi zenu katika njia ya ALLAH kufanya hivyo ndio kheri kwenu ikiwa mnatambua. Na lau faida ingeli kuwa ipo papo kwa papo, na safari yenyewe ni fupi,hakika wangekufuateni lakini wameona ni mbali kuna mashaka na watakuapieni kwa ALLAH,tungeliweza tungetoka pamoja na nyie hali ya kuwa wanaangamiza nafsi zao na ALLAH anajua hakika wao ni waongo. ALLAH amekusamehe ewe-Muhammad-kwa nini umewapa idhini kabla haijakubainikia kwako wale wanao sema kweli na ukawajua waongo. Wasikutake idhini-ewe Muhammad-wale ambao wanao muamini ALLAH na siku ya mwisho wapiganiae kwa mali zao na nafsi zao na ALLAH ni mjuzi kwa wanao muogopa. Na si vinginevyo watakutaka idhini wale wasio muamini ALLAH na siku ya mwisho na mioyo yao ikapatwa na mashaka na wao katika mashaka yao ni wenye kutatizika. Na laiti wangelitaka kutoka hakika wangelimuandalia maandalizi isipokuwa ALLAH ameona karaha kutoka kwao akawatia uzito na ikasemwa, ikaeni pamoja na wenye kuika. Na laiti wangeliwatokea wasingekuzidishieni isipokuwa ni machafuko, na wangepanya haraka kueneza baina yenu usengenyeji na miongoni mwenu wangewasikia na ALLAH anawajua watu waovu. Hakika wametafuta fitina toka hapo mwanzo na wakakugeuzia wewe-Muhammad-mambo mpaka ikafika haki na likadhiri jambo la ALLAH hali yakuwa wao

wakikarahika. Na kuna miongoni mwao wanasema nipe idhini na wala usinitie kwenye fitina, kwa hakika wameporomoka ndani ya fitina na hakika moto wa jannama ni wenye kuwazingira makafiri. Ukipatwa ewe-Muhammad-na jema wao linawaumiza na ukipatwa na matatizo wanasema hakika tumechukua jambo letu hapo mwanzo na wanaondoka na wao ni wenye furaha. Sema ewe-Muhammad-halita tupata isipokuwa lile alilo tupangia ALLAH na yeye ndiye msimamizi wetu na kwa ALLAH wategemee waumini. Sema ewe-Muhammad-hivi mnatungoja sisi tupatwe na lolote isipokuwa moja kati ya mema mawili,na sisi ni wenye kuwangojea ALLAH akufikishieni adhabu itokayo kwake au kwa mikono yetu basi subirini hakika sisi tupo pamoja na nyie ni wenye kusubiri. [Attauba: 38-52]

Na anasema ALLAH Mtukufu pia kuhusu vita hivi katika sura hiyo hiyo.

﴿أَسْتَغْفِرُ لَهُمْ أَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ لَهُمْ إِنْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ﴾ ٣٨ فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ بِمَقْعَدِهِمْ خِلَافَ رَسُولِ اللَّهِ وَكَرِهُوا أَنْ يَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ ٣٩ فَلْيَضْحَكُوا قَلِيلًا وَلْيَبْكُوا كَثِيرًا جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ٤٠ فَإِنْ رَجَعَكَ اللَّهُ إِلَى طَائِفَةٍ مِنْهُمْ فَاسْتَشَدُّوكَ لِلْخُرُوجِ فَقُلْ لَنْ تُخْرَجُوا مَعِيَ أَبَدًا وَلَنْ تُقَاتِلُوا مَعِيَ عَدُوًّا إِنَّكُمْ رَضِيتُمْ بِالْقُعُودِ أَوَّلَ مَرَّةٍ فَاقْعُدُوا مَعَ الْخَلْفِينَ ٤١ وَلَا تَصِلْ عَلَى أَحَدٍ مِنْهُمْ مَاتَ أَبَدًا وَلَا تَقُمْ عَلَى قَبْرِهِ إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَمَاتُوا وَهُمْ فَسِقُونَ ٤٢ وَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَأَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الدُّنْيَا وَتَهْتِكَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ٤٣ وَإِذَا أَنْزَلْتَ سُورَةَ أَنْزَلْنَا مِنْهَا آيَاتٍ لِلَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَجَاهَدُوا مَعَ رَسُولِهِ اسْتَعْتَدْنَاكَ أُولَئِكَ الظُّلُمَاتُ مِنْهُمْ وَقَالُوا ذَرْنَا نَكُنْ مَعَ الْقَاعِدِينَ ٤٤ رَضُوا بِأَنْ يَكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطُبِعَ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ٤٥ لَكِنَّ الرُّسُولَ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ جَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ وَأُولَئِكَ لَهُمُ الْخَيْرَاتُ

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٨٧﴾ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ذَلِكَ الْقَوْمُ الْعَظِيمُ ﴿٨٨﴾ وَجَاءَ الْمُعَذَّبُونَ مِنَ الْأَغْرَابِ لِيُؤْذَنَ لَهُمْ وَقَعَدَ الَّذِينَ كَذَبُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ سَيُصِيبُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٨٩﴾ لَيْسَ عَلَى الضُّعَفَاءِ وَلَا عَلَى الْمَرْضَى وَلَا عَلَى الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ مَا يُنْفِقُونَ حَرَجٌ إِذَا نَصَحُوا لِلَّهِ وَرَسُولِهِ مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِنْ سَبِيلٍ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٠﴾ وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لَا أَجِدُ مَا أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ تَوَلَّوْا وَأَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا أَلَّا يَجِدُوا مَا يُنْفِقُونَ ﴿٩١﴾ إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَسْتَدِينُونَكَ وَهُمْ أَغْنِيَاءُ رَضُوا بِأَنْ يَكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطَبَعَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٩٢﴾ يَتَعَذَّرُونَ إِلَيْكُمْ إِذَا رَجَعْتُمْ إِلَيْهِمْ قُلْ لَا تَعْتَذَرُوا لَنْ تُؤْمِنَ لَكُمْ قَدْ نَبَأْنَا اللَّهَ مِنْ أَخْبَارِكُمْ وَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَىٰ عِلْمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾ سَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ إِذَا انْقَلَبْتُمْ إِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُوا عَنْهُمْ فَأَعْرِضُوا عَنْهُمْ إِنَّهُمْ رَجَسٌ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٤﴾ يَخْلِفُونَ لَكُمْ لِتَرْضَوْا عَنْهُمْ فَإِنْ تَرْضَوْا عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٥﴾ [التوبة: 80-96]

Waombe msamaha wao-ewe Muhammad-au usiwaombe msamaha na kama utawaombe msamaha mara sabini basi ALLAH hato wasamehe kuto samehewa huko kwakuwa wao wamepinga ALLAH na mtume wake na ALLAH hawezi ongoza watu wachafu. Wamefurahi wale walio kwenda kinyume na mtume kwa kukaa kwao kwa kwenda kinyume na mtume wa ALLAH na wakapaka karaha kuto pigania kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya ALLAH na wakasema msitoke kwenye joto kali sema-ewe Muhammad-moto wa jahannama ndio wenye joto kali laiti wangelijua. Basi na wacheke kidogo na walie sana ni malipo kwa yale waliyo kuwa wakiyachuma. Basi kama ALLAH atakurejesha kwenye kundi miongoni mwao kisha wakakutaka idhini sema ewe-Muhaammad- hamta toka pamoja na mimi na hamta mpiga adui pamoja na mimi hakika nyinyi mmeridhia kuikaa toka mara ya kwanza basi ikaeni pamoja na wenye kuikaa. Na wala usimwaliye

yeyote miongoni mwao na wala usisimame kwenye kaburi lake hakika wao wamempinga ALLAH na mtume wake na wakafa hali ya kuwa ni wachafu. Na wala zisikushangaze mali zao na watoto wao si vinginevyo anataka ALLAH awaadhibu kwa hizo mali na watoto hapa duniani na zitoke nafsi zao wakiwa ni wapingaji. Na inapo teremshwa sura kuwa muaminini ALLAH na mpigane pamoja na mtume wake wanakutaka idhini wale wenye uwezo miongoni mwao na wakasema tuache tuwe pamoja na wenye kuikaa. Wameridhia kuwa pamoja na wenye kwenda kinyume na ALLAH akapiga mihuri mioyo yao na wao hawatambui. Isipokuwa mtume na wale ambao walio amini pamoja nae wamepigana kwa mali zao na nafsi zao na hao ndio wenye kheri na wao ndio walio faulu. ALLAH amewaandalia bustani ikipita chini yake mito wataishi humo huko ndiko kufaulu kuliko kukubwa. Na wakaja wale walio taka udhuru miongoni mwa mabedui ili uwape idhini na wakabakia wale walio msimea urongo ALLAH na mtume wake na karibu watapatwa wale ambao walio pinga miongoni mwao adhabu chungu. Haikuwa kwa madhaifu wala kwa wale wenye maradhi wala kwa wale ambao hawana cha kutoa tatizo pindi wanapo toa nasaha kwa ajili ya ALLAH na mtume wake na hawana njia wale wafanyao wema na ALLAH ni msamehevu mpole. Na haikuwa juu wale ambao wanapo kujia ili uwezi kuwapa wao ukasema ewe -Muhammad-sina mimi cha kuwapa na macho yao yakibubujikwa na machozi hali ya kuwa ni huzuni kuto pata cha kutoa. Na si vinginevyo njia kwa wale ambao wanao kutaka idhini na wao ni wenye uwezo wameridhia wawe pamoja na wenye kwenda kinyume na ALLAH akapiga mioyo yao mihuri na wao hawajui. Watakutakeni udhuru pindi mtakaporudi kwao sema-Muhammad- msitoe udhuru hatuta waamini hakika ALLAH ametueleza habari zenu na karibu ALLAH ataona matendo yenu na Mtume wake kisha mtarejeshwa kwa mjuzi wa mambo yaliyo jificha na yenye kuonekana kisha atakuelezeni kwa yale mliyo kuwa mkiyafanya. Karibu watakuapieni kwa ALLAH pindi

watakapo wageukia ili muwezi kuwapuuza basi wapuuzieni wao hakika wao ni wachafu na mafikio yao ni ndani ya moto wa jahannama hali ya kuwa ni malipo kwa yale waliyo kuwa wakiyachuma. Wanakuapieni nyinyi ili muwezi kuwaridhia wao kama mtawaridhia basi hakika ALLAH hawezi kuwaridhia kunako watu wachafu. [Attauba: 80-96] Na anasema ALLAH aliyetakasika na kutukuka -kwa kuwaridhia waumini wale waliomfuata Nabii wake katika vita hivi.

﴿لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ مِنْ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبَ فَرِيقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ إِنَّهُ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٧﴾ وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خُلِفُوا حَتَّىٰ إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنْفُسُهُمْ وَظَنُّوا أَن لَّا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْتَوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١١٨﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴿١١٩﴾ مَا كَانَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَمَنْ حَوْلَهُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ أَن يَتَخَلَّفُوا عَنْ رَسُولِ اللَّهِ وَلَا يَرْغَبُوا بِأَنْفُسِهِمْ عَنْ نَفْسِهِ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ لَا يُصِيبُهُمْ ظَمَأٌ وَلَا نَصَبٌ وَلَا مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَطَّوِّقُونَ مَوْطِنًا يَعْغِظُ الْكُفَّارَ وَلَا يَنَالُونَ مِنْ عَدُوِّ نَيْلًا إِلَّا كُتِبَ لَهُم بِهِ عَمَلٌ صَالِحٌ إِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢٠﴾ وَلَا يُنْفِقُونَ نَفَقَةً صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً وَلَا يَقْطَعُونَ وَادِيًا إِلَّا كُتِبَ لَهُم لِيَجْزِيَهُمُ اللَّهُ أَحْسَنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢١﴾ وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنْفِرُوا كَافَّةً فَلَوْلَا نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَاتِلُوا الَّذِينَ يَلُونَكُمْ مِنَ الْكُفَّارِ وَلْيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً وَعَلِمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٢٣﴾﴾ [التوبة: 117-123]

Hakika ALLAH amemsamehe mtume na na Muhajirina na maanswar na wale ambao walio wafuata katika kipindi kizito baada ya kukaribia kupondoka mioyo ya kundi miongoni mwao kisha ALLAH akawasamehe hakika yeye kwa wao ni msamehevu mpole. Na juu ya wale watatu ambao walio achwa nyuma mpaka dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake na zikapata dhiki nafsi

zao na wakadhania hakuna makimbilio kutoka kwa ALLAH isipokuwa kwakwe yeye kisha akawasamehe ili wawezi kutubia hakika ALLAH ndiye mkubali msamaha mpole. Enyi ambao mlio amini muogopeni ALLAH na muwe pamoja na wakweli. Haikuwa kwa watu wa madina na wale walio pembeni yao miongoni mwa mabedui wabaki nyuma ya mtume wa ALLAH na wala hawapendi kujitolea kwa nafsi zao kwa ajili ya Mtume, hayo ni kwakuwa wao hakiwapati kiu wala uchovu wala njaa katika njia ya ALLAH na wala hawapigi hatua wakiwakasirisha makafiri na wala hawapati kutoka kwa adui tatizo isipokuwa wanaandikiwa wao matendo mazuri hakika ALLAH hapotezi malipo ya wafanyao wema. Na wala hawatoi matumizi madogo wala makubwa wala hawakati bonde isipokuwa wanaandikiwa wao ili ALLAH aweze kuwalipa mema kwa yale waliyo kuwa wakifanya. Na haitakikani kwa waumini watoke wote basi ni bora lipatikane kundi miongoni mwa makundi ili wawezi kujifundisha katika dini na waweze kuwaonya jamaa zao wanapo rudi kwao ili wajihadhari. Enye ambao mlio amini wapigeni wale ambao walio karibu yenu, na wapate kutoka kwenu ugumu na tambueni kuwa ALLAH yupo pamoja na wacha mungu. [Attauba: 117-123]

Kuhiji Abubakar na Waumini (MWAKA 9H): [913]

Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-Aliufungua mji wa Makkah katika mwezi wa Ramadhani mwaka wa nane wa Hijiria, na hakuhiji katika mwaka huo, na wala hakuweka kiongozi yeyote wa kusimamia maswala ya Hija, kisha akashughulika Sala na Amani ziwe juu yake na kupokea misafara na idadi kadhaa ya vita na vikosi vikiwemo vita vya Tabuk. Na ulipokuja msimu wa Hija katika mwaka wa tisa wa Hijiria hakupendezwa Sala na Amani ziwe juu yake kuhiji katika mwaka huo, ilikuwa ni wakati ambao washirikina wa kiarabu walikuwa wakienda kuhiji kama ada yao, na ndio maana alisema Sala na Amani ziwe juu yake: "Hakika huhudhuria watembea uchi

wa kishirikina wakitufu katika nyumba ya Al-kaaba sipendi kuhiji mpaka kusiwe na hali kama hiyo"³¹⁶.

Na akamchagua Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- Abuubakari kuwa kiongozi katika msafara wa Hija kwa mwaka huo,na wakati wa kutoka kwake alimuita Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-Ally bin Abii Twalib-Radhi za ALLAH ziwe juu yake-na akambebesha mwanzo wa suratu Baraa (Tauba)ili awafikishie watu katika Hija,kukiwa ndani yake na tangazo kuwa washirikina wasiukaribie msikiti mtukufu baada ya mwaka huo,na kutengua ahadi zote kwa yeyote aliyekuwa na ahadi yake pembezoni mwa msikiti mtukufu katika washirikina,na ndio maana alipupia Mtume ampatie mmoja miongoni mwa watu wa nyumbani kwake ili akafikishe,na akasema kumwambia Ally-Radhi za ALLAH ziwe juu yake- "Hapaswi yeyote kulifikisha hili isipokuwa mmoja kutoka katika nyumba yangu"

Na akatoka Ally -Radhi za ALLAH ziwe juu yake-akiwa juu ya Al Adh-baa (Ngamia) wa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-akakutana na Abuubakari Swiddiq katika eneo la Dhul hulaifa, na Swiddiq alipomuona alimuuliza kwa adabu sana: Ni kiongozi au muongozwa? Ally-Radhi za ALLAH ziwe juu yake- akajibu kwa adabu ya hali ya juu:Bali muongozwa.³¹⁷

Na akaendelea na safari mpaka akafika Makka, na Swiddiq akasaidizana na Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- kiasi

³¹⁶ Siirat An-Nabawiyat, kitabu cha Muhammad Abuu Shuhbat Juzuu ya 2/536

³¹⁷ Tazama: bin kathiri, Assiratun nabawiyya, 4/69, na tazama: riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, kitabut tafsiri, mlango wa kauli yake"Fasiihuu fil Ardhwii" 5/202.

kwamba Swiddiq alikuwa ndio kiongozi wa Hija na muhutubu wao, na imamu wao, na Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake akisoma aya kutoka katika suratu Baraa kwa watu, ambayo ndani yake kuna kauli yake Mtukufu:

﴿بَرَاءَةٌ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١﴾ فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ
وَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَأَنَّ اللَّهَ مُخْزِي الْكَافِرِينَ ﴿٢﴾ وَأَذَانٌ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى
النَّاسِ بِعَمِّ الْحُجِّ الْأَكْبَرِ أَنَّ اللَّهَ بَرِيءٌ مِنَ الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ فَإِنْ تُبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ وَإِنْ
تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَبَشِّرِ الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ
مِنَ الْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ يَنْفُكُوا شَيْئًا وَلَمْ يُظَاهَرُوا عَلَيْكُمْ أَمْحَا فَأَتِمُوا إِلَيْهِمْ عَهْدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ
إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٤﴾ فَإِذَا انسَلَخَ الْأَشْهُرُ الْحُرْمُ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ وَخُذُوهُمْ
وَأَحْضُرُوهُمْ وَأَقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصِدٍ فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ إِنَّ
اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥﴾ وَإِنْ أَحَدٌ مِنَ الْمُشْرِكِينَ اسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ حَتَّىٰ يَسْمَعَ كَلِمَةَ اللَّهِ ثُمَّ أَبْلِغْهُ
مَأْمَنَهُ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦﴾ كَيْفَ يَكُونُ لِلْمُشْرِكِينَ عَهْدٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ رَسُولِهِ إِلَّا
الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ فَمَا اسْتَقْتُمُوا لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧﴾
كَيْفَ وَإِنْ يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ لَا يَرْقُبُوا فِيكُمْ إِلَّا وَلَا ذِمَّةً يُرْضُونَكُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ وَتَأْبَىٰ قُلُوبُهُمْ
وَأَكْثَرُهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٨﴾ أَشْتَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِهِ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا
يَعْمَلُونَ ﴿٩﴾ لَا يَرْقُبُونَ فِي مُؤْمِنٍ إِلَّا وَلَا ذِمَّةً وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُعْتَدُونَ ﴿١٠﴾ فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ
وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ فِي الَّذِينَ نَفَقْتُمْ الْأَيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾ وَإِنْ نَكَثُوا أَيْمَانَهُمْ مِنْ
بَعْدِ عَهْدِهِمْ وَطَعَنُوا فِي دِينِكُمْ فَقَاتِلُوا أَيْمَةَ الْكُفْرِ إِنَّهُمْ لَا أَيْمَانَ لَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَنْتَهُونَ ﴿١٢﴾ أَلَا
تُنْقِلُونَ قَوْمًا نَكَثُوا أَيْمَانَهُمْ وَهَمُّوا بِإِخْرَاجِ الرَّسُولِ وَهُمْ بَدَّوْكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ أَتَخْشَوْنَهُمْ فَاللَّهُ أَحَقُّ
أَنْ تَخْشَوْهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾ فَتِلْوُهُمْ يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْرِجُهُمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ
وَيَهْزِبْ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾ وَيُذْهِبْ غَيْظَ قُلُوبِهِمْ وَيَتُوبُ اللَّهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلِيمٌ
حَكِيمٌ ﴿١٥﴾ أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُتْرَكُوا وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ

وَلَا رَسُولِهِ وَلَا الْمُؤْمِنِينَ وَلِجَنَّةٍ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾ مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِم بِالْكَفْرِ أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ وَفِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ ﴿١٨﴾ إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَلَمْ يَحْشَ إِلَى اللَّهِ فَكَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَنْ يَكُونُوا مِنَ الْمُهْتَدِينَ ﴿١٩﴾ ۝ أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ كَمَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهَدَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٠﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ أَعْظَمَ دَرَجَةً عِنْدَ اللَّهِ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢١﴾ يُبَشِّرُهُمْ رَبُّهُمْ بِرَحْمَةٍ مِّنْهُ وَرِضْوَانٍ وَجَنَّتْ لَهُمْ فِيهَا نَعِيمٌ مُّقِيمٌ ﴿٢٢﴾ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا ءَابَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْإِيمَانِ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٤﴾ قُلْ إِن كَانَ ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ أُقْتَرَفْتُمُوهَا وَبِئْرَةٌ تَحْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرْتَضُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾ لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحَبَتْ ثُمَّ وَابَيْتُمْ مُدْبِرِينَ ﴿٢٦﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَّمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَٰلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿٢٧﴾ ثُمَّ يَتُوبُ اللَّهُ مِنْ بَعْدِ ذَٰلِكَ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٨﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَٰذَا وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ إِنِ شَاءَ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٩﴾ [التوبة: 1-28]

"Hili ni elezo la kujiepusha litokalo kwa ALLAH na Mtume Wake na ni tangazo la kuachana kabisa na makubaliano yaliyokuwako kati ya Waislamu na Washirikina. Tembeeni aridhini miezi minne na mtambue kuwa nyinyi hamuwezi kushindana na ALLAH na hakika ALLAH ni mwenye kuwadhalilisha wapingaji. Tangazo kutoka kwa ALLAH na Mtume wake kwa watu ya eid kuwa

kuwa ALLAH amejitenga na washirikina na mtume wake amejitenga basi kama mtatubia ni kheri kwenu na kama mtaenda kinyume basi tambueni kuwa nyinyi si wenye kumshinda ALLAH na wape bishara ewe-Muhammad-wale ambao walio pinga kuwa watapatwa wao na adhabu kali. Isipokuwa wale ambao mlio peana ahadi miongoni mwa washirikina kisha hawakuwapunguzia chochote na wala hawakumsaidia juu yenu yeyote basi watimizieni ahadi zao mpaka muda wao ufike hakika ALLAH anapenda wanao mugopa. Itakapo ondoka miezi mitukufu basi wapigeni washirikina popote mtakapo wakuta na wachukueni na muwazingire na muwaikalie kwenye kila mapitio kama wataomba msamaha na wakasimamisha sala na wakatoa zaka waachieni njia yao hakika ALLAH ni msamehevu mpole. Na ikitokea mmoja wa washirikina akahitaji ulinzi basi mpe ulinzi mpaka asikie maneno ya ALLAH,kisha mfikishe mahala pake hayo ni kwakuwa wao ni watu wasio fahamu. Haitakikani kwa washirikina wawe na ahadi kutoka kwa ALLAH na kutoka kwa mtume wake isipokuwa wale ambao mlio wapa ahadi ndani ya msikiti wa makkah basi kwa kiasi watakuwa na msimamo kwenu na nyie kuweni na msimamo kwao hakika ALLAH anapenda wanao muogopa. Itakuwaje nao wakikushideni hawatazami kwenu udugu wala ahadi,wanakufurahisheni kwa midomo yao,na nyoyo zao zinakataa hayo,na wengi wao ni wapotovu. Wameziua aya za ALLAH kwa thamani kidogo kisha wakazuia kunako njia ya ALLAH,hakika wao yamekuwa mabaya mambo ambayo wanayo yafanya. Hawatazami kwa muumini udugu wala ahadi,basi hao ndio waruka mipaka. Basi kama wataomba msamaha na wakasimamisha sala na wakatoa zaka ni ndugu zenu katika dini na tunazipambanua aya kwa watu ili waweze kuzitambua. Na kama watatengua viapo vyao baada ya ahadi zao na wakasema vibaya dini yenu basi muwapige viongozi wa kikafiri hakika wao hawana viapo vya kweli ili waweze kuacha. Kwanini msiwapige watu walio tengua viapo vyao na wakapupia kumtoa Mtume na wao

waliwaanza kwa mara ya mwanzo,hivi mnawaogopa basi ALLAH ndiye mwenye haki ya kuogopwa mkiwa ni waumini. Wapigieni ALLAH atawaadhibu kwa kupitia mikono yenu na atawadhilisha na atakunusuruni juu yao na ataviponya vifua vya waumini. Na ataondosha chuki za nyoyo zao na ALLAH atamsamehe anaye mtaka na ALLAH ni mjuzi mwenye hekima. Hivi mdhania mtaachwa na hali ya kuwa bado hajawatambua ALLAH wale ambao walio pigana miongoni mwenu na wala hamkujifanyia kinyume cha ALLAH wala mtume wake wala waumini watu wa karibu,na ALLAH ni mwenye kueleza kwa yale mnayo yafanya. Haitakikani kwa washirikina kusimamia misikiti ya ALLAH hali ya kuwa wametoa ushahidi juu ya nafsi zao kuwa ni wapingaji hao yameporomoka matendo yao na ndani ya moto ni wenye kuishi milele. Si vinginevyo wanao imarisha misikiti ya ALLAH ni wale walio muamini ALLAH na siku ya mwisho na wakasimamisha sala na wakatoa zaka na hawakumuogopa isipokuwa ALLAH basi hao karibu wawe miongoni mwa walio ongoka. Hivi mmejalia kuwanyweshwa maji mahujaji na kusimamia Msikiti wa makkah ni sawa na yule ambaye aliye muwamini ALLAH na siku ya mwisho na akapigana katika njia ya ALLAH,hawawezi kuwa sawa mbele ya ALLAH,na ALLAH hawaongozi watu madhalimu. Wale ambao walio hama na wakapigana katika njia ya ALLAH kwa mali zao na nafsi zao wana wao daraja kubwa mbele za ALLAH na wao ndio walio faulu. ALLAH anawapa bisha njema kwa huruma itokayo kwake na kuridhiwa na mabustani wana wao ndani ya mabustani neema za kudumu. Wataishi humu milele hakika kwake yeye ALLAH kuna malipo makubwa. Enye ambao mlio amini msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa ni vipenzi kama watapenda upingaji zaidi kuliko Imani,na atakaYe wafanya kuwa ni vipenzi miongoni mwenu basi hao ndio watu madhalimu. Sema-ewe Muhammad-kama watakuwa baba zenu na watoto wenu na ndugu zenu na wake zenu na familia zenu na mali mnazo hofia kupata kwake hasara na makazi mnayo yaridhia ndio vinapendeza zaidi kuliko

ALLAH na Mtume wake na kupigania katika njia yake basi subirini mpaka lije jambo la ALLAH na ALLAH hawaongozi watu wachafu. Hakika ALLAH amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulipokupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu, na ardhi ikawa dhiki kwenu juu ya upana wake, kisha mkageuka mkarudi nyuma. Kisha akateremsha ALLAH utulivu juu ya mtume wake na kwa waumini na akateremsha askari nyie hamkuwaona na akawaadhibu wale ambao walio kufuru na hayo ni malipo kwa wapingaji. Kisha ALLAH anasamehe baada ya hapo kwa anaye mtaka, na ALLAH ni msamehevu mpole. Enye ambao mlio amini hakika washirikina ni najsi basi wasiusogelee Msikiti wa Makkah baada ya mwaka wao huu, na kama mtahofia Umasikini karibu ALLAH atakutajirisheni kutokana na fadhila zake akitaka hakika ALLAH ni mjuzi mwenye hekima. [Attauba: 1-28]. Na walikuwa baadhi ya maswahaba wakifikisha aya hizo kwa watu pamoja na Ally -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- kwani yeye alikaa badala ya Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- katika jambo hili, na wakiwasisitiza kuwa asihiji tena Mshirikina yeyote baada ya mwaka huo, na wala asitufu yeyote katika Al-ka'aba akiwa uchi. Amepokea Bukhari kutoka kwa Abuu Huraira "Yakwamba Abuubakari Swiddiq Radhi za ALLAH ziwe juu yake- alimtuma katika Hija ambayo alipewa uongozi na Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kabla ya Hija ya kuaga ilikuwa ni siku ya kuchinja (siku ya Idd) akiwa pamoja na kundi la watu wawatangaziYe watu kuwa asihiji tena baada ya mwaka huo Mshirikina yeyote na wala asitufu yeyote katika Al-ka'aba akiwa uchi"³¹⁸

³¹⁸ Tazama, sahihi Bukhari, kitabu Al Maghazi, babu Hajju Abuubakari bin naasi. 5/115

Na hakuna shaka kuwa Ally -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- ni katika watu wa nyumba ya Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- hivyo anamuwakilisha Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na watu pia wanamuamini, na hasa hasa wale waliokuwa na ahadi na Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na Ally ndiye mtu wa karibu zaidi katika watu wa nyumba ya Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, na katika desturi za Waarabu (Katika kufunga mikataba na kuitengua, nikuwa asisimamie hilo isipokuwa mkuu wa kabila au mtu katika watu wake),³¹⁹Ikawa kulisimamia Ally jukumu hili ni kutia mkazo kwa watu wote kuwa hili ndilo alilolitaka ALLAH na Mtume wake, Na aliwahi kuulizwa Ally -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- kuwa uliagizwa nini katika Hija? Akasema niliagizwa kwa mambo manne: 1- Haitoingia peponi isipokuwa nafsi ya muumini, 2-Na wala asitufu katika Al-ka'aba mtu akiwa uchi, 3- Na wala wasikusanyike waislamu na makafiri katika Al-ka'aba baada ya mwaka huu, 4- Aliyekuwa kati yake na Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- na ahadi basi ahadi yake itatimizwa kwa wakati wake, na ambaye hakuwa na ahadi naye anapewa muda wa miezi minne.³²⁰

Na ama walionufaika na tukio la kuthaminiwa kati ya Abuubakari na Ally -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- hapa si mahala pake kulizungumzia swala hilo, kwani kila mmoja kati yao ana ubora wake na ana umuhimu katika swala la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na kila mmoja alikuwa akitekeleza jambo alilo amrisha, na kila mmoja alimpenda mwenzie na kumuheshimu nakuwa na adabu anapokuwa pamoja naye, bali wote wawili kila mmoja alisaidia

³¹⁹ Siirat An-Nabawiyat ,kitabu cha Muhammad Abuu Shuhbat ukurasa 2/539.

³²⁰ Binil Qayyim, zadul maaad uk. 655 kaipokea Tirmidhi katika sahihi yake, hadithi namba: 3091 na Ahmad katika Musnad wake, 1/79.

katika kazi ya mwenzie -Radhi za ALLAH ziwe juu yao-, na wakashirikiana nao maswahaba wengine, sawa sawa iwe katika kutekeleza ibada ya Hijja na majukumu yake, au katika kuzifikisha aya za suratu baraa kwa watu katika Hijja, wao walikuwa wakikamilisha baadhi yao kwa baadhi (Anapoishia mwenzie mwenzie anamalizia), wote lengo lao ni moja, nalo kulinyanyua neno la Laa ilaaha illa Ilaah (Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ALLAH) katika Hijja na maeneo mengine, na ikiwa katika zama hizi tunatilia mkazo yale aliyoyafikisha Ally -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- katika kuwazuia Kuhuji washirikina waliokuwa Uchi, basi kwa hili hata maswahaba wengine katika zama za Ally radhi za ALLAH ziwe juu yake ni lazima wasimamie jukumu hili pamoja naye, kwa lengo hilo hilo wakati washirikina wakiendelea kuwepo, ambao walitoweka Makka baada kusikia kwao kutoka kwa Ally na wale waliomsaidia, na Waislamu hawakuwa na haja ya kulirudia hilo tena kwa sababu washirikina walitoweka kabisa Makka.

Hili Lilikuwa ni Onyo na ilikuwa Hijja hii Hija hii utangulizi wa Hija ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika mwaka uliofuata (Hija ya kuaga),³²¹kiasi kwamba viwanja vyote vilikuwa safi kwa kutokuwa na Washirikina, na nafsi za mahujaji zilikuwa safi kwa ajili ya kumpokea Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, katika Hijja ya wenye kumpwekesha ALLAH na katika kumuaga Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- kwa watu wote, ili aliyehudhuria amfikishiye asiyekuwepo.

³²¹ Angalia Hija ya kuaga katika hiki kitabu:

MISAFARA YA MAKABILA [921]

Neno(Wafdu) ni Misafara ni wingi wa neno msafara, nalo ni kundi lililoteuliwa kutoka katika jamii fulani, ili liwawakilishe kukutana na waheshimiwa, na viongozi na kwenda kwao na kuwawakilisha katika majukumu.³²²

Ujumbe wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ni wa ulimwengu kwa watu wote, kwani alikuwa na pupa Rehema na Amani ziwe juu yake tangu mwanzo juu ya kuyaunganisha makabila moja moja na kwa makundi,³²³na akawafikishia ujumbe.

Na swala hili lilizidi baada ya makuraishi kumbana Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake-, akawa anazunguka katika makabila katika nyakati za misimu akiwafikishia Uislamu, na akitafuta nusura yake. Na alikuwa pamoja naye katika mizunguko yake mingi rafiki yake Abuubakari Swiddiq -Radhi za ALLAH ziwe juu yake-, anye -Radhi za ALLAH ziwe juu yake- alikuwa akiyajua vizuri makabila na nasaba³²⁴

Na yalitofautiana majibu ya makabila, na matokeo yake yakawa ni kuenea kwa habari za Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na ujumbe wake katika makabila mbali mbali, alikutana Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- kabla ya kuhama kutoka Makka na makundi mengi ya makabila tofauti tofauti, kukawa hakujabakia mtaa

³²² Tazama: An nawawiy sherehe ya sahihi Muslim, 1/181.

³²³ Tazama kwenda kwa Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- yeye mwenyewe katika makabila ndani ya kitabu hiki. Tazama: Thalabi; Abdul Azizi, Mu'jaz Muhammad Rasuulullaah, (Sehemu ya kwanza Ujumbe wa Muhammadi kwa umati zote) chapa ya tatu, Darul gharbil islami, Beirut, 106H, 1/21

³²⁴ Tazama: Asswalaabi, Assiratun nabawiyya, 2/387.

wowote isipokuwa walisikia habari za Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na ujumbe wake.³²⁵

Na baada ya kuhama zilisambaa habari za Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- na wale waliokuwa pamoja naye miongoni mwa Waislamu, na hasa hasa baada ya vita vya Badri.

Na yalikusanya makubaliano ya Amani ya Hudaibia baadhi ya vipengele kama: (Yeyote atakayetaka kuingia katika makubaliano ya Muhammadi au mikataba yake basi na aingie, na atakayetaka kuingia katika makubaliano na mikataba ya makuraishi basi aingie),³²⁶na kwa ajili hiyo ikawa kwa makabila yaliyoko karibu na eneo la tukio yakachagua moja kati ya pande mbili zilizokuwa zikivutana kwa kuwafanya kuwa ni watu wao wa karibu (kwa ujamaa wa kuapizana), Likaingia kabila la Khuzaa katika makubaliano ya Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-, na wakaingia Banu Bakri katika makubaliano ya makuraishi, na ukawa uadui wa Banu Bakri kwa kabila la khuzaa kwa msaada wa Makuraishi ni alama ya Makuraishi kuvunja makubaliano yao ya Amani kati yao na Mtume-Rehema na Amani ziwe juu yake-, jambo lililopelekea kufunguliwa mji wa Makka, na kuporomoka nguvu ya washirikina ndani yake.

Na baada ya ufunguzi wa Makka jambo likawa wazi mbele ya makabila ya Waarabu yakuwa uongozi pekee katika kisiwa cha Arabuni ni wa Uislamu na nabii wake Sala na Amani ziwe juu yake.

³²⁵ Tazama kujitangaza Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- yeye mwenyewe katika makabila kutoka katika kitabu hiki.

³²⁶ Angalia Hati ya makubaliano ya Hudaibia katika hiki kitabu:

Misafara ikaanza kuja kwa wingi katika mwaka wa tisa mpaka ukaitwa kuwa ni mwaka wa Misafara,³²⁷, pamoja na kuwa baadhi yake ilifika kabla ya mwaka huo, na baadhi yake ilikuja mapema katika mwaka wa tano wa Hijiria, kisha ikarudi mara nyingine mwaka wa tisa wa Hijiria.³²⁸Na lilikuwa kila kabila likionyesha nafasi yake na Utukufu wake, kiasi kwamba walikuwa wakihutubia wahutubu wao na yakitolewa mashairi kutoka kwa washairi wao, na alikuwa Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- akiwaamrisha baadhi ya maswahaba wake kujibu hotuba kwa hotuba, na shairi kwa shairi, likawa lengo la Mtume-Sala na amani ziwe juu yake- ni kulinyanyua neno la ALLAH na kuwaita watu katika neno hilo, na kuja katika dini yake, na kueneza maadili na Uadilifu, na wala si kwa ajili ya ukabila wala Ufahari, na kwa ajili hiyo matokeo yake yalikuwa makubwa na ya kutisha, yenye malengo mazuri mbele ya wengine, yenye mtazamo wa juu na kiwango cha juu, jambo lililopelekea makabila kumkubali Sala na Amani ziwe juu yake kwa hilo. Na alikuwa Sala na Amani ziwe juu yake akiikirimu misafara na akiwapa zawadi na akiwapa elimu na akiwaamrisha maswahaba kuwafundisha, kama ambavyo alikuwa Sala na Amani ziwe juu yake alikuwa akiwasaidia mtu wa kupangilia mambo yao wanapotaka kuondoka,³²⁹ na akiwapangia fungu lao la zaka, akiwaliwaza masikini wao kupitia matajiri wao, na anakuwa kiongozi wao na mwalimu wao.

³²⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 3/559.

³²⁸ Tazama: Muhammad Abuu Shaiba, Assiratun nabawiyya, 2/542.

³²⁹ Tazama: Sahihi Bukhari, kitabul Maghazi, Mlango wa msafara wa banu Tamimi, Na kitabu tafsiri, suratul Hujurati, Mlango (Hakika wale wanaokuita nyumba ya nyumba), 6/46. Na tazama: Msafara wa Banu Tamim, katika kitabu hiki.

Kama ambavyo Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-alikuwa akijibu maswali yao mbali mbali ambayo mengine yalikuwa yakihusiana na hali halisi ya maisha wanayoishi, au chakula na vinywaji wanavyovitumia katika miji yao, au matukio mbali mbali yanayowatia uzito, na wakati mwingine yanayowahusu wao wenyewe na si watu wengine.

Na yalitokea baadhi ya matukio wakati walipokutana na Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- ambayo ziliteremka aya ndani ya Qur'ani, kama ilivyotokea kwa Msafara wa Bani Tamim na kuteremka kwa suratu Hujurat.³³⁰

Na alifungamanisha bin Hisham kati ya Misafara na kuteremka kwa suratun naswir, akasema: "Makundi kwa makundi wakija kwake kutoka kila upande" Anasema ALLAH Mtukufu kumwambia Nabii wake:

﴿إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿٢﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٣﴾﴾ [النصر: 3-1]

Itakapo kuja nusra ya ALLAH na ufunguzi. Na utawaona watu wakiingia ndani ya dini ya ALLAH makundi makundi. Basi takasa kwa sifa za MOLA wako na umtake msamaha hakika yeye amekuwa ni mkubali tauba. [An naswir: 1-3].³³¹

³³⁰ Tazama: Sahihi Bukhari, kitabul Maghazi, Mlango wa msafara wa banu Tamimi, Na kitabu tafsiri, suratul Hujurati, Mlango (Hakika wale wanaokuita nyumba ya nyumba), 6/46. Na tazama: tafsiri bin kathiri 2/1744

³³¹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/560.

Waafid Daus (Atufail bin Amri): [932]

Dausi, ni kabila lenye asili ya Yemen, linakutana na kabila la Azadi katika ukoo, linatokea kwa Zahran bin Ka'bu, na kwasasa zaidi linaitwa Zahran,³³² na makazi yake ni kusini mwa mji wa Twaif,³³³ katika mkoa wa Baha, na lilikuwa na ngome maarufu, na lilikuwa na nafasi kubwa katika makabila ya waarabu wakati ule.³³⁴

Makuraishi kabla ya kuhama Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake- walikuwa na pupa kubwa ya kuwazuia wanaoingia Makka kumsikiliza Mtume-Sala na Amani ziwe juu yake-. Anasimulia Tufail kuwa yeye aliingia Makka na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akiwa huko: wakamfuata wanaume katika makuraishi, na alikuwa Tufail ni mtu mwenye heshima mshairi na mwerevu, wakasema kumwambia: Ewe Tufail hakika wewe umekuja katika miji yetu, na huyu mtu tuliyenaye ameshatuchosha, na amesambaratisha umoja wetu, na amevuruga mambo yetu, bali zaidi ya hapo maneno yake ni kama uchawi, anauwezo wa kumtenganisha kati ya mtu na baba yake, na kati ya mtu na kaka yake, na kati ya mtu na mke wake, na sisi tunakuhofia wewe na watu wako yale yaliyotufika sisi, usimsemeshe na wala usimsikilize chochote. Akasema: Wakaendelea kunisisitiza mpaka nikadhamiria kutomsikiliza chochote wala kumzungumzisha, mpaka nikaziba pamba masikioni mwangu nilipokwenda msikitini nikihofia kisinifikie chochote katika kauli zake hali yakuwa sitaki kusikia. Akasema nikaenda msikitini,ghafla nikamuona Mtume -Sala na Amani ziwe

³³² Tazama: Assamaani, Al Ansab, 5/361. bin Hazm, Jamharatu ansaabil Arab, uk 379

³³³ Tazama: (Tarehe: 1/5/1432H www.arwikiPedia.org)

³³⁴ Tazama: Assamaan, An saab, 5/361.

juu yake- akiswali katika Al- ka'aba. Akasema: Nikasimama karibu naye lakini ALLAH akakataa lolote kwangu zaidi ya kunisikilizisha baadhi ya kauli zake. Akasema: Nikasikia maneno mazuri, akasema: Nikasema ndani ya nafsi yangu: Nimpoteze mama yangu, (yaani ni hasara iliyoje!) Wallahi (Namuapa ALLAH hakika mimi ni mtu mwerevu na mshairi, hakuna kinachoweza kunitatiza nisijue kizuri na kibaya, kwani nini kinanizuia mimi kumsikiliza huyu mtu haya anayoyasema!?, ikiwa haya anayoyasema ni mazuri basi nitayakubali, na kama yatakuwa ni mabaya basi nitayaacha, Akasema: Nikakaa mpaka akaondoka Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwenda nyumbani kwake nikamfuata mpaka akaingia nyumbani kwake nami nikaingia nikasema: Ewe Muhammadi hakika watu wako wamenieleza kadhaa wa kadhaa, nikamueleza waliyoyasema, Wallahi Namuapa Mwenyezi Mungu waliendelea kunitisha kuhusu jambo lako mpaka nikaziba masikio yangu kwa pamba ili nisisikie kauli yako, kisha Mwenyezi Mungu akakataa zaidi ya kunisikilizisha kauli yako, nikasikia maneno mazuri sana, hebu niwekee wazi jambo lako.

Akasema: Akaniwekea wazi Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- Uislamu, na akanisomea Qur'ani, Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu sijawahi kusikia maneno mazuri kuliko hayo wala jambo la Uadilifu kuliko hilo. Anasema: Nikasilimu na nikatamka shahada ya kweli, na nikasema: Ewe Mjumbe wa ALLAH hakika mimi ni mtu ninayesikilizwa kwa watu wangu, na mimi ninarudi kwao ninakwenda kuwalingania waingie katika Uislamu, niombe kwa ALLAH anipe alama (muujiza) ambao utakuwa ni msaada kwangu juu yao katika yale ninayowaitia: Akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu mpe alama".

Anasema: Nikatoka kwenda kwa watu wangu, mpaka nilipofika katika kijimlima kinachonifanya nitokeze katika miji, ilitokea nuru baina ya macho yangu mfano wa taa, nikasema: Ewe Mwenyezi Mungu naomba iwe mahala pengine tofauti na uso wangu, hakika

mimi ninahofia wasije kudhania ni adhabu (au ni ugonjwa) umejitokeza usoni kwangu kwa sababu ya kuacha dini yangu. Anasema: Ikahama ile nuru ikahamia katika kichwa cha mjeledi wangu. Anasema: Waliokuwepo wakaanza kuonyeshana nuru hiyo katika mjeledi wangu mfano wa chemli (kandili) iliyotundikwa, na mimi nikishuka kutoka juu ya kijimlima hicho, anasema mpaka nikafika kukapambazuka nami nikiwa kwao, anasema niliposhuka alinjia baba yangu, na alikuwa ni mzee mtu mzima, Akasema: nikasema: Kaa mbali nami ewe baba yangu, mimi si miongoni mwako wala wewe si miongoni mwangu (Hatuna mahusiano mimi na wewe), Akasema: Na ni kwanini ewe mwanangu? Akasema: Nikasema: Mimi nimesilimu na nimefuata dini ya Muhammad -Rehema na Amani ziwe juu yake-, Akasema: Dini gani tena hiyo mwangu?, dini yangu ndio dini yako, Akasema: Nikasema: Basi nenda kaoge na usafishe nguo zako, kisha njoo ili nikufunze niliyojifunza. Akasema: Akaenda akaoga na akasafisha nguo zake. Akasema: Kisha akarejea nikamuwekea wazi Uislamu na akasilimu.

Akasema: Kisha akanijia kipenzi changu, Nikasema: Usinikaribie, mimi na wewe hatuna mahusiano, akasema kwa nini? Nitoe fidia ya baba yangu na mama yangu, Akasema: nikasema: umetutenganisha mimi na wewe Uislamu na nimefuata dini ya Muhammadi -Rehema na Amani ziwe juu yake-, Akasema: Dini yangu ndio dini yako, akasema: Nikasema: Basi nenda kwa Hannaa dhi Sharaa (Anasema bin Hisham: Na huitwa pia Humma Dhi Sharaa) ukajisafishe huko.

Anasema: Na Dhi Sharaa lilikuwa ni sanamu la kabila la Dausi na kulikuwa na uzio wamelizungushia, na kulikuwa na matone ya maji yanayodondoka kutoka juu ya mlima. Akasema: Akasema yule mwanamke: Nimtoe fidia baba yangu na mama yangu, je unahofia kupata matatizo kutoka kwa Dhi Sharaa?, anasema: Nikasema: Hapana, mimi nachukua dhamana yako, yule mwanamke akaenda akaoga kisha akaja nikamueleza kuhusu Uislamu akasilimu.

Kisha nikawaita kabila la Dausi katika Uislamu, wakawa wazito, kisha nikamjia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akiwa Makka, nikasema kumwambia: Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu hakika mimi Dausi wamenizidia kwa sababu ya zinaa yao, waombe laana, Akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu waongoze kabila la Dausi" Rudi kwa watu wako kawaite katika Uislamu na uwe mpole kwao. Akasema: Nikaendelea kubakia katika ardhi ya kabila la Dausi nikiwaita katika Uislamu, mpaka akahama Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Kwenda Madina, na akapita maeneo ya Badri na Uhudi na Khandaq, kisha nikaenda kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- nikiwa pamoja na wale waliosilimu pamoja nami katika watu wangu na wakati huo Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akiwa Khaibar. Mpaka nikashuka Madina nikiwa na watu sabini au themanini kutoka kabila la Dausi, kisha tukaungana na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Khaibari akatuunganisha na waislamu"

Kusilimu kwa Tufail kama inavyoonekana kulikuwa Makka, kiasi kwamba alirudi baada ya hapo akawa nimfikishaji wa ujumbe kwa watu wake, na wakasilimu wachache, na kabila likampinga, akaja mara nyingine kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Madina na akamfafanunulia hali halisi, na akamtaka awaombe adhabu watu wake, isipokuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- aliwaomba dua nzuri, kama ilivyokuja katika riwaya ya Bukhari, kwani Tufail alisema: "Hakika kabila Dausi limeangamia wameasi na wamekataa, muombe Mwenyezi Mungu awashushie mabaya, akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu waongoze Dausi na uwalete kwangu"³³⁵Na zilijibiwa dua za Mtume -Rehema na Amani ziwe juu

³³⁵ Kaipokea Bukhari katika sahihi yake, (Mlango: wa kisa cha Tufail bin Amri Ad dausi), 5/123.

yake- Wakasilimu watu wa kabila Dausi na ukaja msafara wake pamoja na Tufail bin Amri, na msafara huo ulikuwa na watu sabini au themanini katika watu wake, na Tufail alikuwa pamoja na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- pindi alipoifungua Makka, na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alimuagiza kuyavunja baadhi ya masanamu pande za Dausi,³³⁶kisha akawa pamoja na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mpaka alipofariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, akashiriki katika tukio la walioritadi katika vita mbali mbali, mpaka alipokufa shahidi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- katika vita vya Yamama katika mwaka wa kumi na moja wa Hijiria katika utawala wa Abuubakari Swiddiq -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-.³³⁷

Msafara wa Abdul kaisi: [941]

Na Abdul kaisi ni kabila linalotokana na Rabia bin Nizar,³³⁸wakazi wake wanatokea maeneo ya Bahrein wako wanaoishi mjini na vijijini, mahusiano yao na Uislamu yalikuwa tangu zamani, kiasi kwamba ulikwenda msafara miongoni mwao kabla ya mwaka wa tano wa Hijiria, akiwemo bwana mmoja akiitwa Ashaju Abdul Kaisi mmoja kati ya viongozi wao, na aliwahi kumsifia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kwa kauli yake: "Hakika una mambo mawili

³³⁶ Siirat Nabawiyyat cha Bin Saad kutoka katika Twabakatul kubra juzuu ya 2/157 Siirat Nabawiyyat Bin Hishaam juzuu ya 1/385

³³⁷ bin Hisham, Assiratun nabawiyy, 2/258; Na tazama: Tarjama yake katika kitabu cha Al Iswaba cha bin Hajari, 2/225.

³³⁸ Tazama: bin Hajari, Fat-hul bari, 16/207, bin Hazmi Jamharatu Ansaabil Arab uk 295.

anayapenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, upole na utaratibu"³³⁹.

Na msafara wa kwanza ulikuja mapema kipindi cha mvutano kati ya Makuraishi na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake, imekuja katika kitabu cha Bukhari katika sahihi yake mlango mzima kauita (Mlango wa msafara wa Abdul Kaisi),³⁴⁰ Ameandika ndani yake hadithi ya bin Abbas -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- Amesema: Ulikuwa msafara wa Abdul Akais kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Akasema: Karibuni enyi watu msifedheheke wala msisikitike, wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakika kati yetu sisi na wewe kuna washirikina wa Mudhwar, na sisi hatuwezi kufika kwako isipokuwa katika miezi mitukufu, tuhadithie sentensi moja katika maamrishi ambayo tukiyaifanyia kazi tutaingia peponi, na tutaitumia kuwafundisha walioko nyuma yetu. Akasema: "Ninakuamrishi mfanye mambo manne, na muache mambo manne, kumuamini Mwenyezi Mungu, hivi mnajua ni nini maana ya kumuamini Mwenyezi Mungu? Ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na kusimamisha swala na kutoa zaka, na kufunga mwezi wa Ramadhani, na mtoe moja ya tano katika mali ya ngawira. Na ninakukatazeni mambo manne, vilivyokamuliwa katika vyungu, na mapipa, na mashina ya mitende na mabakuli (vyote ni vyombo vya kuandalia

³³⁹ Yeye ni Abdillahi bin Aufu, na inasemekana kuwa Al Mundhiri bin Aufu, bin Hajari kitabu Al-Is'waba, 2/356.

³⁴⁰ Sahihi Bukhari, 5/116.

pombe)³⁴¹. Na msafara huu ulikuwa umekuja kwa ajili ya kusilimu watu wa Bani Abdil Kais³⁴²

Miongoni mwao alikuwemo mtu mmoja akiitwa Jaarud bin Amri, aliyeupenda Uislamu na alikuwa katika Ukristo, akasema: Mimi nilikuwa katika imani ya dini lakini ninaacha dini yangu kwa ajili ya dini yako, je, uko tayari kunidhamini? Akasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**:- "Ndiyo, mimi ninakudhamini, kwakuwa amekuongoza Mwenyezi Mungu katika kile kilicho bora zaidi", basi akasilimu na wakasilimu watu wake.³⁴³Na ulikuwa mzuri Uislamu wa msafara huu kutoka kwa Abdul Kaisi, na wakaupeleka Uislamu katika maeneo ya Jawatha (Baharain) na pembe zake, na ndiyo maana imekuja kutoka kwa bin Abbasi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao. "Ijumaa ya kwanza watu kukusanyika baada ya ijumaa ile iliyofanyika katika msikiti wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ilifanyika katika Kijiji cha Jawatha, ni kijiji kiko Bahrain"³⁴⁴

³⁴¹ Kaipokea Bukhari, kitabul Maghazi, babu wafdu Abdul Kais, 1/116, Na tazama: Bin Hisham, Assiratun Nabawiyya, 4/575, na aina hii ya vyombo hukamuliwa pombe.

³⁴² Tazama: Sahihi Bukhari, 5/116, na Bin Hisham, Assiratun Nabawiyya, 3/575

³⁴³ Tazama: Bin Hajari, Al Iswaba, 1/216, bin Hisham, Assiratun Nabawiyya, 4/575.

³⁴⁴ Kaipokea Bukhari, kitabul Maghazi, Babu wafdu Abdul Kaisi, 5/116. (Na bado msikiti wa Jawatha una athari zake za zamani zinafahamika mpaka sasa katika mji wa Ahsaa maeneo ya Katwif, na nilizifuatilia athari hizo mimi mwenyewe).

Na kabla ya kuondoka kurudi Bahraini waliomba toka kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- vipando, akawaomba radhi Akasema: "Sina kipando cha kuwapa"³⁴⁵Wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu: Hakika katika miji yetu huwa kuna vipando vilivyopotea miongoni mwa vipando vya watu, je, tunaweza kuvitumia kusafiria katika miji yetu? Akawakataza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- vipando hivyo. Na akasema: "Hakika hivyo ni muwako wa moto" Na hivi ndivyo alivyowafundisha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Uharamu wa mali za watu, pamoja na kuwa watu hawa wana shida, na pamoja nakuwa vipando hivi viko jangwani na hakuna ajuaye mmiliki wake, lakini pamoja na hivyo akawakataza.³⁴⁶Na akaeleza mpokezi kuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- aliwasifia watu hawa na akasema: "Utakuchomozeeni kutoka upande huu msafara ambao ndio msafara bora katika watu wa mashariki"³⁴⁷Akasimama Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- akaelekea upande wanaojia, akakutana na watu kumi na tatu walioko katika vipando, akawapa habari njema.

Hivi ndivyo watu hao walirejea wakiwa na dini nzuri na tabia nzuri na Uaminifu pia. Na lilipotokea swala la kuritadi katika miji yao na kwa watu wao baada ya kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kwa kuathiriwa na Wafalme waliokwenda mbio kuwaritadisha kuwarudisha katika Ukristo, akasimama mbele yao

³⁴⁵ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/575.

³⁴⁶ Kaipokea Muslim, na Tazama: Binil Qayyim, Zaadul Maad, uk 661.

³⁴⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Kathiri juzuu ya 1/90.

Jaarudi akawahutubia na akawaita kurudi katika Uislamu, na akatangaza kuthubutu kwake katika Uislamu, na kwamba yeye anashuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu nakuwa Muhammadi ni mja wake na ni mtume wake, nakuwa anakufuru yeyote ambaye hatoshuhudia hivyo.³⁴⁸

Msafara wa Thaqiif:

Kabila la Thakif linarudi kwa Hawazini katika kabila la Mudhwar³⁴⁹. Lilikuwa likiishi Twaif, mji uliokaribu zaidi na Makka, na wenye mahusiano ya karibu zaidi na Makka, na mji wa Twaif una hewa safi na unauzalishaji mkubwa wa kilimo, una mabonde mengi ya kilimo yanaye uzalishaji mkubwa unafahamika kwa hilo, wafanyabiashara wa Makka walikuwa wakichukua mashamba na sehemu za kupumzika, wakikimbilia huko kutokana na joto la Makka katika kipindi cha kiangazi.³⁵⁰

Na kabila la Hawazini lilikuwa jirani na Thakif katika mji wa Twaif na miji ya pembezoni mwake isipokuwa utawala wa mji wa Twaif ulikuwa chini ya Thakif, hivyo Thakif likawa ndani ya Twaif, na Hawazini likawa kijijini, Thakif likawa katika ushirikina wakiabudu

³⁴⁸ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/575.

³⁴⁹ Kitabu cha Assamaaniy, Al Ansaab, 3/134, na tazama bin Hazmi, kitabu: Jamharatu Ansaabil Arab uk 266

³⁵⁰ Yaaqutul Hamawiy, Muujamul Buldaan, 4/11, Al bilaad, Muujam Maalimul Hijaaz 5/224

sanamu mashuhuri la kiarabu la Lata,³⁵¹ ambalo Qur'ani iliteremka na kulitaja, katika kauli yake:

﴿أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٩﴾ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ ﴿٢٠﴾﴾ [النجم: 19-20]

"Mnawaonaje, enyi washirikina, waungu hawa mnaowaabudu: Lāta, 'Uzzā" "na mwingine wa tatu ni Manātu, je hao wamenufaisha au kudhuru mpaka wawe ni washirika wa Mwenyezi Mungu? [An najmu: 19-20] Na lilishiriki kabila la Thakif dhidi ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika vita vya Hunain wakishirikiana na Hawazini na makabila mengineyo,³⁵² na vita vikamalizika kwa Waislamu kupata ushindi dhidi yao baada ya kuparaganyika katika vita, na hii ndiyo iliyoashiriwa na kauli yake Mtukufu:

﴿لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّذِيرِينَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ ۖ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَّمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ وَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ يَتُوبُ اللَّهُ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢١﴾﴾ [التوبة: 25-27]

Hakika ALLAH amewanusuru katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulipo kupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu, na ardhi ikawa na dhiki kwenu juu ya upana wake, kisha mkageuka mkarudi nyuma. Kisha Mwenyezi Mungu Alimteremshia utulivu Mtume Wake na Waumini wakasimama imara, na Mwenyezi Mungu Akawaongezea askari wasiowaona

³⁵¹ Kitabul Kubraa, Muujamu mastujima, 3/886, Yaaqutul Hamawiy, Muujamul Buldaan, 4/11, Al kubra.

³⁵² Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab. uk 491

miongoni mwa Malaika. Hapo Aliwapa ushindi juu ya adui yao na akawaadhibu wale waliokufuru. Hayo ni mateso ya Mwenyezi Mungu kwa wenye kuzuia dini ya Mwenyezi Mungu isifuatwe, wenye kuwakanusha Mitume Wake. Kisha ALLAH anamsamehe baada ya hapo anaye mtaka,na ALLAH ni msamehevu mpole" [Attaubah: 25-27]

Kisha akaenda Twaif Rehema na Amani ziwe juu yake mwezi Shawwal mwaka wa nane Hijiria, baada ya vita vya Hunaini, na akauzingira takribani siku ishirini, wakazidi kuwa waasi, pamoja na kutumia vifaru na makombeo, na ngome za Twaif zilichangia kuuzuia mji huo.

Na baada ya ndoto aliyoiona Rehema na Amani ziwe juu yake, alitambua kuwa Twaif haitofunguliwa kwa wakati huo, akaondoka kurudi Makka.³⁵³.

Na katika eneo la Joorana Alihifadhi Rehema na Amani ziwe juu yake ngawira, ulimjia msafara kutoka katika kabila la Hawazini nao ni watu wa vijijini wa Twaif, walikua na mateka katika vita vya Hunaini, wakaja wakiwa ni madhalili wakiomba utetezi kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- wakimuomba arudishe mali zao na mateka wao, akawaacha huru Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- wale mateka aliokuwa nao, Waislamu wote wakaiga kutoka kwake wakawaacha huru mateka wa Hawazini, na kiongozi wao alikuwa ni Maliki bin Auf alikimbia kwa watu wa thakif katika mji wa twaif, Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akawaeleza watu wake kuwa: ikiwa atakuja akiwa ni Muislamu na mwenye kutubia basi atamrudishia mali zake na familia yake, na ziada ya ngamia mia

³⁵³ Tazama: Vita vya Hunaini na kuzingirwa kwa Twaif ndani ya kitabu hiki.

moja, Maliki akasikia habari hiyo, akaja kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akitubia na akimsifu Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, akampa uongozi kwa waliosilimu katika watu wake, na akamuamrisha apigane na Thakif na awabane katika mji wa Twaif, kiasi kwamba akawa ndio hifadhi ya wanaokimbia baada ya kufunguliwa Makka, akaanza kuwabana kabila la Thakif na akiwapiga vita, hali ikawa mbaya kwa Thakif, ndani ya wakati huo huo alikuja Urwa bin Masoud Ath thaqafi kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akasilimu, na alikuwa ni mtu anayependeka kwa watu wake, akatoka kwenda kwao katika mji wa Twaif akiwaita katika Uislamu (Alipotokeza katika eneo la juu, hali yakuwa tayari amekwisha kuwaita katika Uislamu na akawatangazia dini yake, wakamrushia mishale kutoka kila upande ukampata mshale mmoja ukamuua, wakamuuliza urwa unasemaje juu ya kuuliwa kwako? Akasema: Hii ni heshima kanipa Mwenyezi Mungu, na ni shahada kaileta kwangu Mwenyezi Mungu, sina kwangu zaidi ya yale waliyoyapata mashahidi waliouliwa pamoja na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, kabla hajatoka kwenu, nizikeni pamoja nao, wakadai kuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alisema: "Hakika mfano wake katika watu wangu ni kama mfano wa mtu watu wa Yasini kwa watu wake"³⁵⁴Kisha baada ya tukio hili kwa miezi kadhaa kabila la Thakifu liliridhika kuwa halina uwezo wa kupigana vita na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- wakaandaa msafara, akaingia Abuubakari kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akamueleza kuhusu ujio wao kwake.³⁵⁵

³⁵⁴ Tazama Bin Hishaam Kitabu Kiiwacho Siirat Al-Nabawiyat juzuu ya 4/538;na Bin Hajar Al-Isaabat,juzuu ya 2/478.

³⁵⁵ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/539.

Na walipofika kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- aliwajengea hema upande wa msikiti wake, akawa Khalid bin Saidi bin Aswi anakwenda kati yao na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, mpaka wakaandika ujumbe, na aliyandika ujumbe wao ni Khalid kwa mkono wake, na walikuwa hawali chakula chochote kinachotoka kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mpaka kwanza ale Khalid, mpaka wakashilimu na wakahitimisha mkataba wao, na ilikuwa miongoni mwa yale waliyomuomba Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- awaachie Twaghiya, (Nalo ni sanamu la Lata) asilibomoe kwa muda wa miaka mitatu, akawakatalia hilo Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- walipoendelea kumuomba lau hata mwaka mmoja na anawakatalia, mpaka wakamuomba hata mwezi mmoja baada ya kurejea kwao, akawakatalia kuacha kitu chochote kiitwacho sanamu, bali walilitaka hilo kwa jinsi walivyokuwa wakionyesha nikuwa wasalimike kwa kuachwa sanamu hilo kwa wajinga wao na wake zao na watoto wao, na hawakupenda kuwatia hofu watu wao kwa kubomolewa sanamu mpaka uwaingie Uislamu, Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akakataa akamtuma Abu Sufian bin Harbi na Mughira bin Shu'uba ili wakalibomoe, na pamoja na hilo la sanamu pia walikuwa wamemuomba awasamehe kuhusu ibada ya swala, na masanamu yao wasiyavunje wao kwa mikono yao, akasema Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-: "Ama kuyavunja masanamu yenu nyinyi wenyewe kwa mikono yenu hilo tutakusameheni, na ama kuhusu kuswali, hakuna ubora wowote katika dini bila swala" wakasema: "Ewe Muhammadi tutaitekeleza swala hata kama kutakuwa na unyonge ndani yake"³⁵⁶

³⁵⁶ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/540.

Na waliposilimu na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akawaandikia ujumbe wao, alimfanya Othman bin Abil Aswi kuwa kiongozi wao, na alikuwa ndiye mdogo kuliko wote kiumri, hii ni kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa na hamasa kubwa ya kujifunza Uislamu na kujifunza Qur'ani. Akasema Abuubakari kumwambia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, "Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika mimi nimemuona huyu kijana ndiye mwenye pupa kubwa kuliko wote ya kujifunza Uislamu na kujifunza Qur'ani",³⁵⁷Na aliendelea kuwa kiongozi wao kwa muda wote wa zama za Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, kisha katika kipindi chote cha utawala wa Abuubakari Swiddiq baada ya hapo.³⁵⁸

Na msafara huu ulijifunza sehemu katika Qur'ani na mambo ya Dini, na akakubali Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kuwapa jukumu la kuyabomoa masanamu watu wengine, na kuwa yasiachwe hata sekunde moja, na akatuma msafara kwenda pamoja na jukumu lao ni kuwalinda kutokana na watu wao, ili waweze kutekeleza jukumu lao la kuyabomoa masanamu, wanawake wa kabila la Thakif wakayalilia masanamu yao,³⁵⁹Kisha Uislamu ukaenea katika kabila la Thakif na kwa watu wa Twaif wa mjini, wakawa wakazi hao ni miongoni mwa watu waliodumu katika Uislamu baada ya kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na wala hawakuritadi.³⁶⁰

³⁵⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/539-540.

³⁵⁸ Angalia kitabu cha Siyar Alaam Nubalaa, juzuu ya 2/374.

³⁵⁹ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/542.

³⁶⁰ Tazama: Abalaadhiry, Futuuhul buldaan uk. 115

Msafara wa bani Tamiim [965]

Hili ni moja katika makabila ya Adinan, wanajinasibisha kwa Murra bin Add, nalo ni katika makabila makubwa ya waarabu,³⁶¹ Makazi yao ni Bahrain na mashariki mwa Najidi na pande za Ahsaa.³⁶²

Na ulikuja msafara wao katika mwaka wa tisa wa Hijiria baada ya kurejea Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- kutoka katika vita vya Tabuk, na ilisemwa kuwa kuna msafara au mtu mmoja waliwaua kikatili watu wao kabla ya mwaka huu. Na ameweka wazi Bukhari katika sahihi yake mlango kamili kauita (Mlango wa msafara wa Banii tamim) Ametaja ndani yake hadithi nyingi.³⁶³

Na ulikuwa msafara wao ni katika misafara maarufu ya makabila kwa Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- katika hadithi, na kulikuwa miongoni mwao na viongozi maarufu kwa makabila yote ya waarabu, miongoni mwao ni Al Aqrau bin Haabisi, na Zabarkaani bin Badri, na Hab-haab bin Yazidi, na Atwaridi bin Haajib, na Uyaina bin Hisn na wengineo.³⁶⁴

Na msafara ulipofika Madina Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- alikuwa katika vyumba vya mama wa waumini, wakaingia

³⁶¹ Tazama: bin Hajari, Fat-hul bari, 16/205, bin Hazmi Jamharatu Ansaabil Arab uk 207.

³⁶² Bin Hisham, Assiratun nabawiyy, 4/575, Al hamdaan, Swafhatu Jaziiratul Arab uk 281.

³⁶³ Tazama Sahihi Bukhari, 4/115-116

³⁶⁴ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/560.

msikitini na wakaanza kumuita Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-: "toka uje ewe Muhammadi, kwani sifa zetu ni nzuri na kutukanwa kwenu ni kubaya"³⁶⁵ Akaudhika Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kutokana na kauli yao hiyo na akasema: "Mwenye sifa nzuri na kumdhalilisha mtu huyu ni mwenyezi Mungu pekee"³⁶⁶ Na kwa sababu yao ikateremka kauli yake Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يُتَادُونَكَ مِنْ وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ۗ وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّى تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [الحجرات: 4-5]

"Hakika ya wale wanaokuita, ewe Nabii, nyuma ya vyumba vyako kwa sauti ya juu, wengi wao hawana akili" Na lau wangalisubiri mpaka ukawatokea ingalikuwa bora zaidi kwao mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amewaamrisha wao kukuheshimu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha kwa yale yaliyotokea kwao ya madhambi na utovu wa adabu kwa kutojua kwao, ni Mwingi wa rehema kwao kwa kutowaharakishia mateso." [Al Hujuraat: 4-5]

Na baada ya kutoka Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- walimtaka amruhusu mzungumzaji wao Atwaridi bin Haajibu, akatoa hotuba ambayo ndani yake kulikuwa na: "Ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni zake fadhila na neema zilizo juu yetu, naye ndiye mstahiki, aliyetufanya sisi kuwa wafalme, na akatupa mali nyingi tunazozitumia kwa wema, na akatufanya kuwa watukufu miongoni

³⁶⁵ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/562.

³⁶⁶ Marejeo yaliyotangulia.

mwa watu wa mashariki, na akaendelea kuwasifia bani Tamim mpaka akamaliza hotuba yake.³⁶⁷

Alipomaliza Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** alimuamrisha Thabit bin Kaisi bin Shammasi amjibu, akasimama - Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- akatoa hotuba, na ilikuwa miongoni mwa yale aliyoyazungumza alisema: "Kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu ambaye mbingu na Ardhi ni katika viumbe vyake, akahukumu ndani yake maamuzi yake, na Kursiy yake (mahala pa kuweka miguu Rahman) imeenea elimu yake, na hapakuwa na chochote katu isipokuwa elimu yake. Na akaendelea na hotuba yake iliyokuwa imejawa na imani na ukweli na kuwalingania watu kuja kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kumsifia Mwenyezi Mungu na Mtume wake **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**
368

Baada ya hapo akasimama mshairi wa Tamim (Azzabarqaan bin Badri) na akatoa kaswida yake mbele ya Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, iliyokuwa imejikita katika kujifaharisha kwa watu wake bani Tamim, na miongoni mwa sehemu yake ni:

Sisi ni watukufu hakuna kiumbe mwenye kulingana nasi

³⁶⁷ Tazama: Nukuu ya hotuba kwa BIn Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/562

³⁶⁸ Tazama: Nukuu ya hotuba kwa BIn Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/562

Miongoni mwetu kuna wafalme na kwetu hunasibishwa masinagogi.³⁶⁹

Basi Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake akamuita Hassan Bin Thaabit ili amjibu baada ya kumaliza kwake, basi akasoma Hassan-Radhi za ALLAH ziwe juu yake- kaswida ambayo washairi hawawezi kuleta mfano wake miongoni mwayo ni:

Hakika watukufu wa kabila la Fihiri na ndugu zao *

Wamebainishia watu mwenendo wenye kufuatwa.

Anauridhia kila mwenye kuwa ndani ya moyo wake

na uchamungu na kheri zote hutengenezwa na hilo.

Na yalikuwa maana ya Qaswida aliyoisoma Hassan inabeba maana ya Uislamu uliokuwa na kiwango cha juu,na kujifaharisha nao,na kijifaharisha na Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na amani ziwe juu yake- na inasemekana kuwa Qaswida zilibadilishwa kati ya Zubriqaan na Hassan -Radhi zaAllah ziwe juu yake-na walipomaliza Aqrau bin Haabis akasema namuapia Baba yangu kwa hakika mtu huyu anamaandalizi ya kutosha,uzungumzaji wake ni mzuri kuliko uzungumzaji wetu,na mashairi yake ni yamepangika kuliko mashairi yetu,na sauti yake ni nzuri na tamu kuliko sauti zetu)(976)

Na kwa hakika watu walisilimu na wakajifunza kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake- na akawaamrisha baadhi ya Maswahaba wajifunze na wakawa

³⁶⁹ Tazama: Bin Hishaam,siirat An-nabawiyat juzuu ya 4/8564. neno Al-baiat linakuja kwa maana ya kutawalisha na kusimika wafalme,Al-muujumul wasiitwu ukurasa wa 79.

wakimuuliza Mtume wa Mwenyezi mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-**

Na kwa hakika maepokea Bikhari katika sahihi yake kutoka kwa Imran Bin Huswain amesema: lilikuja kundi katika kabila la bani Tamim kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-** Akasema: "Ikubalini habari njema enyi bani Tamim",wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu tayari umetupa habari njema basi tupatie, likaonekana hilo katika uso wake, likaja kundi jingine kutoka Yemen wakasema: Ikubalini habari njema ikiwa hawatoikubali bani Tamim, wakasema bani Tamim: "Tumeikubali ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu"³⁷⁰

Na msafara ulipotaka kurejea katika miji yao aliwaruhusu Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na Abuubakari na Omari walikuwa na rai mbili tofauti kuhusu swala la kuchagua kiongozi wa watu hawa. Amepokea Bukhari kutoka kwa Abdullahi bin Zubair -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: "Walikuja wasafiri kutoka katika kabila la bani Tamim kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-** Abuubakari akasema: Mpe uongozi Ka'kaau bin Ma'bad bin Zurara, Omari Akasema: "Mpe uongozi Akrau bin Habisi, Abuubakari akasema: "Hujataka zaidi ya kunipinga, Omari akasema: "Hapana, sijataka kukupinga, wakabishana mpaka wakanyanyua sauti zao, hapo ikateremka katika swala hilo kauli yake Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُقِيمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ؕ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢١﴾
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ
بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٢٢﴾ [الحجرات: 2-1]

³⁷⁰ Tazama sahihi Bukhari, mlango wa msafara wa bani Tamim, Hadith namba: 4365.

Enyi ambao mliyo amini msitangulize baina ya mbele ALLAH na Mtume wake,hakika ALLAH ni msikivu mjuzi. (Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui) (2) [Al Hujurat: 1-2] mpaka mwisho wa sura.³⁷¹

Msafara wa Bnii A'amir:

Bani Aamiri wanatokana na Swa'swa kutoka kwa kaisi kutoka kwa Ailan kutoka katika kabila la Mudhwar.³⁷²wanaishi katika mji wa Najidi uliokaribu na Madina, Na alikuwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katuma watu katika masahaba zake kwenda kuwalingania, wakauawa katika tukio maarufu la kisima cha Mauna.³⁷³

Na ulikuja msafara wa Bani Aamiri akiwemo Aamiri bin Tufail, na yeye ni miongoni mwa waliowapita vita masahaba wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika kisima cha Mauna, na alikuwa mwarabu katili, Mtume akamtaka asilimu. akasema: "Unanipa nini nikisilimu?, Akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Utapata haki zote walizonazo Waislamu na majukumu yote waliyonayo Waislamu". Akasema kumwambia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-: "Nipe Uongozi baada yako" akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Hiyo si haki yako wewe wala kaumu yako, lakini chukua kamba za kufungia farasi, akasema: Mimi wakati huu

³⁷¹ Tazama: Sahihi BUKhari, kitabu tafsiri, "Suratul Hujurat", mlango wa (Walaa tarfauu) 6/46; Tazama pia tafsiri bin Kathiri, 2/1743

³⁷² Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab 2/271

³⁷³ Tazama: Tukio la kisima cha Mauna, ndani ya kitabu hiki.

niko katika kamba za farasi za Najidi, nipe Ngamia nawe nitakupa nyumba,³⁷⁴Akasema Rehema na amani ziwe juu yake, "Hapana," Aamiri akasema: "Hapana na mimi" Kisha akampa vitisho Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**:- Akisema: "Basi ngojeni nitahakikisha ninakuleteeni farasi na wapiganaji, Akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Mwenyezi Mungu atakuzuia" "Ewe Mwenyezi Mungu nitosheleze kwa huyu Aamiri bin Tufaili" akaota kinyama kooni, akawa anapiga kelele na maradhi mabaya nyumbani kwa saluuliya, kisha akachukia kufia katika nyumba ya saluuliya, akapanda Farasi yake, na akatoka nje huku akisema: Yaani nimeugua ugonjwa wa kinyama kama Ngamia, na inawezekanaje kufia katika nyumba ya saluuliya? Akaendelea kutembea mpaka akafia mbali.³⁷⁵

Na alikuwa pamoja naye katika msafara huu Arbadi bin Kaisi, wakapania kumvamia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, na akarudi kwa watu wake, na alikuwa mtovu wa adabu na Mwenyezi Mungu, mpaka kuna wakati alisema: Ametuita Muhammadi tuabudu kitu ambacho natamani kingekuwa karibu yangu ningekichoma na mishale. Kisha baada ya hapo akaondoka baada ya kukaa takribani siku moja au mbili, akakumbwa na moto wa Radi ikamuunguza, na inasemekana iliteremka kwa sababu ya mtu huyu kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ وَالْمَلِكَةُ مِنْ خِيفَتِهِ وَيُرْسِلُ الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَنْ يَشَاءُ وَهُمْ يُجَادِلُونَ فِي اللَّهِ وَهُوَ شَدِيدُ الْمِحَالِ﴾ [الرعد: 13]

³⁷⁴ Neno wabar: (Ngamia) Hapa linakusudiwa kijijini likinasibishwa na wachungaji wa Ngamia, na neno Madar: Ni wakazi wa vijijini.

³⁷⁵ Bin Hishaam Siat Nabawiyat juzuu ya 3/ج4; Bin Kathiir, katika Tafsiiri yake juzuu ya 1/1008.

"Na radi linamtakasia Mwenyezi Mungu sifa Zake njema, matakaso yanayoonyesha dalili kwamba linamnyenyekea Mola Wake. Na Malaika wanamwepusha Mola wao na kila la upungufu kwa kumuogopa kwao Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anatuma vimondo vyenye kuangamiza, Akawaangamiza kwavyo anaowataka kati ya viumbe vyake. Na makafiri wanabisha juu ya upweke wa Mwenyezi Mungu na uweza Wake kufufufua, na hali Yeye Ana uweza mwingi na nguvu na ujabari wa kuwatesa waliomuasi." [Radi: 13]³⁷⁶

Msafara wa banii Hanifah: [984]

Bani Hanifa ni kabila linalojinasibisha kwa Bani Bakri bin Waili.³⁷⁷

Makazi ya bani Hanifa yalikuwa katika mji wa Yamama katika bonde lililojulikana kwa jina lao, na sehemu zake, na yalikuwa ni maeneo mashuhuri kwa kilimo cha ngano na mazao mengine, bidhaa zake zilikuwa zikifika Makka,³⁷⁸Na pia kulikuwa kati yao na Makuraishi miamala ya kibiashara. Na kabla ya kufunguliwa mji wa Makka aliwahi kutekwa mmoja kati ya viongozi wao ambaye ni Thumama bin Uthali, Amepokea Bukhari kutoka kwa Abu Huraira Amesema: Alituma Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- Wapanda Farasi kuelekea maeneo ya Najidi wakaja na mtu mmoja kutoka katika kabila la Bani Hanifa akiitwa Thumama bin Uthali, wakamfunga katika nguzo miongoni mwa nguzo za Msikiti, akatoka

³⁷⁶ Tazama: Bin Hajari, Al Iswaba, 1/1008, bin Hisham, Assiratun Nabawiyya, 4/568.

³⁷⁷ Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab 2/ص309

³⁷⁸ Tazama: Abdallah bin Muhammad bin Khamis, Mu'jamul Yamama, chpa ya pili, Arriyadh 1400H

kwao Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Akasema: "Umekuwaje we Thumama?" Akasema: "Ah, mimi sina zaidi ya kheri ewe Muhammadi: Ikiwa utaniua basi utakuwa umeua ndugu yako wa damu, na ikiwa utanisamehe basi utakuwa umemsamehe mtu mwenye shukurani, na ikiwa unataka mali niombe chochote utakacho. Thumama akaachwa mpaka kesho yake, kisha akasema kumwambia: "Unasemaje we Thumama?" Akasema: Yale yale niliyokueleza jana, ikiwa utasamehe basi utakuwa umemsamehe mtu mwenye shukurani, kisha akaachwa mpaka siku ya tatu, Mtume akasema: "Unasemaje we Thumama?" Akasema: "Ni yale yale niliyokueleza" Mtume akasema: "Mwacheneni huru Thumama" Akaondoka mpaka katika mtende uliokaribu na Msikiti, akaoga kisha akaingia Msikitini, Akasema: Ninashuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ninashuhudia kuwa Muhammadi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Ewe Muhammadi hapakuwa juu ya Ardhi hii na uso ninao uchukia kuliko uso wako, ila umekuwa uso wako unapendeka zaidi kwangu sasa kuliko nyuso zote, Wallahi (Namuapa Mwenyezi Mungu) Hapakuwa juu ya Ardhi na dini ninayoichukia kuliko dini yako, ila imekuwa dini yako inapendeka zaidi sasa kwangu kuliko dini yoyote,, Wallah hapakuwa na mji ninaouchukia kama mji wako, ila mji wako umekuwa unapendeka sana kwangu kuliko mji wowote, na ikiwa Farasi yako itatumika kunipeleka Makka kwenda kufanya ibada ya Umra we waonaje? Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Akampa habari njema na akamuamrisha afanye Umra, na alipofika Makka, kuna mtu alimwambia: "Umekuja katika dini yako?", Akasema: Hapana, bali nimesilimu pamoja na Muhammadi Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake- Na ninamuapa Mwenyezi Mungu hakuna kitakachokujieni kutoka

Yamama hata punje moja ya ngano mpaka aniruhusu katika punje hiyo Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-.³⁷⁹

Na Bukhari alimfanya Thumama kuwa mtu wa pekee kwa kutomuweka pamoja katika msafara, katika anwani ya mlango (Msafara wa bani Hanifa baada ya kusilimu kwake, na jinsi alivyoona Thumama ukweli wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na huruma yake na uzuri wa muamala wake, "Uso wako ulikuwa unanichukiza sana kuliko nyuso zote, lakini umekuwa ndio unapendeka zaidi kuliko nyuso zote")³⁸⁰

Na baada ya kusilimu kwake alitoka kuelekea Makka kwa ajili ya Umra. Na Makuraishi walipata taarifa za kusilimu kwake wakamkamata na wakamtia maudhi kisha wakamuachia, kwa kuhofia kuwa hilo lisije kuwaathiri katika swala la kupata chakula kutoka Yamama, ni kiukweli alipofika Yamama aliwazuia wasibebe chakula kupeleka Makka na wawabanie kiasi kidogo, watu wa Makka wakadhurika, wakaandika barua kwenda kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kuhusu hilo wakimkumbusha swala la kuunga udugu, akamuandikia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- awaache mahusiano ya biashara ya chakula kati yao na Makuraishi yaendelee kutoka Yamama.³⁸¹

Na hiyo ilikuwa ni sehemu ya vikwazo vya kiuchumi kwa Makka, na kusilimu kwa Thumama kulileta mchango mkubwa sana wa kuufikisha Uislamu katika mji wa Yamama ambao ndio makazi ya

³⁷⁹ Kaipokea Bukhari, Mlango wa msafara wa bani Hanifa, 4/117,118.

³⁸⁰ Bukhari, 4/117, bin Hisham, Assiratun nabawiya, 4/639.

³⁸¹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/639.

bani Hanifa, na watu wengi wakaathirika na kusikiliza ujumbe na lengo lake.

Na katika mwaka wa tisa wa Hijiria ilikuwa miongoni mwa misafara iliyokuja kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** ni msafara wa bani Hanifa, wakiwemo viongozi wao. Wakiwa pamoja na Musailamatul Kadhabu, kabla ya kudai kwake Unabii alikuwa katika mwanzo wa kulifikiria hilo.

Na aliwapokea Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** katika nyumba ya (Ramla bint Harithi), na palikuwa pameandaliwa kwa ajili ya wageni wa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, akawajia Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** na mkononi mwake kukiwa na kuti la mtende akiwa na baadhi ya masahaba akiwemo (Thabit bin Kaisi Al Shammās) akasimama kwake Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** akazungumza naye,³⁸²Na huenda riwaya nyingine ya Bukhari ndiyo iliyoeleza vizuri zaidi tukio kamili kuliko kulifafanua. Kwani amepokea bin Abbasi Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- Amesema: "Alikuwa Musailama Al Kadhabu kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** akaanza kusema: "Ikiwa Muhammadi ataniachia utume baada yake nitakuwa tayari kumfuata, na alikuja akiwa na watu wengi katika watu wake, Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** akamfuata akiwa pamoja na Thabit bin kaisi bin Shammās, na katika mkono wa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** kukiwa na kipande cha shina la mtende mpaka akasimama kwa Musailama akiwa na jamaa zake, akasema: "Laiti hata ungeliniomba kipande hiki nisingelikupa, na wala msitarajie kulipata jambo la Mwenyezi Mungu (Utume) kwenu nyinyi, na ikiwa nitaondoka basi atakuadhibu Mwenyezi Mungu, na mimi

³⁸² NI katika riwaya za Bukhari katika sahihi yake, kitabul maghazi, babu qiswatil As-wadi Al-ansiy, 5/119.

ninakuonyesha kile nilichoonyeshwa katika utume ambacho hujakiona, na ninakuachia huyu hapa Thabiti anakujibu kwa niaba yangu" Kisha Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- akaondoka akamuacha. Anasema bin Abbas: Nikauliza kuhusu kauli ya Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- "Na mimi ninakuonyesha yale niliyoonyeshwa katika utume ambayo hukuonyeshwa".³⁸³.

Na imekuja katika ndoto aliyोजना Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*-, kama ilivyokuja katika Bukhari kutoka kwa Abuu Huraira, anasema: Amesema Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*:- "Siku moja nikiwa mimi nimelala nililetewa hazina, yakawekwa katika viganja viwili mataji mawili ya dhahabu, likanishangaza hilo, Mwenyezi Mungu akanifunulia wahyi kuwa ebu zipulize hizo, nikazipuliza zikaondoka, nikazitafsiri hazina hizo kuwa ni waongo wawili ambao mimi niko nao wakati huu, yule wa Sanaa (Yemen) na yule wa Yamama".³⁸⁴

Jibu la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu lilikuwa ni jibu la kukata kauli na lenye nguvu mbele ya muongo yule.

Bani Hanifa waliungana pamoja na Musailama pindi alipodai utume, wakamfuata bani Hanifa aliporejea Yamama lilikuwa kundi kubwa, pale aliposema mmoja wao: "Ninashuhudia kuwa wewe ni muongo, lakini muongo wa kabila la Rabi'a tunampenda kuliko mkweli wa kabila la Mudhar"³⁸⁵

³⁸³ Tazama: Riwaya ya Bukhari, Kitabul Maghazi, Mlango wa msafara wa bani Hanifa 5/118.

³⁸⁴ Tazama: Riwaya ya Bukhari, Kitabul Maghazi, Mlango wa msafara wa bani Hanifa 5/118.

³⁸⁵ Twabari, Tarikh yake, Matukio ya mwaka wa kumi na moja, 3/514.

Na aliandika Ujumbe Musailama kwenda kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ukisema: "kutoka kwa Musailama mtume wa Mwenyezi Mungu kwenda kwa Mtume Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu, Amani iwe juu yako, ama baada ya kusema hayo; kwa hakika mimi nimeshirikishwa katika jambo la utume pamoja nawe, na kwa hakika sisi tuna haki ya nusu ya Ardhi na Makuraishi wana haki ya Nusu iliyobakia, lakini makuraishi ni watu wenye kupituka mipaka) (995)

Na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akamjibu: "kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema na mwenye kurehemu, ujumbe kutoka kwa Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwenda kwa Musailamatul Kaddhab (Muongo). Amani iwe juu ya mwenye kufuata uongofu, ama baada ya kusema hayo; Nakufahamisha kuwa Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu anamrithisha amtakaye katika waja wake na mwisho mwema ni wa wacha Mungu". Na barua zake na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- zilikuwa katika mwaka wa kumi wa Hijiria.³⁸⁶

Na lilipata nguvu jambo la Musailama pamoja na wale aliokuwa nao, na wakawapa vitisho waislamu katika mji wa Madina baada ya kifo cha Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, Na ilikuwa katika kazi za mwanzo za Abuubakari Swiddiq -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- ni kuwamaliza walioritadi, akatuma majeshi matatu kwa ajili ya kupigana na Musailama, ambaye nguvu yake iliongezeka baada ya kujiunga pamojanaye makabila mengine ya bani Tamim kwa muda maalumu, mpaka pale waislamu walipoweza kuwamaliza walioritadi, katika vita maarufu vya Yamama ambavyo walikufa mashahidi masahaba wengi katika masahaba wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na walikuwa zaidi ya mia tatu, kukiwa

³⁸⁶ Twabari, Tarikh yake, 3/248

miongoni mwao na maanswari (watu wa Madina) na alikuwa miongoni mwao Zaidi bin Khatwab kaka yake na Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- na Abuu Dujana na wengineo.³⁸⁷

Misafara ya Yemen:

Yemen inakusanya eneo kubwa. Na katika zama za utume kulipatikana makabila mengi. Na mahusiano kati ya miji hiyo yakiwemo makabila na wakazi wake na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- yalikuwa ni ya tangu wakati wa mwanzo alipotumwa Rehema na Amani ziwe juu yake na kabla hata hajahama kwenda Madina Munawara, na ulikuwa mji mmoja au kabila moja na misafara mingi tofauti tofauti, na matukio mengi yenye uhusiano na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ambayo ni vigumu kuyaweka mahala pamoja.

kumtuma kwake Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- Muadh bin Jabali -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- yeye pamoja na viongozi wake kwenda Yemen kulikuwa na mchango mkubwa wa kuja misafara mingine ya ziada mwishoni mwa uhai wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-³⁸⁸. Na katika misafara muhimu zaidi kati ya hiyo ni:

³⁸⁷ Rejea ufafanuzi wa vita katikakitabu Al futuuhul Islaamiyya abra usuur, cha Abdul Azizi A umari, uk, 103, na Twabari, Tarikh yake, 3/252.

³⁸⁸ Tazama: Bin Hisham Nabawiyat juzuu ya 4/592 Mahdi Rizqi Ilah ,Al- siirat Al- Nabawiyat fii dhauil maswaadiri Al asliyya. 6/676

Msafara wa Al-ash'aryiina:

Wanajinasibisha kwa Ash'ari bin Zaidi bin Kahlan bin Sabai, na makazi yao ni Yemen.³⁸⁹

Na ulipofika msafara wao akiwemo Abuu Mussa Al Ash'ariy - Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Akasema Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**: "Wamekuja watu wa Yemen, hawa wana vifua laini (ni watu wenye huruma) na wana nyoyo dhaifu (ni wepesi wa kuelewa haki) na imani iko Yemen, na utambuzi wa sheria (Fiq-hi) uko Yemen, na hekima iko Yemen"³⁹⁰.

Na katika hadithi nyingine nikuwa yeye Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** alisema: "Wamekujieni watu wa Yemen kana kwamba ni mawingu(kwa wingi wao) hao ndio watu bora zaidi katika Ardhi hii"³⁹¹

Walikuwa na imani na kusadikisha, na kukubali kauli na amri zote za Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** bila kusita sita, na kufika kwao kuliambatana na msafara wa bani Tamim kwa wakati mmoja. Imepokelewa kutoka kwa Imran bin Huswain -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: "lilikuja kundi katika kabila la bani Tamim kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** Akasema: "Ikubalini habari njema enyi bani Tamim",wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu tayari umetupa habari njema basi tupatie, likaonekana hilo katika uso wake, likaja kundi jingine kutoka Yemen

³⁸⁹ Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab uk 397

³⁹⁰ Kaipokea Muslim, Tazama bin Qayyim, Zaadul Maadi, uk, 667; Na kaipokea Bukhari, kitabul Maghazi, Mlango wa kuja AL Ash'ariyyiin na watu wa Yemen, 5/122.

³⁹¹ Kitabu Zaadul Maad cha Bin Qayyim, uk 667.

wakasema: Ikubalini habari njema ikiwa hawatoikubali bani Tamim, wakasema bani Tamim: "Tumeikubali ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu"³⁹²

Na imepokelewa pia kuwa wao walikuwa wakijifunza kutoka kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** na wakimuuliza kuhusu mambo mbali mbali, miongoni mwake ni swali la mwanzo wa kuumba, ikawa miongoni mwa yale aliyoyasema Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**: "Alikuwapo Mwenyezi Mungu peke yake na hapakuwa na kitu chochote zaidi yake, na Arshi yake ilikuwa juu ya maji, na akaandika katika ubao kila kitu, na akaumba mbingu na Ardhi"³⁹³

Na inaonekana wazi katika riwaya hizi kuwa wao walianza mapema kusilimu kwao, kabla hata ya kufika msafara wao kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, bali hata baadhi yao kushiriki katika kuhama kwenda Habasha na katika ufunguzi wa Khaibar.³⁹⁴

Msafara wa bani Muraad (Fur-wat bin misiik)

Muradi ni kabila asili yake linatokana na Kahlan kutoka sabai Al Himyariya,³⁹⁵Na linaishi Yemen na liko jirani na kabila la Hamdan, na

³⁹² kaipokea Bukhari katika sahihi yake, kitabul Maghazi, mlango wa Ash'ariyiin wa ahlul Yaman, 5/122.

³⁹³ Kaipokea Bukhari, kitabu badi il khalq, 4/73.

³⁹⁴ Angalia ufunguzi wa Khaibar kutoka katika kitabu hiki.

³⁹⁵ Bin Hazmi, Jamharatu ansaabil Arab, uk 406, 407.

linahesabika ni kabila lililokuwa chini ya wafalme wa kinda katika maeneo hayo.³⁹⁶

Na alikuja Fur-wat bin Misyak Al Muraadi kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** katika mji wa Madina Munawara kwa ajili ya kusilimu katika mwaka wa tisa wa Hijiria, na akazungumza na Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** kuhusu wale waliouawa katika watu wake katika vita kati yao na kabila la Hamdan, Akasema Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**: "Ama hilo halijawazidishia watu wako katika Uislamu isipokuwa heri"³⁹⁷

Na alitumia Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** bwana huyu katika makabila kadhaa ya Yemen.

Msafara wa Hamdan:

Hamdan ni kabila la Yemen linalorudi kwa Kahlan bin sabai.³⁹⁸ Makazi yake ni Yemen katika pande za Sukun na Hashid, na linaishi karibu na kabila la Ash'ariyiin, Na baadhi yao walifika Makka, na wakaungana na Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** kabla ya baiatul akaba ya kwanza, na walisikia kutoka kwake, kama walivyosikia wengine wakati Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu**

³⁹⁶ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/581.

³⁹⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/583.

³⁹⁸ Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arabuk 392

yake- akijitangaza mbele ya makabila kabla ya kuhama,³⁹⁹mpaka uelewa wao juu ya uislamu ukaongezeka na ukawa mwingi.⁴⁰⁰

Ukaja msafara wao katika mji wa Madina Munawara katika mwaka wa tisa wa Hijiria, baada ya kurudi Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kutoka katika vita vya Tabuku,⁴⁰¹na kulikuwa na idadi kubwa ya viongozi wao, wakiwa na mavazi maalumu na vipandwa vya kipekee. (wakiwa na vipande vya nguo za pamba, na vilemba vya kiyemen, kukiwa na urembo katika vipandwa vyao, wakiwa na urembo na nakshi"⁴⁰²

Na watu wakirindima kwa beti za nyimbo za mashairi, na muonekano wao na nyimbo zao ziliwafanya watu wa Madina wageuke kuwatazama kwa mshangao! Wakaja wakimkubali Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, Akasimama kiongozi wao Maliki bin Namat, akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kizazi cha Hamdan kuanzia wa mjini na vijijini wamekuja katika mkusanyiko uliokuja haraka, wakiwa wameshikamana na kamba za Uislamu, hawaogopi katika jambo la Mwenyezi Mungu lawama za mwenye

³⁹⁹ Assakuun na Assakaasiku ni mikoa iko Yemen, inanasibishwa katika kabila hilo kwa jina hilo hilo, tazama kitabu Yaqutu Hamawiy, na Mu'jamul Buldan 3/229.

⁴⁰⁰ Al Hamdan, Swifatu Jaziiratul Arab, uk 101, 105.

⁴⁰¹ Bin Sa'd, Attwabaqaatul kubraa, 1/341, bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/588.

⁴⁰² Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/597. (Na urembo wa vipando umetengenezwa kutokana na mbao, na neno Mahriya, na Arhabiya: ni ngamia wanaonasibishwa katika kabila la Mahriya la Yemen na kabila la Arhabiya "Bin Hisham, 4/597, Hamish namba: 3,4,5)

kulaumu, kuanzia maeneo ya Kharif na Yamu, watu wa Sud na Kud, Wamekubali ujumbe wa Mtume, na wameachana na miungu na mizimu, ahadi yao haitovunjwa kwa muda wote ambao nuru itaendelea kun'gaa, Na uoto wa asili na jangwa vikibakia" (Yaani hawatobadili imani yao kwa lolote liwalo)⁴⁰³⁴⁰⁴

Na aliwaandikia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ujumbe kwa ajili ya kuyalinda maeneo yao.⁴⁰⁵

safara wa Kindi:

Kinda ni kabila maarufu la kiyemen linarudi asili yake kwa kahlan bin Sabai.⁴⁰⁶Na makazi yake ya asili ni Yemen, maeneo ya Sakasiki na Sakuun, Na limeenea katika maeneo mbali mbali katika miji ya ya kiarabu, na wana utawala na wafalme wanaofika mpaka sehemu za Sham (Iraq, Syria, Palestina, Jordan) Na uliwafikia Uislamu kwao katika nchi ya Yemen wakashilimu kabla ya kufika katika mji wa Madina, kama inavyoonekana wazi katika baadhi ya ushahidi, na msafara wao ulikuja ukiwa na watu themanini, akiwa pamoja nao Al Ash'ath bin Kaisi Al kindi kutoka Kinda asilia ya Yemen, Wakaingia kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- msikitini kwake, na

⁴⁰³ Neno Naswiya (kiarabu): maana yake: ni waheshimiwa katika jamii fulani.

⁴⁰⁴ Ya'fur: ni uoto wa asili, na swal'a: Ni Ardhi isiyokuwa na mimea mfano wa kipara, na maelezo haya yametoka kwa bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/598, Tazama: Hamish, 7,8.

⁴⁰⁵ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/598.

⁴⁰⁶ Tazama: Assamaani, Al Ansab, 10/485. bin Hazm, Jamharatu ansaabil Arab, uk425

msafara wao ulitembea kwa miguu, wakiwa wametia wanja machoni mwao, na wamevalia kanzu za vitambaa vya pamba, wakiwa mabegani wamezishonea vitambaa vya hariri, wakaingia kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akasema: "Hivi bado hamjasilimu?" Wakasema: "Tayari" Akasema: "Ni za nini hizi hariri katika shingo zenu?", Anasema mpokezi: walizichana na wakazitupa)⁴⁰⁷⁴⁰⁸

Na alipatwa na utata Ash'ath bin Kaisi baada ya kifo cha Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**-, isipokuwa alitubia juu ya hilo, na akashikamana na Uislamu, na akamuoa dada yake na Abubakari Swiddiq Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Mama Farwa, na alikuwa na mtihani mzuri katika zama za funguzi wa miji ya Kiislamu katika zama za Abubakari na Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao-⁴⁰⁹

Msafara wa Al-Azd(na Jursh):

Azadi hao ni Azadi Shanuuu, na wanarudi kwa Kahlan bin Sabaj,⁴¹⁰ na makazi yao ni maeneo ya Jurashi katika Ardhi ya Yemen.⁴¹¹

⁴⁰⁷ Neno kaftu (kiarabu) Maana yake ni kushona mkono wa bega kwa kitambaa. Tazama: hashiyatu bin Hisham katika Assira, Na: 5, 4/585

⁴⁰⁸ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 5/585.

⁴⁰⁹ Tazama: Tarjama yake: kwa bin Hajari, Al Iswaba, 1/51, na bin Sa'd, na Twabaqaat, 6/22, Adh-habi, Siyar A'laamun nubalaa, 2/37.

⁴¹⁰ Kitabu Assam'aani, Al Ansab, 1/198

Na alikuja Suradi bin Abdallah Al Azadi akiwa katika kundi miongoni mwa watu wake kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina katika mwaka wa tisa wa Hijiria,⁴¹²Akasilimu yeye pamoja na wale aliokuwa pamoja nao, na ukawa mzuri Uislamu wao, akamuamrisha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- yeye pamoja na wale waliosilimu pamoja naye kupigana jihadi na washirikina katika maeneo yao. Suradi bin Abdillahi akatoka akitembea kwa amri ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, mpaka akashuka maeneo ya jurashi nayo wakati huo ulikuwa ni mji uliotelekezwa, na ndani yake kulikuwa na makabila kadhaa katika makabila ya Yemen, na waliungana naye kabila la khuth'am wakaingia katika mji huo pamoja nao, kwani walisikia mwendo wa waislamu kwao, wakawazingira takribani mwezi mzima, na wakakatalia humo, kisha akarudi nyuma akawaacha mpaka alipofika katika mlima uitwao Shukri, wakadhani watu wa Jurashi kuwa amekimbia kwa kushindwa, wakatoka kumtafuta mpaka walipompata, akawavamia wote akawaua vibaya mno.

Watu wa Jurashi walikuwa wamewatuma watu wawili miongoni mwao kwenda kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina wazunguke wakiangalia, ghafla wakiwa kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- jioni nyakati za laasiri, mara Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akasema: "Ni katika mji gani wa Mwenyezi Mungu kuna SHUKRI?" Wakasimama mbele yake wale mabwana wawili kutoka Jurashi wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, katika mji wetu kuna mlima unaitwa SHUKRI, na ndivyo wanavyoita watu wa Jurashi, wakaendelea kusema: "Kwani

⁴¹¹ Tazama: Yaaqutul Hamawi, Mu'jamul Buldaan 2/11.

⁴¹² Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/587.

umekuaje mlima huo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Akasema: "Hakika wanyama wa Mwenyezi Mungu wanachinjwa huko sasa hivi" akasema: Wale mabwana wawili wakakaa kwa Abubakari au Othman, akawaambia: "Ole wenu msipozinduka! Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake- anakutangazieni misiba ya ndugu zenu huko mlikotoka, hebu simameni muende kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mkamuombe amuombe Mwenyezi Mungu awaondolee watu wenu mtihani walionao, wakasimama wakamuendea na kumuomba hilo. Akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu waondolee" Wakatoka kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kurudi kwa watu wao, wakakuta watu wao wamepatwa na msiba siku walipokumbana na Suradi bin Abdallah katika siku ambayo Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- aliwaambia, na katika muda ule ule wa tukio linafanyika.⁴¹³

Tukio hili liliwaathiri watu wa Jurashi, wakaandaa msafara maalumu ukaenda kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina wakakutana naye na wakatangaza Uislamu wao, na akawaandikia ujumbe Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na akawawekea mipaka maalumu ya kijiji chao, ukiwazuia watu wengine kuwaingilia.⁴¹⁴.

⁴¹³ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/587, 588.

⁴¹⁴ Tazama: Bin Hisham Nabawiyat juzuu ya 2/588 Mahdi Rizqi Ilah ,Al- siirat Al- Nabawiyat fii dhauil maswaadiri Al asliyya uk 655

Msafara wa Al-harith bin Ka'b:

Familia ya harith bin kaabu ni makabila mengi yanarudi katika asili yake kwa Kahlan bin Sabai.⁴¹⁵Na makazi yao ni maeneno ya Najrani.⁴¹⁶

Na walijulikana kwa waarabu kwa ukali na nguvu, na kuteka kwao sehemu nyingi za Najrani na pembezoni mwake. Na aliwatumia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- Khalid bin Walidi akiwa na jeshi la waislamu, na akamuamrisha awaite katika Uislamu kabla hajawapiga vita kwa muda wa siku tatu, na awakubalie ikiwa wataasilimu na wala asiwapige vita, akafika Khalidi katika maeneo yao na akatawanya wapanda Farasi kila upande wakiwaita bani Harith katika Uislamu wakiwafikishia: "Enyi watu silimuni msalimike" watu wakashilimu,⁴¹⁷akabakia kwao Khalidi yeye na wale aliokuwa nao katika maswahaba akiwafundisha Uislamu, na akiwasomesha kitabu cha Mwenyezi Mungu, na akiwafundisha mafundisho yake na dini yake.

Na Khalidi bin Walidi na wale aliokuwa nao -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao- wakafurahishwa na hilo,⁴¹⁸na Mwenyezi

⁴¹⁵ Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab uk 416

⁴¹⁶ Bin Hisham, Assiratun nabawiyya 4/593, na tazama: Muhammad bin Iwadh Al atiiq, Najrani fii Asrin nubuwwa wal Khilaafatu rraashida, Risaalatu Maajistiir Muqaddimatun liqismi taarikh wal hadhwara, kitivo cha elimu ya Jamii, Chuo kikuu cha Imam.

⁴¹⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/595.

⁴¹⁸ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/593.

Mungu akawatosheliza waislamu kupigana, na Khalidi akamuandikia ujumbe Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, na ilikuwa katika yale yaliyokuwa katika ujumbe wake ni: "Wamesilimu na wala hawajapigana, na mimi ninakaa kwao nikiwaamrisha yale aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu na kuwakataza aliyoyakataza, na ninawafundisha misingi ya Uislamu na Sunna za nabii wake -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- mpaka nitakapopata ujumbe mwingine wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, na Amani iwe juu yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Rehema zake na baraka zake". Na alimjibu Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- arudi akiwa na msafara miongoni mwao,⁴¹⁹akaja Khalidi Madina akiwa pamoja na msafara katika wao kukiwa na idadi kubwa ya viongozi wao, walipofika kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na akawaona, Akasema: "Ni akina nani hao watu ambao kana kwamba ni watu kutoka India" Wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hao ni watu kutoka katika kabila la bani Harith bin Ka'bu" waliposimama kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- wakamsalimia na wakasema: "Tunashuhudia kuwa wewe ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu nakuwa Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, akasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu: "Na mimi ninashuhudia kuwa Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu nakuwa mimi ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kisha akasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-: "Nyinyi ni wale ambao mkikemewa mnarekebishika?" wakanyamaza hakuna aliyemjibu miongoni mwao, kisha karudia tena mara ya pili, hakuna aliyemjibu, kisha akarudia mara ya tatu hakuna aliyemjibu, kisha akarudia mara ya nne, akasema Yazidi bin Abdi Madani: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi

⁴¹⁹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/593.

Mungu sisi ni wale ambao tukikemewa tunarekebishika" Naye akarudia hilo mara nne, akasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**:- "Laiti kama Khalidi asingeliniandikia ujumbe kuwa nyinyi mmesilimu na wala hamkupigana, basi ningelivitia vichwa vyenu chini ya miguu yenu" Akasema Yazidi bin Abdi- Madani: "Ama wallahi sisi hatujakusifia wewe wala Khalidi. Akasema: "Hivyo mmemsifia nani?" wakasema: "tumemsifia Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kutukuka aliyetuongoza kwako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Akasema: "Ni kwa sababu gani mlikuwa mkimshinda kila anayepigana nanyi zama za ujinga?" Wakasema: "Hatukuwa tukimshinda yeyote" Akasema: "Ndivyo ilivyo" Wakasema: "Tulikuwa tukitengeneza umoja na wala hatutengani, na wala hatumuanzi mtu kumpiga kwa dhulma". Akasema: "Hapo mmesema kweli" Na Mtume akawapa kuwa kiongozi wao Kaisi bin Huswain.⁴²⁰

Na baada ya msafara kurudi katika miji yao, aliwatumia Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**- Amri bin Hazim kuwa mwalimu wao na awape maarifa, na awe kiongozi wa kukusanya Sadaka (Zaka) na akampa ujumbe uliyo kamilika, ukiwapa habari njema na kuwaonya, na ukiweka wazi mafungu ya Zaka ya wajibu.⁴²¹

⁴²⁰ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/595.

⁴²¹ Tazama: Maelezo haya katika kitabu cha Bin Hisham, 2/1015, na tazama: Takhriji yake na hukumu ya hadithi hii kwa Mahdi Rizqullah, uk 66, na tazama: Muhammadi bin Iwadh Al utaibi, Najrani fii Asrin nubuwwa wal khilafatur rashida, Risala ya Majisteri, uk 75.

Misafara ta Wakristo wa Kiarabu: [1033]

Ukristo ulikuwa Ukienea katika idadi kubwa ya watu wa mjini na makabila ya vijijini katika miji ya waarabu, na watu wake walikuwa ni watu wa kitabu (Mayahudi na Wakristo) walikuwa na elimu, na uliwafikia ujumbe wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, wakawa baadhi yao na misafara na wengine wanakuja mmoja mmoja kukutana na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na wakamuamini.⁴²² Na yalikuwa maombi yake Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ni kuhakikisha ujumbe wake kuwa wa Dunia na huruma yake imuenee kila aliyeko Ardhi, kama wanavyojua kuhusu manabii waliotangulia, na kumsubiri kwao nabii wa mwisho, hilo liliwatofautisha na misafara mingine.

Msafara wa Al-daryyina:

Wanajinasibisha kwa Dari batwin kutoka kwa Lakhmi, na makazi yao ni sehemu tofauti tofauti kwanzia palestina na Sham karibu na Bait Lahmi na Ramla na sehemu nyingine.

Nao hao ni katika wakristo wa kiarabu ambao uliwafikia ujumbe wa Uislamu, na walikuja watu kumi miongoni mwao kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina baada ya kurudi kwake kutoka Tabuk, walikuwa wakristo wakashilimu, na wakaja kukutana na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akiwemo Tamim Addari na ndugu yake Nuaim, na aliwakatia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kabila la Tamim sehemu ya Ardhi huko Sham ikiwa bado haijafunguliwa. Na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikuwa na uhakika wa kuifungua Ardhi hiyo kwa muda wa karibuni, na Tamim walikubaliana na hilo na wakaliamini hilo, na ndiyo maana walimuomba Mtume -Rehema na Amani ziwe

⁴²² Tazama: Ufafanuzi maalumu wa misafara kwa Farouq Hamada, Al Alaaqaatul Islamiyyatun nasraaniya fii ahadi nubuwa, uk 93.

juu yake- awakatie Ardhi, ilipofunguliwa Sham katika zama za Abubakari Swiddiq -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- aliwapa Ardhi hiyo.⁴²³.

Na imekuwa mashuhuri hadithi ya Tamimu Dari kwa jina la Dajjali, kiasi kwamba Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** aliisikia kutoka kwake, na akawakusanya watu katika msikiti wake ili waje wasikilize kisa chake, ambacho kupitia kisa hicho inaonekana wazi kusafiri kwa Tamim Dari baharini kabla ya kufika kwake Madina Munawara.⁴²⁴

Msafara wa Taghlib:

Taghlabu ni moja ya makabila ya kiarabu ambayo yanajinasibisha kwa Taghlabu bin Wail kutoka kwa Rabia bin Nizar Al Adnani, nao wako matumbo mengi,⁴²⁵Na wanaishi kaskazini mwa kisiwa cha Arabuni, na wanasogea baadhi ya ndugu zao mpaka Sham na Iraq.

Na hili lilikuwa ni miongoni mwa makabila muhimu ya wakristo wa kiarabu, ndani yao kulikuwa na wanachuoni na wasomi wa kikristo wenye ushawishi mkubwa kwa watu wao na kwa makabila mengine, na walikuwa na mahusiano na Roma na Najrani, bali na Habasha pia (Ethiopia).

⁴²³ Angalia kitabu cha Siyar Aalaam Nubalaa, juzuu ya 2/442.

⁴²⁴ Tazama: Imamu Muslim katika sahihi yake, Fitina na alama za kiyama, mlango wa kisa cha jasusi, uk, 4325, Siyar a'lamun nubalaa, 6/373, 2/442, Hashiya namba: 2

⁴²⁵ Kitabu cha Assamaaniy, Al Ansaab, 3/62, na tazama bin Hazmi, kitabu: Jamharatu Ansaabil Arab uk 303

Na katika mwaka wa kumi wa Hijiria ulikuja msafara miongoni mwao kukiwa na watu kumi na sita,⁴²⁶Baadhi yao wakiwa ni wakristo na baadhi wakiwa tayari ni waislamu, Na aliwakaribisha Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** katika nyumba ya Ramla bint Harith,⁴²⁷ alipokuwa akikaribishia wageni. Na walimsikiliza Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** na wakafunga naye mkataba wa maridhiano, na ulipofika wakati wa kuifungua Iraq walikaidi, na baadhi yao wakaungana na waroma na wakavunja makubaliano yao, kukawa na muamala tofauti kutoka kwa Omari ikiwa ni matokeo ya kwenda kwao kinyume na makubaliano.⁴²⁸

Msafara wa Twayi:

Twayi ni kabila la kiarabu la Qahtwan linarudi kwa Kahlan bin Sabai.⁴²⁹Na makazi yao ni pande za Milima ya Aja-a na Sulma, Kaskazini mwa Najidi na inaitwa Jabalai Twayi,⁴³⁰Na linakwenda kabila hili mpaka Iraq na sehemu za kusini mwa miji ya Sham, pamoja na kaskazini mwa Kisiwa cha Arabuni.⁴³¹

⁴²⁶ Bin Sa'd, Twabaqaatul Kubraa, 1/361.

⁴²⁷ Al-iswabt cha Bin Hajar,juzuu ya 4/305.

⁴²⁸ Yahya bin Adam, Al Kharaj, uk 200, Al Qaasim bin Salam, Al Am-wal uk 36, Na Al Balaadhriy, Fat-hula buldaan uk 251

⁴²⁹ Bin Hajar, Jamharatu Ansabil Arab, Assam'aaan, Al Ansaab, 8/187.

⁴³⁰ Al Hamadhani, Swaf-hatu Jaziiratul Arab uk 266, Omar Ridhwaa kahaala, Mu'jamu Qabaailul Arab, 2/688.

⁴³¹ Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab uk 399, 400.

Ulikuwa msafara wa kabila la Twayi kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika mwaka wa tisa wa Hijiria,⁴³²na alikuwemo mtukufu wao Zaidul Khaili, naye ni mtoto wa Muhalal bin Zaidi bin Ghauth kutoka kwa Twayi.⁴³³Na alikuwa Zaidi ni mshairi maarufu katika wapanda farasi wa zama za ujinga, zilienea sifa zake kwa waarabu na akawa mashuhuri kwa ukarimu, na alisilimu yeye na wale aliokuwa nao baada ya kukutana kwao na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na uislamu wao ukawa mzuri.

Na ametaja bin Hisham kuwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- alisema kuhusu Zaidi kuwa: "Hajawahi kutajwa mtu kwangu katika warabu kwa ubora na fadhila zake kisha akaja isipokuwa nilikuwa ninabaini yuko tofuati na sifa zinazosemwa kwake isipokuwa Zaidul Khaili, kwani yeye hajayafikia yale yote aliyokuwa nayo" Kisha Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akamuita Zaidul Khairi, akampatia kiasi cha mali⁴³⁴na vipande viwili vya Ardhi, na akamuandikia vitu hivyo.⁴³⁵Na wakati wa kurejea kwake Najidi alifariki kwa sababu ya kuugua homa,⁴³⁶na inasemekana kuwa aliishi

⁴³² Bin hajari, Al Iswaba, 1/572.

⁴³³ Tazama: bin Hazim, Jamharatu Ansaabil Arab uk 404.

⁴³⁴ Ni sehemu maarufu iko mashariki mwa mji wa Haili hivi sasa.

⁴³⁵ Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/577, Tazama: Bin Sa'd, Atwabaqaatul kubraa, 1/321.

⁴³⁶ Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/578, Tazama: Bin Sa'd, Atwabaqaatul kubraa, 1/355.

mpaka zama za Omari bin Khatwab -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-.⁴³⁷

Msafara wa Fur-wat bin Amr Al-juzaamy: [1051]

Judham ni kabila la kiarabu linatokana na Kahlan kutoka kwa Qahtwan, na makazi yao yanakaribiana na Roma pande za Jordan katika mji wa Maan na pembezoni mwake mpaka magharibi mwa pande za Madian Magharibi mwa Tabuk, na linakwenda mpaka Palestina.⁴³⁸ Na alikuwa Farwa bin Amri ni kibaraka wa Waroma dhidi ya warabu wa Maan, na alikuwa katika Ukristo ukamfikia ujumbe wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, akasilimu na akatuma msafara kuja kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Madina ukiwa pamoja na zawadi kwa ajili ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, Waroma walipojua kusilimu kwake walimkamata wakamfunga kisha wakamuua, na imeelezwa kuwa alipopelekwa kwenda kuuawa alituma salamu zake kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika ubeti wa mashairi, na kwa Waislamu wote, miongoni mwake ni kauli yake:

Wafikishie Waislamu wote kuwa mimi

nimeusalimisha mwili wangu kwa Mola wangu mtukufu.

Msafara wa Ghasaan:

Ghasan ni kabila maarufu la kiarabu linarudi katika asili yake kwa Azadi.⁴³⁹ Walikuwa na mamlaka huko Damaskasi na pembezoni

⁴³⁷ Bin hajari, Al Iswaba, 1/572.

⁴³⁸ Tazama: Farouk Hamaadat, Al-alaqaatil Islaamiyat Al-Nasraaniyat Fil Ahad Nabawiy, ukurasa 127.

⁴³⁹ Tazama: Farouk Hamaadat, Al-alaqaatil Islaamiyat Al-Nasraaniyat Fil Ahad Nabawiy, ukurasa 155.

mwake na miji iliyoko kati yake na Himswi, Walikuwa chini ya Warumi, na wafalme wao walijulikana kwa jina la Ghasaasina, na walikuwa katika Ukristo, na walikuwa pamoja na warumi katika kupambana na Uislamu, na walikuja watu watatu kwa Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**- mwezi wa Ramadhani mwaka wa kumi wa Hijiria,⁴⁴⁰wakasilimu na wakarudi katika miji yao, na hawakuudhihirisha Uislamu kwa kuwaogopa waroma, na wakafariki wawili miongoni mwao, kabla ya kufunguliwa sham, na wa tatu akaenda kwa Abuu Ubaida kabla kidogo na mji wa Yarmuuk akamkirimu.⁴⁴¹

Kifo cha Ady bin Twaaii: [1057]

Ni bin Hatim Attwaiy mwarabu maarufu kuliko wote kwa ukarimu zama za ujinga, na ni mmoja kati ya viongozi maarufu wa kabila la Twayyi, alikuwa katika viongozi wa wakristo wa kiarabu⁴⁴²Rukuusiyya⁴⁴³Nalo ni kundi maarufu katika wakristo katika zama za Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, wanaunganishwa na mahusiano maalumu na wakristo wa Sham, na hasa hasa

⁴⁴⁰ Tazama: Bin sa'd, Twabaqaat, 1/338, bin Qayyim, Zaadul Maad, 3/669

⁴⁴¹ Tazama: Bin Qayyim, Zaadul maad, 3/669, Na bin Sayyidin nasi, Assiratun nabawiyya, 2/256.

⁴⁴² Walijulikana wakristo wa Iraq kwa kufuata kwao madhehebu ya Yakubi huko Sham na Nasturi huko Iraq, Abdul Azizi Athalabiy, Muhaadhwaraaati fii taarikhil Adiyani, uk 148, Al-fayuumi, katika Alfikari Addinil Jaahili, uk 68.

⁴⁴³ Arukuusiya: Ni kundi lina dini yake madhehebu yake kati ya wakristo na wasabai, lilijulikana katika zama za Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwa warabu. Mu'jamul Wasit, uk 369.

Ghasaasina, na wakristo wa Iraq kama Munadhara na wengineo, pamoja na mahusiano yake na kabila lake la Twayyi, alikuwa kiongozi miongoni mwa viongozi wao.

Na ziliwafikia habari za Uislamu mapema lakini wakasita kuwasiliana na Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- na kusikia kutoka kwake, pamoja nakuwa habari za Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- zilienea kwa warabu na waajemi (wasio warabu), na huenda kufika kwa Zaidul Khair "Zaidul Khail" kwa Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- pamoja na baadhi ya viongozi wa Twayyi na kusilimu kwao liliwaathiri tukio hilo kabila la Adiy, Kiasi kwamba anasema: Alitumwa Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*-: "Nikachukua zaidi ya jinsi ninavyokichukua kitu chochote, nikaondoka mpaka nikafika mwisho wa miji ya warabu karibu na Roma, nikajikuta hapo nilipo napachukua zaidi kuliko nilikotoka mara ya kwanza"⁴⁴⁴

Hakutoka kwenda kukutana na Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- isipokuwa baada ya kutekwa dada yake, na Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- akaishi naye vizuri na akawa akimpa habari zinazomuunganisha na ndugu yake Adiy bin Hatim.

Na hii nikuwa katika moja ya vikosi vya Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- vikiongozwa na Ally bin Abii Twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- vilivamia katika baadhi ya pande za Twayi, katika mwezi wa Rabi'u Thani (4) mwaka wa tisa wa Hjjiria, na lengo lao ilikuwa ni kulibomoa sanamu la (Ghulsu) na wakaweza kuwateka baadhi ya watu wa Twayi akiwemo Safana bint Hatim Twayi dada yake na Adiy,⁴⁴⁵ Akawekwa bint Hatim katika uzio

⁴⁴⁴ Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 142.

⁴⁴⁵ Siirat Nabbawiyat ya Bin Saad Juzuu 2/164.

kwenye mlango wa msikiti walipokuwa wakifungiwa mateka, akapita hapo Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na alikuwa ni mwanamke mrembo, akasema: Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mzazi wangu amefariki, na msafara wangu umeondoka, nakuomba unisaidie Mwenyezi Mungu atakusaidia nawe pia. Akasema: "Na ni upi msafara wako?" Akasema: "Ni Adiy bin Hatim". Akasema: "Huyu aliyemkimbia Mwenyezi Mungu na Mtume wake?" Safana anasema: Kisha akaondoka Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na akaniacha, mpaka ilipofika kesho yake, akapita tena nilipo, Nikasema kumwambia maneno yale yale niliyomwambia jana, na akanijibu mfano wa yale aliyoyasema jana. Nikasema: mpaka ilipofika kesho kutwa yake, akapita tena nilipo nikiwa tayari nimekwisha mkatia tamaa, akaashiria kwa mtu aliyekuwa nyuma yake katika watu wangu kuwa nimweleze huyo. Nikasema: Nikasimama nikamfuata nikamwambia: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mzazi wangu amefariki, na msafara wangu umeondoka, Nisaidie Mwenyezi Mungu atakusaidia pia" Akasema Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- "Sawa nimekubali, lakini tulia usiwe na haraka ya kuondoka mpaka upate mtu katika ndugu zako atakayekuwa mwaminifu kwako mpaka akufikishe katika mji wako" Kisha utanitaka ruhusa ya kuondoka" Nikauliza kuhusu mwanaume ambaye aliniashiria nizungumze naye mwanzo, nikaambiwa huyo ni Ally bin Abii Twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-, basi nikaendelea kukaa mpaka ulipokuja msafara kutoka kwa bani Bali au Kudhwa'a. Akasema: Ninataka kwenda kwa kaka yangu huko Sham. Akaendelea kusema: Nikamwendea Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Nikasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu tayari umekuja msafara katika watu wangu, ninawaamini na wanaweza kunifikisha. Akasema: Akanipa nguo nzuri Mtume -Rehema na Amani

ziwe juu yake- na akanipa kipando na akanipa matumizi ya njiani, nikaondoka nao mpaka nikafika Sham".⁴⁴⁶⁴⁴⁷

Adiyi bin Hatim alikuwa na taharuki kubwa baada ya kutekwa dada yake na kukimbia kwake Sham.

Na baada ya kukirimiwa dada yake na akarudi Sham, anaelezea Adiy hali ya kurudi kwa dada yake: "Wallahi mimi nilikuwa nimekaa kwa familia yangu, ghafla nikaona kipando kikinielekea mimi kwa amani" Akasema: " Ah, ni bint Hatim?!" Anasema: "Hakika kumbe alikuwa ni yeye, akasimamisha kipando mbele yangu upesi huku akisema: "Wewe ni msaliti dhalimu mkubwa, uliondoka na familia yako na watoto wako, na akawaacha wazazi wako wakiwa watupu" Akasema: Nikasema: Jamani dada yangu!, usiseme ila mazuri, Wallahi namuapa Mwenyezi Mungu kiukweli sina udhuru wowote, nikweli nilifanya hayo uliyoyasema. Akasema: "Kisha akashuka na akasimama mbele yangu, nikamwambia -Na alikuwa ni mwanamke asiyependa masihara- Unataka tufanye nyinyi katika jambo la huyu bwana? (Mtume), Akasema: Ninachokiona Wallahi nenda umfuate haraka sana iwezekanavyo, ikiwa kama atakuwa ni mtu aliyepewa unabii basi tufanye hara kwenda kupata fadhila zake, na kama atakuwa ni mfalme basi basi hautodhalilika katika utukufu wa yemen, Na wewe ni mtukufu. Akasema: Nikasema: "Wallahi haya ni mawazo mazuri"⁴⁴⁸⁴⁴⁹

⁴⁴⁶ Ni uzio maalumu unaotengenezwa kwa ajili ya mateka, Tazama: Bin Hisham, Assiratun nabwiyya, 4/579 (Hashiya namba: 3)

⁴⁴⁷ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/579.

⁴⁴⁸ Alinyanyua sauti yake kwa kumlaumu na masikitiko.

Na baada ya hapo alitoka Adiy bin Hatim kuelekea Madina Munawara kwa ajili ya kukutana na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, na hii ilikuwa kati kati ya mwaka wa tisa wa Hijiria.⁴⁵⁰

Na alipofika Madina watu walimpokea kwa heshima, na inaonekana kuwa alifika akiwa katika muonekano mzuri kwanzia katika mavazi yake na kipando chake, na huenda hata aliyekuwa pamoja naye katika safari, kiasi kwamba alifanya watu wa Madina wamtazame kwa mshangao, kisha akaingia msikitini kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akamtolea salamu: Akasema: " Ni nani huyo? Nikasema: Ni Adiyi bin Hatim. Akasimama Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akaondoka pamoja nami mpaka nyumbani kwake, Wallahi alikusudia kunichukua kwenda kwake, ghafla akakutana na mwanamke dhaifu kikongwe akamsimamisha, akasimama kwa sababu yake muda mrefu akizungumza naye kuhusu shida zake. Anasema: Nikasema moyoni mwangu: Wallahi huyu si mfalme. Anasema: Kisha akaondoka nami Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- mpaka tukaingia nyumbani kwake mara akachukua mto uliotengenezwa kwa ngozi ukawekwa sufi ndani yake, akausogeza kwangu akasema: "Kalia mto huu" Anasema: Nikasema: Hapana, kaa wewe, akasema bali kaa wewe, nikaukalia, na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akakaa chini, Akasema: Nikasema ndani ya nafsi yangu: Wallahi hii si tabia ya wafalme, kisha akasema: "Ehee, Ewe Adiyi bin Hatim haukuwa Rukuusiya (Moja ya Madhehebu katika ukristo zama hizo) Anasema: Nikasema: Nikweli, Akasema: "Haukuwa ukitumia kanuni ya robo, kuchukua mali ya ngawira kwa watu wako (Kama Chifu wao)? Anasema: Nikasema: Ni

⁴⁴⁹ Kitabu cha Historia ya Bwana Mtume cha Bin Hishaam juzuu ya 4/580.

⁴⁵⁰ Hii ni katika riwaya za bin Abii shaiba, A Maghaz, uk 142

kweli. Akasema: "Basi hilo halikuwa halali kwako katika dini yako" Anasema: Nikasema: Wallahi ni kweli. Anasema kwa hayo nikabaini kuwa yeye ni Nabii aliyetumwa anayajua wasiyoyajua watu. Kisha akasema: "Huenda wewe Adiyi kinachokuzuia kuingia katika dini ni kwa sababu ya umasikini unaouona walionao waliyoko ndani ya dini, Wallahi, Si muda mrefu zitafurika mali kwao mpaka atakakosekana wa kuzichukua. Na huenda pia wewe kinachokuzuia kuingia katika dini hii ni kwa sababu ya wingi wa maadui unaowaona, na uchache wa idadi ya waliyoko ndani ya dini. Wallahi namuapa Mwenyezi Mungu si muda mrefu utakuja kusikia mwanamke akitoka Kadisia (Iraq) mpaka atafika kuizuru nyumba hii (Al-ka'ba) wala haogopi chochote" Na huenda wewe pia kinachokuzuia kuingia katika dini hii ni kwa sababu ya kuona kuwa ufalme uko kwa watu wengine na sisi hatuna ufalme, Wallahi si muda mrefu utakuja kusikia Makasri meupe yakifunguliwa katika Ardhi ya Babeli (Iraq)" Anasema: Nikasilimu. Na alikuwa Adiyi akisema: Tayari yametokea mawili katika hayo aliyoyasema, na limebakia la tatu, Na wallahi litakuwa, Na niliyaona Makasri (Ikulu) nyeupe huko Babeli zikifunguliwa, na nilimuona mwanamke akitoka Kadisia (Iraq) akiwa juu ya mnyama na wala haogopi chochote mpaka anafika kuhiji katika nyumba hii (Al'ka'ba) Nami namuapa Allah hilo la tatu pia litakuwa, mali zitabubujika mpaka kusiwe na mtu wa kuzichukua"⁴⁵¹

Na ulimazika mkutano wa Adiyi kwa kusilimu chini ya mikono ya Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*- kwa kukinaika vizuri kwa hoja alizopewa alizosisikia wakati wa mazungumzo yake alipokutana na Mtume -*Rehema na Amani ziwe juu yake*-, na kutokana na yale

⁴⁵¹ Attwabari, Tarikh yake, 3/150, Na tazama: Riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, na tazama: Bin Abii Shaiba, Al Maghazi, uk. 142, Na bin Hisham, Assiratun nabawiyya 4/581.

aliyoyaona kwanzia unyenyekevu wake na ukarimu wake, na tabia zake njema, na kuujua kwake Ukristo na asili yake, na ni namna gani ulivyopotoshwa. Na mambo aliyokuwa akiyafanya Adiyi ikiwemo kuchukua robo ya mali katika ukristo, ambayo ni haramu kwake.

Na mazungumzo haya yalikuwa marefu, na huenda alifanya mahojiano na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwa zaidi ya mara moja na zaidi ya siku moja, kwa muda wote aliokaa Madina, na miongoni mwa hayo nikuwa: Siku moja aliingia kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na shingoni kwake Adiyi kukiwa na msalaba uliotengenezwa kwa madini ya fedha, basi Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akasoma aya hii:

﴿اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرَهْبَتَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا إِلَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ﴾ [التوبة: 31]

"Mayahudi na Manaswara wamewafanya wanavyuoni na watu wema kuwa ni miungu wenye kuwawekea hukumu za sheria, wakawa wanajilazimisha kuzifuata na wanaacha sheria za Mwenyezi Mungu. Na pia walimfanya Al- Masīḥ, 'Īsā mwana wa Maryam, kuwa ni mungu, wakamuabudu. Na hakika Mwenyezi Mungu Amewaamrisha wao wamuabudu Yeye Peke Yake, bila ya mwingine. Yeye Ndiye Mungu wa haki. Hakuna mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Yeye. Amejiepusha na Ametakasika na kila kile wanachokizua watu wa ushirikina na upotevu." [Suratu Tauba] Akasema: Wao hawakuwaabudu, Akasema: "Ndivyo hivyo, wao waliwaharamishia halali, na wakawalalishia haramu, na wao wakawafuata kwa hilo, na huko ndiko kuwaabudu hao" Na akasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-: "Ewe Adiyi, Hivi unasemaje? Inakukera nini ikiwa patasemwa Allahu Akbaru (Mungu Mkubwa)? Hivi kitu gani chochote unachokijua ni kikubwa kuliko Mwenyezi Mungu? Kipi kinakukera? Unakereka nini pakisemwa: Laa ilaaha illa llahu (Hapana

Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu?) Je wajua Mungu mwingine zaidi ya Allah? Kisha akamuita kuingia katika Uislamu na akasilimu, na akatoa shahada ya kweli.⁴⁵²

Na kulikuwa kusilimu kwa Adiyi bin Hatim ni msukumo kwake wa kujifunza kutoka kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na kuuliza yale yanayomtatiza. Na miongoni mwa hayo ni yale yaliyothibi katika sahihi Bukhari (Kutoka kwa Adiyi bin Hatim Amesema: Nilisena: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika mimi huwatumba mbwa waliofunzwa, na ninataja jina la Mwenyezi Mungu, akasema: "Ukiwatumba mbwa waliofunzwa na ukataja jina la Mwenyezi Mungu juu yake, basi kula", Nikasema: Na ikiwa watakiua kiwindwa? Akasema: "Hata wakikiua, madamu hajashiriki mbwa mwingine zaidi yao, kwani wewe ulitaja jina Mwenyezi Mungu kwa mbwa wako na wala hukutaja kwa mbwa wa mtu mwingine" Nikamwambia: Mimi hurusha mkuki kwa kiwandwa na ukakipata. Akasema: "Utakapotupa mkuki kwa kiwandwa kikapata basi kula, na ikiwa kitajichoma chenyewe basi usile kwani hicho ni sawa na mzoga" Na katika tamko jingine la kwao pia (Bukhari na Muslim) "utakapomtuma mbwa wako basi taja jina la Mwenyezi Mungu akikukamatia na ukakikuta kiwindwa kiko hai basi kichinje, na ukikuta kakiua na hajala chochote pia kula, ikiwa mbwa atakichukua kile alichokiua, na katika riwaya nyingine, ikiwa atakula basi usile, kwani nachelea huenda akawa kajiwindia mwenyewe"^{453, 454}

⁴⁵² Tafsiir Ibnu Kathiir.juzuu 1/874.

⁴⁵³ Kaipokea Bukhari katika sahihi yake, Kitabu cha kuchinja na kuwinda, mlango wa Mishale, 6/218. (Na neno waqidh: Ni mnyama aliyekufa kwa kupigwa na wala hajajeruhiwa akatokwa na damu, nayo ni ile iliyokuja katika kauli yake Mtukufu: "Mmeharamishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama Aliye chinjwa

Adiyi bin Hatim aliipenda dini na mihimili yake, mpaka ilipokelewa kutoka kwake, -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Amesema: "Haukuingia wakati wa swala isipokuwa na mimi nilikuwa na shauku nayo".⁴⁵⁵.

Na imethibiti yakuwa Adiyi bin Hatim alikuwa amethubutu katika Uislamu wakishirikiana na Abubakari Swiddiq katika utawala wake katika zama za walioritadi, Alichangia kukusanya sadaka za watu wake, na kuwatetea waislamu dhidi ya walioritadi. Ametaja Bukhari katika sahihi yake mlango akauita kwa jina la (Kisa cha msafara wa Twayi) Na hadithi ya Adiyi bin Hatim, alitaja ndani yake hadithi ya Adiyi bin Hatim, Amesema: Tulikwenda kwa Omari bin Khattwab tukiwa msafara, akawa akiita mmoja mmoja, na anawauliza majina, nikasema: Kwani mimi hunijui ewe kiongozi wa waislamu? Akasema: Ndiyo, Ulisilimu walipokufuru, na ulirudi walipokimbia, na ulitimiza ahadi walipo saliti, na ulikubali ukweli walipoukataa. Adiyi akasema: Sitojali kama ndivyo.⁴⁵⁶

Na alikuwa mtu wa mwanzo kutanguliza sadaka yake kwa Abubakari Swiddiq katika mji wa Madina baada ya kifo cha Mtume -

si kwa ajili ya Allah Mtukufu, na Aliye kufa kwa kunyongeka koo, na Aliye kufa kwa kupigwa, na Aliye kufa kwa kuanguka, na Aliye kufa kwa kupigwa pembe, na Aliyeliwa na mnyama, ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama iliyo chinjiwa masanamu. Na ni haramu kupiga ramli. Hayo yote ni upotofu." [Al Maida: 3]

⁴⁵⁴ Bin Kathiri, tafsiri 1/582, katika kutafsiri suratul Maida, Na ametaja hadithi.

⁴⁵⁵ Chanzo kilichotangulia.

⁴⁵⁶ Sahihi Bukhari, kitabul Maghazi, 5/123.

Rehema na Amani ziwe juu yake- Na alikuwa na mchango mkubwa katika kuwakemea watu wake na kuwazuia kutokana na kuritadi.⁴⁵⁷

Kama alivyoshiriki -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Katika funguzi za miji katika zama za Abubakari Swiddiq na Omari bin Khattwab -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao-, Na alishuhudia ufunguzi wa miji ya Iraq na Farisi ikiwemo Madaini ambao ni mji mkuu wa Fursi, na akaona kwa macho yake hazina za kisra mikononi mwa waislamu, kama alivyoahidi hilo Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na alikaa Kufa na alikuwa pamoja na Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-.⁴⁵⁸.

Msafara wa Najran: [1076]

Najrani ni eneo pana kusini mwa kiwani cha kiarabu,⁴⁵⁹ yanaishi makabila mengi, na kuna tamaduni tofauti tofauti, na ulienea ukristo ndani yake na ukapata nguvu kabla ya uislamu.

Ulikuwa ni mji wenye mafungamano makubwa na wakristo wa kiarabu wa miji ya Sham, na kaskazini mwa kisiwa cha Kiarabu, na vile vile Habashi (Ethiopia),⁴⁶⁰ na kulikuwa na mabadilishano kati yao ya tamaduni za dini, Kiasi kwamba wanachuoni wa kiarabu walikuwa wakihama kutoka hapo na wengine wakiingia, ndiyo maana ilihesabika kuwa ni ngome kuu ya Ukristo katika zama za Mtume -

⁴⁵⁷ Bin Hajari, Fat-hul bari, 2/328.

⁴⁵⁸ Bin Hajari, Fat-hul bari, 2/329.

⁴⁵⁹ Al hamawiy, Mu'jamul Buldaan, 5/266.

⁴⁶⁰ Jawad Ally, Al-mufasssal katika Historia ya waarabu kabla ya uislamu 6/614

Rehema na Amani ziwe juu yake-.⁴⁶¹Na waliujua ujumbe wa Mtume - Rehema na Amani ziwe juu yake- kabla ya kuhama kwake kwenda Madina,⁴⁶²kama ilivyothibiti kwa njia nyingi kumsikia Mtume - Rehema na Amani ziwe juu yake- Askofu wa Najrani Kasi bin Saaida katika zama zake akitoa hotuba katika soko la Ukadhi.⁴⁶³.

Na ilihesabika Najrani kuwa ndio kituo kikuu cha Ukristo kusini mwa miji ya kiarabu, ikiwa na mfumo, pamoja na idara na vyeo kama (cheo cha Marejeo -paroko), nacho kama wanavyosema wana Historia nikuwa: Ni kiongozi wao na mshauri wao, ambaye hawatoirai isipokuwa kwanza mpaka wasikilize rai yake, na (Mtakatifu), Naye ni muhasibu wao na mtunza hazina wao "Msimamizi wa mali za umma" Na (Askofu), naye ni msomi wao na kiongozi wao wa ibada na muhusika wa shule zao yeye pamoja na Mtakatifu, hawa ndio wanaongoza jamii, na usimamizi wa mambo ya siasa na mali, na anasimamia mahitaji ya jamii yote, katika mambo yote yaliyobakia.⁴⁶⁴.

Na utawala wa Najrani haukuwa ni madaraka ya kikabila, bali walikuwa wakifuata marejeo ya dini yaliyoepukana na ubaguzi na

⁴⁶¹ Jawad Ally,Al-mufassswal katika Historia ya waarabu kabla ya uislamu 6/616

⁴⁶² Tazama: Muhamad Iwadh Al Utaibi, Najrani katika zama za utume na utawala mtukufu, Risala ya Majisteri, ikiwa ni utanguliza wa kitengo cha Tarekh wa hadhwara, Chuo kikuu cha Imam, uk19

⁴⁶³ Jawad Ally,Al-mufassswal katika Historia ya waarabu kabla ya uislamu 6/616

⁴⁶⁴ Yamenukuliwa kutoka kwa Jawwad Ally, Fasl, 6/617

ukabila, kiasi ambacho walishiriki katika uongozi watu wa makabila mbali mbali⁴⁶⁵

Aliwaandikia barua Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- wakrsito wa Najrani.

Ilipomfikia barua askofu, ikamchukiza sana, na ikamfadhisha sana, akamuita mtu mmoja katika watu wa Najrani akiitwa Shurahbili bin Wada'a na alikuwa anatoka katika kabila la Hamdani, na hapakuwa na yeyote anayeitwa kabla yake linapotokea jambo zito, si watawa, wala paroko, askofu akampa Shurahbil barua ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akaisoma, Askofu akasema: Ewe baba Mariam, Ni ipi rai yako? Akasema Shurahbil: Wewe unafahamu aliyomuahidi Mwenyezi Mungu Ibrahim katika kizazi cha Ismail katika Unabii, Haiaminiki huenda mtu huyu akawa ndiye yule aliyetabiriwa, binafsi sina rai yoyote katika unabii, laiti kama lingekuwa ni jambo katika maswala ya kidunia basi ningekushauri kwa mtazamo wangu, na ningejitahidi kwa ajili yako. Askofu akasema kumwambia: Hebu sokea pembeni na ukae. Shurahbil akasogea pembeni na akakaa. Askofu akaagiza mtu mwingine katika watu wa Najrani, akiitwa: Abdallah bin Shurahbil, huyu anatokana na kabila la As-bah kutoka Himyari, akamsomea barua, na akamuuliza kuhusu rai yake katika ujumbe huo. Naye akamwambia maneno mfano wa yale ya Shurahbili. Askofu akasema kumwambia: Hebu kaa. Akakaa, na akajitenga kando kidogo. Askofu akaagiza mtu mwingine katika watu wa Najrani, akiitwa Jabari bin Faidh, kutoka katika kabila la bani Harith bin Ka'bu, mmoja kati ya bani Hamasi, naye akamsomea ujumbe. Na akamuuliza kuhusu rai yake. Naye

⁴⁶⁵ Jawad Ally, Al-mufassswal katika Historia ya waarabu kabla ya Uislamu 6/618

akamjibu kama alivyojibiwa na Shurahbil na Abdallah. Askofu akamwamrisha akae kando.

Rai zilipokutana katika kauli hizo zote, Askofu akaamrisha kengele igongwe, Na mioto na mishumaa ikanyanyuliwa juu ya kanisa, hivi ndivyo walivyokuwa wakifanya wanapopatwa na jambo la mshituko au mfadhaiko wakati wa mchana, na unapokuwa mfadhaiko nyakati za usiku wanapiga kengele, na mioto inanyanyuliwa katika kanisa. Watu wakakusanyika ilipopigwa kengele na watu wa bondeni wakanyanyua mishumaa juu na chini, na kwa urefu, umbali wa mpanda farasi kutembea kwa kasi siku nzima, kukiwa na vijiji sabini na tatu, na kukiwa na wapiganaji laki moja. Askofu akawasomea ujumbe wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na akawauliza ni ipi rai yao katika hilo. Wazee wenye muono wakakubaliana wamtume Shurahbili bin Wada'a Al Hamdan.⁴⁶⁶

Na wakati wakilifanyia utafiti wasomi wao na wakibadilishana mawazo, walikuja watu sitini wenye vipando, wakiwemo ishirini na nne katika viongozi wao, na wale ishirini na nne katika wao kuna watu watatu ambao wanawategemea katika mambo yote (Paroko) kiongozi wao na mwenye maamuzi na ndio mshauri wao, na ambaye hawawezi kutoa maamuzi yoyote isipokuwa kwa rai yake na amri yake, na jina lake alikuwa akiitwa Abdul Masihi, na Muhazini wao, na muangalizi wa msafara wao na jamii yao nzima, na jina lake alikuwa akiitwa: Ayhum, na Abuu Haritha bin Alkama ni ndugu na banii Bakari bin Waili (Ambaye ndiye askofu wao) na msomi wao na kiongozi wao na msimamizi wa shule zao.

Na Abuu Haritha walikuwa wamempa cheo, na alisoma vitabu vyao, na wafalme wa Roma katika wakristo walimuheshimu sana na

⁴⁶⁶ Angalia Bin Kathiir Tafsiri yake juzuu ya 1/370,371.

wakamuweka karibu na wakawa wakimtumikia, na wakamjengea kanisa, na wakamkunjulia neema mbali mbali kwa sababu ya kuwawakilisha, na hii ni kwa sababu ya elimu yake na juhudi zake katika dini yao.

Wakavua nguo za safari na wakavaa nguo zao za mapambo wakiziburura, kwanzia majoho na pete za dhahabu, kisha wakaondoka mpaka wakaja kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- wakamsalimia, hakuwajibu salamu, wakang'ang'ana kuzungumza naye mchana kutwa lakini hakuwasemesha lolote wakiwa katika mapambo yale na zile pete za dhahabu, wakaondoka wakimfuata Othman bin Affan, na Abdurrahman bin Auf, hao ndio waliokuwa wakiwafahamu, kwa sababu walikuwa wakitoa misafara kwenda Najrani zama za ujinga kwa ajili ya biashara, wakinunua ngano, matunda, na mahindi, wakawakuta (Othman na Abdurrahman) wakiwa wamekaa pamoja na watu katika maanswari na Muhajirina katika kikao, wakasema: "Ewe Othmani na ewe Abdurrahman, hakika huyu nabii wenu alituandikia ujumbe, tukaja kuitika wito wake, tukamjia tukamsalimia hakutujibu salamu yetu, na tukamtaka tuzungumze naye mchana kutwa , lakini tukashindwa kuzungumza naye, mnatushauri nini nyinyi, je, turudi? Wakasema kumwambia Ally bin Abii Twalib naye akiwa amekaa pamoja nao: Unasemaje ewe Abuu Hasan kuhusu hawa watu? Ally akasema kumwambia Othman na Abdulrahman -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao-: "Ninachoshauri wavue hayo mapambo yao na pete zao kwanza na wavae nguo zao za safari kisha wamwendee, ule msafara ukalitekeleza hilo, wakavua mapambo yao na pete zao, kisha wakarudi kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, wakamsalimia akawajibu salamu yao.⁴⁶⁷

⁴⁶⁷ Bin Qayyim, Zadul Maad, 3/629-633.

Na walipokutana na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, akasema Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kumwambia askofu wa Najrani: "Ewe Abu Harithi silimu", Akasema: Mimi ni muislamu, akasema: "Ewe Abu Harithi silimu", Akasema: Mimi ni muislamu kabla yako. Akasema Nabii wa Mwenyezi Mungu: "wewe ni muongo" Yanayokuzuia kuwa muislamu ni mambo matatu: Kudai kwako kuwa Mungu ana mtoto, na kula kwako nyama ya nguruwe, na kunywa kwako pombe¹⁴⁶⁸

Na yalijiri kati yao na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- majadiliano marefu, kiasi ambacho alisema kiongozi wao kumwambia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Unamtukana mtu wetu na unasema kuwa yeye ni mja wa Mwenyezi Mungu?, Kisha akasema mmoja wao: Ni nani baba yake na Yesu? Akarudia tena, "Ni nani baba yake na Yesu? Akanyamaza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na alikuwa hafanyi haraka kujibu mpaka Mola wake amuamrishe. Hapo akateremsha Mwenyezi Mungu Mtukufu kauli yake:

﴿إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ﴾ الْحَقُّ
 مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُن مِّنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٦١﴾ فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِن بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا
 نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ
 عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦٢﴾ [آل عمران: 61-59]

"Hakika mfano wa Mwenyezi Mungu kumuumba Isa, bila ya baba, ni kama mfano wa Mwenyezi Mungu kumuumba Adam, bila ya baba wala mama. Mwenyezi Mungu Alimuumba kutokana na

⁴⁶⁸ Bin Abii Shaiba, Al Maghazi, uk. 409, na tazama: bin Hajari, fat-hul bari, 16/259, na Omari bin Shiu'ba Taarikhul Madina, 1/583.

mchanga wa ardhi kisha Akamwabia, «kuwa kiumbe», akawa. Basi madai ya uungu wa 'Īsā kwa kuwa aliumbwa bila ya baba, ni madai ya uongo. Ādam, amani imshukie, aliumbwa bila ya baba wala mama, na wote wamekubaliana kwamba yeye ni mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu.* Haki isiyo na shaka kuhusu mambo ya 'Īsā ni ile iliyokujia, ewe Mtume, kutoka kwa Mola wako. Endelea kwenye yakini yako na juu ya msimamo ulionao wa kuacha uzushi. Na usiwe ni miongoni mwa wenye shaka. Katika haya pana kumtia moyo Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na kumtuliza. Watakao kuhoji katika haya baada ya kufikiwa na elimu hii waambie:Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu,na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya ALLAH iwashukie waongo. [Al Imran: 59-61].

Na zilipotaremka aya za kulaaniana kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- aliwaita ili walaaniane, na akawaahidi wakutane kesho yake, wakakaa kushauriana kati yao na walikuwa ni katika wasomi wa kikristo. Wakasema baadhi yao: :wallahi huyu mtu kama atakuwa nabii na tukamlaani basi hatutofaulu sisi wa la vizazi vyetu baada yetu,⁴⁶⁹Na akaasema mwingine: "Ikiwa huyu mtu atakuwa ni nabii na tukamlaani basi hata nywele haitobakia katika Ardhi hii wala kucha isipokuwa itaangamia"⁴⁷⁰

Kisha baadhi yao baada yakuwa wameona uadilifu wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na uzuri wa mazungumzo yake na ukweli wake, wakakubaliana kuwa chini ya hukumu yake na yale anayoyaamrisha na wala wasimlaani, kiasi kwamba alisema kiongozi

⁴⁶⁹ Omari bin Shu'ba, Tarukhul Madina, 2/584.

⁴⁷⁰ Tafsiir Ibnu Kathiir juzuu 1/371

wao Shurahbili: "Hakika mimi ninaona huyu mtu haku hukumu kwa dhulma kamwe"⁴⁷¹

Alikuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- siku ya kesho yake akiwa pamoja na Fatma na Hassan na Hussein na Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote-. Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akawaita, wakaogopa na wakajificha baadhi yao katika kona za msikiti kwakuwa wanajua dua zake zinapokelewa, wakahofu asije kuwaomba mabaya, kisha akaenda kiongozi wao Shurahbili kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Akasema: "Hakika mimi nimepata wazo zuri kuliko kukulaani. Akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Ni lipi hilo?" Akasema: "Hukumu yako mpaka usiku na kuanzia usiku mpaka asubuhi lolote utakalohukumu juu yetu sisi tuko tayari kulikubali. Akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Hue nda nyuma yako kuna mtu anakutupia lawama?" Akasema: Muulize mwenzangu, akamuuliza maswali ya kutosha, naye alikuwa hawezi kutoa rai isipokuwa rai ya Shuhbili, Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akarudi na wala hakuwalaani. Wakarudi kesho yake akaingia nao makubaliano, na akawaandikia ujumbe ambao ulikuwa na maudhui zifuatazo: "Haya ndiyo aliyoyaandika Muhammadi Nabii na Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa watu wa Najrani, kuwa hukumu yake itakuwa juu yao, na itakuwa katika kila cheupe na cheusi na njano na tende na mtumwa, na vilivyo bora kwao akawaachia, kuwa kwa kila mapambo elfu mbili katika kila mwezi wa swafari watatoa mapambo elfu moja, na katika kila mwezi wa Rajabu mapambo elfu moja katika kila pambo uqiya moja (sawa na Gramu 200), kitakachozidi katika kodi au kupungua chini ya uqiya moja basi hicho kitakuwa chini ya miliki ya muhusika, na vile wakatavyovipata katika ngao za

⁴⁷¹ Kitabu Zaadul Maad cha Bin Qayyim, juzuu ya 3/643.

vita, au Farasi, au Mizigo, au thamani yoyote basi vitachukuliwa kulingana na hesabu, na kwa Maeneo yote ya Najrani kutakuwa na wajumbe wangu, na watachukua mifugo ishirini, na asiache kuchukua mjumbe yeyote zaidi ya mwezi, na watakuwa na vifaa vya vita vya kuazima, ngao thelathini, na Farasi thelathini, na Ngamia thelathini, hivi ni kwa sababu ya kujihami ikiwa kutatokea uvamizi kutoka Yemen au dharura yoyote, na kitakachoharibika katika vile walivyomuazima mjumbe wangu katika Ngao au Farasi au mizigo basi dhamana yake itakuwa juu ya mjumbe wangu mpaka awalipe, na katika haki za Najrani inatosha kwao kuwa jirani na Mwenyezi Mungu na kupata dhima ya Nabii Muhammadi juu ya nafsi zao, na mila zao na ardhi yao, na aliyesafarini na aliyepo na familia zao, na wala wasibadilishe yale waliyokuwa nayo katika haki zao, na mila zao, na wala wasibadilishe askofu yeyote katika maaskofu wao, wala padri katika mapadri wao, wala utiifu kwa yeyote wanayemtiii,⁴⁷² na kila wanachokimiliki kiwe kidogo au kikubwa na wasiwe na shaka yoyote kwacho kama umwagaji damu enzi za ujinga na wala si kwa kupokonya wala kudhulumu, na wala ardhi yao lisikanyage jeshi lolote, na atakayewaomba haki yake basi watende uadilifu wasidhulumu wala kudhulumiwa, na atakayekula mali ya riba huyo ajue dhima yangu kwake iko mbali (simtambui), na wala asiadhibiwe mtu kwa dhulma ya mtu mwingine, na yote yaliyoko katika waraka huu yako chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu na dhima ya Muhammadi Nabii na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, waendeleo

⁴⁷² Neno Al-wafhiya: Ni kuchukua ahadi ya utiifu (Baiya), Al wafih: Ni mtu aliyeko katika ahadi ya utiifu, Tazama: Hamishi (2) kwa Omari bin Shu'ba katika kitabu cha Tarikhul Madina. 2/585

kuyatekeleza mpaka Allah alete amri nyingine, na wasirudi katika dhulma"⁴⁷³

Na katika tukio hili ziliteremka aya katika suratu Al Imran.

﴿إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُن فَيَكُونُ﴾ الْحَقُّ
مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُن مِّنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٥٩﴾ فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِن بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا
نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ
عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٦٠﴾ إِنَّ هَذَا لَهَوٌ الْقَصَصُ الْحَقُّ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦١﴾
فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٦٢﴾ قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ
أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا
فَقُولُوا أَشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٣﴾ [آل عمران: 59-64]

Hakika mfano wa Issa mbele ya ALLAH ni kama mfano wa Adam, Alimuumba kwa udongo kisha-ALLAH-akasema kuwa akawa. Haki isiyo na shaka kuhusu mambo ya 'Īsā ni ile iliyokujia, ewe Mtume, kutoka kwa Mola wako. Endelea kwenye yakini yako na juu ya msimamo ulionao wa kuacha uzushi. Na usiwe ni miongoni mwa wenye shaka. Katika haya pana kumtia moyo Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na kumtuliza. Basi atakaye kuhoji baada ya kufikiwa na elimu basi sema njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu na wanawake wetu na wanawake wenu na sisi wenyewe kisha tuombe kwa unyenyekevu tuombe laana ALLAH iwashukie waongo. Hakika haya ndiyo maelezo ya kweli, Na hakuna mungu isipokuwa ALLAH, Na hakika ALLAH ndiye mwenye nguvu mwenye hekima. Na wakikataa

⁴⁷³ Omari bin Shu'ba, Tarikhul Madina, 2/586, Tazama: Abuu Yusuf, kitabu Al kharaji, uk, 73, Na bin Asa'd Attwabaqat, 1/358

kukuamini na kukufuata, basi wao ndio waharibifu. Na Mwenyezi Mungu Anawajua na Atawalipa kwa hilo. Sema enyi mayahudi na wakristo njooni kwenye neno la sawa baina yetu na nyiye tusimuabudu isipokuwa ALLAH na wala tusimshirikishe na chochote na wala tusiwafanye baadhi yetu kuwa ni miungu kinyume na ALLAH na kama watakengeuka basi semeni shuhudieni kuwa sisi ni waislamu. [Al Imran: 59-64]. Na katika mwanzo wa aya na mwisho wake kuna majadiliano ya pamoja kwa wakristo wa zama zote na mahali popote. **Ukweli unatoka kwa mola wako basi usiwe miongoni mwa wenye mashaka.** [Al-Imran: 60]. Na Wakristo wengi katika zama hizi wanajua ukweli wa ujumbe wa Muhammadi na Utume wake kama walivyoyujua Wakristo wa Najrani katika zama zao, lakini ni kwa sabababu tu ya uwasi kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Na alipokubaliana Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** na Wakristo wa Najrani walimtaka yakuwa: Tutumie mtu muaminifu aondoke nasi. Akasema Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake: "Hakika nitakutumieni mtu mwaminifu, tena muaminifu kweli, wakapata shauku ya hilo wanafunzi wa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, akasema: Simama ewe Abuu Ubaida bin Jarahi" Akamuagiza aondoke nao.⁴⁷⁴

Na uliporejea Najrani msafara, wakajitetea mbele ya watu wao, nakwamba wao wameandika mkataba na wakalipa kodi kwa kuogopea dua mbaya, na wakaonyesha kujua kwao unabii wake. Lakini pamoja na hivyo hawakusilimu, wawili miongoni mwao wakaenda mbio Madina kwenda kukutana na Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na mmoja wao alisilimu na anaitwa Bishiri, na

⁴⁷⁴ Bin Abii Shaiba, Al Maghazi, uk. 408, Tazama Sahihi Bukhari, Mlango wa kisa cha watu wa Najrani, 5/121.

akaungana na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- mpaka akafa shahidi akiwa muislamu.⁴⁷⁵

Na alimtuma Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- Abuu Ubaida kwenda Najrani, akawa kiigizo chema na mwalimu mwenye baraka, na akawa mfanya kazi katika idara ya fedha, akasimamia majukumu yake ipasavyo.⁴⁷⁶Na kulikuwa kukiendelea kati yake na Wakristo wa Najrani midahalo ya kielimu kuhusu yale yaliyoteremka ndani ya Qur'ani, na vile vile kati yao na masahaba aliyekuwa akiwatuma Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwenda Najrani. Na miongoni mwake ni yale aliyoyapokea Mughira bin Shu'ba -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Amesema: Alinituma mimi Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwenda Najrani wakasema kuniambia: Hakika nyinyi mnasoma ndani ya kitabu chenu:

﴿يَأْخُذْتَهُرُونَ مَا كَانَ أَبُوكَ أَمْرًا سَوِيًّا وَمَا كَانَتْ أُمُّكَ بَغِيًّا﴾ [مریم: 28]

"Ewe dada yake Harun hakuwa baba yako ni mtu muovu, na wala mama yako hakuwa malaya" (Suratu Mariam: 28). Na hali yakuwa kati ya Mussa na Yesu kuna tofauti ya miaka mingi. Nikakosa la kuwajibu, mpaka nikarudi kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- nikamuuliza akasema: "Si ungewaambia kuwa kwani nyinyi si mlikuwa mkiwaita majina hayo ya manabii wenyewe na watu wema kabla yenu?"⁴⁷⁷.

⁴⁷⁵ Bin Qayyim, Zadul Ma'ad, 3/637, bin Kathiri, Al Bidaaya wan nihaaya, 5/55

⁴⁷⁶ Kwa Bin Abii Shaibah katika Maghaazi, ukurasa wa 409.

⁴⁷⁷ Bin Abii Shaiba, Al Maghazi uk409, na hadithi kaitoa Muslim kutia njia ya bin Abii Shaiba, Tazama: Bin Kathiri, Tafsiri yake, 2/1185

Na alimtuma Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Ally bin Abii Twalib kwao katika mwaka wa kumi wa Hijiria kwa ajili ya kukusanya kodi zao na sadaka za Waislamu wa Najrani, akaenda kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika Hija ya kuaga.⁴⁷⁸

Na yalipita maisha ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- yaliyobakia na Wakristo wa Najrani kwa salama, na mkataba uliendelea kubakia kati yao na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-.

Na baada ya kufa kwake Rehema na Amani ziwe juu yake, kulidhihiri kuritadi sehemu nyingi, ikiwemo maeneo ya Najrani kwa baadhi ya waliosilimu miongoni mwao, si mbali hilo wako pia walioshiriki harakati za walioritadi katika uasi wa jeshi kutoka kwa wasiokuwa waislamu katika watu miji hiyo, sawa sawa ni katika wakristo au wengineo kwa njia ya wazi au isiyokuwa ya wazi.

Lakini utawala wa Abuu bakari swiddiq ulipita salama na wala hakujataokea kati ya Wakristo wa Najrani na Waislamu tofauti yoyote.

Na zilipofika zama za Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- na miji ikafunguliwa makabila mengi ya warabu yaliamia miji iliyofunguliwa, na hasa hasa yale yaliyoshiriki katika ufunguzi. Na Wakristo wa Najrani walikuwa wamejitegemea wako nje ya dola ya Kiislamu, hawakushiriki katika funguzi kwa hukumu iliyotolewa ya kubakia katika dini yao, basi nafsi zao zikapenda kuchukua ardhi mpya, na hawakuwa na haki ya kufanya hivyo kwakutokuwa kwao Waislamu na kushiriki kwao. Na muda huo huo idadi ya Wakristo wa

⁴⁷⁸ Bin Qayyim, Zadul Maad, 3/637, na tazama: Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/60, Na tazama Hijjatul Wadaa, ndani ya kitabu hiki.

Najrani ikawa inaongezeka na hata rai yao kwa Waislamu ikaanza kutazamiwa.

Na ameandika bin Abii Shaiba kwa isinadi yake amesema: Watu wa Najrani walikuwa wamefikia elfu arobaini (40,000), Akasema: Na alikuwa Omari akiwaogopea wasije kuwazidia waislamu wakachukiana wao kwa wao. Akasema: Wakamjia Omari wakasema: Hakika sisi tumechukiana sisi kwa sisi tuhamishe. Anasema: Na alikuwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kaandika ujumbe kuwa wasitolewe, Anasema: Akatumia fursa hiyo Omari akawahamisha, baadae wakajuta, wakamfuata wakasema: Turudishe, akakataa kuwarudisha, alipokuja Ally wakamwambia: Hakika sisi tunakuomba kwa mwandiko wa mkono wako na kwa utetezi wako kwa nabii wako usituache hapa, akakataa na akasema: Ole wenu, Hakika Omari alikuwa na mtazamo zaidi katika jambo hili, Akasema Salim: Wakawa wanaona kuwa laiti kama Ally angelikuwa ni mwenye kumlaumu Omari katika mambo aliyoyafanya bas angelimlaumu katika swala la watu wa Najrani",⁴⁷⁹. Kama inavyoonekana wazi katika ushahidi huu kuwa Omari alinunua sehemu ya ardhi yao na maeneo yao nyeti.⁴⁸⁰

Na inasemekana kuwa sababu ya kuja kwao kwa Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Nikuwa wao walikula riba, haliyakuwa waliwekewa sharti la kutokula riba katika makubaliano yao na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- wakahofia kuadhibiwa na Omari hivyo wakafanya haraka kuhamia Iraqi na Sham. Na kilicho wazi zaidi kutoka katika riwaya mbali mbali nikuwa wao walikwenda kinyume na makubaliano yao na Mtume -**Rehema**

⁴⁷⁹ Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 408.

⁴⁸⁰ Al-maghaaz cha Bin Hishaam ukurasa 407.

na Amani ziwe juu yake- huko Najrani katika miji mipya iliyopatikana kwa ufunguzi ambayo waliongeza ukubwa wa eneo lao kulingana na ombi lao, kama ambavyo walilipwa fedha kwa ajili ya kuachia maeneo yao, aseti zao, lakini walijuta baadae wakajaribu kurejeshewa maeneo yao, Omari -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- akakataa, baada yakuwa wamekamilisha makubaliano nao ya kibiashara. Kilichofuata walihamia Iraq wakiwa pamoja na barua ya Omari kwenda kwa viongozi wa maeneo hayo, ili wasipate tabu na iwe rahisi kupata ardhi ya kushi. katika yaliyokuwa ndani ya barua: "Huu ni ujumbe wa Omari kiongozi wa Waislamu kwenda Najrani, atakaye safiri miongoni mwao basi huyo yuko katika Amani ya Mwenyezi Mungu hivyo asiwadhuru yeyote katika Waislamu, hii ni kuwatimizia yale aliyowaandikia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na Abuubakari, Ama baada ya hayo; Na watakaofika kwa viongozi wa Sham na viongozi wa Iraq basi wawape nafasi katika ardhi, watakayoindeleza basi hiyo kwao itakuwa ni sadaka, na hatima ya ardhi hiyo itakuwa miliki yao na wala hana haki yeyote ya kuwatoa au kuwadai fedha, ama baada hayo; Muislamu yeyote atakayekuta wakidhulumiwa basi na awasidie kutetea haki yao kwani wao wako chini ya dhima, na wasidaiwe kodi (Jiziya) baada ya kufika kwao kwa muda wa miezi ishirini na nne, na wala wasilazimishwe isipokuwa kuiendeleza ardhi waliyoichukua bila kudhulumiwa, na wala wasifanyiwe ukatili wowote". Alishuhudia ujumbe huu Othman bin Affan na Muaikib bin Abii Fatma, wakafika baadhi yao Iraq na wakaishi mahala walipopaita Najrania maeneo ya Kufa (Iraq).

Kubomowa Masanamu:

Masanamu yalikuwa yameenea kila mahali katika miji ya warabu, na Makka yaliwekwa ndani ya msikiti karibu na Al-Ka'aba, Na

imekuja katika Qur'ani kutajwa kwa majina ya baadhi yake, kama Lata na Uzza na Manata. Na makabila ya waarabu walikuwa wakijifaharisha kwa masanamu hayo na wakiyaabudu kinyume na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na zimekuja aya nyingi katika aya za Qur'ani zikitahadharisha kuhusu masanamu, na vita vya manabii dhidi yake kwa kila zama.

﴿رَبِّ إِتَّهَنُ أَضَلَّنْ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ ط فَمَن تَبِعَنِ فَإِنَّهُ مِثِّي ط وَمَن عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾ [إبراهيم: 36]

Mola wangu hakika hayo masanamu yamepoteza wengi miongoni mwa watu, basi atakaye nifuata atakuwa pamoja na mimi, na atakaye kwenda kinyume basi hakika wew -ALLAH-ni msamehevu mpole. [Ibrahim: 36]. Na ilikuwa hamu kubwa ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ni kuyang'oa yale yaliyokuwa ndani ya nyoyo za watu katika itikadi na ushirikina, na kuyavunja masanamu na kuyabomoa kabisa na kuyafuta moja kwa moja yasiwepo tena, na ndiyo maana alifanya haraka Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kuyavunja masanamu yaliyokuwa yameizingira Al-ka'aba na katika msikiti mtukufu tena mbele za watu na watu pia wakisikia wakati ulipofika wakuufungua mji wa Makka, na alikuwa akikariri kauli yake Mtukufu:

﴿وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَرَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا﴾ [الإسراء: 81]

Sema-ewe MUHAMMAD-ukweli umekuwa na uwongo umeondoka hakika uwongo umekuwa ni wenye kuondoka. [Al Israa: 81]⁴⁸¹Na alilenga Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kuyabomoa masanamu mahala popote ambapo nguvu yake inafika,

⁴⁸¹ Angalia ufunguzi wa Khaibar kutoka katika kitabu hiki.

akatuma vikosi kutoka kwake katika kila upande kwa ajili ya kusimamia zoezi hili tangu ulipofunguliwa mji wa Makka, na warabu wakamuogopa na akaitawala miji yao, kaisi ambacho alipupia kuyaondoa masanamu na kuyavunja katika maeneo na katika nafsi za wenye nayo, yaani waabudu masanamu, na miongoni mwa vikosi hivyo vilivyoandaliwa kwa ajili ya kuvunja masanamu.

Kikosi Cha Khalid bin Al'walid kwenda kuvunja Sanamu la Uzaa: [1101]

Uzza lilikuwa ni sanamu lililoko katika mtende mashariki mwa Mji wa Makka kati yake na mji wa Twaifu katika mji wa Hudhaili.⁴⁸² Na lilikuwa likiabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu, na ndilo ambalo iliteremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kulizungumzia:

﴿أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٩﴾ وَمَنْوَةَ الْغَالِيَةَ الْأُخْرَىٰ ﴿٢٠﴾﴾ [النجم: 19-20]

"Mnawaonaje, enyi washirikina, waungu hawa mnaowaabudu: Lāta, 'Uzzā" "na mwingine wa tatu ni Manātu. [An najmu: 19-20] Na warabu walikuwa wakiliomba na kulitukuza kinyume na Mwenyezi Mungu,⁴⁸³ Na ndio maana tunaona kuwa Abuu Sufian alilitukuza katika vita vya Uhudi, Akasema: "Sisi tuna Uzza na wala nyinyi hamna Uzza", Akaamrisha Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** ajibiwe: "Mwenyezi Mungu ndiye Mlezi wetu na wala hamna mlezi nyinyi"⁴⁸⁴ Na alimtuma Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu**

⁴⁸² Tazama: Bin Kalbi, Al Snamu, uk, 16, Na Jawad Ally, Al Mfswal 77/235.

⁴⁸³ Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabu tafsiri, Suratun najmi, Mlango wa "Afara aitumullata wal Uzza, 6/51, bin Kathiri, Tafdiri yake, 2/1780.

⁴⁸⁴ Tazama: BIn Abii Shaiba, Al Maghazi, uk 238, Tazama: Vita vya Uhudi, ndani ya kitabu hiki.

yake- Khalidi bin Walid katika kikosi chake kwa ajili kulibomoa sanamu la Uzza baada ya kufunguliwa mji wa Makka, akaenda na akalibomoa, katika kisa kirefu.⁴⁸⁵

Kikosi cha Amr bin Al'aswi kubomowa Sanamu la Suwaa [1106]

Suwa'a ni sanamu la kabila la Hudahili mashariki mwa Makka, na limetajwa ndani ya Qur'ani, katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَقَالُوا لَا تَدْرُنَّ ءَالِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَلَا سُوَاعًا وَلَا يَغُوثَ وَيَعُوقَ وَنَسْرًا﴾ [توح:

[23

Na wakasema msiiyache miungu yenu na wala msimuache-mungu-Wadda wala Suwaa wala Yaghutha na Yauqa na Nasra. [Nuhu: 23] Na alilitumia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Amru bin Aswi baada ufunguzi wa Makka katika kikosi kwa ajili ya kulibomoa, na walidai wahudumu wake kuwa litajitetea lenyewe, na kwamba Amru hatoweza kuliboa, lakini baada ya wahudumu kumuona Amru akibomoa jiwe moja moja na wala halijinufaishi lenyewe wala kumdhuru yeyote, walisilimu baada ya hapo na likabomolewa sanamu hilo milele mpaka leo.⁴⁸⁶

Kikosi cha Sa'ad bin Al'ashihaly kwenda kubomowa Sanamu la Manata:

Lilikuwa sanamu la manata⁴⁸⁷ sehemu za mish-lal katika eneo la kadidi⁴⁸⁸ kati ya Makka na Madina, Walikuwa wakiliabudu warabu

⁴⁸⁵ Vyanzo vilivyotangulia, Bin Saad, Al-Twabaqqat Al-kubraa, juzuu ya 2/145.

⁴⁸⁶ Tazama: bin kathiri, tafsiri yake, 1/1923.

⁴⁸⁷ Tazama: bin kathiri, tafsiri yake, 2/1781.

wote, na hasa hasa washirikina wa kabila la Ausi na Khazraji, na walikuwa wakilitolea kafara (Vikurubisho) Na ndilo lilitajwa katika kauli yake Mtukufu:

﴿أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٩﴾ وَمَنْوَةَ الْعَالِيَةَ الْأُخْرَىٰ ﴿٢٠﴾﴾ [النجم: 19-20]

"Mnawaonaje, enyi washirikina, waungu hawa mnaowaabudu: Lāta, 'Uzzā" "na mwingine wa tatu ni Manātu. [An najmu: 19-20]

Na akamtuma Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- Sa'di bin Yazidi Al Answari akiwa na jeshi la Waislamu kwa ajili ya kulibomoa baada ya ufunguzi wa Makka, akafanikiwa kulibomoa sanamu na kulimaliza kabisa, bila kupambana na wahudumu wake ambao wanadai kuwa linaweza kujitetea lenyewe. Hivi ndivyo lilivyobomolewa sanamu katika mazingira na katika nafsi za wenye nalo.⁴⁸⁹

Kikosi Cha Ally bin Abi Twalib kwenda kubomowa Sanamu la Twaii[1111]:

Na kilikuwa kikosi cha Ally bin Abii Twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- mwaka wa tisa wa Hijiria, Rabiul Akhir, Akavamia Twayi na akalibomoa sanamu lao na akachukua ngawira ya hazina ya sanamu hilo, na akakamata mateka baadhi ya watu, na alikuwa miongoni mwa mateka ni Safana bint Hatim Attwayi, na

⁴⁸⁸ Jawad Ally, A Mufaswal, 6/246, Tazama: Hali ya dini kwa warabu kabla ya Uislamu ndani ya kitabu hiki.

⁴⁸⁹ Tazama: Bin Sa'di Attwabaqatul Kub-raa 2/146, Na Haithami, Sharhul mawahibu diniya, 2/348.

ndiye aliyekuwa sababu ya kaka yake Adiyi kuja na kusilimu.⁴⁹⁰ Kama ilivyotangulia kuelezwa na kufafanuliwa.⁴⁹¹

Kikosi cha Tufeil bin Amr kwenda kubomowa Sanamu la (Thul-Kafain) kwa Daus:

Baada tu ya vita vya Hunaini, alimuelekeza Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** Tufaili bin Amri Addausi kwenda kulibomoa sanamu la Dhul-kafaini katika makabila ya Amri bin Hamhama, akaliendea na akalibomoa na akalichoma moto, kisha akarudi na akakutana na Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** akiwa bado kaizingira Twaif.⁴⁹²

Kikosi cha Jarir bin Abdillah Albajaly kwenda dhil Khulswat: [1115]

Hili lilikuwa sehemu za Bijila huko Yemen katika kabila Khadh'am likiitwa sanamu hilo kwa jina la Dhul-Khisla,⁴⁹³ Na lilikuwa ndio tegemeo kubwa la makabila ya ukanda huo mpaka baadhi yao wakiita nguzo za Al-kaaba kwa jila hilo.

Akasema Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** Kumwambia Jariri bin Abdallah: "Hivi haunipumzishi na hili Dhul-Khisla" (Yaani: Haulivunji nikapumzika), Jariri akasema: Nitafanya hivyo ewe

⁴⁹⁰ Attwabari, tarikh yake, 3/148, AL Bukhari Sahihi yake, Kitabul Maghazi, Hadithi namba: 4340, bin Sa'd Assiratu nabawiyya kutoka katika kitabu cha Attwabaqat 2/164

⁴⁹¹ Tazama: Misafara ya wakristo wa kiarabu ndani kitabu hiki (Na kuja kwa Adiyi ni Hatim)

⁴⁹² Tazama: Bin Sa'd: Attwabaqat 2/157, Na Waqidi, Al Maghazi, 3/922, Muhammad Asswalabi, Assiratun nabawiyya: 2/666

⁴⁹³ Bin Hajari, Fat-hul bari, 16/190.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na alikuwa -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- hawezi kukaa vizuri katika Farasi, Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akamuomba dua na akampiga kifua huku akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu mpe uimara na umfanye kuwa muongofu mwenye kuongoka" Basi hakuwahi kudondoka tena kutoka juu ya Farasi baada ya hapo. Na alikwenda Jariri akiwa pamoja na wapanda Farasi Hamsini (50) mpaka katika sanamu la Dhul Khisla akalibomoa, na akatuma habari njema hiyo kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-. Na amepokea Bukhari katika sahihi yake kutoka kwa Jariri bin Abdallah Amesema: "Alisema kuniambia mimi Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**:- Hivi haunipumzishi na hili Dhul Khisla. Nikasema: Nitafanya hivyo, nikaondoka nikiwa na watu mia moja na hamsini (150) waliopanda farasi kutoka Ahmasi, na walikuwa wataalamu wa kupanda Farasi, na mimi nilikuwa siwezi kutulizana juu ya farasi, nikamueleza hilo Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, akanipiga kwa mkono wake juu ya kifua changu, na akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu mpe uimara na umfanye kuwa muongofu mwenye kuongoka". Anasema: Sikuwahi tena kuanguka kutoka juu ya farasi baada ya hapo. Anasema: Na Dhul-Khisla ilikuwa ni nyumba iliyoko Yemen ya kabila la Khath'am na Bujaila, ndani yake kulikuwa na sanamu likiabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu likiitwa Al-kaaba" Anasema: Akalifuata na akalichoma moto na akalivunja, Anasema: Na alipofika Jariri Yemen kulikuwa namtu aliyekuwa akipiga ramli, akaambiwa hakika mjumbe wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- amekwisha fika hapa, ikiwa atakupata atakuua. Anasema: Akiwa bado anaendelea kupiga ramli mara ghafla Jariri akasimama mbele yake, akasema: Chagua, ima ulivunje sanamu mwenyewe au ushuhudie kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, au nikuuwe, akasema: Akalivunja sanamu mwenyewe, na akasilimu, kisha akamtuma Jariri mtu mmoja kutoka Ahmasi akiitwa kwa jina la utani Abu Artwa kwenda kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akampe habari njema

ya hilo, alipofika kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**:- Akasema: Ewe mujmbe wa Mwenyezi Mungu, namuapa yule aliyekutuma kwa haki, sijaja hapa isipokuwa nimehakikisha nimeliacha (Sanamu) kama ngamia aliyebabuka kwa moto au ugonjwa, akasema: akawaombea baraka Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ngamia wa Ahmasi na watu wake mara tano".⁴⁹⁴

Hija ya kuaga [1118]

Hija ni nguzo ya tano katika nguzo za Uislamu. Na imeitwa kwa jina lake sura katika sura za Qur'ani Tukufu, na ikaizungumzia pamoja na maeneo yake mengi matukufu katika aya za Qur'ani ambazo idadi yake inafikia aya kumi na mbili.

Na ni jambo la uhakika kuwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- alikuwa akihiji kabla ya kuhama kwake, kwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu kupitia ibada ya Ibrahim -Amani iwe juu yake-, nakuwa yeye alikuwa akishuka kwa kutofautiana na Makuraishi katika maeneo kwa kufuata suna ya Nabii Ibrahim, pamoja nakuwa Hija haikufaradhiswa isipokuwa baada ya kuteremka kauli yake Mtukufu:

﴿ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا يُبْرَاهِيمَ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مِنَ اسْتِطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴾ [آل عمران: 97]

{Na Mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye Hija katika nyumba hiyo, yule awezaye kufunga safari kwenda huko, na atakayekanusha (Na asiende na haliyakuwa anauwezo) Basi

⁴⁹⁴ Bukhari katika sahihi yake, Hadithi namba: 4357.

Mwenyezi Mungu si muhitaji wa kuwahitajia walimwengu}. [Al Imran: 97]⁴⁹⁵.

Na baada ya kuhama kwake Rehema na Amani ziwe juu yake kwenda Madina, haijathibiti habari yoyote kuwa aliwahi kuhiji zaidi ya Hija ya kuaga ambayo ilikuwa katika mwaka wa kumi wa Hijiria,⁴⁹⁶ pamoja nakuwa Swiddiq aliwaongoza watu katika Hija mwaka wa tisa wa Hijiria.⁴⁹⁷

Na alikuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ana pupa kubwa ya kutaka kutoona mazingira yoyote ya ushirikina katika mji wa Makka, na hii ndio sababu iliyopelekea kuchelewesha Hija mpaka mwaka wa kumi, na kuwafikishia watu kuwa hawana haki washirikina ya kuukaribia Msikiti Mtukufu:

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَذَا وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ إِن شَاءَ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾ [التوبة: 28]

"Enyi mkusanyiko wa Waumini, hakika washirikina ni najisi na ni wachafu, hivyo basi msiwape nafasi kusongea kwenye eneo la Ḥarām baada ya mwaka huu wa tisa wa hijria (kalenda ya Kiislamu). Na iwapo mtachelea umasikini, kwa kukatikiwa na

⁴⁹⁵ Tazama: Bin Qayyim, Zadul Maad, 3/595, na tazama: Riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, kitabul Maghazi, Mlango wa Hija ya kuaga, 5/26, bin kathiri, Assiratun nabawiyya, 4/263.

⁴⁹⁶ kama zilivyowekwa sehemu maalumu na baadhi ya wanachuoni wa hadithi, kwa bin Hajari, Kitabu Fat-hul Bari, 16/299, katika riwaya za Bukhari 5/123.

⁴⁹⁷ Tazama: Hija ya Abuubakari kuwaongoza watu, katika kitabu hiki.

biashara zao, Mwenyezi Mungu Atawapa badala yake na Atawatosheleza kwa fadhila Zake Atakapo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi mno wa hali zenu, ni Mwingi wa hekima katika kuyapeleka mambo yenu. [Attauba: 28]

Na Hija ya kuaga ndio mafundisho ya kivitendo ya ibada za Hija kutoka kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** na kwa amri yake, kiasi kwamba alisema: (Huku akisema:) "Hakikisheni mnachukua kutoka kwangu ibada zenu, kwani sijui huenda nisihiji tena baada ya Hija yangu hii"⁴⁹⁸

Na kutokana na umuhimu wa swala hili ameweka Bukhari katika sahihi yake mlango akauita (Mlango wa Hija ya kuaga)⁴⁹⁹

Kabla ya mwezi wa Dhul Hija mwaka wa kumi wa Hijiria Alitangaza Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**kuwa atahiji, (Wakaenda Madina watu wengi kila mtu miongoni mwao anataka kujifunza kutoka kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**)⁵⁰⁰

Kulikuwa kutoka kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** katika mji wa Madinatul Munawwara ni tarehe ishirini na tano katika mwezi wa Dhil Ka'da, na alikaa njiani siku nane, watu ndani ya

⁴⁹⁸ Kaipokea Muslim katika sahihi yake, mlango wa sunna ya kutupa mawe ya mlima Akaba, siku ya kuchinja akiwa juu ya kipando. Na kubainisha kauli yake **-Rehema na Amani ziwe juu yake** "Hakikisheni mnachukua kutoka kwangu ibada zenu, 4/79

⁴⁹⁹ Tazama Sahihi Bukhari Kitabu Maghazi, Mlango wa Hija ya kuaga, 5/123, Bin Hisham, Assiratun nabawiyya Anwani: (Hija ya kuaga) 4/601

⁵⁰⁰ Bin Hajari, Fat-hul bari, 16/229.

muda huo walikuwa wakijifunza kutoka kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** idadi yao ikawa inaongezeka kidogo kidogo, kiasi kwamba waliambatana naye watu wengi na makabila mbali mbali kutoka pande mbali mbali za miji ya warabu,⁵⁰¹ pamoja na wale waliokuwa pamoja naye katika familia yake na wake zake na katika watu wa Madina.⁵⁰²

Alikuwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** akileta Talbiya (Akisema: "Labbaika Ilaahumma Labbaika) na watu wakirudia Talbiya yake, na wakiipokea kwa sauti ya wazi, na kwa kutakasa ibada yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa kumpwekesha yeye Aliyetakasika na kutukuka: "Labbaika Ilaahumma Labbaika, Labbaika Laashariika laka Labbaika, Innal hamda wan ni'mata laka wal-mulku Laashariika laka Labbaika".⁵⁰³ Kuitika huku ambako umma umepokezana na bado umma unaendelea mpaka leo ni tangazo la nguvu na wazi kujiepusha na ushirikina na washirikina na kuurudisha Ufalme na neema kwa Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika wake.

Na alilala Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** katika siku ya nnne ya Dhul Hija karibu na Makka, na akaingia asubuhi siku ya tano, na akaingia nyumba tukufu huku akikariri kauli yake: "Ewe

⁵⁰¹ Tazama: Bin kathiri, Hija ya kuaga uk 145 katika riwaya za Imam Ahmad.

⁵⁰² Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabul Maghazi, Mlango wa Hija ya kuaga, 5/125.

⁵⁰³ Tazama: Bin Kathiri, Hija ya kuaga, uk 135, katika riwaya ya Muslim, na riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, kitabul Hajji, Mlango wa Talbiya, 2/147

Mwenyezi Mungu hakika wewe bila shaka ni Amani, na Amani hutoka kwako, tuhusihe sisi kwa Amani"⁵⁰⁴Na alipoiona Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake Al-ka'ba- akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu izidishie nyumba yako hii heshima na utukufu na takrima na uzuri"⁵⁰⁵

Na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akaelekea katika Al-ka'ba na akatufu (akaizunguka) naye akiwa kapanda juu ya Ngamia wake akiwatazama watu katika pande zote, wakawa wakimuiga na wakimuuliza, walikuja kutoka kila mahali wakimzunguka na wakimtazama yale anayoyafanya na wakisikiliza anayoomba katika dua.⁵⁰⁶

Na alilipokea Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- jiwe jeusi kwa mkongojo uliokuwa mkononi mwake, na akatembea haraka katika mizunguko mitatu ya mwanzo,⁵⁰⁷ na alipomaliza alisoma Rehema na Amani ziwe juu yake- kauli yake Mtukufu:

﴿وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْعَاكِفِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ﴾ [البقرة: 125]

"Na Kumbuka, ewe Nabii, wakati tulipoifanya Alka'ba ni marejeo ya watu; wanakuja kuikusudia, kisha wanarudi makwao kwa watu wao, kisha wanairudia tena, ni makusanyiko yao katika Hija, Umra, kutufu na kuswali, na pia ni amani kwao: hakuna adui

⁵⁰⁴ Tazama: Takhriji yake kwa bin Kathiri, Hija ya kuaga, uk. 166.

⁵⁰⁵ Tazama: Takhriji yake kwa bin Kathiri, Hija ya kuaga, uk. 165.

⁵⁰⁶ Tazama: Takhriji yake kwa bin Kathiri, Hija ya kuaga, uk. 146.

⁵⁰⁷ Tazama: Takhriji yake kwa bin Kathiri, Hija ya kuaga, uk. 168.

anayewashambulia wakiwa hapo na tukasema, “Pafanyeni hapo Maqām Ibrāhīm ni mahali pa kuswali. Maqām Ibrāhīm ni jiwe ambalo Ibrāhīm alisimama juu yake alipokuwa akijenga Alka'ba. Na tulimletea Wahyi Ibrahīm na mtoto wake Ismāīl kwa kuwaambia, «Isafisheni Nyumba Yangu na kila najisi na uchafu kwa ajili ya wenye kuabudu kwa kutufu pembezoni mwa Alka'ba au kuketi Itikafu (I'tikāf) Msikitini na kuswali hapo.” [Al Baqarah: 125] Na akasali rakaa mbili katika kisimamo cha Ibrahim (Maqamu Ibrahim) kiasi ambacho aliifanya sehemu hiyo kuwa kati yake na Alka'ba, akasoma katika rakaa ya kwanza (Qul Yaa ayyuhal kaafirun) na katika rakaa ya pili (Qul huwallaahu Ahad), kisha akaielekea nguzo na akaelekea katika swafa huku akisoma kauli yake Mtukufu:

﴿إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِن شَعَائِرِ اللَّهِ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّفَ بِهِمَا وَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ﴾ [البقرة: 158]

"Hakika Swafa na Marwa, nayo ni majabali mawili madogo karibu ya Alkaba upande wa Mashariki, ni miongoni mwa alama za dini ya Mwenyezi Mungu zilizo wazi ambazo Mwenyezi Mungu Amezifanya ni sehemu za ibada kwa waja Wake kutembea baina yake. Hivyo basi, yoyote mwenye kuikusudia Alkaba kwa kuhiji au kufanya Umra, si dhambi kwake kutembea baina ya hayo majabali mawili, bali ni wajibu kwake kufanya hivyo. Na yule mwenye kufanya mambo ya kutii amri, kwa hiyari yake, hali ya kumtakasia Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushukuru, Analipa juu ya kichache kwa kingi, ni Mwenye kuzijua amali za waja Wake: Hazipotezi wala Hampunji yoyote chochote hata kama ni uzito wa chungu mdogo" [Al baqara: 158] Mpaka alipopanda juu ya Mlima swafa akaelekea ka'ba na akatoa takbira (Allahu Akbaru) na akasema: "Laailaha illa llahu wah'dahuu laa shariikalahuu,lahul mulku alahul hamdu wahuwa alaa kulli shain qadiir, Anjaza wa'dahu wanaswara abdahu wa hamazamal ahzaba wahdahu," Kisha akaelekea mlima Marwa kisha akakamilisha

kukimbia kwake, alikuwa Rehema na Amani ziwe juu yake akikumbuka na akikumbusha nusura na ushindi wa Mwenyezi Mungu kwa makundi ya washirikina waliomuudhi katika mji wa Makka, na kudhihiri kwa Tauhidi, nakuwa Mwenyezi Mungu aliyetakasika na kutukuka ametimiza ahadi yake kuwa atawanusuru waislamu na atawatimizia aliyowaahidi.

Na alibakia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika mji wa Makka siku nne alikuwa amekaa Abtwaha. Na ndani ya kipindi hiki alikuja Ally bin Abii twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kutoka Yemen, na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikuwa kamtuma huko, na akamkabidhi mke wake kipenzi Fatma binti wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.⁵⁰⁸

Ilipofika asubuhi siku ya tarwiya, siku ya alhamisi ya (siku ya nane ya) Dhil Hija alitoka Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- pamoja na mahujaji kwenda Mina, mpaka alipofika Mina akawasalisha watu swala ya Adhuhuri na Laasiri kwa kuziunganisha na kuzipunguza, na vile vile magharibi na ishaa, Na Bilali -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- alikuwa akimuadhinia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-⁵⁰⁹Na watu wakitaka baraka kupitia maji ya udhu wa

⁵⁰⁸ Tazama riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, kitabul Maghazi, mlango wa aliowatuma Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akiwemo khalidi kwenda Yemen kabla ya Hija ya kuaga, Hadithi namba: 4353, na bin Kathiri Asiratun nabawiyya, na bin Hisham Asiratun nabawiyya, 4/602

⁵⁰⁹ Tazama Sahihi Bukhari, kitabul Maghazi, mlango wa kumtuma Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Ally bin Abii Twalib na Khalid bin Walidi kwenda Yemen, 5/110, na bin kathiri Assiratun nabawiyya, 4/335

Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na asubuhi ya siku ya Arafa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- aliwasalisha watu swala ya Alfajiri Mina, na baada ya kuchomoza jua akaelekea maeneo ya Arafati, na aliamrisha ajengewe hema Namira, na akaenda kinyume na kawaida ya Makuraishi, na akavuta hisia ya amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kauli yake:

﴿ثُمَّ أَيْضًا مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ النَّاسُ وَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [البقرة:

[199

"Na iwe kuondoka kwenu kutoka kisimamo cha Arafa, ambapo ndipo alipoondoka Ibrahim, amani imshukie, ni katika hali ya kumkhalifu, kwa hilo, yule asiyesimama hapo miongoni mwa watu wa zama za ujinga. Na muombeni Mwenyezi Mungu Awasamehe madhambi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaghufiria waja wake waombao maghufira, wanaotubia, ni mwenye huruma kwao." [Al-baqara: 199]

Na akashuka -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika hema alilojengewa hapo Namira, na siku hiyo ya Arafa ilikuwa sambamba na mwezi march mwaka 632G, nao ni mwezi wa tatu mwishoni mwa masika na mwanzoni mwa kiangazi, kiasi kwamba Makka ilijulikana kwa joto kali mpaka hata wakati wa masika, ni vipi wakati wa kiangazi!.

Na ndio maana hema hilo lilikuwa ni kwa ajili ya kutaka kivuli, na ili watu wajue alipo Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwa mwenye kumuhitajia na akachagua sehemu maalumu pa kusimama katika Arafa yake, na akabakia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika hema akimtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu, na akiyatekeleza aliyoyasema -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-: "Dua bora ni ya siku ya Arafa, na neno bora nililosema mimi na Manabii kabla yangu, Laa ilaaha illa Ilaahu, wahdahu laa shariika lahu" Na

katika upokezi "Laa ilaaha illa Ilaahu, wahdahu laa shariika lahu, lahul mulku walahul hamdu wahuwaalaa kulli shai in Qadiir"⁵¹⁰

Na amepokea Zubair bin Awwam -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- anasema nilimsikia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akisoma aya:

﴿شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ
الْحَكِيمُ﴾ [آل عمران: 18]

"Mwenyezi Mungu Ameshuhudia kuwa Yeye hapana mola mwingine wa haki ila yeye Na na Malaika pia wameshuhudia na watu wenye elimu juu ya kitu kitukufu zaidi chenye kushuhudiwa, nacho ni Tawhīd umoja Wake Aliyetukuka na kusimamia Kwake haki na uadilifu. Hapana Mola ispokuwa Yeye, Aliye Mshindi Ambaye hakuna kitu Atakacho kiwe kikakataa kuwa, Mwenye hekima katika maneno Yake na vitendo Vyake." [Al-Imran: 18]. Na imepokelewa kuwa ilikuwa miongoni mwa dua zake siku ya arafa. "Ewe Mwenyezi Mungu hakika wewe unasikia maneno yangu, na unaiona nafasi yangu, na unaijua siri yangu na uwazi wangu, na halifichiki lolote katika mambo yangu, mimi ni mwenye shida fakiri, ninayetaka msaada na ulinzi, mwenye hofu na uoga, mwenye kukiri na kukubali madhambi yangu, ninakuomba maombi ya masikini (mwenye haja) na ninajinyenyekeza kwako kujinyenyekeza kwa mtu dhalili, na ninakuomba maombi ya mtu mwenye hofu na mnyonge, iliyeinama kwa ajili yako shingo yake, na macho yake kububujika machozi kwa ajili yako, na ukadhalilika mwili wake kwa ajili yako, na pua yake ikapata mchanga kwa ajili yako, Ewe Mwenyezi Mungu

⁵¹⁰ Maalik bin Anas, Al Muwattwa,i, kitabul haji, Babu Jaamiul Haji, uk 350.

usinifanya katika maombi yangu hayo Mola wangu kuwa ni mwenye bahati mbaya, na uwe kwangu mpole mwenye huruma, ewe mbora wa waombwaji, na ewe mbora wa watoaji"⁵¹¹Na imethibiti kuwa aliomba dua hii akiwa juu ya Ngamia wake -**rehema na Amani ziwe juu yake**-⁵¹²

Na akaendelea Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kuomba akiwa ndani ya hema lake mpaka lilipopinduka jua (Muda kati ya saa tano na saa sita) akaamrisha aletewa ngamia wake aitwaye Al-Qaswaa, akampanda na akaja chini ya bonde akaamrisha watu wanyamazishwe,⁵¹³ ili wasikilize hotuba yake na waizingatie, basi watu wakatawanyika wakinadi kwa sauti wakisema yale aliyoyasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwa watu,⁵¹⁴ na zimekuja riwaya mbali mbali kuhusu sehemu ya yale aliyoyasema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika hotuba yake, ikawawea vigumu baadhi ya wapokezi kuyakusanya yote kama nukuu moja, lakini wao walielewa maana yake, na wakaandika sehemu hizo za hotuba katika riwaya mbali mbali, na maudhui mbali mbali. na ilikuwa miongoni mwa yale aliyoyasema:⁵¹⁵"Enyi watu sikilizeni kauli yangu, kwani mimi sijui kama nitakutana nanyi baada ya mwaka wangu huu, katika sehemu hii milele, Enyi watu!, Hakika

⁵¹¹ bin kathiri, Hijatul wadai, uk 241, na tafsiri yake, 1/358

⁵¹² tazama: sahihi Bukhari, Hadithi namba 4399, 4400.

⁵¹³ Bukhari katika sahihi yake, Hadithi namba: 4404.

⁵¹⁴ Tazma Historia yas Twabariy juzuu ya 3/169.

⁵¹⁵ Tazama: Kitabu Alfu minal khutba biunwani: "Al-Waswiyyatun nabawiyya lil ummatil islaamiyya" cha Dr. Farouq Hamad, Darul kasim, Damaskas, 1422H.

damu zenu na mali zenu juu yenu ni haramu mpaka mtakapokutana na Mola wenu, kama ulivyo uharamu wa siku yenu hii, na kama uharamu wa mwezi wenu huu, na hakika nyinyi iko siku mtakutana na Mola wenu na atakuulizeni kuhusu matendo yenu, na mimi nimefikisha, yeyote mwenye amana ya mtu basi airejeshe kwa yule aliyemwamini, na tambueni kuwa miamala yote ya riba iwacheni isipokuwa mitaji yenu msidhulumu na wala msidhulumiwe. Amekwisha hukumu Mwenyezi Mungu kuwa hakuna riba (katika miamala), na hakika riba iliyokuwa kwa Abbasi bin Abdil Muttwalib imefutwa yote, na hakika kila kisasi cha damu ya mtu kilichokuwa katika zama za ujinga kimefutwa, na hakika kisasi cha damu yenu cha kwanza ninachoanza kukifuta ni kisasi cha Rabia' bin Harith bin Abdil Muttwalib, Huyu alipelekwa kwenda kunyonya kwa bani Laith wakamuua bani Hudhail, huyu ndiye wa kwanza ninaye anza naye katika damu za zama za ujinga. Ama baada ya hayo, Enyi watu, hakika shetani amekwisha kata tamaa ya kuabudiwa tena katika ardhi yenu hii milele, lakini huikanyaga ardhi yenu kwa mambo mengine yasiyokuwa hayo, kwani yeye ameridhika na mambo madogo madogo mnayoyadharau katika matendo yenu, mtahadharini sana juu ya matendo yenu, Enyi watu: Hakika kuichelewesha miezi ni kuzidi kukufuru (walikuwa wanapotaka kupigana katika miezi iliyokatazwa wanabadili kalenda wanafanya huo ni katika miezi walioruhusiwa) wanapotezwa kwa hilo wale waliokufuru, wakaihalalisha mwaka fulani na wakaharamisha mwaka fulani ili waweze kuziruka siku alizozikataza Mwenyezi Mungu na wakahalalisha aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu. Hakika siku zimezunguuka kama ilivyo kawaida yake tangu siku alipoumba Mwenyezi Mungu Mbingu na Ardhi, na hakika idadi ya miezi mbele ya Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili, miongoni mwake kuna miezi minne mitukufu mitatu inafuatana, na mmoja ni Rajab, ulioko katika ya mwezi Jumada na Shaban. Ama baada ya hayo, Enyi watu: Hakika nyinyi mna haki zenu kwa wake zenu, na wao pia wana haki zao kwenu, katika haki zenu kwao asilale katika

vitanda vyenu yeyote mumchukiaye, na ni jukumu lao kuwa wasileta uchafu wa wazi, ikiwa watafanya basi Mwenyezi Mungu amekupeni ruhusa nyinyi ya kuwahama katika malazi, na muwapige kipigo kisicho jeruhi,, ikiwa watakomeka, basi wana haki ya kuhudumiwa chakula na mavazi ila kwa wema (pasina kuwabana wala kupitiliza katika matumizi), na ishini na wanawake kwa wema, kwani hao ni wasaidizi kwenu nyinyi, hawamiliki chochote kwa nafsi zao, na mkumbuke kuwa mliwachukua kwa (ahadi ya) amana ya Mwenyezi Mungu, na mkahalalisha tupu zao kwa neno la Mwenyezi Mungu, itieni akili enyi watu kauli yangu hii, hakika mimi nimefikisha (Ujumbe) Na hakika nimekuachieni kwenu nyinyi mambo ambayo ikiwa mtashikamana nayo kamwe hamtopotea milele, jambo liko wazi, ni kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho yanabii wake. Enyi watu sikilizeni vizuri kauli yangu na muizingatie, mnajua kuwa kila muislamu ni ndugu wa muislamu mwingine nakuwa waislamu wote ni ndugu, hivyo si halali chochote cha ndugu yake isipokuwa kile alichompa kwa ridhaa yake mwenyewe, hivyo msizidhulumu nafsi zenu, Jamani (Ewe Mwenyezi Mungu) Je nimefikisha?." Nilielezwa kuwa watu walisema: -Ewe Mwenyezi Mungu- ndiyo, akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu shuhudia".⁵¹⁶

Na alichokisema ni hiki: "Hakika Mwenyezi Mungu kampa kila mwenye haki haki yake basi haifai kutoa usia wa mali kwa mrithi, na mtoto ni wa godoro na mzinifu atazuliwa, na atakayedai kuzaliwa na asiyekuwa baba yake au akadai bwana asiye bwana yake basi huyo ana laana za Mwenyezi Mungu na Malaika na watu wote kwa ujumla, wala hatokubali Mwenyezi Mungu kutoka kwake wajibu

⁵¹⁶ Bin Hisham, Assiratun nabawiyya: 4/605, na tazama: Sehemu miongoni mwake katika kitabu cha Sahihi Bukhari, hadithi namba: 4403, na bin Kathiri Assiratun nabawiyya, 4/342.

wala sunna",⁵¹⁷Na miongoni mwa yale aliyoyasema: "Msirudi baada yangu mkawa makafiri mkawa mkiuwana baadhi yenu kwa baadhi"⁵¹⁸

Na imepokelewa hotuba kwa matamko mengine pia, pamoja na kuafikiana katika maana, yale aliyoyaandika bin Hisham, na huenda baadhi yake ilikuwa katika siku ya Idd au siku nyingine, na miongoni mwake ni yale yaliyoandikwa katika sahihi Bukhari katika hadithi za Abii Bakra kutoka kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake, amesema: "Zama zimezunguka kama kawaida yake tangu siku aliyounda Mwenyezi Mungu mbingu na Ardhi, mwaka ni miezi kumi na mbili miongoni mwake ni miezi minne mitukufu, miezi mitatu inafuatana nayo ni: Dhul qa'da na Dhul Hijja, na Muharram, na Rajab Mudhwar, ambao uko kati ya Jumada na Shaban, kisha akasema: "Tambueni, ni siku gani hii?" Tukasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wajuzi, akanyamaza mpaka tukadhania kuwa ataita kwa jina lisilokuwa lake, akasema: "Kwani hii si siku ya kuchinja?" Tukasema: Ndivyo, kisha akasema: "Ni mwezi gani huu?" Tukasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wajuzi, akanyamaza mpaka tukadhania kuwa ataita kwa jina lisilokuwa lake, akasema: "Kwani huu si mwezi wa Dhul Hija?" Tukasema: Ndivyo. Akasema: "Ni mji gani huu?" Tukasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wajuzi, akanyamaza mpaka tukadhania kuwa ataita kwa jina lisilokuwa lake, akasema: "Kwani huu si mji wa Makka? Tukasema: Ndivyo, akasema: "Basi hakika damu zenu na mali zenu, na ninadhani pia alisema: "na heshima zenu ni haramu juu yenu kama uharamu wa siku yenu hii ndani ya mwezi wenu huu

⁵¹⁷ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/605.

⁵¹⁸ Hadithi hiyo ameipokea Bukhari katika Sahihi yake (Hadithi namba 4403).

katika mji wenu huu, na mtakwenda kukutana na Mola wenu na atakuulizeni kuhusu matendo yenu, basi tambueni msirudi baada yangu kuwa makafiri baadhi yenu wakiwaua baadhi, Tambueni, Hivi nimefikisha? Tambueni, na amfikishie aliyepo asiyekuwepo miongoni mwenu, huenda anayefikishiwa akawa ni msikivu zaidi kuliko baadhi ya waliosikia, akawa Muhammad kila anapokumbuka anasema: Amesema kweli Muhammad Rehema na Amani ziwe juu yake- kisha akasema: "Hivi je, nimefikisha?" Akakariri mara mbili".⁵¹⁹

Na ni wazi kuwa hotuba hii au hotuba hizi zinahesabika kuwa ni katiba ya ubinadamu kwa ujumla kwa zama zote za maisha ya binadamu na vizazi vyake, mpaka atakapoirithi Ardhi Mwenyezi Mungu na vilivyomo, nayo ndio hotuba muhimu zaidi katika hotuba zote alizohutubia wa mwisho katika manabii wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake Rehema na Amani ziwe juu yake, kwa amri ya muumba akizielekeza kwa viumbe, Ndani yake kuna kumpwekesha Mwenyezi Mungu, na kuhifadhi haki za mwili na roho na mali, na kumewekwa mipaka ya haki za mwanamke na heshima yake, na kumeheramishwa kuvunja haki za wengine, na pupa ya kutekeleza amana kwa wenye nazo, na ukaanza mfumo mpya wa ulimwengu unaotegemea uchumi wake kwa kuzuia riba, na kuleta matumaini kwa kusahau yaliyopita, pamoja na yale yaliyomo miongoni mwa visasi vya damu, na pupa ya kuihifadhi kwa wakati huu na ujao, na kimaadili kutahadharishwa na shetani na matendo yake yenye lengo la kuharibu mahusiano kati ya watu na kuenea kwa ugaidi na umwagaji damu hovyoo.

Na imetia mkazo hotuba hii juu ya usawa wa binadamu wote nakuwa wao ni ndugu na asili yao ni moja, na kuwakumbusha marejeo ya kisheria, nayo ni Qur'ani na mafundisho ya Mtume, na

⁵¹⁹ Bukhari katika sahihi yake, Hadithi namba: 4406.

Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- hapa anatilia mkazo juu ya mfumo wa sheria na marejeo yake, na kuijenga jamii ya kibinadamu kwa mfumo aliouweka muumba wao, ili jamii iweze kufikia kuwa na Amani kati yao, na kumridhisha muumba -Aliyetakasika na kutukuka-, na kuelewana katika maisha salama ya kidunia, na utamaduni wa kibinadamu uliosimama katika misingi sahihi, na usawa baina ya watu.

Kama ilivyoonekana wazi pupa ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kuwa watu washuhudie kuwa yeye ametimiza amana ya utume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na ametimiza wajibu wake, na ndio maana aliposikia kutoka kwao ushuhuda alinyanyua kidole chake mbinguni na akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu shuhudia", Alikuwa Rehema na Amani ziwe juu yake akivuta hisia juu ya yale anayowaeleza watu akawa ananyanyua macho juu, akitaka radhi za Mwenyezi Mungu -Aliyetakasika na kutukuka- ambaye anayemuona yeye na watu wote.

Na akasisitiza Rehema na Amani ziwe juu yake kuwa Arafa yote ni mahala pa kusimama, kama alivyosisitiza kuwa Muzdalifa yote ni mahala pa kusimama, na alisisitiza katika Mina pindi alipochinja kuwa Mina yote ni mahala pa kuchinja.⁵²⁰

Na baada ya hotuba yake Rehema na Amani ziwe juu yake⁵²¹ ikateremka juu yake kauli yake Mtukufu:

⁵²⁰ Tazama: Musnadul Imamu Ahmad, 1/72, na tazama: Attwabari, Tarikh yake, 4/170.

⁵²¹ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4407.

﴿حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أَلْمَيْتَةُ وَالْدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنْزِيرِ وَمَا أُهْلَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ
 وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَاللَّطِيحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُيِّعَ عَلَى الثُّبِّ وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا
 بِالْأَزْلَمِ ذَلِكَ مِنْ نِسْئِ الْيَوْمِ يَسِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ الْيَوْمَ
 أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمْ الْإِسْلَامَ دِينًا فَمَنِ اضْطُرَّ فِي
 مَخْمَصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمٍ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [المائدة: 3]

"Mwenyezi Mungu Amewaharamishia mfu, naye ni mnyama aliyekufa mwenyewe bila ya kuchinjwa. Na pia Amewaharamishia nyinyi damu inayotiririka inayomwagwa, nyama ya nguruwe, mnyama ambaye wakati wa kuchinjwa ametajiwa jina lisilokuwa la Mwenyezi Mungu, mnyama aliyenyongwa kwa kuzibwa pumzi zake mpaka akafa, mnyama aliyekufa kwa kupigwa gongo au jiwe, mnyama aliyeanguka kutoka mahali pa juu au aliyeanguka kisimani akafa na mnyama aliyekufa kwa kupigwa pembe na mwenzake. Na pia Amewaharamishia mnyama aliyeliwa na mnyama mwingine kama simba, chuimarara, mbwamwitu na mfano wake. Mwenyezi Mungu, Aliyetakasika na sifa za upungufu, Amewatoa, miongoni mwa wale Aliwaharamisha, kuanzia wale walionyongeka na waliofuatia, wale mliowahi kuwachinja kabla hawajafa, hao ni halali kwenu. Na Amewaharamishia nyinyi wanyama waliochinjiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu miongoni mwa vitu vilivyosimamishwa viabudiwe, viwe ni mawe au vinginevyo. Na Amewaharamishia kutaka kujua mambo, mliyoandikiwa na msiyoandikiwa, kwa viapo; navyo ni vipande ambavyo walikuwa wakitaka uamuzi kwavyo wakitaka kufanya jambo kabla hawajalifanya. Hayo mliyotajiwa katika aya hii kati ya yaliyoharamishwa, yakifanywa, huwa ni kutoka kwenye amri ya Mwenyezi Mungu na twaa Yake na kwenda kwenye maasia. Sasa imekatika tamaa ya makafiri kwamba nyinyi mtaiacha Dini yenu muende kwenye ushirikina baada ya mimi kuwapa ushindi juu yao. Basi msiwaogope wao na mniogope mimi. Leo

nimeshawakamilishia dini yenu, Dini ya Uislamu, kwa kuuhakikisha ushindi na kuikamilisha Sheria, nimewatimizia neema zangu kwenu kwa kuwatoa kwenye giza la ujinga na kuwapeleka kwenye mwangaza wa Imani na nimewaridhia kwamba Uislamu ndio Dini, basi shikamaneni nayo wala msiiache. Na yule aliyepatikana na dharura ya njaa ikambidi ale mfu, na akawa hakukusudia kutenda kosa, basi inafaa kwake kumla. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kumsamehe na ni Mwenye huruma naye." [Al Maida: 3] Alipoisikia aya hii Omar akalia. Akasema Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- "kipi kinakuliza?" Akasema: Kilichoniliza nikuwa sisi tulikuwa katika kuongeza maarifa kila wakati, ama mafundisho yanapokamilika basi hakuna kitu kinachokamilika ila hupungua, akasema: "Umesema kweli", ikawa aya hii inatangaza kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-
522

Na zinakuja kuteremka aya zikithibitisha kusikia kwa Mwenyezi Mungu ushuhuda wa watu kuwa Mtume wake amefikisha ujumbe na ametekeleza amana na ameunasihii umma, aya hizi ili zilitia mkazo kuwa dini imekamilika na neema ya Allah imetimia kwa kutekeleza Muhammad Rehema na Amani ziwe juu yake jukumu lake, na kufikisha kwake ujumbe wake, na kuwaaga kwake watu na kukaribia kuondoka kwake, na ukweli wa kauli ya swahaba: "Tulikuwa tukizungumza kuhusu Hija ya kuaga na Mtume Rehema

⁵²² Al Halabiy, Assiratul Halabiyya, 3/325, na tazama riwaya ya Bukhari katika sahihi yake, 5/127, na tazama: Bin Kathiri, Assiratun nabawiyya, 1/579

na Amani ziwe juu yake akiwa nasi na wala hatukujua ni ipi Hija ya kuaga".⁵²³

Na katika mambo ya uhakika nikuwa kulikuwa na hotuba zingine nyingi za Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake katika Mina na Makka,⁵²⁴sawa ziwe zile zilizokuwa siku ya kuchinja na swala ya Idd au zinginezo, wamepokezana kuzipokea wanachuoni na wasomi wa Hadithi, na wakanukuu sehemu miongoni mwake.⁵²⁵Na miongoni mwake ni ile aliyopokea bin Omari katika kitabu cha Bukhari yakuwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake: "Alimshukuru Mwenyezi Mungu na akamsifia, kisha akamtaja masihi dajali akakithirisha kumtaja, na akasema: "Hakuwahi kutuma Mwenyezi Mungu Nabii isipokuwa aliutahadharisha naye umma wake, alitahadharisha Nuhu na Manabii waliokuja baada yake, na hakika atatoka kwenu nyinyi, yale atakayoyaficha katika mambo yake hayatofichikana kwenu, lakini pia hali yake haitofichikana kwenu, Hakika Mola wenu hayuko katika yale yaliyofichikana kwenu" Akarudia kauli hiyo mara tatu, "Hakika Mola wenu si chongo, na hakika yeye (Masihi dajali) ni chongo wa jicho moja jicho lake ni kama zabibu iliyofifia"⁵²⁶

⁵²³ Tazama: Hadithi bin Omar kwa Bukhari katika sahihi yake, kitabul Maghazi, Mlango wa Hijjatul Wadai, 5/126.

⁵²⁴ Tazama: Ibrahim, Muhammad Ibrahim Muhammad. Al Jaanibul I'laami fii Khutwabir rasul, chapa ya kwanza, Al Maktabul Islami, Beirut, 1406H, uk119,129.

⁵²⁵ Bin Hajari, Fat-hul bari, 16/233.

⁵²⁶ Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabul Maghazi, Mlango wa Hija ya kuaga, 5/126.

Na baada ya kumaliza hotuba siku ya Arafa Bilali bin Rabaha - Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- aliadhini , kisha akakimu na Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akawasalisha watu Adhuhuri rakaa mbili, kisha akakimu Bilali tena mara nyingine, akawasalisha Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake watu Lasiri rakaa mbili, kisha akapanda Ngamia wake, na akamuelekeza katika jangwa, chini ya mlima Rahma na akaelekea kibla akaanza kuomba Rehema na Amani ziwe juu yake.⁵²⁷

Lilipozama jua alipanda pamoja naye Osama bin Zaidi (Nyuma yake) kisha akaondoka viwanja vya Arafa.⁵²⁸ Na alikuwa akisoma kauli ya Mwenyezi Mungu:

﴿ثُمَّ أَيْضًا مِنْ حَيْثُ أَقَاصِ النَّاسِ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [البقرة:

[199

"Na iwe kuondoka kwenu kutoka kisimamo cha Arafa, ambapo ndipo alipoondoka Ibrahim, amani imshukie, ni katika hali ya kumkhalifu, kwa hilo, yule asiyesimama hapo miongoni mwa watu wa zama za ujinga. Na muombeni Mwenyezi Mungu Awasamehe madhambi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaghufiria waja wake waombao maghufira, wanaotubia, ni mwenye huruma kwao." [Al-baqara: 199] Na alikuwa Mtume

⁵²⁷ Al Halabiy, Assiratul halabiyya, 3/324.

⁵²⁸ Tazama: Riwaya ya Bukhari, kitabul Haji, Mlango wa kushuka Arafa na kuunga swala, 2/176.

Rehema na Amani ziwe juu yake akiwaamrisha watu "Enyi watu, kuweni na utulivu, utulivu"⁵²⁹

Na alikuwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akitoa talbia (Akisema: Labbaika Ilaahumma Labbaika mpaka mwisho) Mpaka Bilali aliponyanyua sauti ya adhana kisha akakimu akasali swala ya magharibi, kisha akasali Isha'a kwa kuipunguza, kisha akalala Rehema na Amani ziwe juu yake, ilipochomoza Alfajiri aliisali mwanzo wa wakati wake, kisha akaenda mash'aril Haram akaelekea kibla na akaanza kuomba kwa uchungu mpaka mawingu yalipoanza kuwa ya njano, huku akiwa kampakiza nyuma yake Al-Fadhlu bin Abbasi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-.

Na imepokelewa yakuwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake "Alirudia kuuombea dua umma wake katika eneo la Muzdalifa, akazidisha kuomba, Mwenyezi Mungu akamteremshia wahyi: kuwa hakika mimi nimewasamehe isipokuwa dhulma walizodhulumiana wao kwa wao, Akasema: Ewe Mola wangu hakika wewe ni muweza wa kumlipa aliyedhulumiwa mazuri zaidi kuliko kile alichodhulumiwa, na ukamsamehe huyu aliyedhulumu, hakumjibu kwa usiku ule, ilipofika kesho yake huko Muzdalifa alirudia kuomba tena, Mwenyezi Mungu akamteremshia wahyi kuwa: Hakika yeye amewasamehe kila kitu, Shetani akaanza kujiombea maangamivu na hasara, huku akijimwagia mchanga kichwani kwake".⁵³⁰

Na akamuamrisha bin Abbasi amuokotee mawe saba madogo madogo kwa ajili ya kurusha, watu walichukua kipimo cha mawe

⁵²⁹ Tazama: Sahihi Bukhari, kitabu Hajji, Mlango wa kuamrisha Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake utulivu, 2/176

⁵³⁰ Abu Shaiba, Assiratun nabawiyya, uk 576.

yake mpaka leo hii,⁵³¹Mpaka alipofika Mina, akarusha mawe ya akaba (eneo) akiwa juu ya kipando baada ya kuchomoza jua akitoa takbira (yaani: akisema: Allahu Akbaru) kwa kila jiwe analorusha,⁵³²Kisha akarudi Mina na akawahutubia watu asubuhi ya siku ya Iddil Adh-ha.

Na ilikuwa miongoni mwa yale yaliyokuja katika hotuba yake: (Na huku Bilal akiongoza kipando chake, na Osama bin Zaidi akimkinga na jua huko Mina) ni kutilia mkazo wa uharamu wa riba na zina na mali za watu na heshima zao, na atakaja utukufu wa siku ya kuchinja, na utukufu wa Makka kwa miji yote, akasema: "Enyi watu, ni siku gani hii?" Wakasema: Ni siku tukufu, Akasema: "Na ni mji gani huu?" Wakasema: Ni mji mtukufu, akasema: "Na ni mwezi gani huu?" Wakasema: "Ni mwezi mtukufu" Akasema: "Basi hakika damu zenu na mali zenu na heshima zenu juu yenu ni haramu, kama ulivyo uharamu wa siku yenu hii katika mji wenu huu, katika mwezi wenu huu" Akakariri maneno hayo mara kadhaa (Kisha akanyanyua kichwa chake na akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu je, nimefikisha?, "Ewe Mwenyezi Mungu je, nimefikisha? basi na amfikishie aliyehudhuria miongoni mwenu asiyekuwepo, Msijekurudi baada yangu mkawa makafiri baadhi yenu wakiwaua baadhi" Na akawaamrisha wachukua ibada zao kutoka kwake, huenda yeye anaweza asihiji tena baada ya mwaka wake ule, na kusimama kwake kulikuwa baina ya jamaati, na watu wako waliokuwa wamesimama na wako waliokuwa wamekaa.⁵³³

⁵³¹ Tazama Takhriji kwa: Ibrahim Al Ally, Sahihi Siratun nabawiyya, uk. 546

⁵³² Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyyat juzuu ya 4/373

⁵³³ Swaleh Al Ally, Sahihi Siiratun nabawiyya, uk 327

Na miongoni mwa yaliyohifadhiwa katika hotuba yake Rehema na Amani ziwe juu yake: "Muabuduni Mola wenu na msali swala zenu tano na muwe watiifu mnapoamrisha, (mkifanya hivyo) mtaingia katika pepo ya Mola wenu".⁵³⁴

Na yalikuwa miongoni mwa yale yaliyohifadhiwa kutoka kwake Rehema na Amani ziwe juu yake- kutoka katika hotuba ile pia ni: "Hakuna ubora kwa mwarabu kwa asiyekuwa mwarabu, wala asiyekuwa mwarabu kwa mwarabu, wala mweupe kwa mweusi, wala mweusi kwa mweupe isipokuwa kwa uchamungu, watu wote wametoka kwa Adamu na Adamu katokana na udongo"⁵³⁵

Na wanaweza kudhania baadhi kuwa katika hilo kuna kosa katika riwaya katika kukariri maana, lakini kinachoonekana wazi nikuwa - Na Allah ndiye Mjuzi- Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikusudia kusisitiza katika baadhi ya matukio na maana, katika zaidi ya hotuba moja katika Hija ya kuaga, na wala si kuchanganya katika upokezi, bali ni kuyakariri yale ambayo ndani yake kuna masilahi kwa baadhi ya yale yaliyozungumzwa katika hotuba ya kuaga katika maeneo zaidi ya moja.⁵³⁶

Na baada ya hapo alielekea Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mahala pa kuchinja, akachinja vichinjo sitini na tatu kwa mkono wake mtukufu, na hii inaendana na idadi ya umri wa miaka yake -Rehema na Amani ziwe juu yake- kisha akaacha na akamuamrisha Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- achinje vilivyobakia katika mia moja, na hii inaonyesha ubora wa

⁵³⁴ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/392

⁵³⁵ Asswallabiy, Assiratun nabawiyya, 2/780

⁵³⁶ Asswallabiy, Assiratun nabawiyya, 2/776

kuchinja na pupa yake Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- juu ya kulitekeleza hili yeye mwenyewe, na ilikuwa inamtosheleza idadi chini ya hapo, lakini yeye -Rehema na Amani ziwe juu yake- alijua fadhila za kuchinja, na ndio maana alizidisha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- idadi na wala haikuhesabika hii ni katika israfu (Ubadhirifu), bali ni katika ibada na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Kama ambavyo sehemu hii inavyoonyesha nafasi ya Ally bin Abii Twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, kiasi kwamba alimalizia vichinjo wa hija alivyoviandaa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na kumchagua kwake kwa jukumu hili pasina mtu mwingine, nako ni kumpa heshima Ally bin Abii Twalib -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kukaa badala ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika nafasi hii maalumu.

Na alikula Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika nyama za vichinjwa vyake, kiasi ambacho alichukua katika kila mnyama sehemu ndogo na akaweka katika chungu na ikapikwa na akala Rehema na Amani ziwe juu yake katika nyama hiyo na akanywa mchuzi wake, na aliamrisha Rehema na Amani ziwe juu yake kugawanywa nyama za vichinjwa vyake na ngozi zake kwa watu, na akaamrisha mchinjaji malipo yake asipewe katika nyama hiyo.⁵³⁷

Kisha akanyoa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kichwa chake kitukufu, alinyolewa na Ma'mar bin Abdillah, akaanza kunyoa upande wake wa kulia, kisha upande wake wa kushoto, na alieleza kuwa alimpa nusu ya nywele zake Abuu Twalha Al-Answari, ambaye

⁵³⁷ Tazama: Sahihi Bukhari, kitabul Haji, Hapewi chochote mchinjaji katika nyama ya Udh-hiya, 2/176, na mlango wa kutoa sadaka ya ngozi za Udh-hiya, 2/186.

ni mume wa mama Sulaim, na yeye akampa nusu nyingine na akamuamrisha aigawanye kwa watu.

Na walikuwa wakitaka baraka kutoka katika nywele zake na jasho lake na harufu yake nzuri Rehema na Amani ziwe juu yake, na aligawa kwa kila mtu nywele moja au mbili au tatu.⁵³⁸

Na hakika aliomba Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: "Ewe Mwenyezi Mungu wasamehe walionyoa", wakasema: Na waliopunguza, akarudia kuomba Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- hivyo hivyo, nao wakarudia mpaka mara tatu, na akasema ya nne: na wenye kupunguza"⁵³⁹.

Na baada ya kunyoa kwake, Aisha mama wa waumini -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- alimtia manukato aliyokuwa kayabeba wakati wa safari.⁵⁴⁰ Na watu walikuwa wakimuuliza maswali, wako waliotanguliza kunyoa na wako waliotanguliza

⁵³⁸ Sahihi Muslim kitabul Haj, 4/82, Na tazama: Sahihi Bukhari, kitabul Haji, Mlango wa kunyoa na kupunguza na kujivua katika hija, 5/188.

⁵³⁹ Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabul Haji, mlango wa kunyoa na kupunguza wakati wa kumaliza hija, 2/188

⁵⁴⁰ Bin kathiri, Assiratun nabawiyya, 3/378, Na tazama sahihi Bukhari hadithi namba: 4410 na namba: 4411, na ufafanuzi wake kwa bin Hajari katika Fat-hul Bari, 16/236.

kuchinja, akawa akisema Rehema na Amani ziwe juu yake-: "Fanya na wala hakuna tatizo".⁵⁴¹

Na baada ya hapo akaelekea Makka na akatufu twawafu ya kuaga, kisha akanywa katika maji yalioandaliwa na A-Abbasi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-, na akaelekea katika Zamzam na akanywa hapo Rehema na Amani ziwe juu yake- na alikuwa anataka kushuka pamoja na Bani Abbasi bin Abdil Muttwalib lakini akahofia watu wanaweza kuwa wengi wakawazidia katika kunywa Zamzam, akasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Shukeni enyi bani Abbasi, laiti nisingelihofia watu kukuzidini wakati wa kunywa kwenu basi ningeshuka pamoja nanyi"⁵⁴²

Kisha akarejea Rehema na Amani ziwe juu yake Mina na akabakia hapo siku zote za kubanika nyama akirusha mawe ya Akaba (eneo) na mawe mengine ya kati na ndogo, kila siku baada ya kupinduka jua kwa vijiwe saba, akitoa takbira kwa kila jiwe, na alikuwa akiwaruhusu masahaba zake kuitembelea nyumba tukufu wakati wa kubanika nyama (siku tatu za sikukuu).

Alikuwa Rehema na Amani ziwe juu yake akiunganisha swala kati ya Adhuhuri na Lasiri na kati Magharibi na Isha, akiwafundisha watu lbada zao, na akijibu maswali yao, na akizungumza nao kwa mazungumzo yanayoashiria kuwa anawaaga, na walisambaa watu katika maeneo ya Mina wakiwemo Muhajirina na Maanswari, na makabila mengine, na alikuwa Rehema na Amani ziwe juu yake

⁵⁴¹ Ni katika hadithi za Bukhari katika sahihi yake, kitabul Haji, babul Fitya ala daba indal jamra: 2/19, bin Kathiri, Assiratun nabawiyya, 4/393, na tzama: Al-Ally Sahihu ssira, uk. 548.

⁵⁴² Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyyat juzuu ya 4/381

akisema: "Mina ni kituo cha waliotangulia".⁵⁴³ Na alikuwa akiwapa ruhusa wachunga mifugo na wenye udhaifu wa afya na wanawake zaidi kuliko watu wengine. Na imepokelwa kuwa yeye alihutubia katika siku ya pili ya sikukuu na inaitwa ni siku ya vichwa,⁵⁴⁴ Na akataja katika hotuba hiyo baadhi ya yale yaliyokuwa katika hotuba ya Arafati na siku ya kuchinja na akaongeza mengine, na miongoni mwa aliyoyasema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Tambueni kuwa msidhulumu, Tambueni kuwa msidhulumu, Tambueni kuwa msidhulumu, hakika si halali mali ya muislamu isipokuwa kwa ridhaa ya nafsi yake mwenyewe"⁵⁴⁵

Na imepokelewa kuwa yeye aliteremka juu yake suratun nasri, kauli yake Mtukufu:

﴿إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿۱﴾ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿۲﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿۳﴾﴾ [النصر: 1-3]

Itakapo kuja nusra ya ALLAH na ushindi. Na ukawaona watu wanaingia ndani ya dini ya ALLAH makundi makundi. Basi takasa kwa sifa za MOLA wako na umtake msamaha hakika yeye

⁵⁴³ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/398

⁵⁴⁴ Imeitwa ni siku ya vichwa; kwa sababu ni siku ambayo watu hula vichwa vya vichinjwa vyao walivyochinja siku ya Idd, (Bin kathiri) Assiratun nabawiyaa, 3/405. (Na bado inaitwa kwa jina hilo kwa watu wote mpaka sasa).

⁵⁴⁵ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/401

amekuwa ni mkubali tauba. [Al-nasri: 1-3], Ikabainika kuwa anaaga.⁵⁴⁶

Na baada ya kukamilisha matendo yote ya Hija aliondoka Rehema na Amani ziwe juu yake kutoka Mina na akashuka Abtwaha katika mji wa Makka, nayo ni sehemu inayoitwa kwa jina la Khaifu bani kinana au Al-Mukhadhwabi,⁵⁴⁷na ilikuwa ni sehemu nzuri sana ya kufanyia maandalizi ya kutoka kwake Rehema na Amani ziwe juu yake katika mji wa Makka.

Na imepokelewa kuwa Osama bin Zaidi alimuuliza Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**:- Kesho utashuka wapi? Akasema: "Na je, watu wa Akili wametundalia nyumba ya kufikia?" Kisha akasema: "Sisi tutashuka kesho -In Shaa Allah- katika kituo cha bani kinana, akikusudia Makhdhwab sehemu ambayo makuraishi walikula kiapo dhidi ya ukafiri"⁵⁴⁸

Na ilipofika asubuhi ya siku inayofuata Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- aliwasalisha watu swala ya Alfajiri katika Al-ka'ba na akasoma suratu Tur yote, kisha akaizunguka Al-kaaba (Twawafu)

⁵⁴⁶ Bin kathiri, Assiratun nabawiyya, 4/403, Tazama: Hadithi ya Bukhari, kitabu ttafsiri, Suratu (Idhaajaa anusrullahi wal fat-hu), 6/93-94

⁵⁴⁷ BIn kathiri Assiratun nabawiyya, 4/410, Ibrahim Al Ally, Sahihu ssira, uk 549.

⁵⁴⁸ Bin kathiri Assiratun nabawiyya, 4/407, ni katika riwaya ya Bukhari.

Mizunguko saba na akasimama kati jiwe na Al-ka'ba na akaanza kuomba dua Rehema na Amani ziwe juu yake⁵⁴⁹

Na aliwaamrisha Rehema na Amani ziwe juu yake watu watufu twawafu ya kuaga, akasema: "Asiondoke yeyote mpaka kuwe kuaga kwake kwa mwisho ni katika nyumba tukufu"⁵⁵⁰

Na alikuwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** akichunga sana hali za masahaba zake na mama wa waumini, huyu hapa Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- alitaka kufanya Umra, hakuwa na budi Rehema na Amani ziwe juu yake ya kumuita Abdul Rahman bin Abii Bakri Aswiddiq akamwambia: "Nenda na dada yako nje ya Msikiti akatie nia ya Umra, kisha aje aizunguke Al-kaaba mimi ninakusubirieni hapa" Aisha anasema: Tukatoka na nikatia nia kisha nikarudi nikatufu katika nyumba tukufu na nikakimbia swafa na Marwa tukaja kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**nyumbani kwake ukiwa ni usiku mwingi, akasema: "Vipi, umemaliza? Nikasema: Ndiyo, basi akawaruhusu masahaba zake kuondoka"⁵⁵¹

Na kulikuwa kutoka kwake Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** chini ya mji wa Makka kuelekea Madina, na ilikuwa Hija hii ndiyo ya kwanza baada ya kuhama kutoka Makka, na ya mwisho

⁵⁴⁹ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/411

⁵⁵⁰ Kaipokea Muslim katika sahihi yake, kitabul Haji, mlango wa twawafu wada'a, na kuondolewa kwake kwa mwenye hedhi, 4/93, Na Bukhari sahihi yake, mlango wa twawafu ya kuaga.

⁵⁵¹ Kaitoa Bukhari, katika mlango wa Hija juu ya kipando, na mlango wa kauli yake Mtukufu: "Hija ni miezi maalumu" Na Muslim katika sahihi yake, kitabul Haji, kubainisha namna za ihiramu, Na tazama Al Ally, Sahihussira, uk 534. Na bin kathiri Assiratun nabwiyya, 4/410.

kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, kama ambavyo ilivyokuwa ziara hii ndiyo ya kuuaga mji wa Makka, hakuuzuru tena na wala hakuuona tena Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- baada ya hapo mpaka alipofishwa Rehema na Amani ziwe juu yake.⁵⁵²

Na alipokuwa Makka wakati wa Hija ya kuaga Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikuwa na pupa ya kuwafuatilia masahaba zake na kuchunguza hali zao katika hija, pamoja na kushughulika kwake na mahujaji wote alijua kuugua kwa Sa'di bin Abii Wakasi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, naye alikuwa sahaba wake tangu kabla ya kuhama na baada ya kuhama, na ni mmoja kati ya waliobashiriwa pepo, Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akamtembelea, katika hadithi ya sa'di bin Abii Wakasi katika kitabu cha Bukhari Amesema: "Alinitembelea mimi Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- wakati wa hija ya kuaga nilipokua mgonjwa maradhi yaliyokaribia kunipeleka katika mauti, nikasema: ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu maumivu ya maradhi yamenifikisha hapa unapopaona, na mimi ni mtu mwenye mali na sina wa kunirithi isipokuwa binti yangu mmoja, je, nitoe sadaka ya theluthi mbili ya mali yangu? Akasema: "Hapana", akasema: Nitoe sadaka nusu yake? Akasema: "Hapana", Nikasema: na theluthi moja? akasema: "theluthi moja sawa, japo na theluthi moja pia ni nyingi, kwani hakika wewe ukiwaacha watoto wako wakiwa matajiri ni bora zaidi kuliko kuwaacha wakiwa masikini wakiomba omba misaada kwa watu, na hautotoa matumizi yoyote ukitaraji malipo kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu atakulipa kwa matumizi hayo, hata tonge unaloliweka katika kinywa cha mke wako" Nikasema:

⁵⁵² Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabul Maghazi, Mlango wa Hija ya kuaga, 4/126.

Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, je, niache msimamizi katika jamaa zangu? Akasema: "hakika wewe hutoacha msimamizi ukafanya jambo hilo ukitaraji radhi za Mwenyezi Mungu isipokuwa utaongeza daraja kwa jambo hilo, na huenda wewe ukaishi muda mrefu mpaka wakanufaika kupitia wewe kaumu ya watu wengi na wengine wakakudhuru, ewe Mwenyezi Mungu zipitisha thawabu za kuhama kwa masahaba zangu na wala usiwakatalie ukawatupia katika shingo zao".⁵⁵³

Na katika jambo hili kunaonyesha upole wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na huruma yake kwa masahaba zake, na kuwafuatilia kwake, kama ambavyo kuna muujiza wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, kwani baada ya hapo aliendelea kuishi Sa'di bin Abii wakasi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- na aliishi muda mrefu baada ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, na akaongoza majeshi ya waislamu huko kaadisia, na katika ufunguzi wa Madaini, kiasi ambacho aliingia mji mkuu wa fursi (Irani) mapema akiwa anapiga takbira huku akinyanyua sauti yake kwa kutoa shahada yakuwa Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kuwa Muhammadi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na hivi ndivyo ilivyosema kweli kauli ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- alipomwambia: ((Na huwenda ukatawalishwa mpaka wanufaika watu kupitia wewe na wapate madhara wengine kwa ajili yako)).{1179}

Mambo mihimu ya Hija ya Kuaga:

⁵⁵³ Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabul Maghazi, Mlango wa Hija ya kuaga, 4/127.

Nayo ni hijjah ya kipekee ambayo umma wa kiislamu ulishudia pamoja na Mtume sala na amani ziwe juu yake,Na umma ukachukua kutoka kwa mtume hukumu za hijjah na sheria zake papo kwa papo.

Upokezi umekithiri kunako hijjah ya Mtume kutokana na kushuhudiwa na watu walio kuwa pamoja na Mtume sala na amani ziwe juu yake,Na hakika walikuwa pamoja na Mtume wamama wa waumini kutokana na wale ambao kulipatikana fatawa zilizo kuwa nyingi katika hija kwa kulingana na hali zao na kwa yale yalio tokea kwa wao.

Na walikuwa watu ni mashahidi wakichukuwa hija kutoka kwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake papo kwa papo,kama alivyo sema Mtume: Zichukuweni kutoka kwangu ibada zenu), Kama yalivyo mapokezi ya hotuba ambayo aliyo itoa Mtume sala na amani ziwe juu yake na miongoni mwa hotuba muhimu katika hizo ni hotuba aliyo itoa kwenye viwanja vya arafah,zimekuja kwa idadi zinakamilishana baadhi kwa baadhi nyingine,bila ya kugongana baina ya hizo hotuba,na inaweza kuwa kujirudia ndio makusudio yenyewe baina ya hotuba nyingine kwa utofauti wa wasikilizaji muda mungine na kwa ajili ya kutilia mkazo jambo katika masikio ya watu,kama ilivyo shuhudiwa na watu kunako makabila na sehemu tofauti waliyo muona Mtume sala na amani ziwe juu yake na wakatambua wosia wake,na wakauchukuwa katika kila upande wa miji ya waarabu na nje yao.

Mtume sala na amani ziwe juu yake aliwataka watu ushahidi,na akawaamrisha wafikishe yale waliyo sikia na ikapendeza sana Mtume kwa ushuhuda wao kuwa yeye amefikisha namna ilivyo kuwa ni kwa yaqini kuwa ALLAH atamuuliza kuna jambo hilo.

Pupa ya Mtume sala na amani ziwe juu yake katika hotuba zake zilizo kuwa kwa idada nyingi ilikuwa ni juu ya kutilia mkazo juu ya kumpwekesha ALLAH-mtukufu-na kuwa yeye ametumwa kutoka kwake kwa yale ambayo kuna patikana kheri kwa viumbe,na akatilia

mkazo juu ya umuhimu wa kutekeleza haki za waja na kuhifadhi damu zao na mali zao,na kuto vuka mipaka baadhi yao kwa baadhi nyingine,na mtu kumdhulumu mtu mungine,na hivyo hivyo kuhifadhi haki za mwanamke na kuto kuwadhohofisha,na umma kuto ungana na mambo ya zama za ujinga,na tamaduni zake zilizo kuwa mbaya katika kila sehemu,na miongoni mwa hizo sehemu ni watu kutafuta pato kwa uharamu wa riba,hivyo hivyo kujiepusha na uzinifu,na baki ya mambo ya dhulma,kama jinsi alivyo tilia mkazo katika hotuba yake juu ya usawa baina ya watu,na akaharamisha juu ya kumwaga damu za watu na kupora mali zao na kuvunja heshima zao.

Na akatilia mkazo Mtume sala na amani ziwe juu yake ya kwamba kunapatikana utaratibu na marejeo ambayo watu watakuwa wakihukumiana kwayo,nacho ni kitabu cha ALLAH na mafundisho ya Mtume wake sala na amani ziwe juu yake,na kuwa umma hauta potea kama watashikamana na viwili hivyo,na kutokana na hayo ni kutengamaa kwa viumbe muda wote mpaka siku ALLAH atairithi ardhi na vilivyomo,na haya ndio yanapelekea umma na watu wake kuwa na umuhimu wa kujifundisha qurani na sunnah na kuwafundisha watu kizazi na kizazi.

Na hakika ametilia mkazo Mtume sala na amani ziwe juu yake juu kupatikana ulazima wa kufikisha: ((Basi aliye kuwepo amfikishiye asiye kuwepo huwenda mfikishaji akawa amehifadhi zaidi kuliko msikilizaji)).⁵⁵⁴

Na jambo hili Mtume sala na amani ziwe juu yake alitekeleza yeye mwenyewe,kisha ikafidisha kila mnasaba ili aweze kuwalea

⁵⁵⁴ angalia dalili ya hotuba kwenye hiki kitabu.

watu na awafundishe na awape fatwa na awaongoze sala na amani ziwe juu yake.

Na ALLAH-aliye takasika na utukufu- akadhahirisha ukamilifu wa dini hii kwa kuteremsha aya ya ukamilifu,amesema ALLAH aliye mtukufu:

﴿حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالْدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهِلَّ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَالطَّيْحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَمِ ذَلِكَمْ فِسْقٌ ۗ النَّيْمَ يَبْسُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنَ اللَّهَ ۗ يَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيْتُ لَكُمْ الْإِسْلَامَ دِينًا فَمَنِ اضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمٍ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [المائدة: 3]

"Mwenyezi Mungu Amewaharamishia mfu, naye ni mnyama aliyekufa mwenyewe bila ya kuchinjwa. Na pia Amewaharamishia nyinyi damu inayotiririka inayomwagwa, nyama ya nguruwe, mnyama ambaye wakati wa kuchinjwa ametajiwa jina lisilokuwa la Mwenyezi Mungu, mnyama aliyenyongwa kwa kuzibwa pumzi zake mpaka akafa, mnyama aliyekufa kwa kupigwa gongo au jiwe, mnyama aliyeanguka kutoka mahali pa juu au aliyeanguka kisimani akafa na mnyama aliyekufa kwa kupigwa pembe na mwenzake. Na pia Amewaharamishia mnyama aliyeliwa na mnyama mwingine kama simba, chuimarara, mbwamwitu na mfano wake. Mwenyezi Mungu, Aliyetakasika na sifa za upungufu, Amewatoa, miongoni mwa wale Aliwaharamisha, kuanzia wale walionyongeka na waliofuatia, wale mliowahi kuwachinja kabla hawajafa, hao ni halali kwenu. Na Amewaharamishia nyinyi wanyama waliochinjiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu miongoni mwa vitu vilivyosimamishwa viabudiwe, viwe ni mawe au vinginevyo. Na Amewaharamishia kutaka kujua mambo, mliyoandikiwa na msiyoandikiwa, kwa viapo; navyo ni vipande ambavyo walikuwa wakitaka uamuzi kwavyo wakitaka kufanya

jambo kabla hawajalifanya. Hayo mliyotajiwa katika aya hii kati ya yaliyoharamishwa, yakifanywa, huwa ni kutoka kwenye amri ya Mwenyezi Mungu na twaa Yake na kwenda kwenye maasia. Sasa imekatika tamaa ya makafiri kwamba nyinyi mtaiacha Dini yenu muende kwenye ushirikina baada ya mimi kuwapa ushindi juu yao. Basi msiwaogope wao na mniogope mimi. Leo nimeshawakamilishia dini yenu, Dini ya Uislamu, kwa kuuhakikisha ushindi na kuikamilisha Sheria, nimewatimizia neema zangu kwenu kwa kuwatoa kwenye giza la ujinga na kuwapeleka kwenye mwangaza wa Imani na nimewaridhia kwamba Uislamu ndio Dini, basi shikamaneni nayo wala msiache. Na yule aliyepatikana na dharura ya njaa ikambidi ale mfu, na akawa hakukusudia kutenda kosa, basi inafaa kwake kumla. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kumsamehe na ni Mwenye huruma naye." (Al Maida: 3)

Kama ambavyo umma ulipata habari njema ya kuteremka kwa sura nasri, na Masahaba wakahuzunika, kiasi kwamba walielewa kutoka katika sura hiyo kukaribia kwa mauti ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-. Na Hija hii ilikuwa kweli ni ya kuaga umma Nabii wao Rehema na Amani ziwe juu yake, kiasi kwamba Alimshuhudisha Mwenyezi Mungu juu ya kutimiza kwake amana.

Hija nzima -hasa hasa kuanzia kufanya talbiya (kusema Labbaika Ilaahumma labbaika) na dua zote zilizofanyika katika maeneo yote matukufu- ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtukuza Mwenyezi Mungu na kujitenga mbali na ushirikina na kuitekeleza ibada kama alivyoamarisha Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَأْتِمُوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ وَلَا تَحْلِقُوا رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحَلَّهُ ۚ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيضًا أَوْ بِهِ أَذًى مِّن رَّأْسِهِ ۖ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ۖ فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامٌ

ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةَ إِذَا رَجَعْتُمْ تِلْكَ عَشْرَةٌ كَامِلَةٌ ذَلِكَ لِمَنْ لَمْ يَكُنْ أَهْلُهُ حَاضِرِي
 الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٩٦﴾ [البقرة: 196]

Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya ALLAH,na ikiwa mkizuiwa basi chinjeni wanyama walio wepesi kupatikana,wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjioni mwao,na atakaye kuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidia kwa kufunga au kwa sadaka au kuchinja wanyama,na mtakapo kuwa salama,basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji,basi achinje mnyama aliye mwepesi kumpata,na asiye pata afunge siku tatu katika Hija na siku saba mtakapo rejea,hizi ni kumi kamili,hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawakuwa Msikiti wa Makkah,na muogopeni ALLAH hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. [Al-Baqara: 196]

Alizingatia sana Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- swala la upole na utulivu katika hija, na akawaamrisha watu kufanya hivyo, na akawapa wepesi wenye matatizo ya kiafya miongoni mwa wanawake na wachunga mifugo na wengineo.

Matukio ya ibada ya hija mengi yameambatana sana na aya za Qur'ani sawa sawa ziwe ambazo ziko katika suratul Haji ambayo imeitwa kwa jina hili, au aya za Qur'ani zenye kuhusiana na hili, na miongoni mwake ni kauli yake Mtukufu:

﴿وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنَا وَانْتَحَدُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلِّينَ وَعِوَدُنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ
 وَإِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ﴾ [البقرة: 125]

"Na Kumbuka, ewe Nabii, wakati tulipoifanya Alka'ba ni marejeo ya watu; wanakuja kuikusudia, kisha wanarudi makwao kwa watu wao, kisha wanairudia tena, ni makusanyiko yao katika Hija, Umra, kutufu na kuswali, na pia ni amani kwao: hakuna adui

anayewashambulia wakiwa hapo na tukasema, “Pafanyeni hapo Maqām Ibrāhīm ni mahali pa kuswali. Maqām Ibrāhīm ni jiwe ambalo Ibrāhīm alisimama juu yake alipokuwa akijenga Alka'ba. Na tulimletea Wahyi Ibrahīm na mtoto wake Ismāīl kwa kuwaambia, «Isafisheni Nyumba Yangu na kila najisi na uchafu kwa ajili ya wenye kuabudu kwa kutufu pembezoni mwa Alka'ba au kuketi Itikafu (I'tikāf) Msikitini na kuswali hapo.” [Al Baqarah: 125] Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ فَمَنْ حَجَّ أَلْبَيْتَ أَوْ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَنْ يَطَّوَّفَ بِهِمَا وَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ﴾ [البقرة: 158]

"Hakika Swafa na Marwa, nayo ni majabali mawili madogo karibu ya Alkaba upande wa Mashariki, ni miongoni mwa alama za dini ya Mwenyezi Mungu zilizo wazi ambazo Mwenyezi Mungu Amezifanya ni sehemu za ibada kwa waja Wake kutembea baina yake. Hivyo basi, yoyote mwenye kuikusudia Alkaba kwa kuhiji au kufanya Umra, si dhambi kwake kutembea baina ya hayo majabali mawili, bali ni wajibu kwake kufanya hivyo. Na yule mwenye kufanya mambo ya kutii amri, kwa hiyari yake, hali ya kumtakasia Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushukuru, Analipa juu ya kichache kwa kingi, ni Mwenye kuzijua amali za waja Wake: Hazipotezi wala Hampunji yoyote chochote hata kama ni uzito wa chungu mdogo" [Al baqara: 158] Inatakiwa katika hija watu wajiweke mbali na upuuzi na maovu.

﴿الْحُجُّ أَشْهُرٌ مَعْلُومَاتٌ فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحُجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحُجِّ وَمَا تَفَعَّلُوا مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمُهُ اللَّهُ وَتَزُودُوا فَإِنَّ خَيْرَ الرِّزَادِ التَّقْوَىٰ وَاتَّقُونِ يَا أُولِيَ الْأَلْبَابِ﴾ [البقرة: 197]

"Wakati wa Hija ni miezi ijulikanayo, nayo ni Mfungomosi, Mfungopili na siku kumi za Mfungotatu. Basi mwenye kujilazimisha nafsi yake kuhiji ndani ya miezi hiyo, kwa kutia nia ya kuhirimia

Hija, ni haramu kwake kuundama na vitangulizi vyake vya kimaneno na kivitendo. Pia ni haramu kwake kutoka kwenye twaa ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka kwa kutenda maasia, kubishana, katika Hija, kuletako hasira na chuki. Na wema wowote mnaoufanya, Mwenyezi Mungu Anaujua, na Atamlipa kila mtu kwa amali yake. Na jichukulieni akiba ya chakula na kinwaji kwa safari ya Hija, na akiba ya amali njema kwa nyumba ya Akhera. Hakika akiba iliyo bora zaidi ni kumuogopa Mwenyezi Mungu. Basi niogopeni, enyi wenye akili timamu." [Al Baqara: 197]. Na inakuja aya inayotilia mkazo uwajibu wa Hija kwa mwenye uwezo:

﴿ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا يُبْرَاهِيمَ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ ءَامِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴾ [آل عمران: 97]

Katika Nyumba hii kuna alama waziwazi ya kwamba hiyo ni katika ujenzi wa Ibrāhīm na kwamba Mwenyezi Mungu ameitukua na kuipa heshima. Kati ya alama hizo ni Maqām ya Ibrāhīm, amani imshukie, nayo ni lile jiwe ambalo alikuwa akisimama juu yake wakati alipokuwa akiziinua nguzo za Alkaba, yeye na mwanawe Ismā'il. Na yoyote mwenye kuingia Nyumba hii atapata amani ya nafsi yake, hapana yoyote atakayemkusudia kwa uovu. Na Mwenyezi Mungu Amewajibisha kwa mwenye uwezo katika watu, popote atakapokuwa kuiendea nyumba hii ili kutekeleza matendo ya Hija. Na yoyote mwenye kuikanusha faradhi ya Hija, basi huyo amekufuru. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi naye, Hana haja ya hija yake wala amali yake na wala Hana haja na viumbe vyake vyote. [Al-Imran: 97]. Ili kutilia mkazo chanzo cha kutiwa wepesi nao nikuwa Hija ni kwa mwenye kuweza na si wajibu kwa asiyeweza. Zimekuwa za kipekee siku za Hija kwa majina yake maalumu ambayo yana maana yake, miongoni mwake ni siku ya tarwiya, na siku ya Arafa, na siku ya kuchinja, na siku ya kubanika nyama, na ndio iliyokuja katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَأذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ لِمَنِ اتَّقَىٰ وَآتَقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾ [البقرة: 203]

"Na mtajeni Mwenyezi Mungu kwa kuleta Tasbihi na Takbiri, katika siku chache, nazo ni siku za tashriq: siku ya kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu za mwezi wa Mfungotatu. Atakaye kufanya haraka kuondoka Mina kabla ya kutwa jua la siku ya kumi na mbili, baada ya kurusha vjiwe, hana makosa. Na yule atakaye kuchelewa kwa kulala Mina kungojea mpaka arushe vijiwe siku ya kumi na tatu, pia hana makosa, kwa aliyemcha Mwenyezi Mungu katika Hija yake. Na kuchelewa ni bora zaidi, maana huko ni kujiongezea mapato katika ibada na kufuata kitendo cha Nabii Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Na muogopeni Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu, na mumweke mbele katika amali zenu zote; na mjue kwamba nyinyi kwake Yeye Peke Yake mtakusanywa baada ya kufa kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa." [Al-baqara: 203] Hakika miongoni mwa mambo ambayo umma ulijifunza kutoka kwa Mtume wao sala na amani ziwe juu yake ni kumsikiliza yeye kwa mapenzi ya watu wake kwa ujumla na kuwatanguliza na kuwafanya ni bora, na hasa hasa kiongozi wa waumini Ally bin Abi Twalib-ALLAH mridhiye-wamepokea kutoka kwake Mtume kwa watu wake hayo mapenzi na kumuheshimu kiongozi wa waumini Ally-ALLAH amridhiye-na kwa watoto wake na baki ya watu wake. Na yule ambaye aliye tufundisha mapenzi haya sala na amani ziwe juu yake ndiye ambaye aliye tufundisha Tauheed na siyo sharti kuwapenda watu wa nyumbani Mtume kuvuka mpaka katika kuwapenda ikawatoa kwenye ubinaadamu wao na wakashirikishwa wao kinyume na ALLAH mpaka wakafikia baadhi yao kuwafanya kuwa ni miungu na kuwaabudu na kuwaomba kinyume na ALLAH na wao wanahitaji kwa atakaye waomba, sio kwa atakaye waomba wao baada ya kuwa wamekufa, haitakikani kuwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake aridhiye au

watu wa nyumbani kwake walio wazuri waliyo wasafi kwa jambo hilo.

Na uvukaji mipaka huku siyo kuwapenda isipokuwa ni ushirikina mkubwa anao uridhia shetani na anawaweka mbali kutokuwa watu wa nyumbani kwa Mtume na wala shetani hawaridhii wao, kwa wengi wanao kuwa karibu na watu wa nyumbani kwa Mtume, na jambo hili halifai pamoja na Mtume sala na amani ziwe juu yake wala yeyote miongoni mwa watu wa nyumbani kwake, na ALLAH hakuwachukia wakristo isipokuwa ni kwa sababu ya kuvuka kwao mipaka kwa Issa-amani iwe juu yake-ewe ALLAH tufufue pamoja na wanao kupwekesha na pamoja na watu wa nyumbani kwa Mtume walio wazuri.

Kama unavyo kuja wosi wake Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa watu wa nyumbani kwake hali ya kuwa ni maandalizi ya kukutana na Mola wake, na wala hakubakia Mtume sala na amani ziwe juu yake baada ya hija ya kuaga isipokuwa takriba miezi mitatu, na ikasadikika kauli yake kwa watu. ((chukuweni kutoka kwangu ibada zenu huwenda mimi nisikutane na nyinyi baada ya mwaka wangu huu)).⁵⁵⁵

Hadithi ya Ghadir Khom:

Tukio hili lilitokea kipindi ambacho Mtume alikuwa akirudi kutoka kwenye hija ya kuaga kurudi madinah, waislamu wote wanatambua kuwa Ally bni Abi Twalib-ALLAH amridhie-ni mtoto wa baba yake mkubwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake na ni mkwe wake, na ni mingoni mwa watu wanao pendwa na Mtume zaid na ni katika watu wa karibu yake na anayo Ally daraja mahususi kwakuwa

⁵⁵⁵ Swahihu Bukhariy, kitabu cha Fadhila zamji wa Madina, Hadithi Namba 3654.

ni mume wa fatma na ni mzazi wa Hussein na Hassani wajukuu wa Mtume sala na amani ziwe juu yake,Ally ni wa mwanzo kuingia ndani ya uislamu katika vijana,na nimiongoni mwa walio bashiriwa pepo,kiongozi wa waislamu wanne kati ya makhalifa waongofu-ALLAH amridhie-

Mtume alimtuma kwenda kwenye jambo muhimu sehemu za Yemeni akawa mwema muaminifu mkweli,na huwenda baadhi ya walio kuwa naye walimchukia,kwakuwa hakuwafadhilisha kwa wasiyo kuwa wao,alikuwa muaminifu mkweli muadilifu mwenye usawa,na inavyo fahamika kuwa Ally-ALLAH amridhiye- alifika mji wa makkah kipindi Mtume sala na amani ziwe juu yake akiwa kwenye hija ya kuaga na kabla ya siku ya arafah,na hakika alishughulika Mtume sala na amani ziwe juu yake na wale walio kua naye kwenye hija.

Na alipo kuwa njiani kurudi madinah,na alipo fika sehemu ya maji inayo itwa ghadir khom au kabla ya sehemu hiyo walisema wale walio kuwa wakitembea karibu na Ally katika safari yake ya Yemeni wakimsema vibaya Ally mbele ya Mtume sala na amani ziwe juu yake,katika hadithi aliyo pokea Zaid bni Arqam amesema: ((Ali tusimamia Mtume sala na amani ziwe juu yake,hali ya kutuhutubia kwa maji yanayo itwa Ghadir khom,baina ya Makka na Madina akasema:ama baada ya hayo enye watu hakika mimi ni kiumbe inakaribia kunijia mjumbe wa Mola wangu kisha nimuitikiye Mola wangu,na hakika mimi nimeacha kwenu vizito viwili,cha kwanza ni kitabu cha ALLAH ndani yake kuna uwongofu na mwangaza,basi chukuweni kitabu cha ALLAH na mshikamane nacho,himizeni juu ya kitabu cha ALLAH na muwavutiye watu ndani yake,kisha akasema na watu wa nyumba yangu,nawakumbusha kwa ALLAH kwa watu wa nyumba yangu,nawakumbusha kwa ALLAH kwa watu ya nyumba yangu,nawakumbusha kwa ALLAH kwa watu ya nyumba yangu.

NA hakika hadithi hii imepokelewa kwa matamshi mengine kuwa yeye Mtume sala na amani ziwe juu yake amesema:alichukuwa mkono wa Ally: ((Ambaye nikuwa kwakwe ni kipenzi basi huyu ni kipenzi chake,ewe ALLAH mtawalishe yule atakaye mpenda na mfanyiye uwadui atakaye mfanyia uwadui))⁵⁵⁶

Na hapana mashaka kuwa Ally alifanyiwa udhia kutoka kwa baadhi ya watu wa jeshi ambalo walikuwa nae upande wa Najran,kama alivyo fanyiwa maudhi Mtume sala na amani ziwe juu yake kutoka kwa baadhi ya walio shiriki katika jeshi la vita ya Hunayni.

Na umma mzima umekubaliana juu ya uongozi wa Ally-Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-na kumpenda na kumtetea, na hasa hasa watu wanaofuata mafundisho ya Mtume na muongozo wa masahaba,na wa mwanzo wao ni masahaba wa Mtume-**Rehema na Amani ziwe juu yake**-waliosikia maneno yake walipo kuwa Ghadiri khom na sehemu nyinginezo na wakatambua mapenzi ya Mtume kwa Ally,Mtume akawapendezeshea zaid ya vile walivyo kuwa wakimpenda mwanzo,na yeye Ally anastahili kupendwa,na kama maswahaba wangelisikia kutoka kwa Mtume kitu kingine kinacho fungamana na Ukhalifa na jambo lingine wasinge acha kutekeleza wosia wa Mtume Sala na Amani ziwe juu yake,Hasa hasa kuwa jambo hili siyo jambo lepesi linaloweza kuachwa kutekelezwa,na wala haingii Akilini awe Mtume amesema jambo katika hilo na wingi huu wa maswahaba wasiligundue jambo lenyewe na wao miongoni mwa maswahaba na wala hawakulinukuu walio kuja baada ya

⁵⁵⁶ Ameitoa hadithi hii Imamu Annasai,katika mambo mahususi ya Ally ukurasa wa 21,na angalia utokaji wake kwa Swalah Al-aly ukurasa wa 551,na angalia utoaji wa bni Kathir kwa hadithi katika sirah ya Utume,juzuu 4/425.

maswahaba kisha wadai watu walio kuja baada na walio kuja baada ya maswahaba kuwa wao wanafahamu zaidi maneno ya Mtume sala na Amani ziwe juu yake kuliko maswahaba wenyewe ambao walio sikia kutoka kwa Mtume papo kwa papo na wakashuhudia tukio.

Haiwezekani kuwa umma wa Muhammad sala na amani ziwe juu yake na malezi yake kwa maswahaba kuwe na ubaya kwa yale wanayo yadai hao walio chupa mipaka kwa Ally-ALLAH amridhie-ambao wamefikia baadhi yao kumchupia mipaka mpaka kumfanya kuwa ni Mungu juu ya kumuabudu yeye,yupo mbali ALLAH waache kitu alichu kiamrisha Mtume sala na Amani ziwe juu yake,na sisi tunafahamu kuwa Ally-ALLAH mridhie-hakusema jambo lolote na yeye alikuwa ni miongoni mwa watu mahodari katika zama zake,na wala hawakuwa hao wanao wasema vibaya maswahaba ni mahodari kama Ally,Na wala walikuwa hawana mapenzi makubwa kwa Ally kuliko maswahaba wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake,ewe ALLAH tufufue pamoja na Ally na Abubakar na Omar-ALLAH awaridhie-miongoni mwa maswahaba wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake.

Kulituma jeshi la Osamah bni Zaid:1184

Walikuwa Waroma ndani ya miji ya Sham,na hakika aliandika Mtume wa ALLAH sala na Amani ziwe juu yake kwenda kwa Mfalme wao Hiraql mwaka wa sita toka kuhama kwa Mtume kwa maandishi yake yaliofahamika.⁵⁵⁷

Na ilikuwa vita vya mu'ta ndani ya mwaka wa nane toka Mtume kuhama sehemu za Sham ya kusini,upande wa Urdun,kwa namna walikufa mashahidi idadi kubwa ya maswahaba,miongoni mwao ni

⁵⁵⁷ Angalia:kuandika kwa Mtume kwenda kwa Hiraql,katika kitabu hiki.

Abdullah bni Rawaha na Jafar mtoto wa Abiy Twaalib na Zaid bni Haarithah(alikuwa kiongozi wa jeshi) muachwa huru wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake,⁵⁵⁸ikafuatia baada ya hapo vita vya Tabuk ambayo aliiongoza Mtume Sala na Aman ziwe juu yake karibu na Urdun,namna mipaka ya Waroma ilikuwa imewazingira,isipokuwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake hakutoa vitimbi,⁵⁵⁹namna Mfalme wa Roma aliamrisha kuto ambatana nguvu za waislamu,na huwenda kutosheka kwake ni kwakuwa waislamu walikuwa wametoka kueneza uislamu kwa yale yaliyo kuwa chini ya vikanyagio vyake kutoka sehemu za Sham na sehemu nyinginezo na kuwa hii ni ahadi ya kiungu aliitambua ilipokuwa nyuma ya kujizuia kwake kuto pambana nao.

Na Mtume sala na Amani ziwe juu yake akarejea Madinah baada ya kuwapa ahadi idadi ya viongozi wa sehemu na akaweka wazi nguvu ya waislamu na uwezo wao na kutoka kwao sehemu iliyopo mbele ya Tabuk.

Na baada ya kurejea kwake Mtume sala na Amani ziwe juu yake alishughulika na mambo mengi miongoni mwayo ni Hija ya kuaga,na baada ya kurejea kwake Madinah kutoka kwenye Hija na yakatulia mambo ya waislamu mwanzoni mwa mwaka wa kumi na moja toka kuhama kwa Mtume Aliwasunishia watu kuwapiga Waroma mwishoni mwa mwezi wa Swafari na Mtume akamuaga Osamah bin Haarithah,naye ni mtoto wa shahidi na kiongozi wa jeshi la Muuta Zaid bni haarithah muachwa huru wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake-ALLAH awaridhie-na alikuwa kijana mdogo kwenye miaka kumi

⁵⁵⁸ Angalia Vita vya Mu'ta kutoka katika kitabu hiki.

⁵⁵⁹ Angalia Vita vya Tabuuk kutoka katika kitabu hiki.

na nane na Mtume akamuamrisha⁵⁶⁰akisema: ((Nenda sehemu alipo uliwa baba yako kisha uwasimamishe farasi,hakika nimekutawalishia jeshi hili,na uwende mwendo kama mtu anaye kimbilia habari,na kama ALLAH atakuonesha wao basi ninasema kaeni kwao na chukua watu watakao kujulisha njia,na tanguliza majasusi na wapelelezi))⁵⁶¹

Ilikuwa lengo la jeshi limewekewa mipaka napo ni sehemu ya Takhom Albalqaa kwenye ardhi ya Palestina,⁵⁶²Na malengo yalikuwa wazi nako ni kithibitisha nguvu na kueneza kuzingira,na mpango ulikuwa wazi nao ni haraka ya kupitisha jambo muhimu na wasirefushe muda.

Na hakika Mtume sala na Amani ziwe juu yake alichagua idadi kubwa katika jeshi hili linakadiriwa kufikia idadi ya wapiganaji elfu tatu,⁵⁶³na walikuwa miongoni mwao watu wazima wa kiswahaba mfano Abubakar na Omar-ALLAH awaridhie-⁵⁶⁴

Na baadhi ya maswahaba walishangaa Mtume kumpa uwongozi wa jeshi Osamah bin Zaid,na yeye ni kijana amekulia kwa watu wazima wanao mzidi miaka kuliko hata baba yake walisilimu kabla hata hajazaliwa ,na wao ni watu wenye uwezo wa kuongoza vita na uwelewe,jambo hilo likamfikia Mtume sala na Amani ziwe juu yake

⁵⁶⁰ Ibn Sa'd Atwabaqaat,kitabu cha sirah kutoka kwenye Atwabaqaat.juzuu ya 2/248

⁵⁶¹ Ibn Sa'd,Atwabaqaat,kitabu cha sirah kutoka kwenye Atwabaqaat.juzuu ya 2/190

⁵⁶² Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 2/1056

⁵⁶³ Alwaaqid,Kiatabu cha Almaghazi,juzu ya 3/1120.

⁵⁶⁴ Kwa Bin Abii Shaibah katika Maghaazi, ukurasa wa 376.

akasema: Kama mtakosoa uwongozi wake basi mlikuwa mnakosoa katika uwongozi wa baba yake hapo mwanzo, namuapia ALLAH hakika baba yake alikuwa ni mtu anaye stahili uwongozi, na alikuwa ni miongoni mwa watu walio pendeza kwangu, na hakika huyu Osamah ni miongoni mwa watu wanao pendeza kwangu mimi baada ya baba yake))⁵⁶⁵

Na Mtume akaanda bendera ya Osamah kwa mikono yake na akampatia na akamuelekeza kwa maelekezo na Osamah akaweka kambi ya jeshi lake sehemu ya Jaraf kaskazin mwa mji wa Madinah kwa kusubiri amri ya Mtume sala na Amani ziwe juu yake kwa ajili ya kuondoka, isipokuwa maradhi ya Mtume sala na Amani ziwe juu yake yalizuia kuondoka jeshi, namna ambayo Osamah aliendelea kuweka kambi ya jeshi lake katikati ya maradhi na baada ya kufa Mtume sala na Amani ziwe juu yake walishirikiana kumswalia mtume, na wakarudi kwenye kambi zao kusubiria amri ya Abubakar Aswidiq ambayo aliidhinisha, kama jinsi alivyo iandaa na akausia kwa jambo hilo Mtume sala na Amani ziwe juu yake (tekelezeni jeahi la Osamah) 1194 Kisha ikawa kuondoka kwa jeshi la Osamah na owongozi wake ni kwa umuhimu wa Mtume hali ya kuwa ni baraka kubwa juu ya uislamu na nchi yake ambayo waliyo kuwa wakii subiria maadui baada ya kufa kwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake, ikawa kuondoka kwa jeshi ni jambo lenye kuwaogopesha maadui walio kuwa wakisubiri, ambao walirudi kwa ajili ya walio hifadhi juu ya sehemu zao badala ya kufikiria kuiteka Madinah, kama jinsi walivyo thibitisha Waroma kuendelea waislamu kwenda

⁵⁶⁵ amepokea Imamu Bukhar katika sahihi yake (mlango wa Mtume kumtuma Osamah bin Zaid katika maradhi yake aliyo fia) Hadithi namba 4468, na mapokezi ya bin abiy Shaybah, kitabu Almaghazi ukurasa 376.

kutekeleza mpango wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake ambao aliuwanza yeye mwenyewe kwa lengo la kueneza Uislamu ndani ya miji ya Sham na sehemu zingine,sehem ambazo zilikuwa zipo chini ya uwangalizi wa Waroma,na kuwa kifo cha Mtume sala na Amani ziwe juu yake haikuzuia malengo ya Uislamu,namna alivyo weka Mtume Sala Amani ziwe juu yake mpango wake kwa ajili ya kusambaza mwanga sehemu za Sham na jirani zake baada ya kufa kwake Mtume sala na Amani ziwe juu yake.

Alikuwa Osamah na wale aliyo kuwa nao ni muendelezo wa baba yake(Zaid Ibn harithah)na wale aliyo kuwa nao miongoni mwa walio beba ulinganizi wa Laa Ilaha Ila ALLAH.

Kama jinsi Osamah alivyo bainisha kubakia kwa Abubakar baada ya kutawala ukhalifa kwa kuwatangazia wote kwa lengo la kuondosha ubaguzi,na kwenda kwa kupita njia ya Mtume sala na Amani ziwe juu yake katika kuchunga maslahi ya umma na kujiweka mbali na ubaguzi,na kuwa uwongozi ni kwa yule aliye kuwa bora kwa umma,na siyo kwa wenye hesabu na ukoo basi au kwa ukubwa wa miaka,na ndani yake vile vile kulikuwa na tangazo la wazi kwa kumpenda Mtume wa ALLAH kwa Osamah Ibn Zaid na mzazi wake kabla yake,ALLAH awaridhie.

Kusimamisha Nchi ya Kiislamu.

Ilikuwa ni jambo lipo wazi toka kutumwa kwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake kuwa yeye anakwenda haraka kueneza upwekeshaji wa uwabudiwa kwa ajili ya ALLAH-aliye mtukufu-na kusimamisha Nchi ya Kiislamu yenye upole na katiba yenye uwadilifu ikitekelezwa ndani yake sharia za ALLAH juu ya viumbe wake,na sharia yote ni huruma na uwadilifu.

Na toka masiku ya mwanzo ya ulinganizi wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake ndani ya mji wa Makkah alikuwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake akiwapa bishara swahaba zake kwa kuenea Uislamu katika kila sehemu na kupata kwake ushindi juu ya ushirikina na kanuni zake zilizo tofauti.

Na ulikuwa mji wa Makkah na jirani ya mji wa Makkah ndiko ambako kulianza ujumbe wa Uislamu,umekosa utaratibu umesimama juu ya mila na desturi ambazo zilikuwa kawaida yake ni dhulma na ujeuri,na hakuna ndani yake sharia yenye mipaka wala desturi yenye asili wala hukumu zenye usawa,wala sharia zinazo fahamika,na ilikuwa kukiongezeka baina yao kufanya madhabi yenye kuangamiza kama vile uzinifu na pombe,kula riba,kuuwa watoto wakike,kumdharau mwanamke,na kisha baada ya hapo hakika mji wa Makkah na miji ya pembeni yake kwa ule ujinga walio kuwa nao uliwapelekea kuzuia kuenea Uislamu kwa yale yanayo pelekea kutokana na desturi na uwadilifu na usawa na la mwanzo wake ni kumpwekesha ALLAH.

Na Uislamu kama tunavyo tambua umekuja kwa sharia zake katika wakati tofauti tofauti,isipokuwa misingi yake ipo wazi toka mwanzo,nayo ni kuhifadhi haki za ALLAH na haki za viumbe wake,na kuwa nahuruma na uwadilifu na usawa baina ya watu,na kufanya wema kwenye kila kitu,pamoja na siasa za ndani na njee kwenye

jamii hii ni kuchunga haki na uwadilifu na huu ndiyo jambo muhimu na misingi kwenye jamii yeyote ile yenye lengo la maendeleo.

Na pindi jambo lilipokuwa na ugumu kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake katika kubadilisha mji wa Makkah kuwa ni jamii na Nchi ya kiislamu alianza kwa kutafuta kwenye kila sehemu na Makabila mengine ambayo yataweza kumsaidia, kwenye sehemu husika na watu watakao fungamana kwenye Nchi ya Kiislamu, wataishi waislamu ndani yake kwenye jamii yenye utu wa kiislamu ulio salimika wenye kusaidiana, walio jengeka kuwa ni umma unao shinda nyumati zingine na utashikamana kwa ALLAH na sharia zake ili iweze kuwaongoza viumbe kwenye utukufu na ukamilifu na kuwa sawa wenyewe, na watu wa dini zingine miongoni mwa watakao tafuta maisha yenye utukufu.

Kwa ajili hiyo alianza Mtume saa na Amani ziwe juu yake akijitambulisha yeye mwenyewe kwenye makabila kipindi cha Hija na vipindi vingine kutokana na misimu ya Waarabu na masoko yao hali ya kuwa akitafuta atakaye msaidia na kumnusuru ili aweze kusimamisha jamii isiyo tofautiana ndani yake baina ya Waarabu na wasio kuwa Waarabu akiweza juu ya kupangilia yeye mwenyewe na kuzuia kuwa kwake mbele ya maadui walio tofautiana, hali ya kuhifadhi uwadilifu na Imani.

Na kwa msaada wa mlezi (ALLAH) Mtume wa ALLAH alipata watakao mpa nguvu kwa Maaswar wa mji wa Madinah, ambao walimkubali katika msimu wa Hija na wakamsikiliza Mtume na wakamkubali na wakajiandaa kuufanya Mji wao kuwa ni kiongozi wa Nchi ya Mtume sala na amani ziwe juu yake walio shikamana na wakiwa ni jamii iliyo salimika walio Waislamu, na watu wake ni wanajeshi wenye kupata nusra kwa nafsi na mali kwa ajili ya Dini hii na yale yanayo takikana kutokamana na desturi.

Anasema Muhammad Humayd Ilah ndani ya kitabu chake "Al'wathaiqu Alsiaasiyyah lil'ahad Al'nabawiyah walkhilaafat

Alraashidah" (Hakika Siasa za kihukumu zama za Mtume-juu ya jamaa yake iwe Amani-likuwa imewekewa misingi yake kabla ya kuhamia Madinah kwenye kiapo kilicho fanyika kwenye kizingiti cha mwanzo na cha pili)1195 Na ikatimia kufanyia kazi kwa hatua za kiutendaji baada ya kuhama,mpaka kutimia kuijenga Nchi.

Na hakika vitabu vimetungwa na pekuzi mbalimbali zimefanyika kunako kusimama kwa Nchi ya Mtume sala na Amani ziwe juu yake na mpangilio wake na watumishe wake na wasimamizi wake,na huwenda yaliyo wazi ni yale aliyo andika Alkhuzaiyu katika utoaji wa dalili za kusikika,⁵⁶⁶ ambako kumewekewa ufafanuzi upande wa Shekh Abdul Hayyi Alkatany ndani ya kitabu chake "Nidhwamu Alhukuumat Al-Nabawiyat" Kinacho itwa "Atritiibu Al-idaariyat" na hivyo hivyo aliyo andika Auni Asharifu Qasim ndani ya kitabu chake "Nashiatu Adaulat Al-islamiyat" na hakika alisema Alkatany ndani ya utangulizi wa kitabu "Upangiliaji wa Kiidara. (Na alikuwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake akishughulika na cheo cha Utume wa Kidini juu ya kuongoza dini zote za sawa baina ya Siasa za Kidinii na Dunia kwa pamoja kwa kuchanganya baina ya vyeo viwili, kwa namna ya vilikaribia kuingiza chini ya Uitwaji mmoja nao ni Dini na hivyo hivyo ndivyo ilitokea, zilikuwa Idara zenye kulazimikiana kwenye Siasa mbili juu ya zama zake kuwa ni kituo cha utawala wake wenye kuzingira na watumishi kwa utimilifu wa utendaji kazi wao kufikia daraja za juu, na matendo yakawa ni yenye kwenda)⁵⁶⁷

⁵⁶⁶ Alkhuzay, Abul Hasan Ally Ibn Muhammad Altilimisaniy (alifishwa: 741 H) Utokaji wa dalili za kisharia juu ya yale yaliyo kuwa zama za Mtume sala na Amani ziwe juu yake Alhirafu waswiyaanat wal-amaliyat Ashariiyat, amehakiki Ahmad Muhammad Abu Salamah, Baraza kuu la mambo ya kiislamu, Cairo. 1401 H.

⁵⁶⁷ Al-kattaniy Kwenye kitabu "Atartiibu Al-idariyat, juzu 1/9.

Hakika ilitimia upangiliaji wa Mtume kunako mambo ya kiidara na wafanya kazi wa umma,na upangaji wa Nchi na yale yaliyo bebwa kutokana na mifano ndani ya mwenendo na njia ya Mtume kuwa ndiyo Misingi waliyo pangilia kwa misingi hiyo watunzi na wanazuoni wa kifiqh ndani ya vitabu vya hukumu za kiutawala,kwa yale waliyo ambatanisha kwayo katika kuonesha mpangilio wa Kiislamu na idara za kinchi kwa vipengele tofauti,sawa sawa miongoni mwazo ni idara za kisiasa,au za kimali,au za kijeshi,au za kijamii au nyinginezo.

Hakika imekuwa baina ya ule upangiliaji na uwekaji wa sheria na baina ya matokeo ya kihistoria yanaendana na yanafungamana yametufanya tufahamu upambanuzi wa ndani kwa yale aliyo yatekeleza Mtume sala na Amani ziwe juu yake kwa ajili ya kujenga Nchi ya Kiislamu na jamii yake nakuifanya kuwa Nchi ya kwanza na desturi za kisiasa ndani ya Uislamu zilikuwa ni sifa kwa yale yalikuja baada yake kutokana na Katiba na Nchi tofauti na kutofautiana kwa yale waliyo kuwa nayo kwa kuchukuwa kutoka kwenye mafundisho ya Mtume sala na amani ziwe juu yake kwenye upande huu.

Hakika ilikuwa dhulma inatokea juu ya maswahaba wa Mtume sala na Amani ziwe juu yake wakiwa Makkah,Mtume akiwapa bishara kuwa itafika siku itazuiliwa dhulma ndani ya mji wa Makkah na kutasimamishwa uwadilifu na siyo Makkah peke yake,isipokuwa katika sehemu nyingi wanazo zifahamu,na pindi alipo peleka mashitaka Khabab Ibn Arat kwa yale aliyo kuwa akikutana nayo kutokana na Udhia,na akaomba kutoka kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake amuombe kwa aliye mdhulumu,Mtume akamwambia: Na Mwenyezi Mungu atatimiza jambo la Dini hii mpaka msafiri atatembea kutoka Swanaa mpaka Hadhara Mauti bila ya kuogopa chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu, ila atawaogopea kondoo wake kutokana na mbwa mwitu.

Na yalikuwa yale aliyo Ahidi ALLAH na Mtume wake kupata nusra Uislamu na kutawala Waislamu katika Ardhi na kuimarika wao, anakusudia Amani yao, na tena kusimama kwa upangikaji na utaratibu unahakikika ndani ya utulivu, inakusanya baina ya kuwekewa sharia na kuifanyia kazi katika matokeo ndani ya siasa za kidunia na dini, na Ahadi hii ilikuwa wazi ndani kauli ya ALLAH Mtukufu.

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾ [النور: 55]

Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini miongoni mwenu na wakafanya matendo mema kwamba atawarithisha ardhi ya washirikina na atawafanya ni wasimamizi wa hiyo ardhi, kama alivyofanya kwa waliokuja kabla yao kati ya wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, na Aifanye Dini yao ambayo Ameridhika nayo na Akawachagulia, nayo ni Uislamu, ni Dini yenye ushindi na uthabiti, na Azigeuze hali zao kwa kuwaondolea kicho na kuwaletea amani, iwapo watamuabudu Mwenyezi Mungu, Peke Yake, na watasimama imara kwa kumtii, na wasimshirikisha na kitu chochote. Na Mwenye kukanusha baada ya hilo la kupewa usimamizi, amani, uthabiti na utawala kamili, na akakanusha neema za Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waliotoka nje ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu. Al- Nuur:55 Hakika kutawala kwenye Ardhi inakusudia kusimamisha hukumu na kuipangilia na kupangialia siasa zake na kuziendesha. Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَنُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضِعُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ﴾ [القصص: 5]

Na tunataka tuwaneemeshe wale ambao walio tenzwa nguvu katika ardhi na tuwajalie kuwa ni viongozi na tuwajalie kuwa ndio wenye kurithi. Al-qaswas:5 Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ﴾ [الأنبياء:

[105

Nakika tumeandika ndani ya zabur baada ya ukumbusho kuwa kuwa ardhi watairithi waja wangu walio wema. Suratil Anbiyaa:(105), Na hakika ilikuwa wazi kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake kuwa katiba ya Uislamu za kisiasa ambao alio anzisha Mtume itabakia kuwa ni katiba za kidunia za hivi sasa,kama vile katiba za wafalme wa Fursi,na katiba za wafalme wa Roma,Basi amepokea Jaabir Ibn Samurah kuwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake amesema: Hakika mtafungua ardhi ya kisra na kikundi miongoni mwa Waislamu,⁵⁶⁸ Na wakati wa kuchimba mahandaki kabla ya vita vya Makundi mwaka wa tano toka kuhama Mtume ilionekana jiwe kubwa kwa baadhi ya maswahaba Mtume akasimama ili aweze kulipasua,na pindi alipo lipiga likatoa cheche Mtume akasema>Allahu Akbar"kisha maswahaba nao kasema>Allahu Akbar" pamoja naye,kisha akalipiga kwa mara ya tatu,akasema>Allahu Akbar" na wakasema maswahaba>Allahu Akbar"pamoja naye,na hakika alisema Mtume sala na Amani ziwe juu yake baada ya pigo la kwanza: ALLAH mkubwa nimepewa ufunguo wa Sham,namuapia ALLAH hakika mimi ninaona Miji ya Sham yenye rangi nyekundu muda huu,kisha akapiga pigo la pili kisha akasema:ALLAH mkubwa nimepewa ufunguo wa Fursi,namuapia ALLAH hakika mimi ninayaona majumba ya kifalme ya Madyan yenye rangi nyeupe,kisha akapiga pigo la

⁵⁶⁸ Tazama Bin Is-haqa ,Al-siirat Al-Nabawiyat ukurasa wa 271.

tatu,akasema:ALLAH mkubwa namuapia ALLAH nimepewa Funguo za Yemen,hakika mimi ninaona milango ya swanaa sehemu yangu hii muda huu.⁵⁶⁹

Na alikuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akiwalea maswahaba zake kwa lengo la kuusambaza uislamu na Dola yake kwenye sehemu mbalimbali hapa Duniani,na kuwa waislamu watazikomboa sehemu hizo,ili kuwaelekeza watu kwenye kumuabudu Mwenyezi mungu-Kutakasika na machafu ni kwake na mtukufu-watazikomboa kwa Nidhamu ya muasisi wa kidini na kiidara na kisiasa ambaye watu wa kawaida walimjuwa na watu maalumu miongoni mwa waislamu pia walimjuwa,na ndiyo maana tunamkuta Rib-iiyu Bin Aamir anaongelea lengo hili tukufu lenye msukumo wa kusimamisha Nidhamu iliyogubikwa na uadilifu baina ya watu,alimwambia Rustum akiwa anajadiliana nae kabla kidogo ya vita vya Qaadisiyyat: ((Kwa hakika Mwenyezi Mungu ametutuma ili tumtoe amtakaye miongoni mwa waja wake kwenye kuwaabudu wanadamu na kuelekea kwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu,na kuwatowa kwenye Dhiki ya Dunia na kuwaelekeza kwenye Faraja ,na kuwatowa kwenye Dhulma za Dini Mbali mbali na kuwapeleka kwenye uadilifu wa Uislamu...))(1201)

Na kwa hakika alifanya bidii Mtume wa Mwenyezi mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kuanzia mwanzo wa Daawa yake ya mwanzo mpaka kusimama Nidhamu ya kiuanadamu akiwaongoza watu kwa uadilifu na usawa,kwa hakika kusimama kwa Dola ya

⁵⁶⁹ Ameipokea Ahmad katika Musnad wake juzuu ya 4/303 na Maulamaa wengi wakaifanya kuwa ipo kwenye Daraja la Hasan,miongoni mwa hao maulamaa ni Bin Hajar Tazama kitabu kiiwaco Al-siirata Nabawiyyat Swahihat kilichotungwa na Doctor Ak-rim Dhiyaaul Omariy juzuu ya 2/423.

Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- ilikuwa ni kwa hatua baada ya hatua;ilianza pamoja na ulinganiaji na utume,na ikathibitika baada ya kuhama mtume,na ikakuwa na kupiga hatua ya kimaendeleo baada ya kuukomboa mji wa Makkah mpaka Dola ya Mtume ikawa ni yenye kuenea katika pande zote za Kisiwa cha Waarabu,na Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akashughulika na cheo cha uongozi wa juu katika Dola ya kiislamu pamoja na kuwa na utukufu wa utume na ufikishaji ujumbe wakati mmoja,na amewaandaa maswahaba wake baada yake ili kuupangilia Ulimwengu wote na kusimamaisha Tauhiid na Uadilifu.

Na kwa hakika mtume aliyadhibiti Mambo ya Dola kwa kuweka Nidhamu na vyeo na kazi mbalimbali na Nyadhifa ambazo kupitia hivyo vyeo nyadhifa ilisimama Dola yake na ikawa hali yake ni yenye kufurahisha ,na zikapangika nguvu zake za kibinadamu na kimali na kijamii na kiusalama na mambo yake yote ya Ndani na nje.(1202)

Na idara hii yenye kufanya kazi nzuri ilikuwa ni sehemu katika Dini ya uislamu ambao mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-aliyoibeba mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kwa kuwahurumia wanadamu,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾ [الأنبياء: 107]

Na hatujakutuma isipokuwa ni rahma kwa watu wote [Al Anbiyaai: 107]. Pale ambapo Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alikusanya baina ya Dini na Dunia kwa namna ambayo iliwashituwa waislamu na wengine.

Anasema Michael H.Hart ndani ya kitabu chakr "miongoni mwa watu Mia moja walio watukufu katika Historia ya wanaadamu"(Kwa hakika umoja huu wa kipekee ambao hauna mfano wake kwa kuathirika kidini na kidunia pamoja ni miongoni mwa mambo yanayompa haki Muhammad azingatiwe kuwa mtukufu wa kipekee mwenye ushawishi katika Historia ya wanadamu)(1203)

Upangiliaji Dola ya Kiislamu na Tawala zake:

Ilikuwa Miji ya Kiarabu na Haswa Hijaaz na Najdi,iko Mbali sana na Nidhamu ya Kisiasa na Kiidara,zikiwa chini ya uongozi wa mila na kikabila ambayo ilikuwa ikijiendesha yenyewe bila utaratibu,pasina kufuata Siasa na Dola fulani kwa kawaida,wala hapakuwa kwenye mji wa Makkah uongozi wenye kusikika wala Idara iliyokuwa na majukumu,na wala Madina hapakuwa cha namna hiyo,pale ambapo paligubikwa na nidhamu ya ukabila mazoea yake,liche ya kuwa wao ni wakazi wa Mjini lakini hawakuwa na Mpangilio idara maalumu,mpaka ikawa chini ya Hukumu ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**

Na kwa hakika ilikuwa idara yenye kutoa Hukumu na mpangilio wake ni moja ya alama zilizojitokeza waziwazi ambazo zilikuja katika Qur'an tukufu,anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُمْ بِهِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ فَإِنْ تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿58-59﴾

Na kwa hakika Mwenyezi Mungu Anawaamrisha nyinyi kutekeleza aina zote za amana mlizoaminiwa nazo kwa wenyewe,Na muhukumu baina ya watu kwa uadilifu, mtakapohukumu baina yao.Hilo ni jambo bora zaidi Analowaidhia Mwenyezi Mungu na kuwaongoza mlifanye. Hakika Mweyezi Mungu Aliyetukuka ni Msikizi wa maneno yenu, Anayajua matendo yenu na Anayaona. Enyi ambao mliyo amini mkubalini ALLAH na mumkubali mtume na wale wenye mamlaka miongoni mwenu na kama mtatatizana kwenye jambo basi lirejesheni kwa ALLAH na mtume ikiwa nyinyi mnamuamini ALLAH na siku ya

mwisho kufanya hivyo ndio bora na makimbilio mazuri. Al- Nisaa 58-59. Na anasema ALLAH mtukufu:

﴿لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ وَأَنْزَلْنَا
الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَن يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ
عَزِيزٌ﴾ [الحديد: 25]

Hakika tumetumiliza Mitume wetu kwa hoja zilizo wazi na kuwateremshia Vitabu vyenye hukumu na sheria, na tukateremsha mizani ili watu waamiliane baina yao kwa uadilifu, na tukateremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa mengi kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu Amjue, ujuzi wenye kujitokeza kwa watu, yule anayetetea Dini Yake na Mitume Wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Asiyetendeshwa nguvu, ni Mshindi hakuna anayeweza kushindana na Yeye. [Al Hadid: 25].

Alikuwa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- ni kingozi wa Dola na akawateuwa watumishi na wafanyakazi.(1204)na alikuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akipupia uongozi na kupangilia majukumu.na tangia Ungaji mkono wa Aqabah ya kwanza alipangilia mtume waungaji mkono na akawataka wamtotele viongozi watokao kwao ambao watakuwa ndiyo wahusika wakuwasimamia wengine ili wapokee Amri na maelekezo na ufuatiliaji na utekelezaji wa kila linalomuhusu.(1205)

Na Uungaji mkono ulikuwa ni wa wanaume na wanawake ni wenye maana maalumu(1206)imepokelewa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعْنَكَ عَلَىٰ أَنْ لَا يُشْرِكْنَ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقْنَ وَلَا يَزْنِينَ وَلَا يَقْتُلْنَ أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ وَأَرْجُلِهِنَّ وَلَا يَعْصِينَكَ فِي مَعْرُوفٍ فَبَايِعْنَهُنَّ وَأَسْتَغْفِرْ لَهُنَّ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [الممتحنة: 12]

Ewe Nabii! Wakiwajia nyinyi wanawake wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na kuwaahidi kuwa hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu katika kumuabudu, wala hawataiba chochote, wala hawatazini, wala hawataua watoto wao baada ya kuzaliwa au kabla yake, wala hawatawanasibishia waume zao watoto wasiotokana na wao, wala hawataenda kinyume na wewe katika jema unalowaamrisha kwalo, basi waahidi kwa hayo na uwaombe msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe sana dhambi za waja Wake wenye kutubia na ni Mwenye kuwarehemu. Al-Mumtahinat:12

Na yalikuwa maamrisha ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- yapo wazi katika upangiliaji wa majukumu katika mkusanyiko wowote sawa uwe mkubwa au mdogo na kwa hakika alisema-**Rehema na amani ziwe juu yake**:- ((Haifai kwa watu watatu waliopo safarini kuwapo wenyewe bila ya kiongozi,bali atawaongoza mmoja wao))(1207)

Na alikuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akiendesha mambo ya Nchi kijeshi na Kiraia ,hivyo alikuwa akituma majeshi vikosi,na hupagilia viongozi wake,bali alikuwa akiweka akichukuwa tahadhari mpaka asiweze kuhisi kuwa ndani yake kuna cheo cha uongozi,na katika Vita Mu'utah,alimwachia mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-Jeshi la Mu'uta liongozwe na Zaid Bin Haaritha na akasema: ((Na ikiwa atauwawa Jaafar Bin Abii Twaalib,basi atafuata Abdullahi Bin Rawaaha,basi ikiwa atauwawa,basi waislamu wamchague mtu watakao mridhia))(1208)

Na kwa hakika ilikuwa upangiliaji na utaratibu wa uongozi na usikivu na utiifu ni katika malezi aliyowalea Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- huu Umma

Na kwa hakika Mji Mji wa madinah ulikuwa ni Mji mkuu wa Dola ya kiislamu,na alikuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-ndiye Hakimu na Mtendaji wa mji wa madinah yenye Nuru,na mwenye kutilia umuhimu uendeshaji wa mambo ya mji huo,kama ambavyo alikuwa Mtume mwenye kumwachia Mji wa Madinah yule aliyemchaguwa miongoni mwa maswahaba wake wakati atakapo kuwa hayupo Madina,na kwa hakika wametaja watu wa Historia katika kila Vita,walitaja mtu ambaye Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- alimwachia Mji wa Madinah.

Na miongoni mwa watu ambao mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-aliwaachia mji wa Madina wakati alipokuwa hayupo:Abdullahi Bin Umami Maktuum,(1209)pale ambapo ilitajwa kuwa alimwachia mji Takriba siku kumi na tatu,(1210) miongoni mwa vita ambazo aliwaachia watu mji wa Madina Vita Vya Badri,(1211) na Miongoni mwa ni vita vya Hamraul Asad na Vita vinginevyo,(1212)kama ambavyo alimuachia Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-Othman bin Affan Mji wa Madina wenye Nuru katika baadhi ya vita vyake (1213)

Na Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alimwachia mji wa Madina Kiongozi wa Waislamu Ally Bin Abii Twaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake- katika Vita vya Tabuk,na Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake- aliposita kuhusu jambo hilo,Mtume--**Rehema na amani ziwe juu yake**- alimwambia: ((Hivi Hauridhii kuwa wewe kwangu mimi katika nafasi aliyekuwa nayo Haruna kwa Mussa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu))(1214) Na kwa ujumla Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alikuwa akipupia siku zote kubakia mtu atakayekuwa badala yake katika kuendesha mambo ya watu wa Madina,hata kama muda wa kukosekana kwake utakuwa ni muda mfupi,na hili

linatupa ushahidi wa wazi juu Mtume kutilia Umuhimu upande huu wa Kiidara na upangiliaji katika Serekali ya kiutume.

Na kipindi ilipotanuka Dola ya Kiislamu katika zama zake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na mpaka ikavuka mipaka ya mji wa madinah wenye Nuru, akaanza Mtume kutuma watumishi miongoni mwa watawala na maqadhi na wengineo sehemu mbalimbali kwenye wilaya na vitongoji, bali vilevile alituma kwenye makabila ,kwa ajili ya mambo mengi na kwa muda maalumu, na akawawekea muda Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na kwa ujumla ni ilikuwa ni Udhibiti wa jumla, na kwa hakika ilikuwa kuna utofauti kati ya mji na mji na tofauti kati ya wilaya na wilaya.

Uadilifu na Usawa:

Uadilifi ni msingi wa Kiislamu na kiuanadamu ulio Muhimu, unayahukumu mambo ya waislamu katika kila hali zake kwa ujumla na maalumu, na hasa hasa ikiwa ikiwa jambo linawahusu watu wengine pindi wanapokuwa wanasimamia jambo linalohusu watu wengine na ni Fadhila ya hali ya juu hufikiwa pale kwenye kuitekeleza Nidhamu hiyo katika kila Zama na kila mahala, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ
يَعْظُمُ عَلَيْكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴾ [النحل: 90]

Hakika ALLAH anakuamrisheni kufanya uwadilifu na wema na kuwapa ndugu wa karibu na anawakataza kunako uchafu na vitu vyenye kuchukiza na ujeuri, ALLAH anakukatazeni ili muweze kukumbuka. [An Nahli: 90]. Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا
بِالْعَدْلِ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُمْ بِهِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴾ [النساء: 58]

Hakika ALLAH ana kuamrisheni mtekeleze amana kwa wenyewe na mnapo hukumu baina ya watu basi muhukumu kwa uwadilifu,hakika haya anayo kuwaidhini ALLAH ni mzuri sana,hakika ALLAH amekuwa mwenye kusikia mwenye kuona. [An Nisaai: 58]. Na amesema Allah Mtukufu:

﴿فَلِذَلِكَ فَادَّعِ وَأَسْتَقِمْ كَمَا أُمِرْتَ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَقُلْ ءَامَنْتُ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ كِتَابٍ وَأُمِرْتُ لِأَعْدِلَ بَيْنَكُمْ اللَّهُ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ لَنَا أَعْمَلْنَا وَلَكُمْ أَعْمَلْنَا لَا حُجَّةَ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ اللَّهُ يَجْمَعُ بَيْنَنَا وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ﴾ [الشورى: 15]

Kwa ajili hiyo omba na uwe na msimamo na wala usifuate matamano yao,na useme nimeamini kwa yale aliyo teremsha ALLAH kutokana na kitabu,na nimeamrisha nifanye uwadilifu baina yetu,ALLAH ndiye mola wetu,sisi tuna matendo yetu na nyinyi mnayo matendo yenu,hatuna hoja baina yetu na baina yenu,ALLAH ndiye atakaye tukusanya baina yetu na kwake ndio marejeo. Al- Shuurat:15 Kama amabvyo Qur'an ilivyotilia mkazo kwenye kutahadharisha Dhulma,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفِيلاً عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ﴾
 مُهْطِعِينَ مُقْنَعِي رُءُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ وَأَفْعَدْتُهُمْ هَوَاءَهُمْ ۗ وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ
 الْعَذَابُ فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا أَخِّرْنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ نُجِبِ دَعْوَتَكَ وَتَتَّبِعِ الرَّسُولَ ۗ أَوْ لَمْ
 تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِّن قَبْلِ مَا لَكُم مِّن زَوَالٍ ۗ﴾ [ابراهيم: 44-42]

Basi msimdhaniye ALLAH ni mwenye kughafilika kwa yale wafanyao watu waovu,hakika ALLAH anawachelewesha kwa siku ambayo macho yatakodoka. Na wako mbioni vichwa chini,na macho hayapepesi na nyoyo zao tupu. Waonye watu siku watakayo jiliwa na adhabu kisha waseme wale ambao walio jidhulumu ewe Mola wetu tusubirisha mpaka siku iliyo karibu

tujibu wito wako na tuwafuate mitume,hivi hamkuwa ni wenye kuapia hapo mwanzo hamna nyie wa kuwaondolea(adhabu) Ibrahiim 42-44). Na Uadilifu ni wenye kuhitajiaka kwa wote hata kwa Maadui,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوِّمِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلَىٰ ءَلَا تَعْدِلُوا ءَعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ﴾ [المائدة: 8]

Enyi mliyo amini kuweni wasimamizi kwa ajili ya ALLAH hali ya kuwa ni mashahidi kwa uwadilifu,na usikuzuiyeni mambo ya watu kuto tenda uwadilifu.fanyeni uwadilifu ndio karibu zaidi ya uchamungu,na muogopeni ALLAH,hakika ALLAH ni mwenye kueleza kwa yale mnayo yafanya. [Al Maaida: 8].

Na hapana shaka kuwa uadilifu siyo tu kwenye kuhukumu,bali ni Uadilifu ni maelekezo ya Ujumla kwa kila waislamu,nao ni mpango kazi wa kiidara,pale ambapo muhusika wa Idara fulani anapaswa kuwa Muadilifu pamoja na watumishi wake na awe na uadilifu na wenye mahusiano kazini,na watu wenye maslahi yanayoambatana na kazi yake,na Uadilifu ni wenye kutakikana kwa kila mwanadamu mpaka kwenye uendeshaji wa Familia yake na kazi yake binafsi,basi vipi ikiwa ni mwenye cheo na kazi ikawa ni yenye mahusiano na watu wote au baadhi

Na pindi alipodai mmoja wa wajinga kuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-hakufanya uadilifu kwenye kugawa Mali za Hunain,alikasirika Mtume wa Mwenyezi Mungu kutokana na tuhuma hii nzito lkawa mtazamo wake,na kumtuhumu kwake kutokuwa na uadilifu,naeye Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-ni katika watu waadilifu zaidi na Mwema kuliko yeyote miongoni mwao,na ni mfano wa kuigwa kwa watumishi wote kwenye kusimamaia mambo ya watuna haki za waja ,na wala hakubali Dhulma kwa yeyote basi vipi awe nimwenye kuidhulumu nafsi yake mwenyezi Mungu Mtukufu amweke mbali na hilo

Na alikuwa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akijihadhari na Dhulma na miongoni mwa kujihadhari ni pale kwenye kauli yake aliposema: Ogopeni dhulma; kwa hakika dhulma ni giza siku ya kiyama. Na ogopeni ubahili; kwa hakika ubahili umewaangamiza walio kuwepo kabla yenu. umewapelekea kumwaga damu zao, na kuhlalisha yaliyo haramu kwao

Kama ambavyo alikuwa akiamrisha kuufanyia kazi uadilifu na kusimamisha hukumu kwa mtu Dhaifu na Mwenye Nguvu,na alikuwa akitahadharisha kupuuzia jambo hilo kwa maneno yake aliposema: ((Kwa hakika waliangamia waliokuwapo kabla yaenu,hakika wao walikuwa akiiba mtu miongoni mwao kama ni kabila tukufu wanamuacha,na akaiiba mtu Dhaifu miongoni mwao wanamuhukumu,na ninamuapia Mwenyezi Mungu kama Fatma Bint Muhammad angeliiba ningemkata mkono wake))(1210)

Na alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akisimamia hukumu yeye mwenyewe kwenye kuwahukumu watu(1217)akijitahidi kufanya uadilifu na akiogopea kuwafichia wagomvi wao kwa wao,na alikuwa akitahadharisha kuzifanyia uadui haki za wengine hata kama ni kwa hukumu ya kisheria ya Qadhi,na hivyo imepokelewa kuwa yeye mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- ((Siku moja alisikia ugomvi mbele ya mlango wa chumba chake ,basi akawatokeana akasema:kwa hakika mimi ni mwanadamu,na kwa hakika kuna wakati hunijia waliogombana na huenda baadhi yenu wanakuwa ni fasaha kuliko wenzao basi nikadhania kwa ufasaha huo kuwa ni mkweli basi nikampa haki ya Muislamu,na kwa hakika si vinginevyo hiyo haki niliyompa ni kipande cha moto basi aangalie akichukuwe kipande hicho au akiwache))(1218)

Na kwa hakika alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akiwahukumu watu wote na akitenda haki kwa wanaostahili sawa wawe waislamu au makafiri,alikuwa akiweka wazi

misingi ya Tabia njema kwa mahakimu na walioshtakiyana,na akaitahadharisha kuepukana na uwongo kwenye mashtaka,au viapo ambavyo vitapelekea kuchukuwa haki za watu zisizokuwa zake,na kwa hakika imepokewa kutoka kwa Abdullah Bin Masoud -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema ,amesema Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** ((Yeyeto atakae apia na hali yakuwa anajuwa kuwa yeye ni muovu,ili achukuwe mali ya muislamu,atakutana na Mwenyezi Mungu akiwa mwenyezi mungu Amemkasirikia))(1219) Na katika hili lliteremka neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُولَٰئِكَ لَا خَلَاقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾ [آل عمران: 77]

Hakika wale ambao wanao uza ahadi za ALLAHa na viapo vyao kwa thamani ndogo hao hawana nafasi siku ya mwisho na ALLAH hata wasemesha na wala hata watazama siku ya qiyamah na hata watakasa na wana wao adhabu chungu. [Al-Imran: 77]. Na amefungamanisha maneno ya Uongo na Shirki katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمِ حُرْمَتِ اللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ عِنْدَ رَبِّهِ وَأُحِلَّتْ لَكُمْ الْأَنْعَامُ إِلَّا مَا يُنْتَلَىٰ عَلَيْكُمْ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ﴾ [الحج: 30]

Kwa ajili hiyo na yeyote atakaye tukuza alama za ALLAH basi kheri kwake mbele ya mola wake,na mmehalalishiwa nyinyi wanyama isipokuwa wale mlio elezewa juu yenu,basi jiepusheni uchafu utokanao na shetani na mjiepushe na maneno ya uwongo. Suratil Hajj:30. Na maelekezo yake yalikuwa wazi kwenye kutenda haki kati ya wagomvi wawili,na kuwacha kuhukumu kwa matamania,na hukumu iwe kwa kutumia Nidhamu ya kisheria iliyokuwa wazi,na miongoni mwa kauli hizo ni : ((Ushahidi unakuwa kwa mwenye Kudai na Kiapo kinakuwa kwa mwenye kupinga))(1220) Kama ambavyo yeye aliziba njia za madai yaliyo batili basi akasema:

((Lau kama watu wangelipewa kwa mujibu wa Madai yao,basi wangedai Damu za watu na mali zao))(1221) Na alitilia mkazo Juu ya umuhimu wa kutoa Ushahidi:

﴿فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا ذَوَى عَدْلٍ مِّنكُمْ وَأَقِيمُوا الشَّهَادَةَ لِلَّهِ ذَٰلِكُمْ يُوعَظُ بِهِ مَن كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَن يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ﴿٢﴾﴾ [الطلاق: 2]

Basi watakapo fikia muda wao hao wanawake ishini nao kwa wema au achaneni nao kwa wema na muwaweke mashahidi wale wenye uwadilifu miongoni mwenu na msimamisha ushahidi kwa ajili ya ALLAH,hivyo ndivyo mnavyo elekezwa kwa yule ambaye anamuamini ALLAH na siku ya mwisho,na atakaye muogopa ALLAH atampa njia ya kutokea. Al-twalaaq:2 Na akazingatia kuwa kutoa Ushahidi ni katika sababau za Uadilifu.

Na Qur'an ikamtaka kufanya uadilifu pasina kufuata matamania ya nafsi,hata kama itakuwa haki ipo dhidi ya mtu mwenye cheo cha juu kuliko wengine kwa wanadamu,bali hata kama ingekuwa ndio yeye mwenyewe.

﴿يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُوفُوا قَوْمِينَ بِأَلْقُسِطِ شُهَدَاءَ اللَّهِ وَلَوْ عَلَىٰ أَنفُسِكُمْ أَوِ الْوَالِدِينَ وَالْأَقْرَبِينَ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا فَاللَّهُ أَوْلَىٰ بِهِمَا فَلَا تَتَّبِعُوا الْهَوَىٰ أَن تَعْدِلُوا وَإِن تَلَوُّا أَوْ تَعْرِضُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٣٥﴾﴾ [النساء: 135]

Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkafuata sheria Zake kivitendo, kuweni ni wasimamizi wa uadilifu, wenye kutekeleza ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hata kama ni kinyume na maslahi ya nafsi zenu au baba zenu au mama zenu au jamaa zenu, namna atakavyokuwa yule mwenye kutolewa ushahidi awe ni tajiri au masikini, kwani Mwenyezi Mungu ni bora kwa wao wawili kuliko nyinyi, na ni Mjuzi zaidi wa mambo ambayo

yana maslahi kwao. matamaniao na mapendeleo yasiwapelekee nyinyi kuacha uadilifu. Na mkiupotosha ushahidi, kwa ndimi zenu, mkautoa kwa namna isiyokuwa ya kweli, au mkaupuuza kwa kuacha kuutekeleza au kwa kuuficha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa matendo yenu ya ndani na Atawalipa kwayo. [An Nisaai: 135]. Qur'an ikamtaka kufanya uadilifu hata kwa maadui katika maneno yake aliposema mwenyezi mungu mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوْمِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلَىٰ ءَآلٍ ءَعْدِلُوا ءَعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ﴾ [المائدة: 8]

Enyi mliyo amini kuweni wasimamizi kwa ajili ya ALLAH hali ya kuwa ni mashahidi kwa uwadilifu,na yasikuziuyeni mambo ya watu mkaacha kufanya uwadilifu ,fanyeni uwadilifu ndio karibu zaidi ya ucha mungu,na muogopeni ALLAH hakika ALLAH ni mwenye kueleza kwa yale mnayo yafanya. [Al Maaida: 8]. Na imepokelewa katika Hadithi Al-Quds (Enyi waja wangu hakika mimi nimeharamisha Dhulma katika nafsi yangu na nimeifanya kuwa haramu baina yenu hivyo msidhululiane)(1222).

Na kwa haika tabia za kiislamu zilikuja,ili kuchukuwa Dhamana ya uadilifu na kutakasa Hukumu na wenye kufanya kazi ya uhakimu,basi akatahadharisha Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kuhukumu kwa matamaniao au kutokuwa na elimu,kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يٰۤاِدٰوُدُ اِنَّا جَعَلْنٰكَ خٰلِيفَةً فِى الْاَرْضِ فَاَحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوٰى فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيْلِ اللّٰهِ اِنَّ الَّذِيْنَ يَضِلُّوْنَ عَن سَبِيْلِ اللّٰهِ لَهُمْ عَذٰبٌ شَدِيْدٌۢ بِمَا نَسُوْا يَوْمَ الْحِسَابِ﴾ [ص: 26]

Ewe Dāwūd! Sisi tumekufanya ni msimamizi ardhini na tumekupa mamlaka huko, basi hukumu baina ya watu kwa uadilifu na uchungaji haki, na usifuate matamaniao katika kuhukumu, kwani

hilo litakupotosha na Dini ya Mwenyezi Mungu na Sheria Yake, hakika wale wanaopotea njia ya Mwenyezi Mungu watapata adhabu ya uchungu humo Motoni, kwa kughafilika kwao na Siku ya kulipwa na kuhesabiwa. Katika haya pana ushauri kwa viongozi wahukumu kwa haki iliyoteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka na kuwa juu, wala wasipotoke nayo wakapotea njia Yake. Surat Swaad:ukurasa wa 26. Na kwa hakika alitahadharisha mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-Mahakimu Madhalimu kwa maneno yake aliposema: ((Mahakimu wapo wa aina tatu,mahakimu wawili wataingia motoni,na hakimu mmoja ataingia Peponi,Mtu ambaye amehukumu pasi na haki na akajuwa kuwa amehukumu pasi na kutenda haki,basi mtu huyo ataingia motoni,na Hakimu asiyekuwa na ujuzi akaangamiza haki za watu basi ataingia motoni,na Hakimu aliyehukumu kwa kutenda haki,basi huyo ataingia peponi))(1223)

Kama ambavyo Uislamu umeharamisha Rushwa,Rushwa ambayo inapelekea Dhulma na kuwadhulumu watu haki zao na huathiri kwenye kutoa hukumu na mahakimu,amesema Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani- ((Amemlaani Mwenyezi Mungu Mtoaji Rushwa na na mpokeaji Rushwa na mwenye kutaka Rushwa))(1224)

Na hukumu ilikuwa ni yenye kuenea kwenye jamii ya waislamu na kufanyiwa kazi katika zama za Mtume,akawa ni mwenye kuingia katika hukumu Muislamu na asiyekuwa Muislamu,na takwa la uadilifu lilikuwa ni la wote kwa waislamu na wasiokuwa waislamu,anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿سَمْعُونَ لِلْكَذِبِ أَكْلُونَ لِّلَسُخْتِ إِن جَاءُوكَ فَأَحْكُم بَيْنَهُمْ أَوْ أَعْرِضْ عَنْهُمْ وَإِن تُعْرِضْ عَنْهُمْ فَلَن يَضُرُّوكَ شَيْئاً وَإِن حَكَمْتَ فَأَحْكُم بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ﴾ [المائدة: 42]

Mayahudi hawa wanakusanya kati ya usikilizaji urongo na ulaji haramu. Basi watakapokujia wakishtakiana kwako, basi hukumu kati yao au waache. Na usipohukumu kati yao, hawataweza kukudhuru kwa chochote. Na iwapo utahukumu, basi hukumu kati yao kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda waadilifu. Al-maidah:42. Kwa hakika Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-aliweka sheria katika kila jambo ambalo linahitajia Uadilifu kwa kuchaguwa mahakimu katika sehemu za mbali ya mji wa Madinah,na kwa hakika Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-alituma idadi kubwa ya maswahaba kwenda kuhukumu kwenye magomvi ya watu,na miongoni mwa mahakimu waliokuwa mashuhuri katika hawa ni Ally Bin Abii twaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-pale alipomtuma Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-baadhi ya sehemu katika mji wa Yemen awe ni Hakimu,na wala hakurudi isipokuwa wakati wa Hija ya kuaga,na kwa hakika palipita mjadala kati yake na na Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-kuhusu misingi ya uhakimu kama tuyvyotangulia kutaja mna miongoni humo mjadala ni maneno ya Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-alipomwambia Ally: ((Wakikujia wagomvi wawili basi usimhukumu kwa kumpa haki mmoja wao mpaka uwe umeshamsikiliza anavyosema mwingine)) (1225)

Kama alivyomtuma Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-Muaadh Bin Jabal-Radhi za Allah ziwe juu yake-kwenda Yamen,na alikuwa shughuli yake ni kuwahukumu watu,na kwa hakika Mtume alijadiliana na muaadh Bin Jabal alipomtuma Yemen akasema:((Utahukumu kwa kutumia hukumu gani?akasema Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume wake,akasema,ikiwa hautapata kwenye kitabu?,akasema nitahukumu kwa Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu,akasema ikiwa hautapata?akasema nitajitahidi kutumia Rai yangu,akasema mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake na amani-Namshuru Mwenyezi Mungu ambaye amempa muwafaka mjumbe wa Mtume

wa Mwenyezi Mungu kwa jambo ambalo linamridhisha Mtume mtume wake)) (1226)

Na hapakubakia na Jimbo lenye kufuata Dola ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-isipokuwa alilipangia viongozi na watu wenye kuwahukumu watu na wenye kusimamisha uadilifu kwao,na huenda katiba ambayo ilikuwa Mashuhuri katika hukumu ulimwengu mzima,ni Ujumbe wa Omar Bin Khattwab kwenda kwa Abuu Mussa Al-ash-ariy katika Hukumu.(1227)

Na jambo ambalo halina shaka ndani yake ni kuwa Omar alitaka kumpa miongoni mwa alivyojifunza kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake na amani-katika mambo ya uhakimu na uadilifu,na kwa hakika imekuja katika huo ujumbe. Ama baada ya kusema hayo kwa hakika Kuhukumu ni jambo la lazima lilopitishwa,na ni Sunna yenye kufuatwa,basi juwa utakapoletewa mashitaka basi tambua hakuna faida ya kuzungumza haki isiyotekelezwa,na waonyeshe watu unyenyekevu katika uso wako na uadilifu wako na ukaaji wako,ili asijepatwa na tamaa mwenye cheo kwa kutotenda kwako haki na wala asikate tamaa mtu dhalili ya kutofanya kwako uadilifu,Ushahidi ni kwa mwenye kuleta mashtaka na kiapo ni kwa mwenye kupinga mashitaka,na Upatanishi unafaa baina ya waislamu isipokuwa upatanishi wakuhalalisha haramu na kuharamisha halali.na wala isikuzuie hukumu uliyoihukumu jana kuihukumu leo ikiwa akili yako imeirudia na ikaongozwa kwa uongofu wako ukaacha kurudi kwenye haki;kwani hakika haki ya zamani haibatilishwi na chochote,na kuirudia haki ni bora kuliko kuendelea na Batili,na jaribu kufahamu na kutambua mambo kwa undani jambo ambalo linazingazinga katika moyo wakona halipo kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu-Mtukufu- wala halipo kwenye Sunna za Mtume wake,kisha jitahidi ujuwe vyenye kufanana na pima mambo kwa mujibu wa yanavyoendana,na muwekee mwenye kudai haki ambayo haipo au ushahidi muda wenye ukomo ,na yeyote atakae leta ushahidi basi utamchukulia

haki yake na utamtatulia Qadhia yake kwa kumpa haki yake,kwani kufanya hivyo kunaondoa shaka zaidi na kuweka wazi kilicho jificha,na waislamuni waadilifu wao kwa wao isipokuwa yule aliyepigwa viboko katika hukumu,au alishawahi kutoa ushuhuda wa uongo,au ni mwenyekudhaniwa vibaya kwenye utawala wake na unasaba wake,kwani kwa hakika Mwenyezi Mungu amesamehe wenye kujiepeusha na viapo,na kujitetea kwa uthibitisho,jiepushe na mfadhaiko na kukemea na kumuudhi mshtakiwa kwani kwa hakika haki ikiwa kwenye sehemu ya haki,basi Mwenyezi Mungu huyakuza malipo,na huifanya itajwe kwa uzuri na amani) (1228)

Na hapana shaka kuwa mpangilio wa maisha na uislamu katika jamii yoyote ya wanaadamu,haiwezi kusimama isipokuwa kwa kufuata Nidhamu na kanuni na sheria iliyo wazi ambayo wanakuwa sawa watu wote mbele ya sheria hiyo,pamoja na kupatikana marejeo ya hukumu ili kuhifadhi haki,na kuwa na nguvu zenye kusaidia kurudisha haki kwa watu wake na kuzuia Dhulma na kutekeleza hukumu ,na hili linapelekea Amani kwa watu wote na kusimama na hukumu hii yenye uadilifu na yenye kusimamia haki,na yenye kusaidia kuwa na maisha mazuri,na uzalishaji ulio sahihi na uliombali na wizi,na uporaji wa mali zao au Heshima zao au Nafsi zao.

Na namna hii ndivyo mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-aliitengeneza jamii ya kiislamu katika mji wa madina kwa kutumia muongozo wa Mwenyezi Mungu na utendaji wa kiutume na yote yaliyotokea chini ya hukumu yake na uendeshaji wake kwa uadilifu kwenye pande zote za kisiwa cha Waarabu,na ikawa hii Nidhamu ni Taa kwa dola za kiislamu na jamii yake,inazidi Kupata Amani yake na Imani yake kila wanapoifuata na kwenda kwa mfumo wake,na kupoteza haki kila wanapokuwa mbali na njia yake.

Na kwa hakika walitunga maulamaa na wanazuoni wa sheria katika Nyanja hii kiasi yakuwa inakuwa vigumu kudhibiti kwake

katika mirathi ya kielimu kisiasa kiidara kikanuni kisheria kiuadilifu,(1229) hawakuijuwa wengi miongoni mwa watoto wa Umma huu,na wakashindwa kuifahamu wengi miongoni mwa viongozi na wenye maamuzi hivyo wakawa ni wenye kupotea na wenye kupoteza.

Upangaj wa ulinzi na usalama

Uwepo wa Uhifadhi wa Amani ni hitajio la mwanadamu,na ni Dharura ya msingi katika kila jamii ya wanadamu,na alipotumwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-ilikuwa miji ya waarabu wakiishi katika hali ya fujo kwa kukosa amani, pale amabapo mwenye nguvu amuonea mnyonge,na fujo ikawa imetawala na watu wakashindwa kusafiri na kuzilinda nafsi zao isipokuwa kwa kutumia nguvu na washirika wakishirikiana kulinda amani,na wala hapakuwepo na Nidhamu au Sheria na kanuni inayowalinda watu na kutofanyiwa uwadui na watu wengine,na zikaja Aya za Qur'an ili ziwakumbusha watu umuhimu wa Amani na ikafungamanisha na riziki katika maneno yake Mtumkufu:

﴿الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِّنْ جُوعٍ وَآمَنَهُمْ مِّنْ خَوْفٍ﴾ [فريش: 4]

Ambaye Amewapa wao chakula wakati wa njaa kali na akawapa amani na utulivu wakati wenziwao wapo katika khofu) Quraish:4 Na kauli yake:

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾ [النور: 55]

Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini miongoni mwenu na wakafanya matendo mema kwamba atawarithisha ardhi ya

washirikina na atawafanya ni wasimamizi wa hiyo ardhi, kama alivyofanya kuwa walio kuja kabla yao kati ya wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, na Aifanye Dini yao ambayo Ameridhika nayo na Akawachagulia, nayo ni Uislamu, ni Dini yenye ushindi na uthabiti, na Azigeuze hali zao kwa kuwaondolea hicho na kuwaletea amani, iwapo watamuabudu Mwenyezi Mungu, Peke Yake, na watasimama imara kwa kumtii, na wasimshirikishe na kitu chochote. Na Mwenye kukanusha baada ya hilo la kupewa usimamizi, amani, uthabiti na utawala kamili, na akakanusha neema za Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waliotoka nje ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu. Al- Nuur:55 Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ الْقُرَى الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا قُرَى ظَلِيمَةً وَقَدَرْنَا فِيهَا السَّيْرَ سِيرُوا فِيهَا لِيَالِي وَأَيَّامًا آمِنِينَ﴾ [سبأ: 18]

Na tulijaalia, baina ya watu wa Sabai na hali wao wako Yaman, na ile miji tuliobarikia, nayo ni Shām, kuwe na miji iliyoshikana, aliye kwenye mji wowote kati ya hiyo huuona mji mwingine. Na tukafanya mwendo wa kutembea humo ni mwendo uliokadiriwa, kutoka nyumba hadi nyumba, bila mashaka, na tukawaambia, «Nendeni kwenye miji hiyo , wakati mnapotaka wa usiku au mchana, mkiwa mko kwenye amani hamuogopi adui, njaa wala kiu. Sab'ai :18 Na kauli yake:

﴿فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا يُبْرَاهِيمُ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ﴾ [آل عمران: 97]

Katika Nyumba hii kuna alama waziwazi ya kwamba hiyo ni katika ujenzi wa Ibrāhīm na kwamba Mwenyezi Mungu ameitukuza na kuipa heshima. Kati ya alama hizo ni Maqām ya Ibrāhīm, amani imshukie, nayo ni lile jiwe ambalo alikuwa akisimama juu yake wakati alipokuwa akiziinua nguzo za Alkaba, yeye na mwanawe Ismā'il. Na yoyote mwenye kuingia Nyumba hii

atapata amani ya nafsi yake, hapana yoyote atakayemkusudia kwa uovu. Na Mwenyezi Mungu Amewajibisha kwa mwenye uwezo katika watu, popote atakapokuwa kuiendea nyumba hii ili kutekeleza matendo ya Hija. Na yoyote mwenye kuikanusha faradhi ya Hija, basi huyo amekufuru. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi naye, Hana haja ya hija yake wala amali yake na wala Hana haja na viumbe vyake vyote. [Al-Imraan: 97]. Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَامَ ﴿٣٥﴾﴾
[إبراهيم: 35]

Na kumbuka, ewe Mtume, pindi Ibrāhīm aliposema akimuomba Mola Wake, baada ya kumfanyia makao mwanawe wa kiume, Isma'il, pamoja na mamake, Hajar, kwenye bonde la Makkah, «Ewe Mola ijaalie Makkah ni mji wa amani, awe kila aliye humo yuko kwenye amani, na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu. [Ibrahim: 35] kama ambavyo ameliashiria hilo kwenye maneno yake mtukufu:

﴿وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ إِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْعَاكِفِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢٥﴾﴾ [البقرة: 125]

"Na Kumbuka, ewe Nabii, wakati tulipoifanya Alka'ba ni marejeo ya watu; wanakuja kuikusudia, kisha wanarudi makwao kwa watu wao, kisha wanairudia tena, ni makusanyiko yao katika Hija, Umra, tukufu na kuswali, na pia ni amani kwao: hakuna adui anayewashambulia wakiwa hapo na tukasema, "Pafanyeni hapo Maqām Ibrāhīm ni mahali pa kuswali. Maqām Ibrāhīm ni jiwe ambalo Ibrāhīm alisimama juu yake alipokuwa akijenga Alka'ba. Na tulimletea Wahyi Ibrāhīm na mtoto wake Ismāīl kwa kuwaambia, «Isafisheni Nyumba Yangu na kila najisi na uchafu kwa ajili ya wenye kuabudu kwa kutufu pembezoni mwa Alka'ba

au kuketi Itikafu (I'tikāf) Msikitini na kuswali hapo.” [Al Baqarah: 125] Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا ءِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ ٱلْأَمْنُ وَهُمْ مُّهْتَدُونَ﴾ [الأنعام: 82]

Wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakafuata sheria Yake kivitendo, na wasichanganye imani yao na ushirikina, wao ndio wenye utulivu na usalama na wao ndio walioongozwa kwenye njia ya haki. [Al An'am: 82]. Na mwenyezi Mungu akabainisha katika visa vya manabii waliopita umuhimu wa Amani katika maisha ya Nyumati zilizopita ,na kwa watu wa Swalehe alisema:

﴿أَتَتْرَكُونَ فِي مَا هَهُنَا ءَامِنِينَ﴾ [الشعراء: 146]

«Je, mnafikiri kuwa mtaachwa salama katika haya yaliyopo kwenu? Al- Shuaraai:146 Na kwa vijiji vyote na miji amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿أَفَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَن يَأْتِيَهُم بَأْسُنَا بَيِّنًا وَهُمْ نَائِمُونَ﴾ ﴿أَوْ أَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَن يَأْتِيَهُم بَأْسُنَا ضُرْحَىٰ وَهُمْ يَلْعَبُونَ﴾ ﴿أَفَأَمِنُوا مَكْرَ ٱللَّهِ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْقَوْمُ ٱلْخَٰسِرُونَ﴾ [الأعراف: 99-97]

Kwani wanadhani hawa watu wa mijini kuwa wao wameokoka na wamesalimika na adhabu ya Mwenyezi Mungu kuwa haitawafika kipindi cha usiku wakiwa wamelala? Au kwani wanajiaminisha watu wa mijini kuwa wamesalimika na adhabu ya Mwenyezi Mungu kuwa haitawafika kipindi cha mchana wakiwa wameghafilika, wameshughulika na mambo ya dunia yao? Mwenyezi Mungu Amezihusu nyakati mbili hizi kwa kuzitaja, kwa kuwa mwanadamu nyakati hizi huwa wameghafilika zaidi, kwa hivyo kuja adhabu katika nyakati hizi huwa na kitisho zaidi na ni kali zaidi. Je, wamejiaminisha, watu wa miji iliyokanusha, na vitimbi vya Mwenyezi Mungu kwao na kuwapa Kwake wao

muhula, kwa kuwaachilia na yale Aliyowaneemesha nayo katika dunia yao, kwa njia ya kuwatesa sababu ya vitimbi vyao? Basi hawajiaminishi na vitimbi vya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu wenye kuangamia. Al-aaraaf:97-99. Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ ءَامِنَةً مُّطْمَئِنَّةً يَأْتِيهَا رِزْقُهَا رَغَدًا مِنْ كُلِّ مَكَانٍ فَكَفَرَتْ بِأَنْعَمَ اللَّهُ فَأَذَّاقَهَا اللَّهُ لِبَاسَ الْجُوعِ وَالْخَوْفِ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ﴾ [النحل: 112]

Na Mwenyezi Mungu Amepiga mfano wa mji wa Makkh. Ulikuwa uko kwenye salama ya kutofanyiwa uadui, utulivu kutokana na dhiki za maisha na unajiliwa na riziki zake kwa uzuri na wepesi kutoka kila upande, wakazi wake wakazikanusha neema za Mwenyezi Mungu kwao, wakamshirikisha na wasimshukuru, hapo Mwenyezi Mungu Akawatesa kwa njaa kwa kuviogopa vikosi vya Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukiye, na majeshi yake yaliyokuwa yakiwatisha, na hili ni kwa sababu ya ukafiri wao na vitendo vyao vya ubatilifu. Al-nahli:112 Na kwa hakika Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- aliwapa Bishara Maswahaba katika sehemu nyingi kuwa Amani itatawala katika hii Dini,na miongoni mwa hizo Bishara ni maneno yake aliyomwambia Adiu Bin Haatim: ((Namuapia Mwenyezi Mungu Inakaribia kusikiwa kuwa Mwanamke anatoka kutoka Qadisya akiwa kwenye Ngamia wake,mpaka ataweza kuitembelea Nyumba hii na wala hatamuogopa yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu))(1230) Na amesema Rehema na Amani ziwe juu yake: Na Mwenyezi Mungu atatimiza jambo la Dini hii mpaka msafiri atatembea kutoka Swanaa mpaka Hadhara Mauti bila ya kuogopa chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu, ila atawaogopea kondoo wake kutokana na mbwa mwitu.

Na ulikuwa ulinzi na usalama baina ya watu ni katika malengo ya uislamu,na kilichofuata ilikuwa ni kulazimiana na jambo la kuipiga vita Khofu na vyenyekupelekea kuwa na Khofu,na kwa hivyo lilikuwa

lengo la utawala wa Dola ambayo alikuwa akiendesha Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-na kuhakisha Usalama.

Na Hukumu na vitendea kazi vyake na uwekaji wake wa Sheria vikifanya kazi ya kuhakikisha uwepo wa uadilifu usalama na amani na ukawa ni wenye kuhifadhi Roho za watu.

﴿مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَن قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ بَعَدَ ذَلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ﴾ [المائدة: 32]

Kwa sababu ya uhalifu huu wa mauaji, tuliwaekea sheria Wana wa Isrāīl kwamba yoyote mwenye kumuua mtu pasi na sababu ya kulipiza kisasi au ya uharibifu katika ardhi, kwa aina yoyote kati ya aina za uharibifu zinazopelekea mauaji, kama ushirikina na uharamia, atakuwa ni kama kwamba amewaua watu wote kwa jinsi atakavyostahili mateso makubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kwamba yule atakayejizuia asiue mtu ambaye Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuuawa, ni kama kwamba amewahuisha watu wote. Hivyo basi, kulinda heshima ya binadamu mmoja ni kulinda heshima ya binadamu wote. Hakika Mitume wetu waliwajia Wana wa Isrāīl kwa hoja na dalili juu ya usawa wa yale waliyowalingania kwayo ya kumuamini Mola wao na kuyatekeleza yale yaliyofanywa wajibu kwao na Mola wao. Kisha, wengi kati yao, baada ya kujiwa na Mitume ni wenye kupita mipaka ya Mwenyezi Mungu kwa kuyafanya yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu na kuyaacha maamrishi yake. [Al Maaidah: 32]. Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ لَا تَسْفِكُونَ دِمَاءَكُمْ وَلَا تُخْرِجُونَ أَنْفُسَكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ ثُمَّ أَقْرَرْتُمْ وَأَنْتُمْ تَشَاهُونَ﴾ [البقرة: 84]

Na Kumbukeni, enyi Wana wa Isrāīl, tulipochukua kwenu ahadi ya mkazo katika Taurati ya kuharamisha umwagaji damu baina yenu, nyinyi kwa nyinyi, na kutoana majumbani nyinyi kwa nyinyi. Kisha mkakubali hilo na hali nyinyi mnashuhudia kuwa ni kweli. Al-Baqarat:84. Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَمًا﴾ [الفرقان: 68]

Na ambao hawaombi pamoja na Mwenyezi Mungu asiyekuwa Yeye, wala hawaziui nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuuawa ispokuwa kwa kitu kinachopasisha kuuawa, kama vile kukufuru baada ya kuamini au kuzini baada ya ndoa au kumuua mtu kwa uadui, wala hawazini bali wanazihifadhi tupu zao ispokuwa kwa wake zao au wale ambao mikono yao ya kulia imemiliki. Na mwenye kuyafanya madhambi haya makubwa atakuta mateso huko Akhera. [Al Furqaan: 68].

﴿وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيَيْهِ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفُ فِي الْقَتْلِ إِنَّهُ كَانَ مَنْصُورًا﴾ [الإسراء: 33]

Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuuawa, isipokuwa kwa haki ya kisharia, kama kisasi au kumpiga mawe mzinifu aliyeingia kwenye hifadhi ya ndoa au kumuua aliyeritadi. Na mwenye kuuawa pasi na haki ya kisheria, basi tumempa msimamizi wa mambo yake, awe ni mrithi au ni hakimu, uwezo wa kutaka muuaji auawe au kutaka dia. Na haifai kwa msimamizi wa mambo ya aliouawa kupita mpaka wa Mwenyezi Mungu katika kuchukua kisasi, kama vile kuua watu wawili au wengi kwa mmoja au kumua muuaji kwa njia ya kumtesa. Mwenyezi Mungu ni Mwenye kumsaidia msimamizi wa aliyeuawa juu ya aliyewa mpaka aweze kumuua kwa njia ya kisasi. [Al Israai: 33].

﴿وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَمًا﴾ [الفرقان: 68]

Na ambao wanampwekesha Mwenyezi Mungu na hawamuombi wala kumuabudu mola asiyekuwa Yeye, wala hawaii nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuuawa ispokuwa kwa kitu kinachopasisha kuuawa, kama vile kukufuru baada ya kuamini au kuzini baada ya ndoa au kumuua mtu kwa uadui, wala hawazini bali wanazihifadhi tupu zao ispokuwa kwa wake zao au wale ambao mikono yao ya kulia imemiliki. Na mwenye kuyafanya madhambi haya makubwa atakuta mateso huko Akhera. [Al Furqaan: 68].

Na alikuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akitilia mkazo katika mazungumzo yake na hotuba zake juu ya suala la amani kati ya watu na kuwalinda na pia kuwacha kuwafanyia uadui,na alikuwa akitilia mkazo jambo hilo kwenye kuungwa kwake mkono,imepokelewa kutoka kwa Ubaadat Bin Swaamit -Radhi zaAllah ziwe juu yake-amesema:((Nilimuunga mkono Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenye kikundi akasema:Ninawaungeni mkono yakuwa msimshirikishe mwenyezi mungu na kitu chochote,na wala msiibe wala msizini na wala msiwauwe watoto wenu na wala msilete uzushi ambao mnauzuwa kwa mikono yenu na miguu yenu,na wala msiniasi kwenye jambo jema,na mwenye kutekeleza hayo basi malipo yake ni kwa Mwenyezi Mungu,na atakayepata katika hayo chochote na akakichukuwa hapa Dunia basi itakuwa kwake ni kafara na utakaso,na aliyesitiriwa na mwenyezi mungu basi hilo ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu,akitaka atamuadhibu na akitaka atamsamehe))(1232)

Na miongoni mwa kauli mashuhuri aliyoisema Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-katika Hija ya kuaga katika siku ya Arafa: Hivi ni mwezi gani muujuawo kuwa utukufu wake ni mkubwa?wakasema

twajuwa ni mwezi wetu huu.akasema:ni mji gani muujuawo kuwa ni mji mtukufu?wakasema:twajuwa ni huu mji wetu.akasema:Ni siku gani muijuayo kuwa ni tukufu?wakasema:Twaijuwa ni siku yetu hii,akasema:kwa hakika Mwenyezi Mungu-Mtukufu-amewaharamishia Damu zenu na Mali zenu na Heshima zenu,isipokuwa kwa haki yake kama alivyo haramisha siku yenu hii,katika mji wenu huu na katika Mwezi wenu huu,fahamuni vyema je nimefikisha ujumbe?akasema hivyo mara tatu,marazote hizo wanamjibu: Ndiyo,akasema Adhabu itakuwa juu yenu ikiwa mtarudi baada yangu mkawa makafiri baadhi yenu wakiwauwa baadhi yao))(1233)

Na kwa hakika alitilia mkazo Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-suala la amani katika maisha ya Mwanadamu kwa maneno yake: ((Yeyote miongoni mwenu atakaye amka asubuhi Familia yake ikiwa ipo salama,mwili wake ukiwa na afya njema,na anacho chakula cha siku yake hiyo mtu huyo anakuwa kama vile ameikusanya Dunia nzima))(1234) Na kwa hakika amesema Mtume-**Rehema** za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: ((Siyo halali kwa muislamu kutisha muislamu mwenzake))(1235) Na alikuwa katika Dua yake akisema: ((Ewe mola wangu wa haki ni sitiri mimi Aibu yangu na uniepushe na mfadhaiko))(1236)

Na kwa hakika Dola ya Kiislamu katika Mji wa Madina ilitekeleza jukumu lake katika kueneza amani na salama baina ya watu,kwa waislamu na wasiokua waislamu,na jambo hilo ndilo lilikuwa ni nguzo ya makubaliano ya Madina baina ya Mtume na **-Rehema na amani ziwe juu yake**-na wakazi wote kwa ujumla na makabila ya watu wa Madina,ni ulinzi shirikishi na kueneza amani katika mji na kuwacha kuwasaidia wenye kusababisha hofu kwa watu wa madina miongoni mwa wenye kuzuwa mambo na wengineo.(1237)

Na alikuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake** akifuatilia yeye mwenyewe usalama wa Madina na usalama wa watu wake

wenye kuja kwenye mji huo,na alikuwa akisimamisha hukumu za kisheria kwa watu waovu ambao walikuwa wakifanya uharibifu katika Ardhi na wakimwaga Damu,na huondosha usalama na amani kwa watu kama alivyofanya na watu wa Uraniyyiina.na kwa hakika aliweka Bukhari mlango katika kitabu chake sahihi akaita (Mlango wa usimamaishaji Hukumu na kinachotahadharishwa miongoni mwa utekelezaji wa hukumu) (1238) na ameleta humo milango mingi,miongoni mwa milango ni (Usimamishaji wa Hukumu kwa wenye utukufu na wasio na utukufu)(1239),na mlango wa machukizo ya kumuomba msamaha katika kutekeleza hukumu pindi itakapokuwa imeshafika kwa kiongozi(1240) Imepokelewa humo kutoka kwa Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake- (Kuwa Maquraish liliwasukuma jambo la mwanamke wa kabila la Makhzuum ambaye aliiba wakasema ni nani atakaye mtetea kwa mtume mwanamke huyu?) wakasema pia na ni nani atakayekuwa na ujasiri zaidi ya Osamah Bin Zaid Kipenzi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-** basi Osamah akamsemesha mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-**:Ewe Usamah hivi unatetea hukumu katika hukumu za mwenyezi Mungu?kisha akasimama na akasema:kwa hakika waliangamia waliokuwepo kabla yenu kwa kuwa wao ilikuwa akiiba mwenye Hadhi wanamuacha na akaiiba mtu Dhalili wanamsimamishia hukumu,na ninamuapia Mwenyezi Mungu lau kama angeiba Fatma Bint Muhammad ningemkata mkono wake)(1241) na kwa hakika Qur'an tukufu iliamrisha kumkata Mwizi Mkono katika maneno yake matukufu:

﴿وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَزِيزٌ
حَكِيمٌ﴾ ﴿٣٨﴾ فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ إِنَّ اللَّهَ عَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٩﴾
[المائدة: 38-39]

Na mwizi wa kiume na mwizi wa kike, wakateni, enyi watawala, mikono yao kuambatana na Sheria. Hayo yakiwa ni malipo yao

kwa kuchukua kwao mali ya watu pasi na haki, na ni mateso ambayo kwayo Mwenyezi Mungu Anawazuia wengineo kufanya mfano wa kitendo chao. Na Mwenyezi Mungu ni Mshindi katika mamlaka Yake, ni Mwenye hekima katika amri Zake na makatazo Yake. Basi yule atakaye tubia baada ya dhulma na akatengeneza kwa uzuri hakika ALLAH anamsamehe hakika ALLAH ni msamehevu mpole. Al-Maidah :38-39)

Na kwa hakika Ameweka Bukhar katika sahihi yake, Mlango katika neno lake Mtukufu:

﴿وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جِزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَزِيزٌ

حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾ [المائدة: 38]

(Na mwizi wa kiume na mwizi wa kike wakateni mikono yao hali ya kuwa ni malipo ya walichokichuma ni Adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na ni mwenye hekima) Al-Maida:38.(1242) na kwa hakika Mtume - **Rehema na amani ziwe juu yake**-alitekeleza Hukumu ya Mwizi kwa mwanamke wa kabila la Makhzuumiyyat, na wala Hadhi yake haikumsaidia chochote, wala uombezi wa Osamah Bin Zaid na wengine miongoni mwa mamwinyi wa Makkah haukumfaa kwenye kuzuia utekelezaji wa hukumu ya kisheria juu yake. na inaonekana wazi kuwa yeye alitekeleza Hukumu ya kumkata mwizi mkono zaidi ya mara moja katika maisha yake.(1243)

Na hukumu ya kumkata mwizi mkono ilikuwa na mchango mkubwa katika kulinda usalama wa watu na mali zao, mpaka uwizi ukapotea na ukakaribia kukosekana katika wakati wa Mtume- **Rehema na amani ziwe juu yake**-

Na hapana shaka kuwa mji wowote na jamii yoyote katika ulimwengu panapo simamishwa hukumu ya mwizi basi hupunguwa humo wizi, na watu wanakuwa na usalama wa mali zao. kama vile

ambavyo kuuwa ilikuwa adhabu yake ni kuuwawa isipokuwa kama wenye ndugu aliyeuliwa watasamehe.na kwa hakika imekuja hukumu waziwazi katika kitabu cha Mwenyezi Mungu katika maneno yake Mtukufu aliposema:

﴿وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيهِ سُلْطَانًا فَلَا يُسْرِفُ فِي الْقَتْلِ إِنَّهُ كَانَ مَنْصُورًا﴾ [الإسراء: 33]

Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameharamisha kuuawa, isipokuwa kwa haki ya kisharia, kama kisasi au kumpiga mawe mzinifu aliyeingia kwenye hifadhi ya ndoa au kumuua aliyeritadi. Na mwenye kuuawa pasi na haki ya kisheria, basi tumempa msimamizi wa mambo yake , awe ni mrithi au ni hakimu, uwezo wa kutaka muuaji auawe au kutaka dia. Na haifai kwa msimamizi wa mambo ya aliouawa kupita mpaka wa Mwenyezi Mungu katika kuchukua kisasi, kama vile kuuwa watu wawili au wengi kwa mmoja au kumuua muuaji kwa njia ya kumtesa. Mwenyezi Mungu ni Mwenye kumsaidia msimamizi wa aliyeuawa juu ya aliyeya mpaka aweze kumuua kwa njia ya kisasi. [Al Israai: 33]. Na jambo lilikuwa wazi ya kuwa katika hukumu ya Kisasi kunazuia watu kufikiria kuuwa na kumwaga Damu za watu pindi watakapokuwa wamekuwa kwa Damu zao limetoka tamko la vitisho kwa ajali yake.na kuwa kisasi kinawafuata ikiwa watafanya jambo hilo,na kisha ni kuwa kisasi kinazuia umwagaji Damu na kulinda maisha ya watu,kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيَاةٌ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ﴾ [البقرة: 179]

Na hakika katika kuwekwa sheria ya kisasi na utekelezaji wake kwa kutarajia kufikia uchaji Mwenyezi Mungu na kumuogopa kwa kumtii daima, kuna maisha ya amani kwenu, enyi wenye akili timamu) Al-Baqarah:179). Na kwa Hakika Hukumu ya Ugaidi ilijulikana zamani ,nayo ilikuja kutoka katika maneno mtukufu:

﴿إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِنْ خِلَافٍ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ذَلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٣٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٤﴾﴾ [المائدة: 33-34]

Hakika malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na wanaojitokeza wazi kumfanyia uadui na kuzifanyia uadui hukumu zake na hukumu za Mtume Wake na kufanya uharibifu katika ardhi kwa kuwaua watu na kupora mali, ni wauawe au wasulubiwe pamoja na kuuawa (Kusululubiwa ni kufungwa mhalifu juu ya bao) au ukatwe mkono wa kulia wa mpiga vita na mguu wake wa kushoto. Iwapo hatatubu {kwa kuendelea na uharamia wake}, ukatwe mkono wake wa kushoto na mguu wa kulia, au wahamishwe wapelekwe mji usiokuwa wao, wafungwe kwenye jela ya mji huo mpaka iyonekane toba yao. Na haya ndiyo malipo Aliyo yaandika Mwenyezi Mungu kwa wenye kupiga vita; nayo ni unyonge wa duniani. Na huko Akhera itawapata adhabu kali iwapo hawatatubia. Lakini atakayekuja kati ya wale wanaopiga vita kabla hamjawatia mkononi na akaja akiwa mtiifu mwenye majuto, atafutiwa yale yaliyokuwa ni haki ya Mwenyezi Mungu. Na jueni, enyi Waumini, kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha kwa waja Wake, ni Mwenye kuwarehemu. Al-Maidah:33-34)

Na kwa hakika imepokelewa kuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake aliwakirimu watu miongoni mwa waarabu walimjia wakiwa ni wagonjwa, nao ni kikundi miongoni mwa kabia la Ukal walifunga msafara kwenda kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na wakawa katika Suffah ,na wakaelekea Madina ,na wakasema ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu: tunahitajia maziwa, Mtume akawaambia sina maziwa ya kuwapa lakini nendeni mpaka mfike kwenye Ngamia wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi na wakaenda na nawakanywa maziwa yake na mikojo yake mpaka

wakapata afya na wakanenepa,na wakamuuwa mchungaji wa Mtume na wakaswaga kundi la ngamia ukamfikia Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-ukelele,basi akatuma watafutaji wawafuatilie nyuma yao na mchana haukufika mpaka wakawa wamesha wafikia,basi akaitisha Misumari na ikapashwa moto na akawatoboa macho yao na kuwakata mikono yao na miguu yao na wala hakutaka sulhu na wao,kisha akawatupa katika sehemu yenye joto kali wakawa wanaomba kunyweshelezwa maji na wala hakuwanywesheleza mpaka wakafa,Amesema Abuu Qalaabah:Waliiba na wakauwa na wakafanyia uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake(1244) na kwa hakika Mtume alijuwa haja za watu za kuitaka amani na wasiwe ni wenye kulindwa,basi walipata amani maadui zake walipoingia katika mji wa Makka Aliopingi akwa ajili ya kuukomboa ,pale ambapo alitangaza kuwa atakaeingia Nyumba ya Abuu Sufiani basi atakuwa amesalimika,na atakae jifungia mlango wa nyumba yake basi atakuwa amesalimika ,na atakaeingia msikitini basi atakuwa amaesalimika .(1245)

Alikuwa Mtume ni mwenye kuufahamu zaidi umuhimu wa Usalama katika maisha ya Mwanadamu,na kwa hivyo basi lilikuwa jambo la kwanza alilowaeleza watu baada ya kuukombowa mji wa Makka ilikuwa ni kuharamisha umwagaji wa Damu(1246)na kwa hakika usalama ulikuwa ni wa watu wote katika Dola ya Kiislamu,kuanzia ilipoanza mpaka kuwepo kwake katika mji wa Madina yenye Nuru,na kwa hakika Usalama na amani kwa ujumla ndiyo lengo la kwanza katika Dola ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-tangu kuanza kwake.

kwa hakika ulinzi na usalama umekusanya kati ya kuzuia uovu na kutekeleza hukumu kwa muovu,na kuhifadhi haki,na kupangilia Uadilifu,na kueneza Uaminifu,na hili ndiyo hitajio la kibinadamu baada ya Dini na Tauhiid pamoja na utafutaji wa Rizki,na hayo yote yamekuja waziwazi kwenye muujiza katika maneno yake mtukufu:

﴿فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ۖ الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِنْ جُوعٍ وَآمَنَهُمْ مِنْ خَوْفٍ﴾ [قریش: 3-

[4

"Basi, wamshukuru na kumuabudu Bwana wa Nyumba hii ya Alkaaba, Ambaye kwa ajili Yake wametukuzwa, na wampwekeshe na kumtakasia ibada." "Ambaye Amewapa wao chakula wakati wa njaa kali na akawapa amani na utulivu kutokana na hofu kubwa na mbabaiko." (Quraish:3-4) kwa hakika usalama na amani umefungamanishwa na Tauhiid na Riziki katika Muujiza huu,na umefungamanishwa na Nyumba ya Mwenyezi mungu na Upande waelekeo waislamu ikiwa ni alama ya sehemu na mpangilio na Dini kwa wakati mmoja.

Kutengeneza Adabu katika Jamii(1247)

Kwa hakika Jamii ya wanaadamu yote kwa ujumla na Haswa Jamii ya Kiarabu tabia zao zilikuwa mbovu,na wao kwa wao walikuwa wakifanyiana ubaya na wakidharauliana wao wa wao(1248)na Uthubutu wa Mtume-**rehema na amani ziwe juu yake**- ni wa nguvu na bidii kubwa katika kuibadilisha jamii iliyokuwepo ndani ya Makkah,kwa kujaribu kwake kuueneza uislamu na yanayofungamana nayo miongoni mwa sheria na ujenzi wa Tabia na mafunagamano ya kibinadamu,na mahusiano ya upole baina ya mtu mmoja mmoja na ujumla na kwa hakika makuraishi walikaidi na wakazuia Da'wa na wakamzuia ,na wakampiga vita mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na wakawaudhi maswahaba wake,jambo ambalo lilipelekea kutafuta sehemu nyingine ili aanzishe jamii ya kiislamu yenye Amani,pale ambapo kundi la muhaajiriina lilikuja na wakaweka mazoea kuunda udugu na Answaar,na kukapatikana baina yao jambo lilojulikana kwa jina la Nidhamu ya kuunga udugu ambayo ilionyesha Thamani ya Jamii iliyosafi yanye kuunga undugu kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شَحْنًا فَاُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ﴾ [الحشر: 9]

Na wale walio andaa makazi na imani kabla yao wana wapenda wale walio hamia kwao na wala hawapati ndani ya vifua vyao tabu kwa yale waliyo yatoa na wana wapendelea zaid kuliko nafsi zao na hata kama watakuwa ni wenye kuhitajia na atakaye zuia ubakhili wa nafsi yake basi hao ndio walio faulu. Al-hashir:9)

Ulikuwa ujengaji wa mazoea na Uungaji Udugu kwa ajili ya kizazi cha maswahaba na kizazi cha umma mzima na watakaokuja baada yao,anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ﴾ [الحشر: 10]

Na wale walio kuja baada yao wanasema-EWE-mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu ambao walio tutangulia katika imani na wala usitujalie ndani na mioyo yetu vinyongo kwa wale ambao walio amini-EWE-mola wetu hakika wewe ni mrehemevu mpole. Al-Hash-ri:10) Kwa hakika ilikuwa kuitakasa Nafsi na kujenga Tabia ni miongoni mwa misingi ya Da'wa ya Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-imekuja katika maneno yake mtukufu:

﴿كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِنْكُمْ يَتْلُو عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ﴾ [البقرة: 151]

" Kama tulivyo watumia mtume miongoni mwenu anawasomea juu yenu dalili zetu na akiwatakasana na akiwafundisheni kitabu na hekima na akiwafundisheni yale ambayo mliyokuwa

hamuyafahamu. Suratil" (Baqarat :151) Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْ أَنْفُسِهِمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ﴾ [آل عمران: 164]

"Hakika Mwenyezi Mungu Amewapa neema Waumini, miongoni mwa Waarabu, Alipomtumiliza Mtume atokaye katika jinsi yao, akawa anawasomea wao aya za Qur'ani, anawatakasa na ushirikina na tabia mbaya na anawafundisha Qur'ani na Suna, pamoja na kwamba kabla ya Mtume huyu walikuwa kwenye upotevu na ujinga ulio wazi". [Al-Imran: 164]. Na vilevile maneno aliposema:

﴿هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ﴾ [الجمعة: 2]

" Ni yeye ambaye amemtuma kwa wasio jua kusoma na kuandika mtume anawasomea juu yao dalili zake na akiwatakasa na akiwa fundisha kitabu na hekima na walikua hapo kabla ndani ya upotevu ulio wa wazi". (Surah Al- jumua:2)

﴿رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾ [البقرة: 129]

"Ewe mlezi wetu na umtume kwao mtume miongoni mwao akiwasomea juu yao dalili zako na akiwa fundisha kitabu na hekima na akiwatakasa hakika wewe ni mwenye nguvu mwenye hekima". (Surah Al-Baqarah 129) Na kwa hakika zimekuja sheria mbalimbali za Uislamu ili kuweka mahusiano mazuri baina ya mtu mmoja mmoja na jamii,(1249) na baina ya Familia moja ,akasema mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- ((Wema ni Tabia Njema))(1250) Na alisema: ((Mbora wenu ni yule mzuri wenu wa

Tabia))(1251) Na uislam ukatilia mkazo kwenye kutengeneza vizuri mahusiano ya watoto na baba zao na baba na watoto wao,pale ambapo hilo lilikuwa ni jambo la Mwenyezi Mungu kuwafanyia wema wazazi wawili yaani kutengeneza mahusiano kati ya jamii na jamii nyingine,na kueneza Huruma na mafungamano. Na kwa hakika iikuwa kuwatendea wema wazazi wawili kumefungamanishwa na kumtii Mwenyezi Mungu-Mtukufu-kama alivyosema:

﴿وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۖ إِنَّمَا يُبَلِّغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا آفٍ وَلَا تَنْهَرُهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ ۖ وَخَفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيْتَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾﴾ [الإسراء: 23-24]

Na Mola wako, ewe mwanadamu, Aameamrisha na kulazimisha na kupasisha Apwekeshwe, kutakata na sifa za upungufu ni Kwake na kutukuka ni Kwake, kwa kuabudiwa Peke Yake, na Aameamrisha kuwafanyia wema baba na mama, hasa wakiwa katika hali ya ukongwe: usione dhiki wala uzito kwa jambo lolote ulilonalo kwa mmoja wao au kwa wao wawili, wala usiwasikilizishe neno baya, hata kama ni sauti ya kuonyesha kutoridhika ambayo ni neno baya la daraja ya chini kabisa, wala usiwafanyie tendo baya, lakini kuwa mpole kwao na uwaambie wao daima maneno mepesi yenye ulaini. Na uwe, kwa mamako na babako, mdhalilifu na mnyenyekevu kwa kuwahurumia, na umuombe Mola wako awarehemu kwa rehema Zake kunjufu wakiwa hai na wakiwa wamekufa, kama walivyovumilia juu ya kukulea ulipokuwa mdogo usiokuwa na uwezo wala nguvu. (Al-israa:23-24).

Kama amabvyo Qur'an ilitilia mkazo kuhusu ndugu wa karibu na muamala mzuri kati yaokatika maneno yake mtukufu:

﴿وَأْتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تَبْذُرْ نَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾﴾ [الإسراء: 26]

"Na mpeni ndugu wa karibu haki yake na Masikini na mpita njia aliye katikiwa na safari wala msifanye Ubadhirifu"(Al-israa 26)kama alivyokuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-kwenye kilele cha juu kabisa kwenye Tabia kama alaivyosifiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kauli yake:

﴿وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقِي عَظِيمٌ﴾ [القلم: 4]

Na hakika wewe, ewe Mtume ni mwenye tabia njema zaidi, nazo ni zile tabia njema zilizomo kwenye Qur’ani. Kwani kule kuifuata Qur’ani kulikuwa ni sifa yake, akitekeleza amri zake na kukomeka na yale yanayokatazwa nayo. [Al Qalam: 4]. Na akaamrisha Mwenyezi Mungu-kutakasika na machafu ni kwake-watu wamuige yeye kwa maneno yake mtukufu:

﴿لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ

كَثِيرًا﴾ [الأحزاب: 21]

Hakika mtume wa ALLAH amekuwa kwenu nyie ni mfano mzuri kwa yule ambaye anamhitaji ALLAH na siku ya mwisho na akamtaja ALLAH mara nyingi. (Surat Ahzaab: 21) Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: Kwa hakika nilitumwa ili kukamilisha tabia njema}{(1252)

Na alikuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-ni mnyenyekevu akiwatembelea wagonjwa,na akalifuata Jeneza,na akaiitikia wito,na alikuwa hapendi watu wamsimamie,alikuwa akinyenyekea kwa wakubwa na wadogo,mpaka mgeni akimjia anamkuta akiwa yupona maswahaba zake hana utofauti kwenye kukaa,na alikuwa mkarimu na akisisitiza ukarimu,mkarimu na akaimarisha ukarimu,mtakasifu na akaimarisha usafi na kujizuia kutegemea watu,Shujaa,mpole akisisitiza upole,mpole akiamrisha upole,mwenye harufu nzuri na msafi na akiamrisha usafi,na jambo linaloongoza yote hayo ni Tabia njema kwa Mwenyezi Mungu-Aliye

takasika na kutukuka-akianzia Tauhiid na kuridhia uabudiwa wake,na dhana nzuri na kutegemea kwake-Kutakasika na machafu ni kwake,na kutarajia yaliyo kwake na kumuogopa yeye kwa mbali na kwa karibu,na kujiliwaza kwa kumtaja kwake na kumshukuru kwake na kumuabudu kwa njia iliyo nzuri:

﴿إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣﴾﴾ [الأنفال: 2-3]

"Hakika wenye kumuamini Mwenyezi Mungu kikweli kweli ni wale ambao akitajwa Mwenyezi Mungu hulainika nyoyo zao na wasomewapo aya za Mwenyezi Mungu zinawazidishia Imani na kwa Mola wao wanategemea" Wale ambao wanaendelea kutekeleza Swala zilizofaradhiwa kwa nyakati zake, na katika kile tulichowaruzuku wanatoa kwenye yale tuliyoamrisha. Al-anfaal :2-3) Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِي وَلَا تَكْفُرُونِ ﴿١٥٢﴾﴾ [البقرة: 152]

(Basi nikumbukeni kwa kunishikuru na mnishukuru na wala msinikufuru) {Al-baqra 152} Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani:

﴿مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٣﴾ وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١٤﴾﴾ [نوح: 13-14]

Mnani nini enyi watu, hamuweki Heshima kwa Mwenyezi Mungu(13) na hali yeye Amewaumba nyinyi katika miongo yenye kufuatana : tone la manii, kisha pande la damu, kisha nofu la nyama, kisha mifupa na nyama? (Surat Nuuh 13- 14) Na yeye ndiye msemaji:

﴿وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْرُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ﴾ [يونس: 61]

Na huwi, ewe Mtume, kwenye jambo lolote katika mambo yako, na husomi chochote kile katika aya za Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na hafanyi yeyote katika ummah huu tendo lolote lema au baya, isipokuwa sisi huwa ni mashahidi juu yenu ni wenye kuliona hilo, mnapolichukua na kulitenda, tukawahifadhia na tukawalipa kwalo. Na haufichamani na ujuzi wa Mwenyezi Mungu uzito wa chungu mdogo ardhini wala mbinguni, wala kitu kidogo kabisa wala kikubwa kabisa, isipokuwa kiko kwenye Kitabu kilichoko kwa Mwenyezi Mungu kilicho waziwazi chenye ufafanuzi, ujuzi Wake umekizunguka na Kalamu Yake imekiandika. Yunus:61, Na kwa hakika alisema mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-hali ya kukumbusha tabia njema kumfanyia Mwenyezi Mungu: Muoneeni haya Mwenyezi Mungu kikwelikweli,hifadhini kichwa na kilichomo ndani ya kichwa,na mlihifadhi tumbo na ilichokibeba,na yakumbukeni mauti na kuoza))(1253)

Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: ((Na mwenyezi Mungu ndiye mwenye haki zaidi ya kuonewa haya kuliko watu wote))(1254) Na miongoni mwa Tabia njema na Mwenyezi Mungu ni kukimbilia kwake na kumtaka msamaha na kurejea na kukimbilia kwa Mwenyezi mungu,kama alivyosema:

﴿فَفِرُّوا إِلَى اللَّهِ إِنِّي لَكُمْ مِنْهُ نَذِيرٌ مُبِينٌ﴾ [الذاريات: 50]

Basi kimbieni, enyi watu , kutoka kwenye mateso ya Mwenyezi Mungu na muelekee kwenye rehema Yake kwa kumuamini Yeye na Mtume Wake, kufuata amri Yake na kufanya mambo ya utiifu Kwake. Hakika mimi, kwenu nyinyi, ni muonyaji ambaye maonyo

yake yako waziwazi. Na Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, alikuwa akizungukwa na mambo hukimbilia Swala, na huku ndiko kumkimbilia Mwenyezi Mungu. Adh-Dhaariyaat:5) Na kumbuka kuwa Neema kutoka kwake ni kama alivyosema:

﴿وَمَا بِكُمْ مِنْ نِعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْأَرُونَ﴾ [النحل: 53]

Na neema yoyote mliyonayo ya uongofu au afya ya mwili, ukunjufu wa riziki na watoto na yasiyokuwa hayo, inatoka kwa Mwenyezi Mungu Peke Yake, Yeye Ndiye Mwenye kuwaneemesha nayo. Kisha yanapowapata magonjwa, matatizo na ukame, basi ni kwa Mwenyezi Mungu Peke Yake mnalia kwa maombi. Al-Nahli:53 Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِي وَلَا تَكْفُرُونِ﴾ [البقرة: 152]

Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Amewaamrisha Waumini wamtaje Yeye na Akatoa ahadi kwa hilo malipo bora zaidi, nayo ni kumsifu yule anayemtaja Yeye mbele ya viumbe walioko juu. Pia Amewaamrisha Waumini wamshukuru Yeye Peke Yake kwa maneno na vitendo na wasizikanushe neema Zake juu yao. {Al-baqra 152} Na kumbuka ukarimu wake na Fadhila zake na Ihsaan zake na kuwachunga na kuwafuatilia viumbe wake:

﴿مَنْ عَمِلْ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أَنْفَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهٗ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾ [النحل: 97]

Mwenye kufanya tendo zuri, akiwa ni mwanamume au ni mwanamke, na huku ni mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake , basi tutampa maisha mema yenye utulivu duniani hata kama ni mchache wa mali, na tutawalipa huko Akhera thawabu zao kwa uzuri zaidi ya walivyofanya duniani. [An Nahli: 97]. Al-Nahli:97

﴿وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنْصِتُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾ [الأعراف: 204]

Na isomwapo Qur’ani isikilizeni, enyi watu, na mnyamaze ili muielewe kwa matarajio kwamba Mwenyezi Mungu Awarehamu kwayo. Al-aaraf:204) Na miongoni mwa Adabu ambazo Uislamu umeukuza nao Umma wa Kiislamu ni,ni kuwa na Adabu na Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-katika maisha yake na baada ya kufa kwake,kama katika maneno mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيْ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبِطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٣﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِنَ وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّى تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥﴾﴾ [الحجرات: 1-5]

Enyi mliyo amini msitangulize mbele ya ALLAH na mtume wake,na mcheni ALLAH,hakika ALLAH ni mwenye kusikia,mwenye kujua. Enyi mlioamini msiziuone sauti zenu juu zaidi ya Sauti ya Mtume,wala msiseme nae kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi,visije vitendo vyenu vikakosa thawabu na hali yakuwa hamtambui,kwa hakika wale ambao wanainamisha sauti zao kwa Mtume,hao ndiyo ambao Mwenyezi Mungu amezitakasa nyoyo zao wa kumuogopa Mwenyezi mungu,basi watakuwa na maghafira na thawabu zilizokuwa kubwa. "Hakika ya wale wanao kuita, ewe Nabii, nyuma ya vyumba vyako kwa sauti ya juu, wengi wao hawana akili ya kuwapelekea kuwa na adabu nzuri pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na kumheshimu." Na lau wao wangali ngojea mpaka uwatokee ingeli kuwa kheri kwao,na ALLAH ni msamehevu mpole. Al-Hujuraat:1-5

Na kwa hakika Qur'an imeamrisha waswahaba wa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-kufuata maamrishi yake na kutokumuasi yeye katika maneno yake mtukufu:

﴿لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنْكُمْ لِوَاذًا فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾
[النور: 63]

Msilinganishe kumuita mtume kama mnavyo itana baadhi yenu kuwaita wengine hakika amejua ALLAH wale ambao wanao toka kwa kujificha miongoni mwenu basi wachukuwe tahadhari wale ambao wanao kwenda kinyume kunako jambola -mtume-wasije patwa na fitna au wakapatwa wao na adhabu chungu. [An Nur 63] Na alisema:

﴿مَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَى فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَىٰ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ﴾ [الحشر: 7]

Yale ambayo aliyoyatekeleza ALLAH juu ya mtume wake kutokana na watu wa miji basi ni kwa ajili ya ALLAH na mtume na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na wapita njia ili isije kuwa ni chakula baina ya matajiri miongoni mwenu na alicho kupeni mtume kichueni na alicho wakataza kiacheni na muogopeni ALLAH hakika ALLAH ni mkali wa kuadhibu. (Surah Al-Hashr 7) Na alisema:

﴿فَلَا وَرَيْكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾ [النساء: 65]

Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Anaapa kwa nafsi Yake tukufu, kwamba hawa hawataamini kikweli mpaka wakufanye wewe ni

hakimu kwenye ugomvi unaotokea baina yao katika uhai wako na watake uamuzi wa Sunnah yako baada ya kufa kwako, kisha wasiingiwe na dhiki katika nafsi zao kwa matokeo ya hukumu yako, na wakwandame, pamoja na hivyo, kwa kukufuata kikamilifu. Kutoa uamuzi kulingana na aliyokuja nayo Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukiye, kutoka kwenye Qur’ani na Sunnah katika kila jambo katika mambo ya kimaisha, pamoja na kuridhika na kusalimu amri, ni miongoni mwa uthabiti Imani (An- nisaa:65) Na katilia mkazo tabia njema pamoja na mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-na wala wasiondoke wakamuacha pindi wanapokuwa wamekusanyika nae kwenye jambo lilowakusanya isipokuwa waondoke kwa Idhini yake:

﴿إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَإِذَا كَانُوا مَعَهُ عَلَىٰ أَمْرٍ جَامِعٍ لَمْ يَذْهَبُوا حَتَّىٰ يَسْتَأْذِنُوهُ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ فَإِذَا اسْتَأْذَنُوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأَذَنَ لِمَن شِئْتَ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفِرَ لَهُمُ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ عَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٣﴾ لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنْكُمْ لِوَاذًا فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٤﴾﴾ [النور: 62-63]

Kwa hakika Waumini kikwelikweli ni wale ambao Wamemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakazitumia sheria Zake, na wakiwa wapo pamoja na Nabii, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, katika jambo ambalo amewakusanya kwalo la maslahi ya Waislamu, hawaondoki mpaka wamuombe ruhusa. Kwa hakika wale wanaokuomba ruhusa, ewe Nabii, ndio wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kikweli. Basi wakikuomba ruhusa kwa baadhi ya haja zao, mruhusu unayemtaka miongoni mwa wale waliokuomba ruhusa kuondoka kwa udhuru, na uwaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe dhambi za waja Wake wenye kutubia, ni

mwingi wa huruma kwao. Msiseme, enyi Waumini, mnapomuita Mtume wa Mwenyezi Mungu, «Ewe Muhammad!» wala «Ewe Muhammad bin Abdillahi!» kama wanavyosema hivyo baadhi yenu kuwaambia wengine. Lakini mtukuzeni na msemi, «Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu! Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!» Kwa kweli Mwenyezi Mungu Anawajua wale wanaoondoka kutoka kwenye kikao cha Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kwa siri, bila ya ruhusa yake, wakisaidiana kujificha. Basi na wajihadhari wanaoenda kinyume na amri Yake wasije wakashukiwa na janga na shari au adhabu yenye uchungu iumizayo. (Al-Nuur: 62-63) Na kama alivyomrisha Umma kumsikiliza na kumtii Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-

﴿إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَنْ يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥٤﴾ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَخْشِ اللَّهَ وَيَتَّقْهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٥٥﴾ وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِنْ أَمَرْتَهُمْ لَيَخْرُجُنَّ قُلْ لَا تُفْسِمُوا طَاعَةَ مَعْرُوفَةَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٥٦﴾ قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلَ وَعَلَيْكُمْ مَا حُمِّلْتُمْ وَإِن تُطِيعُوهُ تَهْتَكُوا وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ﴿٥٧﴾﴾ [النور: 54-51]

Ama Waumini wa kweli, msimamo wao ni kwamba wanapo itwa kwenda kuhukumiwa, katika ugomvi ulio kati yao, na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na hukumu ya Mtume Wake, wanakubali uamuzi unaotolewa na wanasema, «Tumesikia tuliyo ambiwa na tume mtii aliyetuita kwenye hilo.» Na hao ndio walio faulu wenye kufuzu kupata matakwa yao kwenye mabustani ya Pepo yenye neema. Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake katika kufuata maamrishi na kujiepusha na makatazo na akaogopa mwisho mbaya wa uasi na akajihadhari na adhabu ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio wenye kufuzu kupata neema Peponi. Na wanafiki waliapa kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, kwa upeo wa juhudi yao, viapo vizito, «Ukituamrisha, ewe Mtume,

kutoka kwenda kwenye jihadi pamoja na wewe, tutatoka tena tutatoka» Sema uwaambie, «Msiape viapo vya urongo, kwani utiifu wenu unajulikana kuwa ni wa ulimini tu. Kwa kweli Mwenyezi Mungu Anayatambua mnayoyafanya, na Atawapa malipo yake. Na useme, ewe Mtume, kuwaambia watu, «Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume.» Na wakiipa mgongo, basi jukumu la Mtume ni kufanya aliyoamrisha ya kuufikisha ujumbe, na ni jukumu la watu wote kuyafanya waliyoamrisha ya kufuata. Na mki mtii yeye mtaongoka. Na jukumu la Mtume ni kuufikisha ujumbe wa Mola wake mafikisho yaliyo wazi. (Al-Nuur:51-54) Na alikuwa Mtume- Rehema na amani ziwe juu yake- anasema: Mwenye kufurahishwa kuwekwa mbali na moto na kuingizwa peponi basi na ajitahidi yamjie mauti yake na akiwa anashuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja wake na mtume wake,na awafanyie watu yale anayopenda yeye kufanyiwa)(1255)

Na alikuwa Mtume- Rehema na amani ziwe juu yake-ni mwenye kuipa nyongo Dunia na akiamrisha hilo,na alisifika na sifa za hali ya juu ambazo zinahimiza usafi na kuheshimu hisia za wengine kwenye kula kwake na kunywa kwake na kuvaa kwake,na kuhisi kwake na muonekano wake,na alikuwa akiamrisha kueneza mapenzi na amani baina ya watu,amesema Mtume- Rehema na amani ziwe juu yake- Hivi siwajuzeni mwenye kupendeza kwangu mimi zaidi,na alaiyekuwa karibu yangu miongoni mwenu kwenye makao siku ya kiama,ni Mbora wenu wa Tabia wapole kwa wanaowazunguka wanaweka mazoea na wanazoeleka))(1256) Kama alivyosema Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- Namuapa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, Hamtoingia peponi mpaka muamini, na hamtoamini mpaka mpendane, je nisikufahamisheni juu ya jambo ambalo mkilifanya mtapendana? toleaneni salamu kwa wingi kati yenu. Na alikuwa akiwasalimia mtume- Rehema na amani ziwe juu yake-Watoto pindi anapo wapitia walipo

Na kwa hakika Mwenyezi mugnu aliamrisha kutaka kubisha Hodi na kutoa salamu kama katika maneno yake aliposema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّى تَسْتَأْذِنُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَى أَهْلِهَا ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ﴾ [النور: 27]

Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkazitumia sheria Zake, msiingie kwenye nyumba zisizokuwa zenu, mpaka muwatake ruhusa wenyewe ya kuingia na muwaamkie. Na matamshi ya maamkizi hayo yatokayo kwenye Sunnah ni, «Assalāmu ‘alaikum. Je, niingie?» Kutaka ruhusa huko ni bora kwenu nyinyi. Huenda mkazikumbuka, kwa kufanya kwenu hivyo, amri za Mwenyezi Mungu na mkapata kumtii. [Al-Nuur: 27] Na Qur'an ikatilia mkazo katika kujenga kwake Tabia ya Jamii juu ya unyenyekevu na amani pamoja na watu katika maneno yake mtukufu:

﴿وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا﴾ [الفرقان: 63]

Na waja wa ALLAH ni wale ambao wanao tembea juu ya ardhi kwa upole na wanapo semeshwa na wa wajinga wanasema amani. Al-furqaan:63. Na kauli yake:

﴿وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طَوْلًا﴾ [الإسراء: 37]

Na usitembee ardhini kwa kujigamba na kujivuna, kwani wewe hutaipasua ardhi kwa kutembea juu yake kwa namna hiyo na hutaifikia milima katika urefu kwa kujigamba kwako, kujivuna kwako na kutakabari kwako. Al-israa:37

﴿وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرْحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿١٨﴾
 وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَاغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿١٩﴾﴾ [لقمان: 18-

[19

«Na usizungushe uso wako ukauepusha na watu unaposema na wao au wanaposema na wewe, kwa kuwadharau na kuwafanyia kiburi, wala usitembee kwenye ardhi baina ya watu kwa kujigamba na kujivuna. Hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila mwenye kiburi, mwenye kujifahiri katika nafsi yake, pambo lake na maneno yake. «Na unyenyekee katika kwenda wako na uishukishe chini sauti yako usiipandishe juu, kwani sauti mbaya zaidi na inayochukiza zaidi ni sauti ya punda wanaojulikana kwa upumbavu wao na sauti zao za juu.» Luqman:18-19 Kama alivyokuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-akiamrisha upole,nao upole ni katika sababu za mazoeano katika Familia na Jamii hivyo akasema: ((Hakika ALLAH anapenda upole kwenye kila jambo)),⁵⁷⁰ Kama alivyo sema ((Haukuwa Upole kwenye kitu isipokuwa umependezesha kitu hiko)).⁵⁷¹ Na hakika Mtume alifuatisha upole na ulaini kwa maswahaba,kama alivyo sema ALLAH Mtukufu:

⁵⁷⁰ amepokea Bukhar katika sahihi yake,kitabu Al-Adab,mlango wa upole kwenye kila jambo.juzu 8/7.

⁵⁷¹ Amepokea Muslim katika sahihi yake,kitabu cha Albir,mlango wa upole,juzu 8/22,na amepokea Ahmad kwenye musnad wake,juzu yz 6/58,112.

﴿فِيمَا رَحْمَةٍ مِنَ اللَّهِ لَئِنَّ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَانْفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾﴾
 [آل عمران: 159]

Na kwa ajili ya rehema za Mwenyezi Mungu kwako na maswhaba wako, ewe Nabii, Mwenyezi Mungu Alikuneemesha ukawa laini kwao. Na lau ungalikuwa na tabia mbaya, mwenye moyo mgumu, maswahaba wako wangalijitenga na kuwa mbali na wewe. Kwa hivyo, usiwe na hasira nao kwa yaliyotokea kwao katika vita vya Uhud. Basi muombe Mwenyezi Mungu, ewe Nabii, Awasamehe na uwashauri katika mambo yanayohitajia ushauri. Na utakapoazimia kufanya jambo kati ya mambo yoyote, baada ya kushauri, litekeleze hali ya kumtegemea Mwenyezi Mungu, Peke Yake. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wenye kujitegemea Kwake. [Al-Imran: 159]. Pamoja na upole na ulaini yalikuwa mapenzi ya Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa umma na pupa yake juu yao.

﴿لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿١٢٨﴾﴾ [التوبة: 128]

Hakika amakufikieni mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni na anakuhangaikieni ,na kwa walioamini ni mpole na mwenye huruma. (Al- taubah 128)

﴿لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَاخْفِضْ جَنَاحَكَ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾﴾ [الحجر: 88]

Usiziangalie kwa macho yako mawili zile starehe za duniani ambazo tuliwastarehesha nazo makafiri aina mbalimbali, na usisikitike juu ya ukafiri wao, na uwanyenyekee wenye kumuamini MwenyeziMungu na Mtume wake. [Alhijr:88]

﴿وَإِخْفِضْ جَنَاحَكَ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ﴾ [الشعراء: 215]

Na uwe laini wa mwenendo na maneno, kwa unyenyekevu na huruma, kwa yule ambaye imekufunukia kutoka kwake kuitika mwito wako. [Ash-shuara]

Alikuwa Mtume ni mfano kwenye Huruma na utoaji na tabia njema, Khadija alimpa taarifa hiyo-Radhi za Allah ziwe juu yake Khadija-na akamtuliza kutokana na woga aliokuwa nao baada ya kuteremka wahyi kwake, akimkumbusha tabia yake iliyokuwa ya hali ya juu: ((Siyo hivyo kwa hakika namwapia Mwenyezi Mungu mwenyezi Mungu hatokufedhehesha, kwa hakika wewe ulikuwa ukiunga udugu na ukibeba matatizo na ukileta vilivyokuwa havipo na ni mwenye kumkirimu mgeni na kusaidia watu matatizo yanayowatokea))(1260) Na kwenye hilo kuna kutilia mkazo kwa umma wote kwa ujumla wao. (Hakika tabia njema na mambo mazuri ni sababu ya Amani kutokana na mkwaruzano wa ubaya)⁵⁷² Na pindi Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- alipo ingia Makkah hali ya kuufungua alikuwa mnyenyekevu mwenye kuinamisha kichwa chake bila ya kujifakharisha wala kiburi,⁵⁷³ Na alikuwa anasimama pamoja na mwanamke mdhaifu na mtoto akiwasikiliza wao wakimueleza na akikidhi mahitajiyo yao,⁵⁷⁴ Na

⁵⁷² Ameipokea Imamu Bukhariy katika sahihi yake, mlango unao "Kifa Kana Bad' Alwahyi Ila Rasuli Ilaah" -Rehema na amani ziwe juu yake- nayo ni Hadithi ya Tatu katika Sahihi Bukhari katika sahihi yake, juzuu ya 1/3.

⁵⁷³ Ahmad Bin Abdul aziz Al-haddad. Akhlaaq za Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- katika Qur'an na Sunna, juzuu ya 1/77.

⁵⁷⁴ Angalia ufunguzi wa Makka kutoka katika kitabu hiki.

huenda hadithi ya Anas-ALLAH amridhiye-inaweka wazi hilo kwenye kauli: (Alikuwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake akitembelea wagonjwa,na akishiriki kusalia maiti,na akipanda punda,na akiitikia wito wa mtumwa,akasema na ilikuwa siku ya kabila la bany quraydha akiwa juu ya punda aliye fungwa kamba itokanayo na ngozi na juu ya mgongo wa punda kuna kikatio kitokanacho na ngozi)⁵⁷⁵Na alikuwa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alikuwa hapendi kuongozwa na mtu mwingine au mtoto mdogo,na mara nyingi alikuwa anayemuongoza ni Osama Bin Zaid-radhi za Allah ziwe juu yao wao wawili-na wakati mwingine walimuongoza Baadhi ya wake zake(1265) Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: ((Kwa hakika Mwenyezi mungu Mtukufu alinipa wahyi ya kuwa muwe wanyenyekevu mpaka asiweze kujifaharisha mtu kwa mtu mwengine))(1266)⁵⁷⁶

Na mtume sala na amani ziwe juu yake alikuwa akifanya kazi pamoja na swahaba zake akiwa safarini alikuwa akitafuta kuni na alikuwa akifanya sehemu ya kazi kama wengine miongoni mwa watu,na alishiriki kujenga msikiti wake,kama alivyo shiriki kwa watu wake kwenye kazi zao za nyumbani. (anakuwa yupo kwenye kufanya kazi yakuwasaidia watu wake.)⁵⁷⁷Hakika ilifika mbali Aibu ya Mtume

⁵⁷⁵ Tazama sahihi Muslim ,Mlango wa unaozungumzia Ukaribu wa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- kwa watu

⁵⁷⁶ Amepokea Atrimidhiy,kitabu cha jeneza,mlango,(32),hadithi namba:1017,juzu ya 3/337.

⁵⁷⁷ kutokana na Hadithi ya Aisha-ALLAH amridhiye- kwa Bukhar,kitabu Adabu,mlango,Kaifa Yakunu Rajulu Fii Ahalihi,juzu ya 7/83

sala na amani ziwe juu yake na ALLAH akamsifu kwa hilo kwa kauli yake:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَى طَعَامٍ غَيْرٍ نَاظِرِينَ إِنَاهُ
وَلَكِنْ إِذَا دُعِيتُمْ فَادْخُلُوا فَإِذَا طَعِمْتُمْ فَانْتَشِرُوا وَلَا مُسْتَأْنِسِينَ لِحَدِيثٍ إِنَّ ذَلِكُمْ كَانَ يُؤْذَى
النَّبِيَّ فَيَسْتَحْيِي مِنْكُمْ وَاللَّهُ لَا يَسْتَحْيِي مِنَ الْحَقِّ وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَاسْأَلْنَهُنَّ مِنْ وَرَاءِ
حِجَابٍ ذَلِكُمْ أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ وَلَا أَنْ تُنْكِرُوا
أَرْوَاحَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبَآ إِنَّ ذَلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا ﴾ [الأحزاب: 53]

Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, msiingie nyumba za Mtume, isipokuwa kwa ruhusa yake, kwa kula chakula bila ya kungoja kuiva kwake. Lakini mkiitwa ingieni, na mkimaliza kula ondokeni, bila ya kujipumbaza kwa mazungumzo baina yenu. Kwani kule kungoja kwenu na kujipumbaza kwenu kunamkera Nabii, naye anawaonea haya kuwatoa kwenye hizo nyumba pamoja na kuwa hiyo ni haki yake, na Mwenyezi Mungu Haoni haya kueleza haki na kuifunua. Na mkiwaomba wake za Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, wawapatie kitu chochote mnachokihitajia katika vyombo vya nyumbani na mfano wake, basi waombeni mkiwa nyuma ya pazia. Kufanya kwenu hivyo kunatakasa zaidi nyoyo zenu na nyoyo zao na kuziepusha na mawazo ambayo yanawapitia wanaume kuhusu mambo ya wanawake na wanawake kuhusu mambo ya wanaume, kwani kuona ndio sababu ya kufitinika. Na haifai kwenu kumkera Mtume wa Mwenyezi Mungu wala kuwaoa wake zake baada ya kufa kwake kabisa, kwa kuwa wao ni mama zenu, na haifai mtu kumuoa mamake. Hakika kumkera kwenu Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na kuwaoa wake zake baada yake ni dhambi kubwa kwa Mwenyezi Mungu. Ummah huu ulitekeleza amri hii na ulijiepusha na kile Mwenyezi Mungu Aliukataza nacho. [Al-Ahزاب]53].

Na alikuwa akifundisha kuwa na uwiano na kuambatanisha kati ya dunia na Akhera, na isiwe dunia na mapambo yake ndio hamu kubwa ya kwanza kwa mwanadamu:

﴿رُزِينَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْحَبْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ وَالْخَرْثِ ذَلِكَ مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الْمَآبِ ﴿١٦﴾﴾ [آل عمران: 14]

"Wamepambiwa watu kupenda matamaniao ya wanawake na watoto wa kiume na mali mengi ya dhahabu, fedha, farasi wazuri, wanyama wa mifugo miongoni mwa ngamia, ng'ombe na mbuzi na kondoo na ardhi inayotayarishwa kwa kupandwa miti na makulima. Hayo ni mazuri ya uhai wa kilimwengu na pambo lake lenye kutoweka. Na kwa Mwenyezi Mungu kuna marejeo mazuri na thawabu, nayo ni Pepo." [Al-Imran: 14]. Na kauli yake:

﴿قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ الرِّزْقِ قُلْ هِيَ لِلَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا خَالِصَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾﴾ [الأعراف: 32]

"Sema, ewe Mtume, uwaambia washirikina, «Ni nani aliyewaharamishia vazi zuri ambalo Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Amelifanya kuwa ni pambo kwenu? Na ni nani Aliyewaharamishia kujistarehesha kwa chakula kizuri cha halali kilicho ruzukiwa na Mwenyezi Mungu?» Sema, ewe Mtume, uwaambie hawa washirikina, «Kwa hakika vile alivyoviruhusu Mwenyezi Mungu, miongoni mwa mavazi na vitu vizuri miongoni mwa vyakula na vinywaji, ni haki kwa walioamini pamoja na wengineo katika maisha ya ulimwenguni, na ni haki kwa walioamini peke yao Siku ya Kiyama. Maelezo kama hayo ni mafundisho ambayo Mwenyezi Mungu Anayaelezea kwa watu wenye kuyajua mambo wanayoeleza na kuyaelewa wanayofafanuliwa. [Al A'raf: 32].

﴿وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا وَأَحْسِنْ كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ وَلَا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ﴾ [القصص: 77]

«Na utafute, kwa mali Aliyokupa Mwenyezi Mungu, malipo mema ya Nyumba ya Akhera, kwa kufanyia mambo ya kumtii Mwenyezi Mungu duniani, na usiache fungu lako la duniani la kustarehe humo kwa halali bila kupita kiasi, na uwafanyie watu hisani kwa kuwapa sadaka kama vile Mwenyezi Mungu Alivyokufanyia hisani kwa kukupa mali mengi haya, na usitafute kile Alichokiharamisha Mwenyezi Mungu cha kuwadhulumu watu wako, kwani hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi waharibifu, na Atawalipa kwa matendo yao mabaya.» [Al qaswas: 77] Na kauli yake:

﴿فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَنَاسِكَكُمْ فَادْكُرُوا اللَّهَ كَذِكْرِكُمْ آبَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا فَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الْآخِرَةِ وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِن خَلْقٍ ﴿٢٠٠﴾ وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿٢٠١﴾ أُولَئِكَ لَهُمْ نَصِيبٌ مِّمَّا كَسَبُوا وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٠٢﴾﴾ [البقرة: 200-202]

"Basi mtakapokamilisha ibada yenu na mkamaliza amali zenu za Hija, mtajeni Mwenyezi Mungu na mumsifu kwa wingi kama vile mnavyotaja fahari za wazee wenu na zaidi ya hivyo. Kwani wamo miongoni mwa watu kikundi ambacho hima yao yote ni dunia. Hapo, wao huomba wakisema, «Ewe Mola wetu, tupe duniani yaliyo mazuri, mali na wana.» Hao hawana Akhera fungu lolote, kwa kuipuza Akhera na kujishughulisha na dunia tu. "Na miongoni mwa watu kuna kikundi chenye Imani kinacho sema katika dua yake, «Mola wetu, tupe duniani yaliyo mazuri.Na katika Akhera, tupe Pepo na utuepushie adhabu ya Moto.» Dua hii ni miongoni mwa dua zilizokusanya. Kwa hivyo, ilikuwa ni dua ambayo Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, alikuwa

akiiyomba mara nyingi zaidi, kama ilivyothibiti kwenye Sahihi Mbili: ya Bukhari na ya Muslim. "Wale wenye kuomba dua hii wana thawabu kubwa kwa sababu ya amali njema walizozichuma. Mwenyezi Mungu ni mwepesi wa kuvihesabu vitendo vya waja wake na Mwenye kuwalipa navyo." [Al-Baqara: 200-202]

Na alikuwa Rehema na Amani ziwe juu yake na pupa kubwa ya kuwajua masahaba kwa sababu ya mapenzi yake kwao, na kwa ajili hii siku moja alimhadithia Mua'dh bin Jabal akasema: "Ewe Mu'adhi, Wallahi hakika mimi ninakupenda, kisha ninakuusia ewe Mu'adhi, hakikisha usiache mwisho wa kila swala kusema: Allaahumma ainniy alaa dhikirika -Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie mimi niweze kukutaja wewe, Washukurika- na kukushukuru, Wahusni ibaadatika -Na kuzifanya vizuri ibada zako."⁵⁷⁸Na amesema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Atakapompenda mmoja wenu ndugu yake basi na amfahamishe"⁵⁷⁹kama ambavyo alivyokuwa akihimiza kila jambo ambalo linaleta mapenzi kati ya watu, kama vile kutembeleana na kupeana zawadi,⁵⁸⁰na kutabasamu ambako alisema: "Na tabasamu yako katika uso wa ndugu yako ni sadaka"⁵⁸¹Na akawafundisha wasalimiane wao kwa wao kwa salamu iliyo bora zaidi.

⁵⁷⁸ Tazama: Musnad Imamu Ahmad, 5/245

⁵⁷⁹ ameipokea Imamu Ahmad katika Musnad yake juzuu ya 4/30.

⁵⁸⁰ Sunan tirmidhiy, Kitabul birri uk 34,mlango wa Maa jaa fii Kabuul Al-hadiya Wal-lthaabat Alayha,hadithi namba:153, 4/338.

⁵⁸¹ Sunan TirmidhiY, kitabul Biri uk, 36,Maa jaa fii Swanaai'i Al-maaruuuf ,namba: 1956, 4/340. Alikusanya Abdullah Najib Salim sehemu zote zilizopokelewa kutabasamu kwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake katika kitabu cha Assiratun nabawiyya, kitabu

﴿وَإِذَا حُيِّئْتُمْ بِهِ فَاَحْسِنُوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَسِيبًا﴾

[النساء: 86]

"Na Muislamu akiwatolea salamu, muitikieni kwa maneno mazuri zaidi na kwa furaha zaidi, au muitikieni salamu kama vile alivyowatolea. Na kila mmoja ana thawabu zake na malipo yake. Hakika Mwenyezi Mungu Aliyetukuka ni Mwenye kulipa kwa kila kitu (mnachokifanya)." [An nisaai: 86] Na ameweka Bukhari katika sahihi yake katika kitabu Al'istiidhani , mlango Babu Ifshaa Asalam,⁵⁸²kama alivyoweka katika sahihi yake katika kitabu cha Imani, mlango Asalamu Minal Islami,na akaweka Tirmidhi katika sahihi yake, Mlango Bubu maa dhukira fii Fadhwul Asalam.⁵⁸³

Kama ambavyo Qur'ani ilivyozuia watu kujiona bora kuliko wengine, na ikawakumbusha asili yao ni moja, na ikaharamisha mtu kumkejeli mwingine, katika kauli yake Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا يَسْخَرُ قَوْمٌ مِنْ قَوْمٍ عَسَىٰ أَنْ يَكُونُوا خَيْرًا مِنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِنْ نِسَاءٍ عَسَىٰ أَنْ يَكُنَّ خَيْرًا مِنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا أَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِالْأَلْقَابِ بِئْسَ الْأَسْمُ الْفُسُوقِ بَعْدَ الْإِيمَانِ وَمَنْ لَمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ﴾⁵⁸² يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَبَ بَعْضُكُم بَعْضًا أَيُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَنْ يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَحِيمٌ﴾⁵⁸³ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ

akakiita: (Tabasamu za Mtume), Cha Daru Iqraa Addauliyya, chapa ya 1, Cairo 1427.

⁵⁸² Tazama: Sahihi Bukhari, 7/128

⁵⁸³ Sahihi Bukhari, 1/12, Sahihi Muslim, 7/2, Na tazama: kitabul Isti idhani 5/52.

وَأَنْتَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ
 خَبِيرٌ ﴿١٣﴾ [الحجرات: 11-13]

Enyi mlio amini lisipatikane kundi likadharau kundi lingine huwenda wale wanao dharauliwa wakawa ni bora kuliko wao na wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao huwenda wale wanao wadharau wakawa ni bora kuliko wao na wala msiuwe nafsi zenu na wala msipeane majina mabaya yamekuwa ni majina mabaya baada ya kuamini na yule ambaye hata acha basi hao ndio watu madhalimu. "Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkafuata Sheria Zake kivitendo, Jiepusheni na dhana mbaya nyingi kwa Waumini, kwani dhana nyingine ni dhambi. Wala msipekue aibu za Waislamu, wala msisemane nyinyi kwa nyinyi maneno yenye kuchukiwa na wenye kusemwa na hali wao hawapo. Je, anapenda mmoja wenu kula nyama ya ndugu yake akiwa amekufa? Nyinyi mnalichukia hilo, basi lichukieni lile la kumsengenya. Na muogopeni Mwenyezi Mungu katika yale Aliyowaamrisha nyinyi na kuwakataza. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kukubali toba za waja Wake Waumini, ni Mwingi wa rehema kwao. "Enyi watu! Sisi tumewaumba nyinyi kutokana na baba mmoja, naye ni Ādam, na mama mmoja, naye ni Ḥawwā', hivyo basi hakuna kufadhilishana baina yenu kinasaba, na tumewafanya nyinyi kwa kuzaana kuwa mataifa na makabila mbalimbali ili mjuane nyinyi kwa nyinyi, hakika mtukufu wenu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule anayemcha Yeye zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu Anawajua sana wachamungu na Anawatambua." [Al-Hujuraat: 11-13] Na ikitilia mkazo juu ya udugu wa waumini katika kauli yake Mtukufu:

﴿إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾

[الحجرات: 10]

"Hakika Waumini ni ndugu katika Dini, basi fanyeni upatanishi baina ya ndugu zenu wawili wakipigana. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu katika mambo yenu yote , kwa kutarajia mrehemewe. (Al-huj-raat 10) Na aliwajibisha kusuluhisha baina yao inapo tokea ugomvi na alikuwa akisimama dhidi ya muovu na kuendelea katika kusuluhisha kwenye kauli yake ALLAH mtukufu:

﴿وَأَنْ طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ فَاصْلِحُوا بَيْنَهُمَا فَإِنْ بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَى فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّى تَفِيءَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ فَإِنْ فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ﴾ [الحجرات: 9]

Na mapote mawili ya Waumini yakipigana, fanyeni upatanishi, enyi Waumini, baina yao kwa kuyaita yakubali kuamuliwa na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah ya Mtume Wake, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na kuridhika na uamuzi wa hivyo viwili. Iwapo pote mojawapo ya yale mawili litalifanyia uadui pote lingine na litakataa kukubali mwito huo wa upatanishi, basi lipigeni vita mpaka lirudi kwenye uamuzi wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na likirudi fanyani upatanishi baina ya hayo mawili kwa haki, na mfanyeni uadilifu katika uamuzi wenu kwa kutotoka nje ya hukumu ya wenyezi Mungu na hukumu ya Mtume Wake katika uamuzi wenu. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda waadilifu katika uamuzi wao, wanaohukumu baina ya viumbe Vyake kwa haki. Katika aya hii pana kuthibitisha sifa ya mapenzi kwa Mwenyezi Mungu kihakika, kama inavyonasibiana na utukufu Wake Aliyetakasika na kila sifa ya upungufu. [A Hijri: 9]. Kama alivyo kataza Mtume sala na Amani ziwe juu yake kunako kusengenya,⁵⁸⁴ na kunako kudharau baadhi juu ya wengine:

⁵⁸⁴ Angalia sunan ya Tirmidhiy, kitabu cha Albir, mlango Maa jaa fil ghibah, juzu ya 4/329

(Yamtosha mtu kuwa ni mwenye shari anapo mdharau ndugu yake muislamu)⁵⁸⁵kama alivyosema Allah Mtukufu:

﴿وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ﴾

[لقمان: 18]

Na wala usiwatazame watu kwa upande mmoja kwa kiburi wala usitembee katika ardhi kwa majivuno hakika ALLAH hampendi kila mwenye kujivuna mwenye kujifakharisha. [Luqman: 18]. Na ALLAH akaamrisha kusamehe na kupuuzia watu kwenye kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ الْحُرِّ بِالْحُرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنثَىٰ بِالْأُنثَىٰ فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتِّبَاعٌ بِالْمَعْرُوفِ وَأَدَاءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ ذَلِكَ تَخْفِيفٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾ [البقرة: 178]

Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkafanya vitendo vinavyoambatana na Sheria ya Mwenyezi Mungu Alioifanya faradhi kwenu kwamba mlipize kisasi kwa muuaji aliyewa kwa kukusudia, kwa sharti ya kufanya usawa na kufananisha malipo: auawe muungwana kwa kumuua mfano wake, na mtumwa kwa mfano wake, na mwanamke kwa mfano wake. Na yule atakayesamehewa na msimamizi wa aliyeuawa kwa kumuondolea kisasi na kutosheka kwa kuchukua dia, nayo ni kiwango cha mali maalumu akitoacho mhalifu kikiwa ni badali ya kusamehewa, ni juu ya pande mbili zizilazimishe tabia njema: yule msimamizi adai diya yake bila kutumia nguvu, na yule muuaji

⁵⁸⁵ Amepokea Tirmidhiy katika kitabu cha Albir, mlango(18), Maa jaa fii shafakat Al-muslim, Hadithi namba:1927, juzu 4/325, na Imamu Ahmadi kwenye Musnad wake, juzu 3/491

ampatiye haki yake kwa wema bila kuchelewesha wala kupunguza. Msamaha huo, pamoja na kupokea hiyo dia, ni masahilisho ya Mola wenu na ni huruma kwenu kwa ule wepesi na kujinufaisha. Hivyo basi, mwenye kumuua muuaji baada ya msamaha na kupokea dia, atapata adhabu kali ya kuuawa kwa njia ya kisasi duniani au kutiwa Motoni Akhera. [Al-Baqarah]178. Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولِي الْقُرْبَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلْيُغْفِرُوا وَلْيُصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [النور: 22]

"Na wala wasiache kusaidia wale wenye uwezo miongoni mwenu kuwapa ndugu wa karibu na masikini na muhajirina katika njia ya ALLAH na wasemehe na wapuzeye hivi hampendi ALLAH akusameheni na ALLAH ni msamehevu mpole". [An-Nnuur:22] Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِثْلُهَا فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ﴾ [الشورى: 40]

"Na malipo ya ubaya wa mtu mbaya ni kumtesa kwa ubaya mfano wake bila kuzidisha. Na mwenye kumsamehe aliyemfanyia ubaya asimtese, na akatengeneza mapenzi baina yake yeye na yule aliyemsamehe kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu, basi malipo mema ya kusamehe kwake yako kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wenye kudhulumu wanaowaanza watu kwa uadui na kuwafanyia ubaya". [Al-Shuura:40]

Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَكِيٌّ حَمِيمٌ﴾ [فصلت: 34]

"Na haulingani wema na uwovu zuia-ovu-kwa lile ambalo ni jema basi na yule ambaye baina yake na yeye kuna uwadui mfanye kama kipenzi mwenye kukuonea huruma" (Fuswwilat:34). Na amesema Allah Mtukufu:

﴿وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَحَتَّىٰ عَرْضَهَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ وَالْكَاظِمِينَ الْغَيْظَ وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣٤﴾﴾
[آل عمران: 133-134]

"Na kimbilieni, kwa kumtii kwenu Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ili kupata msamaha mkubwa utokao kwa Mola wenu na mpate Pepo kunjufu, upana wake ni sawa na mbingu na ardhi, Ameiandaa Mweyezi Mungu kwa wachamungu. Wale ambao wanao toa kwenye faraja na madhara na wenye kuzuia hasira na wenye kusamehe watu, na ALLAH anawapenda wafanyao wema (134)" [Al-Imran:133-134] Usawa wote huu na kuwaheshimu wengine na kutengeneza baina ya wenye kugombana ni kwa ajili ya kujenga jamii ya kiislamu yenye tabia njema yenye kuungana yenye kushikamana.

﴿لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِضْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١١٤﴾﴾ [النساء: 114]

"Hakuna manufaa katika mengi ya maneno ya watu ya siri baina yao, isipokuwa yawapo ni mazungumzo yenye kuita kwenye kufanya mema ya utoaji sadaka au maneno mazuri au kuleta upatanishi baina ya watu. Na mwenye kuyafanya mambo hayo, kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, akitarajia thawabu Zake, tutampa thawabu nyingi zilizo kunjufu". (An-nisaa:114) Na hakika alimumrisha ALLAH Mtume wake sala na amani ziwe juu yake kuwa Mpole na akamuusia kwa hilo, na akawaaamrisha watu kupeana wasia, hakika Amesema ALLAH Mtukufu:

﴿ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ﴾ [البلد: 17]

"Kisha akawa, baada ya kufanya amali njema zilizotajwa, ni miongoni mwa waliotakasa Imani yao kwa Mwenyezi Mungu, wakausia kusubiri juu ya kumtii Mwenyezi Mungu kwa kufuata maamrishi Yake na kujiepusha na vitendo vya kumuasi na wakausia kuwahurumia viumbe". [Al-balad:17] Kama alivyosema Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- (Si vinginevyo ALLAH anawahurumia wale wenyehuruma)⁵⁸⁶Na alisema: (Wahurumieni viumbe wa aridhini atakuhurumieni aliye mbinguni(ALLAH)[1277] Na akatilia mkazo juu ya kuhurumiana kwa pamoja baina ya Waislamu na jamii iwe yenye kushikamana: Mfano wa waumini katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao na kufanyiana kwao upole, ni kama mfano wa kiwiliwili, kinapopata tabu kiungo kimoja vinitana kwaajili ya hicho kimoja viungo vyote kwa kukesha na maumivu⁵⁸⁷

Swala inahesabika kuwa ndio miongoni mwa lbada zenye umuhimu kwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake,pamoja na hivyo hakika Alikuwa akifupisha kwa kuwaonea huruma watoto,Hakika amepokea Bukhar kutoka kwa Abiy Qatadah-ALLAH amridhiye-Kuwa Mtume sala na amani ziwe juu yake amesema: (Hakika mimi ninaingia ndani ya swala kisha nataka nirefupishe swala ninasikia

⁵⁸⁶ Amepokea Bukhar katika sahihi yake,kitabu cha Al-janaaiz,mlango 33,kauli ya Mtume sala na amani ziwe juu yake Al-mayitu yuadhabu Bibukaai Ahlih A'alaih,2/81.

⁵⁸⁷ kutokana na Hadithi ya Tirmidhiy,kitabu cha Albir,mlango (16)juzu ya 4/324

sauti ya mtoto kisha ninafupisha kwa kile ninacho tambua kutokana ni shida na tabu kwa mama yake kutokana na kilio chake))⁵⁸⁸

Na alikuwa mpole kwa upole na watumwa,na akafanya kuwaacha wao huru ni miongoni mwa mambo ya kujisogeza karibu,na ni miongoni mwa mlango ya kutoa kafara tofauti,na Uislamu ukabana mlango wa utumwa baada ya kuwa ipo wazi katika kila sharia na katiba katika zama za Mtume sala na amani ziwe juu yake,na Mtume aliwausia wao kheri kwa kusema: (Ndugu zenu watumwa wenu ALLAH amewafanya wapo kwenye mikono yenu,basi yule ambaye ndugu yake atakuwa yupo chini ya mikono yake basi ampe chakula kutokana na kile anacho kula yeye,na amvishe kile anacho vaa,na msiwalazimishe kutokana na kazi wasizo ziweza,basi mkiwalazimisha wasaidieni,na asiseme mmoja wenu mtumwa wangu na kijakazi wangu,isipokuwa aseme kijana wangu na bint yangu)⁵⁸⁹

Hakika kuhurumiana huku na Adabu za kiubinaadam hazikukomea kwa Waislamu tu,isipokuwa ziliendelea kwenye kuwa ni sharia za Uislamu mpaka kwa wanyama kumuonea huruma kumpa chakula na kuto mfanyia udhia na kuto muua pasi na huruma wala faida,kama alivyo sema Mtume sala na Amani ziwe juu yake: Kwenye kila chenye chene Ini kuna malipo)1281] Na alisema: Asiyewahurumia watu Mwenyezi mungu hata muhurumia Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu

⁵⁸⁸ kutokana na upokezi wa Bukhar katika sahihi yake,kitabu Al-Adhana,mlango(65) Min akhaf Aswalat,juzu ya 1/172,na amepokea Imamu Ahmad katika Musnad wake juzuu 3/205.

⁵⁸⁹ Amepokea Ahmad kwenye musnad wake,juzu ya 2/247,na amepokea Bukhar,kitabu cha Imani,mlango Alma'aswi min amri Aljaahiliyah a,juzu ya 1/13.

yake na amani: Ameingia motoni mwanamke kutokana na Paka alimfunga mpaka akafa ikawa sababu ya kuingia motoni si wakumpa chakula wala maji pindi alipo mfunga wala si wakumuachia ale majini ya aridhini))⁵⁹⁰Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: (ALLAH amemlaani yule atakaye jifanyia kitu chenye roho ni kilengwa Shabaha)1284]⁵⁹¹

Mafundisho yote haya ni katika haki za Wanyama Uislamu umewatangulia Dunia ya hivi sasa kwa karne zingi zilizopita nayo ni huruma ya ALLAH ambayo ameiweka kwa waja walio Waumini kwake,wenye kufuata uwongofu wake,ili wawe ni huruma kwa kila kitu chenye Uhai,itakuaje kwa MwanaAdam?

Uislamu umetilia Mkazo juu ya kuwasaidia watu na kusimama pamoja na wenye kuhitajia,na kuzuia maudhi kunako baki ya watu Wanamume kwa Wanawake,akasema ALLAH Mtukufu ndani ya aya zilizozungana kwa baadhi nyingine,

﴿وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولِي الْقُرْبَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ لَعُنُوا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٥٩﴾ يَوْمَ تَشْهَدُ

⁵⁹⁰ kutokana na upokezi wa Bukhari katika sahihi yake,kitabu Almusaaqaat,Babu fadhwul Saqy Almaaa ,juzu ya 3/77.

⁵⁹¹ Hadithi wamekubaliana Bukhari na Muslim kutokana na upokezi wa Abiy Hurayrah,angalia sahihi ya Bukhar,kitabu cha Adab,Babu Rahmati Alwalad Watqbiilih Wamuaanaqih,juzu ya 7/75,na angalia sahihi ya Muslim,Hadithi namba 4282.

عَلَيْهِمْ أَلْسِنَتُهُمْ وَأَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٢﴾ يَوْمَئِذٍ يُرَوِّبُهُمُ اللَّهُ دِينَهُمُ الْحَقَّ وَيَعْلَمُونَ
أَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ الْمُبِينُ ﴿٢٥﴾ [النور: 22-25]

"Wala wasiape watu wema katika Dini na wakunjufu wa mali kuacha kuwaunga watu wao wa karibu wasiokuwa na kitu na wahitaji na wageni waliokula makwao na kuwanyima matumizi kwa sababu kuna kosa walilifanya. Basi na wayasamehe maovu yao wala wasiwatese. Kwani nyinyi hamupendi Mwenyezi Mungu Awasamehe? Basi wasameheni. Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwasamehe waja Wake, ni Mwenye huruma kwao. Katika haya pana mahimizo juu ya kusamehe na kusahau kabisa, hata kama mtu atatendewa uovu. Kwa kweli wale wanaowasingizia kitendo cha uzinifu wanawake wenye kujihifadhi, wasiofikiria machafu na walio Waumini ambao halijawapitia jambo hilo kwenye nyoyo zao, hao ni wenye kufukuzwa kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu ,duniani na Akhera, na watapata adhabu kubwa kwenye moto wa Jahanamu. Kwenye aya hii kuna ushahidi juu ya ukafiri wa mwenye kumtukana au kumtuhumu mke yoyote kati ya wake za Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kwa jambo ovu lolote. Hiyo ndiyo adhabu ya Siku ya Kiyama, siku ambayo ndimi zao zitatoa ushahidi kinyume na wao kwa yale ambayo hizo ndimi zimeyatamka, na itazungumza mikono yao na miguu yao kuhusu yale ambayo hiyo mikono na miguu iliyatenda. Katika siku hiyo, Mwenyezi Mungu Atawalipa malipo yao kamili juu ya matendo yao kwa usawa, na watajua kwenye mkusanyiko huo mkubwa wa kisimamo kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Ukweli ulio wazi, Ambaye Yeye ni kweli, ahadi yake ni ya kweli, makemeo yake ni kweli na kila kitu kitokanao na yeye ni kweli, Ambaye hamdhulumu yoyote chochote hata kama ni kadiri ya uzani wa chungu mdogo". [Al-Nnuur:22-25] Na qura'ni ikaweka

mkazo juu ya kufanya wema katika kuamiliana pamoja na jirani na kumfanyia wema yeye,⁵⁹²kama alivyo sema ALLAH Mtukufu:

﴿وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْبِتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَالْحَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْحَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا﴾ [النساء: 36]

"Na muabuduni ALLAH na wala msimshirikisha na kitu chochote na wazazi wawili muwafanyie wema na ndugu wa karibu na mayatima na masikini na jirani wakaribu na jirani wa ubavuni na jamaa wa pembeni na mpita njia na vijakazi wenu hakika ALLAH hapendi kila mwenye kujidai kwa kujifakharisha". [An Nisaai: 36]. Kama alivyosema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- (Yeyote mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi na asimuudhi jirani yake)(1286) Na amesema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Hakuacha Jibril kuendelea kunihusia kuhusu jirani mpaka nikadhania kwamba yeye atamrithisha". Kama alivyosema Mtume - Sala na Amani ziwe juu yake- ((Namuapia ALLAH hatu kuwa na Imani namuapia ALLAH hatu kuwa na Imani,ikasemwa nani huyo ewe Mtume wa ALLAH?Akasema:mtu ambaye jirani yake hatu pata Amani kutokana na vitimbi vyake))⁵⁹³Na jambo halikuishia kwa waislamu bali lilivuka na kwenda kwa wengine katika jambo ambalo

⁵⁹² Ameweka Bukhari katika sahih yake,mlango unaohusu kumfanyia uasi jirani,juzuu ya 7/78,nayo ni Hadithi waliokubaliana Bukhari na Muslimu kuhusu usahihi wake.

⁵⁹³ Ameipokea Bukhari katika sahihi yake,Babu man kaana yu'umini nu billahi walyaumi Al'akhiri falaa ju'dhi jaarahu,juzuu ya 7/78,na Hadithi wakubaliana Bukhari na Muslim.

lipo wazi kwenye uzuri wa kuamiliana pamoja nao,na ikiwa ni wenye Salama katika maneno yake mtukufu:

﴿لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ﴾ إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٥﴾ [الممتحنة: 8-9]

"Mwenyezi Mungu Hawakatazi nyinyi, enyi Waumini, kuwakirimu kwa wema makafiri ambao hawakuwapiga nyinyi vita kwa ajili ya dini wala hawakuwatoa kutoka majumbani mwenu, na kuwafanyia usawa kwa hisani yenu na wema wenu kwao, kwani Mwenyezi Mungu Anawapenda wale wanaofanya uadilifu katika maneno yao na matendo yao. Hakika Mwenyezi Mungu Anawakataza, kuhusu wale waliowapiga vita kwa ajili ya dini na wakawatoa majumbani mwenu na wakawasaidia makafiri kuwatoa nyinyi, kufanya urafiki nao kwa kusaidiana na kupendana. Na yoyote anayewachukua wao kuwa ni wasaidizi dhidi ya Waumini na ni vipenzi, basi wao ndio madhalimu wa nafsi zao, wenye kutoka nje ya mipaka ya Mwenyezi Mungu." (Al-mumutahina:8-9).⁵⁹⁴

Na kwa hakika Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-aliamrisha kuwafanyia wema mateka wenye kupigana miongoni mwa Maadui katika maneno yake aliposema:

⁵⁹⁴ Ameweka Bukhari katika sahihi yake,Babu Alwaswaat biljaar,juzuu ya 7/78,nayo ni Hadithi waliokubaliana Bukhari na Muslimu kuhusu usahihi wake.

﴿وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكْرًا ﴿١﴾ [الإنسان: 8-9]

"Na wanalisha chakula, pamoja na kuwa wanakipenda na kukihitajia, kumpa fukara asiyeweza kuchuma, asiyemiliki chochote katika vitu vya kilimwengu, na kumpa mtoto aliyefiliwa na babake kabla ya kubaleghe na asiye na mali, na kumpa mtu aliyetekwa vitani miongoni mwa washirikina na wengineo, na huku wanasema katika nafsi zao, «Hakika sisi tunawafanyia wema kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na kutaka malipo yake. Hatutaki badala wala hatukusudii kushukuriwa wala kusifiwa na nyinyi" (Al-insaan:8-9).

Na hakika ameamrisha Mtume sala na amani ziwe juu yake kufanya wema kwa Mateka wa Badr na wengineo miongoni mwa washirikina, Wakawa Waislamu wakiwapa chakula ambavyo wana vyakula na wakiwafanyia muamala mzuri miongoni mwa mambo yaliyo acha alama na ikapelekea kuingia ndani ya Uislamu baada ya hapo.⁵⁹⁵

Na miongoni mwa tabia nzuri ambazo zilijenga umma ni Ukarimu na Utoaji.1290]Na ilifahamika Utoaji kwa Umma kwa tabaka zote, na miongoni mwa huwo Utoaji wa kimali sawa sawa iwe kwenye Zaka au Sadaka ambazo zilizo kusanywa pamoja na swala katika sehemu nyingi, miongoni mwazo ni kauli ya ALLAH Mtukufu:

⁵⁹⁵ angalia :Vita vya Badr, kwenye kitabu hiki.

﴿إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴿١٩﴾ إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ﴿٢٠﴾ وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٢١﴾ إِلَّا الْمُصَلِّينَ ﴿٢٢﴾ الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ﴿٢٣﴾ وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٢٤﴾ لِلسَّائِلِ
وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٥﴾ وَالَّذِينَ يُصَدِّقُونَ بَيْنَ الَّذِينَ بَيْنَهُمُ ﴿٢٦﴾﴾ [المعارج:19-26]

"Hakika binadamu ameumbwa akiwa na tabia ya babaiko na pupa. Likimpata jambo baya, anababaika sana na kufa moyo. Na yakimpata mambo mazuri na ukunjufu wa maisha, huwa ni mwingi wa kuzuia na. Isipokuwa wenye kuswali wanaochunga kuitekeleza katika nyakati zake zote, hakuna shughuli yoyote inayowashughulisha nayo. Na wale ambao katika mali yao kuna fungu maalumu alililowafaradhia Mwenyezi Mungu, nalo ni Zaka Kwa wenye kuomba na wasioomba)(25) Na wale ambao wanaiamini Siku ya kuhesabiwa". (Al-Maarij:19-26) Na katika kauli yake Mtukufu:

﴿فَأَمَّا مَنْ أَعْطَى وَاتَّقَى ﴿٥﴾ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَى ﴿٦﴾ فَسَنِيَرُهُ لِلْيُسْرَى ﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنْ بَخِلَ
وَاسْتَغْنَى ﴿٨﴾ وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَى ﴿٩﴾ فَسَنِيَرُهُ لِلْعُسْرَى ﴿١٠﴾ وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ﴿١١﴾ إِنَّ عَلَيْنَا
لَلْهُدَى ﴿١٢﴾ وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَى ﴿١٣﴾﴾ [الليل: 5-13]

"Basi, ama mwenye kutoa na akamchamungu* "Na akaliafiki lilojema* Basi tutamfanyia wepesi. Ama yule ambaye atafanya Ubakhili na asiwe na haja na viumbe wenzake Na akakadhibisha mambo mema na asiyafanye tutamsahilishia njia ya kwenda motoni. Wala hayatamfaa yeye mali yake aliyoyafanyia ubakhili atakapotumbukia Motoni. Na ni juu yetu kuwabainishia njia ya kheri na njia ya shari Na ni yetu sisi Akhera na Dunia" (Al-lail:5-13) Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَأَنْفُسِكُمْ وَمَا
تُنْفِقُونَ إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُؤْتِ إِيَّكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَظْلَمُونَ ﴿٢٧﴾﴾ [البقرة:

[272

"Si jukumu lako, ewe Mtume, kuwapa makafiri taufiki ya uongofu, lakini Mwenyezi Mungu Anavifungua vifua vya Anaowataka kwa Dini Yake na kuwaafikia kuifuata. Na mali yoyote mnayoyotoa, nafuu yake itawarudia nyinyi wenyewe kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Waumini hawatoi isipokuwa kwa kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Na mali yoyote mnayoyotoa, kwa kumtakasia Mwenyezi Mungu, mtapewa kikamilifu thawabu zake na hamtapunguziwa chochote katika hizo". (Baqarat :272) Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنْفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمْ يَوْمٌ لَا بَيْعٌ فِيهِ وَلَا حُلَّةٌ وَلَا شَفَاعَةٌ وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴾ [البقرة: 254]

"Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na kumsadiki Mtume Wake na kufanya amali zinazoambatana na uongofu Wake! Toeni Zaka zilizofaradhiwa na mtoe sadaka ya vitu mlivyopewa na Mwenyezi Mungu kabla haijaja Siku ya Kiyama, wakati ambapo hakuna kuuziana ikapatikana faida, wala mali ambayo nyinyi mtajikomboa nayo nafsi zenu kutokana na adhabu ya Mwenyezi Mungu, wala urafiki wa rafiki wenye kuwaokoa, wala muombezi anayemiliki kuwafanya mpunguziwe adhabu. Na makafiri ndio madhalimu na wakeukaji mipaka ya Mwenyezi Mungu". [Al baqara: 254]. Na katika Hadithi Tukufu akasema Mtume -*Rehema na amani ziwe juu yake*- ((Kwa hakika Mwenyezi mungu ni Mkarimu na Anapenda Ukarimu))(1291) Na katika njia ya kuwaweka mbali watu na Vinyongo na uhasidi na kuwa mbali na mauwaji kwa ajaili ya mali,amesema Mtume -*Rehema na amani ziwe juu yake*- ((Ugopeni Ubakhili kwa hakika waliangamia waliokuwa kabla yenu,iliwapelekea kumwaga Damu zao na kuhalalisha yaliyokuwa haramu kwao))(1292)

Hakika maelekezo haya yaliyo mazuri ni kwa ajili ya kujenga umma na jamii yake juu uzuri wa utoaji alikuwa Mtume sala na

amani ziwe juu yake akihimiza kipindi cha uhai wake na mwenendo wake,mpaka akafahamika kuwa yeye ni mkarimu kwa watu walio juu ya mgongo wa Ardhi,namna alivyo kuwa akihimiza kutoa sadaka hata kama itakuwa ni chache. Uogopeni moto hata kwa kipande cha tende Na kwa hakika walikuwa waislamu katika zama zake wakishindana katika utowaji wa sadaka na kutowa kwa wenye kuhitajia miongoni mwa waislamu.na kuandaa wanajeshi wao na kuwakirimu wageni wake -**Rehema na amani ziwe juu yake**-na anakuja wa mwanzo katika hawa ambaye ni Uthman Bin Affan-Radhi zaAllah ziwe juu yake-ambaye aliliandaa jeshi wakati wa hali ngumu(1294)

Kama ambavyo ilikuwa kutekeleza Ahadi ni katika Tabia muhimu za Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na waislamu wote kwa ujumla mtume aliitekeleza kwenye maisha yake pamoja na marafiki zake na maadui zake.

﴿لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ
الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالرَّبِّينِ وَأَتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ
السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا
وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ﴾
[البقرة: 177]

"Hapana kheri, mbele ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, kuelekea kwenye Swala upande wa mashariki na magharibi, iwapo hilo halitokamani na amri ya Mwenyezi Mungu na sheria Yake. Hakika kheri yote iko katika imani ya aliyemuamini Mwenyezi Mungu na akamkubali kuwa Ndiye muabudiwa, Peke Yake, Hana mshirika Wake, na akaiamini Siku ya kufufuliwa na Malipo, na akawaamini Malaika wote na vitabu vyote vilivyoteremshwa, na Mitume wote bila kubagua, na akatoa mali yake kwa hiyari yake, pamoja na kuwa anaipenda sana, kuwapa jamaa zake na

mayatima wenye uhitaji waliofiliwa na wazazi wao hali wao wako chini ya umri wa kubaleghe, na akawapa masikini ambao ufukara umewaelemea, na wasafiri wanaohitaji walio mbali na watu wao na mali yao, na waombaji ambao imekuwa ni dharura kwao kuomba kwa uhitaji wao mkubwa, na akatoa mali yake katika kuwakomboa watumwa na mateka, na akasimamisha Swala na akatoa zaka za faradhi, na wale wenye kutekeleza ahadi, na mwenye kusubiri katika hali ya ufukara wake na ugonjwa wake na katika vita vikali. Hao wenye kusifika kwa sifa hizo, ndio waliokuwa wakweli katika imani zao, na wao ndio waliojikinga na mateso ya Mwenyezi Mungu wakajiepusha na vitendo vya kumuasi". [Al Baqara: 177]. Na kauli ya Allah Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَوْفُوا بِالْعُقُودِ أُحِلَّتْ لَكُمْ بَهِيمَةُ الْأَنْعَامِ إِلَّا مَا يُتْلَى عَلَيْكُمْ غَيْرَ مُحِلِّي الصَّيْدِ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ مَا يُرِيدُ﴾ [المائدة: 1]

"Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkazifuata sheria Zake kivitendo, timizeni ahadi za Mwenyezi Mungu zilizotiliwa mkazo za kuamini Sheria za Dini na kuzifuata, na tekelezeni ahadi mlizopeana nyinyi kwa nyinyi miongoni mwa amana mlizowekeana, biashara na mengineyo kati ya yale yasiyoenda kinyume na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtume Wake Muhammad , rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Na hakika Mwenyezi Mungu Amewahalalishia wanyama wa mifugo, nao ni ngamia, ng'ombe na mbuzi na kondoo, isipokuwa yale ambayo Mwenyezi Mungu amewaelezea ya kuwaharamishia mfu, damu na mengineyo; na ya kuwaharamishia kuwinda mkiwa kwenye hali ya ihramu (kwa ibada ya Hija au Umra). Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anahukumumu Anachokitaka kulingana na hekima Yake na uadilifu Wake". (Al-maidah:1) Kama ilivyo kuwa kutekeleza amana ni miongoni mwa mambo ya msingi ya kitabia ambayo iliyo jengewa nayo Uislamu:

﴿إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ يَحْمِلْنَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا
الْإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا﴾ [الأحزاب: 72]

"Sisi tuliiorodhesha amana- ambayo Mwenyezi Mungu Amewapatia waliokalifishwa na Sheria waitunze, nayo ni kufuata maamrishi na kujiepusha na makatazo- kwa mbingu, ardhi na majabali, vikakataa kuibeba na vikaogopa visiweze kusimama kuitekeleza, na akaibeba binadamu na akashikamana nayo pamoja na udhaifu Wake. Hakika yeye ni mwingi wa udhalimu na ujinga wa nafsi yake". [Al-Ahzab:72] Na alikuwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake akipigiwa mifano kwa Maqurayshi kabla ya kupewa Utume na baada yakempaka wao walikuwa wakimuita Mkweli Muaminifu, Na alikuwa mkweli kwa mwenendo wake na Tabia zake na ALLAH akamsifu kwa tabia hizo katika kauli yake:

﴿وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ﴾ [الزمر: 33]

"Na yule aliyekuja na ukweli wa maneno na vitendo, miongoni mwa Manabii na wafuasi wao, na akaukubali kiimani na kivitendo, hao ndio waliokusanya sifa za uchamungu, akiwa mbele yao yule aliye mwisho wa Manabii na Mitume, Muhammad, rehemama ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na wale wenye kumuamini, wanaoifuata Sheria yake kivitendo miongoni mwa Maswahaba, radhi za Mwenyezi Mungu ziwashukie, kisha wale wenye kuja baada yao mpaka Siku ya Malipo". (Al-zumar:33) Na alikuwa Mtume-Rehemama na amani ziwe juu yake-akihimiza ukweli na akiamrisha na akiwalea watu kwenye ukweli akasema: Kutoka kwa Abdillah bin Mas'udi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Amesema: Amesema Mtume -Rehemama na Amani ziwe juu yake-: "Shikamaneni na ukweli, kwani ukweli hupelekea katika wema, na hakika wema hupelekea katika pepo, na hatoacha mtu kuwa mkweli na akishughulika na ukweli mpaka ataandikwa kwa Mwenyezi Mungu kuwa ni mkweli, na tahadharini na uongo, kwani uongo

unapelekea katika uovu, na hakika uovu hupelekea katika moto, na hatoacha mtu kuendelea kuwa muongo, na akishughulika na uongo mpaka ataandikwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa ni muongo". Kama alivyootahadharisha Mtume-Rehema na amni ziwe juu yake--((Alama za Mtu muongo ni tatu,akiongea anasema uongo,akiahidi hatekelezi,na akiaminiwa anafanya khiyana))

Na kwenye sehemu za kitabia za kijamii za kifamilia,Hakika Uislamu ulizingatia kuijenga jamii hali ya kuchukua katika kudhania kutokea tofauti,na kuingiliana mafungamano,kwa hiyo ilikuja sharia na utendaji kazi wake katika sehemu za hali za watu na sheria za kifamilia kwa kile ambacho kuna mafungamano ya Ndoa na Talaqa na yale ambayo yanayo ambatana nayo yanaonekana,na Matumizi na kistareheshaji na malezi na tabiya na uwangalizi na usimamizi,na ukaweka Haki za wazi na Mipaka yenye kuchunga kila upande,Asidhulumiwe yeyote,Na asipatikane yeyote akachupa mipaka kwa yeyote juu ya haki.

Na akawatahadharisha waislamu kutoziharibu nidhamu hizo na kanuni za Mwenyezi Mungu.na huenda yaliyokuja katika Suratil Baqaa ni miongoni mwa hizo hukumu na zinazo weka wazi Nidhamu ya hali ya juu kutoka katika Aya(226)kutoka katika Suratil Baqarat mpaka aya ya (237)katika sura hiyohiyo

Na hakika zimekuja Kanuni nyingine tofauti upande wa yale ambayo yanayo fungamanisha Ndoa kwa kuanzia Uchumba mpaka kuachana na zikaamrisha wana ndoa kwa kuishi kwa wema.

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا يَجِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا النِّسَاءَ كَرِهًا وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَا آتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ فَإِنْ كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا ﴿١٩﴾ [النساء: 19]

"Enyi mlio amini, haifai kwenu kuwafanya wake wa baba zenu ni miongoni mwa mali yalioachwa kurithiwa, mkawa mnafanya

mtakavyo kwao: kwa kuwaoa, kuwakataza wasiolewe au kuwaoza waume wengine, hali ya kuwa wao hawayataki hayo yote. Na pia haifai kwenu kuwadhuru wake zenu kwa kuwa mnawachukia, ili wapate kusamehe baadhi ya mlivyowapa, mahari au vinginevyo. Isipokuwa wakiwa wamefanya jambo ovu, kama uzinifu, hapo mnayo nafasi ya kuwazuia mpaka mkitwae mlichowapa. Na kule kukaa kwenu na wake zenu yatakikana kuwe ni juu ya misingi ya heshima na mapenzi na kuwatekelezea haki zao. Na iwapo mtawachukia kwa sababu yoyote katika sababu za kidunia, basi kuweni na subira. Kwani huenda mkachukia jambo, miongoni mwa mambo, na ikawa ndani yake muna kheri nyingi". [An-Saai:19] Na imeitwa Surat Nisaa, ili kuwapa heshima yao kwenye mtazamo wa jamii, kama ambavyo sheria ilimfanya mwanamke ni muwakilishi wa mama ni mtu wa Thamani zaidi na mwenye haki ya kufanyiwa wema mbele ya mwanadamu, na ikayafanya maisha ya unyumba ni yenye kujengwa na mapenzi na huruma na utulivu, nayo ni maana kubwa sana katika mapenzi:

﴿وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً
 وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ﴾ [الروم: 21]

"Na miongoni mwa dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu ni uumbaji mbingu na kuwa juu kwake bila ya nguzo, na uumbaji ardhi ikiwa imekunjuka na kupanuka, na kutafautiana lugha zenu na kuwa mbalimbali rangi zenu. Hakika katika hayo kuna mazingatio kwa kila mwenye elimu na busara". (Al-ruum:21) Na aliamrisha kwa kumpenda mwenzi wake na mwanamke akaamrisha kumtii mume wake(1297) na kwa hakika imekuja sheria kuharamisha mahusiano ya kijinsia na yenye kupelekea kwenye hayo mahusiano yaliyo nje ya utaratibu wa wanandoa, kwa kuwa kufanya hivyo ni kumfanyia kosa mtoto kwa kumnasibisha na asiye kuwa Baba yake na kupelekea kudhoofisha mafungamano ya Kindoa, na wanawake kuwakosea waume zao na waume kuwakosea

wake zao,na pia ikichangia Maradhi ya Mwili,na sheria ikaihesabu Zinaa ni katika madhambi makubwa,bali ikamuamrisha mwanaume na mwanamke kuinamisha macho,na wasimwangelie isipokuwa yule waliohalalishiwa na mwenyezi mungu katika wake na wale wanawake ambao ni Haramu kuwaoa.

﴿قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَعْضُوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَلِكَ أَزْكَ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ﴾ وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي أَخَوَاتِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوِ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولِي الْإِرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا عَلَىٰ عَوْرَاتِ النِّسَاءِ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِنْ زِينَتِهِنَّ وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾ [النور: 30-31]

"Waambie waumini wa kiume wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao kufanya hivyo ndio usafi kwao hakika ALLAH ni mjuzi wa wanayo yafanya. Na waambie waumini wa kike wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao na wasizihirishe mapambo yao isipokuwa yalio onekana kwenye hayo mapambo na wajifunike shungi zao mpaka juu ya shingo zao na wala wasizihirishe mapambo yao isipokuwa kwa waume zao au baba zao au baba wa waume wao au watoto wao au watoto wa waume zao na kaka zao watoto wa kaka zao au dada zao au wanawake wao au watumwa wao au wale wanaume wanao wafatia wasio kuwa na matamano au watoto ambao wasio tambua tupu za wanawake na wala wasipige migu yao ili ionekane yaliyo jificha kutokana na mapambo yao na tubieni kwa ALLAH nyote kwa pamoja enye waumini ili mpate kufaulu". An-nuur:30-31

Na hizi Aya zimekusanya Tabia ambazo zinamfanya mwanaume hamtazami isipokuwa mke wake na vilevile mke,na kutazama

wengine hakufai ili kumuweka wanadamu mbali na sababu ambazo zitapelekea mahusiano yaliyo haramu,na jambo hilo ni kinga ya kwanza na Tiba ya kuleta uaminifu kati ya wanyumba wawili.

Na katika wakati ambao mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alipojenga Jamii ya kiislamu kwenye Tabia iliyo bora kwa hakika alitahadharisha Tabia iliyo mbaya ,na miongoni mwayo ni kuwadhulumu watu kwenye maneno yake Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿فَقَدْ كَذَّبْتُمْ بِمَا تَقُولُونَ فَمَا تَسْتَطِيعُونَ صَرْفًا وَلَا نَصْرًا وَمَنْ يَظْلِمِ مِنْكُمْ نُذِقْهُ عَذَابًا كَبِيرًا﴾ [الفرقان: 19]

"Hapo waambiwe washirikina, «Kwa kweli, wamewakanusha nyinyi, hawa mliowaabudu kwenye madai yenu juu yao. Enyi hawa, nyinyi hamuwezi kuzikinga nafsi zenu na adhabu wala kuziokoa. Na mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu, akajidhulumu nafsi yake, akamuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu na akafa katika hali hiyo, mwenyezi Mungu Atamuadhibu adhabu kali". (Al-Furqaan:19) Na amesema Rehema na Amani ziwe juu yake: "Na ogopa maombi ya aliyedhulumiwa, kwani hayo hayana kizuizi kati yake na Mwenyezi Mungu". kama ambavyo ameliashiria hilo kwenye maneno yake mtukufu:

﴿أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَى مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ فَقَدْ آتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَآتَيْنَاهُمْ مُلْكًا عَظِيمًا﴾ [النساء: 54]

" Au je, kwani wao wanamuhusudu Muhammad , rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie kwa neema za unabii na utume alizopewa na Mwenyezi Mungu na kuwahusudu Masahaba wake kwa neema ya kuongozwa kwenye Imani, kuukubali utume, kumfuata Mtume na kupewa uwezo katika ardhi, wakawa wanatamani neema hizi ziwaondokee? Hakika sisi tuliwapa watu

wa kizazi cha Ibrāhīm, amani imshukie, Vitabu Alivyoviteremsha Mwenyezi Mungu kwao, wahyi mwingine usiokuwa kitabu chenye kusomwa na tukawapa , pamoja na hayo, utawala wenye kuenea". [An Nisaai: 54]. Kama alivyotahadharisha kuhusu Kughushi akasema: {Yeyote atakae tufanyia ghushi mtu huyo siye katika sisi} Na kwa hakika Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-Kujionyesha kama ilivyokuja katika neno lake Mwenyezi mungu Mtukufu:

﴿قَوْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ۝ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ۝ الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ۝ وَيَمْنَعُونَ

الْمَاعُونَ ۝﴾ [الماعون: 4-7]

"Adhabu kali itawathibitikia wenye kusali(4) ambao wameghafilika na Swala zao: hawazisimamishi kama ipasavyo wala hawazisali kwa nyakati zake. "Ambao huonyesha watu amali zao za kheri kwa njia ya ria." "Na wanazuia misaada" (Al- maaun:4-7)

Na ametahadharisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-Kujionyesha na akasema: ((Kwa hakika jambo ambalo nalikhofia zaidi kwenu nyinyi ni Shirik ndogo,wakasema,na ni ipi Shiriki Ndogo ewe mtume wa Mwenyezi Mungu?akasema ni Kujionyesha))(1300) Kama alivyokataza kudanganyika na kujiona mwenyewe na ni katika mambo yenye kuangamiza sana,kama alivyosema Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- ((Mambo matatu ni yenye kuangamiza,Ubakhili wenye kutiwa,na matamania yenye kufuatwa,na mtu kujisikia na kujiona mwenyewe))(1301) Na kwa hakika aliamrisha Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-yakuwa Mwanadamu asidanganyike kwa mali zake au Ibada zake au Nguvu zake au utukufu wake au kazi zake,na kwa hakika ameamrisha mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-kuwa mwanadamu asidanganyike na chochote katika hivyo kama alivyosema mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- Fanyeni matendo na muwe na msimamo, na tambueni kuwa hatosalimika mmoja wenu kwasababu ya matendo yake, wakasema: Hata wewe Ewe Mjumbe wa

Mwenyezi Mungu?! Akasema: Hata mimi isipokuwa atakaponifunika mimi Mwenyezi Mungu kwa huruma zake na fadhila zake

Kama alivyokuwa mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- akichukia uvivu na akijilinda na uvivu katika maneno yake: ((Ewe mola wangu wa haki hakika mimi najilinda kwako kutokana na Kushindwa na uvivu na uoga na uzee ulio mbaya na Ubakhili))(1303)

Na huenda miongoni mwa mambo ambayo uislamu umeyapa kipaumbele kwa ajili ya jamii ya wanadamu ni kutilia umuhimu wakati na mpangilio wake,na kutofautisha kati ya matendo ya mchana na utulivu wa usiku,na kutumia muda kwa mambo yenye manufaa kutopoteza wakati kwa mambo yasiyokuwa na manufaa na kwenye kugawanya muda wa swala na kuupangilia kwa kina kunaonyesha wazi kuwa uislamu umetilia umuhimnu wakati ambao ndiyo maisha ya Mwanadamu na ndiyo msaada wake katika kugawanya Dakika za siku yake na anayofungamana nayo miongoni mwa Ibada na kazi,na hitajio la kujipumzisha na haki ya mwanadamu mwenyewe katika huu utaratibu, ni kama haki ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake katika kutilia umuhimu katika Ibada na kupangilia muda wake.

Na kutokana na uwazi kwa kila mwenye akili timamu kuwa sheria hizi na utendaji kazi wa kitabia katika zama za Mtume sala na Amani ziwe juu yake na kutokana na mwendo wake katika kuunganisha jamii na mshikamano wake,na mapenzi yake kwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake na kwa yale aliyo yawekeka ALLAH sheria .

Na wala Athari ya hiyo sheria haikuishia katika zama zile tu ,bali Baraka zake zilienea katika Umma na kwa wanadamu mpaka hivi sasa.

Uundaji Jeshi(1304)

Alianza Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-Da'awa yake katika mji wa Makkah na akaidhihirisha baada ya muda unaokaribia miaka mitatu tangu kupewa utume,na maudhi mengi yalimpata kutoka kwa maquraish,kama ambavyo walipata maswahaba wake maudhi makubwa mpaka baadhi yao wakauwawa kutokana na adhabu kali,mfano wa ni Ammar na Sumaiyyat.

Na alikuwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake akiwatuliza na akiwaombea wao na akiwaamrisha kuwa na Subra na akiwaahidi kupata Ushindi na Utulivu,na akiwakataza kupigana.

Na baada ya kusilimu Omar Ibn Alkhatwab na Hamza Ibn Abdil Mutwalib Uislamu ulipata nguvu,pamoja na hayo hawakupewa Amri ya kupigana,na wala Udhia haukusimama kuto wapata Waislamu kwa jumla wao wala kunako Mtume sala na amani ziwe juu yake yeye kama yeye,mpaka Maqurayshi walijaribu kumuua Mtume usiku alio kuwa anahamia Madinah ALLAH akamkinga na shari zao.

Na baada ya kuhama Mtume sala na amani ziwe juu yake kwenda Madinah na wale alio kuwa nao miongoni mwa walio hama na kujiunga kwao na Maanswar wakiwa ndani ya nyumba ya kuhamia[Daarul Hijra] wakawa wenye idadi kubwa na nguvu,pamoja na yote hayo hawakupewa amri ya kupigana kwa kipindi cha mwanzo,pamoja na kuwa mkusanyiko walikuwa ni wenye kujiandaa kwa yale aliyo waamrisha Mtume sala na Amani ziwe juu yake,alikuja mzungumzaji wa Maanswar pindi walipo mpa Mtume kiapo cha utiifu kwenye kizingiti kwa mara ya pili,na wakasema: ((Tunamuapia yule aliye kutuma kwa haki ukitaka hakika tutawaendea watu wa Mina kesho na panga zetu Mtume sala na amani ziwe juu yake akajibu: sija amrisha kwa hilo lakini rudini kwenye miji yenu))1305]

Walikuwa Muhajirina wote kwa pamoja na Maanswar ni Watu mashujaa wa Vita wenye kupambanulika kwa hilo,na ikaongezeka idadi yao na ikapata nguvu ule umoja wao na wakawa wapo kwenye maandalizi ya vita kwa amri ya Mtume sala na amani ziwe juu yake,na zilikuja aya nyingi za qurani zikiwapa idhini wao ya kupigana kwa ajili ya kuondosha dhulma kunako nafsi za o,na uendeleo uwezo huo kwa maswahaba pamoja na kuendelea baada ya hapo katika kukuza zile nguvu zenye kukua ikateremka kauli ya ALLAH Mtukufu:

﴿أَذِّنْ لِلَّذِينَ يُقَاتِلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلُمُوا وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَهَدَمَتْ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدٌ يُذْكَرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾ الَّذِينَ إِنْ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ وَلِلَّهِ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ ﴿٤١﴾﴾ [الحج: 39-41]

Waislamu, mwanzo wao, walikuwa wamekatazwa kupigana na makafiri, wameamrisha kuvumilia maudhi yao. Maudhi ya washirikina yalipofikia upeo wake na Mtume akatoka Makkah hali ya kurudi kwenda Madina na Uislamu ukawa na nguvu, Mwenyezi Mungu Aliwaruhusu Waislamu kupigana kwa sababu hiyo ya maonevu yaliyowashukia na uadui. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwanusuru na kuwadhalilisha maadui wao. "Wale ambao walilazimishwa kutoka majumbani mwao, si kwa lolote isipokuwa ni kwa kuwa wamesilimu na wamesema, «Mola wetu ni Mwenyezi Mungu Peke Yake.» Na lau si mpango Aliouweka Mwenyezi Mungu wa kuondoa maonevu ambayo kwayo wananufaika watu wa dini zote zilizoteremshwa na kuurudisha ubatilifu kwa kuruhusu kupigana, haki ingalishindwa katika kila umma, ardhi ingaliharibiwa, sehemu za ibada zingalivunjwa, miongoni mwa mahekalu ya watawa, makanisa ya Wanaswara, majumba ya ibada ya Mayahudi na misikiti ya Waislamu ambayo

Wanaswali ndani yake, na wanamtaja Mwenyezi Mungu humo kwa wingi. Na mwenye kufanya bidii kuitetea Dini ya Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu Atamnusuru juu ya adui yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Asiyeshindwa, ni Mshindi Asiyefikiwa, Amewatenga nguvu viumbe na Amezishika paa za nyuso zao." Wale tuliowaahidi kuwa tutawanusuru ndio wale tukiwapa utulivu kwenye ardhi na kuwatawalisha humo kwa kuwapa ushindi juu ya adui wao, wanasimamisha Swala kwa kuiitekeleza kwa nyakati zake kwa namna zake, wanatoa Zaka za mali zao kuwapa wastahiki wake, wanaamrisha kila ambalo Mwenyezi Mungu Ameliamrisha la haki Zake na haki za waja Wake na wanakataza kila ambalo Mwenyezi Mungu Amelikataza na Mtume Wake. Na ni wa Mwenyezi Mungu Peke Yake mwisho wa mambo yote, na mwisho mwema ni wa uchamungu. Al-Haji:39-41] Na ikateremka baada ya hapo sura ya Al-Anfaal ambayo ilijulikana kuwa ni Sura ya Vita, na ndani yake kuna sheria kubwa ya kujitolea na zikafuatana Aya baada ya hapo kwa lengo la kukuza nguvu na kujiandaa kwa Waislamu na miongoni mwazo:

﴿وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْحَيْلِ تُرْهَبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ
وَأَخْرَيْنَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ
وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ﴾ [الأنفال: 60]

Na Tayarisheni, enyi makundi ya Waislamu, ili kukabiliana na maadui wenu, chochote mkiwezacho cha wingi wa watu na zana, ili muingize, vitisho katika nyoyo za maadui wa Mwenyezi mungu na maadui wenu wanaowavizia; na muwatishe wengine ambao uadui wao bado haujajitokeza kwenu hivi sasa, lakini Mwenyezi Mungu Anawajua na Anayajua yale ambayo wanayadhamiria. Na mali yoyote na vinginevyo mnavyovitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, vingi au vichache, Mwenyezi Mungu Atawapa badala yake duniani na Atawaeke thawabu zake mpaka Siku ya Kiyama; na

nyinyi hamtapunguziwa malipo ya hayo chochote. Al-Anfaal:60] Na Aya zikatilia mkazo juu ya uzuri wa mwendo wa mashahidi mbele ya ALLAH katika kauli yake:

﴿وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٩﴾ فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَيَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِمْ مِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٧٠﴾﴾ [آل عمران: 169-170]

Wala usidhani, ewe Mtume, kwamba wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu ni wafu hawahisi chochote. Bali wao wako hai uhai wa barzakh kwenye ujirani wa Mola wao Ambaye walipigana jihadi kwa ajili Yake na wakafa katika njia Yake, inawapitia riziki yao huko Peponi na wananeemeshwa. Furaha iliwaenea, wakati Mola wao Alipowaneemeshwa na kuwapa neema na radhi zenye kuwaliwaza macho yao, zikiwa ni miongoni mwa ukarimu Wake na takrima Yake. Watakuwa wakiwafurahia ndugu zao wenye kupigana jihadi waliowaacha duniani wakiwa hai, wakiwatarajia wafaulu kama walivyofaulu wao. Kwa kuwa wao waelewa kwamba hao ndugu zao, waliowaacha duniani wakiwa hai, watapata heri waliyoipata wao, iwapo watakufa mashahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu hali ya kumtakasia Yeye, na kwamba hawatakuwa na chochote cha kuogopa kuhusu mambo ya mustakbali wao huku Akhera wanayoyakabili wala hawatakuwa na huzuni juu ya yale yaliyowapita wakayakosa ya hadhi za kilimwengu. Al-Imran:169-170] Na kama zilivyo tilia mkazo Aya nyingine juu ya umuhimu wa kujitolea(jihad) bila ya kuchupa mipaka:

﴿وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿١٩٠﴾﴾ [البقرة: 190]

Na wapigeni katika njia ya ALLAH wale wanao kupigeni na wala msivuke mipaka hakika ALLAH hapendi wanao vuka mipaka. [Al-baqara: 190]

Na zikafuatia sheria katika sehemu za kuwapiga vita Washirikina na Makafiri maisha mazima ya Mtume sala na amani ziwe juu yake na zikapata hukumu za jihadi nafasi zake kwa wanazuoni wa sheria mpaka vikatungwa kwa jambo hilo vitabu na milango mahususi na Ufahamu wa Jihad.⁵⁹⁶

Nahakika ilikuwa uwekaji wa jeshi la Mtume sala na amani ziwe juu yake ni kwa upana, ulio pangika wenye nguvu, kwa upatikanaji wa silaha na kuandaa kwa mtu mmoja mmoja kwa kawaida, na hakika alitegemea Mtume sala na amani ziwe juu yake juu utaratibu wa juu kwa kuandaa nguvu zake na jeshi lake, na pamoja na yote hayo ni kuendelea kuwapa mazoezi na matendo ya kweli kwa maswahaba kipindi anapo tuma kikosi kazi ambacho alikituma kutoka Madinah. Na walikuwa watu wa Madinah wakisimama kidete kwa kazi za kijeshi zenye malengo na njia na owongozi, baadhi yake ikiwa ni kwa ajili ya kazi za kijeshi, na baadhi ya yake kwa ajili ya kambi za kijeshi, na baadhi yake kuwagonganisha maadui, na baadhi yake ni kukata muendelezo wao, na yote hayo ni kwa kutofautiana muelekeo wao pamoja na kuhakikisha kwake kwa ajili ya malengo yake mahususi yaliyo saidia kwenye kufunza na kukuza uwezo wa kijeshi kwa maswahaba wa Mtume sala na amani ziwe juu yake, na ikaongezeka kutokana na uwezo wao wa kivita na owongozaji na kuwavumilia kwao shida na kujiandaa kwa kujitolea na kupata shahada (kufia vitani) Maswahaba wakapigana pamoja na Mtume sala na amani ziwe juu yake katika vita vya Badr na Uhud na Khan'daq na matukio yote yalikuwa ni dhidi ya Washirikina na wasaidizi wao, mpaka ALLAH alipo ufungua mji wa Makkah, na dhidi ya Mayahud mpaka ALLAH akawatoa Madinah baada ya kufanya

⁵⁹⁶ tazama: Kurkais Awad, Misingi ya Urithi ya Kijeshi kutoka kwa Waarabu, Majmaa Al'ilimy Al'iraaqy, Baghdad, 1402 H, juzuu ya 3.

kwa hiyana,na wakaufungua mji wa Khaybar na wakaanza Waislamu kwenda njee ya kisiwa cha Waarabu katika vita vya Mu'ta,na katika vita vya Tabuk,ambavyo vilithibitisha uwezo mkubwa wa nguvu za kijeshi kidogo kidogo katika maisha ya Mtume sala na amani ziwe juu yake mpaka ikabadilisha muelekeo wa Historia ya Watu,kwa muendelezo wake katika ufunguzi mkubwa kupitia Makhalifa waongofu baada ya kufa Mtume sala na amani ziwe juu yake,kwa Usimamizi wa maswahaba zake na jeshi lake ambao Mtume alisimamia Mafunzo yao ili ALLAH awatekelezee aliyo waahidi katika kauli yake:

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾ [النور: 55]

Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini miongoni mwenu na wakafanya matendo mema kwamba atawarithisha ardhi ya washirikina na atawafanya ni wasimamizi wa hiyo ardhi, kama alivyofanya kwa waliokuja kabla yao kati ya wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, na Aifanye Dini yao ambayo Ameridhika nayo na Akawachagulia, nayo ni Uislamu, ni Dini yenye ushindi na uthabiti, na Azigeuze hali zao kwa kuwaondolea hicho na kuwaletea amani, iwapo watamuabudu Mwenyezi Mungu, Peke Yake, na watasimama imara kwa kumtii, na wasimshirikishe na kitu chochote. Na Mwenye kukanusha baada ya hilo la kupewa usimamizi, amani, uthabiti na utawala kamili, na akakanusha neema za Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waliotoka nje ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu. Al- Nuur:55

Na yawezekana kufupisha kwa kutaja vipengele muhimu katika Nidhamu za kijeshi za Dola ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-katika Nukta,miongoni mwazo ni:

*Ni kuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alikuwa akiliongoza Jeshi yeye mwenyewe na akishirikiana nao katika Jihadi na kujitolea,na kuwa yeye alipatwa na majeraha katika mwili wake,na akapigana yeye mwenyewe na akapatwa na matatizo kama walivyopatwa watu wengine miongoni mwa wanajeshi,na alikuwa akipata tabu pamoja nao,na akiwaliwaza na kuwatibu majeruhi wao,na wala hakuwa ni mwenye kiburi wala kujikweza,alikuwa ni mkunjufufu kwenye muamala wake na mpole kwa wanajeshi wake.

*Na alikuwa akichaguwa wenye kufaa katika uongozi kwa ajili ya mambo muhimu ya kijeshi,na japokuwa kulikuwepo na waliotangulia kusilimu au wenye umri mkubwa,alikuwa akimchagua kiongozi wa kuongoza watu hali yakuwa miongoni mwao kuna mtu ambaye ni mbora kuliko yeye,kwa sababu yeye alikuwa muangalifu na mwenye maono kwenye vita.(1307)

Alikuwa Mtume sala na amani ziwe juu yake hamlazimishi yeyote miongoni mwa Waislamu kujiunga na jeshi,wala hamtenzi nguvu kwa hilo,pamoja kuwa yeye alikuwa akiwapendezeshea wao kupigania kwa mali na nafsi zao,na akiwapigia wao mfano kwake mwenyewe,na akiwakumbusha ahadi za ALLAH kwa wenye kupigania kwa ujumla wao na kwa wale watakao kufa kwenye jihadi kwa umahsusi wao na ilikuwa jeshi la Mtume sala na Amani ziwe juu yake ni jeshi la juu kwenye ardhi kiukamilifu na wenye muonekano na malengo na wengi wao walikuwa ni wenye huruma kwa viumbe,na wenye hamasa kwa kutekeleza jambo la lazima.

Na walikuwa wanajeshi wote wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-ni miongoni mwa wenye kujitolea,ambao alikuwa akiwaamini kushiriki nao Jihad,na walikuwa hawasubiri malipo au ujira wa hapa Duniani,na walikuwa ni wenye majukumuya kujiandaa wao wenyewekwa Silaha na matumizi ya lazima katika msafara wa kijeshi na vikosi na Vita vya Kijihadi,wakiwa wanatafuta Radhi za mwenyezi mungu na kila mmoja akipangiwa majukumu kwa mujibu

wa uwezo wake ,miongoni mwao walikuwa wapanda farasi na wenye kutembea kwa miguuu ,na miongoni mwao walikuwepo wenye kutupa mishale na wenye kubeba Bendera ,na miongoni mwao kuna wenye kuhusika na uchunguzi,na miongoni mwao kuna wenye kuhusika na unyweshelezaji,na miongoni mwao wachungaji mifugo ,wakitoshelezana wao kwa wao,kila mmoja akijitahidi kupambana na maadui,akiwa tayari kujitoa muhanga katika njia ya Mwenyezi Mungu na kutafuta radhi zake,na kukazingatiwa kukimbia siku ya mpambano ni katika madhambi makubwa,kama alivyosema mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَنْ يُؤَلِّمُ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّرًا إِلَىٰ فِتْنَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ﴾ [الأنفال: 16]

(Na atakae wageuzia mgongo wake siku hiyo isipokuwa amegeukia kwa kushambulia au amegeuka ili akaungane na sehemu nyingine ya jeshi hili hili la waislamu-ikiwa siyo hivyo - atastahiki Ghadhabu za Mwenyezi Mungu mahala pake ni jahannam na ni mafikio mabaya ya kufikia humo) [Al-anfaal: 16].

Pamoja na jambo la kutafuta mahitajio ni jambo la kawaida kwa askari wao kama wao kikawaida hakika ALLAH aliwahimiza katika kuwapa wapiganaji na kutoa mali pamoja na nafsi kwenye jambo hili.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ تِجَارَةٍ تُنْجِيكُمْ مِنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١١﴾ تُوْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ ذَلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ﴾ [الصف: 10-11]

Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkafuata sheria Zake kivitendo! Je niwaonyeshe njia ya biashara yenye mapato makubwa ambayo itawaokoa na adhabu yenye kuumiza? Ni mwendelee daima kumuamini kwenu Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na mpigane jihadi katika njia ya

Mwenyezi Mungu kuinusuru Dini Yake kwa mali mnayoyamiliki na nafsi zenu, hilo ni bora kwenu kuliko biashara ya duniani. Basi mkiwa mnajua vitu venye madhara na manufaa, fuateni amri hiyo. Al- swaff:10-11 Hivyo wengi miongoni mwa maswahaba walijulikana kutokana na wingi wa utowaji wao kwa ajili ya wapiganaji jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu,mingoni mwao ni Othman Bin Affan-Radhi zaAllah ziwe juu yake-katika vita vya Tabuk (1308) na Twalha Bin Ubaidillah-Radhi za Allah ziwe juu yake-Swahaba ambaye Mtume Alimuita Twalha jina la Ukarimu kwa kujitolea kwake mali nyingi katika moja ya vita miongoni mwa vita.

Na hakika wanawake walishiriki pamoja na wanaume katika kujiandaa kimali na upatikanaji wa mahitajio katika kunywesha maji na kuwatibu majeruhi.⁵⁹⁷

Anacho kipata Muislamu kutokana na mali za maadui ni chake njia yake na mpangilio wake upo katika kukigawanya,kipo miongoni mwacho kuwa ni ngawira nayo ni(kile kilicho patikana kwa Waislamu kushinda vita mpaka wapate nguvu),⁵⁹⁸ na vile vile ilijulikana faiy nayo ni:(Waislamu hawakuiendea kwa farasi wala misafara).1311}⁵⁹⁹

Na sheria ilikuwa wazi katika kugawanya yale wanayo yapata Waislamu kutoka kwa maadui,ngawira hupewa kwayo mpiganaji,na inaanza kwa yule aliye pigana ni haki yake kile alichonyang'anya,(1312)kisha huchukuliwa fungu la tano kwa ajili ya ALLAH na Mtume Mtume analiweka fungu hilo kwa namna

⁵⁹⁷ Abdul aziz Al- Saluumiy,Diwan Al-Jundiy ukurasa 373

⁵⁹⁸ Al-kharaaj- Yahya bin Adam ukurasa wa 17.

⁵⁹⁹ Al-kharaaj- Yahya bin Adam ukurasa wa 17.

awezaavyo kwa ajili ya maslahi ya umma kwa kile anacho kiona,na jambo hilo limepokelewa kwenye kauli yake ALLAH aliye mtukufu:

﴿وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ
وَابْنِ السَّبِيلِ إِن كُنْتُمْ أَمِنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ التَّقَىٰ الْجُمُعَانِ وَاللَّهُ
عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾ [الأنفال: 41]

Na jueni, enyi Waumini, kwamba kile mlichokipata kutoka kwa adui yenu kupitia jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi Sehemu yake ya Tano ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume, iwekwe kwenye manufaa ya Waislamu wote; ya pili ni ya jamaa wa karibu na Mtume, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukiye, nao ni waliozalikana na Hashim na waliozalikana na Muttalib. Wawekewa sehemu hiyo ya tano mahali pa sadaka, kwani sadaka si halali kwao. Ya tatu ni ya mayatima; ya nne ni ya masikini, na ya tano ni ya msafiri aliyemalizikiwa na matumizi, iwapo nyinyi mnaukubali upweke wa Mwenyezi Mungu, mnamtii Yeye, ni wenye kuyaamini yale Aliyomteremshia mja Wake Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukiye, miongoni mwa aya, usaidizi na ushindi katika siku Aliyopambanua baina ya haki na upotofu hapo Badr, siku lilipokutana kundi la Waumini na kundi la washirikina. Na Mwenyezi Mungu juu ya kila kitu ni Mwenye uwezo, Hashindwi na chochote. (Al-anfaal:41). Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿فَكُلُوا مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلَالًا طَيِّبًا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾ [الأنفال: 69]

Basi kuleni mlichokipata katika ngawira na fidia ya mateka, kwani hiyo ni halali nzuri. Na jilazimisheni na hukumu za Mwenyezi Mungu na sheria Zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha kwa waja Wake, ni Mwenye huruma nao. Al-Anfal:69]

Ama kuhusu Faiun nayo ni mali iliyokuja kwenye kitabu Cha Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ مَا قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْنَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَىٰ أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْرِجَ الْفَاسِقِينَ ﴾ وَمَا أَقَاءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ وَلَكِنَّ اللَّهَ يُسَلِّطُ رَسُولَهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿ مَا أَقَاءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴾ [الحشر: 7-5]

"Mitende mnayoikata au mnayoiacha imesimama juu ya mashina yake bila ya kuigusa , ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na amri Yake, na ili Awadhhalishe kwa hilo wale waliotoka nje ya utiifu wake wenye kuenda kinyume na amri Yake na makatazo Yake, kwa kuwapa nguvu nyinyi kuikata mitende yao na kuichoma. Na zile mali ya Mayahudi wa Banū al- Nadīr ambayo Mwenyezi Mungu Amewaletea, hamkupanda farasi wala ngamia ili myapate, lakini Mwenyezi Mungu Anawapa nguvu wajumbe Wake juu ya anayemtaka miongoni mwa maadui Wake, wakajisalimsha bila ya vita. (Mali hayo yanaitwa fay'), na fay' ni mali yaliyochukuliwa kwa makafiri kwa haki bila ya vita. Na Mwenyezi Mungu kwa kila jambo ni Muweza, hakuna kitu chochote kinachomshinda. Hayo mali ya washirikina wa watu wa miji ambayo Mwenyezi Mungu Amewaletea bila kupanda farasi wala ngamia, basi hayo ni ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume Wake, yatatumiwa kwa maslahi ya Waislamu kwa jumla, jamaa wa karibu wa Mtume, rehemu ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, na mayatima: nao ni watoto maskini waliofiliwa na baba zao, maskini: nao ni wenye uhitaji na ufukara, na ibn al-sabīl: naye ni mgeni msafiri ambaye matumizi yake yameisha na mali yake yamemalizika. Hiyo ni kwa sababu mali yasiwe ni milki inayozunguka kwa matajiri peke yao,

na mafukara na maskini wakanyimwa nayo. Na mali yoyote ambayo Mtume Amewapatia au sheria yoyote aliyowawekea, basi chukueni, na chochote kile alichowakataza basi komekeni nacho. Na muogopeni Mwenyezi Mungu kwa kufuata amri Zake na kuepuka makatazo Yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye mateso makali kwa anayemuasi na kuenda kinyume na amri Yake na makatazo Yake. Na aya hii ni msingi wa ulazima wa kufuata Sunnah iwe ni ya maneno, ya vitendo au ya kukubali jambo lifanyike kwa kutolikataza". (Al-hashir:5-7)

Al-Kharaaj katika wakati wa Omar na waliokuja baada yake waliifanyia kazi kama ya Faiun yaani waliigawanya kwa Maslahi ya Umma chini ya uangalizi wa Khalifa,waliigawa kwa uadilifu na utaratibu ambao iliwaenea waislamu wote na maslahi yao,na ulikuwa ugawaji upo mbali kwa ajili ya maslahi maalumu ya makhalifa,kwa kufanyia kazi sunna za mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-Kama ilivyotokea katika mali za Bani nadhiir baada ya kuzichukuwa mtume Ngawira zao(1313)Na kwa hakika vilitungwa vitabu katika hizi hukumu ambazo Umma ulikwenda nazo katika zama za Makhhalifa waongofu na waliokuja baada yao(1314)

Na kwa hakika mtume alizitilia umuhimu silaha na kujifunza utumiaji wake,kwa hakika alikuwa akizipa kipaumbele na kuzitumia,kwa hakika alitumia upanga na mkuki na kutupa kwa kutumia upinde na kuvaa ngao na kofia ya kivita ya chuma na akasema ((Kwa hakika Mwenyezi Mungu ameiweka Riziki yangu chini ya kivuli cha Mkuki wangu,na akaufanya Udhalili na kuonekana mdogo ni kwa yeyote atakaye kwenda kinyume na amri yangu)) (1315) Na alihimiza Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kuzitengeneza sila na akasema: ((Kwa hakika Mwenyezi Mungu kuatakasika na machafu ni kwake na mtukufu huwaingiza watu watatu peponi kwa mkuki mmoja,Mtengenezaji wa mkuki ambaye anatarajia malipo mema kwa kutengeneza kwake,na mwenye

kuutowa,na mwenye kuurusha))(1316) Kama alivyosema Mtume - Sala na Amani ziwe juu yake- "Ichungeni karne yenu haita acha kuwa imejawa na utukufu milele"⁶⁰⁰⁶⁰¹

Uandaaji wa Silaha (1318) Na kuandaa kwake sehemu miongoni mwa uandaaji wa nguvu ambayo Mwenyezi Mungu amemuamrisha katika maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْحَيْلِ تُرْهَبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ
وَأَخْرَيْنَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ
وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ﴾ [الأنفال: 60]

"Na Tayarisheni, enyi makundi ya Waislamu, ili kukabiliana na maadui wenu, chochote mkiwezacho cha wingi wa watu na zana, ili muingize, kwa hio, hofu katika nyoyo za maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui wenu wanaowavizia; na muwatishe wengine ambao uadui wao bado haujajitokeza kwenu hivi sasa, lakini Mwenyezi Mungu Anawajua na Anayajua yale ambayo wanayadhamiria. Na mali yoyote na vinginevyo mnavyovitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, vingi au vichache, Mwenyezi Mungu Atawapa badala yake duniani na Atawawekea thawabu zake mpaka Siku ya Kiyama; na nyinyi hamtapunguziwa malipo ya hayo chochote". [Al-Anfaal:60] Na walikuwa Baadhi ya Maswahaba wadogo wakiweka manyoa katika mishale na kuiandaa,na ikawa wakiulizwa kuwa ulikuwa una miaka mingapi wakati huo, basi hujibu kwa kusema nilikuwa naweka magoya mishale na kutia manyoa.

⁶⁰⁰ Sahihi Bukhari (Fat-hul Bari)12/56

⁶⁰¹ Al-Daaramiy fii sunanihi juzuu ya 2/24.

(1319) na Walikuwa Baadhi ya Maswahaba wakitengeneza mishale na wakija nayo msikitini ili kuitoa sadaka. (1320)

Walikuwa maswahaba wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-wakijifunza utumiaji silaha mfululizo kwa mujibu wa maelekezo yake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na alikuwa akishuhudia pamoja nao na hasa hasa utupaji mishale, mpaka wao wakawa katika baadhi ya masiku wakitupa siku nzima.(1321)

Na kwa hakika Amebainisha umuhimu wa kijifunza akasema: "Kila kitu anachokicheza mtu ni upuuzi ni Batili isipokuwa mtu kurusha mshale kwa upinde wake na kumfunza Farasi wake, na kumchezea mke wake", Na akasema: "Atakaye acha kutupa mishale baada ya kujifunza kwa hakika atakuwa amekwenda kinyume na kile alichofundishwa" (1322)

Na twaweza kusema kuwa upangaji wa jeshi na yanayofungamana nayo miongoni mwa maandalizi maalumu, sawa iwe majengo ya kijeshi au uwekaji wa Ngome mbali mbali katika zama za Mtume yalikuwa yakusanya uhandisi wa kijeshi.

kwa hakika kulikuwa katika mji wa Madina na idadi kadhaa za Ngome zilizokuwa chini ya Answaar na zilikuwa na mchango wake katika kuwalinda wanawake na watoto na wasiopigana katika vita ambavyo viliilenga mji wa Madina, mfano wa Ngome ya Faariy (1323) na ngome zingine, na mji wa Madina unahitajia ukuta sehemu zote ili kuulinda kutokana na maadui katika zama za Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- na kwa hivyo mji wa Madina ulitegemea Ngome, na kwa hakika zilipatikana Ngome nyingi kwa Mayahudi wa Madina, mayahudi ambao Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alipigana nao na Mwenyezi Mungu akampa ushindi Mtume dhidi yao, licha ya kuwa Ngome zao zilikuwa madhubuti, kwa hakika Mwenyezi Mungu alimnusuru Mtume wake na akamuwezesha kukaa kwao, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ مَا ظَنَنْتُمْ أَنْ يَخْرُجُوا وَظَنُّوا أَنَّهُمْ مَانِعَتُهُمْ حُصُونُهُمْ مِنَ اللَّهِ فَأَتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ يُجْرِبُونَ بِيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ الْأَبْصَارِ ﴿2﴾

[الحشر: 2]

"Yeye, kutakasika ni Kwake, Ndiye Aliyewatoa wale walioukanusha unabii wa Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, miongoni mwa watu waliopewa Kitabu, nao ni Mayahudi wa ukoo wa Banū al Nadīr, kutoka majumbani mwao ambayo wakiwa humo walikuwa ni majirani na Waislamu pambizoni mwa Madina. Huko kulikuwa ndio mwanzo wa kutolewa nje ya Bara Arabu hadi Shām. Hamkudhani, enyi Waislamu, kuwa watatoka majumbani mwao kwa unyonge huu na utwevu (udhalili), kwa silaha kali waliokuwa nazo na hifadhi ya nguvu waliokuwa nayo. Na walidhani Mayahudi kuwa ngome zao zitawakinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu na kuwa hakuna anayeziweza. Basi amri ya Mwenyezi Mungu ilizijilia kwa namna ambayo haikupita kwenye akili zao, na Mwenyezi Mungu Akawatia hofu na woga mkubwa, wakawa wanazivunja nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya Waumini, basi zingatieni, enyi wenye busara timamu na akili nyingi kwa hayo yaliyowafika wao". [Al-Hashri: 2] Na katika kauli yake Mtukufu kuhusu Banii Quraidhwa:

﴿وَأَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ صَيَاصِيهِمْ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا ﴿26﴾﴾ [الأحزاب: 26]

"Na Mwenyezi Mungu Akawateremsha Mayahudi wa Banū Quraidha kutoka kwenye ngome zao kwa kuwa waliyasaidia Mapote katika kupigana na Waislamu, na Akatia hofu ndani ya

nyoyo zao wakashindwa, mkawa mnaua kundi katika wao na mnateka kundi lingine". [Al-ahzaab: 26]

Na walipoupiga vita Mji wa Madina Munawwar makuraishi pamoja na waliokuwa pamoja nao miongoni mwa makundi, Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-aliwatangulia kwa kutengeneza Mahandaki pambizoni mwa mji wa Madina, pale ambapo Salman Al-faarisiy -Radhi za Allah ziwe juu yake- alipowaelekeza kufanya hivyo, Basi Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-yeye mwenyewe akaanza kufanya kazi ya kuisoma Jiografia ya sehemu ile, na akaweka alama ya sehemu ambazo watachimba mahandaki yaliyochimbwa pambizoni mwa Madina, mahandfaki yanayowazuia maadui wa makundi ya Makuraishi kuingia katika mji wa Madina.(1324)

DOLA YA MTUME REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE NA AMANI YA ULIMWENGU.

Ilisimama Dola Ya Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-kwa Amani kwa yule aliyekusudia kuwa chini ya utawala wake, sawa wawe waislamu au Ahludhimma (wenye kupewa dhima), Dola iliwapa Dhamana ya uadilifu na Amani na kuilinda Dini ya Mwenyezi Mungu kutokana na Uadui, na kwa hakika ilitanuka Dola yake kwa awamu mpaka ikaenea Kisiwa cha waarabu na ikaenea kwa kuwa na mahusiano ya nje sawa mahusiano hayo yawe pamoja na makabila ya kiarabu yaliyopo nje au pamoja na Dola zinazoizunguka Dola ya kiislamu.

Na alikuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-tangu kutumwa kwake na kabla ya kutumwa alikuwa akijua nguvu za ulimwengu unaomzunguka, hivyo kuchagua kwake Habasha (Ethiopia) kwa ajili ya maswahaba zake wahamie huko ni kutokana na kujua kwake vyema kuwa watu wa nchi ile na nidhamu zake na

mfalme wake, na kwa ajili hiyo Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alitaka kutoka kwa maswahaba zake wahamie huko na akawafahamisha kuwa: "Kwa hakika katika Nchi hiyo kuna Mfalme ambaye kwake hakuna yeyote anayedhulukiwa" Na yakatokea aliyoyasema Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kama alivyojitangaza kwenye makabila mbali mbali kabla ya kuhama, sawa iwe katika mji wa Makka wakati wa msimu wa Hija au kwenye masoko na misimu katika miji ya kiarabu. (1326) Na jambo hili ni kutilia mkazo mahusiano ya nje, na baada ya kuhama Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- aliandikishiana na wafalme na viongozi wa Dola na makabila akiwepo katika hao Kisra wa Fursi na Kaisari wa Roma (Italia) (1327) katika ujumbe uliokuwa wazi ili kufikisha ujumbe na amani kwa mwenye kutaka amani hali ya kutoa ujumbe huo kwenye kila Ujumbe: "Amani iwe juu ya kila mwenye kufuata muongozo" pale ambapo neno salamu (Amani) lilikuwa la kwanza katika matamko yake, na alikuwa Mtume akiwapa habari maswahaba wake kuwa ujumbe wake utaendelea na utafika katika kila sehemu, kwa kusema: "Kwa hakika dini hii itafika ambapo usiku na mchana umefika", na huo ni msisitizo kwa ulimwengu kupitia Ujumbe wake.

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾ [الأنبياء: 107]

"Na hatujakutuma isipokuwa ni rahma kwa watu wote". [Surah Al-Anbiya: 107].

Na mwenye kupitia jumbe za Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kwenda kwa Wafalme na viongozi atakuta huu upeo na pupa ya amani kwa wanadamu wote (1328) na kuwa alichokiweka Mwenyezi Mungu na Mtume wake miongoni mwa sheria ni Nidhamu ambayo inadhamini Amani kwa watu wote hata kama mtu hajaingia katika Uislamu, kwa Sharti kuwa asiwafanyie uadui waislamu au kuwazuia watu wasisikilize yanayohusu uislamu na wasiwazuie wafuasi wake watakapouchagua uislamu, kwa hakika

hiyo ni sheria ya Dola ya Kiislamu katika Zama za Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-(1329)

Mtazamo wa Ulimwengu kwa ujumla, na mahusiano yake yamejengwa juu ya msingi wa Amani na kuwafikishia watu wote ujumbe, na kuacha kujitenga na jamii ya wanadamu na kuacha msugvano na jamii (1330) na kufikisha heri na tabia na amani ambayo imekuja kwenye uislamu (1331) na uwezekano wa kuishi pamoja na wahalifu katika mwanga wa kuhifadhi haki za wote, ikiwemo haki ya kutoa zaka kwa waislamu na kutoa Jizya kwa wasiokuwa waislamu wanaoishi ndani ya Dola ya kiislamu, basi yeyote atakaye zuia utoaji wa Zakkah basi huyo ni Mwenye kupinga Nidhamu na sheria. Na vilevile kuzuia watoa Jizya, pamoja na kusaidia kuzuia Dhulma na Vibaba na kusimamaisha viunganishi vya kiuchumi na sehemu zingine na mataifa ya Jirani, na kulinda njia za misafara ya Kibiashara na kutekeleza Ahadi na makubaliano na Dola na makundi na makabila kwa ajili ya kubadilishana maslahi na kuishi pamoja, na uwajibu wa utekelezaji ndiyo katika vianzio vya Kidini na kisheria vyenye kuendana na Masharti mbali mbali ambayo yameafikiwa,⁶⁰²Na kwa hakika kumetungwa vitabu vingi katika huu uthibitisho na Makubaliano ya kiutume waweza Kurejea vitabu hivyo. (1333)⁶⁰³

⁶⁰² Tazama Doctor Abdul wahab Kal-ziyyat,Rejeo lilotangulia uk 6

⁶⁰³ Tazama Qi-atu Jii, Muhammad Rawaas, Qiraatu Siyaasiyyat Liksiirat al-nabawiyyat chapa ya 2 Daaru Nafaais Beirut 1420 ukurasa wa 304.

KUFARIKI KWA MTUME REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE. [1334]

Alikuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-ili kuwafundisha watu namna ya kumuabudu Mwenyezi Mungu na kujiandaa na siku ya mwisho na kukutana na Mwenyezi Mungu, na alikuwa akiwakumbusha kuhusu Mauti na Kiama, na kwa hakika limekuja neno Mauti zaidi ya sehemu 50 katika Qur'ani Tukufu, tangu mwanzo wa kutumwa Mtume na Kuteremshiwa Qur'an alikuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake ni mwenye kuwakumbusha.

﴿وَلِلْآخِرَةِ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ۗ وَكَسُوفٌ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ۗ﴾ [الضحى: 5-4]

Na Nyumba ya Akhera ni bora kwako kuliko nyumba ya ulimwengu. (4) Na kisha Mola wako atakupa na utaridhia (5) [Al-dhuhaa: 4-5] Na zikaja Aya za Qur'an kutangaza wazi wazi:

﴿إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ ۗ ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ۗ﴾ [الزمر:

[31-30]

"Wewe ni mwenye kufa, ewe Mtume, na wao ni wenye kufa" (30) "kisha nyote, Siku ya Kiyama. Kwa Mola wenu mtazozana, hapo Ahukumu baina yenu kwa uadilifu na usawa"⁶⁰⁴[Azzumar: 30,31] Zinakuja Aya nyingi zikiwahusu makafiri wa Kikuraishi ambao walikuwa wakisubiri kufa kwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-ili Ujumbe wake uwe umekwisha kama walivyodai:

﴿وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِنْ قَبْلِكَ الْخُلْدَ أَفَإِنْ مِتَّ فَهُمُ الْخَالِدُونَ ۗ﴾ [الأنبياء: 34]

⁶⁰⁴ Ameipokea Ahmad katika Musnad yake juzuu ya 4-210;na Ameisahihisha Al-albaaniy katika Sil-silat kwa namba 2497.

"Na hatukumfanya mwadamu yeyote kabla yako, ewe Mtume, asalie duniani milele. Basi ufapo wewe, kwani wao wana matumaini ya kuishi daima baada yako?" Hili haliwi. [Al-anbiyaau: 34.] Na jambo hili ndiyo msingi wa jumla kwa kila mwanadamu na kila kiumbe:

﴿كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَنَبَلُوكُم بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ﴾ [الأنبياء: 35]

"Kila nafsi ni yenye kuonja kifo hapana budi namna utakavyo refuka umri wake duniani. Na kuweko kwake maishani hakukuwa isipokuwa ni mtihani wa majukumu ya maamrishi na makatazo na mabadiliko ya hali, mazuri na mabaya, kisha baada ya hapo kuna kurudi na kurejea kwa Mwenyezi Mungu, Peke Yake, ili kuhesabiwa na kulipwa." [Al-anbiyaau: 35] Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ وَيَبْقَى وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ﴾ [الرحمن: 26-27]

"Kila aliye juu ya uso wa ardhi miongoni mwa viumbe ni mwenye kuangamia", (26) "Na utasalia uso wa Mola wako Mwenye utukufu, ubora, kheri nyingi na upaji" (27). Katika aya hii pana kuthibitisha sifa ya uso kwa Mwenyezi Mungu kwa namna inavyonasibiana na Yeye, kutakasika ni Kwake, bila kufananisha wala kueleza namna ulivyo. [Al-rahmaan: 26-27] Na katika kauli yake ALLAH Mtukufu:

﴿وَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ لَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ

تُرْجَعُونَ﴾ [الفصص: 88]

"Wala usiabudu, pamoja na Mwenyezi Mungu, muabudiwa mwingine. Hapana muabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu. Kila kitu ni chenye kuangamia na kutoeka isipokuwa uso Wake. Uamuzi ni Wake. Na Kwake Yeye mtarudishwa baada ya kufa kwenu ili muhesabiwe na mlipwe". Katika aya hii kuna

kuthibitisha sifa ya uso wa Mwenyezi Mungu, aliyetukuka, kama inavyonasibiana na ukamilifu Wake, ukubwa Wake na utukufu Wake. [Al-Qaswas: 88]

Na kauli yake:

﴿أَيُّنَمَا تَكُونُوا يُدْرِكْكُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّسَيَّرَةٍ وَإِنْ تُصِيبُهُمْ حَسَنَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَإِنْ تُصِيبُهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ قُلْ كُلٌّ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ فَمَالِ هَؤُلَاءِ الْقَوْمِ لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ حَدِيثًا﴾ [النساء: 78]

"Popote mlipo mtafikiwa na kifo, pawe ni mahali popote pale mnapokuwa, muda wenu ukikoma, hata kama muwapo ndani ya ngome zilizoimarishwa zilizoko mbali na kiwanja cha mapambano na mapigano. Na wakipatwa na mambo ya kuwafurahisha ya starehe ya maisha haya (ya ulimwenguni), wanayanasibisha kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka kuwa Ndiye Aliyewapatia, na watokewapo na matukio wanayoyachukia, wanayanasibisha kwa Mtume Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, kuwa yamesababishwa na yeye kwa ujinga wao na kwa fikira zao kuwa yeye amewaletea mkosi. Na hawakujua kwamba yote yanatokana na Mwenyezi Mungu Peke Yake, kwa uamuzi Wake na makadirio Yake. Basi kwa nini wao hawakaribii kuelewa maneno yoyote unayowaelezea?" [Al-Nisaa: 78] Kama vile ambavyo yeye Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-alipomuaga Muadh Bin Jabal kabla ya kusafiri kwake kwenda Yemen, alisema: "Ewe Muaadh huenda usinikute baada ya mwaka wangu huu Hivyo ikiwa utanikosa utapita kwenye Kaburi langu na Msikiti wangu"(1335) Basi Muaadhi Akalia -Radhi zaAllah ziwe juu yake-

Katika wakati ambao Mtume alijiandaa yeye mwenyewe ili akutane na Mola wake, na akajiandaa kwa hilo basi Qur'an ikawa

ikiwaandaa maswahaba wake na umma wote kwa ajili ya kutengana naye na kuutaka umma udumu kwenye dini yake baada yake:

﴿وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَى عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾﴾ [آل عمران: 144]

"Hakuwa Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, ni kiumbe aina nyingine, isipokuwa yeye ni Mtume wa jinsi ya Mitume wengine waliokuweco kabla yake, alifikisha ujumbe wa Mola wake. Basi iwapo atakufa, kwa kumalizika muda wake, au atauawa, kama walivyoeneza uvumi maadui, kwani mtarudi nyuma na kuacha dini yenu na kuyaacha aliyowaletea Mtume wenu? Basi yeyote miongoni mwenu atakayerudi nyuma akaiacha dini yake, yeye hatamdhuru Mwenyezi Mungu chochote, bali ataidhuru nafsi yake madhara makubwa. Ama atakayekuwa na msimamo imara juu ya Imani yake na akamshukuru Mola wake juu ya neema ya Uislamu, hakika Mwenyezi Mungu Atamlipa malipo mazuri kabisa". [Al-Imran: 144]. Na ilikuwa aya hii ni miongoni mwa vilivyomtia nguvu Abubakari-Mwenyezi Mungu amridhie- pindi alipofishwa Mtume sala na mani ziwe juu yake aliisoma mbele za Watu na ikawa ni msaada wa kuwatuliza na kuwapa nguvu, na hakika alisema Mtume sala na amani ziwe juu yake kumwambia bint yake Fatma. "Hakika Jibrili alikuwa akinisomesha Qur'ani (kwa kurejea) mara moja kwa mwaka na hakika yeye amenihudhushia Qur'ani mara mbili kwa mwaka mmoja, na sioni kwa jambo hilo isipokuwa ni kukaribia kwa kifo changu"⁶⁰⁵

⁶⁰⁵ Amepokea Bukhar, hadithi namba: 3624, na amepokea Muslimu katika sahihi yake.

Na hakika imepokelewa kutoka kwa Aisha -ALLAH amridhie- alikuwa Mtume sala na amani ziwe juu yake akikithirisha kusema kabla hajafa (Sub-haanaka wabihamdika astaghfiruka wa atuubu ilaika) akasema: nikasema: Ewe Mtume wa ALLAH: maneno gani haya mageni nakuona ukiyasema? akasema Mtume: "Yamefanywa kwangu kuwa ni alama katika umma wangu utakapoyaona ninayasema:

﴿إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿٢﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٣﴾﴾ [النصر: 1-3]

(Itakapo kuja nusura ya ALLAH na ushindi, (1) Na ukawaona watu wanaingia kwenye dini ya ALLAH makundi kwa makundi, (2) Basi tukuza kwa sifa za Mola wako na umtake msamaha, Hakika yeye amekuwa ni mwenye kukubali msamaha (3) (surah Al-Nnasru:1-3)⁶⁰⁶

Na kama alivyokuwa Mtume sala na amani ziwe juu yake na pupa ya kuwaaga walio hai, hakika ndivyo ilivyokuwa alikuwa na pupa juu ya kutembelea kaburi za waliyo kufa miongoni mwa waislamu mwisho wa siku zake, alitembelea Mtume sala na amani ziwe juu yake makaburi ya waliyo kufa mashahidi katika vita vya Uhud kama kuwaaga wao.⁶⁰⁷

⁶⁰⁶ Amepokea Muslmu, kitabu swalat, Babu maa yuqaal fii ruquuy wa sujuud,juzuu ya 2/50,angalia Tafsiri ya Ibn Kathiri.surah Al-Nnasru, juzuu ya 2/2043.

⁶⁰⁷ Aliyu, sahihi Sirah, ukurasa wa 554: na angalia Ibn abii Shaybah, Almaghazy ukurasa 418.

Kama alivyo pupia Mtume sala na amani ziwe juu yake kutembelea makaburi ya Baqii na kuwaombea wao na watu wao.⁶⁰⁸

Kujiskia maumivu Mtume sala na amani ziwe juu yake:

Mwishoni mwa mwezi wa pili kabla ya kufa Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa siku Ishirini na tano alianza Mtume sala na amani ziwe juu yake kujiskia maumivu, alikuwa ni mwenye subira na kutarajia malipo kwa Mwenyezi Mungu, alikuwa haelezei isipokuwa kwa mnasaba, alidhihirisha kulalamikia maumivu ya kichwa kwa mama wa waumini Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-, alipotoka kutembelea makaburi ya Bakii. ((Anasema Aisha mke wa Mtume sala na amani ziwe juu yake: alirudi kwangu Mtume akitoka Baqii akanikuta na mimi nikiugulia maumivu na mimi nikisema: Eeh! kichwa changu, akasema Mtume sala na amani ziwe juu yake (Bali mimi ndiyo nina maumivu ewe Aisha, Eeeh maumivu ya kichwa"⁶⁰⁹Akasema Aisha: kisha Akasema Mtume sala na amani ziwe juu yake: "Kipi kitakudhuru ewe Aisha kama utakufa kabla yangu kisha nikuoshe na nikuvike sanda, na nikusalie na nikuzike? Akasema Aisha: nikasema: "Nina muapa ALLAH, ni sawa kama utanifanyia hivyo, kisha ukarejea nyumbani kwangu ukafurahia Harusi na baadhi ya wake zako, akasema Aisha: Mtume akatabasamu, na yakaendelea maumivu yake na yeye akitembelea wake zake, mpaka yakaongezeka na yeye akiwa kwenye nyumba ya

⁶⁰⁸ Ally, Sahihi Sirah, ukurasa wa 553, na angalia Ibn Hishami, Al-Ssirah Al-Nnabawiyah juzuu ya 2/662.

⁶⁰⁹ Ameipokea Bukhar katika sahihi yake, kitabu maradhi, Babu (inni wajiu au waa ra'saahu au ishtada bii alwajau) juzuu ya 7/8, na angalia: upokezi mwingine katika kitabu Al-Maghazy, Babu (Maradhu Annabiyi wawafaatuhu) juzuu ya 5/142, na angalia: kitabu Al-Ahkaam, Babu Al-istikhlaaf, juzuu ya 8/125.

Maimunah akawaita wake zake, akawataka idhini aende akaugulie kwenye nyumba yake, wakampa idhini".⁶¹⁰

Imepokelewa kutoka kwa mama Fadhil Bint Al-haarith amesema: nimemsikia Mtume sala na amani ziwe juu yake akisoma katika sala ya maghreeb sura Al-mursalat kisha hakusali tena nasi baada ya hapo mpaka ALLAH alipo mfisha,⁶¹¹na huenda Hadithi ya mama Fadhili inaashiria Magharibi ya usiku ambao ndio maumivu ya Mtume sala na amani ziwe juu yake yalimzidia, kama alivyo taja Aisha -ALLAH amridhie -na huenda siku hii ndiyo siku ya Jumatatu kabla ya kufishwa kwake kwa wiki mbili kama walivyo taja baadhi ya wanazuoni⁶¹²

Kuzidi kwa Maradhi ya Mtume sala na amani ziwe juu yake:

Ilikuwa kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake muda kidogo kabla ya kufa kwake alikuwa na wake tisa miongoni mwa mama wa waumini, na alikuwa akipumzika kwa mama Aisha-ALLAH amridhie-na pindi alipougua Mtume saa na amani ziwe juu yake alikuwa ni mwenye kupupia kuwapa haki zao za kulala, pamoja ya yote hayo kulikuwa kama na usumbufu kwake kuhama hama kwa kila siku hali ya kuwa ni mgonjwa, na pindi yalipozidi maradhi alikuwa akiwauliza "kesho nitakuwa kwa nani" akikusudia siku ya Aisha, wake zake wakampa idhini awe popote anapotaka, akawa nyumbani

⁶¹⁰ Ibn Hisham, Al-Sirah Al-Nnabawiyah, juzuu yz 4/643,na angalia: sahihi Al-Bukhar, Hadithi namba: 4442.

⁶¹¹ Amepokea Bukhari katika sahihi yake (Babu maradhi Annabiyi wawafaatuhi) juzuu ya 5/137.

⁶¹² Sahihi Bukhari ,Fat-hul Baar, 16/260.

kwa Aisha mpaka akafia kwake⁶¹³Na baadhi ya riwaya zimeweka wazi namna alivyo hamia Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa ajili ya maradhi kwenye nyumba ya Aisha.⁶¹⁴

Na hakika ametunukulia sisi Mama Aisha -ALLAH amridhie- kwa kila ukweli na uaminifu sehemu inayo bainisha nafasi ya Fatma- ALLAH amridhie- kutoka kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake na yale ambayo Mtume aliyo muhusisha kutokana na Elimu ambayo Mtume hakumpa yeyote akasema Aisha: Alikuwa Fatma akitembea na ulikuwa mwendo wake ni kama mwendo mwa Mtume sala na Amani ziwe juu yake Mtume akasema: "karibu ewe bint yangu" kisha Mtume akamkalisha upande wake wa kulia au kushoto kwake, kisha akampa siri, kisha Fatma akalia, nikamwambia: kwanini walia? kisha Mtume akampa siri nyingine Fatma akacheka, nikasema: sijawahi kukuona kama siku ya leo ni mwenye furaha iliyo karibu kuliko huzuni, Aisha akamuuliza Fatma yale aliyo ambiwa na Mtume sala na amani ziwe juu yake? Fatma akasema: Sikuwa ni mwenye kufichua siri ya Mtume sala na amani ziwe juu yake, mpaka alipofishwa Mtume sala na amani ziwe juu yake Aisha akamuuliza Fatma. Fatma akasema: Alinipa siri mimi kuwa Jibrili alikuwa akinihudhurishia Qurani kwa mwaka mara moja, nakuwa mwaka huu amenihudhurishia Quran mara mbili kwa mwaka, na sioni isipokuwa ni kuwa karibu kifo changu, na hakika wewe ndiye wa kwanza kwa watu wa nyumbani kwangu kunifuatia kwa kufa nikalia, kisha akasema Mtume: Hivi huridhii ewe Fatma uwe mtukufu wa

⁶¹³ Ameipokea Bukhar katika sahihi yake (Baabu maradhi Annabiy wawafaatuhu) juzuu ya 5/142.

⁶¹⁴ Amepokea Bukhar katika sahihi yake (Baabu maradhi Annabiyi wawafaatuhu) juzuu ya 5/138.

wanawake wa Peponi? au mtukufu wa wanawake wa waumini? hilo likanifanya nicheke.⁶¹⁵

Hakika tukio hili na riwaya zinatoa uwazi uliyo timia katika umahususi wa Fatma- ALLAH amridhie- kwa Elimu na kuelezwa na Mtume sala na amani ziwe juu yake kuwa yeye ni mtukufu wa wanawake wa Peponi, kama ilivyo Aisha-ALLAH amridhie- alikuwa ni mkweli kunukuu kutoka kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake basi ndivyo ilivyo kuwa yeye Aisha anaelezea Fadhila za Fatma, katika kitabu cha Al-Manaqib kwa Bukhar-ALLAH amuhurumie- na kwa asiye kuwa yeye, na kwa yale ambayo Mtume aliyo mpendelea Fatma, na jambo hili ni miongoni mwa dalili kubwa juu ya mahusiano ya kweli kati ya mama wa waumini na baina ya wengineo katika Familia ya watu wa nyumbani kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake, na matukio yote kwa ujumla wake katika kuelezea ubora wa Fatma na Ally -ALLAH awaridhie- imepokelewa kwa mapokezi ya mama wa waumini Aisha-ALLAH amridhie.

Na huenda katika maradhi ya Mtume sala na amani ziwe juu yake katika nyumba ya Aisha kuna Hekima zilizo kuwa nyingi, na kwa kuongezea kwa kule kustarehe Mtume sala na amani ziwe juu yake pamoja naye, hakika alikuwa Aisha ni mwepesi wa kuhifadhi aliyo yasema Mtume sala na amani ziwe juu yake kuliko akinamama wengine wa waumini wakati Mtume akiwa katika siku zake za mwisho. Na katika sehemu zingine ambazo ni maalumu kwa Fatma - ALLAH amridhie- pindi yalipomzidia maradhi Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake, Fatma Mwenyezi Mungu amridhie alisema:

⁶¹⁵ amepokea Bukhari katika kitabu cha Al-Anmbiyai, hadithi namba: 3623,3624,3625,na amepokea Muslimu katika kitabu Fadhwul swahabat, namba ya hadithi 99-2450 na Tirmidhiy katika kitabu AL-manaaqib, hadithi namba 3964.

"Nasikitika kwa misukosuko ya baba yangu!" Akasema Rehema na Amani zimfikie: "Baba yako hana misukosuko tena baada ya leo"⁶¹⁶

Kama ilivyopokelewa kutoka kwa Aisha-ALLAH amridhie- Amesema: alisema Mtume sala na amani ziwe juu yake katika maradhi yake: "Natamani laiti wangelikuwa kwangu baadhi ya maswahaba", Tukasema: ewe Mtume wa ALLAH -sala na amani ziwe juu yake- hivi tusikuitie Abubakar?, Akanyamaza, tukasema: hivi tusikuitie Omari? Akanyamaza, tukasema hivi tusikuitie Othmani? Akasema ndiyo, akaja Othmani, wakajitenga wao wawili akawa Mtume sala na amani ziwe juu yake akimzungumzisha na uso wa Othmani ukibadilika)⁶¹⁷

Na imepokelewa kuwa Othmani Ibn Afan -ALLAH amridhie- Alisema siku ya nyumba (alipo zingirwa na Khawariji): Hakika Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake alinipa Ahadi, na mimi naelekea kuwa kwenye Ahadi hiyo", wakawa wakimuona siku hiyo.

Na imepokelewa kutoka kwa Aisha- Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kuwa Mtume-**Rehema na Amani ziwe juu yake-**amesema: "Ewe Othmani, ikiwa Mwenyezi Mungu atakupa utawala siku moja, na wakataka wanafiki wakuvue kanzu yako ambayo

⁶¹⁶ kutokana na Hadithi ya Bukhar katika sahihi yake, juzuu ya 5/144

⁶¹⁷ amepokea Ibn Majah, katika utangulizi, ukurasa wa 113, na Ibn saad, katika kitabu chake Atwabaqaat ,juzuu ya 3/66, na ameisahihisha Albani, angalia: Ahmad Jad, kufa kwa kipenzi, ukurasa wa 76.

ALLAH amekuvisha basi usiivue", akisema maneno hayo mara tatu)⁶¹⁸

Na imethibiti kutoka kwa Osamah bin Zaidi-ALLAH amridhie- alisema pindi Mtume sala na amani alipo pata uzito, nikashuka na watu wakashuka ndani ya Madinah kisha nikaingia kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake akawa amenyamazishwa wala haongei, akawa Mtume sala na Amani ziwe juu yake akiweka mikono yake kwangu mimi na akiitoa nikatambua kuwa ananiita (1350) na inavyo fahamika kuwa Osamah Ibn Zaid-ALLAH amridhie- alikuwa amepewa amri kipindi kile kabla ya kuugua Mtume sala na amani ziwe juu yake kuongoza jeshi sehemu za Balqaa.

Na imethibiti kutoka kwa Abdillah Ibn Masoud-ALLAH amridhie- amesema: Niliingia kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake na yeye akiumia kwa maumivu nikamshika kwa mikono yangu nikasema ewe Mtume wa ALLAH: Hakika wewe unaugulia maumivu makali sana, akasema Mtume sala na amani ziwe juu yake: "Ni kweli hakika mimi ninaugulia maumivu kama maumivu ya watu wawili miongoni mwenu" akasema: nikasema: kwa hiyo unamalipo mara mbili? akasema Mtume sala na amani ziwe juu yake "Ni kweli", kisha akasema Mtume sala na amani ziwe juu yake hakuna muislamu yeyote atakaye patwa na udhia wa maradhi na yasiyo kuwa hayo isipokuwa ALLAH atamporomoshea kwa maradhi hayo makosa yake kama jinsi mti unavyo poromosha majani yake"⁶¹⁹

⁶¹⁸ Ni katika riwaya za Tirmidhiy katika sahihi yake, Al-manaaqib, ukurasa wa 3705.

⁶¹⁹ amepokea Bukhar katika sahihi yake, Babu shidatl maradhi] hadithi namba 5647, na Babu Ashad Nnaas balaa Al-anmbiyaa, hadithi namba: 5648, 927.

Na katikati ya Maradhi ya Mtume sala na amani ziwe juu yake alipita Abubakari kwenye kikao miongoni mwa vikao vya Maanswari nao wakilia, akasema: kitu gani kinawaliza?wakasema: Tumekumbuka kikao chetu tukiwa pamoja na Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake", kisha akaingia Abbas kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake akamueleza Mtume jambo la Maanswar kulia, Mtume sala na amani ziwe juu yake akatoka hali ya kuwa ni mwenye kujifunika shuka juu ya mabega yake, na akiwa amejifunika kilemba cheusi mpaka akakaa juu ya mimbari akamshukuru ALLAH na akamsifia, kisha akasema: "Ama baada ya hayo: Enye watu hakika watu watakuwa wengi, na Maanswar watapungua mpaka watakuwa kama chumvi ndani ya chakula, basi yeyote miongoni mwenu atakayesimamia jambo lenye kumdhuru yeyote au lenye manufaa na akubali kutoka kwa mwema miongoni mwenu na amsamehe mkosevu miongoni mwao"⁶²⁰

Na miongoni mwa Hotuba ambazo zimenukuliwa kutoka kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake katika maradhi yake ni yale aliyo pokea Ibn Abbas-ALLAH amridhie -amesema: Alitutokea sisi Mtume sala na amani ziwe juu yake katika maradhi ambayo alifishwa kwayo, akiwa amejifunga kichwa chake kwa kitambaa, kisha akakaa juu ya mimbari, akamshukuru ALLAH na akamsifu kisha akasema: "Ni kwamba hakuna yeyote miongoni mwa watu alikuwa ni muaminifu kwangu katika nafsi yake na mali zake kuliko Abubakari Ibn Abi Kuhafah, na laiti ningalikuwa ni mwenye kujifanyia mwandani miongoni mwa watu hakika ningemfanya Abubakari kuwa mwandani wangu isipokuwa udugu wa Uislamu ni bora, nizibieni

⁶²⁰ Ni katika riwaya za Bukhar katika sahihi yake juzuu ya 4/277 na angalia:Ibn Hisham,Al-Sirah Al-Nnabawiyah, juzuu ya 4/650.

mimi kila aina ya pengo katika msikiti huu isipokuwa pengo la Abubakari"⁶²¹

Na hapana shaka kuwa upokezi huu kutoka kwa Ibn Abbas-ALLAH amridhie- ndani yake wapo wanao dai kinyume na hivyo baina ya Abubakar -ALLAH- amridhie- na baina ya watu wa nyumbani kwa Mtume,huyu hapa mmoja wa wanazuoni wa watu wa nyumbani kwa Mtume anazungumza kuhusu Ubora wa Abubakar Swiddiq katika maneno yake ya mwisho ambayo aliyazungumza kwayo Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa watu.

Imepokelewa Kutoka kwa Abuu Saidi Al khudriy Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, amesema: alihutubu Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake, akasema: "Hakika ALLAH amempa hiyari mja yale yaliyopo baina ya Dunia na yale yaliyopo kwake, Mja akachagua yale yaliyopo kwa ALLAH, akalia Abubakar -ALLAH amridhie- nikasema kwenye nafsi yangu kitu gani kinacho mliza huyu shekh? kama atakuwa ALLAH amemhiyarisha yale ya Dunia na yale yaliyopo kwake, na akachagua yale yaliyopo kwa ALLAH? kisha ikawa Mtume sala na amani ziwe juu yake ndiye mja, na akawa Abubakari ndiye aliyefahamu zaid kwetu sisi, akasema "Ewe Abubakar usilie hakika miongoni mwa watu walio niamini mimi, na wakawa karibu na mali zao ni Abubakar, na kama ningelikuwa ni mwenye kujifanyia mwandani hakika ningalimfanya Abubakar kuwa mwandani isipokuwa udugu wa Uislamu na mapenzi yake, usibakie

⁶²¹ amepokea Bukhar katika sahihi yake, kitabu swalaat, juzuu ya 1/120, na Ahmad katika Musnad wake juzuu ya 1/270, angalia upokezi wa Muslimu katika sahihi yake, kitabul masaajid (532)

ndani ya msikiti mlango isipokuwa ufungwe isipokuwa mlango wa Abubakar"⁶²²

Pamesemwa hakika Abubakar Swiddiq-ALLAH amridhie- pindi alipo fahamu maneno ya Mtume sala na amani ziwe juu yake alilia na akasema (isipokuwa tunakutoa fidia kwa baba zetu na mama zetu na nafsi zetu na mali zetu ewe Mtume wa ALLAH, kisha akashuka na hakusimama Mtume walau kwa muda wa saa)⁶²³ na hii ni dalili kuwa hii ndiyo ilikuwa Hotuba ya mwisho ya Mtume sala na amani ziwe juu yake.

Na kutokana na Hotuba hii na kuficha kutoka kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake alifahamu Swidiq kuaga kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake na kukaribia kifo chake, akalia na akatangaza kujiandaa kumtolea fidia Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa kila anacho kiweza, basi Mtume sala na amani ziwe juu yake akawa anambadilishia mawazo na akimsifia na akimpa ubora alioupata peke yake -ALLAH amridhie- nao ni kuwa awe na njia moja ambayo atakuwa akiingia kwayo ndani ya msikiti wa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake, na hili ndani yake kuna ishara kuwa yeye atakuwa Imamu wa Waislamu kwa ajili ya kuwasalisha wao baada ya Mtume sala na amani ziwe juu yake na hili lilitokea baada ya hapo.

⁶²² amepokea Bukhari katika sahihi yake, Babul khaukhat walmamar fil masjid, hadithi namba: 466, angalia, Sirah ya Mtume, ukurasa wa 649.

⁶²³ amepokea Daaramiy katika utangulizi, Baabu wafaat Annabiy, juzuu ya 1/36

Hakika walijikusanya kwake yeye Mtume watu wa Nyumbani kwake na maumivu yakiwa yamemzidia,⁶²⁴wakashauriana baina yao, wakakubaliana wamnyunyuziye dawa iliyoletwa kutoka Ethiopia (iingizwe dawa upande wa mdomoni kwake) nayo ni dawa mahususi kwa upande huo, Mtume akawaashiria wao wasifanye hivyo, wakasema: hiyo ni hali tu ya mgonjwa kukataa dawa, Mtume sala na amani ziwe juu yake akaamrisha azuiliwe kila aliye kuwepo kwenye jambo hilo. "Asibakie yeyote katika watu wa nyumbani isipokuwa azuiliwe, nisimuone isipokuwa Abbas, kwani yeye atakuwakilisheni".⁶²⁵Na alitaka Mtume sala na amani ziwe juu yake kuwafanyia kisasi wao ikiwa ni kuwasafisha, kumkosea yeye ni jambo kubwa kuliko mtu yeyote, akihofia wasije siku ya Kiyama wakahesabiwa kwa kitendo chao kile walicho mkosea Mtume sala na amani ziwe juu yake na alikuwa mwenye kupupia juu ya kusamehewa wao kwa kuwafanyia kisasi kwa kuwaonea huruma wao, na si kuwaadhibu kama wanavyo dhania baadhi ya watu.⁶²⁶

Kama ilivyothibiti yakwamba yalipoongezeka kwake maumivu yake akasema: "Nimwagilieni juu yangu katika kata saba za maji ambazo hazijafunguliwa niliziacha kwa Ally, huenda mimi nikapata nguvu za kuwaaga watu" Wakamkalisha ndani ya beseni (chombo cha kuoshea nguo au chombo cha kubadilishia rangi za nywele) cha Hafswa Mke wa Mtume sala na amani ziwe juu yake kisha tukabakia

⁶²⁴ Ahmad Jad, Wafatul Habibi, uk 64.

⁶²⁵ Kutoka katika Riwaya ya Tirmidhiy katika sahihi yake, katika Kitabu cha Adabu, Hadithi namba: 4458

⁶²⁶ Angalia Azzarqaani, Al-mawahibi Alladuniyah Bilmanhi Almuhammadiyah, juzuu ya 3/379, na yale yaliyo baina ya mabano ni kutokana na tamshi la Bukhar, hadithiya Aisha namba: 4442]

tukimwagilizia maji kwa kile chombo, mpaka akawa akituashiria kwa mkono wake hakika mmefanya, akasema Hafswa kisha Mtume akawatokea watu akawasalisha wao na akawatolea Hotuba)⁶²⁷

Kama ilivyo thibiti kutoka kwa Aisha-ALLAH amridhie- kuwa yeye alisema: "Pindi Mtume alipo shukiwa na maradhi alikuwa akijifunika nguo (nguo nyeusi ya pembe nne) usoni mwake anapo zinduka anaifunua kutoka usoni kwake"⁶²⁸

Na ilikuwa miongoni mwa Sunna zake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- ni kujipulizia yeye mwenyewe akiwa mzima na pia akiwa mgonjwa, na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Aisha-Radhi zaAllah ziwe juu yake- (Kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake alikuwa akipatwa na Maradhi anajipulizia yeye mwenyewe kwa kutumia sura za kinga (Qul audhu birabil falaq, qul audhu birabi nnaas) na kujipaka kwa miokono yake, na alipopatwa na Maumivu ambayo ilikuwa ni sababu ya kufariki kwake nikaanza kumpuliza kwa kutumia sura za kinga (Qul audhu birabil falaq, qul audhu birabil nnaas) ambavyo alikuwa akipuliza, na ninampangusa kwa kutumia mikono yake Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake)⁶²⁹

Na imepokelewa kuwa yeye Mtume sala na amani ziwe juu yake alikuwa akiugulia kutokana na sumu ambayo aliila kwenye mbuzi aliye pewa na mwanamke wa kiyahud, kwenye chakula ambacho alimpikia Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake wakiwa

⁶²⁷ Ni katika hadithi za Bukhar, namba: 4444, kutoka kwa Aisha (ALLAH amridhie)

⁶²⁸ Ni katika hadithi za Bukhar, namba: 4442

⁶²⁹ Kutoka Riwaya ya Imau Bukhariy Hadithi namba 44392.

Khaybar, na alikusudia kumuua, hakika imepokelewa kutoka kwa mama wa waumini Aisha -ALLAH amridhie- amesema: Alikuwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake anasema kwenye maradhi yake aliyofia: "Ewe Aisha sikuacha kuwa nikisikia machungu ya chakula ambacho nilikula siku ya Khaibar, na muda huu ninahisi sehemu ya sumu ile ikizunguka"⁶³⁰

Na katika siku za mwisho maumivu yaliongezeka kwa Mtume wa ALLAH sala na amnai ziwe juu yake, na watu wake walikuwa wamejikusanya kwake hasa hasa masahaba wake kwa ajili ya kumsalimia na kumpa utulivu, na ambaye hakuingia kumuona alikuwa anamuuliza aliyeingia, na Ally-ALLAH amridhie- alitoka kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake kipindi cha maumivu yake ambayo Mtume alifishwa kwayo watu wakasema: Ewe baba Hassani Mtume ameamkaje? akasema: "Al-hamd lillah, meamka akiwa na ahueni" kisha Abbasi akamshika mkono akasema: Namuapia Mwenyezi Mungu hivi wewe humuoni baada ya siku tatu huenda akazidi kuzidiwa, namuapia ALLAH hakika mimi namuona Mtume wa ALLAH atafishwa kwa maumivu anayo sikia, na hakika mimi nafahamu kwenye uso wa watoto wa Abdul Mutwalib alama za kifo, tupeleke kwa Mtume wa ALLAH tukamuulize nani atakuwa na jambo la (utawala) kama itakuwa ni kwetu basi tutafahamu, na kama itakuwa kwa wasiokuwa sisi basi tutamtawalisha atakayetupa usia", akasema Ally-ALLAH amridhie- namuapia ALLAH kama tutamuuliza jambo hilo Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake atatuzuia,

⁶³⁰ Amepokea Bukhar, Baabu maradhi Annabiy wawafaatuhu, namba 4428.

wala watu hawatatupa utawala milele, na mimi simuulizi Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake milele.⁶³¹

Na hizi Riwaya zinajulisha kuwa kuhisi Abbas-Radhi za Allah ziwe juu yake-Baba mdogo wa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-alipogundua hali ya Mtume na kukaribia kwa kifo chake,na kuhofia kwake kwa yatakayotokea kwenye familia ya Mtume baada ya Kufa kwake Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- na anasisitiza kuwa wao hawajui ni nani atakayechukua jambo la Ukhalifa baada ya kufa Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-na kuwa Abbas yeye anaona kuna umuhimu wa kutaka kujua kuhusu hilo, lakini Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake- anaona hakuna haja ya kumuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-pamoja na kuwa jambo halikuwa wazi kwa Ally wala Abbas -Radhi za Allah ziwe juu yao wao wawili- na kwa hakika zimepokelewa Hadithi nyingine zinazojulisha kuwa Mtume wa Mwenyezi mungu -Rehema na amani ziwe juu yake-alitaka kuandika ujumbe kwenda kwa watu watakao kuja baada yake isipokuwa mpishano wa mitazamo ulitokea kwa waliokuwa kwa Mtume.

Imepokelewa kutoka kwa Bin Abbas -Radhi zaAllah ziwe juu yake-amesema: "Alipofikiwa Mtume na mauti na Nyumbani kwake walikuwapo watu, akasema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake: "Njoooni niwaandikie ujumbe ambao hamtopotea baada ya kuwaandikia ujumbe huo, basi baadhi yao wakasema: kwa hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-ameelemewa na maumivu na nyinyi mnayo Qur'an, kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu, basi watu wa Nyumba ya Mtume wakatofautiana na kutokuelewana, kuna miongoni mwao wenye

⁶³¹ Amepokea Bukhari kutoka kwa Ka'ab Ibn Malik, hadithi namba; 4447, A ngalia: Ibn Hisham; Sira ya Mtume, ukurasa wa 654.

kusema kuwa mleteeni awaandikie Ujumbe ambao hamtapotea baada yake, na miongoni mwao kuna wenye kusema tofauti na hivyo, na walipo tofautiana na kuzidisha maneno yasiyokuwa na maana, akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake "Ondokeni" Amesema Ubaidillah: Na Ibnu Abbas alikuwa akisema: "Kwa hakika ni Msiba Mkubwa sana kwa kizuizi kilichotokea kikazuia kutoandikiwa Ujumbe na Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-kwa kutofautiana kwao na kupiga kwao makelele yasiyo na maana.(1364)

Na katika mapokezi Mengine kutoka kwa Bin Abbas-Radhi za Allah ziwe juu yake- kuwa Mtume alikisema kile alichokuwa akitaka kiandikwe, na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Bukhari amesema bin Abbas: (Siku ya Al-khamis na kulikuwa na nini katika siku hiyo ya Al-khamis, ni siku ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu yalimzidia Maradhi yake na Akasema: "Nileteeni niwaandikie Ujumbe hamtopotea baada ya ujumbe huo hata kidogo", basi wakazozana na wala haifai mizozo mbele ya Mtume, basi wakasema ana jambo gani nyeti? Hebu mueleweni, basi wakaenda wakitaka kujua, akasema ":Niacheni, hili nililonaldo ni bora kuliko hilo mnaloniitia, basi akawausia mambo matatu akasema: watoeni washirikina katika kisiwa cha waarabu Chukueni Jizia kutoka kwenye Ujumbe uliokuja kwa kiasi nilichokuwa nachukua Jizia kwao". na akanyamazia jambo la tatu au akasema nikalisahau)(1365)

Na kinachoonekana wazi kutoka katika riwaya hizi za bin Abbasi ambaye ni mmoja kati ya wanachuoni wa nyumba ya Mtume, ni swali kuwa ni upi wasia huu aliotaka kuuandika Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake? jambo la msingi nikuwa utawala haikuwa ni katika ajenda za usia ule, kwani hapakuwa na kuteuliwa mtu maalumu, si Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake- wala Abubakari - Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Na laiti kama angemuainisha Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- au yeyote basi asingesubiri jambo hili likae bila kufanyiwa kazi mpaka

dakika zake za mwisho, na angelikuwa kalizungumza zaidi ya mara moja kabla ya kuugua. Kutokana na umuhimu wa jambo hili.

Na inavyofahamika kuwa yeye Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- aliwahutubia watu zaidi ya mara moja na wala hakutaja wala kuashiria chochote kuhusu jambo hilo katika hizo Hutuba pamoja na kuwa jambo hilo lilikuwa linawezekana na ni jepesi kwake kama angekuwa anataka na hasa hasa yeye aliongea maneno machache katika kuleta Taswira kwa mwenye kudai kuwa mapenzi yake yalikuwa ni kumuusia Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake- au kumuusia mtu mwingine.

Kama ilivyo pokelewa kutoka na hadithi ya Aisha -ALLAH amridhie-Amesema: "Aliniambia mimi Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake katika maradhi yake: "Niitie Abubakar na kaka yako ili niwaandikie ujumbe, hakika mimi ninahofia asije tamani mwenye kutamani na akasema msemaji mimi ndiye bora, na ALLAH na waumini hawataki isipokuwa -kiongozi awe- Abubakar"⁶³²Pamoja ya haya kilicho thibiti ni kuwa Mtume hakumuandikia Abubakar-ALLAH amridhie- na hadithi hii yawezekana ikakusanywa baina yake na hadithi nyingine ya Ibn Abbas-ALLAH amridhie- iliyo tangulia kwa Bukhar kwa nia ya Mtume sala na amani ziwe juu yake katika maandishi na tofauti zilizopo walio pembeni yake kisha kuacha kwake kutoandika, na hakika Mtume sala na amani ziwe juu yake huenda alikuwa akinuia kuandika kwa ajili ya Abubakar kama angelikuwa ni mwenye kuacha wosia, hasa hasa kuwa Mtume alimuamrisha kuswalisha watu nafasi yake na hii ni alama yenye

⁶³² Amepokea Muslimu Fii fadhwaail aswahaabat, Baabu fadhil Abubakar swidiq, na Ahmad Ibn Hanbal fii fadhwail swahabat ,ukurasa wa 203-204, na Musnad, juzuu ya 6/36,na Ibn saad katika twabaqaat,juzuu ya 3/181.

nguvu, na watu wanaona kuwa Mtume hakuacha wosia kwa Abubakari wala kwa asiye kuwa yeye.

Na kutokana na jambo linalo tia nguvu kuwa Abubakar swidiq-ALLAH amridhie- aliwasalisha watu kwa siku tatu, na pakasemwa sala kumi na saba kabla ya kufa Mtume sala na amani ziwe juu yake, na ilikuwa sala ya mwanzo ni sala ya isham, hakika imepokelewa kutoka kwa Aisha amesema: Yalimzidia maumivu Mtume sala na amani ziwe juu yake akasema: je watu wamesali? Tukasema: "hapana, wanakusubiri wewe ewe Mtume wa ALLAH" akasema: "Nimwagilieni maji katika beseni" tukafanya hivyo, akasema Aisha Mtume akaoga kisha akataka asimame kisha akapoteza fahamu kisha akazinduka akasema: "Watu wamesali?" Tukasema: "Hapana wao wanakusubiri wewe ewe Mtume wa ALLAH" na watu wakiwa wamesimama ndani ya Msikiti wakimsubiri Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake kwa ajili ya sala ya ishaa, Mtume akatuma ujumbe kwa Abubakar ili awasalisho watu na akawa Abubakar ni Mtu mwepesi sana kulia, kisha akawasalisha Abubakar masiku yale)⁶³³

Hakika imepokelewa katika mapokezi mengine kwa Imam Ahmad kutoka kwa Anas Ibn Maliki -ALLAH amridhie- amesema: aliniamuru mimi Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake nimletee kifaa aandike ndani yake kwa jambo ambalo watu wake hawatopotea baada yake, amesema: Nikahofia isije nipita mimi mwenyewe nikasema: "Hakika mimi ninahifadhi na ninazingatia" akasema: "Nina acha wasia wa kushikamana na Sala na zaka na kuishi kwa

⁶³³ Ibn Hisham, Sira Ya Mtume, juzuu ya 4/652, na Othmani Al-Khamisi, Hazina ya Sunnah, kurasa wa 421.

wema na wale mnao wamiliki kwa mikono yenu"⁶³⁴Na katika upokezi wa mama Salamah: "Mpaka Mtume kukawa kunazunguka ndani ya kifua chake, yale ambayo angeweza kuyaeleza kwa ulimi wake"⁶³⁵

Na katika hadithi kutoka kwa Jabiri bin Abdillah radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu- Rehema na amani ziwe juu yake "Asife mmoja wenu isipokuwa afe akiwa na Dhana nzuri na Mola wake"⁶³⁶

Siku ya mwisho katika Maisha ya Mtume sala na amani ziwe juu yake:

Kufa kwa Mtume ilikuwa ni katika siku ya Juma tatu tarehe 12 katika mfungo sita mwaka wa kumi na moja tangu kuhama Makkah kwenda Madina sawa na tarehe 8 mwezi wa sita (June) mwaka 633 tangu kuzaliwa masihi yesu, na ilikuwa Asubuhi kabla ya mchana katika msimu wa kiangazi. (1371)

Alikuwa Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- kwa hakika ameacha kuwasalisha watu kabla ya kufariki kwake kwa siku tatu (Ijumaa, Jumamosi na Juma pili) licha ya kuwa chumba chake

⁶³⁴ Tazama Al-Dhahabiy Al-Siirat Nabawiyyat ukurasa wa 557; na Tazama Abu turaab Al-Dhwaahiriy, Dhuhuul Al-uquul Biwafaati Al-Rasuul ukurasa wa 33, Na Tazama Riwayat ya Aisha kwenye Sahihi ya Bukhari, kitabu cha Maghaaziy Baabu maradhi Nnabiy-Rehema na amani ziwe juu yake-wawafaatuh, juzuu ya 5/140.

⁶³⁵ Ameipokea Nasaai (Angalia Tarjama yake) katika Dhuhuul Al-uquul Biwafaati Al-Rasuul, ukurasa wa 33.

⁶³⁶ Tazama: Bin Hisham Nabawiyyat juzuu ya 2/ Mahdi Rizqi Ilah, Al-siirat Al- Nabawiyyat fii dhauil maswaadiri Al asliyya uk 689.

kilikuwa ndani ya msikiti na kwenye kona ya msikiti, na katika Asubuhi ya Siku ya Juma tatu ambayo Mtume alifariki siku hiyo - **Rehema na amani ziwe juu yake**- alipupia Mtume kuwatuliza waislamu na kuwaunganisha na kuwa kitu kimoja na kupanga safu zao nyuma ya Abuubakar kwa ajili ya swala ya Jamaa, na kutoka kwa Bukhari kutoka kwa Anas Bin Malik-Radhi zaAllah ziwe juu yake- amesema: (Hakika Waislamu walikuwa katika sala ya Alfajir siku ya juma tatu na Abubakar akiwasalisha wao, ghafla akawatokea Mtume sala na amani ziwe juu yake akiwa ametoa pazia la chumba cha Aisha, akawatazama masahaba wake nao wakiwa wamepanga safu ya sala, kisha akatabasamu na akacheka, Abubakar akarudi nyuma ili asali kwenye safu, na akadhania kuwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake anahitaji kutoka kwa ajili ya sala, akasema Anas: Na wakahamaki waislamu kutaka kufitinika katika sala zao kwa furahia kumuona Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake basi Mtume akawaashiria kwa mkono wake ya kwamba timizeni sala yenu, kisha akaingia chumbani kwake na akafunika pazia)⁶³⁷

Na huu ndiyo ulikuwa mwisho wa kundi la waislamu kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu **-Rehema na amani ziwe juu yake**-na hawakumuona baada ya hapo isipokuwa baadhi yao, na miongoni mwao ni Abuu bakar -Swiddiq- Radhi za Allah ziwe juu yake-pale alipokuwa amefungamana karibu na Mtume wa Mwenyezi Mungu- **Rehema na amani ziwe juu yake**- wakati wa kuugua kwake, kwani nyumbani kwake palikuwa karibu na Mtume **-Rehema na amani ziwe**

⁶³⁷ Ameipokea Bukhari kwenye sahihi yake, kitabu Al-Maghaazyi, Baabu maradhi Annabiy-Rehema na amani ziwe juu yake- wawafaatuh,juzuu ya 5/141;na Tazama Bin Hishaam,Al-siirat Al-nabawiyat,juzuuya 4/653.

juu yake-, lakini alikwenda nyumbani kwake kwingine sehemu iitwayo Al-nas- pembeni kidogo mwa mji wa Madinah alipokuwa mke wake wapili.

Na katika siku ambayo Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-Alifariki alitaka Abuubakar ruhusa kutoka kwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- aitembelee nyumba yake ambayo ipo sehemu iitwayo San-hi akawajulie hali zao, na wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu inachukuliwa Roho yake yeye alikuwa huko San-hi⁶³⁸

Na huenda Hadithi ya Anas kuhusu hali ya Fatma Bint Nabiy - Rehema na amani ziwe juu yake- pamoja na baba yake ilikuwa ni kwenye siku ya kufa kwake mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-Na alipoelemewa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-yalikuwa mauti yakimfanya azimie, basi akasema Fatma- Juu yake Amani-: "Yamempata mateso baba yangu", basi Mtume akamwambia Fatma, "Hapatakuwa na mateso tena kwa Baba yako baada ya leo" (1374)

Na huenda hadithi inajulisha kuwa yeye alimpa habari Fatma yakuwa leo ndiyo siku ya Mwisho katika maisha yake, na kuwa yeye hatokuwa tena ni katika watu wa Duniani baada ya siku ile.

⁶³⁸ Bin Hishaam Al-siirat Al-Nabawiyyat juzuu ya 4/654; Abuu Turaab Al-Dhwahiriyy, Dhuhuul Al-uquul Biwafaat Al-Rasuul -Rehema na amani ziwe juu yake-ukurasa wa 37, na Tazama Riwayat ya Bukhariyy katika sahihi yake, Hadith namba 4452 na Sun-hu Mantwiqat fii Atwraaf Al-madinat ni umbali wa unaokaribia Maili moja kutoka katika Msikiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu-Rehema na amani ziwe juu yake-na humo una mashamba Banii Al-haarith Bin Al-Khazraj karibu na bonde la Batw-han ambalo ni mashuhuri kwa jina la Al-awaaliyy)

Kama ambavyo Upulizaji wa Aisha haukuwa mbali-Radhi za Allah ziwe juu yake- (1375) kumpulizia Mtume ilikuwa zaidi ya mara moja, na miongoni mwazo ni ile siku ambayo Mtume alifariki, pale maumivu yalipozidi kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-

Na kwa hakika Baadhi ya Maswahaba walishuhudia maneno ya mwisho aliyoyasema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na huenda siku hiyo ilikuwa siku ambayo Mtume alifariki-Rehema na amani ziwe juu yake-na miongoni mwa uthibitisho wa hilo ni aliyoyapokea Abuu ubaidah Bin Jarraha-Radhi za Allah ziwe juu yake- alisema; "Maneno ya Mwisho Aliyoyasema Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- ni: "Watoeni Mayahudi wa Hijaz na Mayahudi wa Najraan katika Kisiwa cha Warabu, na jueni watu wenye Shari zaidi ni wale waliofanya makauri ya Mitume wao kuwa ni Misikiti"⁶³⁹Na Haya ndiyo maneno ya Mwisho aliyoyasikia Abuu Ubaidah kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-na yawezekana kuna mwingine alisikia baada yake kitu kingine.

Na katika Riwaya hii yaonyesha wazi kuwa Abuu ubaida Bin Jarrah-Radhi za Allah ziwe juu yake- alikuwa ndiye wa Mwisho kukutana na Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, na hilo linakuwa wazi zaidi kwa utilaji umuhimu wake Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- wa utulivu wa Dola ya Kiislamu, na miongoni mwa umuhimu huo ni kuwatowa Mayahudi na Manaswara pale ambapo walikuwa wakitengeneza vitisho katika hatua waliokuwa wamefikia, na kama ilivyokuwa wazi kuwa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake-alikuwa akitilia mkazo kuzuia watu kufanya makaburi ya manabii kuwa ni misikiti, kwa kuwa katika hilo kuna shirki kubwa,

⁶³⁹ Amepokea Imamu Ahmad katika Musnad wake juzuu ya 1/195, na akasema Al-Haythamii katika Majmuu Al-Zawaa'id wapokezi wake ni wakweli, juzu ya 5/325.

na japo kuwa hili halifai kuwafanyia manabii, basi kwa wengine wasiokuwa Manabii na wafuasi wao ndiyo haifai kabisa, na kilichofuata alipupia juu ya kufanya kuwa wasia wake wa mwisho kwa Umma.

Na Mtume alikuwa anachelea watu wasije wakafanya kaburi lake kama walivyofanya Umma uliopita kwenye makaburi ya manabii wao, kama Mayahudi na Manaswara, na inatilia mkazo vilevile Riwaya ya Mama wa Waislamu Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake- na Bin Abbas -Radhi za Allah ziwe juu yake-katika sahihi Bukhari wamesema wawili hao, yalipomteremkia Mtume wa Mwenyezi Mungu Mauti alianza kutupia shuka lake kwenye uso wake, basi akizimia analitoa usoni mwake naye akisema: "Amewalaani Mwenyezi Mungu Mayahudi na Manaswara ambao waliyafanya makaburi ya Manabii wao kuwa ni misikiti" (1377) anatoa tahadhari kwa waliyoyafanya, kama alivyotilia mkazo Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- katika mapokezi ya mengine alisema: "Kama siyo wasia wake huo basi angeliweka wazi kaburi lake lakini alichelea kuwa litafanywa kuwa ni Msikiti"⁶⁴⁰⁶⁴¹

kwa ajili hiyo kila anaye fanya mfano wa hilo kwenye kaburi lolote la mtu yeyote vyovyote atakavyo kuwa atakuwa ameenda kinyume na Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake na ni mwenye kwenda kinyume na maamrisho yake.

Mswaki:

⁶⁴⁰ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4444.

⁶⁴¹ Hadithi hiyo ameipokea Bukhari katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4441.

Alikwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake akipupia kupiga mswaki maisha yake yote akifanya hilo na akiamrisha waislamu kwa hilo, kila wanapo tawadha na kila wanapotaka kusali, akihimiza juu ya jambo hilo na akilibeba jambo hilo kwa hali yeyote na hata katika safari zake.

Na alikuwa wa Mwisho kuingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**- katika siku ambayo alifariki ni Abdurahman Bin Abiibakar Al-swiddiq-Radhi zaAllah ziwe juu yao wote wawili- pale ambapo ilikuwa kuingia kwake ni maalimu kwa kuruhusiwa na dada yake Mama wa waumini Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake- na kwa kuwa yeye ni maharimu yake (ndugu yake wa kiume), na anasimulia mama wa waumini Aisha Tukio la kuingia Abdu rahman Bin Abiibakari na kupiga mswaki Mtume katika mwisho mwa uhai wake, basi anasema Aisha: "Aliingia Abdurahman Bin Abii bakar kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na mimi nimemuegemeza kwenye kifua changu, na Abdulrahman yupo na mswaki mbichi anaswaki nao, basi Mtume akautazama kwa macho yake basi nikachukua mswaki na nikamng'atiang'atia na nikautikisa na kuutengeza vizuri, kisha nikampa Mtume **-Rehema na amani ziwe juu yake**- basi sijawahi kumuona Mtume akipiga mswaki vizuri kama nilivyomuona alivyoswaki siku hiyo na haukupita muda mrefu kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akainua mkono wake au kidole chake kisha akasema: "Kwa kipenzi aliye juu" mara tatu, na alikuwa Aisha akisema amefia katika kifua changu" (1379)

Na alikuwa Aisha-ALLAH amridhie- ni mwenye kujifakharisha kuchanganyika mate yake kwa mate ya Mtume sala na amani ziwe juu yake kwa sababu ya ule mswaki akisema-ALLAH amridhie-

"ALLAH akakusanya baina ya mate yangu na mate yake mwisho wa siku yake ya Duniani na mwanzo wa siku ya Akhera"⁶⁴²

Na Kabla ya kufa kwake-**Rehema na amani ziwe juu yake**- alipatwa na sauti ya kuugulia machungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**- Aisha akafahamu ayasemayo Mtume, anasema Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake-((Basi nilimsikia Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-katika maradhi yake aliyekufa nayo alipatwa na kuugulia kwa uchungu wa kuugua, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا﴾ [النساء: 69]

"Na mwenye kukubali amri za Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na uongofu wa Mtume Wake Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, basi hao ni wale ambao wana utukufu wa mambo na vyeo. Wao watakuwa pamoja na wale waliopewa neema na Mwenyezi Mungu miongoni mwa Mitume na wa kweli wa Imani, ambao kuamini kwao yaliyoletwa na Mitume kulikamilika kiitikadi, kimaneno na kivitendo na mashahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu na Waumini wema. Na wazuri wa marafiki wa mtu kuwa nao Peponi ni hao". [Al-nisaa: 69] Nikasema: Nikadhani heri wakati huo.⁶⁴³

⁶⁴² Hadithi hiyo ameipokea Bukhari katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4451).

⁶⁴³ Kaipokea Bukhari, Baabu maradhi Annabiy-Rehema na Amani ziwe juu yake- hadithi namba: 4435, na Muslim Fii fabwaaail swahabat.

Na alikuwa rehema na Amani ziwe juu yake na afya yake akizungumza akiwa mzima wa afya ya kuwa "Hakika hakuwahi kufishwa Nabii yeyote katu mpaka aonyeshwa makazi yake peponi kisha anapewa hiyari?" Aisha akasema: "Alipofikwa na mauti Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na kichwa chake kikiwa juu ya mapaja yangu, alipoteza fahamu lisaa limoja kisha akazinduka, akanyanyua macho yake juu ya dari kisha akasema: "Ninamtaka rafiki wa juu"⁶⁴⁴Aisha akasema: Kwahiyo hatuchagui sisi.

Amesema Aisha: "Neno hilo likawa ndio neno la mwisho alilozungumza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kauli yake: "Ewe Mwenyezi Mungu, Nimemchagua rafiki wa juu". Alifarikia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na kichwa chake kikiwa juu ya mikono ya Aisha, na alisema -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: "Hakufariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- isipokuwa naye alikuwa kati ya kifua changu na kidevu changu, sitochukia ukali wa mauti tena kwa yeyote baada ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-"⁶⁴⁵

Kilichohakikiwa nikuwa aliegemeza mgongo wake kwa mama wa waumini Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- katika hatua zake za mwisho, imepokelewa kutoka kwake (Aisha) Nilimsikiliza kabla hajafariki huku akiwa kaegemeza mgongo wake

⁶⁴⁴ AKipokea Bukhari, Baabu man tasawaka bisiwqaak ghayrihi, hadithi namba: 4463, Na tazama: hadithi namba: 890, bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/655.

⁶⁴⁵ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake, Hadithi namba 4440, 4449.

kwangu akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe na unirehemu na unikutanishe na rafiki wa juu"⁶⁴⁶.

Na mwisho alisema: "Na mimi nilikuwa nimemuegemeza kifuani kwangu"⁶⁴⁷ na katika hadithi nyingine inaonyesha kichwa chake kilikuwa juu ya mapaja ya Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- na habari hazipingani. Amepokea Bukhari yakuwa Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Alikuwa Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**- akisema akiwa mzima wa afya: "Hakufishwa Nabii yeyote mpaka aonyeshwe makazi yake peponi kisha anarudishwa kuwa hai au anapewa hiyari", Alipozidiwa na maradhi, na mauti yakamfika na kichwa chake kikiwa juu ya paja la Aisha alipoteza fahamu, alipozinduka alinyanua macho yake juu ya paa la nyumba kisha akasema: "Kwa rafiki aliyejuu"⁶⁴⁸.

Na katika riwaya ya Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- nikuwa "Kulikuwa mikononi mwake na chombo kidogo mithili ya ndoo, au kitu kingine ambacho kilikuwa na maji, akawa anaingiza mikono yake ndani ya maji kisha anafuta uso wake na huku akisema: "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, hakika mauti yanakilevi". kisha akanyoosha mkono wake, huku akisema: "Naelekea kwa rafiki wa juu" Mpaka akafishwa na ukapinda mkono wake"

⁶⁴⁶ Hadithi hiyo ameipokea Bukhari katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4459.

⁶⁴⁷ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4463.

⁶⁴⁸ Tazama: Hadithi namba 4437, katika sahihi Bukhari, ishatangulia kutajwa.

Muonekano wa mwili wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ulikuwa mzuri, pamoja na kuugua kwa takribani wiki mbili ila alikuwa katika muonekano mzuri, na wala maradhi hayakuathiri katika uzuri wake na muonekano wake Rehema na Amani ziwe juu yake.⁶⁴⁹Pamoja na hilo hazikuonekana kwake Rehema na Amani ziwe juu yake athari za uzee au mvi na udhaifu, imepokelewa kutoka kwa Anasi bin Maliki -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Alifariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na hakuna katika kichwa chake wala ndevu zake nywele ishirini nyeupe"⁶⁵⁰

Aisha alikuwa bado kijana alikuwa hajawahi kuona wafu na wala hana uzoefu na hilo, kilipopinda kichwa chake wakati wa kifo likadondoka tone la baridi kutoka kinywani mwake juu ya shingo ya Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- na kifua kwake, kisha akainama upande na akadondondoka katika kitanda, Anasema -Radhi za Allah ziwe juu yake-: "Na nilikuwa sijawahi kuona maiti hata mara moja, nikajua kifo chake kupitia mtu mwingine, akaja Omari akaomba idhini ya kuingia akiwa pamoja na Mughira bin Shu'ba, nikawaruhusu na nikafunika pazia, Omari akasema: "Ewe Aisha kapatwa nini Nabii wa Mwenyezi Mungu? Nikasema: kapoteza fahamu tangu lisaa limoja limepita, akafunua uso wake, akasema: Nasikitika kwa msukosuko huu, hakika huu ndio msukosuko mkubwa wa kupoteza fahamu, kisha akamfunika, Mughira hakuzungumza kitu, alipofika katika kizingiti cha mlango Mughira akasema: "Amefariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ewe Omari, Omari akasema: " Umesema uongo, (Si kweli) Hajafa

⁶⁴⁹ Ahmad Jad, Wafatul Habibi, uk 117.

⁶⁵⁰ Kaipokea Ahmad katika Musnad wake, hadithi namba: 12043.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na wala hawezi kufa mpaka atoe amri ya kuwapiga wanafiki, bali wewe unataka kuleta taharuki"⁶⁵¹

Abubakari Swiddiq ndiye aliyekua mtu wa karibu zaidi na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na alisimama badala yake wakati wa swala kuwasalisha watu kwa amri yake, na watu wakamchukulia kuwa ndiye naibu wa Mtume katika kuwaongoza katika swala na mambo mengine, na wakati wa tukio hilo hakuwepo alikuwa kwa mkewe mwingine maeneo ya Sunhu pembezoni mwa mji wa Madina, takribani umbali wa maili moja, mara tu baada kufariki Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-** watu wakafanya haraka kumuita Abubakari Swiddiq -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-, ambaye alikuja haraka mpaka kitandani kwake, na wala hakuzungumza na yeyote, na akaingia ndani ya chumba cha binti yake Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- na akanyanyua pazia akamtazama Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-**,

﴿إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ﴾ [البقرة: 156]

(Innaa lillaahi wa innaa ilaihi Raajiuun) Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tuta rejea. [AL-Baqara: 156], Alifariki Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-**, kisha akaja upande wa kichwa chake akabusu kichwa chake, na akasema: Masikitiko yaliyoje, Tumempoteza Nabii wetu. Kisha akabusu kichwa chake na akasema: Tumekupoteza kipenzi chetu. kisha akambusu na akasema:

⁶⁵¹ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4495.

Nasikitika kutokwa na kipenzi changu, Amefariki Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-⁶⁵².

Na alisema: "Wallahi hayatokusanywa kwako mauti mara mbili, ama mauti uliyoandikiwa juu yako tayari umekufa" ⁶⁵³ Na ameonyesha Bukhari Abubakari kumbusu Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- katika hadithi zaidi ya moja.⁶⁵⁴

Hali katika msikiti wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ilikuwa ngumu, kiasi kwamba watu walikuwa wanakusanyana, wakiulizana kuhusu afya yake Rehema na Amani ziwe juu yake na wanaridhika, na kwa sababu ya mapenzi yao makubwa kwake baadhi yao hawakuondoka msikitini kwake, na Omari alikuwa hajaamini kifo cha Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akawa anazungumza akiwakemea watu na akitoa vitisho, ⁶⁵⁵ akisema: "Hakika Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- hafi mpaka Mwenyezi Mungu Mtukufu awamalize wanafiki.

⁶⁵² kaipokea Ahmad katika Musnad wake, 6/31, Na tazama: Riwaya ya Bkhari katika sahihi yake, hadithi namba: 4450, kaipkea Tirmidhiy katika Mukhtasaru shamaail, uk. 196.

⁶⁵³ Ni katika hadithi za BUKhari katika sahihi yake, Baabu Adukhul alaa mayyit, na hadithi namba: 4452, kitabul Maghazi, Baabu maradhi Annabiy-Rehema na Amani ziwe juu yake-wawaafatuh na kifo chake, 4/143.

⁶⁵⁴ Na tazama hadithi ya Bukhari, 5/143.

⁶⁵⁵ Kaipokea Bukhari katika sahihi yake, hadithi namba: 4454, bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/655.

Akatoka Abubakari Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- katika chumba cha Aisha kwenda Msikitini, watu walipomuona wakamuacha Omari na wakaelekea kwa Abubakari ili kusikiliza ni nini atasema, na Omari alikuwa bado anazungumza na watu. Na anasimulia bin Abbasi hali ilivyokuwa naye aliishuhudia kwa macho yake, anasema: "Hakika Abubakari alitoka na Omari akizungumza na watu, akasema: "Kaa ewe Omari, Omari akakataa kukaa, watu wakanyanyuka wakamfuata Abubakari wakamuacha Omari, Abubakari akasema: Ama baada ya hayo, Yeyote aliyekuwa akimuabudu Muhammadi basi Muhammad amekwisha kufa, na aliyekuwa miongoni mwenu akimuabudu Mwenyezi Mungu basi hakika Allah yuko hai wala hafi, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾﴾ [آل عمران: 144]

"Hakuwa Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, ni kiumbe aina nyingine, isipokuwa yeye ni Mtume wa jinsi ya Mitume wengine waliokuweco kabla yake, akifikisha ujumbe wa Mola wake. Basi iwapo atakufa, kwa kumalizika muda wake, au atauawa, kama walivyoeneza uvumi maadui, kwani mtarudi nyuma na kuacha dini yenu na kuyaacha aliyowaletea Mtume wenu? Basi yeyote miongoni mwenu atakayerudi nyuma akaiacha dini yake, yeye hatamduru Mwenyezi Mungu chochote, bali ataiduru nafsi yake madhara makubwa. Ama atakayekuwa na msimamo imara juu ya Imani yake na akamshukuru Mola wake juu ya neema ya Uislamu, hakika Mwenyezi Mungu Atamlipa malipo mazuri kabisa". [Al Imran: 144] Akasema: Wallahi ikawa kana kwamba watu hawakuwahi kujua kuwa Mwenyezi Mungu aliteremsha aya hii mpaka alipoisoma Abubakari, watu wote wakaipokea kutoka kwake sikumsikia mtu yeyote isipokuwa alikuwa akiisoma aya hii, na amesema Said bin Musayib: Hakika Omari

alisema: Wallahi mara baada ya kumsikia Abubakari akiisoma, ghafla nikapigwa butwaa, na miguu yangu ikaishiwa nguvu nikadondoka chini alipoisoma aya hiyo, yakuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- amekwisha fariki"⁶⁵⁶.

Na utambuzi na hekima za Abubakari vilikuwa wazi, mwenye msimamo huu alikuwa na utambuzi mkubwa wa Qur'ani na alikuwa mwepesi kukumbuka maneno ya Allah kuliko wote, na kwa ajili hiyo wengi wao mara baada ya kumsikia Abubakari akiisoma aya hiyo wakahisi kana kwamba ndio imeteremka wakati huo, watu wote wakatoka msikitini wakaingia katika mitaa ya mji wa Madina wakiisoma aya hiyo kana kwamba ilitemka kwa ajili ya kuwafariji.⁶⁵⁷.

Na inasemekana Ally -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- alikalishwa lakini hakuweza kwa kukosa nguvu na kwa mshituko mkubwa alioupata, kama ilivyoelezwa kuwa Othman -Radhi za Allah ziwe kwake- alikuwa mithili ya bubu anakwenda huku na kule na wala hazungumzi.⁶⁵⁸

Ama binti yake na kipenzi chake Fatma -Radhi za Allah ziwe juu yake- wa pekee aliyebakia katika mabint zake msiba kwake ulikuwa mkubwa mno, na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikuwa amekwisha mueleza kukaribia kwa mauti yake. Na ananukuu Anas bin Maliki -Radhi za Allah ziwe juu yake- yale aliyoyasema pindi alipojua kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-:

⁶⁵⁶ Kaipokea Bukhari katika sahihi yake hadithi namba: 4449, na bin Abii Shaiba, Al Maghazi uk 410, bi Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/657.

⁶⁵⁷ Al-Qustwalaani, Al-Mawaahibu daniya, uk 391

⁶⁵⁸ Tazama: Asuhaili, Arraudhul Anif, 4/468.

"Yalipomzidia maumivu Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akawa anapoteza fahamu, Fatma akasema: Nalia na misukosuko ya baba yangu. Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akasema kumwambia: "Baba yako hana misukosuko tena baada ya leo". Alipofariki alisema: Ee baba yake ameitika wito wa Mola aliyemuita, Ee baba yake katika pepo mafikio yake, Ee baba yake kwa Malaika Jibrili tunatangaza kifo chake. Alipozikwa Fatma -Amani iwe juu yake- akasema: Ewe Anasi hivi mmejisia vizuri sana kumfukia udongo Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake.⁶⁵⁹

Ama Anasi bin Maliki Mtumishi wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, aliyekuwa na ukaribu mkubwa na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- aliyekuwa akiambatana naye kila mahali, anaeleza yaliyomfika kwa kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kwa kauli yake: Siku ilipofika ya kuingia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mji wa Madina kila kitu kilipata mwangaza, tukiwa bado hatujamaliza kumzika Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- tukaanza kujihisi ndani ya nyoyo zetu kama si sisi⁶⁶⁰

Tukio la kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- lilimkumba kila aliyemfahamu Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na akampenda, Mama Ayman mlezi wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikuwa kahamia Madina na alikuwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akimtembelea na akimjulia hali kila wakati, alipofariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-

⁶⁵⁹ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 4462.

⁶⁶⁰ Kaipokea Tirmidhi katika Manaqib,Baabu Rasuulu Ilah Khaatam Alnabiyyina, 3622, na Ahmad katika Musnad, 3/122, 240

Abubakari alichukua jukumu la kuwa anamtembelea, akasema baada ya kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kumwambia Omari: "Tupeleke kwa Mama Ayman tukamtembelee, tulipofika kwake yule mama alilia, Abubakari akamuuliza ni nini kinakuliza? Yaliyoko kwa Allah ni mazuri sana kwa Mtume wake, akasema: "Wallahi mimi sili, kwakutojua kuwa yaliyoko kwa Allah ni bora zaidi kwa Mtume wake, lakini kinachoniliza mimi nikuwa wahyi umekatika kutoka mbinguni, mama akaamsha hisia zao nao wakaanza kulia.⁶⁶¹

Hakika fikra ya mama Ayman -Radhi za Allah ziwe juu yake- ya kuhisi kuwa watu wa Ardhini wote wanahaja ya kupata wahyi na maelekzo, na kukosa kwao kiunganishi kati ya mbingu na Ardhi, kati ya Mola wa waja na waja wake, kiasi ambacho Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alikuwa yeye ndiye mwalimu na mlezi wa muelekezaji mpole mtetezi Rehema na Amani ziwe juu yake, anapokufa kinakatika kiunganishi kilichokuwepo cha moja kwa moja. Watu wote walikuwa wakimkumbuka Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na walikuwa wakifarijiana wao kwa wao. Na imeelezwa kuwa Bilali bin Rabaha -Radhi za Allah ziwe juu yake- alipoadhini baada ya kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- alipofika neno "Ash-hadu anna Muhammadan Rasuulullaah" (Ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu) Msikiti mzima ulizizima kwa vilio na minung'uniko, alipozikwa - Raheme na Amani ziwe juu yake- Bilali aliacha kuadhini.⁶⁶²

⁶⁶¹ Kaipokea Muslim katika sahihi yake, Baabu fadhwaail aswahaabat ummul Ayman namba: 2454, na tazama bin Abii shaiba Al-Maghazi, uk 413

⁶⁶² Al-kustwalani: Al-Mawahibu daaniya, 3/392.

Kutoka kwa Sahl bin Sa'd Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Amesema: Amesema Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake: "Watu watafarijiana wao kwa wao baada yangu kwa kupeana pole kwa ajili yangu". Na watu walikuwa wakisema ni nini hicho? Alipofishwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** wakawa wanakutana baadhi yao kwa baadhi, wakipeana pole baadhi yao kwa baadhi kwa kumpoteza Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake**.⁶⁶³

Na wakakumbushana katika kauli ya Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**: "Atakapopatwa mmoja wenu na msiba basi na akumbuke msiba wake kwangu, kwani huo ni katika misiba mikubwa"⁶⁶⁴

Na anaeleza sheikh Muhammad Al-Ghazali namna habari zilivyoenea katika mji wa Madina kwa kusema: "Na zilizaga habari za kushitusha kutoka katika nyumba ya huzuni, zikiwa na mzizimo masikioni, zikiwa na uzito mkubwa wa kunyong'onyeza nafsi, na zikizungusha fikra na macho. Na wakahisi wakazi wa Madina kuwa anga yote imekuwa giza, huzuni kubwa ya kupoteza ikawaacha wakitahayari hawajui nini cha kufanya"⁶⁶⁵.

Huzuni ilikuwa kubwa mno kwa waislamu wote, na kwa watu Madina hasa hasa, lakini wao walikuwa wakikumbuka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

⁶⁶³ Al-Haithami, Majmauzzawaaid, 9/38, tazama: Ahmad Jaad, wafaatul habiib uk. 156.

⁶⁶⁴ Amesema Al-Albaniy, hadithi ni sahihi kwa ushahidi wa cheni ya hadithi sahihi, 1106.

⁶⁶⁵ Muhammad Al-Ghazali, fiq-hussira, uk 519.

﴿وَلِلْآخِرَةِ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ۖ وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ﴾ [الضحى: 4-5]

"Na Nyumba ya Akhera ni bora kwako kuliko nyumba ya ulimwengu. (4) "Na kisha mola wako atakupa na utaridhia" (5) [Al-dhuha: 4-5] Wakiamini kuwa kukutana kwa Mwenyezi Mungu na Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- ni neema kwa Mtume, na nikwenda kuipata pepo ya Firdausi ya juu na mto Kauthar alioahidiwa, na umma mzima na waumini wote walikuwa na huzuni na balaa kubwa na msiba mkubwa, Anasema Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: "Alipofariki Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- warabu waliritadi, na mayahudi na wakristo wakachomoza, na unafiki ukadhihiri, na waislamu wakawa mithili ya mbuzi waliotawanyika usiku mnene kwa kumkosa kwao Nabii wao - Rehema na Amani ziwe juu yake, mpaka akawakusanya Mwenyezi Mungu kwa Abubakari Swiddiq -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-"⁶⁶⁶

Na imethibiti kuwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- hakuacha Dinari wala Dirham, kaipokea Bukhari kwa isnadi kutoka kwa Amri bin Harith amesema: "Hakuacha Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- Dinar wala Dirham, wala mtumwa wala kijakazi, isipokuwa nyumbu mweupe aliyekuwa akipanda na silaha yake, na kipande cha ardhi alichokitoa sadaka kwa ajili ya wasafiri"⁶⁶⁷

Na imethibiti kutoka katika sahihi mbili kutoka kwa Aisha -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, yakwamba Mtume -**Rehema na**

⁶⁶⁶ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/665.

⁶⁶⁷ Kaipokea Bukhari katika sahihi yake, hadithi namba 4461, Tazama: Riwaya ya Aisha kwa Imam Ahmad, katika Musnad wake, na tazama bin Kathir, Assiratun nabawiyya, 4/445.

Amani ziwe juu yake- alinunua chakula kwa Yahudi kwa mkopo, na akaweka rehani ngao ya chuma ya vita"⁶⁶⁸

Na imepokelewa kutoka kwa Aisha Amesema: "Alifariki Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-** na ngao yake ya vita ikiwa rehani kwa vibaba thelathini vya ngano"⁶⁶⁹

Na alikuwa Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akisema enzi za uhai wake: "Nina haja gani mimi na dunia, sichochote mimi, mfano wangu mimi na dunia ni kama msafiri aliyesafiri msimu wa kiangazi akakaa chini ya mti ili kupata kivuli kwa lisaa limoja kisha akaondoka na akakiacha"⁶⁷⁰Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-** hakuwa na pupa ya kukusanya mali na kuzilimbikiza kwa ajili ya warithi, na alikuwa akitahadharisha juu ya kitendo hicho, katika kauli yake iliyopokelewa na Harith bin Suwaid amesema Abdillah, amesema Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake-** "Ni nani kati yenu anayependa mali ya warithi wake zaidi kuliko mali yake?" Wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakuna yeyote kati yetu ila mali yake anaipenda zaidi. Akasema: "Hakika mali yake ni ile aliyotanguliza (Kwa Allah) na mali ya warithi wake ni ile aliyoibakiza"⁶⁷¹

⁶⁶⁸ Kaipokea Bukhari, Hadithi namba: 2068, 2916, na 4467

⁶⁶⁹ Al-Baihaqi, Dalaailun nubuwwa, Na tazama: bin kathiri, Assiratuna nabawiyya 4/445

⁶⁷⁰ Kaipokea Bukhari katika sahihi yake, kitabu raqaaq, mlango wa kile alichokitanguliza mali yake, 7/176.

⁶⁷¹ Hadithi hiyo ameipokea Muslimu katika Sahihi yake ,Hadithi namba 3554.

Na kwa hakika amesema Mtume-Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani: "Haturithiwi na vile tulivyoviacha ni sadaka, hakika watu wa familia ya Muhammad hula katika mali hii"⁶⁷² Kama ambavyo inavyofahamika kuwa sadaka si halali kwake wala watu nyumba yake Rehema na Amani ziwe juu yake, bali wanakula moja ya tano.

Na walikuja wabobeza wa mashairi na mashairi tofauti tofauti tangu alipofariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika kumuomboleza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mpaka leo hii, na huenda mkweli wao zaidi alikuwa ni mshairi wake Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Hassan bin Thabit Al-Answari, aliyebobea katika kumsifu Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- enzi za uhai wake, kama alivyokuwa mahiri pia kumuomboleza wakati wa kifo chake, naye ndiye mtu wa kwanza kuwafungulia mlango washairi wa kumuomboleza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, kiasi ambacho alikuwa akimlilia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika shairi la Macho ya shairi, aliloliandika bin Hisham.⁶⁷³

Kuandaliwa kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na kuzikwa kwake:

Alipofariki Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, alikuwa akivaa vazi zito, imepokelewa kutoka kwa Buraida -Radhi za Allah ziwe juu yake, amesema: Alitutolea Aisha kikoi kizito vinavyotolewa

⁶⁷² Kaipokea Bukhari sahihi, Hadithi namba: 2578, Tazama: Babu Alkharaaj wal-Imaarah wal-Fayi qaul Alnnabiy,-Rehema na Amani ziwe juu yake-: laa nuurith maa taknaahu swadaqah".

⁶⁷³ Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, mashairi ya Hassan bin Thabiti katika kumuomboleza Mtume, 4/666-669.

Yemen, na vazi katika mavazi haya ambayo watu huyaita Malida, na katika riwaya nyingine alisema kuwa: "Katika vazi hili ilichukuliwa roho ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-"⁶⁷⁴Na hakuna shaka kuwa Aisha alikiacha chumba chake na akatoka baada ya kumfunika Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- walipokusanyika waislamu kumuona Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ndugu zake wa kiume, waliokizingira chumba kikiwa na mwili msafi wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na wakabakia katika hali hiyo katika kipindi chote ambacho waislamu walikuwa wakishughulika na kupeana habari, na aliyekuwa na huzuni kubwa kuliko watu wote ya kumpoteza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ni mtu wake wa karibu binti yake Fatma -Radhi za Allah ziwe juu yake-, na ndio maana watu walikusanyika kwake na nyumbani kwake hapo kukiwa na ndugu wa nyumba ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, wakiongozwa na baba yake mdogo Al-Abbas bin Abdil Muttwalib, na Ally bin Abii Twalib na zubair bin Awamu, wakiwa pamoja na Twalha bin Ubaidillah -Radhi za Allah ziwe juu yao wote.⁶⁷⁵Kama ilivyoonekana kwa Safia -Radhi za Allah ziwe juu yake- kuwa alikuwa akikaza nguo yake kwa nguvu kiasi awezacho kuonyesha kwa vitendo huzuni yake.⁶⁷⁶

Na nyumba nyingi za masahaba zilikuwa ndogo, kiasi kwamba ilikuwa vigumu watu wengi kukusanyika ndani yake kwa wakati

⁶⁷⁴ Ni katika riwaya za Bukhari, Baabu maa dhukira min dii Alnnabiy - Rehema na Amani ziwe juu yake-wa aswahu wasaifihi, waqad'hih, 3108, na Muslim katika sahihi yake, kitabu zziina, Baabu Atawabwii fiil libaas, 34/2080

⁶⁷⁵ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/650.

⁶⁷⁶ Kwa Bin Abii Shaibah katika Maghaaziy, ukurasa wa 414.

mmoja, na wakakusanyika baadhi ya Muhajirina na Maanswari kwa Abubakari Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake-, huku chumba cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kikiwa kimefungwa, kilibakia kiwiliwili chake siku zilizofuata siku ya juma tatu ambayo ndio siku aliyofariki ndani yake, kiasi ambacho watu walishughulika na kupangilia ni nani atakayechukua nafasi ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-. Na huenda hata walilishughulikia hili mapema kabla hata kuandaa mwili twahara wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na kuuzika, kwa kuhisi kwao kuwa bado wako chini ya amri yake madamu mwili wake bado upo haujafunikwa na udongo, na kuhisi kwao kuwa wana wajibu wakupangilia mrithi wake kabla ya kumzika Rehema na Amani ziwe juu yake, na watu wakashughulishwa na kumpa ahadi ya utiifu (Bai'a) Abubakari Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake-.⁶⁷⁷

Na ilipofika siku ya juma nne ambayo ndiyo siku ya pili ya msiba wake -Rehema na Amani ziwe juu yake- Walikusanyika katika chumba cha Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- ndugu wa nyumba ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, baba yake mdogo A-Abbasi bin Abdil Muttwalib, na Ally bin Abii twalib na watoto wa Ami yake Al-Abbas, kama Fadhlul na Kutham, na Osama bin Zaidi, na Swaleh kijana wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- (aliyemuacha huru)⁶⁷⁸Kisha akanadi kwa sauti ya juu mbele za watu Ausi bin Khauli Al-Answari A-khazraji kutoka kabila la Aufu, na alikuwa ni miongoni mwa watu walioshiriki vita vya Badri, Akasema: Tunakuomba kwa jina la Mwenyezi Mungu na sisi tupate nafasi kwa

⁶⁷⁷ Marwan Habki, Tahdhiib siiratu bin Kathiri uk 683, Na tazama Bai'atul Akaba, ndani ya kitabu hiki, Na tazama: Bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/655.

⁶⁷⁸ Kwa Bin Abii Shaibah katika Maghaazi, ukurasa wa 414.

Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na alikuwa anakusudia kuruhusiwa kushiriki pamoja na Manswari katika kumuosha naye ni moja miongoni mwao (Manswari) Ally Radhi za Allah ziwe juu yake akasema: Ingia" akaingia akaungana nao.⁶⁷⁹

Na inasemekana kuwa Abubakari Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- aliwaamrisha wamuoshe watoto wa baba yake.⁶⁸⁰ Na lilikuwa ni swala la kawaida linalojulikana hata kama asingewaamrisha Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yake- kufanya hivyo, watu wa familia ndio wanaotangulizwa kabla ya jamaa wa karibu katika nafasi kama hii, na katika mambo yaliyo na uhakika nikuwa walimuweka kitandani kwake ndani ya chumba kwa ajili ya kumuosha na kwa ajili ya kuthibiti kumswalia kwake naye akiwa juu ya kitanda chake Rehema na Amani ziwe juu yake.

Na walimuosha Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** bila ya kumtoa nguo zake Rehema na Amani ziwe juu yake, imekuja katika riwaya ya Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: "walipotaka kumuosha Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** walisema: Wallahi hatujui je, tumtoe nguo zake Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** kama tunavyowatoa nguo maiti zetu?, au tumuoshe akiwa na nguo zake?, walipohitilafiana, Allah akawashushia usingizi wote wakasinzia kiasi kwamba hakuna yeyote miongoni mwao isipokuwa kidevu chake kiliinama chini ya kifua chake kwa usingizi mzito, kisha akawasemesha mtu kutoka katika pembe za nyumba hawamjui ni nani, kuwa muosheni Mtume -

⁶⁷⁹ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 46622.

⁶⁸⁰ Kaipokea Tirmidhi katika shamaili, Baabu maa jaa fii wafaat Alnnabiy -Rehema na Amani ziwe juu yake- uk, 200, na akasema Al-Albani hadithi ni sahihi Tazama Hamishi ya riwaya.

Rehema na Amani ziwe juu yake- akiwa na nguo zake, wakashituka kutoka usingizini wakaelekea kwa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** wakamuosha, akiwa na kanzu yake wakimwaga maji juu ya kanzu na wakisugua kwa kutumia kanzu bila kutumia mikono yao, akawa Aisha anasema: "Lau kama jambo hili lingenibainikia kabla hajaoshwa, asingemuosha yeyote wasiokuwa wake zake"⁶⁸¹

Na hii ni Rai yake kwa kuwa wao ni maalumu katika kufaa kuuangalia mwili wake uliotwahara na mkamilifu.

Na jambo ambalo halina shaka ni kuwa Maiti anakuwa anahitajia kusafishwa kutokana na vitu vilivyo tumboni mwake lakini Mtume **Rehema na amani ziwe juu yake-**hawakumkuta na uchafu huo wenye kuhitajia kusafishwa, na kwa hakika imepokelewa kuwa (Ally **-Radhi zaAllah ziwe juu yake-** alitafuta kwa Mtume vinavyotafutwa kwa Maiti na wala hawakupata kitu chochote, akasema: "Namtoa kikomboleo baba yangu na mama yangu wewe ni msafi ulipokuwa hai na baada kufa pia". (1421)

Ilikuwa kuoshwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **Rehema na amani ziwe juu yake-**Kwa Maji na Mkunazi, (1422) na alikuwa Ally **-Radhi zaAllah ziwe juu yake-** akimuegemeza kwenye kifua chake na akiwa na Kanzu yake, na alikuwa Al-Abbas na mwanae Al-fadhil na Qutham wakimbusu pamoja na Ally **-Radhi za Allah ziwe juu yake-**na alikuwa Osama Bin Zaid na Swaleh Mtumishi wa Mtume **-Rehema na amani ziwe juu yake-** wakimwagilizia maji na Ally anamuosha na anasugua na Kanzu pasina kutumia mikono yao.(1423)

⁶⁸¹ ameipokea Abuu daudi Fii sitri Almayyit inda ghaslihi, na tamshi ni lake, 3141' Bin Hishaam, Al-siirat Al-Nabawiyat) juzuu ya 4/662.

Kisha Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akazungushwa kwenye nguo mbili nyeupe na shuka lilofumwa kutoka Yemen (1424) na imesemwa kuwa shuka hilo lilikuwa ni la pamba, na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake-amesema:(Alikafiniwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake** katika nguo tatu nyepesi za rangi nyeupe)(1425) na ilikuwa kuoshwa kwake ni maji yatokayo kwenye kisima kilichopo Kubaa ambacho maji yake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake** alikuwa akiyanywa, na kilikuwa kikiitwa kisima cha Saad Bin Khaithamat.(1426, na hii ni Dalili ya kuwa maji yake ni masafi na ni twahara kuliko maji mengine.

Amesema Aisha -radhi za Allah ziwe juu yake- "Alikafiniwa Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- kwa nguo tatu nyeupe zilizo nyepesi aina ya pamba na hakuwa na Kanzu wa Kilemba" (1427) Na imesema kuwa aliachwa na Kanzu yake ambayo alikuwa nayo chini ya Sanda.⁶⁸²⁶⁸³

Na kwa hakika aliwekwa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-juu ya Kitanda baada ya kukafiniwa kwake kisha waislamu wakashauriana namna ya kumswalia Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na Ikawa Rai ya Abuubakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake-ya kuwa wasimtoe Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kwenye sehemu aliyofia wakasema: Ewe

⁶⁸² kutoka katika riwaya ya Bukhariy katika Kitabu Janaaiz, Baabu alkafan bighair qamiisi, Hadithi namba 1271,1272; na Muslim katika sahihi yake, Kitabu cha Jeneza"Katika kukafini Maiti" juzuu ya 45/941.

⁶⁸³ Tazama Abuu daud,kitabu Al-janaaiz,Baabu Al-kafan) ukurasa wa 353.

Swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**- akasema; "Naam", wakasema: vipi twamswalia? akasema: "Wanaingia watu wanaleta Takbira na wanaswali na wanaomba kisha wanatoka, kisha wanaingia watu wengine wanaleta Takbira wanaswali na wanatoka mpaka waingie watu wote, wakasema: Ewe swahaba wa Mtume Mwenyezi Mungu hivi anazikwa Mtume wa Mwenyezi Mungu? akasema: Ndiyo wakasema anazikiwa wapi?" akasema katika sehemu ambayo roho yake imechukuliwa hapo, kwa hakika Mwenyezi Mungu hakuichukua Roho yake isipokuwa katika sehemu nzuri" Basi wakajua kuwa amesema kweli".(1429)

Kisha watu wakaingia kwa ajili ya kumsalia makundi makundi, wanaingia wanaume wanamswalia mpaka wanapomaliza, wanaingizwa wanawake, wanapomaliza wanaingizwa watoto. na hakuna aliyewaongoza watu katika ibada ya kumsalia Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**- yeyote,⁶⁸⁴na waliokuwa wakimsalia ni kana kwamba walikuwa wakiona kama yuko mbele yao hali yakuwa ashakuwa maiti -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-.

Na hakuna shaka kuwa jambo hili lilihitaji mpangilio na nidhamu, kiasi ambacho watu wote walikuwa na shauku ya kutaka kumsalia Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na nafasi ni ndogo, swala likahitaji kuwa na mpangilio, na inaonekana kuwa watu wazima walikuwa na nafasi katika hilo, na imepokelewa kuwa Abubakari Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- alipokea kutoka kwa Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**- Amesema: "Nilimsikia Mtume - **Rehema na Amani ziwe juu yake**- kitu fulani ambacho sijakisahahu, Amesema: "Hakuwahi kumfisha Mwenyezi Mungu Nabii yeyote

⁶⁸⁴ Bin Sa'd, Attwabaqaat 2/289, bin Hisham, Assiratun nabawiyya, 4/663, Na tazama: Bin Abii Shaiba, Al-Maghazi, uk 412

isipokuwa katika sehemu anayopenda kuzikwa hapo" Hivyo, mzikeni mahala pa kitanda chake.⁶⁸⁵

Na yawezekana mapenzi ya sehemu ya kuzikwa yakawa yanatoka kwa Mwenyezi Mungu ni wapi kaburi la Nabii wake liwe, na yawezekana yakawa ni ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- anachagua ni wapi azikwe, na yote haya yanakwenda sambamba na maamuzi ya Mwenyezi Mungu ya sehemu ya kaburi la nabii wake Rehema na Amani ziwe juu yake, kama alivyomchagulia mahala pa kuhamia, na hatukusikia yeyote aliyetoa rai tofauti kuhusu wapi liwe kaburi la Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kwa kupingana na rai ya Abubakari -Radhi za Allah ziwe ju yake.

Na ama kuhusu shimo la kaburi la Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, baada ya kuhamia kwake Madina ilifariki idadi kubwa ya masahaba wake, na walikuwa wakati mwingine wakichimba mwanandani, nacho ni kitobo kinachochimbwa katika ukuta wa kaburi, na wakati mwingine walikuwa wakipasua kati kati ya shimo,⁶⁸⁶na shimo hili linakuwa katikati ya kaburi, na huu ulikuwa ni mfumo wa watu wa Madina, na njia zote hizi ziko sawa zinafanyiwa kazi kulingana na wale waliokuwa wakisimamia zoezi la uchimbaji wa kaburi. Na alipofariki Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- "Wakahitilafiana kuhusu mwanandani na kishimo, mpaka wakazungumza kuhusu hilo, na zikanyanyuka sauti zao, Omari akasema: Msifanye fujo mbele ya Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- akiwa hai au amekufa, au alisema neno mfano wa hilo,

⁶⁸⁵ kaipokea Tirmidhi kitabul Janaizi, uk, 108, bin Hisham Assiratun nabawiyya, 4/263, bin Abii Shaiba, Al-Maghazi, uk 411.

⁶⁸⁶ Tazama: Sahihi Bukhari, Kitabul Janaiz, mlango wa mwanandani na kishimo katika kaburi, 2/96.

wakaagiza wachimba mwanandani na wachimba kishimo, wakamchimbua mwanandani Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kisha akazikwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-"⁶⁸⁷

Na imepokelewa kuwa aliyekuwa akichimba mwanandani ni Twalha bin Zaidi bin Sahli Al-Answari, na alikuwa mchimbaji wa makaburi ya watu wa Madina, na aliyekuwa akichimba kishimo ni Abuu Ubaida bin Jaraha, na aliyeagiza waitwe ni A-Abbasi bin Abdil Muttwalib -Radhi za Allah ziwe juu yake-, wakaja Manswari kwanza wakamchimbua mwanandani Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-,"⁶⁸⁸na kwa kitendo hicho watu wote kwa ujumla hasa hasa masahaba wakapenda kuchimbiwa mwanandani endapo watakufa. Mfano: Huyu hapa Sadi bin Abii wakasi akiwa katika maradhi yaliyokuwa sababu ya kifo chake, alisema: Nichimbieni mwanandani na mniwekee tofali kama lilivyowekwa kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-"⁶⁸⁹.

Na uchaguzi ukaangukia katika mwanandani kulingana kile walichokua wakikitaka masahaba, kiasi kwamba baada ya kuwaita wale watu wawili walisema: "Ewe Mwenyezi Mungu mchagulie mjumbe wako",⁶⁹⁰ikawa mwanandani ndio alioukadiria Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake.

⁶⁸⁷ Kwa Bin Abii Shaibah katika Maghaaziy, ukurasa wa 414.

⁶⁸⁸ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/663.

⁶⁸⁹ Kaipokea Muslim, kitabul Janaizi, Baabu Allahd wanaswbil labin ulaal mayyit .

⁶⁹⁰ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/663.

Alikuwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- pembezoni mwa kaburi mpaka walipomaliza watu wanaume kwa wanawake wadogo kwa wakubwa kumsalia usiku wa manane, kuanzia mchana wa juma nne mpaka usiku wa kuamkia juma tano wa tarehe 14 ya mwezi Rabil Awwal mwaka wa 11 Hijiria, sawa na tarehe 14-06-633:G

Kisha kikawekwa kando ya kaburi kitanda, na akaingizwa Rehema na amani ziwe juu yake kaburini, Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake- ndiye aliyembeba na Ami yake Al-Abbas na watoto wake wawili Kutham na Alfadhlu, na kijana wake Shakarani,⁶⁹¹na inasemekana kuwa Shakarani kijana wa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- aliweka kimsala kilichokuwa cha mjumbe wa Allah chini yake, alichokuwa akikitandika Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- na akikivaa, akasema: Wallah hakuna atakayekivaa baada yako milele, na hii ni baada ya kuhofia kuwa watu wanaweza kunyang'anyana.⁶⁹²

Na alishirikiana nao katika hilo Ausi bin Khauli Al-Answari -Radhi za Allah ziwe juu yake, na alipowekwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**- kaburini alisimika tofali ili kuzuia udongo (Kama wanavyofanya watu makaburini siku hizi), tunaliona hilo kwa mfumo huo huo mpaka leo, wanafuata katika hilo kilichofanyika kwa Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-, kisha baada kukamilika uwekaji wa tofali na kumfunika udongo wa mwanzo, wakamimina

⁶⁹¹ Bin Sa'd, Attwabaqaat, 2/275, na tazama: Bin Abii shaiba Al-Magahazi, uk 414,415.

⁶⁹² Bin Hisham Assiratun nabawiyya, 4/664, Kitabul Janaizi, Baabu maa jaa fii thaubil waaahid yulqaa tahtal qabrii, (1047) Na tazama: Sahihi Muslim kitabu Janaizi, Baabu ja'li Alqitwiif fiil qabri, 91/968.

udongo juu ya kaburi lake Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na hiyo ilikuwa usiku wa manane.

Anasema mama wa waumini Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- "Hatukujua kuzikwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- mpaka tuliposikia sauti za sururu, usiku wa manane katika usiku wa kuamkia juma tano"⁶⁹³

Na asubuhi ya siku iliyofuata aliadhini Bilali adhana ya alfajiri, aliposema: Ash-hadu anna Muhammadan Rasuulullaah, ninashuhudia kuwa Muhammadi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akalia na akawaliza watu, na ikaonekana wazi huzuni yao juu ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-.⁶⁹⁴

Na lilibakia kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kama lilivyo ndani ya chumba cha Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- bila kuwekwa wazi wala kuzidi kunyanyuliwa kutoka katika kiwango cha ardhi,⁶⁹⁵ nalo ni jambo lililotekelezwa kwa elimu ya masahaba kwa hadithi ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- aliyoipokea Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- na akaongeza kusema kuwa: "Yakwamba yeye Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema akiwa katika maradhi yake ambayo hakunyanyuka tena baada yake": "Amewalaani Mwenyezi Mungu mayahudi na wakristo

⁶⁹³ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyyat juzuu ya 4/664.

⁶⁹⁴ An nadwaa: Assiratuna nabawiyya, uk 414

⁶⁹⁵ Sahihi Bukhari, kutoka kwa Abubakari bin Iyashi, kutoka kwa Sufian Ath thauri, yakwamba yeye aliliona kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- likiwa limenyanyuliwa kidogo (Mithili ya nundu ya mnyama), mlango wa yaliyokuja kuhusu kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- hadithi namba: 1390.

waliyafanya makaburi ya manabii wao kuwa misikiti" Laiti isingelikuwa hivyo basi lingedhihirishwa kaburi lake, isipokuwa alihofia, au palihofiwa kufanywa msikiti.⁶⁹⁶

Na baada ya hapo alizikwa Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yake- jirani na kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kisha akaomba idhini Omari -Radhi za Allah ziwe juu yake- ya kuzikwa ndani ya chumba hicho hicho, Aisha akamuidhinisha, katika kisa kirefu.⁶⁹⁷

Na kaburi la Abubakari liko chini ya kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na kaburi la Omari liko chini ya kaburi la Abubakari, na yako upande wa kibla, kiasi ambacho kichwa cha Abubakari kiko usawa wa bega la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, na kichwa cha Omari kiko usawa wa bega la Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yao- na Abubakari yuko nyuma ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na Omari yuko nyuma ya Abubakari -Radhi za Allah ziwe juu yao- wakawa marafiki wa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- katika chumba kitukufu, kama walivyokuwa marafiki zake enzi za uhai wake -Radhi za Allah ziwe juu yao-⁶⁹⁸Na

⁶⁹⁶ Kaipokea Bukhari, katika sahihi yake, kitabu Janaizi, mlango wa yaliyokuja kuhusu kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na Abubakari na Omari, Namba: 1390.

⁶⁹⁷ Tazama: Omari bin Abii Shaiba, Tarikhul Madina 4/944 bin Sa'd, Attwabaqaat 3/368.

⁶⁹⁸ Tazama: Jinsi gani aliomba idhini Omari kwa Aisha ya kuzikwa pamoja na Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, katika kitabu cha Bukhari katika sahihi yake, Hadithi namba: 1390.

makaburi yote yalikuwa yakinyanyuliwa juu ya ardhi usawa wa vidole vinne.⁶⁹⁹

Walikuwa watu wote na ukaribu mno na Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** wakati wa maradhi yake na wakati wa kifo chake, wakiwemo wanawake mfano wa Aisha **-Radhi za Allah ziwe juu yake-** na wengine waliobakia katika mama wa waumini, na Fatma binti wa Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-**, na katika wanaume kama Abubakari na Omari na watu wa nyumba ya Mtume kama Ally na A-Abbasi na watoto wake, na Anasi bin Maliki na Osama bin Zaidi **-Radhi za Allah ziwe juu yao-** ndio maana imenukuliwa kutoka kwa Aisha **-Radhi za Allah ziwe juu yake-** Sisi tuna habari na usia mwingi kutoka kwake ambao hajaunukuu mwingine yeyote, na hivi ndivyo inavyoonekana kuwa wanawake walikuwa na nafasi kubwa ya kushiriki pamoja na umma mzima katika kumjali Mtume **-Rehema na Amani ziwe juu yake-** wakati wa kuhitaji kwake kufanya hivyo, na hata katika maradhi yake yaliyokuwa sababu ya kifo chake.

Na huenda kumuuguza kwake Mtume-ALLAH amridhie-na kuwa Mtume chumbani kwake, na kifo chake akiwa kwenye kifua chake, na kuwa kwakwe Aisha ni mwenye kumnyanyua mwisho wa uhai wake, imedhihirika juu ya ubora wake na nafasi yake kwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake na yeye Mtume anamfahamu Aisha kuliko mtu yeyote, na ukweli wa watu wa nyumbani kwake na yeye Aisha ni miongoni mwao na umma kumuamini yeye juu ya Mbora wa viumbe sala na amani ziwe juu yake, na alikuwa Aisha ni Msichana mwenye kuhifadhi kwa kila kilicho tokea kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake kutokana na kauli na vitendo, na hakika imethibiti hekima ya Mtume sala na amani ziwe juu yake katika

⁶⁹⁹ Al-kustwalani: Al-Mawahibu daaniya, 3/401.

kuomba kuugulia kwa Aisha-ALLAH amridhie- namna alivyo hifadhi kutoka kwa Mtume na akazingatia, kama alivyo kuwa na mapenzi mahususi ndani ya moyo wa Mtume sala na amani ziwe juu yake na pumziko lake likiwa kwa Aisha na halipatikani kwa yeyote.

Na kisha baada ya kufa kwake hakika ilivyo mapokezi mengi yaliyo fungamana na maradhi ya Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake na kufa kwake na mwisho wa wasia wake zilikuwa ni katika njia ya mama Aisha-ALLAH amridhie- na hili linabainisha ubora wake na elimu yake kwa kila mwenye akili.

Kama ilivyo, kuwakwake katika nyumba ya Aisha alikuwa akimruhusu Abubakar-ALLAH amridhie- kuingia kwa Mtume na kuwasiliana naye zaidi kuliko mtu yeyote, na alikuwa Ally-ALLAH amridhie- na watu wa familia wakiwa karibu kwa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake, wakiungana naye wakimjulia maendeleo yake, na walikuwa watu wa familia na watu wa familia ya Abubakari wamejikusanya na pamoja nao Muhajirina na Maaswari nao ndio vipenzi wa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake kabla ya kufa kwake na baada ya kufa kwake, baina yao kuna kupendana na kuoneana huruma na kuzoeana ukiongeza na ukwe jambo ambalo huwezi pata kwa wengine, na waliokuwa bora zaidi katika kumuandaa Mtume na kumuosha ni watoto wa baba yake walio kuwa karibu, anakusudia watoto wa Abdil-Mtwalib na wajukuu zake, na walisimamia jambo hili kwa kila uaminifu, na wao ndio bora kwenye mfano wa sehemu hii, bila kuwashusha hadhi maswahaba wengine, na walikuwa wengi wao wakifanya kazi papo kwa papo kwa ajili ya kuandaa mwili wa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake ni Ally Ibn Abiy Twalib-ALLAH amridhie- Mtoto wa baba mkubwa na Mtume, akiwa pamoja naye Al-Abbas na watoto wake na waachwa huru wa Mtume wa ALLAH sala na amani ziwe juu yake na kwa kushirikiana na watoa viashirio miongoni mwa Maaswari.

KUCHAGULIWA ABUBAKARI -RADHI ZA MWENYEZI MUNGU ZIWE JUU YAKE:

Alikuwa Mtume sala na amani ziwe juu yake ni kiongozi wa Waislamu katika sala zao, na akaweka misingi ya Nchi ya kiislamu na kuwa yeye ndiye kiongozi wake na mjengaji mkuu, na ilikuwa hekima ya Mtume sala na amani ziwe juu yake na watu wote ni kuendelea kwa Nchi ya kiislamu na upangikaji na kuhifadhi haki na kusimama kwa Dini, na malengo ya Mtume sala na amani ziwe juu yake ni kuendelea pande zote za Dunia zilizo tofauti kwa lengo la kufikisha ujumbe na udamini wa Uadilifu na amani kwa watu wote, pamoja na kufikiria kwake kuanza kwa Wafursi (Irani) na Waroma waliokuwa jirani na miji ya Warabu, na hapo yalikuja maelekezo yake kwa jeshi la Osamah Ibn Zaid kuliandaa kutoka muda mchache kabla ya kifo chake kwenda sehemu za Sham.⁷⁰⁰ na hili linakusudia ulazima wa kuwepo msingi wa uongozi kwa ajili ya Nchi akiisimamia na kupitisha maagizo ya Mtume sala na amani ziwe juu yake na wasia wake, na kusimamisha sheria za ALLAH na kuendeleza Dunia kwa Dola na ulinganizi wa Kiislamu.

Na hili ndilo lilikuwa lengo la Mtume sala na amani ziwe juu yake, pamoja na yote hayo hakika yeye hakumuusia yeyote yeye mwenye ili awe msimamizi wa jambo baada yake .⁷⁰¹ na hakika kulikuwa na ishara zilizo kuwa wazi miongoni mwa hizo kumpambanua Abubakar swidiq-ALLAH amridhie- kwa jambo hili, na alikuwa ndio msingi wa Dola ya Kiislamu kwa daraja la kwanza kwa wakazi wa mji wa

⁷⁰⁰ angalia: sahihi Bukhar, kitabu Al-Maghazy, Baabu biithi Alnabiy Osamah Ibn Zaid fii maradhi mautihi, hadithi namba: 4668-4669.

⁷⁰¹ Tazama: Hadithi namba: 2740, 2741, kwa Bukhari katika sahihi yake, Na tazama: Kifo cha Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ndani ya kitabu hiki.

Maanswari, ukiongezea na Muhajirina -ALLAH awaridhie wote- na kila sehemu yake ni kama mkusanyiko katika utawala na idara za Nchi na Usaidizi kwa Mtume sala na amani ziwe juu yake katika kuendesha mambo tofauti pamoja na kutofautiana katika lengo na nafasi baina ya wana jamii.

Ilikuwa wazi kwa wote aya zilizoteremka zikiamrisha kuiendeleza na kuibeba dini, na yale yanayo hitajika katika nidhamu na kutokurudi nyuma baada ya kifo cha Mtume -**Rehema na Amani ziwe juu yake**-⁷⁰²:

﴿وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَى عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾﴾ [آل عمران: 144]

"Hakuwa Muhammad, rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, ni kiumbe aina nyingine, isipokuwa yeye ni Mtume wa jinsi ya Mitume wengine waliokuweco kabla yake, afikishe ujumbe wa Mola wake. Basi iwapo atakufa, kwa kumalizika muda wake, au atauawa, kama walivyoeneza uvumi maadui, kwani mtarudi nyuma na kuacha dini yenu na kuyaacha aliyowaletea Mtume wenu? Basi yeyote miongoni mwenu atakayerudi nyuma akaiacha dini yake, yeye hatamduru Mwenyezi Mungu chochote, bali ataiduru nafsi yake madhara makubwa. Ama atakayekuwa na msimamo imara juu ya Imani yake na akamshukuru Mola wake juu ya neema ya Uislamu, hakika Mwenyezi Mungu Atamlipa malipo mazuri kabisa". [Al-Imran: 144]. Ndiyo, hakika wao waliwashukuru waliomchagua Abubakari ili waweze kusimamisha nidhani kwa kujiandaa kwa ajili ya kuhukumu kwa kila atakaye rudi nyuma

⁷⁰² Angalia: Riwaya ya Bukhar katika sahihi yake, hadithi namba:3668,kitabu ubora wa maswahaba.hadithi namba: 3668.

miongoni mwa wale walio acha dini na mfano wao, na ikawa wazi maana ya aya katika sehemu hiyo na walio hifadhi juu ya nguvu na mpangilio, na kwa ajili ya kujiandaa kuzuia Dola ya Mtume sala na amani ziwe juu yake dhidi ya walio acha dini ambao ALLAH aliwakutanishia Abubakar na wasaidizi wake miongoni mwa Muhajirina na Maaswar-ALLAH awaridhie-

TUKIO LA SAKIFA:

Na katika siku ya Juma tatu ambayo Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** alifafriki, walikusanyika Answar- Nao ni watu wa Madina waliokuwepo kabla ya Mtume kuhamia Madina-walikusanyika kwa Saad Bin Ubaadah -Radhi za Allah ziwe juu yake-naye ni miongoni mwa wakubwa wa Saqiifa Banii Saaida, katika wakati ambao Ally Bin Abii Twalib na ahlu Bait wengine walikuwa kwa Fatma -Radhi za Allah ziwe juu yake- Na alikuwa Omari -Radhi za Allah ziwe juu yake- na Baadhi ya Answari na Muhaajirina wamekusanyika kwa Abubakar-Radhi za Allah ziwe juu yake-(1149) na hali ilikuwa ni ngumu na fikra ni zenye kuendelea, Answari walikuwa wanaona kuwa wao ni watu wa Madina na wakaukabidhi kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**na kuwa baada ya kufariki Mtume jambo hilo linahitajia kuratibiwa tena upya, na huenda ikawa kwa badhi ya watu katika wanamtazamo wa kurudi uongozi kwa watu wa Madina baada ya kufariki Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na wengi miongoni mwa Muhaajiriina na Answar walikuwa wanamtazamo tofauti, na walikuwa wanaona kuwa Dola ya kiisalmu ni yenye Nidhamu ya kuenea na pana, Dola hiyo ilisimama katika Mji wa Madina na itaendelea baada ya kufariki Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake-**na ipo mbali na taratibu zote za zamani kabla ya kuhama na wengi waliokuwa wanafaa kuiongoza Dola ni watu waliokuwa wakifahamu zaidi nidhamu zake na utaratibu wake na sheria zake, nao ni wale waliohama Mwanzo ambao walifuatana na Mtume katika mji wa Makkah na Madina na wakajifunza kwenye mikono yake, na kiongozi wao ni Abuubakar

Swiddiq, na wao ndiyo wanastahiki zaidi kulishika jambo hilo kuliko watu wengine baada ya kufariki Mtume, na jambo hili ilikuwa linajulikana kwa baadhi ya Answar na Muhaajirina miongoni mwa watu wa Madina

Kwa hivyo watu wa Madina walifanya haraka kumpa taarifa Abuubakar na Omar na waliokuwa pamoja nao taarifa ya kukusanyika Answar katika sehemu ya Saqiifat Banii saaida, na wakawataka wote hao wawili wahudhurie kikao hicho kabla halijatokea jambo ambalo watalichukia, na hii ilikuwa ni dalili ya pupa ya Answari ya kuhudhuria kikao cha masheikh wa Muhaajiriina Omar akamwambia Abuubakar (Twende nasi kwa ndugu zetu hawa Answar ili tuone wanafanya jambo gani) (1450)

Na wakiwa njiani walikutana na watu wawili miongoni mwa Answar nao ni Uwaimir Bin Saaidah Al-answariy na Mian Bin Adiy kutoka kabila la Aj-laan, wakawaambia hamna ulazima wa kuwakaribu enyi kongamano la Muhaajiriina endeleeni na majukumu yenu⁷⁰³ na ilikuwa ni wazi kuwa hapakuwa na ushindani kati ya Answar na Muhaajiriina bali yalikuwa ni mazungumzo na ndani yake kulikuwa na kuheshimiana baina ya pande mbili ambazo amezisifia pande hizo Mwenyezi Mungu kutakasika na machafu ni kwake:

﴿وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ
وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾
[التوبة: 100]

⁷⁰³ kutoka katika Hadithi ya Omar Bin Khattwab ,Al-maghaazyi Libni Abii Sahaibah ukurasa 424, Tazama Al-Raudhul Aniiif juzuu ya 4/472.

"Na walio tangulia mwanzo miongoni mwa muhajirina na maanswari na wale walio wafuata kwa wema ALLAH amewaridhia na wao wamemridhia na amewaandalia wao mabustani yapitayo chini yake mito, wataishi ndani yake milele, huko ndiko kufaulu kukubwa". [Al-Taubah: 100] Ambao waliwafikishia Abuubakar na Omar habari za kukusanyika ni miongoni mwa Answari, na waliosema kuwa si lazima kwenu kuhudhuria kikao hicho endeleeni na majumu yenu ni miongoni mwa Answari, na Omar -Radhi za Allah ziwe juu yake-alisema: "Tupeleke kwa ndugu zetu Answar hivyo kila mmoja alikuwa akiona kuwa yeye ni ndugu wa Mwenzake na siyo mashindano wala kuupenda uongozi, lakini ilikuwa ni kujitahidi kwenye haki na kufikia hatua nzuri zaidi, japo kuwa baadhi yao ambao wanawachukia maswahaba walikuwa na mtazamo mwingine uliojengwa kwa kuwashuku maswahaba na kila walifanyalo.

Na huenda Omar -Radhi za Allah ziwe juu yake- alihisi baadaye kwenye ukhalifa wake mfano wa mtazamo huu, yeye mwenyewe akawahadithia watu yaliyotokea pale Saqiifat Banii Saaida katika hadithi ndefu aliyeipokea Bin Abbas amesema: Nilikuwa nikimjia Abdurahman Bin Aufi na sisi tukiwa na Omari Bin Khattwab sehemu ya Minna, nikimfundisha Abdurahman Bin Auf Qur'an basi nikamjia nyumbani na wala sikumkuta ni kaambiwa kuwa yupo kwa Kiongozi wa Waumin, basi nikamgojea mpaka akaja, basi akaniambia: "kwa hakika leo amekasirika sana sijawahi kumuona amewahi kukasirika mfano wa alivyokasirika siku ya leo", akasema: kwa nini akasirike hivyo? akamfikishia kuwa sababu ni watu Wawili waliozungumzia uchaguzi wa Abuubakar", akasema: "Namuapia Mwenyezi Mungu kuwa jambo hilo ni la haraka sana lisilokuwa na kifani, hivi ni jambo gani linalomzuia mtu ikiwa atakufa huyu asimame na kwenda kwa mtu anayependa na akamuunga mkono ili awe kama alivyokuwa", akasema: Basi akaazimia Omari azungumze na watu, akasema; Nikamwambia :usifanye hivyo ewe Amiri wa waislamu kwa hakika wewe upo kwenye mji ambao wamekusanyika humo makabila

mchanganyiko ya waarabu wote, na wewe ikiwa utaongea maneno, yatachukuliwa kutoka kwako, na yatasambaa kila mahala na huwezijua nini kitatokea baada ya hapo na kwa hakika atakaye kusaidia ni yule ambaye uliyemjua kuwa atakuwa kwenye mji wa Madina, na tulipofika Madina aliachwa mpweke mpaka akaenda na akashika nguzo ya membari upande wa kulia, na akanijia Said Bin Bin Amrou bin Nufail mpaka akakaa nami nika mwambia: utasikia yale niliyokwambia, akasema: walipokusanyika watu alitoka Omar akaja mpaka akakaa juu Membari, kisha akamshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifia, kisha akamtaja Mtume na akamswalia, kisha akasema: "kwa hakika Mwenyezi Mungu amembakisha Mtume baina yetu ukawa wahyi unamteremkia kutoka kwa Mwenyezi Mungu akihalalisha na kuharamisha kwa Wahyi huo, kisha Mwenyezi Mungu akamchukua Mtume wake, akaondosha alichotaka kukiondosha na akabakisha alichotaka kukibakisha basi tukashika baadhi na yakatutoka baadhi, na ilikuwa miongoni mwa tuliyokuwa tukiyasoma, "Msiwachukie Baba zenu, kwani kufanya hivyo kwenu ni kukufuru" na ikateremka Aya ya kupiga mawe, na akapiga mawe Mtume, nasi tukapiga nae, namuapia yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake! kwa hakika niliihifadhi na nilijua na kuitambua, lau kama si kuchelea kuwa watu watasema Omari kaandika vitu ambavyo havipo kwenye Msahafu ningeandika kwa mkono wa wangu, na adhabu ya kupigwa mawe ipo kwa namna tatu, ni kudhihiri kwa Mimba, au kukubali kwa mwenye kosa au kushuhudia mashahidi waadilifu kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu.

Na kwa hakika imenifikia taarifa kuwa watu wanasema kuhusu Ukhalifa wa Abuubakari: kwa hakika jambo hilo lilikuwa la haraka sana lisilokuwa na kifani, na ikiwa jambo hilo ni kama hivyo, basi Mwenyezi Mungu alimpa kheri za ukhalifa na akaulinda kutoka na na shari zake, ni nani miongoni mwenu ambaye watu wanaweza kumkubali kwa pamoja kama ilivyokuwa kwa Abuubakari?, kwa

hakika hayo ndiyo yalikuwa makubaliano ya watu kuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- amefariki tukapewa kiongozi baada yake, nasi tukaambiwa kuwa hakika Answar wamekusanyika sehemu ya Saqiifat Banii Saaida wakiwa pamoja Saad bin Ubaadat wanamchagua yeye, basi nikasimama pamoja na Abubakari na Abuu baidah bin Jaraah na tukaelekea walipo, wakapatwa na mshutuko kuwa huenda kukatokea mpasuko katika uislamu. basi tukakutana na watu wawili miongoni mwa Answar, na ni watu wakweli, nao ni Uwaimir bin Saaidah na Muiin Bin Adiy, basi wakasema hao wawili: "wapi mmekusudia kwenda? tuka wajibu "Tumekusudia kwenda kwa watu wenu, kutoka na habari iliyotufikia kuhusu jambo lao, basi wakasema Rudini kwani hakika nyinyi hamtopingwa, na wala halitolewa jambo ambalo mnalichukia tukalikataa ila tutalipitisha, na mimi nimepokea maneno nataka kuyazungumza, mpaka tukafika kwa watu, ghafla tukawakuta wamejazana kwa Saad nayeye yupo kitandani hali yakuwa ni mgonjwa mno tulipowajia walizungumza na wakasema: "Enyi kongamano la makuraishi, sisi tuna kiongozi wetu na nyinyi mna kiongozi wenu" Akasimama Khubaib Bin Al-Mundhir na akasema:"Hakika mimi ni kisiki cha mti mwenye rai ambayo itaweza kutatua mgogoro huu na mimi nitadhamini kila kitu, ikiwa mtataka, namuapia Mwenyezi Mungu tunaweza kulirudisha jambo kama lilivyokuwa mwanzo, akasema Abuubakari: "Tulieni hivyo hivyo", basi nikaenda kwa ajili ya kutaka kuzungumza, akasema: "Nyamaza ewe Omari", Basi akamuhimidi Mwenyezi Mungu na akamsifia, kisha akasema: "Enyi kongamano la Answar! kwa hakika sisi twamuapia Mwenyezi Mungu kuwa hatupingi utukufu wenu, wala hatupingi misukosuko mliopitia katika Uislamu, wala hatupingi haki zenu za wajibu kwetu sisi, lakini nyinyi mwajua kuwa hiki kijiji ni cha makuraishi ni sehemu ya makazi ya waarabu na humo hakuna wengine wasiokuwa wao,na kuwa Waarabu hawawezi kukusanyika na kumuunga mkono isipokuwa mtu atokanaye na wao,hivyo sisi ni viongozi na nyinyi ni Mawazir Basi muogopeni Mwenyezi Mungu na wala msiusambaratishe uislamu, na wala msiwe watu wa mwanzo

kuleta uzushi eleweni vyema kuwa nimewaridhia, mmoja wa hawa watu wawili ni Mimi na Abu Ubaidat Bin Jarrah, basi yeyote mtakae mchagua kati yao basi huyo ndiye mwaminifu kwenu nyinyi", akasema namuapia Mwenyezi Mungu hakujabakia kitu chochote katika vitu nilivyokuwa napenda kuvisema isipokuwa alivisema vyote siku hiyo isipokuwa maneno haya, namuapia Mwenyezi Mungu ikiwa nitauliwa kisha nikafufuka kisha nikauliwa na kukufuka nikiwa sijafanya maasi ni bora kwangu zaidi kuliko kuwa Kiongozi wa watu ambao Abuubakri yumo miongoni mwao", akasema Omar: "Enyi kongamano la Answaar! Enyi kongamano la Waislamu! hakika mtu anayestahiki zaidi kushika jambo la Mtume baada ya kufa kwake ni yule mtu wa pili katika wawili wakiwa pangoni naye ni Abuubakar mshindanaji wa wazi kabisa kisha nikauchukua mkono wake na akanitangulia mtu miongoni mwa watu wa Madina, akapiga juu ya mkono wake kabla yangu, kisha baada yake nikafuata na wakafuatia watu wengine, basi saad akaenda kinyume kisha watu wakasema ameamgamia Saad, basi nami nikasema: "Muhesabuni kuwa amepata hasara mbele ya Mwenyezi Mungu, kisha tukaondoka na wakati huo Mwenyezi Mungu akajaalia waislamu kukubaliana kumchagua Abuubakar, namuapia Mwenyezi Mungu akawa kwa namna isiyokuwa na mfano kama mlivyosema, Mwenyezi Mungu akampa kheri za ukhalifa na akamkinga na shari zake basi yeyote atakayeomba cheo mfano wake basi hapasi kuungwa mkono yeye wala aliyemkubali"⁷⁰⁴.

Na ilikuwa ni njambo la wazi katika majibishano yalijiri pale Saqiifat banii Saaida hali ya Answar kuwawaheshimu Muhaajiriina ,na muhaajiriina wakawaheshimu Answar na

⁷⁰⁴ Al-Maghaaziy Bin Abii shaibah kurasa wa 422-425;Al-Siirat Nabawiyat juzuu ya 4/659.

kubadilisha na mtazamo,na ukaonekana wazi uchamungu wa Abuubakar na Omar katika Ukhalifa(1453)na pupa yao katika kufuata nidhamu,basi nguvu ya Dola na maslahi ni ya waislamu wote na viongozi wao ni watu wa Makkah na Madinah Dola ambayo walianzisha wao pamoja na Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-Kama alivyokuwa wazi kuwa Abuubakar alikuwa anapupa ya kuwanyamazisha Answaar,na vilevile alikuwa akiwasifia wakati alipokuwa akiwaongelesha,na kwa hakika mmoja wa Answaar alitoa pendekezo kuwa mmoja kati ya Answaar awe ni kiongozi na mmoja katika Muhaajiriina awe kiongozi,Omar akakataa jambo hilo- Radhi za Allah ziwe juu yake-(1454)na kwa hakika kumepokewa Riwaya nyingine kuwa yeye:katika hiyo siku alitoka Abuubakar na Omar mpaka wakaja kwa watu wa Madina akasema Abuubakar "Enyi kongamano la Answaar kwa hakika sisi hatupingi haki zenu,na wala haki haipingiki kuwa haki zenu ni zenyekuhifadhiwa,na kwa hakika namuapia Mwenyezi Mungu hatukuwahi kupata heri yoyote isipokuwa nyinyi mmeshiriki katika kupata heri hiyo,lakini waarabu hawaridhiki wala hawatotulia nafsi zao isipokuwa kwa mtu atokanaye na Quraishi,kwa sababu wao ni mafasaha katika Lugha na ni watu wenye muelekeo na niwarabu wenye nyumba zilizo kati na kati na niwa watu wenye tabia nzuri sana katika Waarabu,basi njooni kwa Omar na mumuunge mkono"akasema:wakasema hapana.Omar akasema kwa nini? wakasema tunaogopa upanga,akasema Omar: ama kuishi unavyotaka haiwezekani basi akasema mchaguweni Abuubakar,basi akasema Abuubakar kumwambia Omar:wewe ni mwenye nguvu kuliko mimi,Omar akasema wewe ni Bora kuliko mimi akasema neno hilo mara ya pili na aliposema neno hilo mara ya tatu Omar akamwambia Abuubakar:kwa hakika nguvu zangu zinaenda sambamba na ubora wako,akasema:basi muungeni mkono Abuubakar akasema:na watu wakamjia Abuu Ubaidat wakati wa kumuunga mkono Abuubakar akasema :hivi mnanijia mimi na hali yakuwa mna mtu wa tatu katika watatu,akasema Bin Auni:nikamuambia Muhammad:ni nani wa tatu

katika utatu?akasema ni neno la Mwenyezi Mungu. ((Ikiwa hamtomnusu kwa hakika alikwisha mnusuru Mwenyezi Mungu wakati walipomtoa wale waliokufuru wakiwa wawili,pindi walipokuwa kwenye pango alipomwambia mwenzake usihuzunike kwa hakika Mwenyezi mungu yupo pamoja nasi)) (Al-Tauba kuazia aya 40)⁷⁰⁵⁷⁰⁶

Na kwa hakika ni jambo la kawaida kubadishana mitazamo na fikra nakutofautiana wakati mwingine na kujadiliana na kusikiliza Rai tofauti tofauti,na hili kikawaida ni linatilia nguvu kuwa mkutano huu ulifanyika bila kuwa na makubaliano kabla ya hapo,na kwa hakika walikwenda wote kwenye kutazama maslahi ya wote na kutafuta haki ya hiyari na nia ya kweli.

Na kwa hivyo ndiyo maana ikawa Rai ya Umar -Radhi za Allah ziwe juu yake-zimeelekea upande wa Sheria pale aliposema: ((Enyi kongamano la Answar ,Hivi siyo nyinyi mnaejuwa kuwa Mtume-Radhi za Allah ziwe juu yake-alimuamrisha Abuubakar awasalisha watu?waka sema ndiyo ni sisi akasema:basi ni nani miongoni mwenu nafsi yake inapenda atangulia Abuubakar?wakasema tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu na kutokumtangulia Abuubakar))(1456)

Na kwa hakika alisimama mzungumzaji miongoni mwa Answari akasema: "Mnajua kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**- alikuwa ni miongoni mwa Muhaajirina na Khalifa wake alikuwa ni miongoni mwa Muhaajirina, na sisi tulikuwa

⁷⁰⁵ Riwaya ya Bukharir katika sahihi yake, Baabu fabwil Abuubakar swiddiq,hadith namba: 3668.

⁷⁰⁶ Bin Hishaam Al-Siirat Al-nabawiyat juzuu ya 4/393

ni watetezi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na sisi ni watetezi wa Khalifa wake kama tulivyokuwa ni watetezi wake" (1457) na akafanya haraka mmoja miongoni mwa Answaar na akamuunga mkono kabla ya Omar Bin Khattwab, (1458) kisha mahudhurio ya Saqiifat yakawa ni yenye kufuatana kwa kumchagua Abuubakar pasina yeye kupenda kuchaguliwa, na wote waliokuwa wakihudhuria walikuwa ni watu wa Madina isipokuwa Abuu Ubaidat Bin Jarraah na Omari Bin Khattwab -Radhi za Allah ziwe juu yao- na Uungaji mkono huu ulikuwa ni maalumu kwa Uungaji mkono wa Saqiifat Banii Saaida kwa aliyehudhuria, na wala hakusemwa vibaya yule ambaye hakuudhuria, na ilikuwa ni siku ya Juma tatu tarehe 12 katika mwezi wa mfungo Sita siku ambayo iko sawa na siku aliyofariki Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na amani ziwe juu yake-

Na hapana shaka kuwa hawa waungaji mkono wangekuwa wanatetesi walau kidogo za wasia wa Mtume-Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu uongozi wa atakaekuwa baada yake kuwa ni wa Abuubakri basi wasinge jadiliana wale waliokusanyika,na wangeunga mkono moja kwa moja na wala wasingebadilisha na Rai na Ushahidi,kama ambavyo ulikuwa wasia kwa Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake- ulifichika na maswahaba hawakuujuwa wasia huo - Radhi zaAllah ziwe juu yao- na waliposhindwa kuujuwa wasia huo,basi waliujuwa waliobora miongoni mwao,nao ni wanafunzi wa Muhammad-Rehema na amani ziwe juu yake-malezi yake na malezi ya maswahaba walibeba silaha na mioyo yao ikawa pamoja nae:

Kuna miongoni mwa waumini wametekeleza yale waliyo muahidi ALLAH,kuna miongoni mwao walikwisha kufa,na baadhi yao wanangojea,wala hawakubadilisha(ahadi)hata kidogo. Al-Ahzaab /23 Na vipi wanaisahau wasia kirahisi hivi,kama ambavyo Ally hakukumbuka wasia wala kuutafuta huo wasia na yeye ni Shujaa mkubwa -Radhi za Allah ziwe juu yake- ametakasika Mwenyezi

mungu siyo hivyo haogopi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lawama ya mwenye kulaumu

Uungaji mkono huu muhimu haukuwa ni wa mwisho,hivyo kukawa na umuhimu wa kuweka Uungaji mkono kwa wote,basi ikawa ni kesho yake nayo ilikuwa ni siku ya Juma Nne baada ya Swala ya ya Al-fajiri,ukawa ni uungaji mkono wa AbuubakarAl-swiddiq baada ya swala na Ulitambuliwa kama Mnasaba mkuu wa kuthibitisha uongozi,na hiyo ilikuwa baada ya kumchaguwa na kumpigia kura kutokana na wingi wa Answar na idadi ndogo ya Muhaajiriina wanaotokana na wahusika wa ufungaji mkataba na uvunjaji,hivyo wakamchaguwa na wakamuunga mkono kwa namna walivyoona kutokana na kuwachiwa na mtu wa Mwenyezi mungu awalishe watu kabla ya kumtanguliza kwake yeyote,na kwa hakika alisimama Omar akaongea na watu.

Amepokea Bin Is-haqa kutoka kwa Anas bin Maalik Amesema: Na alipochaguliwa Abuubakar pale Saqiifat na ikawa imefia hiyo kesho,alika Abuubakar juu ya Membar ,basi akasimama Omar na akaongea kabla ya Abuubakar:Basi akamuhimidi mwenyezi mungu na akamsifia kwa yale anayostahiki kwayo,kisha akasema,Enyi watu kwa hakika mimi jana niliwaambia maneno ambayo sikuyatowa kwenye kitabu cha mwenyezi mungu,na wala maneno hayo hayakuwa ni Ahadi ambayo ameniahidi Mtume wa Mwenyezi mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**- lakini mimi nilikwisha ona kuwa Mtume atalisimamia jambo letu,anasema kuwa jambo hilo litakuwa mwishoni mwetu,na kwa hakika Mwenyezi Mungu amewaachieni kitabu chake ambacho ni muongozo wa mwenyezi mungu na mtume wake-**Rehema na amani ziwe juu yake**-,na ikiwa mtashikamana nacho basi atawaongoza Mwenyezi Mungu kwa muongozo utokae kwake,na kwa hakika Mwenyezi Mungu amelikusanya jambo lenu kwa mtu ambaye ni bora kwenu,ni swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**- wapili katika wawili pale wawili hao walipokuwa

pangoni,basi siamameni na mumuunge mkono,basi watu wakamuunga mkono baada ya Ungaji mkono wa Saqiifat).(1459)

Na huu uungwaji mkono ulikuwa ni wa watu wote kwa ujumla kwa kila aliyehudhuria,na wala hakutaka kutokee upinzani wa aina yoyote katika huu uungaji mkono,siyo kwa Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake - wala kwa mwingine yeyote miongoni mwa AhluBait-Radhi za Allah ziwe juu yao-kwa hakika walikuwa wanafuraha sana kuliko watu wengine kwa kule kuchaguliwa kwa Abuubakari Al-swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake-na walikuwa ni wasaidizi wake wa mwanzo katika mambo ya Dola kwenye upambanaji maalumu na wenye kuritadi.

Na ilipotimia uchaguzi wa Abuubakar swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- aliwahutubia watu Khutba ya ukhalifa,na Khutba hiyo inazingatiwa kuwa ni tangazo rasmi linalohusiana na maelekezo yake na siasa yake ijayo kwa umma na utaratibu wake katika kuendesha mambo ya Umma na miongoni mwa aliyoyasema baada ya kumuhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifia kwa kila anachostahiki alisema hivi: (Ama baada ya kusema hayo enyi watu ,kwa hakika mimi nimefanywa kuwa mtawala wenu namimi siyo bora kuliko nyinyi,basi ikiwa nitafanya vizuri basi nisaidieni ,na ikiwa nitakosea basi nikosoeni,ukweli ni uaminifu na uongo ni Khiyana ,na mtu mumuonae kuwa ni dhaifu kwenu nyinyi basi kwangu mimi ni mwenye nguvu mpaka nimrudishie haki yake kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu,na yule mumuonae ni mwenye nguvu kwenu nyinyi basi kwangu mimi ni dhaifu mpaka nichukue haki kutoka kwake kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu,na watu hawatowacha Jihadi isipokuwa Mwenyezi mungu atawapiga kwa pigo la udhalili,na wala hayatoenea machafu kwa watu isipokuwa mwenyezi mungu atawashushia balaa,ni tiini pale ambapo nitakuwa ni mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake na ikiwa ni tamuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi siyo wajibu wenu kunitii).(1460.)

Na ilikuwa mwanzo wa zama zake-Radhi za Allah ziwe juu yake- ni kwa unyenyekevu,na kutangaza yeye haitukuzi nafsi yake na kuwa yeye siyo mbora kuliko wao ,na kwa hakika alikuwa-Radhi za Allah ziwe juu yake-ni mbora wao kwa namna ambavyo tunajuwa lakini kawaida ya tabia ya uislamu ni unyenyekevu na kumsifia Mwenyezi Mungu na wala siyo kujisifia.

Kama alivyotilia mkazo -Radhi za Allah ziwe juu yake- jambo la uadilifu na na usawa,na kuwa watu wote mbele ya mtazamo wa sheria na dola na Taasisi zake watachukuwa haki zao kwa usawa uliokamilika ,kama alivyowatilia mkazo msingi wa Jihad na kilichukulia kwa nguvu,na kuwa hiyo ndiyo njia ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na ni moja ya sababu za kuwa na nguvu na ni kipawa cha waislamu.

Na kama alivyotahadharisha-Radhi za Allah ziwe juu yake- kuhusu machafu na madhara yake na kuhusu kuyahama machafu,na kuwa hayo machafu ni sababu ya milipuko ya magonjwa na kutaka machafu yahamwe,kwa sababu machafu ndiyo chanzo cha maradhi mbalimbali katika Umma,na natamani kama angeziona hali za watu leo hii na maradhi na akayaona maradhi yatokanayo na machafu yakiongozwa na maradhi ya kijamii,ili apange tena utaratibu wa kukabiliana na machafu,na kusimama mbele na kumzuia mwenye kuueneza baina ya watu.

Kama alaivyobainisha-Radhi za Allah ziwe juu yake- kuwa yeye amakwenda kwa mujibu wa sheria za Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume ,na kuwa kumtii ni wajibu katika mipaka ya kufuata kwake njia hii,na kuwa kumtii yeye hakuasi kuwa kinyume na utaratibu huo,bali kumtii yeye siyo lazima ikiwa yeye atakwenda kinyume na hivyo.

Kwa hakika Khutba hii ambayo inawakilisha mpangilio wa kazi na siasa ya muda ujao,unahitajia kusomwa zaidi na uchambuzi kutoka kwa wafanya pekuzi ,ili kutoa yaliyomo ndani ya Khutba miongoni

mwa Tabia na makusudio na siasa na mpango kazi wa ndani na nje ,mpango wa Dola na utaratibu ambao anakwenda nao.(1461)

Sababu za kuchaguliwa Abu Bakari Asswidiq -Radhi za Allah ziwe juu yake-

Hapana shaka kuwa Abuubakar Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- ni mtu bora katika Umma baada ya Mtume wa Mwenyezi mungu na ni mtu aliyeshikana sana na Mtume wa Mwenyezi mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-** naye ni swahiba wake kati ya watu wote katika Umma kwenye kuhama.na kwa hakika waliashiria maswahaba kilichopokelewa kuhusu jambo hilo kwenye Qur'an tukufu.

﴿إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْعَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾ [التوبة: 40]

Kama hamta mnusuru basi ALLAH ameisha mnusuru pindi walipo mtoa wale walio kufuru hali ya kuwa wakiwa wawili ndani ya pango alipo sema kumwambia rafiki yake usihuzunike hakika ALLAH yupo pamoja nasi kisha ALLAH akateremsha utulivu na jeshi ambalo nyie hamkuliona na ALLAH akajalia neno la wale walio kufuru kuwa chini na neno la ALLAH kuwa juu na ALLAH ni mwenye nguvu mwenye hekma. Surat Taubah:40) (1462)

Na kwa hakika Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** alikuwa akaimtegemea Abuubakar Swiddiq zaidi kuliko swahaba yeyote kwenye maradhi yake ambayo yalikuwa ni sababu ya kufa kwake na kabla ya hapo pia alikuwa akaimtegemea na licha ya kuwa Mtume hakutoa wasia wa moja kwa moja kwa Abuubakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake-na ijapokuwa haukuwa ni wasia pale ambapo Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** aliliwacha jambo hilo liwe ni la kushauriana baina ya waislamu,na ili iwe ndiyo njia endelevu kwa

umma wakiichukua njia hiyo,na kuwe kushauriana ndiyo msingi wa kitabia na kisiasa ,na nidhamu ambayo wanakwenda nayo ikiwa watataka haki na furaha na miongoni mwa viashiria ni hivi:

Kuwa yeye Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** aliamrisha kumfuata Abuubakar na Omar na watakao kuja baada yao,kutoka kwa Hudhaifa Bin Al-yaman amaesema: Tulikuwa tumekaa kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**akasema:sijui muda wangu mimi wa kubakia kwenu,basi wafuataeni wale watakaokuwepo baada ya yangu,na akaashiria kwa Abuubakar na Omar,na fuateni muongozo wa Ammar,na atakayowasimulia Bin Masoud jambo lolote basi msadikisheni)(1463)

Kuwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** alimuamrisha Abuubakar awaswalishe watu pale alipouguwa maradhi ambayo yalimsababishia kifo,baada ya kushindwa kwake kutoka kwa ajili ya kuwaswalisha watu.amepokea Muslimu katika sahihi yake kutoka kwa Aisha-Radhi za Allah ziwe juu yake amesema: (Na alipoingia mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-**kwenye Nyumba yangu alisema Muamrishe Abuubakar awaswalishe watu,akasema:nikasema Ewe Mtume Mtume wa Mwenyezi mungu kwa hakika Abuubakar ni mtu mpole pindi akisoma Qur'an hawezi kuyazuia machozi yake,basi lau ungemwamrisha mtu mwingine asiyekuwa Abuubari,na akarudia kumwambia kauli hiyo mara mbili au mara tatu basi akasema:aswalishe Abuubakar kwa hakika nyinyi wanawake ni watu wa Yusuf).(1464)

Na ilikuwa kurudi Aisha kwa Mtume wa mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake-**kwa kumuogopea baba yake,na kwa hakika kauli hiyo ilikosolewa katika Riwaya ya Bin Hishaam amesema: (Ewe Mtume wa Mwenyezi wa Mungu kwa hakika Abuubakar ni mtu mwepesi mwenye sauti Dhaifu mwenye kulia sana akiwa anasoma Qur'an akamwambia muamrishe aswalishe watu,akasema ,nikarudia kauli yangu ileile ,akasema kwa hakika nyinyi ni wafuasi wa

Yusuf,Muamrishe awaswalishe watu,akasema: kwa hakika mimi sisemi hayo maneno isipokuwa ni kwa ajili tu nilikuwa napenda jukumu hilo liondolewe na kutolewa kwa Abuubakar,na nilijuwa kuwa watu walikuwa hawapendi mtu achukuwe nafasi yake hata mara moja,na kuwa watu watampigia kelele katika kila tukio litakalotokea,hivyo nikawa ninapenda jukumu hilo liondolewe kutoka kwa Abuubakar)(1465)

Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-kumsifia kwake mtume kulikuwa kupo waziwazi na haswa katika Khutba yake ya mwisho ambayo alihutubia mtume pale alipoamrisha kufunga milango ambayo hufunguliwa kwenye msikiti wake isipokuwa mlango mmoja tu uitwao Mlango wa Abuubakar-Radhi za Allah ziwe juu yake-

96- Na kutoka kwa Abuu Saidi Al Answar -Radhi za Allah ziwe juu yake- Amesema: Mtume wa Mwenyezi mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-aliwahutubia watu na akasema:Hakika Mwenyezi Mungu alimpa hiyari Mja kuchagua baina ya Dunia na baina ya vilivyopo kwa Mwenyezi Mungu,basi mja huyo akachaguwa vilivyopo kwa Mwenyezi Mungu,akasema:Basi akalia Abuubakar tukashangaa kutokana na kulia kwake kwa kutoa habari mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**- kuhusu Mja aliyepewa Hiyari,hivyo akawa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- ndiye Mwenyekuchaguwa,na Abuubakar alikuwa ndiye mjuzi wetu zaidi,hivyo akasema Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-kwa hakika mtu muaminifu zaidi kwangu mimi katika kusuhubiana nae na mali yake ni Abuubakar,na lau kama ningekuwa ni mwenye kumfanya kipenzi asiyekuwa mwenyezi Mungu basi ningemfanya Abuubkar kuwa ni kipenzi changu,(1466) lakini undugu wa kiislamu na kumpenda kwake,akasema usibakizwe mlango wowote wa msikiti ila ufungwe isipokuwa mlango wa Abuubakar).(1467)

Kama ilivyokuwa ni katika vigezo vilivyokuwa waziwazi,kama alivyonukuu Bin Abbas -Radhi za Allah ziwe ju yake- kauli ya mar Bi

Khattwab: (Enyi Kongamano la waislamu kwa hakika anaestahiki zaidi miongoni mwa watu kushika jambo la Mtume wa Mwenyezi mungu ni wapili kati ya wawili pindi walipokuwa wawili hao katika pango Abuubakar mwenye umri mkubwa)(1468)

Na kwa hakika watu walikuwa katika enzi za Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-wakiuliza na wakijadiliana kuhusu nani mbora wa Umma baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**-basi wakawa wakimtaja Abuubakar Swiddiq-Radhi zaAllah ziwe juu yake- ndiyo mbora wao;imepokelewa kutoka kwa Bin Omar-Radhi zaAllah ziwe juu yao wawili-amaesema: Tulikuwa tukikhiyarishwa baina ya watu katika wakati wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-Basi tukawa tunamchaguwa Abuubakari kisha Omar Bin Khattwab kisha Othaman Bin Affan) (1469)

Na kwa hakika imepokelewa kutoka kwa Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake -kauli yake ikisema:alipoelemewa Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**- alimwambia Abdurahman Bin Abiibakar:niletee mimi mfupa wa Bega na ubao ili niweze kumwandikia Abuubakar Ujumbe ambao hautozua tofauti kuhusu yeye,basi alipotaka kusimama Abdurahman akasema: Mwenyezi mungu kakataa na waumini pia wamekataa kutofautiana kuhusu wewe Ewe Abuubakar(1470)

Na inavyofahamika ni kuwa Abuubakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake-alikuwa anakichukia cheo cha Ukhalifa na kwa hakika amepokea Raafiu Twaai Rafiki ya Abuubakar Swiddiq aliyekuwa nae katika vita vya Dhaatu Salaasil akasema:basi nikamuuliza yaliyotokea kabla ya Uungaji mkono wao akasema:akiwa kwenye hali ya kumuhadithia yale waliyoyazusha baadhi ya Answaar na yale Omar Bin Khatwab aliyo waambia Answaar na aliyowakumbusha kuhusu mimi kuwaongoza wao kwa Amri ya mtume wa Mwenyezi mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-alipokuwa kwenye maradhi yake,basi wakaniunga mkono kwa ajili ya jambo hilo nami

nikawakubalia jambo hilo na nikaogopea kuwepo kwa fitna ya kuritadi baada ya hapo)(1471)

Kama ambavyo palikuwepo na baadhi ya Ndoto ambazo alizitafsiri Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-zikiwa na maana ya Utawala wa Abuubakar Swiddiq-Radhi zaAllah ziwe juu yake-ambao utakuwa baada yake Mtume.Amepokea Imamu Bukhari Kuwa Abdullah Bin Omar -Radhi za Allah ziwe juu yao wawili-amasema: ((kwa hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-amesema wakati mimi nipo kisimani ninachota maji humo,mara akaja Abuubakar na Omar basi Abuubakar akachukuwa Ndoo akachota maji ndoo moja au mbili na kwenye kuchota kwake kulikuwa ni kwa kinyonge Mwenyezi Mungu amsamehe yeye,kisha akachukuwa Omar Bin Khatwab kutoka kwenye mikono ya Abuubakar basi ukaangukia mikononi mwake mshale ambao haujulikani mrushaji wake na wala sikumuona mwerevu yeyote katika watu mpaka watu wakapatwa na mishale wakiwa kwenye kunyweshelezea Ngamia,-akasema Wahbu:Al-atwan ni sehemu wanazopiga magoti Ngamia kwa ajili ya kunywa maji))(1472) Na kwa hakika imepokelewa"Kuwa Mwanamke mmoja alimjia mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-akamuamrisha arudi kwake.akasema:waonaje nikiwa nitakuja na nisikukute?kanakwamba mwanamke yule anataja kifo.mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akasema (Ikiwa hautanikuta basi mwendee Abuubakar)(1473)

Na niwajibu juu yetu kumtaja Ally Bin Abiitwaalib-Radhi za Allah ziwe juu yake na amani- alikuwa ni katika watu waliokuwa wakimsifia sana Abuubakar kutokana na elimu yake-Radhi za Allah ziwe juu yake-,kwa hakika Bukhari amepokea katika sahihi yake kutoka kwa Bin Abbas-Radhi za Allah ziwe juu yake-amesema: Kwa hakika mimi nilikuwa nimesimama sehemu yenye watu,wakawa wanamuomba Omar Bin khattwab kwa Mwenyezi Mungu na kwa hakika alikuwa Mtume amelazwa kitandani kwake,mara ghafila

akatokea mtu nyuma yangu na akaweka mikono yake juu ya mabega yangu,akisema Akurehemu Mwenyezi Mungu kwa kuwa nilikuwa natarajia akuweke Mwenyezi Mungu pamoja na masawahaba zako wawili,kwa hakika mimi nilikuwa namsikia mara nyingi Mtume wa mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**-anasema:nilikuwa na Abuubakar na Omar,Nilifanya jambo fulani na Abuubakar na Omar,na Nilikwenda na Abuubakar na omar,kwa hakika nilikuwa natarajia kuwa Mwenyezi Mungu atakuweka pamoja nao hao wawili,basi nikageuka mara ghafla namkuta Ally Bin AbiiTwalib)(1474)

Na kwa hakika Ally Bin Abii Twaalib alimsifia sana Abuubakar - Radhi za Allah ziwe juu yake-na akausifia ukhalifa wake,na vilevile akausifia ukhalifa wa Omar Bin Khattwab-Radhi za Allah ziwe juu ya wawili hao- na ushuhuda wa Ally Bin Abii Twalib -Radhi zaAllah ziwe juu yake-yeye mwenyewe wa kuwajibu moja kwa moja aliyejaribu kususema vibaya au kudai ya kuwa Ally anao wasia ambao Abuubakar hakuujuwa-Radhi za Allah ziwe juu yake-.kutoka kwa Abdullah Bin Khair amasema: Nilimsikia Ally Bin Abii Twalib-Radhi za Allah ziwe juu yake -anasema:alichukuliwa mtume roho yake akiwa katika kheri ambayo hakuchukuliwa namna hiyo Nabii yoyote miongoni mwa manabii,akasema kisha akapewa Ukhalifa Abuubakar na akafanya kazi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na sunna zake kisha akachukuliwa Abuubakar akiwa katika uzuri ambao hajachukuliwa kwa namna hiyo yeyote,na akawa ni mtu bora katika Umma huu baada ya mtume wake-**Rehema na amani ziwe juu yake**-kisha akateuliwa Khalifa Omar,basi kaifanyia kazi ujuzi wao hao wawili na Sunna zao kisha akachukuliwa Roho yake kwa namna iliyokuwa nzuri kiasi kwamba hakuna aliyechukuliwa roho yake kama yeye,na akawa ni mtu mwema katika umma huu baada ya Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na baada ya Abuubakar(1475)

Kama ilivyopokelewa kutoka kwa Muhammad Bin Al-hanafiyyat naye ni mtoto wa Ally Bin Abii Twalib-Radhi za Allah ziwe juu yake-amesema: Nilimwambia baba yangu ni mtu gani ni mbora baada ya Mtume wa mwenyezi Mungu-**Rehema na amani ziwe juu yake**- akasema Abuubakar ,nikasema:kisha nani akasema Omar kisha Omar,na nikaogopea kuwa atasema Othaman nikasema:kisha ni wewe,akasema:mimi siyo lolote isipokuwa ni mtu miongoni mwa waislamu tu.)(1476)

Na hapana shaka kuwa mapokezi yanayohusu ubora wa Abuubakar ni katika kauli za Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake-zinatilia mkazo Riwaya ambazo zimetaja uungaji mkono wa Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake- na Abbas na wengine katika watu wa nyumba ya Abuubakar Swiddiq-Radhi za Allah ziwe juu yake- katika uungaji mkono wa jumla baada ya kufa kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- hapohapo katika msikiti wake asubuhi ya siku ya Juma Nne iliyofuata baada ya kufa kwake.(1477)na kilochothibiti ni kuwa Ally Bin Abii Twaalib-Radhi zaAllah ziwe juu yake-hajaachana na Abuubakar katika wakati hata mara moja na wala hajawacha kuswali nyuma yake hata mara moja na alitoka pamoja nae mpaka sehemu iitwayo Dhii Qis'sswah katika vita vya walioritadi.(1478)

Na kwa hakika lilikuwa ni jambo la wazi kuwa mtume aliuwacha umma wake pasina kuwapangia kiongozi,na kuwa yeye-**Rehema na amani ziwe juu yake**- aliweka misingi ambayo inafuatwa kwenye mashauriano na namna ya uteuzi kutoka kwa watu maalumu wenye kufanya uteuzi na kuuvunja(1499)na kwa hakika umma uliijuwa hii misingi na ikawa ndiyo utaratibu alioufuata Omar Bin Khattwab - Radhi za Allah ziwe juu yake-pale ambapo imethibiti kutoka katika sahihi mbili kutoka kwa Omar Bin Khattwab alipochomwa na mshale aliulizwa,hivi haumuweki Khalifa ewe kiongozi wa waislamu?basi akasema ikiwa nitaweka khalifa kwa hakika alishawekwa aliyekuwa bora kuliko mimi yaani Abuubakar-na ikiwa nitawacha kwa hakika

nitakuwa mtu aliye bora kuliko mimi yaani Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema akasema Bin Omar:Nikajuwa pale alipotajwa Mtume wa Mwenyezi Mungu -**Rehema na amani ziwe juu yake**-kuwa yeye siye mwenye kumteua Khalifa)(1480)

kama ilivyopokelewa kutoka kwa Ally-Radhi za Allah ziwe juu yake-kuwa yeye amesema baada ya kuwatakiwa ateuwe Khalifa: (Hakuwahi mtume kumchaguwa Khalifa mpaka nami niweze kumchagua khalifa,lakini ikiwa mwenyezi Mungu atawatakia watu Kheri basi atawafanya kuwa kitu kimoja baada yangu kwa mtu mbora wao,kama alivyowafanya wakawa kitu kimoja baada ya kufa mtume wao mtu aliyekuwa mbora wao).(1481.)

Na anatilia mkazo Bin Kathiir kuwa Ally Bin Abii Twaalib na Zubair Bin Awwam-Radhi za Allah ziwe juu yao wawili,kwa hakika walimuunga mkono Abuubakar Swiddiq katika siku ya kwanza wakiwa pamoja na waislamu na wala hao wawili hawakutofautiana na waislamu wengine,na wanatolea ushahidi wa hilo kwa mashuhuda wa Ally -Radhi za Allah ziwe juu yake-kuswali na Abuubakar tangu kufariki kwa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**- bali kabla ya hapo hakuwacha kuswali nyuma ya Abuubakar Swiddiq kabisa,na alitoka pamoja nae katika vita ya kwanza aliyopigana baada ya kufa mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-mpaka sehemu iitwayo Dhiil kisswat kwa ajili ya kuwauwa walioritadi.(1482)na ukweli kuhusu Ally na Abuubakar ni maneno yake Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهَ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٌ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ﴾ [المائدة: 54]

(Enyi mlioamini yeyote miongoni mwenu atakae ritadi kutoka katika dini yakebasi mwenyezi mungu atawaleta watu ambao

anapenda na wao anawapenda na wao wana mpenda ni wanyenyekevu na wapole kwa waislamu na niwakali kwa makafiri wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na wala hawaogopi lawama ya mwenye kulaumu,hizo ni fadhila za Mwenyezi Mungu humpa amtakae na mwenyezi mungu ni mkunjuaji wa mambo na ni mjuzi)(Al-maidah 54) na wakawa wanampenda mwenyezi mungu na wakipigana katika njia yake,

Na kwa hakika Ally Bin Abii Twaalib alimuunga mkono upya Abuubakar baada ya miezi sita kwa mara nyingine,na wakati huo ilikuwa baada ya kufa Fatma -Radhi za Allah ziwe juu yake- na alifanya hivyo kwa lengo la kutilia mkazo juu ya Ridhaa yake na mahusiano mazuri-Radhi za Allah ziwe juu yao wao wawili-na akakanusha yanoyoenezwa kinyume na hivyo.

Hitimisho:

Mwenyezi Mungu aliwaneemesha waumini kwa kutumwa kwake,na akamfanya kuwa ni Rehema kwa viumbe wote,watu wanamuabudu mwenyezi Mungu kwa kumfuata yeye,aliishi Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-** na matukio yaliyotokea katika zama zake kwa kuwashirikisha miongoni mwa Ahlu Bait na maswahaba ambao walishirikiana nao kwenye matukio na wakaathirika nae na wao wakauathiri Umma,Aliishi Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**maisha yake ambayo Mwenyezi Mungu aliinua utajo wake kama ambavyo haikutoka kutajwa yeyote katika wanaadamu kama alivyotajwa yeye mpaka siku ya kiama,wanapita wafalme na wanasahaulika kwa kupita miaka michache,na zina simama Dola na zinakwisha na zinapita zama na nyakati na husahauliwa aliyepita katika zama hizo,lakini yeye mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake-**ni mwenye kubakia katika mioyo,ili awe ni kiigizo katika tabia,alijulikana kwenye maisha yake na wakati wake kwa uwazi na uaminifu ambao haujawahi tokea kwa yeyote asiyekuwa

yeye,waislamu walimtanguliza Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**- kuliko nafsi zao na kumpenda yeye ni wajibu kwa kila muislamu,na watu wote wameona kuwa yeye Mtume -**Rehema na amani ziwe juu yake**-ni mfano kwa wanadamu aliyempole na mfano wa kuigwa,na mchamungu zaidi na muadilifu na Hakimu mkubwa ,hivyo wakaendelea kuandika kuhusu yeye na kuusu maisha yake na Historia ya -**Rehema na amani ziwe juu yake**-na wataendelea kuandika mpaka siku ya Kiama ,na wala hawatapata mfano wake katika wanaadamu.

Historia ya Mtume wa Mwenyezi -**Rehema na amani ziwe juu yake**-imebarikiwa, kuanzia maisha yake na mwenendo wa Dola yake na jamii na umma, na wafuasi amani na Jihad, kwa nguvu na cheo katika kila kitu, maisha yenye huruma na Ihsan kwa kila aliye hai na kila mwanadamu ,katika somo letu kunakuonyesha kila linalogusa Utu wa Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na anayofungamana nayo, na kujua Wahyi na uhusiano na mafungamano yake na uongofu na kuhusu wakati wake, hivyo yeye ni kiigizo kwa kila mwenye kumtaka Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na akamtaja Mwenyezi Mungu sana, ni Nuru na uongofu na maono na ni kiigizo chema, tunamuomba Mwenyezi Mungu atufufue katika kundi lake, na aturuzuku uombezi wake Mtume-**Rehema na amani ziwe juu yake**-na atunyweshe katika birika lake na wala asitufitinishe baada yake, na Shukuran zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye kwa Neema zake yanatimia yaliyo Mema.

Yaliyomo

KCHAGUA KUTOKA KATIKA HISTORIA YA MTUME MTEULE.....	2
Utangulizi:	4
Malengo ya kuisoma Historia ya Mtume na faida zake.....	8
Katika kuisoma Historia yake -Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na amani- ni kuthibitisha kumpenda kwake.	17
Namna ya kuisoma Historia ya Mtume.....	27
Mambo maalumu yaliyoko kwenye Historia ya Bwana Mtume.	34
Hali za Waarabu katika zama zilizopo kabla ya uislamu.	38
Upande wa Kidini:	38
Maisha ya kijamii:.....	40
Hali ya ulimwengu kidini katika zama kabla ya uislamu.	42
Uyahudi:	43
Unaswara:	43
Majusi - waabudu Moto:.....	44
Budha:	45
Hali ya kisiasa katika zama zilizo kabla ya uislamu.	48
Hali za Waarabu kisiasa:.....	48
Waarabu - Mabedui.	49
Mji wa Makkah na Madinah:	50
Ulimwengu na kumngojea Mtume:	56
MAYAHUDI:	56
MANASWARA:.....	61
ZAMA ZA BWANA MTUME -SALA NA AMANI ZIWE JUU YAKE...	93

NASABA YA BWANA MTUME SALA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:	97
KUZALIWA KWA MTUME KIPENZI -SALA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:	98
YATIMA ALIYELELEWA NA ALLAH:	101
UJANA WAKE MTUME-Sala na Amani ziwe juu yake.....	102
TUKIO LA KUIJENGA AL-KAABA:	109
VIDOKEZO VYA KABLA YA KUPEWA MTUME:.....	111
KUPEWA UTUME NA KUCHAGULIWAKUWA MTUME.....	116
KUTEREMKA KWA WAHYI:	116
KUTEREMKA KWA WAHYI:	116
KUANZA KWAKE KUFIKISHA UJUMBE.	124
Washirikina walimuudhi bwana Mtume -Sala na amani ziwe juu yake- na yaliyomkuta kutoka kwao [203].	133
WA MWANZO KUPATA MISUKOSUKO NA MASHAHIDI.....	139
KUHAMA MARA YA KWANZA KWENDA HABASHI [ETHIOPIA].[212].....	142
KUHAMA KWA MARA YA PILI KWENDA HABASHI (ETHIOPIA):	146
VIKWAZO VYA KIDHALIMU: [226].....	147
KUFARIKI KWA KHADIJA -RADHI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE-: [236].....	150
KUFA KWA ABUU TWAALIBU:	151
KISA CHA SAFARI YA USIKU NA KUPANDISHWA MBINGUNI (ISRAA NA MIIRAJI, MWAKA WA: 9 H).....	153
KUJITANGAZA KATIKA MAKABILA [260]	160

KUKUTANA KWA MARA YA KWANZA NA ANSWAAR (WAKAZI WA MADINA):	164
KIAPO CHA KWANZA CHA UAMINIFU CHA AKABA.	167
AHADI YA UAMINIFU YA PILI YA AKABA:	171
KUHAMA KWA MASAHABA WA MTUME REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:	177
WATU WA SUFA.	181
KUHAMA KWA MTUME -REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE:	183
Abubakari Swiddiq -Radhi za Allah ziwe juu yake- na familia yake na mchango wao katika kuhama:.....	183
ALLY -RADHI ZA MWENYEZI MUNGU ZIWE JUU YAKE- NA KUMLIPIA KWA MTUME REHAMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE NA KUREJESHA KWAKE AMANA ZA WATU.....	191
NJIA YA KUELEKEA MADINA [314]	193
KUFIKA KATIKA MJI WA MADINA.....	198
MADINA NA WAKAZI WAKE:	206
KUJENGWA KWA MSIKITI WA MTUME:.....	210
KUUNGA UDUGU [362]	212
KUUKUZA MJI WA MADINA NA JAMII YAKE.	215
Ni kubadilisha jina la mji wa Madina:	216
Kuupenda mji wa Madina na kuuwekea mipaka ya utukufu:	216
KUONGEZEKA KWA WAKAZI:	218
Ukuaji wa Nadharia ya Kiakili:.....	220
UKUAJI WA KIELIMU:	221

UKUAJI WA KIJAMII:.....	229
UKUAJI KATIKA SEKTA YA AFYA:.....	236
UKUAJI WA UCHUMI:.....	239
RUHUSA YA KUPIGANA:.....	241
FUNGA YA RAMADHANI:.....	250
KUGEUZWA MUELEKEO WA KIBLA:.....	252
MWANZO WA VIKOSI NA VITA:.....	253
VITA VYA KWANZA:.....	260
VITA VYA AB-WAA: (459).....	260
VITA VYA ASHIRA :[465].....	261
VITA VYA SAF-WAN: (BADRI YA KWANZA): [468].....	261
VITA VYA BADRI (TAREHE: 17 RAMADHANI MWAKA 2H) [471].....	262
KATI YA BADRI NA UHUDI.....	278
Vita Vya Watu wa Qainuqaa:.....	279
Vita Vya Uhud(Mwezi Shawwal Mwaka 3 hijiria)(537)..	290
Watu wa Rajii:(569).....	301
Tukio la Biiru Maaunat:.....	304
Vita vya Banii Nadhiir vilivyotokea katika mwezi(Rabiul Awwal 4Hijiria).....	307
Vita vya Makundi(Al-Han-Ndaki) katika mwezi Shawwal mwaka wa 5):(596.).....	318
Vita vya Banii mustwaliq(Al-uraissiy): (Shaaban mwaka 6Hijiria).....	333
Tukio la kusingiziwa -Uongo.....	335

Ujumbe wa Nabii kwenda kwa viongozi wa ulimwenguni(669)	364
.....	
Ujumbe wake kwenda kwa Mfalme wa Roma:.....	366
Ujumbe wake kwenda kwa Kisra:(696).....	382
(705)Mwaka wa Tisa Hijiria.....	385
Ujumbe wake kwenda kwa muqauqis(mtawala wa kabila la Qibtwiya katika Nchi za Misri):.....	388
Jumbe zake kwa wafalme wa Habasha :.....	392
Ujumbe wake kwenda kwa Huudhat Bin Ally Al-Hanafiyy katika mji wa (Yamaamah):	398
Ujumbe wake kwenda kwa Al-Mundhir Bin Saawiy Al-abdiy kayika mji wa Bahrain:.....	402
Ujumbe wake kwenda kwa Farwat Bin Amrou Al-Judhaamiy:	404
.....	
Jumbe zake kwenda kwa Mfalme wa Oman:	405
Ujumbe wake kwenda kwa Haarith Bin Abii Shamriy Al-Ghassan:.....	408
Ujumbe wake kwenda kwa Haarith Bin Abii Shamriy Al-Ghassan:.....	408
Ujumbe wake kwenda kwa Yahinnat Bin Ru'uyat na viongozi wa Ailat:	410
Ukombozi wa Khaibar(ilikuwa ni mwezi Rabiul Awwal mwaka wa 7Hijiria)(795).....	415
Umra ya kulipa iliyopita:(815).....	420
Vita vya Mu'uta (Jumaadatul Uula mwaka wa 8 Hijiria):(824)	423
.....	
Fat-hu Makkah (Ramadhan 20 mwaka 8 Hijiria).....	426

VITA VYA HUNAINI NA TWAIF (SHAWAL MWAKA 8H): [867]	436
VITA VYA TABUK: (RAJAB: MWAKA 9H) [892].	444
Kuhiji Abubakar na Waumini (MWAKA 9H): [913]	460
MISAFARA YA MAKABILA [921]	469
Waafid Daus (Atufail bin Amri): [932]	473
Msafara wa Abdul kaisi: [941]	477
Msafara wa Thaqiif:	481
Msafara wa bani Tamiim [965]	487
Msafara wa Bnii A'amir:	492
Msafara wa banii Hanifah: [984]	494
Misafara ya Yemen:	500
Msafara wa Al-ash'aryiina:	501
Msafara wa bani Muraad (Fur-wat bin misiik)	502
Msafara wa Hamdan:	503
Msafara wa Kindi:	505
Msafara wa Al-Azd(na Jursh):	506
Msafara wa Al-harith bin Ka'b:	509
Misafara ta Wakristo wa Kiarabu: [1033]	512
Msafara wa Al-daryyina:	512
Msafara wa Taghlib:	513
Msafara wa Twayi:	514
Msafara wa Fur-wat bin Amr Al-juzaamy: [1051]	516
Msafara wa Ghasaan:	516
Kifo cha Ady bin Twaaii: [1057]	517

Msafara wa Najran: [1076]	526
Kubomowa Masanamu:	540
Kikosi Cha Khalid bin Al'walid kwenda kuvunja Sanamu la Uzaa: [1101].....	542
Kikosi cha Amr bin Al'aswi kubomowa Sanamu la Suwaa [1106].....	543
Kikosi cha Sa'ad bin Al'ashihaly kwenda kubomoa Sanamu la Manata:.....	543
Kikosi Cha Ally bin Abi Twalib kwenda kubomowa Sanamu la Twaii[1111]:	544
Kikosi cha Tufeil bin Amr kwenda kubomowa Sanamu la (Thul-Kafain) kwa Daus:.....	545
Kikosi cha Jarir bin Abdillaha Albajaly kwenda dhil Khulswat: [1115].....	545
Hija ya kuaga [1118].....	547
Hadithi ya Ghadir Khom:.....	585
Kulituma jeshi la Osamah bni Zaid:1184.....	588
Kusimamisha Nchi ya Kiislamu.....	593
Upangaji wa ulinzi na usalama.....	616
Kutengeneza Adabu katika Jamii(1247).....	630
Uundaji Jeshi(1304).....	676
DOLA YA MTUME REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE NA AMANI YA ULIMWENGU.....	691
KUFARIKI KWA MTUME REHEMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE. [1334].....	694
Kujiskia maumivu Mtume sala na amani ziwe juu yake: ...	699

Kuzidi kwa Maradhi ya Mtume sala na amani ziwe juu yake:	700
Siku ya mwisho katika Maisha ya Mtume sala na amani ziwe juu yake:.....	715
Kuandaliwa kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- na kuzikwa kwake:	734
KUCHAGULIWA ABUBAKARI -RADHI ZA MWENYEZI MUNGU ZIWE JUU YAKE:	748
TUKIO LA SAKIFA:	750
Sababu za kuchaguliwa Abuu Bakari Asswidiq -Radhi za Allah ziwe juu yake-	762
Hitimisho:.....	770
Yaliyomo.....	772



موسوعة المصطلحات الإسلامية
TerminologyEnc.com



موسوعة تضم ترجمات المصطلحات الإسلامية وشروحاتها بعدة لغات



موسوعة الأحاديث النبوية
HadeethEnc.com



موسوعة تضم ترجمات للأحاديث النبوية وشروحاتها بعدة لغات



موسوعة القرآن الكريم
QuranEnc.com



موسوعة تضم تفاسير وتراجم موثوقة لمعاني القرآن الكريم

IslamHouse.com



مرجعية مجانية إلكترونية موثوقة للتعريف بالإسلام



منتقى
المحتوى الإسلامي



موسوعة تضم المنتقى من المحتوى الإسلامي باللغات

الإسلام 100 بأكثر من لغة

جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات



جمعية الدعوة وتوعية الجاليات بالربوة

